KIFUNGUA MLANGO WA KUITALII KURANI TUKUFU

Na

Hadhrat Mirza Bashir-ud-Deen Mahmood Ahmad,
Khalifatul-Masih II[ra]

KIFUNGUA MLANGO WA KUITALII KURANI TUKUFU

Swahili Translation of
Introduction to the Study of the Holy Quran (Kiingereza)

Mwandishi:
Hadhrat Mirza Bashir-ud-Deen Mahmood Ahmad,
Khalifatul-Masih II[ra]

Mfasiri:
Athumani Mwinyi Gakuria

© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza (Kiingereza): 1985
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2021

Kwa maelezo zaidi:

Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dare es Salam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi, Kenya. Simu: +254222111031

Kimechapwa na: Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salam, Tanzania
Simu: +255222111031

ISBN: 978-1-84880-518-7
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

FAHARISI

Maelezo ya mwenezi ix
Neno la mwandishi x
Kifungua Mlango wa Kuitalii Kurani Tukufu 1
Haja ya tafsiri mpya na maelezo 1
Tafsiri ya hivi sasa yaitosheleza haja hii 2
Sifa maalumu za maelezo haya 3
Vitabiu vingine vilivyofunuliwa 6
Kuwepo haja ya Kurani 7
Mungu wa Biblia ni Mungu wa kitaifa 8
Ma-Veda hali kadhalika ni vitabu vya kitaifa 9
Mungu ni Mmoja 10
Dini haikutokana na mawazo ya Kibinadamu 11
Mafundisho yaliyofunuliwa daima huwa kinyume na mawazo yaliyopo 15
Kwa nini mafundisho ya dini mbalimbali yanatofautiana 17
Islam yafundisha umoja wa Mungu na wa wanadamu 18
Yesu si mwalimu wa dunia nzima 20
Maana ya ustaarabu na utamaduni 23
Vipindi mbalimbali vya ustaarabu na utamaduni 26
Utamaduni wa Kiyahudi na wa Kikristo 28
Swali linalostahili 32
Hitilafu katika Agano la kale 39
Mafundisho ya kikatili ya Agano la Kale 46
Mafundisho yasiyo ya kimantiki ya Agano la Kale 48
Manabii wamesingiziwa na Biblia 53
Agano jipya lachunguzwa 57
Yesu mwenyewe yuatangaza 61
Ushahidi wa wanazuoni wa Kikristo 62
Hitilafu katika Agano jipya 69
Ushirikina katika Injili 72
Mafundisho yenye tashwishi ya Agano Jipya 77
Mapachiko katika Ma-Veda 83
Mafundisho ya kikatili ya Ma-Veda 89
Ushirikina katika Ma-Veda 92

Hitilafu katika Ma-Veda 94
Idadi ya miungu wa Ma-Veda 96
Ahadi ya Mwenyezi Mungu kwake Nabii Ibrahim[as] 97
Bishara katika Kumbkumbu la Torati 102
Parani – sehemu ya Arabuni 110
Wakureishi ni wazao wa Hadhrat Ismaeli[as] 112
Mtume Mtukufu[saw] katajwa katika kitabu cha habakuki 116
Ujaji wa Mtume Mtukufu[saw] ulitabiriwa na Nabii Suleiman[as] 120
Bishara za Nabii Isaya[as] 124
Bishara za Danieli 143
Bishara katika Agano Jipya 148
Mtume Mtukufu[saw] — Muhtasari wa maisha yake 160
Maisha ya Mtume[saw] ni kitabu kilicho wazi 164
Hali ya Arabuni zama alipozaliwa Mtume Mtukufu[saw] 166
Ndoa ya Mtume Mtukufu[saw] na Hadhrat Khadija[ra] 172
Mtume[saw] apokea wahyi wake wa kwanza 175
Waislamu wa awali 176
Waaminio wateswa 178
Ujumbe wa Islam 184
Kuhamia Uhabeshi 187
Umar yuasilimu 190
Mateso yazidi kupamba moto 192
Mtume[saw] yuaenda Ta'if 194
Islam yaenea hadi Madina 198
Ahadi ya kwanza ya 'Aqaba 203
Hijra 205
Suraka amsaka Mtume[saw] 207
Mtume[saw] yuawasili Madina 209
Hadhrat Abu Ayyub Ansari[ra] awa mwenyeji wa Mtume[saw] 211
Maisha yawa hatari Madina 213
Mapatano baina ya makabila mbalimbali ya Madina 216
Watu wa Makka wajiandaa kushambulia Madina 218
Vita vya Badr 221

Bishara kuu yatimia....227
Vita vya Uhud....231
Ushindi wafanywa ushinde....233
Uvumi wa kifo cha Mtume[saw] wafika Madina....240
Mapambano na kabila la Banu Mustalik....250
Vita vya Handaki....253
Vita visivyoshindika....256
Usaliti wa kabila la Banu Quraidha....259
Majeshi ya mwungano wa Waarabu yafumukana....266
Kabila la Banu Quraidha laadhibiwa....269
Uamuzi wa Sa'd[ra] waafikiana na Biblia....272
Je, Mtume[saw] alinuia kuendeleza vita?....275
Mafundisho ya Kiyahudi na ya Kikristo juu ya vita....278
Mafundisho ya Kurani juu ya vita na amani....280
Maagizo ya Mtume[saw] juu ya vita....289
Makafiri wafanya mashambulio ya hapa na pale....292
Mtume[saw] yuasafiri Makka na masahaba 1500....293
Mkataba wa Hudaibiya....298
Barua za Mtume[saw] kwa wafalme mbalimbali....301
Barua kwa mfalme wa Iran....307
Barua kwa Najashi....309
Barua kwa Mtawala wa Misri....311
Barua kwa Chifu wa Bahrain....313
Kutekwa kwa mji wa Khaibar....314
Njozi ya Mtume[saw] yatimia....319
Vita vya Mu'ta....322
Mtume[saw] yuaiandama Makka na wafuasi wake elfu kumi....327
Kutekwa kwa mji wa Makka....330
Mtume[saw] yuaingia Makka....333
Masanamu yavunjiliwa mbali....339
Mtume[saw] yuawasamehe maadui zake....342
Ikrima yuasilimu....344
Vita vya Hunain....346
Wito wa "Mtume wa Mungu anawaiteni"....348

Adui mkubwa awa mfuasi mwaminifu....352
Mtume[saw] yuwagawa mateka....353
Njama za Abu 'Aamir....355
Msafara wa kijeshi kwenda Tabuk....356
Hija ya Mwisho....360
Mtume[saw] yuwadokezea kifo chake....364
Siku za mwisho za Mtume[saw]....367
Mtume[saw] yuwaaga dunia....369
Hulka za Mtume[saw] na tabia zake....373
Usafi wa mawazo ya Mtume[saw] na tabia zake....375
Maisha ya kikawaida ya Mtume[saw]....376
Uhusiano wake na Mwenyezi Mungu....382
Kakataza kitubio....390
Tabia yake kwa wakeze....392
Hulka zake tukufu....393
Hali ya kujitawala nafsi....395
Haki na maadili....396
Kuwajali maskini....399
Kulinda masilahi ya maskini....402
Kuwahurumia watumwa....403
Kuwatendea wema wanawake....405
Msimamo wake kuwahusu marehemu....409
Alivyowachukulia majirani....409
Alivyowatendea nduguze....410
Kukaa na watu wema....413
Alisitiri imani ya watu....414
Aliziba aibu za wengine....414
Uvumilivu katika dhiki....417
Ushirikiano....418
Msema kweli....419
Udadisi....420
Unyofu na uaminifu biasharani....421
Kukata tamaa....421
Ukatili kwa wanyama....422
Kustahimiliana katika mambo ya dini....423

Ushujaa....423
Kuvumilia washenzi....424
Kuzingatia mikataba....424
Kuwastahi watumishi wa umma....424
Mkusanyo wa Kurani....425
Njia zilizotumiwa kulindia na kuhifadhia maneno ya Kurani....427
Wakufunzi wa Kurani....429
Makarii wa Kurani....431
Kurani yahifadhiwa kwa moyo....433
Kurani yakusanywa katika jalada moja....435
Nakala zilizosawazika za Kurani....436
Desturi ya kuihifadhi Kurani kwa moyo iliendelea....438
Mpangilio wa sura za Kurani....441
Baadhi ya bishara za Kurani....444
Sifa za pekee za mafundisho ya Kurani....451
Kuamini Mungu Aliye hai....452
Wokovu sawa na Kurani....456
Miujiza....458
Ibada ya Mwenyezi Mungu....465
Msikiti wa Islam....466
Mfungo wa Kiislamu....468
Haji....469
Zaka....469
Serikali ya Kiislamu....471
Isemavyo Kurani juu ya utumwa....473
Roho ya mwanadamu....474
Plani ya Kurani ya malimwengu ya kiroho....478
Mungu wa mataifa yote....481
Mwenyezi Mungu — Chanzo cha viumbe vyote....482
Sifa kuu za Mwenyezi Mungu....485
Sifa nyingine za Mwenyezi Mungu....489
Aina tatu za sifa za Mwenyezi Mungu....493
Sifa za Mwenyezi Mungu hazipingani....496
Mwanadamu — Kitovu cha malimwengu....499
Kilele cha mfululizo wa mabadiliko yaendeleayo....501
Shabaha ya kuumbwa kwa mwanadamu....504

Kanuni ya maumbile na kanuni ya sheria ya kiroho 505
Mabadiliko ya uumbikaji wa malimwengu ya kiroho yalihitimika katika Mtume Mtukufu[saw] 508
Kurani ndicho kitabu kitimilifu.....509
Misingi ya ujenzi wa utaratibu wa kijamii.....510
Maisha baada ya kifo 512
Hadhrat Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa[as] 513
Mwana mwahidiwa wa Masihi Aliyeahidiwa[as] 515
Tafsiri katika lugha zingine 518
Shukrani 520

MAELEZO YA MWENEZI

Twafurahi kuweka mbele ya wasomani wa lugha ya Kiswahili tafsiri ya kitabu '*Introduction to the Study of the Holy Quran*' kilichoandkiwa na Khalifa Mtukufu[ra] wa pili wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya.

Kitabu hiki kimejaa utalaamu wa hali ya juu fika. Msomaji wake atajikuta ameongezeka elimu na maarifa kuhusiana na Kurani Tukufu. Maisha ya Mtume[saw] pia yameelezwa humu kwa ufasaha sana.

Twamshukuru Mzee Athumani Mwinyi Gakuria wa Kenya aliyechukua jukumu la kufasiri kitabu hiki cha muhimu kwa lugha ya taifa. Mzee amewahi kufasiri baadhi ya vitabu vingine pia kwa Kiswahili.

Twamshukuru pia Bwana Abdul Aziz Gakuria, mwanaye mfasiri, aliyepanga herufi zake kwa kompyuta na Sheikh Ansar Hussain ambaye ameshughulikia kutayarisha fomati.

Hii ndiyo zawadi nyingine tena ya Dawati la Kiswahili.

Mwenyezi Mungu Awajaalie wasomaji wa kitabu hiki kuzidi katika ujuzi wa dini na ukaribu wa Muumba wake.

Jamil R. Rafiq
Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan. 21 Agosti 2021

NENO LA MWANDISHI

Lilipotolewa jalada la kwanza la 'Tafsiri na Maelezo' ya Kurani kwa lugha ya Kiingereza, marafiki walitaka kwamba kile 'Kifungua Mlango' nilickokiandika kichapishwe peke yake. Ili kukidhia matakwa yao, hapa kinatolewa katika sura ya kitabu, kiitwacho 'Kifungua Mlango wa Kuitalii Kurani Tukufu'. Hivyo kitaweza kupatikana kwa idadi iliyo kubwa ya watu, kiasi hiki kwamba kwa kunufaika nacho waweze kuyaelewa mafundisho ya Kurani.

Ule udadisi wa 'Tafsiri na Maelezo' ya Kurani, uliofanywa na wataalamu mbalimbali, utashughulikiwa baadaye.

Mirza Bashir-Ud-Din Mahmud Ahmad

(Khalifatul Masih wa Pili)

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [1]

KIFUNGUA MLANGO WA KUITALII KURANI TUKUFU

HAJA YA TAFSIRI MPYA NA MAELEZO

Katika kuwasilisha hii tafsiri mpya ya Kurani Tukufu, twaona yastahili kusema kwamba hii sio shughuli ya kibiashara wala upya wenyewe sio kihimizo chake kikubwa.

Juhudi zetu zimehamasishwa na imani ya kwamba wakati ambapo tafsiri mpya inahitajiwa hivi leo na wale wasiojua Kiarabu, maelezo mapya yanahitajiwa na watu wote, iwe wanajua Kiarabu au la, na hii ndiyo kwa sababu hizi mbili:

(i) Tafsiri zilizoandikwa na watu wasiokuwa Waislamu (isipokuwa tafsiri za Kiurdu na Kiajemi) zote zimetayarishwa na watu walioijua kidogo tu au wasioijua kabisa lugha ya Kiarabu na hivyo hawakuweza kuyaelewa matini ya Kiarabu achilia mbali kuweza kuyafasiri. Baadhi yao walifasiri toka tafsiri zingine, na jambo hili likazifanya tafsiri zao kuwa mbali zaidi na maana za maneno yenyewe ya asili.

(ii) Kwa maelezo yao ya matini ya Kurani Tukufu tafsiri hizi hazitegemei ujuzi wa lugha ya Kiarabu, bali zategemea maelezo ya hapo zamani. Kwa vyovyote maelezo yanategemea sana maoni ya mtu binafsi, inaweza sehemu yake kukubaliwa na mtu mmoja, nyingine na mtu mwingine, na sehemu nyingine kutokubaliwa na yeyote. Tafsiri itokanayo na maelezo fulani yaweza kumaanisha katoa maoni ya mtu binafsi, wala sio maana hasa ya matini yenyewe.

Kwa sababu ya kasoro hizi, ipo haja ya kweli tena ya dharura ya tafsiri mpya iliyoandikwa na wataalamu wajuzi wa Kiarabu, na yenye msingi jadidi wa lugha ya Kiarabu, kanuni zake na nahau zake.

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

TAFSIRI YA HIVI SASA YAITOSHELEZA HAJA HII

Tafsiri hii ya Kiingereza yanuiwa kutosheleza hizi haja mbili na, Insha Allah, itafuatiwa, kwa wakati upasao, na tafsiri za aina hii katika lugha zingine.

Kiarabu ni lugha yenye muundo wa kifalsafa. Maneno yake yameundwa kwa makusudio fulani. Mashina yake yameundwa kwa makusudi ya kuelezea maono asilia na uzoefu, na mashina haya kwa kuyageuza kidogo tu kimatumizi huyapatia maneno ya Kiarabu hali ya kuwa na maana pana tena zenye kina. Kuyageuza kikamilifu katika lugha nyingine hukaribia kutowezekana na kwa kuwa tafsiri peke yake haitoshi, hatuna budi tafsiri kuiongezea maelezo kuonesha upana wa maana zilizofichama katika matini. Tafsiri yetu yenyewe haikuepukana na hali hii. Haiwezi ikatarajia kutoa maana kamili au hata maana zenye kukaribiana na matini ya Kiarabu. Inaweza tu kutumainia kutoa moja ya maana zake ziwezekanazo. Hivyo basi, ili kufidia kasoro hii, tumeiongezea tafsiri yetu maelezo. Lakini hata maelezo yenyewe siyo makamilifu. Hayaleti maana kamili ya matini, lakini yanafidia kwa kiasi fulani kasoro za tafsiri. Chini ya 'Maneno Muhimu' tumeonyesha wasaa wa maana matini ilizonazo; na kwa ajili yake, sisi tumechota toka kamusi za lugha ya Kiarabu ambazo si tu zinatambuliwa na Waislamu bali pia na wajuzi wa Kiarabu wasiokuwa Waislamu. Ni matumaini yetu kwamba utalii wa sahifa hizi utamfahamisha zaidi tafsiri yetu msomaji, na kumridhisha ya kuwa zile maana tulizojaribu kupatia matini ya Kiarabu hazikuwa ni uamuzi wetu sisi tu bali zatokana na matumizi yanayokubaliwa ya lugha ya Kiarabu na kanuni zake. Msomaji asiyejua Kiarabu aamini ya kwamba tafsiri yetu, ijapokuwa haikubaliwi na baadhi ya watu, yatokana na matumizi halisi ya Kiarabu na inaweza kukataliwa tu endapo ushahidi wa sehemu nyingine za Kurani au wa matumizi halisi ya Kiarabu unakwenda kinyume nayo.

SIFA MAALUMU ZA MAELEZO HAYA

Baada ya kusema mengi juu ya tafsiri yetu, tungependa kuzungumzia maelezo yetu.

Tayari yapo maelezo chungu nzima ya Kurani, na inaonekana vigumu kuyastahilishia nyongeza. Lakini sisi tunazo sababu nzuri za kujaribu na kutoa maelezo mapya. Sababu zenyewe ni:

(i) Kama vile tulivyosema, maneno ya Kiarabu yana maana zilizopanuka kupita kiasi. Kwa hiyo, tafsiri inaweza ikatumia moja tu ya maana zinazokubalika. Hivyo ilikuwa ni muhimu kuiongezea tafsiri yetu maelezo, na kuonesha maana nyingine za matini zenye kuweza kukubalika.

(ii) Maelezo yote marefu yaliyoratibiwa ya Kurani ni kwa lugha ya Kiarabu, na haina budi kuwa wazi kwamba wale wasioweza kuisoma Kurani kwa Kiarabu hawawezi wakayatumia maelezo haya.

(iii) Maelezo yaliyoongezewa tafsiri zao na waandishi wasiokuwa Waislamu hayatoshelezi kwa sababu mbili:

(a) Yameathiriwa na maandiko ya wapinzani wa Islam;

(b) Waelezaji wenyewe hawakuwa na ujuzi wa Kiarabu, au walikuwa na ujuzi haba. Hawakuweza kujisomea maelezo marefu zaidi na yenye kutegemewa zaidi. Hivyo basi, wafasiri Wazungu hawataji maelezo haya. Hao hurejesha kwenye yale maelezo ya Kurani yasiyokuwa na uzito mkubwa yenye kupendelewa na wengi. Inapokuwa wao kurejeza kwenye maelezo yoyote marefu, basi hayo huchotwa kutoka kitabu kingine wala si kutoka yale ya asili.

(iv) Kukielewa kitabu kikamilifu au cha kisayansi hakuhitaji ujuzi wa ile lugha chanzi tu peke yake na maelezo ambayo mabingwa wa lugha au maudhui hayo huenda wameyaandika. Bali pia kunahitaji utalii wa ndani wa kitabu chenyewe na maarifa ya istilahi, nahau na kanuni kinazozitumia kitabu hicho, ambazo kutokana nazo yaliyomo humo yanakuwa ni yenye maana. Wale wanaotafuta kukifafanua kitabu bila ya kutalii kitabu chenyewe watajipatia manufaa kidogo tu kutokana

na vitabu vya sherehe. Wafasiri Wazungu na waelezaji wa Kurani hawaonekani walikifanyia Kitabu hiki Kitakatifu utalii wa ndani unaohitajika. Hivyo si jambo la kushangaza ya kwamba mara nyingi maelezo yao huonekana kuwa ni ya kipuuzi.

(v) Kila zama husababisha sayansi mpya mpya ambazo kutokana nazo kila kitabu ambacho kinadai chafundisha kitu chochote hukabiliwa na ukosoaji mpya. Hapo heshima ya kitabu huwa inaimarika zaidi au kitabu chenyewe huzidi kuwa na walakani kuliko hapo mbeleni. Kurani ikiwa haitengani na kanuni hii, maelezo yake mapya lilikuwa ni jambo la lazima katika mwanga wa elimu mpya. Bila ya maelezo mapya hatuwezi tukapima ni kiasi gani Kurani bado ingali na manufaa kama mafundisho au ni kwa kiasi gani imejivunjia rekodi yake.

Sherehe za kwanza za Kurani zilipoandikwa, Biblia ya Kiarabu haikuwepo. Haikuwepo hata nakala moja kamili ya Biblia. Vile vijisehemusehemu vya Biblia vilivyokuwa vimetafsiriwa katika lugha ya Kiarabu havikuwa vyenye kupatikana kwa waelezaji wa Kurani. Hivyo basi, kila ilipowabidi kuzungumzia sehemu za Kurani zenye kugusia Biblia au mafundisho ya Nabii Musa[as], basi hawakuwa na budi kutegemea uvumi au dhana zao wao wenyewe. Wala hapana haja ya kusema kwamba mawazo yao wakati mwingine hayaridhishi na wakati mwingine yanachekesha. Waandishi Wazungu wanaitwisha Kurani makosa yao na kukidharau Kitabu hiki Kitakatifu. Wanasahau kwamba waelezeaji hawa hawakuijua Biblia. Wao walitegemea masimulizi waliyoyapenda watu au maneno waliyosikia kutoka kwa wasomi wa Kiyahudi na wa Kikristo waliowaambia waelezaji hao wa Kurani, akina aambiwalo-ndilo, maneno ambayo wakati mwingine waliyatoa kutoka vitabu vya mafundisho yao wenyewe badala ya Biblia na wakati mwingine kutoka fikara zao chakaramu. Katika shughuli hii waelezaji bila shaka wakaonyesha wameyachukulia mambo kiurahisi na kutokuwa waangalifu, lakini wasomi wa Kiyahudi na wale wa Kikristo wakadhihirisha utovu wa uaminifu na ucha-Mungu. Kwa hiyo Waandishi Wazungu wa wakati huu wetu wana chungu nzima ya sababu za kuulaumu udanganyifu wa mababu

zao kuliko kuwadhihaki waelezaji Kurani wa Kiislamu. Lakini sasa mambo yako tofauti. Leo hii ujuzi wa Biblia umekuwa ni jambo la kawaida. Tafsiri za Kiarabu, Kilatini na Kiyunani zimekuwa ni zenye kupatikana kwa wanavyuoni wa Kiislamu, nasi twaweza kuzielezea kwa njia mpya sehemu za Kurani mlimo na marejeleo ya Biblia na mafundisho ya Nabii Musa[as].

(vi) Hadi kufikia wakati huu wetu, ubishi baina ya dini moja na dini nyingine ulihusikana kidogo na masuala ya hali za kitabia na kijamii na kuhusikana zaidi na masuala ya hali za imani na ibada. Kwa sababu hii mafundisho yahusikanayo na masuala ya hali ya kitabia na ujenzi wa tabia na uhusiano wa kijamii, kiuchumi, na kisiasa hayakuzungumziwa kabisa. Lakini leo hii, dunia hufikiria zaidi sana masuala kulingana na mambo haya yenye manufaa. Kwa hiyo ilikuwa lazima kutoa maelezo ambayo inabidi yayaangazie ya kutosheleza zaidi yale mafundisho ya Kurani ya kutekelezwa kwa vitendo.

(vii) Kurani kikiwa ni Kitabu kilichofunuliwa ndani yake mna bishara. Mazungumzo juu ya bishara hizi hayawezekani hadi pale zitakapokuwa zimetimia. Kwa sababu hii pia tulihitaji maelezo mapya ambayo yawe yatazitaja zile bishara za Kurani ambazo zimetimia mpaka sasa na ambazo ni sehemu muhimu ya dalili ya kuwa Kurani ni Kitabu cha Mungu kilichofunuliwa.

(viii) Kurani yaziangazia dini zingine zote na itikadi. Inajijumuishia ndani yake sehemu bora za mafundisho yao, yaonesha udhaifu wao na kukidhia upungufu wao. Waelezaji wa Kiislamu wa hapo awali walikuwa hawajui dini hizi ziliyofundisha na ziliyowakilisha. Kwa hiyo hawakuweza kuthamini kikamilifu iliyokuwa Kurani ifundishe kuhusu dini hizo na itikadi. Sasa mafundisho yote yaliyofichamana yamefichuliwa kiasi hiki kwamba mafundisho ya Kurani kuhusiana na mafundisho ya dini zingine yamewadhihirikia wafuasi wake. Ili kuondoa upungufu huu katika maelezo ya zamani, pia tunahitaji maelezo mapya ya Kurani.

Kwa sababu hizi ni maoni yetu kwamba tafsiri na maleezo yetu si tu kwamba havina haja ya kunradhi, bali vyatosheleza haja halisi tena muhimu. Katika kuwasilisha tafsiri hii na maelezo sisi twatekeleza wajibu.

Twatumaini kwamba wale wenye kusoma tafsiri yetu na maelezo kwa makini na bila ya chuki watalazimika kuitazama Islam wakiwa na mtazamo mpya. Twatumaini kwamba watasadiki kwamba Islam halisi haikujaa makosa, kama vile wanavyoidhania waandishi wa Kimagharibi, bali kwamba hii ni bustani ya roho iliyopangika vizuri ambayo mwenye kuizuru huweza kukaa humo na kila aina ya harufu inayopendeza na uzuri na ambayo huonesha picha ya Pepo iliyoahidiwa na Waalimu wote wa dini.

VITABIU VINGINE VILIVYOFUNULIWA

Ilipofunuliwa Kurani takriban miaka 1325 iliyopita zilikuwemo duniani dini nyingi na vitabu vingi vya dini. Huko Uarabu na maeneo ya karibu yake walikuweko watu walioamini Agano la Kale na Agano Jipya. Waarabu wengi wakawa wakapata kuelekea kwenye Ukristo. Waarabu walikuwa wakiingizwa katika dini ya Kiyahudi. Miongoni mwao alikuwemo Ka'b bin Ashraf, chifu wa Madina na adui mbaya sana wa Islam, na hata babake. Babake Ka'b alitokana na kabila la Banu Ta'ii. Yeye aliipendelea sana dini ya Kiyahudi kiasi hiki kwamba Yahudi mmoja, Abu Rafi' bin Abi Huqaiq, alimwoza bintiye na Ka'b akatokana na ndoa hii (Al-Khamiis, J. I). Mjini Makka kwenyewe, mbali na watumwa wa Kikristo walikuweko baadhi ya wakazi wa Makka walioupendelea Ukristo. Waraqa bin Naufal, jamaa wa Hadhrat Khadija[ra], mke wa kwanza wa Mtume Mtukufu[saw], alikuwa na imani ya Kikristo. Yeye pia aliifahamu lugha ya Kiyahudi na alitafsiri Injili za lugha ya Kiyahudi kwa lugha ya Kiarabu. Imeandikwa katika Kitabu cha Bukhari ya kwamba:

> Waraqa bin Naufal alikuwa amaeukubali Ukristo katika zama za giza; na alikuwa akitafsiri Injili za lugha ya Kiyahudi kwa lugha ya Kiarabu (Bukhari mlango wa Bad'ul Wahyi).

Upande ule mwingine wa nchi ya Uarabu kuliishi Waajemi, na wao pia waliamini Nabii na Kitabu. Ingawa Kitabu cha Zend-Avista kilikuwa kimefanyiwa mabadiliko na mikono ya watu, hata hivyo kilikuwa kikiheshimiwa na laki za waumini wake na Serikali yenye nguvu ilikiunga mkono. Nchini India vitabu vya Veda vilikuwa vimeheshimiwa kwa maelfu ya miaka. Kilikuwepo pia kitabu cha Gita cha Sri Krishna na mafundisho ya Budha. Dini ya Konfyushasi ilistawi sana huko Uchina lakini athari ya Budha, ilikuwa ikiongezeka.

KUWEPO HAJA YA KURANI

Vikiwepo vitabu hivi vyote na mafundisho, je, dunia ilhitaji kitabu kingine? Hili ni swali limjialo kila mtu aanzaye kutalii Kurani. Jawabu lake litakuwa na sura mbalimbai: Kwanza, je, huu mgawanyiko baina ya dini moja na dini nyingine haikuwa ni sababu tosha ya kuja kwa dini nyingine kuziunganisha zote pamoja? Pili, je, akili ya mwanadamu haikuwa ipate mabadiliko ya pole pole sambamba na yale mabadiliko ambayo mwili wa mwanadamu ulikuwa tayari umeishayapata? Na kama vile tu ambavyo mabadiliko ya kimwili mwishowe yalikuwa yameimarika, je, mabadiliko ya kiakii na ya kiroho nayo pia hayakuwa yakielekea utimilifu wake wa mwisho ambao huo ndio uliokuwa ni mwisho wenyewe wa kuwepo kwa mwanadamu? Tatu, je, vitabu vya hapo awali havikuwa vimepatwa na walakini kiasi hiki kwamba kitabu kipya sasa ikawa ndiyo haja kubwa ya dunia nzima iliyotimizwa na Kurani? Nne, je, dini za awali ziliufikiria Ujumbe wao kuwa wa mwisho kabisa? Je hazikuamini upigaji hatua wa maendeleo ya kiroho? Je hazikuendelea kuwahakikishia wafuasi wao ujaji wa Ujumbe utakaowaunganisha wanadamu wote na kuwafikisha kwenye shabaha yao ya mwisho?

Jibu la maswali haya manne ndilo jibu la swali kuhusu kuhitajika kwa Kurani huku vikiwepo vile vitabu vya hapo awali na Ujumbe pia.

Twayajibu maswali haya moja baada ya jingine.

Je, mgawanyiko baina ya dini na dini nyingine haikuwa ni sababu tosha ya kuja kwa mafundisho mapya yatakayounganisha mafundisho yote ya hapo awali?

MUNGU WA BIBLIA NI MUNGU WA KITAIFA

Dini inayo makusudio maradufu: (i) Huwezesha mwanadamu kukutana na Muumba wake na (ii) humfundisha mwanadamu wajibu wake kwa wanadamu wenzake. Dini zote zilizokuwepo zama za ujaji wa Islam sio tu kwamba zilitofautiana bali zilipingana. Biblia haikumzungumzia Mungu, bali ilizungumzia Mungu wa Israeli. Humo ndani twasoma tena na tena:

> Naye Daudi akamwambia Abigaili, Na ahimidiwe Bwana, Mungu wa Israeli, ambaye amekuleta hivi leo kunilaki (I Sam. 25:32).
>
> Na tena, mfalme akasema hivi, Bwana, Mungu wa Israeli, ahimidiwe, aliyenipa leo hivi mtu wa kuketi katika kiti changu cha enzi, nayo macho yangu yakiwa yanaona hayo (I Fal. 1:48).
>
> Na ahimidiwe Bwana, Mungu wa Israeli, tangu milele hata milele. Na watu wote wakasema, Amina; wakamhimidi Bwana (1 Nya. 16:36).
>
> Akasema Bwana, Mungu wa Israeli, ahimidiwe, aliyenena kwa kinywa chake na baba yangu Daudi, akalitimiza kwa mikono yake, akasema... (2 Nya. 6:4).
>
> Na ahimidiwe Bwana, Mungu, Mungu wa Israeli, Atendaye miujiza Yeye peke yake (Zab. 72:18).

Hata Yesu pia alijichukulia kuwa ni Mwalimu kwa ajili ya Wana wa Israeli. Kama wasiokuwa Waisraeli walimjia, basi yeye kawafukuzilia mbali. Katika Mathayo 15:21-26 twasoma:

> Yesu akaondoka huko akaenda pande za Tiro na Sidoni. Na tazama, mwanamke Mkananayo wa mipaka ile akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu Bwana, Mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo. Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwambia, wakisema, Mwache aende zake; kwa maana anapiga kelele nyuma yetu. Akajibu akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli. Naye akaja akamsujudia,

> akisema, Bwana, unisaidie. Akajibu, akasema, Si vyema kukitwaa chakula cha watoto na kukitupia mbwa.

Isitoshe, Yesu pia aliwaagiza wanafunzi wake akiwaambia:

> Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, wala msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, wakageuka na kuwararua (Mt. 7:6).

MA-VEDA HALI KADHALIKA NI VITABU VYA KITAIFA

Miongoni mwa wafuasi wa ma-Veda, kusoma ma-Veda kulikuwa kumefanywa kuwa ni haki ya Mabaniani sharifu kiasi hiki kwamba Gotama Rishi yuasema:

> Endapo Sudra (Baniani wa tabaka la chini kabisa) atasikia ma-Veda, basi mfalme anawajibika kumziba masikio yake kwa risasi na laka iliyoyeyushwa; endapo Sudra atasoma maneno ya Veda, basi mfalme anawajibika kuukatilia mbali ulimi wake, na endapo atajaribu kusoma ma-Veda, basi ni faradhi kwa mfalme kuukatakata mwili wake (Gotama Smrit 12).

Katika Veda mafundisho juu ya 'maadui' ni makali kupindukia na ya kikatili.

Ndani ya Atharva-Veda, Mabaniani sugu wanafundishwa kuwatia minyororo wale wasiokuwa wafuasi wa Veda na kuzipora nyumba zao:

> Yararue, chambilecho simba, makao yao yote, na chambileche chui wafukuzilie mbali maadui zako. Bwana wa pekee na kiongozi na uliyeungana na Indra, kamata na kutwaa mali za maadui zako. (Atharva-Veda IV, 22:7).

Kadhalika maombi ya ma-Veda yanayoombwa jua, mwezi, moto, Indra na hata nyasi, yanataka kuangamizwa kwa dini zisizo za Ki-Veda. Hivyo basi tunayo maombi haya:

> Huku ukizivuruga akili za maadui zetu, ikamate miili yao na kujiendea zako, Ewe Apva, washambulie, ziwashe moto nyoyo zao na kuziteketeza: basi waache maadui zetu wakae

katika giza tororo.

Huku ukinoa mshale wako na upanga wako mkali,

Ewe Indra, waponde maadui na kuwatawanya

wale watu watuchukiao" (Sama-Veda, Sehemu ya II, ix, iii, 9).

Enyi maadui zangu, mtakuwa vipofu na mtokee kuwa kama vile majoka yasiyokuwa na akili yalivyo: Indra na amuulie mbali kila mbora wenu, moto wa Agni utakapowateketezelea mbali (Sama-Veda Sehemu ya II, ix, iii, 8).

"Ewe Darbha, wapasulie mbali kwa njia ya talasimu, maadui zangu, nyoyo za maadui zangu;

"Inuka na uwapondeponde vichwa vyao" (Atharva-Veda XIX, 8:4).

Pia tunayo maombi haya:

"Usizungumze na wasioamini Veda"(Gotama-dharm. Sut.V).

Atokeapo yeyote kukosoa Ma-Veda, basi mtimulie mbali, yaani, mfunge maisha (Manu Dharm Shastra.).

Ukonfyushasi na Uzorasta nazo pia zilikuwa ni dini za kitaifa. Hazikutangaza Ujumbe wao kwa dunia nzima, wala hazikujaribu kuhubiri kwa kiwango chochote kikubwa. Kama vile dini ya Kibaniani inavyoichukulia India kuwa ndiyo imependwa na Mungu, ndivyo Ukonfyushasi uichukuliavyo Uchina kuwa ni ufalme wa Mungu Mwenyewe. Zipo njia mbili tu za kumaliza huu mgawanyiko na tofauti kati ya dini: ama tuamini ya kwamba kunao miungu wengi, au kama Mungu ni Mmoja, basi ni sharti tumthibitishe kuwa yuko hivyo. Au ni sharti tupaachilie mahali pa dini hizi zinazopinzana pachukuliwe na dini moja badala ya dini hizi.

MUNGU NI MMOJA

Dunia sasa imeendelea sana. Hatuna haja ya kujitahidi kuthibitisha kwamba iwapo dunia inaye Muuamba, Yeye ni Mmoja na yuaweza tu kuwa Muumbaji Mmoja. Mungu wa Israeli, Mungu wa Mabaniani,

Mungu wa Uchina na Mungu wa Iran sio Miungu mbalimbali. Wala Mungu wa Arabuni, wa Afghanistani, na yule wa Ulaya sio Miungu mbalimbali. Wala Mungu wa watu wa Mongolia na wa Wasemiti sio Miungu mbalimbali. Mungu Yu Mmoja, kama vile ilivyo mmoja ile kanuni ambayo chini yake dunia imetiishwa na kama vile ulivyo mmoja utaratibu unaounganisha sehemu yake moja na sehemu yake nyingine. Taaluma ya sayansi inajijenga juu ya imani ya kuwa mabadiliko yote ya kimaumbile na yale yatokeayo kwa athari za kisayansi ni madhihirisho ya kanuni moja. Dunia ina kanuni moja — mwendo — wasemavyo wanafalsafa wa kidunia au hii ina Muumbaji Mmoja. Kama hilo ni kweli, basi usemi kama vile Mungu wa Israeli, Mungu wa Waarabu, Mungu wa Mabaniani, hauna maana yoyote. Lakini kama Mungu ni mmoja, basi ni kwa nini tuwe na dini nyingi mbalimbali? Je, dini hizi zilibuniwa na akili ya mwanadamu? Je, ilikuwa ni kwa sababu hii ya kwamba kila taifa na kila kaumu waliabudu Mungu wao? Kama dini hizi hazikubuniwa na wanadamu, basi ilitokeaje hii tofauti baina ya dini moja na dini nyingine? Kama ilipata kuwepo sababu ya mgawanyiko huu, je, ilistahili kwamba mgawanyiko uendelee kuwepo?

DINI HAIKUTOKANA NA MAWAZO YA KIBINADAMU

Ama kuhusu swali kama dini hizi zilikuwa ni matokeo ya mawazo ya kibinadamu, jibu bila shaka ni kwamba dini hazikutokana na mawazo ya Kibinadamu na hii ni kwa sababu kadha:

Dini zilizostawi humu duniani zaonesha sifa bainishi kadha:

Kwanza, sawa na kiwango chochote cha maisha ya kawaida Waanzilishi wa dini walikuwa ni watu wenye hali ndogo. Hawakuwa na uwezo wala hadhi kubwa. Hata hivyo waliwahubiri watu wakubwa na watu wadogo na wakati ulipofika wao na wafuasi wao wakanyanyuka toka hali duni hadi hali iliyotukuka duniani. Hii inahakikisha kwamba walijaaliwa nguvu na kusaidiwa na Nguvu fulani kubwa.

Pili, Waanzilishi wote wa dini wamekuwa ni watu walioheshimiwa sana na kuthaminiwa kwa usafi wa maisha yao na hata kuthaminiwa

na wale watu ambao baadaye, walipotangaza madai yao, wakawa maadui zao. Ni jambo lisiloingia akili ya kuwa wale watu ambao hawasemi uwongo juu ya wanadamu, kwa ghafla waje kusema uwongo juu ya Mwenyezi Mungu. Kutambulikana duniani kote kwa usafi wa maisha yao kabla hawajatangaza madai yao ni thibitisho la ukweli wa madai yao. Kurani yasisitizia sana jambo hili ikisema:

> Hakika nimekwisha kaa kati yenu umri mwingi kabla ya haya, je, hamfahamu? (Sura Yuunus, 10:17).

Aya hii yamwonyesha Mtume Mtukufu[saw] kama mwenye kutamka akiwaambia watu waliomlaumu, 'Mimi nimeishi maisha yangu yote kati yenu, kama mmoja wenu. Mlikuwa na fursa kuniangalia kwa makini sana; mmekuwa wenye kushuhudia ukweli wangu. Sasa mnawezaje kusema kwamba leo nimeanza kwa ghafla kusema uongo juu ya Mwenyezi Mungu?

Vivyo hivyo Kurani yasema:

> Hakika Mwenyezi Mungu amefanya hisani juu ya waaminio alipoinua Mtume kati yao kutoka miongoni mwao (Sura Aali 'Imraan, 3:165).

Jambo hilo hilo lasisitiziwa katika aya isemayo:

> "Hakika amewafikieni Mtume kutoka miongoni mwenu" (Sura At-Tauba, 9:128)

Yaani, Mtume kwenu nyinyi, ambaye ni mmoja wenu, wala si mtu msiyemjua, bali mnayemjua sana na ambaye usafi wa tabia yake mmeushuhudia nyinyi wenyewe."

Hata kuwahusu Manabii minghairi ya Nabii Mtukufu[saw] wa Islam, Kurani yasema maneno hayo hayo. Waliinuliwa kutoka miongoni mwa watu wao. Isingeweza kusemwa kwamba wale waliowahubiria kwanza hawakuwajua Manabii hao vizuri. Watu wa Motoni watakapotumbukizwa humo, Mwenyezi Mungu atasema akiwaambia:

> Je, hawakuwafikieni Mitume kutoka miongoni mwenu

> wakiwasomeeni aya za Mola wenu, wakiwaonyeni kuhusu mkutano wa hii siku yenu? (Sura Az-zumar, 39:72)

Na pia:

> Enyi makundi ya Majini na watu. Je, hawakuwafikeini Mitume toka miongoni mwenu waliowabainishieni Aya Zangu na waliowaonyeni kuhusu mkutano wa Siku yenu hii? (Sura Al-An'aam 6:131).

Mahali pengine twasoma maneno haya:

> Na Tukawapelekea Mtume kutoka miongoni mwao, aliyesema (akiwaambia), Mwabuduni Allah. Hamna Mungu minghairi ya Yeye (Sura Al-Mu'minuun, 23:33).

Halafu:

> "Na (kumbukeni) siku Tutakaposimamisha shahidi kutoka kila Umati" (Sura An-Nahl 16:85).

Neno "shahidi" lililotumiwa hapa lamaanisha Nabii aliyeinuliwa kwa ajili ya watu. Siku ya Hukumu, Manabii watajidokezea wenyewe kama thibitisho bayana la yale ujumbe wa Mwenyezi Mungu uliyowafanyia. Mwenyezi Mungu atawafedhehesha makafiri, Akisema, "Hebu angalieni alichofikia Nabii Wangu, na kule utovu wenu wa imani ulikowapelekeni". Manabii wote, tunavyoambiwa, waliinuliwa toka miongoni mwa watu wao. Hali za kimazingara alimolelewa kila mmoja wa Manabii na vile kila mmoja wa Manabii alivyozichukulia umati wake ulijua sana. Kwa hivyo, kila umati ulikuwa ni shahidi wa utawa na unyofu wa Nabii wao. Pamoja na hayo pia tunazo katika Kurani aya kama hizi zifuatazo:

> "Na kwa Waadi Tulimtuma ndugu yao Huud". (Sura Al-A'raaf, 7:66)

> "Na kwa Wathamud Tulimtuma ndugu yao Saleh"(Sura Al-A'raaf, 7:74).

> "Na kwa Wamadiani Tulimtuma ndugu yao Shuaibu"(Sura Al-A'raaf, 7:86).

Aya zenyewe zamaanisha kwamba Hadhrat Hud[as], Saleh[as] na Shuaibu[as] walikuwa na hali ya kujulikana sana na watu wao hivi kwamba wangeweza kusemwa kuwa watu hao walijua kila kitu kuwahusu. Kumhusu Nabii Saleh[as] twasoma ya kuwa pale yeye alipojitangaza kuwa kama Nabii kwa watu wake, aliambiwa:

> Ewe Saleh, ulikuwa miongoni mwetu mtu tuliyemtumainia. Je, watukataza kuabudu vile walivyoviabudu mababu zetu? (Sura Huud, 11:63)

Vivyo hivyo, watu wa Nabii Shuaibu[as] walitamka wakimwambia Nabii Shuaibu[as]:

> Ewe Shuaibu, je, Sala yako yakuamrisha kwamba sisi tuviache vile walivyoviabudu mababu zetu, au kwamba tuache kufanya na mali zetu vile tupendavyo. Kwa hakika wewe u mwenye busara na mwongofu (Sura Huud, 11:88).

Kutokana na aya hizi ni wazi kwamba, kulingana na Kurani, Mtume Mtukufu[saw] mwenyewe, na Manabii Huud[as], Saleh[as], Shuaibu[as] na Manabii wengine[as], hawakuwa ni watu wasiojulikana sana kwa watu wao. Kaumu zao walijua vyema ni aina gani ya maisha Waalimu wao waliyoishi na kama hawakuwa watu waaminifu, wacha-Mungu na wanyofu. Hapana mmoja wao ambaye anaweza akasemekana kwamba mtaka makuu asiyeeleweka aliyatafuta kuwadanganya watu wake.

Tatu, Waanzilishi wa dini hawakuwa na ule uwezo na ustadi ambao kwa kawaida huchangia uongozi wa mafanikio. Mambo ya utamaduni na sanaa za wakati wao waliyajua kidogo au hawakuyajua kabisa. Hata hivyo kile alichofundisha kila mmoja wao kilitokea kuwa kitu kilichotangulia wakati wake, kitu mwafaka na kifaacho. Baada ya kufuata mafundisho haya watu walipata ustaarabu mkubwa na utamaduni, na wakabakia na fahari hii kwa karne nyingi. Mwalimu mkweli wa dini huyafanya haya yawezekane. Hata hivyo ni jambo lisiloingia akilini kwamba mtu mkosa makuu ya kawaida, mara aanzapo kusema uwongo juu ya Mwenyezi Mungu, atokee kupata uwezo mkubwa kiasi hiki kwamba mafundisho yake yayashinde

mafundisho mengine yote ya wakati wake. Matukio sampuli hiyo hayawezekani bila ya msaada wa Mungu Mwenye uwezo mkubwa.

MAFUNDISHO YALIYOFUNULIWA DAIMA HUWA KINYUME NA MAWAZO YALIYOPO

Nne, tuyatafakariapo yale waliyoyafundisha Waanzilishi wa dini, twakuta kwamba daima yamekuwa ni kinyume na mienendo yote iliyokuwepo. Kama mafundisho haya yangalikuwa yameafikiana na mitindo ya maisha ya nyakati zao, ingeweza kusemewa kwamba waalimu hawa walionesha sura ya mitindo ya maisha hayo. Badala yake, waliyoyafundisha yakawa ni tofauti kabisa na chochote kile walichokuta kikiweko. Ugomvi hatari ukazuka, ikaonekana kana kwamba nchi imewashwa moto. Hata hivyo, wale waliokana na kuyapinga mafundisho hayo wao wenyewe hatimaye walilazimika kuyakubali. Hii yathibitisha pia ya kwamba Waalimu hawa hawakuwa ni matokeo ya nyakati zao, bali walikuwa ni Waalimu, Mujadidina na Manabii kama vile wao wenyewe walivyodai.

Wakati wa Nabii Musa[as], yalionekana kuwa ya kigeni namna gani mafundisho yake juu ya Mungu Mmoja. Wakati Yesu alipokumbana katika zama zake na imani katika maada tu na kutosadiki kuwepo kwa roho — iliyotokana na tabia ya Mayahudi ya kupenda dunia na athari mbaya ya utawala wa Roma — kulionekana ya ajabu jinsi gani kukazania kwake mambo ya kiroho? Ni sharti uwe ulionekana usiofaa kiasi gani ujumbe wake wa msamaha machoni mwa watu waliotetemeka chini ya udhalimu wa askari wa Kirumi, huku wakati wote wakililia uhalali wa kujilipiza kisasi? Krishna alitokea namna gani wakati usiofaa aliyefundisha kupigana vita, kwa upande mmoja na kwa upande mwingine, kufundisha kujitenga mbali na dunia ili kustavisha hali ya kiroho. Mafundisho ya Kizorasta, yaliyogusia jiha zote za maisha ya binadamu pia ni lazima yawe yaliushtua ufisadi wa wakati ule. Mtume Mtukufu[saw] alidhihiri huko Uarabu na akawahubiria Mayahudi na Waarabu. Hili ni sharti liwe lilionekana kuwa jambo la kigeni sana kwa wale walioamini kwamba hayatatokea mafundisho mengine nje ya mafundisho yao hao wenyewe. Kisha

yeye akawafundisha watu wa Makka waabudu masanamu ya kuwa Mungu ni Mmoja, na kwamba watu wote ni sawa. Mafundisho haya yake ni sharti yawe yalionekana kuwa ya kigeni sana kwa watu walioamini kabisa ubora wa taifa lao. Kufundisha walevi wa kupindukia, na wacheza kamari ubaya wa mienendo yao, kukosoa kila kitu walichoamini au kufanya, kuwapatia mafundisho mapya na kisha kufaulu, kwaonekana kusikowezekana. Ni chambileche kuweza kuogelea dhidi ya mkondo uendao kwa kasi sana. Ni kitu kilichokiuka kabisa uwezo wa kibinadamu.

Tano, Waanzilishi wote wameonyesha Ishara na miujiza. Kila mmoja wao alitangaza mwanzoni kabisa kwamba mafundisho yake yatafanikiwa na kwamba wale ambao huenda wakatafua kuyaangamiza wataangamizwa wao wenyewe. Hawakuwa na njia wala hawakujiandaa vilivyo. Mafundisho yao yalikwenda kinyume na imani sugu na mazoea ya fikara za watu na yalizusha upinzani mkali sana wa watu wao. Hata hivyo walifaulu, na kile walichokuwa wamekitabiri kikatokea. Kwa nini bishara zao na ahadi zao zikatimia? Bila shaka wamepata kuwepo wengine, majemadari na madikteta ambao walionekana kupata ufaulu kama huo huo. Lakini kinachozungumziwa hapa sio ufaulu. Bali ni ufaulu uliotabiriwa, unaohusishwa na Mwenyezi Mungu tangu mwanzoni, ufaulu mnamoegemezwa hadhi nzima ya Nabii mwenyewe na unaopatikana licha ya upinzani ulio mkali mno. Akina Napoleon, Hitler na Chingiz Khan walinyanyuka juu kuanzia na hali dhaifu. Lakini wao hawakusimama dhidi ya wazo lolote lililokuwepo la wakati wao. Wala hawakutangaza ya kuwa Mwenyezi Mungu Akawaahidia ushindi licha ya upinzani uliokuwepo. Wala haikuwabidi kukabiliana na upinzani uliotapakaa sana. Malengo waliyonuia kuyatimiza yaliwavutia wenzao wa zama hizo ambao pengine walipendekeza njia nyinginezo lakini sio malengo tofauti. Kama walishindwa, hata hivyo hawakupoteza chochote. Wao bado walikuwa na taadhima machoni mwa watu wao wala hawakuhofia chochote. Kulikuwa na tofauti kuwahusu Manabii Musa, Yesu, Krishna, Zorasta na Mtume Mtukufu[saw] wa Islam.

Kweli, wao hawakufeli. Lakini kama wangelifeli, basi wao wangelipoteza kila kitu. Wasingelikuwa wametangazwa kuwa ni mashujaa, bali wangelikuwa wamelaumiwa kama wazushi na wachochezi. Historia ingaliwajali kidogo na lawama ya kudumu ndiyo ingelikuwa malipo yao. Hivyo basi, baina yao na watu kama vile akina Napoleon na Hitler, pana chungu nzima ya tofauti — tofauti ile ile kama iliyopo baina ya na ufanisi wao. Hakuna watu wengi wanaomjali au kumheshimu Napoleon, Hitler au Chingiz Khan. Baadhi ya watu wanawachukulia kuwa ni mashujaa na wanayafurahia sana matendo yao. Lakini je wanaweza wakavutia uaminifu halisi wa watu au utiifu halisi? Uaminifu na utiifu ni mambo wanayojaaliwa Waalimu wa dini peke yao, kama vile Manabii Musa, Yesu, Krishna, Zoroasta na Mtume Mtukufu[saw] wa Islam. Watu milioni nyingi wamefanya katika zama zote yale Waalimu hawa waliyowambia kufanya. Mamilioni ya watu wamejinyima yale waliyoyakatazwa Waalimu hawa. Mawazo yao hata yale madogo madogo, maneno na matendo yao yametawaliwa na yale waliyoyafundishwa na viongozi wao. Je, mashujaa wa kitaifa huvutia hata angalau chembe moja ya huu uaminifu na utiifu unaofanyiwa Waalimu hawa? Hivyo basi, Waalimu hawa walitoka kwa Mungu na yale waliyoyafundisha yalifundishwa na Mwenyezi Mungu.

KWA NINI MAFUNDISHO YA DINI MBALIMBALI YANATOFAUTIANA

Lakini swali ni kwamba kama Waalimu hawa wote walitoka kwa Mungu, ni kwa sababu gani mafundisho yao yanatofautiana sana hivyo? Je, Mwenyezi Mungu Angeweza kufundisha mambo tofauti nyakati tofauti? Hata wanadamu tu wa kawaida hujaribu kuwa na msimamo mmoja na hufundisha mambo yale yale katika nyakati mbalimbali. Jibu la swali hili ni kwamba hali zinapobakia vile vile, ingelikuwa ni upuuzi kutoa maagizo tofauti tofauti. Lakini hali zinapobadilika, kubadili mafundisho ndiyo hekima yenyewe. Wakati wa Nabii Adamu[as], yaonekana, wanadamu waliishi pamoja katika sehemu moja ya dunia; kwa hiyo sampuli moja ya mafundisho

iliwatosha. Pengine hadi zama za Nabii Nuhu[as] wao waliendelea vivi hivi. Kulingana na Biblia, wanadamu waliendelea kuishi pamoja katika sehemu moja ya dunia hadi nyakati za Babeli. Biblia sicho kitabu cha historia. Lakini panao ushahidi wenye kuunga mkono masimulizi haya ya Biblia.

Katika mataifa yote duniani, hata miongoni mwa washenzi waishio katika visiwa pweke baharini, twakuta alama za habari za Gharika ya Nabii Nuhu[as]. Haielekei kwamba dunia nzima kwanza ilifunikizwa na gharika iliyoenea kotekote, na kisha habari zake zikaenea katika kila pembe ya dunia. Pana uwezekano zaidi kwamba katika sehemu moja ya dunia ilitokea gharika iliyosababisha mtawanyiko wa watu kuelekea pande mbalimbali. Kama isipothibitishwa kwamba dunia ilikuwa ni moja hadi zama za Wababiloni, historia yaunga mkono rai ya kwamba ilikuwa moja hadi kufikia zama za Nabii Nuhu[as]. Baada ya zama za Nabii Nuhu[as] wakazi wakatawanyikia nchi mbalimbali. Athari ya mafundisho ya Nabii Nuhu[as] ikaanza kufifia, kwa kuwa njia za mawasiliano zilikuwa duni mno. Mwalimu katika nchi moja hakuweza kufikisha Ujumbe wake hadi nchi nyingine. Basi, ilistahili kabisa kwamba Mwenyezi Mungu Awe Alipeleka Nabii katika kila nchi, kusudi iwe haitakuwepo nchi isiyokuwa na mwongozo Wake. Hii ikasababisha mgawanyiko baina ya dini na dini nyingine, kwani akili ya mwanadamu ilikuwa bado haijapevuka. Kwa kuwa akili na fahamu za mwanadamu hazikuwa na ule upevu ambao zilikuwa zije ziupate baadaye, kila nchi ilikuwa na mafundisho iliyoyapelekewa yaliyoafikiana na kiwango cha ustawi ilichokuwa imekifikia.

ISLAM YAFUNDISHA UMOJA WA MUNGU NA WA WANADAMU

Lakini jamii ya wanadamu ilipoanza kupata maendeleo, na nchi nyingi zaidi kuanza kukaliwa, na umbali baina yao kuanza kutoweka, na njia za mawasiliano kuanza kuimarika, akili ya mwanadamu ikaanza kutambua haja ya kuwepo mafundisho kwa ajili ya wanadamu wote, yenye kugusia hali zote mbalimbali za mwanadamu. Kwa njia ya kuwasiliana wao kwa wao watu wakaja kudhihirikiwa na

umoja wa kiasili wa jamii ya wanadamu na Umoja wa Muumba na Mwongozi wao. Kisha katika jangwa la Uarabu, Mwenyezi Mungu Akapeleka Ujumbe Wake wa mwisho kwa njia ya Mtume Mtukufu[saw] wa Islam. Si ajabu kwamba Ujumbe huu waanza kwa kumhimidi Mungu Mola wa walimwengu wote. Wazungumzia juu ya Mungu Ambaye aina zote za hamdi ni Zake, Mwenye kupeleka msaada Wake kwa watu wote na nchi zote na kwa kadiri inayostahili. Yeye haipendelei nchi yoyote au taifa lolote. Hivyo basi, ule ujumbe wenye kuanzia na hayo hapana budi wamalizia na kumwomba Mola wa wanadamu wote, Mfalme wao na Mungu wao. Nabii aliyeleta ujumbe huu alikuwa ni Adamu wa pili. Kama vile katika wakati wa Adamu wa Kwanza palikuwepo na ufunuo mmoja wa Mungu na jamii moja, vivyo hivyo katika wakati wa huyu Adamu wa pili dunia kwa mara ya tena ikawa na ufunuo mmoja na ikawa jamii moja. Kwa hiyo, ikiwa dunia hii imeumbwa na Mungu Mmoja, na kama Mwenyezi Mungu anawajali watu wa mataifa yote na nchi zote kwa usawa, basi ni jambo la lazima kwamba mataifa haya mbalimbali yenye desturi mbalimbali za kidini hatimaye yawe yataungana katika imani moja na katika mtazamo mmoja. Kama Kurani isingelikuja, ile shabaha ya kiroho ambayo kwa ajili yake wanadamu walikuwa wameumbwa ingalibatilika. Kama dunia haiwezi ikakusanyika kwenye kitovu kimoja cha kidini, je tutaweza kweli wakati wowote kuutambua Umoja wa Mungu? Mto unavyo vijito vingi lakini hatimaye huishilizia kuwa mto mpana na ni hapo ambapo nguvu za mto huo na uzuri wake hujitokeza. Ule Ujumbe ambao Manabii Musa, Yesu, Krishna, Zoroasta na Manabii wengineo[as] waliziletea sehemu mbalimbali za dunia wafanana na vijito vinavyojitokeza kabla mto wenye nguvu kujifanyizia mkondo wake. Ujumbe huo wote ulikuwa mzuri na unaofaa. Lakini ilikuwa lazima kwamba Ujumbe huo hatimaye utiririke kwenye mto mmoja, na kuonesha Umoja wa Mungu na kuendeleza ile shabaha ya mwisho ambayo kwa ajili yake wanadamu walikuwa wameumbwa. Na kama Kurani haitimizi shabaha hii, basi yako wapi yale mafundisho yanayoitimiza? Siyo Biblia, kwani Biblia

yazungumzia Mungu wa Waisraeli peke yake. Wala si mafundisho ya Zoroasta, kwa sababu Hadhrat Zoreasta[as] yualeta nuru ya Mwenyezi Mungu kwa watu wa lrani peke yao. Wala si ma-Veda, kwa sababu Marishii wanawatolea adhabu ya kutia risasi iliyoyeshwa katika masikio ya Mashudra — Wahindi asilia — ambao ni jasiri kiasi cha kuweza kusikiza usomaji wa Veda. Wala Hadhrat Budha hatimizi shabaha hii, kwa sababu ingawaje mafundisho ya Budha yalienea Uchina baada ya kifo chake, lakini hata hivyo mpango wake yeye mwenyewe haukuvuka nje ya mipaka ya India. Wala mafundisho ya Yesu[as] hayatimizi shabaha hii.

YESU SI MWALIMU WA DUNIA NZIMA

Yesu yuasema:

> Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiza. Kwa maana, amini, nawaambia, mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie (Mt.5:17-18).

Yale ambayo ameyafundisha Nabii Musa na Manabii wengine wa awali juu ya jambo hili, tayari tumeisha yaeleza. Wamishonari wa Kikristo wamekwenda sehemu zote za dunia, lakini Yesu mwenyewee hakuwa na mpango sampuli hiyo. Swali lenyewe sio kwamba waumini wa Kikristo wanajaribu kufanya nini. Swali linalozungumziwa ni kwamba je, ni nini aliyokuwa ananuia Yesu mwenyewe? Ni nini alichokusidia Mwenyezi Mungu Aliyemtuma Yesu? Hiki hapana awezaye kukieleza vizuri zaidi ya Yesu mwenyewe, na Yesu alisema waziwazi:

> "Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" (Mat. 15:24). "Kwa maana Mwana wa Adamu alikuja kukiokoa kilichopotea" (Mat. 18:11).

Hivyo basi mafundisho ya Yesu ni kwa ajili ya Waisraeli peke yao, si kwa ajili ya watu wengine. Yasemekana kwamba Yesu aliwashauri wafuasi wake kuyaendea mataifa mengine, akiwaambia:

> Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu (Mat. 28:19).

Lakini kudai kutokana na maneno haya kwamba Yesu alikuwa amewaamuru wafuasi wake kuwafikishia Ujumbe wake watu minghairi ya taifa la Waisraeli sio sawa. Maneno haya ya Yesu yanamaanisha hivi tu ya kwamba wafuasi wa Yesu waliamriwa naye kuhubiri Ujumbe wake kwa makabila yote ya Waisreli wala sio kwa mataifa yote na kwa watu wote kama walivyo. Yesu yuaongea kinagaubaga:

> Amin, nawaambia ya kwamba ninyi mlionifuata mimi, katika ulimwengu mpya, atakapoketi Mwana wa Adamu katika kiti cha utukufu wake, ninyi mtaketi katika viti kumi na viwili, mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli (Mat. 19:28).
>
> "Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" (Mat. 15:24).
>
> "Si vyema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa" (Mat. 15:26).

Kisha twasoma haya:

> Hao thenashara Yesu aliwatuma, akiwaagiza, akisema, Katika njia ya Mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie, afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli" (Mat. 10:5-6).

Na asidhani mtu yeyote eti shabaha iliyopo hapa ni kwamba wahubiri wa Kikristo kwanza waiendee miji ya Waisraeli, halafu miji mingine. Kwani kuwaendea kondoo waliopotea wa Israeli hakumaanishi kuitembelea miji yao tu, bali kuwaingiza Ukristoni. Neno zima hasa ndio kwamba hadi pale Waisraeli watakapokuwa wamebatizwa, watu wengine wasijaliwe kabisa. Yesu yuasema wazi wazi kwamba kazi ya kuwahubiria Waisraeli na kuwabatiza haitamalizika hadi Ujaji wake wa Mara ya Pili. Ndiposa twasoma:

> Lakini watakapowafukuza katika mji huu, kimbilieni mwingine;

> kwa maana ni kweli nawaambia, Hamtaimaliza miji ya Israeli, hata ajapo Mwana wa Adamu (Mat. 10:23).

Kutokana na maneno haya ni wazi kwamba Mathayo 28:19 yawataka wahubiri wa Kikiristo kuimarisha Ukristo katika miji ya Waisraeli wala sio kuetembelea tu. Yasemwa kinagaubaga kwamba hii kazi ya kuwahubiria Waisraeli haitakwisha hadi Ujaji wa Mara ya pili. Kwa hiyo wanapowahubiria wengine, ilhali Ujaji wa Yesu wa Mara ya Pili bado haujatukia, wahubiri wa Kikristo wanakwenda kinyume na mafundisho ya Yesu. Hata wanafunzi wa Yesu nao pia wanaona sio sawa kuihubiri Injili kwa wasiokuwa Waisraeli. Ndiposa twasoma hivi:

> Basi wale waliotawanyika kwa sababu ya ile dhiki iliyotukia kwa habari za Stefano, wakasafiri hata Foinike na Kipro na Antokia, wasilihubiri lile neno ila kwa Wayahudi peke yao (Mdo. II 19).

Vivyo hivyo, wanafunzi waliposikia kwamba mahali fulani Petro alikuwa ameihubiri Injili kwa wasiokuwa Waisraeli, waliudhika. Imeandikwa:

> Na Petro alipopanda kwenda Yerusalemu, wale walio wa tohara wakashindana naye, wakisema, Uliingia kwa watu wasiotahiriwa ukala nao (Mdo, 11:2-3)

Hivyo basi, kabla ya Mtume Mtukufu[saw] wa Islam, hapana aliyefikisha Ujumbe kwa wanadamu wote; kabla ya Kurani, hapana kitabu kilichojishugulisha na wanadamu wote. Ni Mtume Mtukufu[saw] aliyetangaza akisema:

> "Enye watu, hakika mimi ni Mtume wa Mungu kwenu nyote (Sura Al-A'raaf, 7:159).

Kwa hiyo, ufunuo wa Kurani ulikusudiwa kuondolea mbali tofauti na migawanyiko iliyokuwa imetokea baina ya dini na dini nyingine na baina ya taifa na taifa jingine na ambayo kwanza ilikuwa imetokea kutokana na ule upungufu uliolazimu wa mafundisho ya hapo mbeleni. Isingelikuja Kurani, migawanyiko hii ingelikuwa imedumu. Dunia isingelipata kujua hata kidogo ya kwamba ina Muumba Mmoja

tu, wala isingelipata kutambua abadan kwamba kuumbwa kwake kulikuwa na shabaha moja pana iliyonuiwa. Tofauti kati ya dini kabla ya Islam zaelekea kutaka wala sio kukinza ujaji wa Mafundisho yasiyokuwa na budi kuziunganisha dini zote.

Swali la pili ni je, haikuwa akili ya mwanadamu ipitie utaratibu wa mabadiliko sawa na ule uliokuwa mwili wa mwanadamu tayari umeupitia? Na kama vile ambavyo mwili wa mwanadamu ulikuwa hatimaye umefikia hali fulani ya kikomo cha umbo, je, haikuwa akili (na roho) ya mwanadamu kutokuwa na budi nayo pia ifikie hali ya kikomo iliyokuwa ndiyo hatima yake?

MAANA YA USTAARABU NA UTAMADUNI

Katika kulijibu swali hili ni sharti tukumbuke kwamba tuchunguzapo kwa kurudi nyuma ustaarabu na utamaduni wa nchi mbalimbali, twakuta kwamba zimekuwepo nyakati mbalimbali zilimopitia nchi hizo. Baadhi ya nyakati hizi zimekuwa ni zenye kujipatia maendeleo kiasi hiki kwamba baina yao na huu wakati wetu ni kana kwamba kuna tofauti kidogo au hapana tofauti. Kama tukiacha kando maendeleo ya mitambo ya dunia ya kisasa, maendeleo ya badhi ya nyakati zilizotangulia za historia ya mwanadamu yaelekea kutofautiana kidogo tu na maendeleo ya wakati wetu. Katika nyanja zote mbili za ustaarabu na utamaduni hali hizo za kufanana zipo. Lakini tukizama ndani vya kutosha, tutakuta tofauti mbili muhimu baina ya nyakati zilizotangulia na nyakati za kisasa.

Kabla hatujazielezea tofauti hizi mbili, twataka kubainisha tunachokielewa kwa ustaarabu na utamaduni. Sawa na maoni yetu, ustaarabu ni wazo la mambo ya kidunia kabisa. Yanapopatikana maendeleo ya kidunia, basi hupatikana katika shughuli za kibinadamu hali fulani ya ulinganifu na pia hali fulani ya urahisi wa mambo. Hali hii ya ulinganifu katika shughuli za watu na urahisi wa mambo huwa ndio ustaarabu. Uzalishaji unaotokana na kazi za kibinadamu, na njia za usafiri zinazohitajika kusombea mazao haya kutoka mahali pamoja hadi mahali pengine huwa ndiyo maendeleo katika ustaarabu. Vivyo

hivyo, mbinu zozote zinazoweza kugunduliwa za kupokezana bidhaa mkono kwa mkono, taratibu zote zinazoweza kuwekwa kustawishia elimu, viwanda, utafiti wa kisayansi, huwa ni maendeleo katika ustaarabu. Chochote kinachoweza kufanywa kulinda usalama wa ndani na kujihami dhidi ya chokochoko za nje huwa ndio ustaarabu wenyewe. Haya yote ni mambo yenye kuathiri shughuli za kibinadamu. Ile nchi iliyopiga hatua katika mambo haya huwapatia wakazi wake mtindo wa maisha ya kila siku unaotofautiana kabisa na ule wa nchi zingine. Ni tofauti hii ambayo huwa ndiyo tofauti katika ustaarabu. Katika nchi isiyokuwa na ustawi wa kilimo chakula cha wakazi wake kitakutwa kikitofautiana sana na chakula cha watu wa nchi iliyopiga hatua kubwa katika uwanja wa kilimo. Nchi iliyo na maendeleo makubwa ya kilimo hutilia shime ulaji wa aina nyingi za vyakula. Itajaribu kutosheleza haja na hamu za aina mbalimbali. Lakini nchi isiyokuwa na maendeleo makubwa ya kilimo, haitaweza kutoa vitu hivyo mbalimbali. Katika nchi kama hiyo hazitatiliwa maanani tofauti za watu katika siha za kimwili au hamu ya lishe bora. Chakula chochote kile nchi inacholima kwa jumla kitatolewa hicho hicho, bila ya hiari ya kuchagua kinginecho au vinginevyo vingi. Vivyo hivyo, nchi yenye hali duni ya viwanda haitaweza kulingana na nchi yenye ustawi mkubwa wa viwanda, kwenye uwanja wa mavazi, maskani na vifaa vya nyumbani na katika masurufu mengine ya maisha ya raha mustarehe.

Ile nchi isiyokuwa na maendeleo makubwa ya kiviwanda haitaweza kutoa nguo za kutosha kwa wakazi wake. Suala la nguo zishonwe mshono gani halitakuwepo. Watu wa nchi hiyo hata hawatajua koti lenyewe ni kitu gani, achilia mbali kujua aina mbalimbali za makoti yenye kuafikiana na hafla mbalimbali. Hata nguo kama vile shati litakuwa ni ghali sana kwao. Viatu vya ngozi ya mwanambuzi havitakuwemo akilini mwao. Kukazania viatu vilivyotengenezwa kwa ngozi ghafi kwao wao kitakuwa ni kitu cha anasa. Bali hata wazo lenyewe la viatu halitakuwa jambo la kawaida. Wenyeji wa nchi hiyo kwa kawaida watatembea bila ya viatu, au wao watatosheka na kipande

cha ngozi ghafi kisichokuwa na sura ya kiatu kilichofungiwa nyayoni mwao. Twayakariri mambo haya bila kunuia. Hatuwezi kuelezea kwa kirefu, lakini tafsili kidogo sana inahitajika kuthibitisha kwamba tofauti kama hizo katika mitindo ya kinje ya maisha yetu ni matokeo ya tofauti katika kiwango cha maendeleo yanayoyapata mataifa mbalimbali katika nyanja za kilimo, viwanda, sayansi na elimu. Tofauti zenyewe ni kubwa kiasi hiki kwamba wale waliozoea aina moja ya maisha hawatatamani kuchanganyikana na wale waliozoea aina nyingine ya maisha. Ni tofauti hizi ambazo, sawa na maoni yetu, ndizo tofauti za ustaarabu na ni tofauti hizi ambazo masaala ya amani na vita yanazitegemea kwa kiasi kikubwa. Ni tofauti hizi ambazo hatimaye husababisha njama za kikoloni na tamaa za kujipatia mamlaka.

Utamaduni watofautiana na ustaarabu. Utamaduni, kwetu sisi, unahusiana na ustaarabu sawasawa kabisa na vile roho ya mtu inavyohusiana na mwili wake. Tofauti za ustaarabu hatimaye kabisa ni tofauti za maendeleo ya kimwili; lakini tofauti za utamaduni zatokana na tofauti za maendeleo ya kiroho. Utamaduni wa watu unaweza kusemewa kuwa ni yale mawazo na amali ambavyo humea chini ya athari za mafundisho ya kidini au mafundisho ya maadili. Mafundisho ya kidini huweka misingi. Hapo wafuasi wa mafundisho hujenga juu ya misingi hiyo. Katika kujenga kwenye misingi hiyo, wafuasi wanaweza wakatokomea mbali na mafundisho ya asili, lakini katu hawawezi wakaachana kabisa kabisa na misingi ile. Mtu ajengaye sawa na ramani ya jengo anaweza akatetereka apendavyo mbali na ramani yenyewe, lakini hata hivyo hawezi kutozijali sehemu muhimu za ile ramani. Vivo hivyo, dini na mawazo huweka misingi ya maisha. Wanachokijenga wafuasi wa dini hizo na mawazo hayo juu ya msingi wa hapo awali hujipatia sura za mitindo mbalimbali ya sanaa na maadili, hivi kwamba mwenye kutazama hana budi kuwaweka wafuasi wa dini mbalimbali katika makundi yanayotofautiana kabisa. Tofauti hizi ni tofauti za utamaduni. Tofauti za utamaduni zimekuwa muhimu mno hivi leo. Kutetea na kudai ustahamilivu na upana wa mawazo ni jambo la kawaida sana hivi leo. Licha ya hayo Mkristo wa

jina tu kivingine ni mkana Mungu, atachanganyikana kwa urahisi sana na Mkristo mshupavu wa dini kuliko vile atakavyochanganyikana na Mwislamu wa jina, kivingine ni mkana Mungu, au kuchanganyikana na Mwislamu mshupavu wa dini. Hapana shaka ya kwamba katika huu wakati wetu misimamo ya kisiasa nayo pia yatawala uhusiano wa pamoja wa watu, na misimamo hii ya kisiasa yatokana na tofauti za ustarabu.[2] Mzungu Mwislamu ni mkunjufu sana kwa Mwislamu wa Bara la Asia; ukunjufu amwonyeshao Mwislamu mwenzake, hamwoneshi kabisa Mzungu mwenzake. Mzungu Mkristo mshupavu wa dini yu mkunjufu kwa Mmarikani mkana Mungu. Je hili kwa kweli ni kwa sababu ya kupendelea dini? La, hasha. Kama yangelikuwepo mapendeleo ya kidini peke yake, basi Mkristo angelijiona karibu sana na moyo wa Mwislamu kuliko ule wa mkana Mungu. Ukweli wenyewe ni kwamba baina ya Mkristo na Mkristo, hata kama mmoja wao awe ni mkosa dini, kunayo mafungamano ya utamaduni, tunaweza tukauita utamaduni wa Kikristo. Mkosa dini wa Kikristo si Mkristo tena katika itikadi za kidini lakini maono yake na matendo havikuepukana na athari ya utamaduni wa Kikristo. Athari zinazojiendeleza zenyewe kwa vizazi vingi hazifutiki kwa urahisi! Mwanasanaa Mkristo ambaye pengine kimawazo amekuwa ni mkana Mungu hata hivyo ataonesha athari ya Kikristo kwenye kuchora picha zake na muziki wake. Kwa kweli, ni bahati kuwa na hiyo athari, waila sanaa yake isingelipendeza chambileche mibaruti katika bustani ya mawaridi.

VIPINDI MBALIMBALI VYA USTAARABU NA UTAMADUNI

Sasa twataka kuainisha kwamba vipindi vya ustaarabu na utamaduni wakati mwingine huja kimoja baada ya kingine na wakati mwingine huja kwa pamoja. Wakati mwingine huja vikitengana na wakati mwingine huja vikijumuika pamoja. Pana wakati ambapo taifa hupata ustaarabu mkubwa lakini kutopata utamaduni wa hali ya juu; na pengine hupata utamaduni wa hali ya juu lakini kutopata ustaarabu mkubwa. Roma katika enzi yake ilikuwa na ustaarabu mkubwa; lakini

[2] Lakini tofauti za utamaduni sio kwamba zina umuhimu kidogo.

haikuwa na utamaduni. Sanaa na falsafa zake hazikutokana na msingi wa wazo lolote. Kila mtu alikuwa huru kujiendeleza kivyake na kuyaelezea maisha bila kutilia maanani kanuni zozote zile kubwa na za kimsingi. Katika karne zake chache za awali za kuwepo kwake Ukristo haukuipatia dunia ustaarabu wowote lakini uliipatia utamaduni wa hali ya juu, utamaduni uliotokana na mtazamo thabiti wa maisha na ambao kwa kulingana na hayo ulikuwa na sifa za namna yake. Wakristo wa awali waliambatanisha shughuli zao na kanuni fulani; maisha yao yaliwekewa mipaka kwa vizuizi fulani. Kanuni hizi na vizuizi hivi waliviwekewa na mafundisho yao ya kidini. Kwa upande mwingine, kanuni na vile vizuizi zilimoangazia fikara za Mrumi vilitawaliwa na tamaa za kidunia. Kwa neno zima, Roma ya hapo awali ilikuwa ni mfano mzuri wa ustaarabu na Ukristo ulikuwa ni mfano sampuli hiyo hiyo wa utamaduni. Baadaye, katika Roma ustaarabu na utamaduni vikachanganyika pamoja. Wakati Roma ilipoingia Ukristo, ilikuwa na ustaarabu na utamaduni vyote viwili, lakini ustaarabu wake ulikuwa umekaliwa na utamaduni wake. Leo hii Ulaya inao ustaarabu na utamaduni pia lakini, kutokana na kutapakaa kwa mawazo ya kidunia, utamaduni wake umekuja kukaliwa na ustaarabu wake. Tunapoitalii historia ya dunia, twakuta kwamba zile nyakati ambapo dini imefaulu katika kujenga falsafa halisi ya maadili au utamaduni halisi zaonekana zilikuwa zimefanana na wakati huu wetu sisi. Vivyo hivyo, zile nyakati ambapo hali ya kuizamia dunia maishani imejenga ustaarabu halisi zaonekana zilikuwa zimefanana sana na hizi zetu. Lakini tofauti mbili zaonekana zajitokeza sana. Ustaarabu na utamaduni uliozuka kabla ya ujaji wa Islam haukuwa wa kidunia nzima kwa sura wala wazo lenyewe. Ustaarabu na utamaduni wenyewe havikuwa vimetokana na kanuni za kidunia nzima. Dini na ustarabu havikufanana na matawi yakichipuka kutoka shina moja. Kama vilipata kuonekana kufanana, basi vilikosa umoja halisi. Katika dini ya Kiyahudi, hapana shaka, juhudi imefanywa kujumuisha ustaarabu na utamaduni. Katika Agano la Kale, kwa kiasi kikubwa, mawazo ya kijamii na maadili

vimejumishwa na mawazo ya kidunia, na yote mawili yana kiini cha dini. Lakini jaribio hili la Agano la Kale linaweza likaelezewa kuwa ni jaribio la awali tu wala si lile jaribio la mwisho lililofaulu. Na hiyo hiyo ndiyo hali ya dini za Kibaniani na Zoroasta. Zile haja chungu nzima za maisha ya kibinadamu zaonekana zahitaji itikadi na mfumo wa mawazo unapukiao vya kutosha uwe ni mwongozo kwa ajili ya shughli zote na haja zote. Mafundisho kama hayo zile dini za zamani zaidi haziyatoi. Mafundisho magumu, yasiyonapukia yenye kuhusu mahitaji ya jamii iliyostaarabika pia yanatolewa na dini hizo. Lakini haja zisizohesabika za jamii iliyopanuka ya wanadamu haziwezi kutoshelezwa na utaratibu wa mafundisho usioweza kupanulika. Kinachotofautisha wanadamu na wanyama wengine ni huu ukweli muhimu ya kuwa wanadamu, huku wakifanana sana, wakati huo huo wao wako tofauti sana mmoja kutoka mwingine. Ulimwengu wa wanyama watambulikana kwa ile hali yao ya kufanana kusikogeuka. Nyati, ng'ombe, simba, chui, mwewe na samaki, kwa neno zima, wanyama na ndege iwe wanaishi nchi kavu, majini au angani wote wafanana katika umbo lao la nje na pia katika muundo wa ubongo wao. Yaonekana wao wanatii kanuni sampuli moja. Lakini mwanadmu yuko tofauti. Kila mwanadamu huja humu duniani na nanma ile ile moja ya kiwiliwili; wana namna ile ile moja ya umbo, na maungo ya na viungo vyao vya kuhisia vyaonekana kuwa ni sampuii moja kabisa. Lakini kwa upande wa akili zao na kwa upande wa kile wakifikiriacho na kukihisi wao watofautiana sana. Ni lazima tuwe na mwongozo kwa ajili ya kila mmoja wa hawa wanadamu wote wa hali za namna namna na tabia tofauti tofauti, basi huo uwe mmoja tu, sharti mwongozo wenyewe uwe ambao umadhubuti wake umelainishwa kwa kiasi kinachotosha cha upanukikaji.

UTAMADUNI WA KIYAHUDI NA WA KIKRISTO

Kadiri dunia ilivyoendelea, imejaribu tena na tena kuelekea hali hii. Hadhrat Musa[as], aliwapatia Mayahudi dini na ustaarabu. Lakini mafundisho yake yakakosa hali ya upanukikaji kiasi cha kutoweza kutosheleza zile namna nyingi za hamu zinazoweza kuwa nazo tabia

ya mwanadamu. Mara tu pale watu wa Israeli walipoanza kufikiria njia mpya na kupokea mawazo na malengo mapya na kuelekea kwenye mambo mapya, yale mafundisho aliyowaachia Nabii Musa[as] yalianza kutofua dafu. Nabii Musa[as] hakufanikiwa kuvifanya vizazi vipya kuwa raia wema wa Israeli. Ni kweli, waliendelea kujihusisha na mafundisho haya lakini ama wakatokea kuwa waasi au wanafiki. Hivyo basi, Ukristo haukuweza ila kuitangaza Sheria kuwa ni laana. Ukristo ulilazimika kutangaza hivyo kwa sababu uliona kwamba Sheria isiyopanulika asilani ya Nabii Musa[as] ilikuwa imewafanya wanadamu kuwa waasi au wanafiki. Kwa vyovyote, Ujumbe wa Yesu ulifikishwa karne nyingi baada ya Nabii Musa[as]. Sheria ya Nabii Musa[as] ilikuwa ni chambileche koti lililoshonwa kwa kipimo cha mtoto ambalo halikumtosha tena Mwisraeli ngumbaru. Yesu[as] akaona upuuzi mtupu wa watu wazima na afya zao kujaribu kuvalia nguo zilizoshonewa watoto wadogo. Nafsi ya Yesu[as] ikalikaidi jambo hili. Afadhali tuseme kwamba kutoka kina cha moyo wa Yesu ikaja sauti ya Mungu kusema: "Kaumu hii wametangulia mbele kabisa ya ule wakati walipopokea mafundisho yao toka kwa Musa. Mafundisho haya yaliwatosha kadiri walivyobakia katika hali yao ya hapo awali. Lakini sasa wao wanahitaji mafundisho mapya, koti jipya kutoshea saizi yao illiyoongezeka." Lakini kumbe yale mafundisho mapya yenyewe Yesu aliyoipendekezea Israeli au, kwa neno zima, yale mafundisho ambayo Wakristo wajao karne nyingi baada ya Yesu wanamnasibishia yeye, muhtasari wake ni kwamba "Sheria ni Laana"! Hapana shaka ya kwamba chakula lisichokiweza tumbo la mtu ni balaa tupu, wala si baraka tena; lakini itakuwa ni makosa kudhania kutokana na hii hali ya tumbo kutokiweza chakula kwamba eti chakula vile kilivyo ni balaa wala sio baraka. Kajikoti kadogo kitaonekana kuwa ni kitu cha kustaajabisha mwilini mwa mtu mzima na afya zake. Na ndivyo liwezavyo wastajabisha jikoti kubwa mwilini mwa mtoto. Kijikoti kidogo mwilini mwa mtu mzima na jikoti kubwa mwilini mwa mtoto vyaonekana vya kustaajabisha, lakini haiwezi ikasemwa kwamba koti lenyewe vile lilivyo ni kichekesho.

Hivyo basi, kwetu sisi, yaonekana kwamba kumnasibishia Yesu yale mafundisho ya kuwa "Sheria ni laana" ni ukatili kabisa. Alichokisema na kukimaanisha Yesu ni sharti kilikuwa hiki tu ya kuwa ile tafsiri ya mafundisho ya Nabii Musa[as] iliyokuwepo wakati wa Yesu ilikuwa ni laana kwa watu wa wakati ule. Kama hivi ndivyo alivyomaanisha, basi huo ulikuwa ukweli wenyewe. Lakini wafuasi wa Yesu wakavuruga maneno haya ya hekima kiasi cha kuyafanya yawe upuuzi mtupu. Kwa vyovyote vile, hata kama Yesu alisema kile sisi tunachofikiria alisema au kile ambacho Wakristo wanafikiria kimakosa kwamba alisema, hawezi pakawa na shaka ya kwamba wakati wake yeye akili ya mwanadamu ilikuwa imepiga hatua mbali sana kuliko vile ilivyokuwa wakati wa Nabii Musa[as]. Sasa ilihitaji mwongozo mpya, maadili mapya, ustaarabu mpya na utamaduni mpya. Lakini pale ambapo Waalimu wa Kiisraeli walikuwa wamembana mwanadamu kwenye mafundisho yaliyokunjamana, Waalimu wa Kikristo wakamwondolea mwanadamu wajibu wote wa maadili na wa kidini. Mafundisho ya Nabii Musa[as] yaliizuilia akili ya Waisraeli dhidi ya kupiga hatua kupita wakati wa Nabii Musa[as], isipokuwa iwe ni katika sura ya uasi au unafiki. Mafundisho ya Kikristo yalimfanya mwanadamu kuwa huru kutokana na wajibu wote na kushawishia imani kwamba Sheria ya Mungu haiwezi kunyanyua mwanadamu kwenye kilele chochote cha maadili. Mwanadamu akampokonya Mungu, kama ilivyokuwa, kazi ya kuuandalia wokovu wake mwenyewe. Matokeo yake yakawa kwamba dini ile ile iliyofundisha kwamba kumtoa Mungu kafara kilikuwa ni kitu cha lazima kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu ilianza kufundisha kwamba kwa ajili ya maendeleo ya maadili ya mwanadamu hapakuwa na lazima ya mwongozo wa Mungu. Tuna kumbukumbu ya kihistoria kamili ya dini ya Waisraeli peke yake. Hivyo, sisi tumechukua mfano wetu toka kwa historia ya Waisraeli. Linapohusikana swali na mwisho yanaoutarajia mfululizo wa mabadiliko, tunaweza tukalijibu tu kwa kuzigeukia kumbukumbu za kihistoria zilizo timilifu katika hatua zao za maendeleo. Historia ya dini ya Waisraeli ni shahidi wa huu ukweli

kwamba akili ya mwanadamu iliendelea kukua kwa muda mrefu. Ilipitia hatua baada ya hatua lakini haikuonekana kufika kikomo chochote cha mwisho. Halikadhalika, historia ya dunia ni shahidi wa ukweli kwamba akili ya mwanadamu imepiga hatua kupitia nyakati nyingi za maendeleo ya kijamii, lakini hata hivyo imekosa kufikia wazo la udugu wa wanadamu wa kidunia nzima. Lakini hizi zote mbili za ushahidi zaonekana zabainisha ukweli kwamba akili ya mwanadamu, chambileche mwili wa mwanadamu, ulikuwa upitie kwenye hatua nyingi za kimabadiliko. Lakini hadi ujaji wa Islam haikufikia hali yoyote ya mwisho katika maendeleo ya kiroho. Katika kupitia hatua mbalimbali za maendeleo ya kijamii akili ya mwanadamu haikuweza kwenda mbali zaidi ya mipaka ya taifa au jamii na fikara ya usawa wa mwanadamu na udugu wa wanadamu haikustawi. Ilipitia kwenye vipindi vingi mbalimbali vya utamaduni, lakini haikufikia Sheria yoyote itoshelezayo, Sheria kwa ajili ya wanadamu wote. Sheria ya Nabii Musa[as] bila shaka ilijaribu kujumisha pamoja maadili ya kijamii na ya kitamaduni, lakini baada ya muda ilianza kutofua dafu kwa sababu kile ilichokuwa imekiwasilisha hakiwa ni neno la mwisho juu ya jambo lenyewe. Yesu bila shaka alijaribu kuleta mabadiliko, lakini mabadiliko yenyewe hayakuhakiki kuwa ni ya kutosha, wala hayakuweza kuzuia wimbi la uasi ambamo wakati ule akili ya mwanadamu ilikuwa imetumbukia. Masalio yote ya mafundisho ya Yesu ni maneno haya tu yanayonasibishwa na Ukristo ya kuwa Sheria ni laana. Maneno haya, yakichukuliwa vile yalivyo, yanachukiza akili ya kila mwenye kutafakari. Isipokuwa yaelezwe kwa njia inayofaa, maneno haya yenyewe ni laana kwani yanachofanya ni kumtokomeza mwanadamu mbali na Mwenyezi Mungu na kumtupilia mbali nje ya mwongozo Wake. Hivyo, yaonekana kwamba kile kikomo ambacho mabadiliko ya akili ya mwanadamu yalikuwa yakikitarajia kilikuwa bado hakijafika. Njia na hatua ambazo ustaarabu wa mwanadamu na utamaduni wa mwanadamu vilikuwa vimezipitia ziliashiria kwenye huu ukweli kwamba hata ustaarabu na utamaduni ulitawaliwa na kanuni ile ile ya mabadiliko ya pole pole

ambayo kwa muda mrefu iliutawala mwili wa mwanadamu. Hivyo, yaonekana kwa yakini kwamba ustaarabu wa mwanadamu na utamaduni vilikuwa viufikie utimilifu wa mwisho kwa njia ile ile ambayo mwili wa mwanadamu, baada ya muda mrefu wa mabadiliko, ulikuwa umefikia utimilifu wa mwisho wa umbo; na hili peke yake laonesha kuhitajika kwa Islam ilihali kunazo dini zingine, kuhitajika kwa dini ambayo iwe itayapatia mwisho yale mabadiliko ya utamaduni wa mwanadamu, mwisho uliotiwa ndani ya mafundisho ya Kurani.

SWALI LINALOSTAHILI

Swali la tatu, ambalo jibu lake ni kusema 'ndiyo' lathibitisha haja ya ujaji wa Kurani, ni kuwa je, vitabu vya hapo awali vilikuwa vimepatwa na kasoro zilizohitaji kitabu kipya, kilichokuwa ni Kurani?

Katika kulijibu swali hili ni sharti tukumbuke kwamba kigezo cha kwanza ambacho kwacho tunaweza tukapimia manufaa ya kitabu ni kutoingiliwa kutoka nje. Kitabu kilichofuniliwa ni bora kuliko kilichoandikwa na mwanadamu, kwani tunaweza tukasadiki kwamba kile kilichofunuliwa hakitatutia makosani. Mwenyezi Mungu ndiye mwongozo wenyewe. Hivyo, katika kitabu kilichofunuliwa Naye tunaweza tukatarajia kukuta humo nuru peke yake na ukweli, sio giza wala makosa. Kama fikra yetu kuhusu Mungu haimaanishi imani sampuli hiyo kwa yale Anayoyafunua, basi fikra sampuli hiyo haina thamani. Kama mawasiliano kutoka kwa Mwenyezi Mungu pia yanaweza yakakosea, basi sisi tunayo sababu gani ya kuyachukulia mafundisho ya kimbingu kuwa ni bora kuliko mafundisho ya kibinadamu? Kukiamini kitabu kunaandamana na imani kwamba kitabu chenyewe hakina makosa. Hata hivyo yawezekana kwamba kitabu kilichofunuliwa mwanzoni na Mwenyezi Mungu kuja kuingiliwa na mwanadamu. Kama yaliyomo kitabuni yameongezwa na kupunguzwa na mikono ya watu, basi kitabu hicho hakiwezi tena kuwa mwongozo.

Tunapovichunguza vitabu vya hapo awali kwa mtazamo huu, tunavikuta visivyoridhisha abadani. Wafuasi wa Agano la Kale wanakiamini kuwa ni kitabu kilichofunuliwa. Wakristo halikadhalika,

wanakielezea kuwa ni kitabu cha Mungu, pia Waislamu wafikiria kwamba kilikuwa ni kitabu kilichofunuliwa. Lakini, ni jambo moja kwa kitabu kufunuliwa na ni jambo jingine kabisa kwa kitabu kile kuyahifadhi kikamillfu maneno yake yaliyofunuliwa. Bila shaka, nyimati zote tatu — Mayahudi, Wakristo na Waislamu — wanakubaliana kwamba Mungu alizungumza na Manabii wa Agano la Kale. Lakini hawaamini tena — wala ushahidi wa ndani na nje hauyaungi tena mkono haya maoni — ya kwamba maandiko ya Agano la Kale vile tulivyonayo leo hii ni neno la Mungu kama vile lilivyofunuliwa kwa mara ya kwanza. Kutoka historia ya Israeli twapata habari kwamba wakati wa Mfalme Nebuchadnezzari vitabu vya Israeli viliteketezwa na kutilifikishwa. Vikaandikwa kwa mara ya tena na Nabii Ezra[as], na kumhusu Nabii Ezra[as] twasoma katika maandiko ya Kiyahudi:

> "Kilikuwa kimesahaulika lakini Ezra akakitengeneza (Suk.20a). Jew.Enc. Vol. 5, uk. 322).

Na tena:

> Ezra akaandika tena Torati (Vitabu vitano vya Musa), akileta humo mwandiko wa Ki-Assyria au herufi za umbo la mraba (Sanh. 21b). Jew Enc. Vol.5, uk 322).

Vivyo hivyo, twasoma:

> Yeye alionyesha tashwishi yake kuhusu usahihi wa baadhi ya maneno ya maandiko hayo kwa kuyatilia nukta juu yao. Kama Eliya atayakubali maneno haya, akasema Ezra, hizo alama hazitatiliwa maanani; akiyakataa, basi hayo maneno yenye walakini yataondolewa maandikoni (Ab.R.N. XXXIV) Jewish Encyclopaedia, Vol. 5, uk. 322.

Kutokana na haya madondoo ni dhahiri ya kwamba Torati, vyovyote vile ilivyokuwa wakati ule — iwe ni katika ile sura ambayo Ezra aliipatia au sura iliyoipata toka wakati wa hapo kabla — ilikuwa ni kitabu kisichokuwa na uhakika na kisichotegemeka. Matini yake ya

kawaida hayakuweza kuchukuliwa ni neno la Mungu lililohifadhika katika usafi wake ule wa asili. "Kitabu cha Ezra" hakitiwi tena ndani ya Biblia kama tuijuavyo leo hii. Hata hivyo, si kitabu kisichotegemewa kuliko vitabu vingine vya Biblia. Chaitwa "Kitabu cha Kiyunani cha Ezra". Nyakati za zamani kilikuwa kikitangulizwa mbele ya vitabu vya Ezra na Nehemia. Baadaye Kasisi mmoja shupavu wa Kikristo aitwaye Jeromi, aliyepewa na Papa jukumu la kuchuja Biblia, akakitupa kitabu cha Ezra nje ya Biblia kwa kisingizio kwamba haikupatikana nakala yake ya asili katika lugha ya Kiebrania. Kitabu hiki chaelezewa na baadhi ya watu kuwa ni kitabu cha tatu cha Ezra na wengine wanakielezea kuwa ni kitabu cha pili. Hata iweje, ionekenavyo ni kwamba ingawaje kitabu hiki kilitupwa nje ya Biblia, idadi iliyo kubwa ya Mayahudi na Wakristo wanakielezea kuwa ni "Kitabu cha Ezra". Katika mstari wa 20-25 wa mlango wa 14 wa kitabu hiki twasoma haya:

> "Tazama, Bwana, nitakwenda kama ulivyoniamuru na kuwakemea watu waliopo; lakini wale watakaozaliwa baadaye, ni nani atakayewaonya. Hivyo dunia imeingia gizani, na wale waishio humo hawana mwangaza. Kwani Sheria yako imeteketezwa, kwa hiyo, hapana ajuaye kazi zile uzifanyazo au zile kazi zitakazoanza. Lakini kama umenirehemu, mtie Roho Mtakatifu ndani yangu, nami niyaandike yale yote yaliyofanyika duniani tangu mwanzoni na yaliyokuwa yameandikwa katika Sheria yako, ili watu wapate kuitambua njia yako, na ili wale watakaoishi zama za baadaye wapate uhai. Naye akajibu akisema, Enenda, ukawakusanye watu pamoja, na kuwaambia wasikujie kwa siku arubaini. Lakini sikiza wewe kusanya miti mingi ya misanduku, na umchukue pamoja nawe Sarea, Dabria, Selemia, Ekanus, na Asieli, hawa watano waweza kuandika kwa kasi; Na uje huku, nami nitawasha mshumaa wa ujuzi moyoni mwako, ambao hautazimwa, mpaka yatakapotendeka yale yote utakayoanza kuyaandika wewe (Apocrypha; II Esdras, 14).

Kutokana na maneno haya yaonekana kwamba Ezra na wale

waandishi watano walijitahidi kwa siku arubaini faraghani na kwa msaada wa Mungu wakatunga vitabu 204. Katika mstari wa 44 wa mlango huu huu twasoma hivi:

> "Katika siku arubaini wakaandika vitabu mia mbili na vinne (Apocrypha; II Esdras, 14).

Kutokana na haya tunaweza twaona kwamba:

(a) Katika wakati wa Nabii Ezra[as], aliyeishi takriban miaka 450 kabla ya Yesu, Torati na vitabu vya Manabii wengine vilikuwa vimechanganyikana;

(b) hapana nakala yenye kutegemewa ya vitabu hivi iliyopatikana wakati huo;

(c) Ezra aliandika vitabu kwa mara ya tena.

Naam, twaambiwa kwamba vitabu vyenyewe vilifunuliwa. Lakini ***kufunuliwa*** kwamaanisha hivi tu kwamba Mungu alisaidia katika utungaji wao. Hii haimaanishi kwamba matini neno kwa neno yalifunuliwa na Mungu. Tunajua kutokana na historia ya Kiyahudi kwamba Ezra mwenyewe alikataa sehemu za maandiko kwa sababu ya kutokuwa zenye kutegemeka, na kwamba yeye alimwachia Eliya uamuzi wa mwisho. Hivyo basi, Torati vile tuijuavyo hivi leo, siyo ile Torati iliyofunuliwa kwake Nabii Musa[as]. Bali hii ni ile Torati aliyoiandika Ezra kutoka kwa kumbukumbu yake, na ambayo kuzihusu sehemu zake yeye alizitilia shaka. Bali hata yatupasa kusema kwamba Torati ya hivi sasa hata siyo ile aliyoiandika Ezra, kwani yeye Ezra aliandika vitabu 204, na hatupati vitabu 204 katika Biblia.

Ama kuhusu kukumbuka kwa Ezra, wanazuoni wa Kikristo wenyewe wanakutilia shaka mno. Bwana Adam Clark, mwelezaji mashuhuri wa Biblia, yuasema katika maelezo yake (ya mwaka wa 1891), chini ya 1 Mambo ya Nyakati (7:168) ya kuwa hapa kwa makosa Ezra yuaandika majina ya wajukuu badala ya wana na kwamba ni kazi bure kujaribu kupatanisha tofauti sampuli hii (uk.168). Katika (7:6) twasoma haya: Wana wa Benyamini: Bela na Bekeri, na Yediali,

watatu; ambapo katika mstari wa 8:1 twasoma haya: Naye Benyamini akamzaa Bela, mzawa wake wa kwanza, na wa pili Ashbeli, na wa tatu Ahiramu, na wa nne Noha, na wa tano Rafa.

Wanazuoni wa Kiyahudi wanaonelea kwamba Ezra hakujua vizuri kama mtu anayetajwa alikuwa ni mwana au ni mjukuu wa mtu mwingine. Sasa haya yakiwa ndiyo maoni yanayoshikiliwa na wanazuoni wa Kiyahudi na wale wa Kikristo kuhusu uwezo wa kukumbuka wa Ezra, basi wanawezaje Mayahudi na Wakristo wa kawaida na watu wa kawaida kuridhika juu ya manufaa ya kiroho ya kitabu kilichopungukiwa mamlaka kama vile Biblia?

Hebu sasa na tugeukie ushahidi wa kindani wa mada hii. Hoja iliyo muhimu na yenye kuamua zaidi kuhusu mada hii yatolewa na kitabu cha Kumbukumbu la Torati (34:5-6) ambamo twasoma:

> "Basi Musa, mtumishi wa Bwana, akafa huko katika nchi ya Moabu, kwa neno la Bwana, Akamzika bondeni, katika nchi ya Moabu, kukabili Beth-peori; lakini hapana mtu ajuaye kaburi lake hata leo".

Mistari hii yaonesha kwa uwazi kwamba ilitungwa na kuongezewa katika kitabu chenyewe miaka mia nyingi baada ya wakati wa Nabii Musa[as]. Haielekei kabisa kwamba Mwenyezi Mungu alipata wakati wowote kumzungumzia Nabii Musa[as] akimwambia "Hapana mtu ajuaye kaburi lako hadi hivi leo". Je, maneno sampuli hii anaweza akaambiwa mtu aliye hai? Je, maneno haya "hadi hivi leo" yanaweza yakatumiwa katika usemi anaouambiwa?

Kisha katika mstari wa 8 wa kitabu hicho twasoma maneno haya:

> "Wana wa Israeli wakamwomboleza Musa katika uwanda wa Moabu siku thelathini; basi siku za maombolezo ya matanga ya Musa zikaisha."

Mstari huu pia waonesha kuwa hauwezi ukawa uliofunuliwa kwa Nabii Musa bali ni nyongeza ya baadaye. Kisha katika mstari wa 10 twasoma:

> Wala hajainuka tena katika Israeli Nabii kama Musa, amabaye

Bwana alimjua uso kwa uso".

Pia mstari huu hauoneshi kuwa ni wahyi wa Nabii Musa[as], bali ni nyongeza iliyofanywa miaka mia nyingi baada ya kifo chake na kupenyezwa katika kitabu cha Nabii Musa[as]. Yawezekana kwamba iwe ni kazi ya Ezra, lakini yaweza pia kuwa ni kazi ya mtu mwingine.

Kwa minajili ya kujipatia ushahidi zaidi wa kindani juu ya jambo hili kwamba Torati, vile tuijuavyo, iliandikwa baada ya wakati wa Nabii Musa[as], na kwamba inayo maandiko ya watu wengine, hatuna budi kusoma kitabu cha Mwanzo 14:14 yanapopatikana maneno haya:

> "Abramu aliposikia ya kwamba nduguye ametekwa mateka, akawapa silaha vijana wake, waliozaliwa katika nyumba yake, watu mia tatu na kumi na wanane, akawafuata mpaka Dani".

Sasa linganisha kifungu hiki na maneno ya kitabu cha Waamuzi 18:27-29, panaposemwa kwamba huu mji unaoitwa Dani katika kitabu cha Mwanzo kwanza uliitwa Laisha. Kama miaka thamanini hivi baada ya Nabii Musa[as] mji huu ulitekwa na Waisraeli na ukapewa jina la Dani. Katika kitabu cha Waamuzi 18:27-29 twasoma maneno haya:

> "Nao wakakitwaa hicho alichokuwa amekifanya Mika, na kuhani aliyekuwa naye, nao wakaifikia Laisha, kwenye watu waliokuwa na starehe na hifadhi, wakawapiga kwa makali ya upanga; wakaupiga moto mji wao. Wala hakuwako mwokozi, kwa sababu huo mji ulikuwa ni mbali sana na Sidoni, nao hawakuwa na shughuli na mtu awe yeyote; na mji huo ulikuwa katika hilo bonde lililo karibu na Bethrehobu, nao wakaujenga huo mji na kukaa humo. Wakauita jina lake Dani, kwa kuliandama jina la babu yao Dani, aliyezaliwa kwake Israeli; lakini jina la mji huo hapo kwanza ulikuwa ukiitwa Laisha".

Tunachosema ni kwamba jina lililopendekezwa miaka 80 baada ya Nabii Musa[as] lisingeliwezekana kwa hakika kuonekana katika kitabu cha Nabii Musa[as]. Hivyo basi, ni dhahiri kabisa kwamba Kitabu cha Musa[as] kilipata nyongeza kilichoziongezewa baada ya kifo chake na

waandishi wengi walikipenyeza fikara na dhana zao wenyewe.

Aina hii ya uhariri haikomei kwenye Kitabu cha Nabii Musa[as]. Vitabu vingine vya Biblia pia vina dosari hiyo hiyo.

Katika Kitabu cha Yoshua 24:29 twasoma maneno haya:

> "Ikawa, baada ya hayo, Yoshua mwana wa Nuni, mtumishi wa Bwana, akafa, mwenye umri wa miaka mia na kumi".

Vivyo hivyo, katika Kitabu cha Ayubu 42:17 yapatikana maneno haya:

> "Basi Ayubu akafa, mzee sana mwenye kujawa na siku".

Kutokana na madondoo haya ni wazi kabisa kwamba Kitabu cha Yoshua hakikuandikwa na Yoshua na kitabu cha Ayubu hakikuandikwa na Ayubu. Badala yake hiyo ilikuwa ni mitungo ya watu waliokuja baadaye, na ambao walivitunga vitabu hivi kutokana na yale waliyoyasikia toka kwa watu wengine. Pia yawezekana kwamba wale Manabii ambao mafundisho yao yameandikwa katika Biblia walilikusanya neno la Mungu lilivyopokelewa nao, lakini kumbukumbu zilizoachwa nao hazikuweza kuepukana na athari mbaya ya dahari, na kumbukumbu hizo zilipokuwa zimetoweka watu waliokuja baadaye wakaziandika tena vile walivyozikumbuka akilini mwao, na katika kufanya hivyo wakapenyeza chungu nzima ya fikara zao na maoni yao wao wenyewe. Basi yawezeje kuwa ni ajabu kwamba vitabu hivi, ambavyo kutokana na ushahidi wa kihistoria na ule vilivyonao, vina kilema na vimelemazwa, hukosa kuwapatia utulivu wasomaji wao? Yawezaje kuwa ni ajabu ya kwamba kwa hiyo Mwenyewzi Mungu naye pia Aliviondolea ulinzi Wake kiasi cha wanadamu kuanza kutafuta na kutamani kitabu kitakachobidi kutokuwa, bali na hata kutoweza, kufanyiwa mwingilio wowote wa kibinadmu? Kama hata baada ya vitabu hivi kuchafuliwa, Mwenyezi Mungu hakuwa ameiufunulia dunia kitabu kingelichoweza kuchukuliwa kuwa ni Neno hasa la Mungu, na kulindwa kwacho dhidi ya mwingilio wa kibinadamu kusingeweza kutiliwa shaka, basi tungelikuwa tumekiri kwamba Mwenyezi Mungu hajali kumwongoza

mwanadamu na kwamba Yeye hupanda mbegu ya imani sio katika ardhi inayozaa yakini na uhakika bali katika ardhi yenye kuzaa shaka na tashswishi na kwamba Yeye yuadhamiria kutoijazi imani hata sawa na ile kadiri ya uhakika ukafiri ulionayo. Lakini je, twaweza kuwa na wazo sampuli hiyo? Je, wazo kama hilo ni stahili ya Mwenyeze Mungu? Kama si kweli, na si kweli kabisa, kwamba Mwenyezi Mungu Hajali kumwongoza mwanadamu, basi hatuna budi kukitafuta kile kitabu kilichoibatilisha Biblia na kilichochukua mahali pa hii chapa ya neno la Mungu iliyopotoshwa na kuchafuliwa.

HITILAFU KATIKA AGANO LA KALE

Ushahidi zaidi wa kindani unaounga mkono rai kwamba vitabu vya Biblia havitoi tena wahyi wa asili wawasilishwa na zile hitilafu zilizopo kati ya sehemu mbalimbali za matini yao.

(1) Mathalan, katika kitabu cha Mwanzo 1:27 twasoma maneno haya:

"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake".

Na mbele kidogo katika Mwanzo 2:17 twasoma:

"Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile".

Madondoo haya mawili yahitilafiana. Kama haya yapatanishwe, basi sharti tudhanie kwamba hata Mungu hana habari na ujuzi wa wema na ubaya. Kwa sababu Adamu akiwa yu mfano wa Mungu, kama yeye hakuwa na habari za ujuzi wa wema na ubaya, basi Mungu pia atabidi kudhaniwa kuwa asiye na uwezo wa kupambanua wema mbali na ubaya, uwezo ambao, kwa hakika, kuwa nao ndiyo inayokuwa sifa ya juu zaidi. Sifa zingine zote ni za chini ya sifa hii. Kama mwanadamu hakuweza kupambanua baina ya wema na ubaya, basi yeye hakuweza lolote la maana. Chenye kufaa na cha thamani ni kile kinachofanywa kwa hiari na panapo na ufahamu timamu. Kinachofanywa bila makusudi wala kufahamu hakina thamani ya kimaadili. Kama mwanadamu hawezi kupambanua baina ya wema na ubaya, basi yeye si kiumbe chenye utu, akiwa hawezi ama kuchagua wema au kuukwepa ubaya.

Je, Mungu naye Hana sifa hii ya kujua wema na ubaya sawa na wanazuoni wa Kiyahudi na wa Kikristo? Je, Mungu hajui wema ni nini na ubaya ni kitu gani? Kama jambo hili hana habari nalo, basi kwa nini Yeye Hutuma Manabii na Anatafuta kufundisha kitu gani kwa njia ya Manabii hawa? Je, Mungu Hahusiani na kuimarisha wema na kuangamiza ubaya? Kama tujisahaulishe kidogo kwamba shabaha hasa aliyoumbiwa mwanadamu ndiyo hii kwamba yeye ajue wema mbali na ubaya, na kama atanyimwa ujuzi huu, basi ilikuwepo haja gani ya kumuumba? Kama mwanadamu hakuweza kuwa na ujuzi wa wema na ubaya, basi yeye yuawezaje kusema eti ameumbwa kwa mfano wa Mungu? Bila ya maarifa ya mambo ya kiutu na ujuzi wa wema na ubaya mwanadamu asingeweza kuonyesha mfano wowote wa Mungu. Kama mwanadamu alikuwa ni mfano wa Mungu, basi ni kosa kufikiria kwamba yeye alikataza kukaribia mti wa wema na ubaya. Kama alikatazwa kuukaribia mti wa wema na ubaya, basi ni kosa kudai kwamba Mungu alimuumba mwanadamu kwa mafano Wake.

(2) Katika Mwanzo 2 :17 twasoma hivi:

> "Kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo, utakufa"

Katika Mwanzo 2:9 twasoma maneno haya:

> "Bwana Mungu akachipusha katika ardhi kila mti unaotamanika kwa macho na kufaa kwa kuliwa; na mti wa uzima katikati ya bustani na mti wa ujuzi wa mema na mabaya."

Mstari huu unaweza ukamaanisha kimojawapo tu cha vitu viwili. Ama kumaanisha kwamba palikuwepo na mti mmoja ulioweza kutoa uzima pamwe na ujuzi wa mema na mabaya; au kumaanisha kwamba ilikuwepo miti miwili, mmoja wa uwezo wa kutoa uzima na mwingine uliotoa ujuzi wa mema na mabaya. Ikiwa kulingana na mstari wenyewe, uliokuwepo ni mti mmoja, basi mstari wa Mwanzo 2:17 wathibitika kubatilika, kwa sababu mstari wa Mwanzo 2:9 waupatia ule mti uwezo wa kutoa uzima, wala sio sifa za kufisha. Ikiwa kulingana na Kitabu cha Mwanzo, kulikuwepo na miti miwili wala si mti mmoja, basi mistari hii miwili inakuwa ni yenye

kugongana moja kwa moja. Kama Adamu angelikuwa amekula mti wa ujuzi wa mema na mabaya, basi mauti hayakumbidi, kwa sababu yeye angeweza kuula pia ule mti wenye kutoa uzima. Kwa hakika, kulingana na Biblia, pale Adamu alipoula mti wa ujuzi yeye angeweza kuula pia ule mti wenye kutoa uzima. Kama matokeo ya kula matunda ya mti mmoja yalikuwa ni kifo tu, basi matokeo ya kula matunda ya ule mti mwingine yalikuwa ni uzima wa milele. Hali aliyokuwemo Adamu ni ngumu kuielewa; mti mmoja ukamtolea uzima wa milele, na mwingine ukatoa kifo.

Twajua kutokana na Biblia kwamba Adamu na mkewe walikula mti wa uzima. Twasoma maeno haya katika Mwanzo 3:2-3:

> "Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustani twaweza kula; lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa."

Sawa na mistari hii yaonekana kwamba Adamu na mkewe walikula matunda ya miti yote isipokuwa mti wa ujuzi. Kama masimulizi haya ya Bibilia ni ya kweli, basi Adamu na mkewe bila shaka walikula matunda ya mti wa uzima, na kama waliula mti wa uzima, wangelikufaje? Twasoma maneno haya katika Mwanzo 3:22:

> "Bwana Mungu akasema, Basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya; na sasa asije akanyosha mkono akatwaa matunada ya mti wa uzima, akala, akaishi milele".

Mstari huu waonesha kwamba Adamu hakuwa ameula mti wa uzima, na haiwezekani kwetu sisi kujua ni upi katika mistari hii, usemao kweli. Je, ni ule usemao kwamba Adamu hakula mti wa uzima au ni mstari ule anamoripotiwa mke wa Adamu kuwahi kusema kwamba, isipokuwa mti wa ujuzi, wao walikula matunda ya miti yote mle bustanini? Wala haiwezekani kwetu sisi kusema kama kuula mti wa ujuzi huwa ni kifo tu au kuula mti wa uzima huwa ni uzima wa milele.

Maneno haya yote yanahitilafiana, na neno la Mungu haliwezi likawa na hitilafu kama hizi. Ni kweli kabisa kwamba maneno haya yaliongezwa Bibliani na waandishi waliopenyeza mawazo yanayohitilafiana. Kitabu chenye maneno yanayohitilafiana hakiwezi kunasibishiwa mwanadamu tu wa kawida mwenye akili zake, sembuse Mungu. Lakini Musa alikuwa Nabii mheshimiwa wa Mwenyezi Mungu, na Torati ilikuwa bila shaka wahyi wa Mwenyezi Mungu uliopokelewa naye. Kwa hiyo, hatuna budi, tuseme hitilafu hizo ni nyongeza za baadaye. Kwa sababu ya hitilafu hizi, hapapatikani lawama juu ya Mungu wala juu ya Nabii Musa[as]. Ila tu ni sharti ya kuwa pale Mwenyezi Mungu alipokata shauri mahali pa Biblia pachukuliwe na kitabu chenye thamani ya kudumu, aliiondolea Biblia ulinzi Wake nayo haikuwa tena salama dhidi ya mwingilio wa kibinadamu na dhidi ya athari mbaya za dahari.

(3) Katika Mwanzo 22:14 twasoma hivi:

> Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-yire, kama watu wasemavyo hata leo, Katika mlima wa Bwana itapatikana.

Lakini katika kitabu cha Kutoka 6:2-3 twasoma maneno haya:

> Kisha Mungu akasema na Musa, akamwambia, Mimi ni Yehova; nami nilimtokea Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, kama Mungu Mwenyezi, bali kwa jina langu Yehova sikujulikana kwao.

Hitilafu baina ya mistari hii miwili iko peupe. Mstari wa kitabu cha Kutoka wasema kwamba jina Yehova kwa mara ya kwanza kabisa lilifunuliwa Nabii Musa[as]. Kabla ya zama zaka hapana Nabii, iwe ni Ibrahimu, Isihaka au Ayubu[as], aliyekuwa amefunuliwa naye jina hili Lake. Lakini ule mstari kutoka kitabu cha Mwanzo wasema kwamba jina hili pia lilifunuliwa kwa Ibrahimu na kwamba yeye aliuita jina hili hili mlima Yehova-Yire.

(4) Vivyo hivyo katika kitabu cha Hesabu 33:38 twapata maneno haya:

> Haruni akakwea mlima wa Hori, kwa amri ya Bwana, akafa hapo, katika mwaka wa arobaini baada ya Wana wa Israeli kutoka

katika nchi ya Misri, mwezi wa tano, siku ya kwanza ya mwezi.

Lakini katika Kumbukumbu la Torati 10:6 maneno tunayoyasoma ni haya:

Wana wa Israeli wakasafiri kutoka visima vya Bene-Yaakani kwenda Mosera; Haruni akafa huko, akazikwa huko; na Eeazari mwanawe...

Ni dhahiri kwamba mtu yule yule mmoja asingeliweza kufia mahali pawili tofauti. Haiwezi ikatiliwa shaka kwamba hii mistari miwili yenye kuhitilafiana ilipenyezwa Bibliani na waandishi wawili tofauti ambao wameandika humo dhana zao wenyewe na kuziwasilisha kama neno la Mungu.

(5) Katika kitabu cha 1 Samweli, 16:10-13 twasoma kwamba Daudi alikuwa mwana wa nane wa Yese:

> Tena, Yese akapitisha wanawe saba mbele ya Samweli. Samweli akamwambia Yese, Bwana hakuwachagua hawa. Kisha Samweli akamwambia Yese, watoto wake wote wako hapa? Naye akasema, Amesalia mdogo wao, na tazama, anachunga kondoo. Basi Samweli akamwambia Yese, Tuma watu wamlete; kwa sababu hatutaketi hata atakapokuja huko. Basi akatuma mtu, naye akamleta kwao. Naye alikuwa mwekundu, mwenye macho mazuri. Na umbo lake lilikuwa la kupendeza. Bwana akasema, Ondoka umtie mafuta; maana huyu ndiye. Ndipo Samweli akaitwaa pembe yenye mafuta, akamtia mafuta kati ya ndugu zake; na roho ya Bwana ikamjilia Daudi kwa nguvu tangu siku ile. Basi Samweli akaondoka, akaenda zake Rama.

Lakini katika kitabu cha 1 Mambo ya Nyakati 2:13-15 twasoma kwamba Daudi alikuwa mtoto wa saba wa Yese:

> Na Yese akamzaa Eliabu, mzaliwa wake wa kwanza na wa pili Abinadabu, na wa tatu Shama; na wa nne Nathanaeli, na wa tano Radia; na wa sita Ozemu, na wa saba Daudi.

Hitilafu hii halikadhalika yaonesha kwamba wanahistoria wenye nia mbalimbali wamepenyeza maoni yao katika Biblia, hivi kwamba

Biblia, vile tuijuavyo hivi leo, haiwezi ikachukuliwa kuwa ni Kitabu cha Mungu kilichohifadhika katika usafi wake wa asili.

(6) Katika kitabu cha II Samweli 6:23 twasoma haya:

"Basi Mikali, binti wa Sauli, hakuwa na mtoto hata siku ya kufa kwake.

Lakini katika II Samweli 2I:8 twasoma maneno haya:

...Na wana watano wa Mikali binti Sauli, aliomzalia Adrieli, mwana wa Barzilai, Mmeholadhi. Kitabu hicho hicho mahala pamoja kimwelezee Mikali kuwa mgumba na mahala pengine kuwa ni mama wa watoto watano.

(7) Vivyo hivyo katika kitabu cha II Mambo ya Nyakati 21:19-20 twasoma ya kwamba mfalme Yeheramu alikuwa na umri wa miaka thelathini na miwili alipoanza kutawala, akatawala huko Yerusalemu miaka minane; akakaa miaka miwili akiwa amevuliwa taji na baadaye akafariki kwa maradhi ya kutisha, yaani, kwa jumla aliishi miaka arubaini na miwili. Lakini katika kitabu hicho hicho mlango wa (22:1-2) twasoma maneno haya:

> Nao wenyeji wa Yerusalemu walimafanyia Ahazia mwanawe mdogo awe mfalme mahali pake; maana wakubwa wote wamekwisha kuuawa na kikosi cha watu waliokuja matuoni mapya na Waarabu. Hivyo Ahazia alikuwa na umri wa miaka arobaini na miwili alipoanza kutawala; katawala mwaka mmoja huko Yerusalemu.
>
> Mstari wa kwanza wasema kwa uwazi kwamba Yehoramu alikuwa na umri wa miaka arobaini na miwili zama alipofariki. Lakini mstari wa pili wadai kwamba mwana mdogo wa Yehoramu, aliyeitwa Ahazia naye pia alikuwa na umri wa miaka arobaini alipokalia kiti cha ufalme kufuatia kifo cha babake. Je, baba na mwana walikuwa rika moja na je, wale watoto wengine wa Yehoramu waliouawa na Waarabu, walikuwa na umri mkubwa zaidi ya baba yao?
>
> Je, anaweza mtu mwenye akili zake akasema maneno haya

yanayohitilafiana? Baba afe akiwa na umri wa miaka arobaini na miwili na mwanawe wa umri huo huo awe mfalme unyounyo nyuma na marehemu babake. Maneno sampuli hii hayawezi yakapatikana hata katika kitabi cha kawaida tu, achilia mbali kitabu kilichofunuliwa na Mungu. Hapawezi kuwa na shaka kwamba hitilafu hizi hazikuwemo ndani ya ufunuo wa asili. Hitilafu hizi hazikuwa zipatikane katika kauli za Manabii. Hizi zikiwa ni hitilafu haziwezi zikanasibishiwa mwandishi mmoja. Hatuna budi kuchukulia kwamba waandishi wengi walipenyeza mawazo yao katika Kitabu cha Mungu, wakitumainia kuyafanya yachukuliwe kuwa eti ni ufunuo. Mwandishi mmoja aliamini kwamba Yehoramu alikuwa na umri wa miaka arobaini na miwili wakati alipofariki; basi yeye akaandika vivyo hivyo. Mwingine akafikiria kwamba Yehoramu alikuwa na umri wa miaka mia moja wakati wa kifo chake, na wakati huo mwanawe mdogo alikuwa na umri wa miaka arobaini na miwili; huyu naye akaandika hivyo hivyo. Maneno haya yanahitilafiana. Yatubidi kukubali kwamba yule mwandishi aliyeamini kwamba Yehoramu alifariki akiwa na umri wa miaka arobaini na miwili hakuamini mwanawe Ahazia kuwa na mika arobaini na miwili wakati wa kifo cha babake, bali pengine miaka kumi a minne au kumi na mitano. Pia yatubidi kuamini kwamba yule mwandishi aliyeamini Ahazia kuwa wa miaka arobaini na miwil zama alipofanywa mfalme hakuamini kwamba babake naye pia alikuwa na umri wa miaka arobaini na miwili. Bali swali lenyewe ni kwamba je, ni manufaa gani ya kiroho yanayoweza kupatikana kutoka kitabu cha namna hii? Ni imani au tegemeo gani kiwezalo kuupatia moyo wa wasomaji wake? Kama madai yenyewe yangekuwa kwamba Kitabu cha Torati ni mkusanyo wa maneno yaliyosemwa na mamia ya maelfu ya waandishi wa Kiyahudi, hata hivyo kitabu chenyewe kingelikuwa na thamani kwa kiasi fulani. Lakini twakuta kwamba, kwa upande mmoja, kitabu hiki chawasilishwa kuwa eti ndilo neno hasa la Mungu,

> na kwamba, kwa upande mwingine, kinayo maelfu ya hitilafu. Madai haya yasiyostahili kwa niaba ya Biblia yanabatilisha hata kile kiasi cha thamani ingelichokuwa nayo, yangelikuwa hayakufanywa madai sampuli hiyo kwa niaba yake. Kitabu kama hicho hakiwezi kikatumika kuwa ni mwongozo, na ni nani awezaye kusema kwamba baada ya kitabu sampuli hii hatukuhitaji kitabu kingine?

MAFUNDISHO YA KIKATILI YA AGANO LA KALE

Sio tu kwamba zimo hitilafu; bali pia twakuta kwamba mara nyingine mafundisho ya kikatili kupindukia yananasibishiwa Biblia, mafundisho yasiyoweza kunasibishiwa Mungu Mwema Mwenye ukarimu.

Katika Kitabu cha Kutoka 21:20-21 twasoma maneno haya:

> Mtu akimpiga mtumwa wake, au kijakazi chake, kwa fimbo, naye akifa mkononi mwake, hana budi ataadhibiwa. Lakini akikaa na kufa baada ya siku moja au mbili hataadhibiwa; maana ni mali yake.

Je, ni makali kiasi gani mafundisho haya kwa watumwa. Mtu katili amtandike vibaya mtumwa au mjakaze wake hivi kwamba maskini huyo afe baada ya siku moja au mbili. Lakini hata hivyo Biblia haimpati adhabu katili huyu eti kwa sababu watumwa na wajakazi ni mali ya bwana wao. Je, mafundisho sampuli hii yangeweza kudumu wakati wote? Je, mahali pa mafundisho haya hapakustahili kuchukuliwa na mafundisho mengine ambayo yapige marufuku desturi ya utumwa ambayo yawakataze makabaila wasiwe katili kwa watumwa? Bila shaka mafundisho haya yalitolewa na Islam. Sio tu kwamba Islam ilileta kanuni za kupigia utumwa marufuku bali iliweka sheria ya kuwa watumwa na wajakazi washindwao kujipatia uhuru wao hawakupaswa kutendewa kikatili. Hadhrat Abu Mas'ud Ansari[ra] alikuwa anamchapa mtumwa wake. Kutoka upande wa nyuma yake akasikia sauti ikisema, "Abu Mas'ud, uwezo Mungu alionao juu yako ni mkubwa sana kuliko ule ulionao juu ya huyu mtumwa". Hadhrat Abu Mas'ud[ra] akageuka nyuma na kumwona Mtume Mtukufu[saw],

akija. Mjeledi wake ukamdondoka mkononi. Akatamka akisema "Ewe Nabii wa Mungu, namwachilia huru mtumwa huyu kwa jina la Mwenyezi Mungu". Na Mtume Mtukufu.[saw] akajibu akisema, "Kama usingelifanya hivyo, moto wa Jahanamu ungelikuunguza usoni" (Muslim: Kitabul-Iman).

Vivyo hivyo, Sahaba mwingine wa Mtume Mtukufu[saw] yuasimulia kwamba, "Sisi tulikuwa tu ndugu watatu na tulikuwa na mjakazi mmoja. Ndugu yetu mdogo akampiga kofi la uso. Mtume Mtukufu[saw] aliposikia hivyo akatoa amri akitaka mjakazi yule kuachiliwa huru, huku akitoa sababu ya kwamba bwana anayempiga mtumwa wake hastahili kuwa na mtumwa"(Bukhari, Kitabul-'Itq).

Mtume Mtukufu[saw], mwenyewe aliweka mfano bora kabisa katika uwanja huu, Alipofunga ndoa yake ya awali, mkewe Hadhrat Khadija[ra] alimpatia mali zake zote pamwe na watumwa wake. Mtume Mtukufu akatangaza kwamba yeye hawezi kuwatia wanadamu utumwani, na mara aliposema hivyo aliwaachilia huru watumwa wote aliokuwa amewapokea kama zawadi toka kwa mkewe, na maisha yake mazima yeye hakuwa na mtumwa abadan.

Katika Kitabu cha Mambo ya Walawi 20:27 twasoma hivi:

> Tena mtu mume au mtu mke aliye na pepo, au aliye mchawi, hakika atauawa; watapigwa kwa mawe; damu yao itakuwa juu yao.

Vivyo hivyo katika kitabu cha Kutoka 22:18 twasoma maneno haya:

> Usimwache mwanamke mchawi kuishi.

Ni kinyume cha mantiki na dhalimu lilioje fundisho hili ikiwa uchawi hapa wamaanisha zile mbinu za kiinimacho zifanywazo na mabingwa wa kuburudisha! Na tuichukulie hii kuwa ni kazi tu ya kawaida. Katika maisha yaliyojaa kukurukakara na taharuki ambayo mara nyingi baadhi ya watu huishi, michezo na burudani huleta maliwazo yenye kupendeza. Hapo ndipo watumbuizaji hawa wanapoyabetua mawazo ya mtu kutoka hali ya ukakamavu wa kikazi hadi kwenye majukwa ya vitimbi vyao wenyewe. Kuuchukulia

utumbuizaji kuwa ni kazi yenye kuadhibika kwa kifo ni dhulma tupu. Kama uganga na uchawi vyamaanisha yule mtu wa ajabu wa ngano za vizimwi amgeuzaye mtu kuwa fahali, mwanamke kuwa ndege, basi fundisho hili la Biblia ni la kipumbavu chambileche vile lilivyo kikatili. Watu wa ajabu kama hao hawajakuwepo asilan, na kumsingizia mtu yeyote ufundi huo usiowezekana na kisha kuamuru kifo chake ndio ukatili wa kupindukia.

Katika Kitabu cha Kumbukumbu la Torati 7:2 twasoma hivi:

> Wakati Bwana, Mungu wako, atakapowatoa mbele yako, nawe utawapiga; wakati huo ndipo uwaondoe kabisa; usifanye agano nao, wala kuwahurumia.

Kumuhusu adui mshinde ni la kikatili kiasi gani fundisho hili. Kuua jamii nzima ya maadui baada ya kuwashinda, kutofanya nao mkataba wowote na kukataa kuwaonyesha huruma yoyote inaweza kuwa tabia ya wafalme makatili wa kidunia. Haiwezi ikanasibishiwa Mungu Mkarimu na Mwenye huruma.

Bila shaka mafundisho sampuli hii ni lazima yawe yalitungwa na Mayahudi wakorofi waliokuja baada ya Nabii Musa[as] na kuyapenyeza mafundisho haya Bibliani na kuichafulia mbali.

MAFUNDISHO YASIYO YA KIMANTIKI YA AGANO LA KALE

Agano la Kale lina maneno mengi yasiyo ya kimantiki.

(I) Katika Kitabu cha Mambo ya Walawi 11:6 twasoma maneno haya:

> Na sungura, kwa sababu hucheua, lakini hana kwato, yeye ni najisi kwenu.

Vivyo hivyo, katika Kitabu cha Hesabu 22:28 yasememwa kwamba punda wa Balaam alizungumza naye.

Katika Kitabu cha Mwanzo 46:27 twasoma kwamba idadi ya Waisraeli walipoingia Misri ilikuwa ni watu sabini, lakini miaka mia mbili na kumi na mitano baadaye, yaani, wakati wa Nabii Musa[as], walikuwa wameongezeka mno hivi kwamba idadi ya wanaume watu

wazima peke yao ilifikia laki sita. Ndani ya Kutoka 12:37 madai haya ndiyo yaliyofanywa:

> Wana wa Israeli wakasafiri kutoka Ramesesi mpaka Sukothi, walipata hesabu yao kama watu sita mia elfu watu waume waliokwenda kwa miguu, bila kuhesabu watoto.

Kama, kwa kuzingatia hii idadi ya wanaume watu wazima, tukikadiria jumla ya kundi hilo zima la Waisraeli, hii inakuwa takriban watu laki ishirini na tano. Lakini huko kungekuwa ni kutilia chumvi mno na kinyume kabisa na uwezekano wa akili. Katika muda wa miaka mia mbili na kumi na mitano kikundi cha watu sabini kisingeweza kuongezeka kiasi cha kuwa watu milioni mbili na mia tano. Hata ushahidi wa kihistoria wapinga makisio haya. Wakati Nabii Musa[as] alipohama kutoka Misri kwenda Kanaani na akalazimika kuingia jangwani kwa miaka arobaini, hii halaiki ya watu milioni mbili na laki tano waliponea chakula gani? Je, wangeweza kujipatia chakula na maji ya kutosha kuwawezesha kuishi jangwani kwa miaka arobaini? Naam, isemavyo Biblia, waliletewa kware na mkate toka mbinguni. Lakini hata sawa na Biblia riziki hii toka mbinguni iliteremka wakati fulani fulani tu. Basi halaiki hii kubwa ya watu walipataje chakula chao pale kilipokosa kushuka kutoka mbinguni?

Pia twapata habari kutoka Biblia kwamba kila moja la makabila hayo ya Waisraeli lilipata maji kutoka chemchemi moja. Lakini je, twaweza kuamini kwamba watu milioni mbili na laki tano wangeweza kupata maji ya kutosha kukidhia mahitaji yao kutoka kwa chemchemi chache. Ardhi walimopitia haina mito midogo au vijito. Ziko chemchemi huko na huko, lakini chemchemi haina ukubwa sana. Basi inawezaje chemchemi kuwapatia watu milioni mbili na laki tano maji ya kutosha? Kitabu chenye maneno sampuli hii yasiyoikubali akili, kisingeweza kutuliza akili ya mtu. Bila shaka hiki kilikuwa ni kitabti kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kiliandikwa na Manabii Wake. Lakini kimepoteza sura yake ya asili. Kimekuwa ni kitabu kilichobanduliwabanduliwa na kimebadilishwa kiasi cha kutotambulikana. Kukihesabu kitabu

kilichoharibiwa kwa njia hii kuwa eti ni neno hasa la Mungu ni kutafuta kumtia lawamani Mwenyezi Mungu na dini pia. Bali ilikuwa lazima ya kwamba baada ya kitabu kama hiki tuwe tulipata kingine itakachobidi kisiwe na mwingilio wa kibinadamu na kisichoingizika maneno isiyoyakubali akili. Ama kuhusu idadi ya Waisraeli, Kurani yatusaidia na kueleza ukweli. Ikasema:

> Je, hukuwaona wale waliotoka katika majumba yao, nao walikuwa maelefu, wakiogopa mauti (Sura Al-Baqara 2:244).

Sawa na Kurani idadi ya watu wa Israeli waliotoroka Misri wakimwogopa Firauni ilikuwa ni elfu kadha tu, na hii yaonekana kuwa kweli kwani Mayahudi milioni mbili na laki tano wasingeliishi wakiogopa makabila madogo madogo ya Wapalestina. Katika wakati wake bora nchi ya Palestina haikuwa na idadi ya wakazi waliozidi milioni mbili au tatu. Hata Palestina ya hivi sasa ina wakazi kati ya milioni moja na milioni moja na nusu. Wazo lolote la wingi zaidi ya wakazi hawa lapingwa sana na Waarabu. Zamani usafirishaji wa chakula haukujulikana. Halaiki kubwa ya wakazi isingeliweza kulishwa na nchi ambazo hazikuwa na mazao yao zenyewe. Wakazi wa Palestina wasingeliweza kuwa zaidi ya elfu chache. Katika habari za vita baina ya Waisraeli na maadui zao jumla ya idadi yao haikuzidi mia kadha au elfu cheche. Kama Nabii Musa[as] aliongoza Waisraeli milioni mbili u nusu mpaka Palestina, basi mbali na zile siku za kuwa jangwani, hata katika siku za kawaida chakula cha kutosheleza idadi kubwa kama hiyo kisingelipatikana. Ama kuhusu upinzani uliokabili umati huu mkubwa nchini Palestina, hapakuhitajika vita kuukomesha. Hii idadi yao kubwa ilitosha kuwafukuzilia mbali wenyeji wa asili.

(2) Vivyo hivyo katika Kitabu cha Kutoka 32:1-6 twasoma hivi:

> Watu walipoona ya kuwa Musa amekawia kushuka katika mlima, wakakusanyana wakamwendea Haruni, wakamwambia, Haya! Katufanyizie miungu itakayokwenda mbele yetu, kwa maana Musa huyo aliyetutoa katika nchi ya Misri hatujui yaliyompata. Haruni akawaambia, Zivunjeni pete za dhahabu

> zilizo katika masikio ya wake zenu, na wana wenu, na binti zenu, mkaniletee. Watu wote wakazivunja pete za dhahabu zilizo katika masikio yao, wakamletea Haruni. Akaipokea mikononi mwao akaitengeneza kwa patasi, akaifanya iwe sanamu ya ndama kwa kuiyeyusha; nao wakasema, Hiyo ndiyo miungu yako, Ee Israeli, iliyokutoa katika nchi ya Misri. Naye Haruni alipoona jambo hili, akajenga madhabahu mbele yake; Haruni akatangaza akasema, Kesho itakuwa sikukuu kwa Bwana. Wakaondoka asubuhi na mapema, wakatoa dhabihu, wakaleta sadaka za amani, watu wakaketi kula na kunywa, wakaondoka wacheze.

Kwa vyovyote, haiyumkiniki, mtu ambaye amepata kusikia sauti ya Mungu awanasibishie wengine uwezo wa Kiungu. Mtu amwonaye ndovu hawezi akamchukulia kuwa ni panya. Mtu mwenye kuliona jua hawezi akalichukulia kuwa eti ni mshumaa. Mtu amwonaye mtu mwingine hawezi akamchukulia kuwa ni mnyoo. Itakuwaje kwa Nabii ambaye amemwona Mwenyezi Mungu na kusikia sauti yake kuweza kumchukulia ndama wa dhahabu kuwa ni Mungu. Kughafilika kama huku sisi hatukutarajii hata kwa mtu punguani, achilia mbali Nabii wa Mungu. Jamii nzima ya Waisraeli ilisameheka. Wao hawakuwa wamepata kumwona Mungu wala hawakuwa wamesikia sauti Yake. Walikuwa wamewasikia tu Nabii Musa na Haruni[as] wakiwazungumzia na wakatokea kuamini yale waliyoyasikia. Hivyo basi wao walikubali lolote lile Samiri alilowafundisha juu ya ndama wa dhahabu. Lakini haiwezekani hata hivyo, sawa na maneno ya Biblia, kumtoa lawamani Nabii Haruni. Yeye alikuwa amemwona Mungu na alikuwa amesikia sauti Yake. Aliwezaje basi kudanganywa na Samiri na akatokea kumchukulia kuwa Mungu yule ndama wa dhahabu aliyetengenezwa na mikono ya wanadamu? Je, yawezekana ya kwamba Mungu Mwenye Kujua yote Ambaye Yuajua siri za vina za nyoyo za wanadamu awe alichagua kwa minajili ya marekebisho ya Israeli mtu ambaye alikuwa yuaja kuwa dhaifu vile alivyothibitika Nabii Haruni kulingana na kisa hiki? Hata wafalme wa kawaida

waweza kuchagua majemadari wafaao na magavana wakuu, na wanajiletea heshima kama wanafanya hivyo, hata hivyo hapana mfalme awezaye kusoma nyoyo za majemadari wake. Lakini sawa na Biblia, Mungu ajua siri zote na yuajua zaidi ya mwanadamu yeyote au mfalme yeyote. Lakini, Yeye alimchagua Nabii Haruni[as] na kumpatia jukumu la kuwarekebisha watu na Akaongea naye na Akajidhihirisha kwake. Lakini Samiri alipomhubiria Nabii Haruni[as] mafundisho yake ya kikafiri, eti Nabii Haruni[as] aliyakubali mafundisho haya na kufuatia ushauri wa watu wake yeye akatengeneza sanamu ya ndama wa dhahabu, akaiweka juu ya madhabahu na akaitangaza kuwa ni mungu! Eti Nabii Haruni[as] akamsahaulia mbali Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kuwaogopa watu wake, akasahaulia mbali kile alichowajibishwa kufundisha, akasahau wajibu wake, akasahau hekima zake zote na, chambileche mpumbavu mshirikina, yeye akaanza kukiinamishia kichwa kitu kisichokuwa na uzima. Wale waliopenyeza dhana zao katika Biblia yamkini walikuwa na akili finyu. Lakini huu ukweli ya kwamba wao walifikiria eti wale watakaokuja baadaye wasingeweza kugundua nyongeza hizi washangaza mno. Hata hivyo, ingali bado ni kweli kwamba baada ya aina hii ya nyongeza hatari Torati haikuweza kubakia na sifa yake ya kitabu kilichofunuliwa. Ilihitaji kitabu kingine kafichue upuuzi wake na kwa mara ya tena kuirejeshea dunia imani ya kwamba Nabii Haruni[as] hakuwa kafiri wala mshirikina. Kitabu hicho ndiyo Kurani. Kilimwondolea Nabii Haruni[as] tuhuma ya ukafiri. Badala ya yeye mwenyewe kuwa eti kafiri, aliwakanya watu wake dhidi ya hii tabia mbovu. Twasoma katika Kurani:

> Na bila shaka Haruni alikwisha waambia zamani, Enyi watu wangu! Hakika nyinyi mmefitinishwa tu kwa kitu hiki na kwa yakini Mola wenu ni Mungu wa rehema, basi nifuateni na tiini amri yangu (Sura Twaa Haa, 20:91).

Kutokana na maneno haya ni wazi kwamba hata kabla Nabii Musa[as] hajarudi toka Mlima wa Sinai, Nabii Haruni[as] alikuwa amewaonya Waisraeli ya kuwa yule ndama wa dhahabu alikuwa ametengenezwa

kuwapotosha, na Mola alikuwa ni Yule Mungu aliyekuwa amewaandalia vitu vyote vya maishani hata kabla hawajazaliwa. Alikuwa amewaambia kwamba yule ndama alikuwa ametengezwa mbele ya macho yao. Kwa hiyo, ilikuwa ni juu yao kumfuata Nabii Haruni, kumtii na kujiepusha na kila aina ya ukafiri.

Ni juu ya watu wote wenye akili zao kufikiria kama kitabu alichokifunuliwa Nabii Musa[as] chapasa kuendelea, kusimamia imani yetu, kinapoanza kuhitilafiana na ukweli uliothibitika na kuingiza itikadi za kijinga. Je, hatupaswi kutafuta kitabu kitakachobidi kutuambia ukweli juu ya matukio ya zama za Nabii Musa[as] hata kiwe kitakaja miaka elfu mbili baadaye.

(3) Katika Kitabu cha Mwanzo I9:26 twasoma:

> Lakini mkewe Lutu akatazama nyuma yake, akawa nguzo ya chumvi.

Haya yaonekana kama 'uchawi'. Kisa kama hiki ni stahili ya ngano waambiwazo watoto juu ya vizuka na vizimwi. Hakina nafasi katika Kitabu cha Mungu. Maelezo ambayo Kurani imeyaelezea kuhusu tukio hili yameepukana na ushirfkina wote. Yasema Kurani:

...Isipokuwa mke wake, alikuwa miongoni mwa wakaao nyuma (Sura Al-A'raaf, 7:84).

Hakugeuzwa nguzo ya chumvi au kitu chochote cha aina hiyo. Alikataa kufuatana na Nabii Luti[as] na akatanguliza mapenzi ya nduguze mbele ya mapenzi ya Mungu.

Ndani ya Kurani mmeelezwa matukio yahusikanayo na wakati wa Nabii Musa[as]. Torati ya hivi sasa yayaelezea matukio hayo kwa njia isiyokuwa sawa lakini Kurani iliyokuja miaka elfu mbili baadaye, yaweza kuyasahihisha masimulizi haya. Yale makosa ambayo Kurani inayataja yanakubalika akilini mara moja.

MANABII WAMESINGIZIWA NA BIBLIA

Hali kadhalika yamepenya katika Biblia maneno ambayo ni ufasiki

katika maana zao. Yaonekana haiwezekani kumnasibishia Mwenyezi Mungu wala Manabii Wake matendo yanayoripotiwa katika maneno hayo.

(1) Katika Kitabu cha Mwanzo 9:20-22 twasoma maneno haya:

> Nuhu akaanza kuwa mkulima, akapanda mizabibu; akanywa divai, akalewa; akawa uchi katika hema yake. Hamu, baba wa Kanaani, akaona uchi wa baba yake, akawaeleza ndugu zake wawili waliokuwa nje.

Habari hii inamwonyesha Nabii Nuhu[as] kwa njia mbaya kupindukia. Kulingana nayo Nabii Nuhu[as] alipanda mizabibu, akapiga mtindi, akawa uchi hemani mwake, mwanawe Hamu akamwona akiwa uchi na akawaambia kaka zake. Habari hii haiko katika hali ya kumsifu Nabii Nuhu[as] kabisa, na huku juu ya Nabii Nuhu[as] twasoma katika Mwanzo 6:9:

> Nuhu alikuwa mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake; Nuhu alikwenda pamoja na Mungu.

Ni jambo lisilofikirika kwamba mtu kama huyu angefanya aibu ya kuwa uchi machoni pa wanawe. Basi ni jambo linalokera uamuzi wetu wa kiutu kufikiria kwamba aibu ifanywe na Nabii Nuhu[as] lakini laana asukumiwe Hamu. Kosa la Hamu, hata kulingana na maneno ya Biblia yenyewe, lilikuwa ni kumwona babake akiwa uchi lakini hata hivyo yeye asingeweza kufanya jingine. Alipomkuta babake akiwa mlevi na uchi, isngewezekana kwake yeye kukosa kumwona katika hali aliyokuwemo lakini hata hivyo sawa na Biblia Nabii Nuhu[as] alitamka akisema, "Na alaaniwe Kanaani".

Kwa kweli Kanaani siye wa kulaumiwa hata kidogo. Kanaani alikuwa mwana wa Hamu, aliyefanya ile aibu isiyoepukika ya kumwona babake aliye uchi. Lakini hata hivyo Nabii Nuhu[as] hakuwa na la kusema katika kumshutumu Hamu. Yeye alimlaani Kanaani, asiyelaumika hata kidogo. Je, hii ni kwa sababu Hamu alikuwa ni mwanawe na Kanaani alikuwa mjukuu wake! Tabia sampuli hii

yachukiza mizani yetu ya kiutu na haiwezi ikansibishiwa Nabii. Kuinasibishia Nabii ni jambo la aibu kwa mwenye kujaribu kufanya hivyo. Hata hivyo twaweza kufahamu vyema, kwamba mambo haya hakufunuliwa Nabii Musa[as] na Mwenyezi Mungu, wala Nabii Musa[as] hakuyafanya yaandikwe katika kitabu chake. Wanazuoni wa Kiyahudi wawaelezeao Manabii kuwa wezi na wanyang'anyi ni sharti walipenyeza vitu hivi katika kitabu cha Nabii Musa kama funikizo ya madhambi yao wao wenyewe. Uingiliaji wao haramu wa Kitabu cha Mungu uliifanya kuwa lazima ya kwamba Mungu afunue kitabu kingine kitakachobidi kuepukana na upuuzi na upotovu vilivyokuwa vimepenya katika hicho kitabu cha hapo kale.

(2) Katika Mwanzo 19:30-36) twasoma maneno haya:

> Lutu akapanda kutoka Soari akakaa mlimani, na binti zake wawili pamoja naye, kwa sababu aliogopa kukaa katika Soari. Akakaa katika pango, yeye na binti zake wawili. Yule mkubwa akamwambia mdogo, Baba yetu ni mzee, wala hakuna mtu mume katika nchi atuingilie kama ilivyo desturi ya dunia yote. Haya, na tumnyweshe baba yetu mvinyo, tukalale naye, ili tumhifadhie baba yetu uzao. Wakamnywesha baba yao mvinyo usiku ule, akaondoka huyo mkubwa akalala naye, wala yeye hana habari alipolala wala alipoondoka. Ikawa siku ya pili, mkubwa akamwambia mdogo. Tazama, nimelala jana na baba yangu, tumnyweshe tena mvinyo usiku huu, ukaingie ulale naye. Wakamnywesha tena baba yao mvinyo usiku ule, akaondoka mdogo akalala naye, wala yeye hana habari alipolala wala alipoondoka. Basi hao binti wote wawili wa Lutu wakapata mimba kwa baba yao.

Hapana haja ya maelezo ya masimulizi haya machafu. Masimulizi haya yanatusi tabia yetu ya kutaka kusema ukweli na ya kiutu. Lakini Torati ya hivi sasa haioni haya kukinasibishia Nabii kisa hiki. Kutokana na masimulizi haya hatuna budi kusema kwamba Torati, vile tuijuavyo leo hii, siyo ile Torati iliyofunuliwa kwa Nabii Musa[as]

Ni lazima Torati hii ya leo iwe iliandikwa baadaye na wanazuoni wa Kiyahudi katika ule wakati walipokuwa wao wamepatwa na chuki dhidi ya wana, wa damu au wa kudhania tu, wa Nabii Luti[as], akina Moab na Ammon. Imani ya wanazuoni hawa wa Kiyahudi ilikuwa imedhoofika, nyoyo zao zilikuwa zimekuwa ngumu hivi kwamba ili kuwasingizia akina Moab na Ammon wao hawakuona haya kumnasibishia Nabii Luti[as] tabia inayolaumika vilivyo na tabia ambayo unasibishaji wake kwa Nabii yeyote hauvumuliki hata kidogo. Je, ulimwengu wa Kikristo na ule wa Kiyahudi leo hii uko tayari kusikia vitu sampuli hiyo vikinasibishiwa Manabii wa Mungu. Kama wako tayari, basi huo ni ushahidi mwingine tu kwamba ilibidi tupate kitabu kikosoe fikara potovu za wakati huu wetu.

(3) Katika Kitabu cha Kumbukumbu la Torati 25:5-6 twasoma maneno haya:

> Wanapoketi pamoja mtu na nduguye, mmojawapo akafa, wala hana mwana wa kiume, mke wa yule aliyekufa asiolewe nje na mgeni; nduguye yule mumewe amwingilie amweke kwake awe mkewe, kumfanyia yampasayo nduguye mumewe. Na iwe, yule mzaliwa wa kwanza atakayemzaa, amfuate nduguye aliyekufa kwa jina lake, lisije likafutwa jina lake katika Israeli.

Mafundisho haya ni mapotovu kupindukia. Yanamruhusu mjane kumwangukia miguuni ndugu ya mumewe na kupata watoto ili wawe watarithi katika jina la marehemu mumewe. Je, wanaweza watoto waliozaliwa na mtu mmoja kuendeleza jina la mtu mwingine? Kama watoto aliowazaa ndugu ya mtu wanaweza wakaendeleza jina lake, basi pana haja gani ya huyu ndugu kufanya unyumba na mjane wa mtu? Kama mwana wa ndugu anaweza akachukuliwa kuwa kama mwana halisi wa mtu, basi hapana haja ya kumruhusu ndugu kufanya unyumba haramu na mke wa mtu. Ingelikuwa afadhali kwa Biblia kutangaza kwamba miongoni mwa hao wana wa ndugu mmoja anaweza akanasibishwa na huyo ndugu mfile. Hii ingelikubalika kidogo. Lakini yaonekana kwamba wanazuoni wa Kiyahudi

walikoroga masingizio machafu dhidi ya Nabii Luti[as], hivyo basi Mungu akawafanya wapenyeze katika Torati agizo ambalo athari yake mbaya iwe itawarejelea hao wanazuoni wa Kiyahudi ambao walikuwa wamejaribu kumsingizia Nabii Luti[as]. Kisasi cha Mwenyezi Mungu kilikuwa ni cha kutisha lakini kilichostahili. Wanawake wa Kiyahudi wakachongewa na agizo lililobuniwa na wanazuoni wa Kiyahudi kutenda kile wasingiziaji wa Kiyahudi walichokuwa wamemnasibishia Nabii Luti[as]. Dosari hizi za Agano la Kale zaashiria kwa uwazi haja ya kitabu halisi kitakachobidi kuepukana na kasoro hizi zote, na kitabu chenyewe ndicho Kurani.

AGANO JIPYA LACHUNGUZWA

Tumeona ya kwamba Agano la Kale limefanyiwa uchafuzi kidhahiri na kibatini. Haiwezekani tena kulitumia kama mwongozo. Hebu sasa na tugeukie Agano Jipya.

Vile vitabu vilivyokusanywa katika sura ya Agano Jipya siyo maneno ya Yesu wala ya wanafunzi wake. Yesu alikuwa Myahudi na wanafunzi kadhalika. Kama maneno yoyote ya Yesu yangekuwa yapatikane yakiwa yamehifadhiwa vile yalivyokuwa hapo awali, basi yangeweza kupatikana tu katika lugha ya Kiebrania, na hali kadhalika maneno ya wanafunzi wake. Lakini hapana hata nakala moja ya Agano Jipya katika lugha ya Kiebrania cha kale ipatikanayo duniani. Nakala za hapo zamani zote ziko katika lugha ya Kigriki. Waandishi wa Kikristo hutafuta kuziba hii kasoro kubwa kwa kudai eti katika wakati wa Yesu lugha iliyotumika kwa kawaida ilikuwa ni Kigriki. Hii haiwezekani kwa sababu zaidi ya moja. Mataifa hayatupilii mbali lugha yao kwa urahisi. Kwao, lugha ni urithi wenye thamani kama rasilimali yoyote au miliki. Huko Ulaya ya Mashariki kuna watu ambao wameishi miaka mia tatu au nne chini ya utawala wa Kirusi, lakini lugha zao zimebakia vile vile hadi leo. Ufaransa imeiitawala nchi ya Moroco, na Uhispania nchi ya Aljeria kwa muda mrefu mno, hata hivyo lugha ya watawaliwa hawa bado ni Kiarabu. Miaka elfu mbili imepita tangu wakati wa Yesu, hata hivyo Mayahudi bado

hawajasahau lugha yao. Hata hivi leo katika maeneo kadha ya Ulaya na Marekani Mayahudi bado wanaongea lugha ya Kiyidish, namna ghafi ya lugha ya zamani ya Kiebrania. Kama huu muda mrefu uliopitishwa miongoni mwa watu wengine haukuifutilia mbali lugha ya Kiyahudi, je, muda mfupi wa kushirikiana na Warumi ungeweza kweli kufanya hivyo? Na tukumbuke kwamba utawala wa Kirumi nchini Palestina ulikuwa umeanza kama miaka hamsini tu kabla ya ujaji wa Yesu. Huu sio muda mrefu wa kutosha watu kuisahaulia mbali lugha yao. Lakini yapo pia mambo mengine muhimu ya kutiliwa maanani.

(i) Mataifa yajipatiayo umuhimu wowote katika historia hayatupilii mbali lugha yao, na Mayahudi walikuwa watu muhimu kwa hakika.

(ii) Dini ya Mayahudi iliandikwa katika lugha ya Kiebrania, na hususan kwa sababu hii, haikuwezekana kwao kutupilia mbali lugha yao.

(iii) Katika mizani za ustaarabu na uungwana, Mayahudi hawakujichukulia kuwa ni duni mbele za Warumi, bali walijiona kuwa ni bora, na hali hii haikosi iliwafanya wajivunie lugha yao na kutokuwa tayari kuitupilia mbali.

(iv) Mayahudi walitumainia kurejea kwa nguvu zao za kisiasa. Mataifa yanayoziogopa siku za usoni hukata tamaa na hivyo basi huelekea kutojivunia lugha yao. Lakini Mayahudi katika wakati wa Yesu walikuwa wakingojea ujaji wa Mfalme wao aliyekuwa aje kusimika kwa mara ya tena utawala wa Kiyahudi. Katika hali ya kuzitumainia siku za usoni jinsi hiyo, wao wasingeliweza kuwa wazembe katika kuinusuru lugha yao.

(v) Waandishi wa Kiyahudi wa wakati ule waliandika katika lugha yao wenyewe au katika namna ghafi ya lugha hiyo. Kama lugha yao ilikuwa imebadilika, basi tusingelikuwa na budi kupata vitabu vya wakati ule vilivyoandikwa katika lugha minghairi ya Kiebrania.

(vi) Miswada ya zamani zaidi ya Agano Jipya iko katika lugha ya Kigriki. Lakini katika wakati wa Yesu, Ufalme wa Kirumi bado

ulikuwa haujagawanyika katika nusu mbili. Makao Makuu ya Ufalme huo bado ulikuwa ni mji wa Roma. Lugha za Kirumi na Kigriki ni ngumu sana. Kama athari za utamaduni wa Kirumi zilikuwa zimepenya hata kidogo katika maisha ya Kiyahudi, basi jambo hili lisingelikuwa na budi kuwa na matokeo ya kuchanganyika kwa maneno ya lugha ya Kilatini (sio Kigriki) katika lugha ya Kiebrania. Lakini hata hivyo miswada yote ya zamani sana ya Injili iko katika lugha ya Kigriki. Jambo hili lathibitisha kwamba Injili ziliandikwa katika wakati ambapo ufalme wa Kirumi ulikuwa umegawanyika na maeneo yake ya mashariki yakawa ni sehemu ya Ufalme wa Kigriki, kwa hiyo lugha ya Kigriki ilikuwa imeanza kuuelekezea Ukristo athari zake na vitabu vyake.

(vii) Maneno kama haya yafuatayo yanayohifadhiwa ndani ya injili katika hali yao asilia yote ni maneno ya Kiebrania.

(1) Hosana" (Mt. 21:9).

(2) "Eloi, Eloi, lama sabakhthani" (Mt. 27:46).

(3) "Rabi" (YN. 3:2).

(4) "Talitha, kumi" (Mk. 5 :41).

(viii) Kutokana na Kitabu cha Matendo (2:4-13) yaonekana kwamba hata baada ya tukio la msalaba, Mayahudi waliongea Kiebrania:

> Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka. Na walikuweko Yerusalemu Wayahudi wakikaa, watu watawa, watu wa kila taifa chini ya mbingu. Basi sauti hii iliposikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa kila mmoja aliwasikia kwa lugha yake mwenyewe. Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, Tazama, hawa wote wasemao si Wagalilaya? Imekuwaje basi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo? Waparthi na Wamedi na Waelami, nao wakaao Mesopatamia, Uyahudi na Kapadokia, Ponto na Asia, Frigia na Pamfilia, Misri na pande za Libia karibu na Kirene, na

> wageni watokao Rumi, Wayahudi na waongofu, Wakrete na Waarabu; tunasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu. Wakashangaa wote wakaingiwa na shaka, wakiambiana, Maana yake nini mambo haya? Wengine walidhihaki, wakisema, Wamelewa kwa mvinyo mpya.

Ni dhahiri kwamba wakati huo lugha iliyokiongewa nchini Palestina ilikuwa ni Kiebrania. Kuongea lugha nyingine lilikuwa ni jambo geni. Miongoni mwa majina yanayotajwa ni Roma, ikimaanisha kwamba lugha ya Kirumi haikuongewa nchini Palestina na yeyote aliyeiongea alionekana kuwa yu mgeni. Hapa sisi hatuitazami habari yenyewe bali tungependa tu kusema ya kwamba maneno haya ya Kitabu cha Matendo yathibitisha kuwa hata baada ya tukio la msalaba lugha ya Mayahudi ilikuwa ni Kiebrania. Wale waliojua lugha zingine walikuwa watu baki. Wakati baadhi ya wanafunzi wa Yesu walipozungumza hizi lugha zingine — kikiwemo Kilatini, watu wengine waliwadhania kuwa wamelewa wakibubujikwa na porojo. Kama nchi kwa jumla ilitumia Kigriki, basi dhana sampuli hii isingeliwezekana.

Kwa hiyo ni wazi ya kwamba lugha amabyo Yesu na wanafunzi wake walizungumza ilikuwa ni Kiebrania, wala sio Kilatini au Kigriki. Hivyo basi, nakala za Agano Jipya zilizoandikwa katika lugha ya Kilatini au Kigriki ni sharti ziwe ziliandikwa muda mrefu baada ya wakati wa Yesu, zama ambapo Ukristo ulikuwa umeanza kulipenya eneo la Kirumi na ambapo dola hilo la kikoloni lilikuwa limegawanyika katika sehemu ya Kiitalia na Kigriki. Vitabu sampuli hii, vilivyoandikwa na waandishi wasiojulikana miaka mia mbili au tatu baada ya Yesu na kisha waandishi hao kuvinasibishia Yesu na wanafunzi wake, vinaweza kuwa na manufaa kidogo tu kwa muumini wa hivi leo. Kwa hiyo, lilikuwa jambo la lazima kwamba tuwe tulipata kitabu tulicholetewa toka mbinguni, kisichokuwa na dosari hizi na kile wangelichoweza wasomi kukichukulia kwa yakini kuwa ni neno hasa la Mwenyezi Mungu.

YESU MWENYEWE YUATANGAZA

Yesu yuatangaza kwa uwazi ya kuwa hakuwa amekuja kutangua bali kuvitimiliza vitabu vya hapo kale. Ndiposa katika Kitabu cha Mathayo (5:17-18) twasoma maneno haya:

> Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie.

Kutokana na haya ni dhahiri kwamba kazi hasa ya Yesu ilikuwa ni kuhuisha mafundisho ya Nabii Musa[as], lakini Agano Jipya vile tulivyo nalo leo hii lafundisha kwamba mafundisho ya Nabii Musa[as] yalitanguliwa mbali na Yesu. Ni wazi kabisa, kwa hiyo, ya kwamba Agano Jipya la hivi sasa silo lile alilolifundisha Yesu na kulihubiri. Mafundisho ya Yesu hayana budi yawe yalikuwa ni machipuko ya mafundisho ya Nabii Musa[as], isipokuwa yale ambayo Waandishi na Mafarisayo waliyokuwa wameyaongezea wao wenyewe. Lakini Agano Jipya latafuta kusahihisha sio tu yale ambayo Waandishi na Mafarisayo walikuwa wameyatunga bali hata yale mafundisho ambayo Nabii Musa[as] na Manabii wa baadaye walikuwa wamefundisha katika wakati wao. Hii ni hali ya kuhitilafiana. Sehemu moja ya Agano Jipya yafundisha jambo moja, sehemu nyingine yafundisha jambo jingine kabisa. Kitabu kinapojihitilafisha, basi hicho hakiwezi kuwa ni kazi ya mwandishi yule yule mmoja, bali kwa vyovyote vile, hakiwezi kuwa ni kazi ya mwandishi mwenye akili zake. Vitabu vya Agano Jipya vyasemekana kuwa eti viliandikishwa na wanafunzi wa Yesu, nasi wala hatuwezi tukasema kwamba hao wanafunzi hawakuwa na akili zao. Wanafunzi wakubwa wakubwa wa Manabii daima huwa na kiwango cha juu cha akili timamu. Hivyo basi, hatuna budi kuamua kwamba wanafunzi hao hawakuandikisha kitu chochote cha aina hiyo. Waliongea walipokuwa wakizunguka. Wale waliowasikia waliwaelezea wengine tafsiri ya yale waliyokuwa wameyasikia wao wenyewe. Na hawa wengine nao zama walipoketi

kuyarekodi yale waliyokuwa wameyasikia, wakapenyeza humo mengi ya mawazo yao wenyewe. Matokeo yake yakawa ni hili Agano Jipya vile tulijuavyo leo hii, furushi zima la mahitilafiano.

USHAHIDI WA WANAZUONI WA KIKRISTO

Baada ya kutaja ushahidi wa ndani wa hali ya kuchanganyikiwa ya Agano Jipya, sasa twakariri ushahidi wa wanazuoni wa Kikristo:

(i) Katika maelezo ya Biblia yaliyoandikwa na Bwana Horn (mwaka 1882) tunayo haya maneno ya kwamba mambo yahusikanayo na utungo wa Injili, ambayo yametufikia toka wanahistoria wa Kanisa, wa hapo kale, yana tashwishi tena ni dhaifu kiasi hiki kwamba hapana uamuzi wenye uhakika unaoweza kufanywa kutokana nayo. Hata wanahistoria wa kutegemeka ni kama wanazichukulia kuwa ni ukweli mtupu zile dhana zilizokuwepo wakati wao, na kwa kuwastahi tu wale wanaokuja baadaye wanakubali maoni ya wanahistoria hao. Masimulizi yenyewe, huku urongo huku ukweli, hupita toka mwandishi mmoja hadi mwingine na baada ya muda huanza kuchukuliwa kana kwamba hayadadisiki tena (J. 4, Sehemu ya 2, mlango wa 2).

(ii) Katika jalada hilo hilo tunayo hii habari ya kwamba Injili ya awali yaonekana ilirekodiwa katika mwaka wa 37 au 38 au 41 au 43 au 48 au 61-62 au 64 A.D.; na ya pili iliandikwa katika wakati wowote ule kuanzia mwaka wa 56 mpaka 65 A.D., pengine baina ya mwaka wa 60 na 63; na ya tatu katika mwaka wa 53 au 63 au 64; na Injili ya nne katika mwaka wa 68 au 69 au 70 au 97 au 98 A.D. Ushahidi kuhusu Waraka kwa Waebrania, Waraka wa pili wa Petro na Waraka wa pili na wa tatu wa Yohana, Waraka wa Yakobo na Waraka wa Yuda, Ufunuo wa Mt. Yohana mbatizaji na Waraka wa kwanza wa Yohana, umevurugika kiasi cha sisi kutokuwa na haja ya kuuzungumzia. Nyaraka hizi zimenasibishiwa wanafunzi wa Yesu bila ya sababu zozote za kuridhisha.

(iii) Bwana Usebio (Eusebius) katika kitabu chake kiitwacho History of the Church yuaandika kwamba Waraka wa kwanza wa Petro ni halisi. Waraka wake wa pili haujapata kuwa sehemu ya Kitabu

Kitakatifu, lakini umekuwemo kisomoni (J. 4, mlango wa 3).

(Iv) Katika kitabu hicho hicho (mlango wa 25) twasoma ya kwamba Waraka wa Yakobo na Waraka wa Yuda na Waraka wa pili wa Petro na Waraka wa Yohana wa kwanza na wa pili zote zimetiliwa shaka sana. Haijulikani kama nyaraka hizi ziliandikwa na waandishi wa Injili ama na watu wengineo wenye majina kama yao.

(v) Katika kitabu kiitwacho Encyclopaedia Biblica J. iv, uk. 4980) tuko na maneno haya:

> Agano Jipya liliandikwa na Wakristo kwa ajili ya Wakristo; na zaidi ya hayo liliandikwa kwa Kigriki kwa ajili ya jamii zenye kuzungumza Kigriki, na mtindo wa kuandika (isipokuwa labda, Kitabu cha Ufunuo) ulikuwa ni ule ule mtindo uliokuwepo wa mitungo iliyoandikwa. Hapajatokea ukatizaji wa maana wa hali ya kuendelea kwa Kanisa liongealo Kigriki na twakuta kulingana na hali hii ya kwamba yapatikana makosa makubwa machache ya kimaandishi katika aina maarufu za maandiko yaliyopo. Hali hii ya mambo yalivyo haikuzuia ugeuzaji; lakini ugeuzaji wenyewe mara nyingi sio wa bahati. Idadi iliyo kubwa sana ya sahifa mbalimbali za miswada ya Agano Jipya ndizo zilikuwa ni ugeuzaji wa awali wa kimataifa. Agano Jipya katika zama za mwanzo mwanzo halikutambulikana kidini, na ugeuzaji na upachikaji ukafanywa pale ilipoonekana kuwa hayo ndiyo matengenezo yenyewe.

Hii maana yake ndio kusema kwamba Agano Jipya liliandikwa na Wakristo kwa ajili ya Wakristo. Aidha, liliandikwa kwa Kigriki kwa ajili ya watu wenye kuongea Kigriki, na mtindo wake wa kimaandishi ulikuwa ni ule ule uliokuwepo kwa kawaida. Hapajatokea ukatizaji wa maana wa kuendelea kwa Kanisa lenye kuongea Kigriki. Hamna, kwa hivyo, makosa makubwa ya yale majalada yaliyopo ingawaje hatuwezi tukasema kwamba hamna hitilafu. Na hata hivyo, hitilafu zenyewe sio za bahati, bali za makusudi tu. Yaonekana kwamba tangu hapo mwanzoni baadhi ya waandishi walipenyeza mageuzi haya ndani ya maandiko ya Agano Jipya.

Ukweli wenyewe waelekea kuwa ni huu ya kwamba Agano Jipya hapo mwanzoni halikuchukuliwa kuwa ni kitabu kilichofunuliwa. Hivyo basi, yakafanywa matengenezo bila ya kusita popote pale matengenezo yenyewe yalipowezekana.

(vi) Halafu twasoma maneno haya:

> La hakika ni kwamba kufikia katikati ya karne ya nne, miswada ya Biblia ya Kilatini ilidhihirisha hali ya maandiko yaliyovurugika zaidi, iliyosababishwa bila shaka kwa upande mmoja na kusahihishwa kutoka miswada ya baadaye ya lugha ya Kigriki na pia ugeuzi wa mbinu za matumizi ya maneno ya Kilatini. Kuvurugika huku kulidumu hadi mahali pa maandiko yote 'Kilatini cha Kale' palipochukuliwa na yale yaliyosahihishwa ya Jerome (383-400 A.D.), kazi iliyokuwa imefanyika kufuatia ombi la Papa Damasus na maandiko ambayo hatimaye yalikuwa ndiyo Biblia ya Kilatini ya Kanisa la Magharibi (Enc.Bib. uk. 499 J. iv).

Ukweli wenyewe ni kwamba kwenye katikati ya karne ya nne, nakala ya Biblia ya Kilatini ilikuwa katika hali ya kuvurugika kabisa. Kuvurugika kwenyewe kulikuwa ni matokeo ya malinganisho na nakala ya Kigriki na aidha yalikuwa ni matokeo ya ugeuzaji katika istilahi za Kilatini. Kuvurugika huku kulidumu hadi yalipowasilishwa maandiko yaliyosahihishwa ya Jerome, yaliyotayarishwa chini ya amri ya Papa baina ya mwaka 383 na 400 A.D., na kuchukua baina ya Wakristo mahali pa yale maandiko ya kale ya Kilatini.

(vii) Vivyo hivyo tunayo maneno haya:

> Ya muhimu zaidi ya mambo haya ya kinjenje ni yale mageuzi ambayo baada ya muda yalipenya ndani ya matini yenyewe. Mengi ya mageuzi haya yalikuwa ni mtelezo wa jicho, au sikio, ufahamu, au maamuzi kwa upande wa mnakili ambaye hakuwa na nia ya kufanya chochote minghairi ya kufuata kilichokuwa mbele yake. Lakini wanakili, hususan wanakili wa hapo awali, kwa vyovyote vile hawakuazimia ule usahihi wa kukata na shoka anaoutazamiwa mhariri aliye macho wa hivi leo. Masahihisho

yalifanywa kwa ajili ya sarufi au fani ya uandishi. Mabadiliko madogo madogo yalifanywa kusudi kulainisha ugumu, mazidisho yakajipenyeza, hususan kutoka masimulizi yanayokwenda sambamba katika Injili, marudio kutoa Agano la Kale yalisawazishwa zaidi au kukamilishwa zaidi. Jambo hili kwamba haya yote yalifanywa kwa uaminifu — tena kwa kuwa haikuwepo picha waziwazi ya jukumu la mnakili — ni wazi sana kutokana na kutokuwepo kabisa kwa uchafuzi wa makusudi wa maandiko kwa faida ya ubishi wa kiitikadi. Pengine yatosha kusema, pamoja na yaliyokwishasemwa, ya kwamba maelezo ya maneno au vikumbusho ambavyo awali viliandikiwa pembezoni, mara nyingi viliishia kupenyezwa katika matini, na kwamba desturi ya kusoma maandiko kwenye hadhara za ibada bila shaka kulileta nyongeza za kikawaida za ibada, kama wimbo wa kumsifu Bwana katika sala yake; wakati ambapo kuanza kwa mahubiri ya Kikanisani kukiwa kumetenganishwa mbali na maneno yake ya asili kulikuwa mara nyingi kukitiliwa nyongeza za baadhi ya maneno ya kuelezea, ambayo muda si muda yalikuja kuchukuliwa kuwa ni sehemu ya maneno ya asili (Enc. Brit. Toleo la 12, uk. 646, J. III).

(viii) Tena tunayo maneno haya:

Ni wazi kutokana na yale ambayo tayari yameshayaona kwamba sehemu kubwa sana ya Agano Jipya ni maneno yasiyokuwa ya kinabii moja kwa moja (Enc. Brit. toleo la 12, uk. 643, Dal. III).

(ix) Na tena:

Lakini hata hivyo, kusema kweli, kila kitabu ndani ya Agano Jipya, isipokuwa zile Nyaraka kuu nne za Mt. Paulo, leo hii ni kitu chenye ubishi, imesemwa kuwa zimetiwa maneno yasiyokuwamo humo zilipoandikwa hizi. (Enc. Brit. toleo ya I2, uk. 643, J. III).

(x) Agano Jipya halikuepukana hata hivi leo na mapachiko na magezo. Tunayo maneno yafuatayo kama mifano:

(i) Katika Injili ya Yohana (5:2-5) tulikuwa na maneno haya:

> Na huko Yerusalemu penye mlango wa kondoo pana birika, iitwayo kwa Kiebrania Bethzatha, nayo ina matao matano. Ndani ya hiyo jamii kubwa ya wagonjwa walikuwa wamelala, vipofu, viwete, nao waliopooza, [wakingoja maji yachemke. Kwa maana kuna wakati ambapo malaika hushuka, akaingia katika ile birika, akayatibua maji. Basi yeye aliyeingia wa kwanza baada ya maji kutibuliwa, akapona ugonjwa wote uliokuwa umempata] Na hapa palikuwa na mtu, ambaye amekuwa hawezi muda wa miaka thelathini na minane. Yesu alipomwona huyu amelala, naye akijua ya kuwa amekuwa hali hiyo siku nyingi, alimwambia, Wataka kuwa mzima?

Kwa miaka mia nyingi tulikuwa na habari hii ikikaririwa katika Injili. Hapana aliyefikiri kwamba haikuwa na uhakika. Lakini pale ubishi ulipoanza baina ya Waislamu na Wakristo katika karne ya kumi na tisa, hapo maneno ya mstari wa nne na sehemu ya mstari wa tatu yakatupwa nje ya ile Biblia iliyosahihishwa na kutolewa kwenye mwaka 1881, kwa kuhofia shutuma za Waislamu, na ikadokezewa pembezoni kwamba majalada mengi ya hapo kale yanarekodi kikamilifu au sehemu tu ya maneo yaliyoachwa nje ya matini. Swali lenyewe ni kwamba kama hii sehemu ilipatikana katika majalada mengi ya hapo kale, basi huu ugeuzi ulifanywa kwa sababu gani. Isitoshe, ukweli wenyewe ya kuwa mstari fulani wapatikana katika nakala fulani na haumo katika nakala zingine ni thibitisho la ukweli kwamba matini ya asili imechafuliwa. Panaweza pakawa na mambo mawili tu. Ama tuwe tutakubali kwamba mstari wenyewe haukuwa ukipatikana katika matini ya asili. Hapo, itatubidi kufikia uamuzi kwamba waandishi fulani walifanya ujasiri wa kubuni maneno hayo wao wenyewe. Au tuwe tutakiri kwamba mstari huo ulipatikana katika matini ya asili. Na hapo basi itatubidi tuwe na maana ya kwamba waandishi fulani kwa makusudi waliutupa mstari wenyewe nje ya matini. Katika haya yote mawili matini itahesabiwa kuwa iliyochafuliwa.

(2) Katika Waraka wa I wa Yohana (5:8-9) tulikuwa na maneno haya:

> Kwa maana wako watatu washuhudiao [mbinguni, Baba, na Neno na Roho Mtakatifu, na watatu hawa ni moja. Kisha wako watatu washuhudiao duniani], Roho, na maji, na damu; na watatu hawa hupatana kwa habari moja.

Maneno yaliyonukuliwa hapo juu yalikuwa ni sehemu ya Agano Jipya kwa karne nyingi, lakini Wakristo walipobishana na Waislamu na Waislamu kuanza kuyaelekezea maneno sampuli hii shutuma zao, hapo Wakristo wakageuza matini ya Maandiko yao matakatifu na yale maneno yaliyo ndani ya mibano ya mraba yakatupwa nje ya Biblia iliyosahihishwa chapa ya 1881. Sasa swali ni hili, kama yale maneno yaliyotupiliwa mbali jinsi hiyo hayakuwa ni sehemu ya matini ya asili na yaliingizwa humo ndani na mtu fulani, basi hii yamaanisha kwamba hapo mwaka wa 1881 wanazuoni wa Kikristo walikiri kwamba maandiko matakatifu ya Kikristo yalikuwa yamechafuliwa. Lakini kama nakala za hapo kale zilikuwa sahihi na haya mageuzi ya hivi sasa yamefanywa kwenye matini kwa kutokuwa na budi kufanya hivyo, basi hii yamaanisha kwamba juhudi za kuchafua Maandiko ya Kikristo bado ziko mbioni.

(3) Katika Injili ya Mathayo 17:14-21 tunayo maneno haya:

> Nao walipoufikia mkutano, mtu mmoja akamjia, akampigia magoti, akisema, Bwana, umrehemu mwanangu, kwa kuwa ana kifafa, na huteswa vibaya; maana mara nyingi huanguka motoni, na mara nyingi majini. Nikamleta kwa wanafunzi wako, wasiweze kumponya. Yesu akajibu, akasema, Enyi kizazi kisichoamini, kilichopotoka, nitakaa pamoja nanyi hata lini? Nitachukuliana nanyi hata lini? Mleteni huku kwangu. Yesu akamkemea pepo, naye akamtoka; yule kijana akapona tangu saa ile. Kisha wale wanafunzi wakamwendea Yesu kwa faragha wakasema, Mbona sisi hatukuweza kumtoa? Yesu akawaambia, kwa sababu ya upungufu wa imani yenu. Kwa maana, amin, nawaambia, Mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali

> mtauambia mlima huu Ondoka hapa uende kule nao utaondoka; wala halitakuwako neno lisilowezekana kwenu. [Lakini namna hii haitoki ila kwa kusali na kufunga]

Wafasiri wa Kikristo, yaonekana, waamini kwamba baada ya kumwamini Yesu, hapana jambo jingine zaidi la amali njema linalohitajika, kujichumia radhi na upendo wa Mwenyezi Mungu. Lakini kutokana na maneno hayo ya Mathayo yaliyokaririwa hapo juu yaonekana kwamba kumbe shabaha hii tukufu haiwezi ikahitimishwa pasi na maombi na saumu. Hivyo basi, maombi na saumu ni vifaa muhimu vya kufaidia rehema ya Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa wanafunzi wa Yesu hawakuvitumia vifaa hivi, wao hawakuweza, sawa na hayo maneno ya Injili, eti kufukuzilia mbali pepo mbaya, licha ya ukweli kwamba wao walikuwa wametangaza imani yao juu ya Yesu. Wadadisi wa Kiislamu waliyatumia haya maneno ya Injili kwa ajili ya lawama muhimu. Walisema kwamba imani tu juu ya Yesu si hoja. Amali njema pia zilikuwa kitu cha lazima na Yesu mwenyewe alikuwa amesisitizia umuhimu wa maombi na saumu, naye alikuwa amezitumia njia hizi kama vifaa vya maendeleo ya kiroho. Kama sala na saumu navyo pia vilikuwa ni vitu vya lazima, basi kumwamini Yesu hakuwezi kukawa hoja tosha, wala kumwondolea mwanadamu faradhi ya kufanya amali njema. Lawama hii ilikuwa ni nzito kiasi hiki kwamba wafasiri wa Kikristo walijikuta wasioweza kutoa jibu lolote. Njia ya pekee waliyojipatia ya kuikwepa lawama hii ilikuwa ni kuifutilia mbali mstari huu kutoka Injili. Kwa hiyo, katika ile Injili rai ya Mathayo iliyosahihishwa, hatuukuti kabisa mstari huu. Mstari wote mzima umefutiliwa mbali na imethibitika ya kwamba matini ya Injili bado yakabiliwa na uingiliaji wa wanadamu.

Yasemewa kwamba katika Injili ya Marko (9:29) neno "maombi"(au sala) bado lingalipo; na kwamba kama ugeuzi ulikuwa umefanywa kutokana na nia yoyote mbaya, basi neno sala lisingeliweza kuwa limebakia katika Injili ya Marko. Lakini huu ndio udhuru usioridhisha. Shutuma za Waislamu hazikutokana na hili neno 'maombi' kwani maombi bado yanafanywa na Wakristo. Lawama hii

ilitokana na neno 'saumu'. Ule mstari ambao umefutiliwa mbali ulidhihirisha kwamba Yesu alikuwa na desturi ya kufunga saumu na aliichukulia saumu kuwa ibada ya lazima katika maendeleo ya kiroho; na hivyo basi Sheria isingeliweza kuhesabiwa kuwa ni laana. Ili kukwepa lawama hii mstari mzima ulitupiliwa mbali na Injili ya Mathayo na neno 'saumu' kufutwa katika Injili ya Marko. Yawezekana kwamba kundi moja la wasahihishaji waliona ni jambo la lazima kuutupa nje mstari mzima, wakati ambapo kundi jingine liliona ilitosha kulibandua neno 'saumu'.

HITILAFU KATIKA AGANO JIPYA

Halafu kunazo hitilafu katika masimulizi ya Injili na hitilafu kama hizi pia zadhihirisha kwamba Injili sio ufunuo wa Mungu au kwamba mwingilio wa wanadamu umeubadili ufunuo kabisa mpaka kutofambulika. Mwandishi yeyote wa kawaida mwenye msimamo wa kawaida wa kudumu hataruhusu hitilafu ndani ya anayoandika. Basi, tunawezaje kuvumilia hitifalu katika kitabu cha Mungu? Hapa tunatoa mifano kadha:

(i) Kuhusu kuzaliwa kwa Yesu twakuta katika Injili ya (Mathayo 1:1-22) na (Luka 1:32-33) ya kuwa Masihi alikuwa awe ni mmoja wa wanadamu wa kawaida, ila tu, yeye alikuwa aitwe mwana wa Mungu. Hata hivyo, kutokana na Injil ya Yohana (1:1) twakuta kwamba Masihi ni neno lililokuwa daima na Mungu na lilikuwa kwa kweli Mungu, hivi kwamba vyote vikaumbwa kutokana naye.

(ii) Kutoka Injili ya Mathayo (3: 13-17), Marko (1:9-12) na Luka (3:21-22 na 4:1) yaonekana kwamba Yesu alipokea ubatizo toka kwa Yohana na baada ya kupokea ubatizo toka kwa huyo Yohana, mara akaachana naye au aliachana naye siku hiyo hiyo. Lakini katika Injiii ya Yohana hamtajwi ubatizo wowote na ule mkutano wa Yesu na Yohana wasemewa uliendelea kwa siku mbili.

(iii) Kutoka Injili ya Yohana (1:19-44) yaonekana kwamba Yesu baada ya kukaa na Yohana na wanafunzi wake kwa siku chache alifululiza hadi Galilaya. Lakini toka Injili ya Mathayo (4:1), Marko:

(1:12) na Luka (4:1), yaonekana kwamba Yesu, baada ya kupokea ubatizo toka kwa Yohana, alienda zake nyikani ili akajaribiwe na Ibilisi, na akakaa huko siku arobaini.

(iv) Toka Injili ya Yohana (1:35-51) yaonekana kwamba, punde tu baada ya kukutana na Yohana, aliwafanya wanafunzi wawili wa Yohana, mmoja Andrea na mwingine asiyetajwa jina, kuwa wanafunzi wake yeye mwenyewe na huko njiani kwenda Galilaya akawafanya akina Simoni Petro na Nathanaeli kuwa wanafunzi wake. Lakini toka Injili ya Mathayo (4:12-22), Marko (1:12-20) na Luka (4:14-15; 5:1-11) yaonekana kwamba baada ya kukutana na Yohana na kukaa nyikani siku arobaini Yesu alifunga saumu, na aliposikia kutupwa gerezani kwa Yohana akaenda Galilaya, na kuhubiri huko mahali pengi na kwa siku nyingi, na kandoni mwa ziwa la Galilaya akawapokea akina Simoni Petro, Andrea, Yohana na Yakobo kama wanafunzi wake. Yaani, pale mahali ambapo, sawa na Injili ya Yohana, watu hawa walipochukuliwa na Yesu kama wanafunzi wake, sipo pale mahali ambapo sawa na Injili zingine, upokelewaji wa wenyewe ulifanyika. Wakati pia ambapo kukubaliwa kwenyewe kulifanyika sawa na Injili ya Yohana sio wakati unaotajwa na Injili zingine. Injili zingine zinautaja wakati wenyewe kuwa ni takriban miezi miwili baadaye.

(v) Katika Injili ya Yohana (4:3 na 43-45) twajulishwa kwamba kwao Yesu kulikuwa ni Judea, na kwamba Yesu, akiamini kwamba Nabii haheshimiwi kwao alihama huko na kwenda zake Galilaya alikoheshimiwa sana. Lakini kinyume na habari hii, katika Injili ya Mathayo (13:54-58), Luka (4:24) na Marko (6:4) twaambiwa kwamba Yesu kwao hakukuwa Yudea bali Galilaya. Kukosa kuheshimiwa Galilaya, yeye akasema, hapakuwa na Nabii aliyeheshimiwa kwao.

(vi) Katika Injili ya Yohana (3:22-26 na 4:1-3) twaambiwa kwamba hata kabla Yohana hajatupwa gerezani, Yesu alikuwa tayari ameshaanza kuhubiri Ujumbe wake na kubatiza watu. Lakini katika Injili ya Mathayo (4:12-17) na Marko (I:14-15), twaambiwa kwamba

Yesu alianza kuhubiri baada ya Yohana kufungwa gerezani.

(vii) Kulingana na Injili ya Luka (3:23) Yusufu, mumewe Mariamu, alikuwa mwana wa Heli; lakini sawa na Injili ya Mathayo (1:16) yeye alikuwa ni mwana wa Yakobo.

(viii) Kulingana na Luka (3:31) Yesu alitokana na Nabii Daudi[as]kwa njia ya Nathani lakini Injili ya Mathayo (1:6) yakariri nasaba ya Yesu kupitia kakake Nathani, Mfalme Sulemani.

(ix) Katika nasaba ambayo imeandikwa na Mathayo kutoka Nabii Yusufu hadi Nabii Ibrahimu[as] tunao watu arobaini na mmoja, lakini katika nasaba iliyoandikwa na Luka tunao watu hamsini na sita. Isitoshe, majina pia katika nasaba hizi mbili hayalingani.

(x) Katika Injili ya Luka (24:50-51) twaambiwa Yesu alichukuliwa juu mbinguni huko Bethania. Lakini katika kitabu cha Matendo (1:12) twasoma ya kuwa eti kupaa kwenyewe kulifanyika katika mlima ulioitwa wa Mizeituni.

(xi) Injili ya Luka (24:21-29, na 36 na 51) yasema kwamba siku ambayo Yesu alifufuka kutoka wafu, au usiku ulioifuatia, yeye alipaa mbinguni. Lakini katika Matendo (1:3) twasoma ya kuwa Yesu alipaa huko angani siku arobaini baada ya kufufuka toka wafu.

(xii) Katika Injili ya Mathayo (10:10) twasoma kwamba Yesu alitamka akiwaambia wanafunzi wake kutochukua "Mkoba wa safari, wala kanzu mbili, wala viatu, wala fimbo", lakini injili ya Marko (6:8-9) yadai kwamba Yesu aliwaambia wanafunzi wake ya kuwa wasichukue kitu cha njiani isipokuwa fimbo tu. Hata hivyo, Marko yuakiri kwamba Yesu aliwaamuru wanafunzi wajifungie viatu. Kutokana na maneno haya yaonekana kwamba sawa na Injilj ya Mathayo, Yesu aliharamisha hata uvaaji wa viatu na uchukuaji wa fimbo lakini kulingana na Injili ya Marko wanafunzi waliamriwa kuchukua fimbo na kuvaa viatu.

USHIRIKINA KATIKA INJILI

Kulitalii Agano Jipya kwaonesha kwamba kitabu hiki hakikuepukana na dalili za ushirikina.

(i) Katika Injili ya Marko (1:12-13) tunayo maneno haya:

> Mara Roho akamtoa aende nyikani. Akawako huko jangwani siku arobaini, hali akijaribiwa na Shetani; naye alikuwa pamoja na wanyama wa mwitu, na malaika walikuwa wakimhudumia.

Visa vinavyorekodiwa hapa si chochote ila ndoto tupu. Sheria za Mwenyezi Mungu zaenda kinyume nayo. Hapa ardhini mwanadamu huishi miongoni mwa watu wala sio miongoni mwa wanyama au mashetani au malaika.

Hapana uwezekano ya kuwa kanuni hizi zilikuwa tofauti wakati ule. Hatuna mashetani wanaoishi kidhahiri shahiri na watu humu duniani, wala hatunao malaika wanaowapatia watu huduma za kidhahiri. Ama kushuhudia vitu sampuli hii katika ndoto, hilo ni jambo jingine. Naam, uzoefu wa namna hii ulitabarukiwa na watu siku zilizopita, na waweza ukatabarukiwa hata hivi leo. Lakini sio hapo kale wala hivi sasa tulipo nao wanadamu wakiishi na wanyama kama vile mbwamwitu na simba. Wala hatuna hali ya Shetani kumjia mwanadamu akienda zake naye hata kwamba mtu mwenyewe humfuata na kumtii kinyume na matakwa yake, akimwasi tu hapa na pale. Wala hatunayo hali ya malaika kuja na kutoa huduma kama vile kuoka mikate, kupika na kuteka maji. Naam, katika ngano za vizimwi tunavyo visa sampuli hiyo, lakini ni thamani gani vinavyoweza kuwa nayo katika kitabu cha dini? Lingelikuwa Agano Jipya ni kitabu chambileche kitabu kiitwacho *Jungle Book* (Kitabu cha Kimsituni) cha bwana Kipling, basi hilo lingekuwa jambo jingine kabisa. Lakini Agano Jipya ni kitabu kwa ajili ya mwongozo wa kiroho wa mwanadamu. Sasa kitabu cha namna hii kinaweza kikawa na faida gani na hekaya za aina hii? Yesu alikuwa ni mtu mwema na mtawa. Hatuwezi tukamnasibishia kitu cha kigeni jinsi hii. Yeye alikuwa ni Nabii mheshimiwa wa Mwenyezi Mungu na alitumwa kwa ajili ya

uongozaji wa watu wake. Haiwezekani ya kuwa eti yeye awe alifundisha vitu sampuli hiyo. Haiwezekani kwamba mafundisho yake yawe yalizifanya akili za wafuasi wake zichanganyikiwe na kuwatokomeza toka njia ya ukweli hadi kwenye mvurugo wa ushirikina. Tunalazimika, kwa hiyo, kusema kwamba mambo haya ya kishirikina yaliongezwa katika Injili wakati fulani wa baadaye. Yesu hahusikani na mambo haya, wala wanafunzi wake. Uingizaji huu wa ushirikina katika matini ya injili wahusikana na wale Wakristo waliokuja baadaye, ambao hawakuwa tena na ghera ya kiroho, waliojitakia sifa za watu badala ya kuzingatia ukweli.

(ii) Katika Injili ya Marko (5 :1-14) twasoma maneno haya:

> Wakafika ng'ambo ya bahari mpaka nchi ya Wagerasi. Na alipokwisha kushuka chomboni, mara alikutana na mtu, ambaye ametoka makaburini, mwenye pepo mchafu; makao yake yalikuwa pale makaburini wala hakuna mtu yeyote aliyeweza kumfunga tena, hata kwa minyororo kwa sababu alikuwa amefungwa mara nyingi kwa pingu na minyororo akaikata ile minyororo, na kuzivunjavunja zile pingu; wala hakuna mtu aliyekuwa na nguvu za kumshinda. Na siku zote, usiku na mchana, alikuwako makaburini na milimani, akipiga kelele na kujikatakata kwa mawe, Na alipomwona Yesu kwa mbali, alipiga mbio, akamsujudia; akapiga kelele kwa sauti kuu, akasema, Nina nini nawe, Yesu, Mwana wa Mungu aliye juu? Nakuapisha kwa Mungu usinitese. Kwa sababu amemwambia, Ewe pepo mchafu, mtoke mtu huyu. Akamwuliza, Jina lako nani? Akamjibu jina langu ni Legioni, kwa kuwa tu wengi. Akamsihi sana asiwapeleke nje ya nchi ile. Na hapo milimani palikuwa na kundi kubwa la nguruwe wakilisha. Pepo wote wakamsihi, wakisema, Tupeleke katika nguruwe, tupate kuwaingia wao. Akawapa ruhusa. Wale pepo wachafu wakatoka, wakaingia katika wale nguruwe; nalo kundi lote likateremka kwa kasi gengeni, wakaingia baharini, wapata elfu mbili; wakafa baharini. Wachungaji wao wakakimbia, wakaieneza habari mjini

na mashamba. Watu wakatoka walione lililotokea.

Mistari hii inayo mawazo mengi ya kishirikina hivi kwamba msomaji hana budi kustaajabishwa na vile yalivyoweza kupenya ndani ya taarifa za Injili. Twaambiwa, kwanza ya kwamba mtu alikuwa amepandwa na mori wa wazimu kiasi hiki kwamba asingeliweza kuzuiliwa na minyororo kabambe. Sayansi ya kitabibu na uzoefu wa kibinadamu wa kawaida vyasuta madai sampuli hii. Bila shaka panaweza pakawepo na minyororo madhubuti ya kuweza kumkwamisha na kumzuilia mwendawazimu mwenye fujo kupindukia. Je, siku zile watu hawakujua njia ya kutengeneza minyororo madhubuti kutosha kuwafungia watu?

Pili, twaambiwa katika mistari hii kwamba mwendawazimu huyo ni aliyejikatakata kwa mawe. Kitu cha namna hii chastaajabisha mno. Miaka nenda miaka rudi mtu ajikatekate kwa mawe kama inavyoonekana, lakini hata hivyo hafilii mbali.

Tatu, twaambiwa Yesu alitamka akimwambia mtu huyu, "Ewe pepo mchafu, mtoke mtu huyu". Kitu cha namna hii chaweza tu kusemwa na watu waliozoea desturi za kishenzi na za kijinga. Hakiwezi kikasemwa na Nabii. Kama pepo wachafu wangeweza kuwaingia wanadamu, mbona hatuoni kitu kama hiki hivi leo? Je, hatuna njia za kuwafichulia hawa pepo wachafu? Ni kweli, sayansi ya utabibu leo hii huyatambulisha maradhi ya akili kuwa ni uchovu wa neva, wazimu, kichaa n.k. lakini sayansi ya kitabibu huyanasibishia maradhi haya visababishi vingine, sio pepo wachafu. Hata hivyo, kisa hicho cha Injili, chatuambia kwamba mtu mwenye akili zake, mkweli kama vile Yesu alifikiria kwamba mtu ashikwapo na wazimu huwa pepo mchafu amemwingia. Kunasibishia Nabii wazo la kishirikina kama hili yaonekana kwetu sisi ni ukatili mtupu. Ni kumwelekezea Mwalimu mkuu mawazo ya mtu ya kishirikina. Yesu mwenyewe asingeliweza asilani kutamka kitu sampuli hiyo, wala wanafunzi wake. Huu kwa hakika ni uzushi wa wakati wa baadaye.

Lakini wazo la kishirikina lenyewe lazidi kukaangwa kwamba Yesu

alimwuliza yule pepo mchafu jina lake na pepo huyo akajibu akisema "Mimi ni Legioni: kwani tu wengi". Hii ndio kusema kwamba hakuwa ni pepo mmoja bali jeshi lao zima.

Twazidi kuambiwa kwamba hao pepo walimsihi Yesu asiwapeleke nje ya nchi ile. Lakini Yesu akadinda, ambapo wale pepo wakamsihi awapeleke ndani ya kundi la nguruwe, ili wakawaingie. Yesu akalikubali hili bila kusita. Hapo wale pepo wachafu wakaenda zao na wakaingia ndani ya nguruwe wale na kundi zima likamtimkia mbio gengeni na kutumbukia baharini. Na kwa njia hii nguruwe elfu mbili wakafa majini.

Chaonekana cha kishirikina kiasi gani na cha kipumbavu kisa hiki! Twaambiwa eti wale pepo wachafu waliomba ruhusa wautoke mwili wa mwanadamu na waingie ndani ya nguruwe. Sasa swali jingine ni hili: Bila shaka kundi hili la nguruwe lilikuwa ni mali ya mtu, basi Yesu alikuwa na haki gani kuteketeza mali ya mtu mwingine? Na kama itadaiwa kwamba mwana wa Mungu alikuwa na haki juu ya namna zote za mali, basi swali ni hili, kwa nini kumwita Mwenyezi Mungu kuwa ni Mungu wa mapenzi? Kama Mungu akiwa Bwana wa kila kitu anaweza akaangamiza vitu vinavyomilikiwa na wanadamu wa kawaida, basi ni sheria au kanuni gani tulizonazo humu duniani? Na ni dalili gani tulizonazo za kuungia mkono ukarimu wa Mungu?

Isitoshe, pana ushirikina mwingine mpevu unaofundishwa katika maneno haya ya Injili. Twaambiwa eti wale pepo wachafu walipoingia ndani ya wale nguruwe, wanyama wale waliteremka mbio gengeni hadi baharin. Swali lenyewe ni hili, wale pepo wachafu walipomwingia mtu, yeye hakujitumbukiza baharini. Lakini walipoingia ndani ya kundi la nguruwe 2000, wote wakatimka mbio hadi baharini na kuangamia. Kwa nini tofauti hii ya mwenendo? Fungu hili zima la maneno ni la kishirikina na kipumbavu. Mtu yeyote mwenye kuamini ukuu wa Yesu na busara yake hawezi akamnasibishia vitu samapuli hii yeye wala wanafunzi wake. Hatakuwa na budi kusema kwamba mafungu ya maneno namna hii

yameongezewa kwenye Agano Jipya na waandishi wa baadaye.

(iii) Kutokana na Agano Jipya yaonekana kwamba Yesu alikuwa akifufua wafu. Na hapo basi katika Injili ya Yohana (11: 43-44) twasoma maneno haya:

> Naye akiisha kusema hayo, akalia kwa sauti kuu, Lazaro, njoo huku nje. Akatoka nje yule aliyekufa, amefungwa sanda miguuni na mikononi, na uso wake umefungwa leso. Naye Yesu akawaambia, Mfungueni, mkamwache aende zake.

Vivyo hivyo katika Injili ya Mathayo (27: 51-53) tunayo maneno haya:

> Na tazama, pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini; nchi ikatetemeka; miamba ikapasuka; makaburi yakafunuka; ikainuka miili mingi ya watakatifu waliolala; nao wakiisha kutoka makaburini mwao, baada ya kufufuka kwake, wakaingia mji mtakatifu, wakawatokea wengi.

Je, anaweza kiumbe yeyote mwenye akili zake kushawishika kukiamini kisa hiki? Kama wangeweza wafu kufufuliwa, basi mbona hayawi hivi leo? Kama itadaiwa kwamba hilo lilikuwa ni daraka maalumu la Yesu, jibu letu ni kwamba hiyo si kweli kabisa kwa sababu Yesu mwenyewe alisema kwamba kama wafuasi wake wawe na imani angalau ndogo chambileche punje ya haradali, wataweza kuonyesha Ishara kubwa kuliko zile alizozionyesha yeye mwenyewe.

Tunayo maneno haya katika Injili ya Yohana (14:12-14):

> Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba. Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya.

Sasa swali ni hili, je, Wakristo leo hii wanaweza wakafufua wafu?

(iv) Katika Injili ya Mathayo (14: 25-27) tunayo maneno haya:

> Hata wakati wa zamu ya nne ya usiku Yesu akawaendea, akienda kwa miguu juu ya bahari. Wanafunzi walipomwona

akienda juu ya bahari, wakafadhaika, wakasema, Ni kivuli; wakapiga yowe kwa hofu. Mara Yesu akanena, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msiogope. Huu nao ni ushirikina mpevu. Ni mtu gani awezaye kutembea juu ya maji?

(v) Katika Injili ya Luka (II: 24-26) yapo maneno haya:

Pepo mchafu amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo maji, akitafuta mahali pa kupumzika; asipoona, husema, Nitarudia nyumba yangu niliyotoka. Hata afikapo, akaiona imefagiwa na kupambwa, ndipo huenda akachukua pepo wengine saba, walio waovu kuliko yeye mwenyewe, wakaingia na kukaa humo; na mtu yule hali yake ya mwisho huwa mbaya kuliko ya kwanza.

Huu ni ushirikina mbovu jinsi gani? Vinaweza vikawa na maana ipi visa sampuli hii? Je, vinaweza vikanasibishiwa mtu kama vile Yesu? Kusema uwongo ni vibaya. Kutunga ushirikina ni vibaya kiasi kama hicho. Lakini kumnasibishia uwongo Mwenyezi Mungu na Manabii Wake ndio ukatili wenyewe. Waandishi wa Injili wasiojali na wajinga wamehusikana na ufanyaji wa ukatili huu. Na kwa kufanya hivyo, wakaziharibu Injili na kuzikosesha thamani kama vitabu vya dini.

MAFUNDISHO YENYE TASHWISHI YA AGANO JIPYA

(i) Katika Injili ya Marko (11:12-14) tunayo maneno haya:

Hata asubuhi yake walipotoka Bethania aliona njaa. Akaona kwa mbali mtini wenye majani, akaenda ili labda aone kitu juu yake; na alipoufikilia hakuona kitu ila majani; maana si wakati wa tini. Akajibu, akaumbia, Tangu leo hata milele mtu asile matunda kwako. Wanafunzi wake wakasikia.

Kutokana na haya yaonekana kwamba (a) Yesu aliyeishi katika nchi ambako mitini ilipatikana kwa wingi kumbe hakuwa na habari za msimu wa matunda ya tini; (b) yeye alikuwa, kama inavyoonekana, mtovu wa adabu kiasi hiki kwamba badala ya kujilaumia kosa lake, alihamakia kuulaani mti usioweza kujitetea, huku akisema, "Tangu leo hata milele mtu asile matunda kwako". Sisi Waislamu hatumwamini

Yesu kuwa ni Mungu. Yeye twamhesabu kuwa ni Nabii wa Mungu tu. Lakini hata sisi hatuamini kuwa yeye angelikuwa mwenye kusema kile ambacho anakinasibishiwa hapa. Sisi hatuna jingine ila kuwastaajibia wale wanaomchukulia kuwa ni mwana wa Mungu, na kama mweka mfano bora wa kitabia, ambao hata hivyo wanayavumilia maelezo haya yanayomnasibishia hii tabia ya utovu wa adabu. Wao hawafikirii hata kidogo kama vitu sampuli hii vinaweza kwa hakika kutamkwa na Yesu wala hawafikirii kama alivinasibishiwa na watu wengine.

Watetezi wa itikadi za Kikristo leo hii wana tabia ya kuyelezea kivingine maneno haya ya Injili ya Marko. Wao wanatoa rai kwamba laana yenyewe haiuhusu ule mtini bali inalihisu taifa la Kiyahudi nayo ina maana hii tu ya kwamba baada ya hapo Mayahudi hawataweza kuzaa matunda yoyote. Maelezo haya ni upuuzi mtupu. Wale wenye kujua mitindo ya kawaida ya kimaandishi hawawezi wakaridhishwa na maelezo sampuli hii. Kama ule mtini ulikuwa utumike kama isitiari, je, ilikuwa lazima ya kuwa Yesu awe atauendea mmoja zama njaa ilipokuwa imembana? Kulingana na maneno yenyewe yaliyomo katika Marko, Yesu aliuona ule mtini ukijaa majani, na akakata shauri kuukaribia, akitumainia kupata matunda. Ilikuwa ni baada ya yeye kuutazama akiwa karibu nao na kutokuta chochote minghairi ya majani (msimu wa tini ulikuwa haujafika) ya kwamba yeye aliulaani mti ule. Yesu, kwa neno zima, yuauendea mti kuzima njaa yake. Mti unayo majani na Yesu yuatumainia kujipatia matunda. Msimulizi wa kisa chenyewe yuadokeza kwamba msimu wa tini ulikuwa haujawadia. Haya yote yaonesha kwamba kisa chenyewe hakikukusudiwa kuwa ni isitiari. Msimulizi yuabainisha waziwazi kwamba Yesu alikwenda kwenye ule mti kwa sababu alikuwa na njaa, na alitumainia kujichumia matunda. Lakini kumbe wakati wa matunda yenyewe ulikuwa haujawadia. Yawezekana kwamba mti ule maalumu ulikuwa umechelewa kuzaa matunda, au kwamba ulipatwa na aina fulani ya uele wa miti na hivyo kukosa kuzaa matunda. Hata hivyo, hasira zikampanda Yesu na akaulani mti. Kama haya yote yameripotiwa sawasawa, je hatuna sababu ya kuuliza kama

wanaovilaani vitu visivyokuwa na uhai kama vile miti na mito, milima au mawe, wanaweza wakahesabiwa kuwa ni watu wenye akili zao? Je, yule mwandishi aliyemnasibishia Yesu vitu hivi alifikiri kwa vizazi na vizazi vitakavyokuja baadaye vitakuvumilia kupakwa matope kwa mtu mwenye busara zake na mnyofu kama Yesu. Wafuasi wa Yesu wanaweza wakadanganyika kwa visa sampuli hii, lakini sisi Waislamu hatuwezi abadan kumnasibishia Yesu vitu hivi, si kwa sababu ya kwamba yeye alitofautiana kwa vyovyote vile na Manabii wengine, bali kwa sababu sisi hatutarajii vitu kama hivi hata kutoka kwa waungwana wa kawaida wenye mienendo mizuri.

(ii) Katika Injili ya Mathayo (7:6) tunayo maneno haya:

> Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, wala msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, wakageuka na kuwararua.

Kinachoelezewa hapa kama "kitakatifu" na "lulu" kwa kweli ni wahyi na Ishara za Mungu. "Mbwa" na "nguruwe" katika mstari huu vyamaanisha wale watu waliokataa kumwamini Yesu. Hapana shaka kabisa ya kuwa Ishara za Mwenyezi Mungu ni takatifu kuliko vitu vitakatifu zaidi. Zina thamani zaidi kuliko lulu. Lakini pia hapana shaka kwamba vitu vilivyo vitakatifu na vyenye thamani chambileche lulu vimekusudiwa wale wasiokuwa navyo. Ishara za Mwenyezi Mungu ni za kuonyeshwa wale wasiomwamini Yeye. Manabii hawaleti imani kwa wale tu ambao tayari wako nayo. Jambo hili liko wazi katika historia ya kwamba Manabii hawajapata kudhihiri isipokuwa katika ukafiri unapopindukia. Manabii wamedhihiri pale tu ambapo dunia imefunikizwa na giza, na kazi yao maalum ni kuitoa dunia toka kwenye giza hadi kwenye nuru. Ujumbe wao huhubiriwa wale waliozama gizani. Ni kwa ajili ya watu hawa ya kwamba Manabii huja duniani. Haiyumkiniki ya kwamba mpendwa wa Mwenyezi Mungu awe atawaelezea kuwa ni mbwa na nguruwe wale ambao kosa lao la pekee ni kwamba nuru ya imani haijawaangazia. Haiwezekani ya kuwa Nabii awe atasema kwamba Ishara za Mungu wasizisimuliwe

makafiri kwa sababu kuchelea kwamba eti wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao. Ingelikuwa Nabii kusema jambo sampuli hii, basi makafiri watakuja kusilimu namna gani? Kumnasibishia Yesu maneno kama haya ndio ukatili. Hii ni sawa na kusema kwamba watu wale wale ambao yeye alikuwa amewajia aliwaelezea kuwa ni mbwa na nguruwe na si kwa sababu ya kosa lao wenyewe, wala si kwa sababu ya fitina yoyote waliyokuwa wamefanya, ila kwa kuwa ukweli ulikuwa bado haujawadhihirikia. Hebu linganisha haya na mfano wa Mtume Mtukufu[saw] wa Islam. Katika Kurani Sura Ash-Shu'araa 26:4 tunayo maneno haya:

> "Huenda utaangamiza nafsi yako kwa sababu hawawi waaminio".

Aya hii yaelezea jinsi gani Mtume Mtukufu[saw] alivyokuwa na shauku ya kuwafikishia makafiri wote ujumbe wake. Tukimlinganisha Yesu wa Injili na Mtume Mtukufu[saw] wa Islam, tunakuta tofauti kubwa mno. Mmoja yuko tayari kujiangamiza nafsi yake kwa ajili ya wale ambao hawataamini; mwingine yuawakwepa, akiwaita mbwa na nguruwe huku akiwaamuru wanafunzi wake wasiwasomee Ishara za Mungu.

Bila shaka Mtume Mtukufu wa Islam yuawapita Manabii wengine wote katika mfano wa maadili yake. Lakini hatuwezi tukaamini kwamba Yesu alikuwa mtovu wa maadili kama vile Injili zinavyomfanya. Naam, yeye hakuwa amevifikia vile vilele vya kiroho alivyokuwa amevifikia Mtume Mtukufu[saw] wa Islam. Hata hivyo, yeye alikuwa ni Nabii wa Mungu na alikuwa ameletwa na Yeye kuwafundisha watu maadili na njia za kiroho. Mfano wake ni sharti uwe ulimtofautisha na mamilioni ya wanadamu wengine, lakini ole wake yule mwandishi mwenye kumnasibishia tabia zisizokuwa na adabu kama hizi.

Na kuhusu jambo hili hatuwezi kutokitaja kile kisa kihusikanacho na mwanamke Mkananayo kilichotajwa katika Injili ya Mathayo (15:21-26) na Marko (7:24-27). Mwanamke huyu alimwendea Yesu kwa unyenyekevu mkubwa. Sawa na desturi za jamii yake akamwangukia

Yesu miguuni na alitaka mwongozo tu toka kwake. Lakini Yesu, sawa na waandishi wa Injili, alitamka akisema, "si vyema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa".

Ni kwa shauku na matumaini gani ambayo ni sharti masikini mwanamke yule alimwendea Yesu. Wala hakwenda kuomba mkate au nguo au kitu chochote cha kimwili kama hicho; alichotaka yeye ulikuwa ni mwongozo wa kiroho. Alitaka kutoka kwake kile Yesu alichokuwa amekuja kukitoa. Lakini masimulizi ya Injili yasema kwamba Yesu alimfukuzilia mbali. Si hayo tu, alimtukana mwanamke kinyama, akamwita mbwa na kumfedhehesha. Yesu, kisa hiki cha Injili kikiwa kweli, hakumfedhehesha mwanamke huyu wa kutoka eneo la Kanaani peke yeke, bali aliwafedhehesha akina mama wote, na kuthibitisha kwa kauli yake yeye mwenyewe ya kwamba hakuwa na cha kuwapatia maskini wanawake. Mawazo yake yote yaliyamulikia masilahi ya taifa la Kiyahudi. Naam, miguu yake kupakwa mafuta na mwanamke asherati wa Kiyahudi (Luka 7:36-38) angeona hili kuwa ni heri kuliko kumtamkia mwanamke asiyekuwa wa Kiyahudi neno la kumfariji. Kama Wakristo wanaikubali sehemu hii ya Injili kuwa ni kweli, basi hiyo ni hiari yao. Lakini sisi kwa upande wetu hatuwezi kuamini kwamba wanafunzi wake wangeliweza kusema kitu kama hiki kumhusu yeye. Mambo haya tuonavyo sisi ni uzushi wa waandmshi wa baadaye. Na yalizushwa wakati yule Yesu wa kweli alipokuwa ametoweka duniani na ambapo Yesu wa bandia alikuwa akitengenezwa na waandishi wasiojua.

(iii) Katika kitabu cha Yohana (2: 1-4) tunayo maneno haya:

> Na siku ya tatu palikuwa na arusi huku Kana, mji wa Galilaya; naye mama yake Yesu alikuwepo. Yesu naye alikuwa amealikwa arusini pamoja na wanafunzi wake. Hata divai ilipowatindikia, mamaye Yesu akamwambia, Hawana divai. Yesu akamwambia, mama, tuna nini mimi nawe? Saa yangu haijawadia.

Vivyo hivyo katika Injili ya Mathayo tunayo maneno haya:

> Mtu mmoja akamwambia, Tazama, mama yako na ndugu zako

> wamesimama nje, wanataka kusema nawe. Akajibu, akamwambia yule aliyempasha habari, Mama yangu ni nani? Na ndugu zangu ni akina nani?

Maneo haya yatokayo kwenye Injili za Yohana na Mathayo yaonesha kwamba Yesu hakuwa na staha ya maana hata kwa mama yake, ulio uhusiano wa damu unaopewa uzito mkubwa na heshima na watu wote walio waungwana. Je, Mkristo wa kawaida wa hivi leo atasema na mamake akimwambia, "Mwanamke, tuna nini mimi na wewe?" Je, Mkristo yeyote hivi leo ataambiza mamake kwa dharau na hata hivyo kuhesabiwa kuwa yu muungwana? Basi ni kwa nini waandishi wa Injili wakamchagulia Yesu maelezo ya kudhihaki sampuli hii? Kuwaheshimu mama wazazi ni wema wa kawaida hata miongoni mwa watu wasiostaarabika. Hii ni namna ya adabu ambayo kwamba hata wanadamu waovu kabisa huionesha. Lakini kama masimulizi haya ya Injili ni ya kukubaliwa, huyu Mwalimu wa mwisho wa Israeli, huyu shujaa wa mila za ki-Musa, aliyekuja kuongoza watu toka gizani hadi nuruni na kuwafunza mienendo mizuri, alikuwa jeuri kwa mamake na alimkosea adabu. Kulingana na imani ya Kikiristo, Yesu alikuwa mwana wa Mungu, si mwanadamu. Kama Yesu alikuwa mwana wa Mungu, basi ni kwa nini alizaliwa mapajani mwa Mariamu. Kama yeye alikuwa ameridhia azaliwe mapajani mwa Mariamu, na kumwonjesha machungu ya mzazi kwa miezi tisa, na alikuwa amemnyonya chuchu zake kwa miaka miwili, na alikuwa amemlemeza kwa miaka kwa kumtwisha wajibu wa malezi yake, je, asingelikuwa ameweza kulipia deni la mama kwa kumfanyia staha na heshima aliyoistahili? Yaonekana ni ukweli wenyewe kwamba hivi ni visingizio tu. Wakristo hawamwamini Yesu hata kwa nusu ya vile wanavyoziamini Injili za kujitungia. Injili za kujitungia ni utungo wao wenyewe, na Yesu alikuwa ni kiumbe cha Mwenyezi Mungu. Hawako tayari kufuata njia iliyonyooka ya kukiri kwamba masimulizi ya Injili yamekosa. Wanaona ni afadhali Yesu asingiziwe kuliko wao kuyakatalia mbali masimulizi ya Injili hizo. Lakini watu wenye akili zao walio waungwana wameyatafakaria maisha ya Yesu na kujaribu

kuelewa mfano wa utakasao wake hawawezi ila kukiri kwamba Injili vile tulivyonazo hivi leo zimejaa uzushi na makosa. Zinayo mambo yasiyojenga, bali ambayo badala yake huelekea kuyavunjilia mbali matumainio ya kiroho ya mwanadamu. Sasa Injili zikiwa katika hali mbovu kama hiyo, ilikuwa ni lazima ya kwamba Mwenyezi Mungu alete duniani wahyi mpya ulioepukana na makosa na uwezao kuingiza nafsini mwa mtu sio tu maadili matukufu bali na sura tukufu ya kiroho pia. Wahyi huo ndio Kurani.

MAPACHIKO KATIKA MA-VEDA

Dini ya tatu iliyo muhimu kuhusu idadi ya wafuasi ni Ubaniani. Sawa na mafundisho ya Kurani sisi tunayo imani ya kikweli kwamba dini ya Kibaniani ilianzia na wahyi wa Mungu na, kwa sababu Mabaniani wanavichukulia vitabu vya Veda kuwa ni vitabu vyao vya kidini, tunalazimika pia kuamini kwamba vitabu vya Veda vinao wahyi uliopokelewa na Manabii wa Kibaniani. Lakini ile hali ambayo vitabu vya Ma-Veda vinapatikana wakati wa hivi sasa yatatanisha mno. Hata hatujui majina ya watu waliopokea wahyi huu. Maandiko ya Ma-Veda mwanzoni yanataja majina kadha, lakini majina haya, kulingana na wanazuoni wa Kibaniani wenyewe, siyo majina ya wapokeaji wa wahyi huo, bali ni majina ya wale walioukusanya. Basi, thamani ya kihistoria ya Ma-Veda ni yenye maana sana.

Wanazuoni wa Ma-Veda wana maoni haya yafuatayo kuhusu Ma-Veda:

(1) Pandit Vedic Muni katika kitabu chake kiitwacho *Veda Sarvasva* yuaandika akisema hivi:

Kusema kweli, mvurugiko ambao umefanywa kwa hiki kitabu cha Atharva-Veda hauna kifani chake katika vitabu vingine vya Ma-Veda. Hata baada ya Sayanacharya vifungu vingi vya maneno (Suktas) vimeongezewa humo. Njia nzuri ya kupachikia maneno imevumbuliwa. Katika hatua ya kwanza kifungu kilichofanyiwa upachikaji kinatiliwa alama kutoka matini kwa neno *Atha* (mwanzo) na *Iti* (mwisho). Wakati msomaji anapoyazoelea mageuzo haya yale

maneno *Atha* na *Iti* yanatupiliwa mbali na kile kifungu kilichofanyiwa mapachiko kinakuwa sehemu ya matini ya kawaida. Kama vile tu katika mkusanyo wa Rig-Veda, *Valkhilya* Sukta zinaongezewa humo, vivyo hivyo kwenye mwisho wa Atharva-Veda panaongezewa *Kuntapa Sukta*. Ukiuliza, "Ni wapi zitokako Sukta hizi tangu *Anu-vaka* ya tano hadi *Kuntapa*?", hupati jawabu. Hali ya kutojua imeenea kiasi hiki kwamba mwishowe maneno, "*Atharva-Veda Samhita Samapta*" yanafikiriwa kuwa ni mdhamana tosha ya kuwa yote yaliyotangulia kimbele ndio mkusanyo wa *Atharva*. Hapana adirikie kuuliza ni akina nani hawa wakusanyaji, na wanayo maarifa gani ya kazi hii (uk. 97).

(2) Pandit Mahesh Chandra Prashad yuaandika katika kitabu chake *Sanskrit Sahitya ka Itihas* akisema:

> Kitabu kiitwacho *Vaja Saneyi Shukla Yajur-Veda Samhita* ni kusanyo la kiajabuajabu. Humo Veda na Brahmana ni sehemu tenganifu. Zote pamoja ziko sura arubaini, lakini watu walio wengi zaidi hawana shaka kwamba ni sura kumi na nane tu zilizo halisi, huku zile zingine zikiwa za kuongezewa baadaye. Sura ya kwanza hadi ya kumi na nane zalingana na *Bhaga Taittiriya Samhita* na *Krishna Yajur-Veda* katika nathari na ushairi. Kuhusu hizi sura kumi na nane tunayo maelezo ya neno kwa neno katika Brahmana zao. Lakini kwa upande wa zile sura zilizobaki tunayo maelezo ya aya chache tu hapa na pale. Katyayana azichukulia sura 26-35 kuwa ni mapachiko. Sura 19-25 zinayo maelezo ya dhabihu. Sura hizi hazipatani na maandiko ya *Taittiriya Samhita*. Sura 26-29 sana sana zinazo aya kuhusu kawaida hizohizo za kutoa dhabihu ambazo zimetajwa katika sura zilizotangulia, ambazo kutokana nazo yaonekana kwamba bila shaka zimeongezewa baadaye (uk. 160).

(3) Pandit Shanti Dev Shastri yuaandika katika gazeti liitwalo *Ganga* (Februari 1931):

> Kwanza kabisa hapakuwepo na uamuzi wa yakini ya kama vitabu vya Veda ni vitatu au vinne., Sawa na Manu Smriti na

> Shatapatha Brahmana, Rig-Veda, Yajur-Veda na Sama-Veda ndivyo vitabu vya ma-Veda peke yao na vinaifanya idadi kuwa tatu. Lakini sawa na Vaja Saneyi Upnishad, Brahamana Upanishad na Mundaka Upanishad vitabu vya Veda kwa idadi ni vinne (uk. 232).

(4) Pandit Hirday Narain yuaandika katika gazeti la ***Ganga*** (Januari,1931) kwamba:

> Katika maandiko ya Charana Vyuha na maandiko mengine ya Shaunaka Rishi maelezo yaliyotolewa juu ya idadi hasa ya aya, maneno yao na herufi zao hayazipasi nakala za sasa za Ma-Veda, jambo ambalo kutokana nalo yaonekana kwamba vitabu vya Veda vimekumbwa na maongezeo mengi na mapunguzo.

(5) Pandit Shanti Dev Shastri yuaandika katika gazeti la Ganga (la Februari 1931) kwamba:

Kilipotungwa kitabu kiitwacho ***Charana Vyuha*** cha Shaunaka Rishi, ***Shakalya Samhita*** katika mkusanyo wa Rig-Veda zilikuwa na maneno 153,826, herufi 432,000 na aya 10,622. Lakini leo hii tarakimu hizi huzipati (uk. 231).

(6) Daktar Tarapad Chaudhri yuaandika katika gazeti la Ganga (Januari 1932) kwamba:

> Mbali na haya, kunayo ndani ya Ma-Veda maneno ambayo yanakuwia wazi kwamba ni mageni katika matini. Yanaonekana kwamba matini yamepatwa na kosa lisilokuwa la maksudi la wale waliyoyaandikisha na wale waliyoyaandika (uk. 74)

(7) Pandit Vedic Muni katika kitabu chake ***Veda-Sarvasva*** yuaandika:

> Wakati ilipoandikwa Gopatha Brahmana ndio ule ule ambapo wateteaji wa dhabihu walikuwa na nguvu. Wakati ule mashabiki wa Rig-Veda, Yajur-Veda, Sama-Veda na Atharva-Veda walikuwemo ndani ya ubishi mkali na kushughulika kufanya mapachiko visingizio mbalimbali. Aya za Rig-Veda waliyoyawazia kila kundi liliyaingiza katika Ma-Veda yao

wenyewe. Kila mmoja alijichukulia kuwa asiyeshutumika na alimchukia kila mwinginewe. Siyo haya tu. Tofauti zilizokuwa zimepenya ndani ya miswada mbalimbali zilikuwa zimewagawanya mashabiki wa Ma-Veda mbalimbali miongoni mwao wao wenyewe. Mashabiki wa ***Vashkala Samhita*** walikuwa wamejitenga mbali na mashabiki wa ***Shakalya Samhita,*** ma mashabiki wa ***Madhyandina Samhita*** wakajitenga mbali na ***Kanva Samhita***, na mashabiki wa ***Shaunaka Samhita*** wakijitenga na wale wa Pippalada Samhita. Kila kundi liliyachukulia yale matini waliyoyapendelea kuwa ndiyo bora zaidi na halisi zaidi na mengineyo yote kuwa yaliyochafuka na uzushi. Zile tofauti nyingi katika matini ya Ma-Veda tunazozikuta hivi leo zilizuka katika zama hizi za ufisadi (uk. 105-6).

(8) Mwandishi huyu huyu yuaendelea kusema kwamba:

Mbali na haya, sehemu za Brahmana Grantha pia zimeongezewa ndani ya Ma-Veda, ambazo msomaji aliye macho anaweza akazigundua mara moja. ***Atharva-Veda*** iko katika hali hiyo hiyo mbaya. Wataalamu wetu wa Ma-Veda ni sharti waitafakarie hali hii. Jambo hili kwamba kitabu cha dini kiwe katika hali hii ya kuhuzunisha ni la kusikitisha mno (Kitabu hicho hicho, uk. 108).

(9) Mbele zaidi yuaandika akisema:

Tayari imekwishasemwa ya kwamba tunazo hivi sasa nakala mbili tofauti za ***Atharva Veda***. Moja ni Pippalada Samhita, nyingine ni Shaunaka Samhita. Katika nakala hizo mbili ile ya ***Pippalada Samhita*** ndiyo yenye kutegemeka zaidi. Lakihi ukweli huu haujatajwa, wala Sayanacharya hakuandika maelezo juu yake. Nakala za kuchapishwa za ***Shaunaka Samhita*** zapatikana katika matoleo matatu mbalimbali yaliyochapwa na matbaa tatu mbalimbali. Katika matoleo hayo, mawili yanatoa matini peke yake na la tatu latoa maelezo ya Sayanacharya pamoja na matini. Moja ya hizo nakala za matini pekee imetolewa na Matbaa ya

> Veda ya mjini Ajmer, nyingine imetolewa na Matbaa ya Bombay, mchapaji akiwa Sevak Lal. Matoleo hayo yote matatu yanatofautiana katika sura na aya. (Kitabu hicho hicho, uk. 109).

(10) Mtaalamu wa Arya Samaji, Pandit Raghunundan Sharma, yuaandika katika kitabu chake kiitwacho Sahitya Bhushana Vaidic Sampati kwamba:

> Kadri tunavyojua, haujatolewa asilan ushahidi kuhusu pale mahali hasa ambapo mapachiko yamefanywa katika Ma-Veda. Wala haijathibitishwa ya kuwa pale mahali ambapo mapachiko yameoneshwa kuwa yapo hapakujulikana na wataalamu wa Ma-Veda. Pale mahali ambapo mapachiko yapo pamejulikana kwa muda mrefu (tangu wakati wa Brahmana Granthas). Siyo mapachiko, bali ni mafafanuzi tu ambayo, kwa sababu ya kupitiliwa kwa wanakili na wachapaji, yakapenya ndani ya matini na yamekuwa vile ionekanavyo sehemu yake. Valkhilya Sukta katika ***Rig-Veda*** (zote kwa pamoja sura kumi na moja na aya 80), Khil yaani Brahmana Bhaga katika ***Yajur-Veda*** (Sura kadha), Sura za Aranyaka na Mahanamni (Sura mbili na aya 65) katika ***Sama-Veda***, na Kuntapa Sukta (Sura kumi na aya 150), katika ***Atharva-Veda*** haya ni mapachiko yafahamiwayo sana na wote, na ambayo kwa ajili yake kunao ushahidi wa kutosha. Mbali na mapachiko haya, kunayo mafungu ya maneno katika ***Yajur-Veda*** na ***Atharva-Veda*** ambayo yamefanyiwa upachikaji na ambayo yanaweza kutambulika kwa urahisi kuwa ni mapachiko. Kwa neno zima, kama vile tu kubadilishwabadilishwa katika nakala mbalimbali kunavyojulikana vizuri, na nakala safi hata hivyo zapatikana, vivyo hivyo mapachiko katika Ma-Veda nayo pia yanajulikana vizuri sana... Twapata ya kwamba Vaja Suneyi Samhita (kitabu cha sasa cha ***Yajur-Veda***) kinazo aya 1900, idadi inayojumlisha aya za Shakvari, kwa sababu twaambiwa... ya kwamba aya mia moja chini ya elfu mbili ni zile za ***Vaja Saneyi*** na idadi yenyewe yajumlisha aya za Shakvari. Kama ni ***Vaja Saneyi Samhita***, basi ni sharti izijumlishe aya za ***Vaja Saneyi*** pekee. Lakini

> twakuta kwamba sura ya sasa hivi ya *Vaja Saneyi* inazo aya 1975. Kutokana na jambo hili ni wazi kwamba aya za Shakvari bila shaka zimejumuishwa katika hiyo idadi ya 1900. Aya 75 zilizosalia zimeongezewa kutoka mahali penginepo (uk. 570-71).

Maneno haya yaonesha kwa uwazi kwamba vitabu vya Veda havikuepukana na uzushi. Wataalamu wa kale wa vitabu vya Veda na wale ambao ni wa kisasa zaidi wanaonekana wote wanakubaliana kwamba vitabu vya Veda vilikuwa vimeongezewa aya zingine. Kusema, kama wataalamu wa kisasa wanavyoelekea kusema, kwamba eti wataalamu wa Ma-Veda wameyagundua mapachiko na kuyatenganisha na sehemu asili za matini, ni kazi bure. Kama wataalamu wa Ma-Veda walikuwa wamesadiki kwamba aya fulani mahususi ni uzushi, basi mbona hawakuyatupilia mbali nje ya matini? Ukweli kwamba hata zile aya zilizozushwa bado zinaendelea kujumuishwa katika matini waonesha kwamba wataalamu wa Ma-Veda hawakuihakikia vizuri hali yenye walakini ya aya hizo. Yule mwandishi wa Arya Samaj mwishowe yuakiri kwamba aya 1900 za *Yajur-Veda* ndiyo peke yake ya asili, na zile 75 zilizosalia ni nyongeza za baadaye. Hata kuzihusu hizo aya 1900, yeye yuakiri kwamba yanajumuisha baadhi ya aya za Shakvari. Maneno haya, yakiwa na sharti zenye maana, yaonesha kwamba hapana ajuaye kwa yakini ukweli wa mambo ulivyo na kwamba kila mmoja yuajaribu kubahatisha. Lakini je, bahati inaweza ikafanywa kuwa ni msingi wa matumaini ya kiroho?

Ukweli waonekana kuwa ni huu ya kwamba uhalisi wa *Atharva-Veda* daima ulipata kutiliwa shaka, na vitabu vya *Yajur-Veda* na *Rig-Veda* vimefanana katika mitungo yao kiasi hiki kwamba yawezekana kabisa kwamba vitabu hivi viwili vimekopeshana bila kizuizi. Hali ya vitabu hivyo ikiwa imevurugika kwa marefu na mapana, ni nani awezaye kusema aya gani ni wahyi halisi na zisizokuwa wahyi, zipi ni mapachiko na ni zipi zisizokuwa mapachiko? Kitabu chenye kutilika shaka kiasi hicho hakiwezi kikawa mwongozo kwa mwanadamu. Ni sharti mahali pake pachukuliwe na kitabu kingine kilichoepukana na

hali ya vurugu na kilicho kinga ya kuingiliwa na binadamu, awezacho kukitegemea mwanadamu na awezacho kukiamini kuwa ni wahyi kwa yakini ile ile awezayo kuviaminia vitu vyote vinavyofanyiza mfumo wa ulimwengu, bali kwa yakini ile ile anayojiaminia kuwepo kwake yeye mwenyewe. Kitabu cha aina hii tu chaweza kuvutia mtu kumtafuta Mungu kwa moyo mwepesi. Kitabu kama hicho ni Kurani.

MAFUNDISHO YA KIKATILI YA MA-VEDA

Twanukuu mifano kadha ya mafundisho ya kikatili ya Ma-Veda:

(i) Katika *Atharva-Veda* tunayo maneno haya:

Angamiza kwa ukali wa simba maskani yao yote, kwa ukali wa simba marara wafukuzilie mbali maadui zako. Bwana wa pekee na kiongozi mwenye kushikamana na Indra, teka, ewe mshindi, mali za maadui zako.

(ii) Katika *Sama-Veda* (Sehemu ya II, ix, iii, 8) tunayo maneno haya:

Vipofu, Enyi maadui zangu, mkawe vile yalivyo majoka yasiyokuwa na vichwa: Indra amuulie mbali kila mbora wenu, pale moto wa Agni utakapokuwa umewaangusheni chini.

(iii) Katika *Sama-Veda* (11:1) tunayo maneno haya:

Ee mungu Indra, hiyo sharubati ya *Soma* iliyotolewa nasi na ikufurahishe na kukulevya. Tujaalie utajiri na uwezo, na maadui zetu uwashinde na kuwafedhehesha.

(iv) Katika *Sama-Veda* tunayo maneno haya:

Waulieni mbali maadui zetu wa Ki-Arya, Enyi mabwana wa mashujaa, waueni maadui zetu wa Ki-Dasa: Wafukuzilieni mbali maadui wote (Sehemu ya II, ii, ii, 8). "Mkanyagenikanyageni chini ya miguu yenu, yule mwenye kutuotea na kutulenga" (Sehemu ya II, iv, i, 16).

(v) Katika *Atharva-Veda* (XIX, 28:4-10) tunayo maneno haya:

Ipasulie mbali, Ee Darbha, kinga iliyo ya adui yangu, moyo wa adui yangu. Vipondeponde vichwa vyao chambileche mimea inayoifunikiza ardhi. Wapasulie mbali wapinzani wangu, Darbha, wapasue wanaojidanganya wanaweza kupigana nami... Wararulie mbali wapinzani wangu, Darbha... Wakatilie mbali wapinzani wangu, Darbha... Wapasuepasue wapinzani wangu, Darbha... Watobolee mbali wapinzani wangu, Darbha... Watobolee mbali watu wanaonichukia, Kinga.

(vi) Katika *Atharva-Veda* (XIX, 29:1-9) tunayo maneno haya:

Wachanechane wapinzani wangu, Darbha... Wasagesage wapinzani wangu, Darbha... Wateketeze wapinzani wangu... Waangamize wapinzani wangu... Waulie mbali wapinzani wangu, Darbha... Waulie mbali wote wenye kunitakia shari.

(vii) Katika *Yajur-Veda* (27:2) tunayo maneno haya:

"Agni, na wasijeruhiwe wale wakupendao sana, makuhani wako watukuke wala sio wengine minghairi yao."

(viii) Katika *Yajur-Veda* (11:80) tunayo maneno haya: Agni, yule atakayedhamiria kutudhuru, yule mtu mwenye kututazama kwa chuki, uwateketeze,

Mbali na Ma-Veda, vitabu vingine vya dini ya Kibaniani vina aina hiyo hiyo ya mafundisho. Katika kitabu cha Manu Smriti, kinachoaminiwa na Mabaniani wote kuwa ni maandiko yanayotegemeka, tunayo maneno haya:

(i) Mtu yeyote wa zile daraja tatu za juu zaidi (daraja za kisharifu sawa na dini ya Kibaniani), akiwa amejizoesha vitabu vizushi atadharau misingi ile miwili ya Sheria, ni sharti atimuliwe nje ya watu wema kama mkanusha Mungu na mwenye kudhihaki wahyi (11:11).

Je, wenye kuvidadisi vitabu vya Veda watimuliwe nje ya nchi?

(ii) Mtu yeyote wa ile daraja ya chini kabisa atakayejiketia kwa

jeuri zake kwenye kiti kimoja na mmoja wa wale wa daraja ya juu kabisa, ama atahamishwa huku akitiliwa alama katika sehemu zake za nyuma, au mfalme atamchanjisha chale matakoni (viii: 281).

(iii) Brahman (Baniani sharifu) anaweza akajinyakulia bila ya kusita, endapo atatindikiwa na riziki, mali ya mtumwa wake wa Ki-Sudra; kwani kama vile mtumwa asivyokuwa na chake, bwanake anaweza akanyakua mali yake (viii: 417).

(iv) Lakini mtu wa daraja ya kitumwa iwe amenunuliwa au kutonunuliwa, yeye (Brahman) anaweza akamlazimishia utumishi wa kitumwa; kwani mtu (Sudra) namna hiyo aliumbwa na Yule Mwenye Kujiwekapo kwa ajili ya kuwatumikia Mabrahman, (viii: 413).

(v) Sudra, hata kama kawekwa huru na bwanake, bado hajaondokewa na hali ya kitumwa; kwani, hii hali ambayo ni ya kimaumbile kwake yeye, anaweza akatolewa na nani humo? (viii: 414).

(vi) Kama yeye (Sudra), kutokana na majivuno, akiwafundisha makuhani kazi zao, basi na aamrishe mfalme yatoneshwe mafuta ya moto kinywani mwake na masikioni mwake (viii:272).

Kutokana na maneno haya ya kitabu cha Manu ni wazi kwamba kulingana na dini ya Kibaniani, rehema na ukarimu wa Mwenyezi Mungu vimekomea kwa koo chache zilizochaguliwa. Kwa ajili ya baadhi ya wanadamu ni dhambi kusoma Ma-Veda au kusikilia usomaji wa vitabu hivyo, na kama watahalifu amri hiyo na kujaribu ama kuvisoma, kuvisikiliza vikisomwa au kukumbuka kwa ghaibu sehemu yoyote ya vitabu hivyo, basi adhabu kali inayoweza kuwa hata kifo ndiyo malipo wanayostahili kulipa.

Mafundisho sampuli hii yanaonesha kikamilifu kwamba dini ya Ki-Veda ilikuwa kwa ajili ya watu wachache. Haikuwa Ujumbe kwa ulimwengu mzima. Mabrahman, Makshatri na Mavaishi si wanadamu

wote. Yatoa ujumbe gani dini hii ya Kibaniani kwa ajili ya yale mataifa mengine ya wanadamu? Je, hapana mwongozo kwa ajili yao? Je, hali ya Mwenyezi Mungu ya kuwa Mola wa walimwengu wote inaweza ikaafikiana na hili wazo la eti Yeye kuongoza sehemu moja ya viumbe Vyake kwa kuachilia mbali sehemu nyingine, akiipeleka Peponi sehemu moja na sehemu nyingine Motoni? Mafundisho kama haya sio ya kikatili tu, bali yanakwenda kinyume na yanamdunisha Mwenyezi Mungu. Mungu wetu amejaa huruma na ukarimu kwa viumbe vyote. Kila sehemu ya ulimwengu iko chini ya ukarimu Wake. Wale wanaoishi juu ya uso wa ardhi, au wale wanaoishi chini ya ardhi au wanaoishi juu angani, wote wanakuwa na kukamilisha majaaliwa yao chini ya ulezi wa Mwenyezi Mungu ulio kwa viumbe vyote. Yeye Amejaalia kila sehemu ya wanadamu uwezo ule ule, azma ile ile na maono yale yale. Zile azma zenye kuwanyanyua watu katika mizani ya kiroho zimeenea kwa kiasi kile kile miongoni mwa wanadamu wote. Hapana watu ambao wamezijaaliwa kwa hali ya kiuhabauhaba, si Wazungu, wala Wamarikani, wala Wajapani, wala Waasia wengine wowote. Mabaniani sio bora zaidi ya wengine kwa hamu ya ruhania au uwezo wa kiakili. Mungu asingeweza kusahaulia mbali sehemu kubwa kubwa za viumbe Vyake Mwenyewe nje ya mwongozo Wake, na kuuchagulia kajisehemu kadogo ka wanadamu. Kuwepo kwa mafundisho sampuli hii kwatangaza kinagaubaga kwamba muda wa mafundisho haya umemalizika. Sasa hivi twahitaji kitabu kipasacho kuwahubiria wanadamu wote, kipasacho kuwakusanya Waarabu na wasiokuwa Waarabu, Mayahudi na wasiokuwa Mayahudi, Mabrahman na wasiokuwa Mabrahman katika kundi moja, na kujenga udugu wa wanadamu wote, na kutufundisha kutowachukulia walio wanyonge na wanaodhulumiwa kuwa wasiofaa, bali kuwa hata wenye kustahili zaidi hisani zetu, huruma na utunzaji. Hii ilikuwa ni haja ya kitabu kipya ambayo Kurani ilikuja kuitimiliza.

USHIRIKINA KATIKA MA-VEDA

Vitabu vya Veda vimejaa ushirikina. Vitu kama vile moto vinaitwa miungu. Naam, inasemwa kwamba vitu hivi sio miungu bali ni

majina tu ya sifa za Mungu. Lakini ni kweli pia ya kwamba vitabu vya Veda vyafundisha, kama tendo la ucha-Mungu: desturi kama ile ya kuwasha moto na kuchoma mafuta, samli na vitu vingine kama hivyo (Rig-Veda 11, 10:4), na haliwi tena jambo la kutiliwa shaka kwamba mafuta, samli, n.k. ni vyakula vya Agni, mungu-moto. Kama Agni ni sifa ya Mwenyezi Mungu, basi kuna shabaha gani huku kuwasha moto na kuuchochea kwa kuni ghali kama hizi? Desturi yenyewe ni sharti iwe ni ushirikina hata kama Agni ni sifa tu. Kama, kwa upande mwingine, Agni yuachukuliwa kuwa ni Mungu, na desturi yenyewe yaonesha kwamha hivyo ndivyo ilivyo, basi jambo hili zima, desturi pamwe na itikadi inayoandamana nayo, si kingine minghairi ya ushirikina mkavu.

Katika ***Rig-Veda*** (11, ii:ii) tunayo maneno haya:

> Kunywa, Ee Shujaa Indra, kunywa ***Soma***; hizo (sharubati) zichangamshazo na zikufurahishe.

Sasa Indra ni jina ama la Mungu au la malaika Wake. Kama Indra ni jina la Mungu, ni wazo la kishenzi sana limfanyalo mtu kumpatia Mungu sharubati ya ***Soma***. Na ikiwa, kwa upande mwingine, Indra ni jina la malaika au roho, hata hapo huo utoaji wa sharubati ya ***Soma*** ni ushirikina mbovu. Kwani Mwenyezi Mungu amefichama, na malaika Wake ni viumbe vya kiroho. Hawahitaji kinywaji.

Mahali hapo hapo (11:15) twasoma maneno haya:

> Na wafurahi wale unaowafurahikia. Indra, kunywa sharubati ya ***Soma*** kwa ajili ya nguvu zako na furaha.

Kufikiria kwamba sharubati ya ***Soma*** itamletea Mungu nguvu au malaika Wake ni jambo la kuchekesha mno.

Siyo aya moja au mbili zinazofundisha ushirikina wa aina hii, mamia ya aya za aina hii zinaweza zikakaririwa. Tunayo miongoni mwa aya hizo, maelezo ya miungu wakipita pita angani, wakikalia mawingu au magari yenye magurudumu manne.

Sehemu kubwa ya Ma-Veda ni fikara za kifasiki. Hizi zahusikana na

mambo ya ngono na ni mawazo yaliyo machafu kiasi hiki kwamba kuyakariri kutautusi uungwana wa msomaji. Ashiki ya ngono na viungo vya ngono vinaelezewa kwa kirefu mno kiasi cha kuvifanya kuwa ni kinyaa kitupu hata iwe ni katika kitabu cha utabibu.

Kwa sababu hizi, tunaweza tukasema kwamba ingawaje kunazo sehemu za Ma-Veda zinazoashiria kutokana kwao na wahyi wa kimbinguni, kunazo sehemu zingine zinazothibitisha kwamba zimekumbwa na uzushi wa kibinadamu. Kutokana na ila hii, vitabu vya Veda haviwezi tena kuchukuliwa kama mwongozo kwa ajili ya mienendo ya wanadamu. Twahitaji badala ya vitabu hivi, kitabu kisichokuwa na dosari zozote za namna hii. Kitabu hicho ni Kurani.

HITILAFU KATIKA MA-VEDA

Chambileche Biblia vitabu vya Veda vina mapachiko chungu nzima yaliyofanywa na watu mbalimbali katika nyakati mbalimbali. Haliwi tena jambo la kustaajibisha kwamba zimo hitilafu nyingi katika matini za vitabu hivi, na hapa ipo baadhi ya mifano ya hitilafu zenyewe:

(i) Vitabu vya Veda vyaleta swali hili, ni nani aliyeumba jua? Kujibu swali hili yanapendekezwa majibu mbalimbali katika sehemu mbalimbali za Ma-Veda. Katika kitabu cha ***Rig-Veda*** (IX, 96:5) twaambiwa kwamba jua lilitengenezwa na mungu-Soma.

Lakini katika ***Rig-Veda*** (VIII, 36:4) twaambiwa kwamba jua lilitengenezwa na mungu-Indra. Kitabu hicho hicho chafundisha kitu kimoja katika mlango mmoja na kitu kingine kabisa katika mlango mwingine. Chafundisha katika mlango mmoja kwamba jua lilitengenezwa na mungu-Soma, na katika mlango mwingine, lilitengenezwa na mungu-Indra. Tugeukiapo vile vitabu vingine vya Veda tofauti huzidi kuwa kubwa mno.

Katika kitabu cha Yajur-Veda (31:12) twasoma kwamba jua lilitengenezwa na Brahma kutokana na jicho lake.

Kitabu cha ***Atharva-Veda*** chazidi kulihitilafisha jambo hili. Katika mlango wa (XIX, 27:7) twakuta kwamba miungu wote walijumuika

pamoja na wakalitengeza jua. Hii yatofautiana, na ni kinyume na yale maelezo mengine yote.

(ii) Vitabu vya Veda vyafundisha kwamba jua hapo mwanzoni lilikuwa juu ya uso wa ardhi, ndipo likapelekwa angani. Masimulizi haya pengine yanachekesha kwenye uwanja wa elimu ya nyota; haja yetu ni kutaka kusema tu ya kwamba hata rai hii ya kiajabuajabu imeelezewa kwa mitindo mbalimbali katika sehemu mbalimbali za Ma-Veda.

Katika *Krishna Yajur-Veda Taittiriya Samhita* (7:1) twasoma ya kwamba jua lilikuwa juu ya uso wa ardhi na hapo miungu wakalichukua juu angani kwa migongo yao na wakaliweka kule.

Katika *Rig-Veda* (X, 156:4) twasoma kwamba mungu-moto alilibeba jua na kuliweka juu angani.

Lakini katika kitabu cha *Rig-Veda* chenyewe mahali pengine (VIII, 12:30) twasoma kwamba mungu Indra peke yake alilipeleka jua mbinguni.

Na tena katika mahali pengine (X, 62:3) yasemewa kwamba jua lilipelekwa na wana wa Angira Rishi hadi mbinguni bila kusaidiwa na mwingine.

Katika *Atharva-Veda* (XIII 2:12) yatolewa habari kwamba jua lilipelekwa mbinguni bila ya msaada, na Atri Rishi kusudi likasababishe miezi (months).

Katika *Shukla Yajur-Veda* (4:31) ipo habari kwamba ilikuwa ni mungu Varuna aliyeliwekelea jua huko angani. Itikadi ya kwamba jua lilibebwa kutoka ardhini hadi juu mbinguni ni kichekesho tosha. Lakini kuwepo kwa habari zinazohitilafiana za itikadi hii kwazidi kuchekesha. Kitabu cha *Rig-Veda* peke yake chatoa habari tatu zinazohitilafiana. Habari moja ni kwamba jua lilichukuliwa na mungu-moto kutoka ardhini hadi mbinguni. Ya pili ni kwamba ilikuwa ni mungu Indra aliyefanya shughuli hii. Habari ya tatu ni kwamba wana wa Angira Rishi waliifanya kazi hii. Kitabu cha *Yajur-Veda* nacho pia chatoa habari zenye kuhitilafiana. Kulingana na

habari moja, wajibu huu ulitekelezwa bila ya msaada, na mungu Varuna. Kitabu cha Atharva-Veda chatoa habari tofauti kabisa, kikitangaza kwamba ilikuwa ni Rishi Atri aliyefanya kazi hii.

(iii) Kuhusu kuumbwa kwa mbingu na ardhi, tunazo habari chungu nzima ndani ya Ma-Veda. Lakini habari hizi zahitilafiana chambileche kuhitilafiana kwa habari za vizuka na vizimwi katika ngano za watoto.

Katika *Sama-Veda*, Purva Archik (VI.I:4), tunazo habari kwamba mbingu na ardhi vilitengenezwa na mungu Soma.

Lakini katika *Rig-Veda*. (VIII, 26:4) twakuta kwamba mbingu na ardhi vilitengenezwa na mungu Indra akiponea sharubati ya Soma.

Mahali pengine katika *Rig-Veda* (11, 40:1) ipo habari kwamba mbingu na ardhi vilitengenezwa na Soma na Pushan.

Katika *Yajur-Veda* (13:4) imeandikwa kwamba mbingu na ardhi vilitengenezwa na Brahma.

IDADI YA MIUNGU WA MA-VEDA

Twaamini, kama vile tulivyosema kimbele, ya kwamba vitabu vya Veda kiasili vilikuwa ni wahyi wa Mungu na katika hali hiyo havikufundisha chochote isipokuwa Umoja wa Mungu. Lakini vitabu vya Veda kama tuvijuavyo leo hii, sivyo vile vitabu vya Veda ambavyo vilifunuliwa kwa Marishii. Vitabu vya Veda hivi leo vimejaa maelezo ya miungu wengi, na maelezo haya yanapatikana kwa wingi kiasi hiki kwamba chochote kidogo kilichopo ndani ya Ma-Veda ambacho bado chaeleza Umoja wa Mungu kimewekwa kisogoni. Twatoa mifano michache hapa chini:

Katika *Yajur-Veda* (7:19) twaambiwa kwamba wako kwa jumla miungu thalathini na watatu, kumi na mmoja ardhini, kumi na mmoja angani, kumi na mmoja majini.

Katika *Rig-Veda* (111, 9:9) twaambiwa kwamba jumla ya idadi ya miungu ni 3,340. Imekuwa hivi, kwa sababu, sawa na *Rig-Veda,*

miungu 3,339 walimwendea mungu-moto na wakamlisha samli. Alipojiunga na hilo kundi kubwa jumla ya idadi ya miungu ikawa 3,3340. Hivyo basi, katika *Rig-Veda* (X, 52:6) jumla ya idadi ya miungu ni 3,340. Kutofautiana huku kwa idadi ya miungu kwenye sehamu mbalimabli za Ma-Veda kwashangaza kabisa; kulingana na *Yajur-Veda* idadi ya miungu ni 33 na sawa na *Rig-Veda* ni 3,340! Kuiachilia mbali itikadi ya Mungu Mmoja ni hatari tosha. Lakini hali hii ya kuhitilafiana kukubwa jinsi hii katika idadi ya miungu inayopendekezwa katika sehemu mbalimbali za Ma-Veda yaonekana kuwa mbaya kuliko hatari. Hitilafu sampuli hii zatulazimisha tufikie uamuzi kwamba ingawaje vitabu vya Veda vya asili kwa kweli vilikuwa vimefunuliwa, hivi vitabu vya Veda vya hivi leo havikubakiwa tena na ile sura ya asili, na haviwezi vikawaridhisha wale wanaotafuta faraja ya kiroho. Mahali pao panataka pachukuliwe na kitabu kingine kitakachobidi kutokuwa na mafundisho yote ya kifasiki, yenye kuhitilafiana, ya kikatili na tena ya kishirikina. Kitabu hicho, tusemavyo sisi, ni Kurani.

AHADI YA MWENYEZI MUNGU KWAKE NABII IBRAHIM[AS]

Swali la nne, ambalo jibu lake bila shaka litafafanua swali lihusikanalo na kuhitajika kwa Kurani, ni kwamba, Je dini za hapo awali zilijichukulia kuwa ndizo za mwisho? Au ziliamini namna fulani ya kuzidi kuendelea mbele kwa hali ya kiroho ambako kungeliishilizia na mafundisho ya mataifa yote kwa ajili ya mwongozo wa wanadamu wote?

Katika kulijibu swali hili, hatuna budi kukiri kwamba mfululizo wa masimulizi ambamo habari za Nabii mmoja zinaunganishwa na zile za Nabii mwingine utapatikana tu katika Biblia. Katika kuregelea habari za manabii, msaada tupatao kutokana na Biblia wafaa sana. Hapana kitabu kingine kilichofunuliwa kabla ya Kurani kinachoweza kutupatia msaada huu. Ili kujibu hili swali iwapo mafundisho ya hapo awali na Manabii wa awali walitabiri au hawakutabiri ujaji wa mafundisho matimilifu na Nabii mtimilifu baada yao, hatuna budi kuigeukia Biblia.

Tunapofanya hivyo, twakuta kwamba Mwenyezi Mungu alimwahidia Nabii Ibrahim[as] ahadi nyingi. Yeye alizaliwa katika sehemu ya Ur ya maeneo ya Chaldea. Kutoka sehemu hii akahama na babake hadi nchi ya Kanaani. Njiani babake akakaa mahali paitwapo Haran na akafia pale. Babake alipokufa Nabii Ibrahim[as] akaamriwa na Mwenyezi Mungu kuitoka Haran na kwenda Kanaani na akapokea huu wahyi unaofuatia:

> Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa (Mwa.12:2-3).

Na tena katika kitabu cha Mwanzo (13:15):

> "Maana nchi hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele

Na tena katika (Mwa. 16:10-12)

> Malaika wa Bwana akamwambia (Hadhrat Hajira[ra]), Hakika nitauzidisha uzao wako, wala hautahesabika kwa jinsi utakavyokuwa mwingi. Malaika wa Bwana akamwambia, Tazama! wewe una mimba, utazaa mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Ismaeli, maana Bwana amesikia kilio cha mateso yako. Naye atakuwa kama pundamwitu kati ya watu, mkono wake utakuwa juu ya watu wote na mkono wa watu wote utakuwa juu yake, naye atakaa mbele yao ndugu zake wote.

Na tena katika (Mwa. 17:9-11):

> Mungu akamwambia Ibrahimu, Nawe ulishike agano langu, wewe na uzao wako kwa vizazi vyao baada yako. Hili ndilo agano langu utakalolishika, kati ya mimi na wewe, na uzao wako baada yako, Kila mwanamume wa kwenu atatahiriwa. Mtatahiriwa nyama ya magovi yenu, na jambo hilo litakuwa ishara ya agano kati ya mimi na ninyi.

Na (Mwa.17:14):

> Na mwanamume mwenye govi asiyetahiriwa nyama ya govi lake, mtu yule atatengwa na watu wake; amelivunja agano langu.

Mbele zaidi katika (Mwa. 17:16) twaambiwa kwamba mkewe Ibrahimu Sarai naye pia aliahidiwa mwana:

> Nami nitambariki, na tena nitakupa mwana kwake, naam, nitambariki, naye atakuwa mama wa mataifa, na wafalme wa kabila za watu watatoka kwake.

Juu ya wazao wa Sarai (kwa njia ya Nabii Isihaka[as]) twaambiwa hivi katika (Mwa.17:19):

> Nami nitafanya agano langu imara kwake kuwa agano la milele kwa ajili ya wazao wake baada yake.

Juu ya Nabii Ishmael[as] twasoma katika (Mwa.17:20-22):

> Na kwa habari za Ismaeli nimekusikia, nimembariki, nitamzidisha, nami nitamwongeza sana sana. Atazaa maseyidi kumi na wawili, name nitamfanya awe taifa kubwa. Bali agano langu nitalifanya imara kwa Isaka, ambaye Sara atakuzalia majira kama haya mwaka ujao. Mungu akaacha kusema naye, akapanda kutoka kwa Ibrahimu.

Tena kwenye (Mwa.21:13):

> "Naye mwana wa mjakazi nitamfanya kuwa taifa, maana huyu naye ni uzao wako".

Tena juu ya Ismaeli, Mungu alisema na Hajiri (Mwa.21:17-18) akimwambia:

> Maana Mungu amesikia sauti ya kijana huko huko aliko. Ondoka, ukamwinue kijana, ukamshike mikononi mwako; kwa kuwa nitamfanya kuwa taifa kubwa.

Tena katika (Mwa. 21:20-21) tunayo maneno haya:

> Mungu akawa pamoja na huyo kijana, naye akakua, akakaa katika jangwa, akawa mpiga upinde. Akakaa katika jangwa la

Parani; mama yake akamtwalia mke katika nchi ya Misri.

Kutokana na maneno haya tuliyoyanukuu, ni wazi kwamba Nabii Ibrahim[as] alikuwa na wana wawili, Ismaeli na Isihaka, Ismaeli akiwa mkubwa na Ishaka akiwa mdogo wake. Mwenyezi Mungu alimwahidi Nabii Ibrahim[as] ya kuwa atakiongeza kizazi chake. Ahadi yenyewe yawahusu wote wawil, Isihaka na Ismaeli. Kutokana na madondoo hayo pia yaonekana kwamba Ishamaeli aliishi katika jangwa la Parani, kwamba nchi ya Kanaani ilipewa wana wa Nabii Ibrahim[as], na kwamba alama ya kidhahiri ya lile agano ambalo Mungu alilifanya na Nabii Ibrahim[as] ilikuwa ni tohara ya wanaume wote. Ahadi hizi zote zilitimizwa. Wazao wa Isihaka waliongezeka sana. Kutoka miongoni mwao wakainuka Manabii, Musa, Daudi, Dhulkifil Ezekieli, Danieli na Yesu[as]. Kwa miaka elfu mbili wao wakaitawala nchi ya Kanaani. Mamlaka yao juu ya nchi hii hayakupata kusitizwa kwa hakika, ijapokuwa kwa muda kadha yalidhoofika. Hata hivyo baada ya karne ya saba ya Kikristo (A.D.) wana wa Isihaka, na wale waliofuata kanuni za Sheria ya Nabii Musa[as] hawakuwa na budi kuitoka nchi ya Kanaani. Wana wa Ishameli, badala yao, wakawa ndio viongozi wa nchi hiyo wa kisiasa na kiroho. Ukweli kwamba wana wa Israeli hawakuwa na budi kuisalimisha nchi ya Kanaani waonesha kwamba wao walikuwa wamekuwa watu wasiostahilia tena ile ahadi ya Mungu Aliyokuwa Amemfanyia Nabii Ibrahim[as]. Ahadi hii ilikuwa kwamba Israeli atadumu akiimiliki nchi hii hadi Siku ya Mwisho, na hii ilikuwa ahadi ya kweli. Siku ya Mwisho katika hiyo ahadi ya kiungu, haiwezi ikamaanisa siku itakayodalilisha mwisho wa dunia, bali ile siku itakapobadilishwa sheria ya Nabii Musa[as] kwa kufunuliwa Sheria mpya kwa ajili ya mwongozo wa dunia. Katika lugha ya wahyi wa kiungu ujaji wa Sheria mpya mara nyingi unaelezewa kuwa ni kuzaliwa kwa mbingu mpya na ardhi mpya. Kama vile ambavyo mbingu mpya na ardhi mpya haviwezi vikaumbwa bila ya msukosuko mkubwa — kwa kawaida unaohusikana na Siku ya Mwisho — hivyo basi, kusimikwa kwa Sheria mpya ni sharti uwemo ndani yake msukusuko mkubwa wa wale watu wenye kuipokea Sheria hiyo. Kwa

hiyo, iliposema bishara ya kuwa wana wa Israeli watadumisha umilikaji wao wa nchi ya Kanaani hadi Siku ya Mwisho, ilimaanisha kwamba umilikaji wao ungeliendelea hadi ujaji wa Nabii mpya Mleta Sheria. Katika kauli za Nabii Daudi[as] tunacho kidokezeo cha maana hii ya bishara yenyewe. Ile bishara iliyomo ndani ya Kitabu cha Mwanzo kwamba Israeli atadumisha umilikaji wa nchi ya Kanaani hadi Siku ya Mwisho yaelezewa kivingine. Ndiposa katika kitabu cha Zaburi (37:29) twasoma maneno haya:

"Wenye haki watairithi nchi, nao watakaa humo milele".

Umilikaji wa milele sio wa Israeli bali ni kwa ajili ya wenye haki. Kauli hii ya Nabii Daudi[as], kusema kweli, lilikuwa ni onyo la kinagaubaga ya kwamba siku za utukufu wa Israeli zilikuwa zimefikia ukingoni. Nabii alionekana kama aliyekuwa akisema kwamba ahadi hiyo ya kiungu, baada ya muda, haikuwa ieleweke katika sura ya kitaifa bali katika maana ya kiroho; kwamba wana wa Ismaeli watazirithi zile ahadi alizopewa Nabii Ibrahim[as] kwa kurithi ukweli na agano jipya litafanywa kwa njia ya hao. Kama maelezo yetu ya bishara si sawa, basi swali ni, Kwa nini Mungu aliwawafanya wana wa Ismaeli — na wanaoamini Ujumbe wa Kurani — watawala nchini Palestina. Bishara likuwa wazi sana. Wana wa Isihaka ilikuwa waitawale nchi ya Palestina hadi Siku ya Mwisho. Sasa swali ni kwa nini hawakufanya hivyo? Mbona Mungu akaruhusu kuhamishiwa uwezo wa kisiasa kutoka wana wa Isihaka hadi wana wa Ismaeli? Kama kuhamishwa kwenyewe kungelikuwa kwa muda mfupi, basi kusingeiletea bishara yenyewe tofauti yoyote. Kunyanyuka na kudidimia kwa hadhi za mataifa ni mambo ya kawaida. Lakini kule kuhamishwa tunakokuzungumzia kulitokea kuwa kwa kudumu. Zaidi ya miaka elfu moja na mia tatu imepita, na nchi ya Palestina bado iko chini ya mamlaka ya Waislamu, wana wa Ismaeli. Mataifa ya Ulaya na Urusi yanafanya chini juu kubadili hali hii, lakini hadi hivi sasa, kwa vyovyote vile, hayajafaulu. Kama yatafaulu katika harakati zao, basi kufaulu kwenyewe hakuna budi kuwe ni kwa muda tu. Walowezi wapya wa Kiisraeli ama watasilimu na kujipatia tena mamlaka juu ya

nchi ya Palestina kwa njia ya agano jipya; au hawatakuwa na budi kuitoka nchi ya Palestina kwa mara ya tena. Nchi ya Palestina ni kwa ajili ya wale wanaozingatia lile agano alilofanya Nabii Ibrahim[as] na Mwenyezi Mungu. Wakristo, bila shaka, wanadai wanalitekeleza agano hilo. Lakini wao wanasahau kwamba agano lenyewe lasisitizia alama muhimu ya kidhahiri. Alama hiyo ni tohara ya wanaume wote. Ni Waismaeli peke yao ambao wamedumisha alama hiyo kabla na baada ya kufunuliwa Kurani.

Kwa neno zima, bishara ya Nabii Ibrahim[as] yawaahidi baraka wote wawili, Ishaka na Ismaeli. Sawa na ahadi hii, wana wa Isihaka wakaikalia nchi ya Kanaani na wana wa Ismaeli wakaikalia nchi ya Arabuni. Lakini Siku ya Mwisho ilipowadia kwa hao wana wa Isihaka, hapo sawa na bishara ya Nabii Daudi[as] ahadi hiyo ikahamishwa kutoka kwake Israeli hadi kwake Ismaeli. Madai ya Israeli yakawa sasa ni madai ya kitaifa. Madai ya Ismaeli yalikuwa ni ya kiroho. Katika misingi ya madai yao ya kitaifa wana wa Ismaeli wakashikilia mji wa Makka na maeneo yaliyoko pembezoni mwake (Sura Al-Baqara, 2:125-129). Katika misingi ya madai yao ya kiroho wakajiongezea nchi ya Kanaani katika miliki yao baada ya kuzorota kwa hali ya kidini ya Israeli.

BISHARA KATIKA KUMBKUMBU LA TORATI

Nabii Musa[as] alipokwenda Mlima wa Horebu kwa amri ya Mungu, yeye aliwahutubia wana wa Israeli akiwaambia:

> Bwana, Mungu wako, atakuondokeshea Nabii miongoni mwa ndugu zao kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye (Kum.18:15).

Mungu aliongea na Nabii Musa[as] akimwambia:

> Mimi nitawaondokeshea Nabii miongoni mwa ndugu zao, mafano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru. Hata itakuwa, mtu asiyesikiliza maneno yangu atakayoyasema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake. Lakini nabii atakayenena neno

> kwa kujikinai kwa jina langu, ambalo sikumwagiza kulinena, au atakayenena katika jina la miungu mingine, nabii yule atakufa. (Kum. 18: 18-20).

Kutokana na maneno haya ni dhahiri kwamba Nabii Musa[as] alitoa bishara juu ya ujaji wa Nabii Mleta Sheria ambaye angelikuja baada yake, na ambaye angelikuwa kutoka miongoni mwa ndugu za Waisraeli.

Ukweli kwamba Nabii huyu angekuwa Mleta Sheria, wala si Nabii wa kawaida uko peupe kutokana na maneno haya "kama Musa". Kama vile Nabii Musa[as] alivyokuwa Mleta Sheria, yule Nabii ambaye angelifanana na Nabii Musa, naye pia angekuwa Nabii Mleta Sheria. Huyo Nabii anayeahidiwa yuaelezewa kuwa ni Nabii "atakayewaambia yote nitakayomwamuru". Kutokana na maneno haya pia yaonekana kwamba huyu Nabii Mwahidiwa angekuwa Nabii Mleta Sheria. Kuletwa kwa Sheria mpya kunamaanisha kuanzishwa kwa silsila mpya, taifa jipye. Hivyo, Nabii mleta Sheria mpya si Mwalimu wa Kawaida au Mujadidi. Yeye hana budi kuwasilisha mafundisho makamilifu, zikiwemo kanuni za kimsingi pamwe na utondoti wa maamrisho. Bila ya hiyo, taifa jipya haliwezi likazalika. Lakini Nabii asiyeleta Sheria mpya, jukumu lake ni kuelezea tu na kufafanua Sheria iliyopo. Sio lazima kwake yeye kuwawasilishia watu wake yote ayapokeayo toka kwa Mwenyezi Mungu. Yawezekana kwamba baadhi ya wahyi wake unuiwe kwa ajili ya ulezi wake yeye mwenyewe binafsi, asiowajibika kuufikisha kwa watu wake. Bishara hali kadhalika yaagizia kwamba huyo Nabii Mwahidiwa "ataongea katika jina langu", na wale ambao hawatamsikiliza, Mungu "atalitaka kwao"; yaani, wale ambao hawatamsikiliza adhabu itahakiki juu yao. Pia twaambiwa kwamba yeyote atakayesingizia kuitimiza bishara hii atauawa.

Kama tukiyatilia maanani masharti yote ya bishara yenyewe, tunalazimika kuamua kwamba hadi kufikia kwa akali wakati wa Yesu hakuwa Nabii amedhihiri duniani angeliyeweza kusemwa kwamba alikuwa amelingana na maelezo ya yule Nabii Mwahidiwa. Kwa hiyo, Manabii wote waliodhihiri baina ya Musa na Yesu wanaweza

kutohesabiwa, pale tutakaposhika njia kumtafuta yule Nabii awezaye kusemwa kwamba ametimiza bishara hii. Wao hawakuacha nyuma wafuasi wala watu wawezao kuyafuatilia madai yao. Anabakia Yesu tu mwenye wafuasi wengi, na anyechukuliwa na wafuasi wake kuwa ndiye Mwalimu wa mwisho kuletwa na Mungu humu duniani. Lakini tunapomnaasibishia Yesu bishara hii, sharti baada ya sharti, twakuta kwamba hapana moja limhusulo yeye:

Kwanza, huyo Nabii Mwahidiwa alikuwa awe ni Nabii Mleta Sheria. Je, Yesu alikuwa Mleta Sheria? Je, yeye alileta Sheria mpya humu duniani kuchukua mahali pa ile ya zamani? Yesu aliltamka kinagaubaga akisema:

> Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie (Mt. 5:17-18).

Wafuasi wa Yesu wakatilia fora kiasi cha kutangaza wakisema:

> Na torati haikuja kwa imani, bali, Ayatendaye hayo ataishi katika hayo. Kristo alitukomboa katika laana ya torati (Gal, 3:12-13).

Yesu hakutoa madai ya kuwasilisha Sheria mpya, na wafuasi wake wanaichukulia Sheria kuwa ni laana. Basi, Yuawezaje Yesu na wafuasi wake kusemwa wanatimiliza ile bishara ya Kumbukumbu la Torati.

Pili, huyo Nabii mwahidiwa hakuwa ainuliwe kutoka miongoni mwa Waisraeli bali kutoka miongoni mwa ndugu zao na Yesu alikuwa Mwisareli.

Watetezi wa Kikristo wakabiliwapo na ukweli huu, wana mazoea ya kusema kwamba Yesu hakuwa na baba wa kiardhini, kwa hivyo anaweza akasemekana kuwa ni mmoja wa ndugu za Israeli. Lakini wazo sampuli hii haliwezi likafua dafu. Bishara yazungumzia ndugu (zao) — jambo linalomaanisha kwamba hilo lingelikuwa ni taifa au jamii ya watu ambao kutoka miongoni mwao huyo Nabii mwahidiwa angedhihiri. Yesu kasimama peke yake kama mwana wa Mungu,

kama pangekuwepo na wana wa Mungu wengineo, yeye huenda angelingana na maelezeo ya bishara. Lakini, mbali na haya, imesemwa kwa uwazi ndani ya Biblia ya kuwa Kristo alikuwa awe ni wa mbegu ya Daudi (Zaburi, 132:11; Jerimia, 23:5). Yesu Anaweza akajiambulia mbali chimbuko lake la Kiisraeli kwa kuwa eti hakuwa na baba wa kidunia: lakini hapo hawezi akabakia tena kuwa mwana na Daudi, hivi kwamba ile bishara ya Zaburi kuhusu Kristo haitamwafiki yeye.

Tatu, bishara yasema: "Nami nitatia maneno yangu kinywani mwake". Lakini Injili siyo maneno aliyoyatia Mwenyezi Mungu kinywani mwa Yesu. Injili zatuelezea tu habari za Yesu na yale aliyoyatamka katika baadhi ya mahubiri yake ya hadharani na yale wanafunzi wake waliyoyasema na kutenda katika nyakati mbalimbali.

Nne, huyo Mwahidiwa alikuwa awe ni Nabii, ilihali rai ya Kikristo ni kwamba Yesu hakuwa Nabii, bali mwana wa Mungu. Sasa, anawezaje Yesu akalingana na maelezeo ya bishara ile?

Tano, katika bishara imesemwa: "Maneno atakayoyasema katika jina langu. La ajabu ni kwamba hamna katika Injili mfano hata mmoja wa maneno anayoweza Yesu kusemekana kwamba aliyapokea kutoka kwa Mungu akiamriwa kuyafikishia wale aliowafundisha.

Sita, humo katika bishara tunayo maneno: "Atawaambia yote nitakayomwamuru." Nabii Mwahidiwa, sawa na maneno haya, alikuwa aipatie dunia mafundisho matimilifu yaliyo na mambo yote. Lakini Yesu hakujidaia wadhifa kama huu. Yeye alijichukulia kuwa ni mtangulizi wa Mwalimu Mkuu zaidi aliyekuwa hajafika. Ndiposa tunayo maneno haya katika (Yn. 16:12-13):

> Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari zake.

Kutokana na maneno haya yaonekana kwamba ile bishara ya

Kumbukumbu la Torati haikutimia katika dhati ya Yesu. Basi, hatuna jingine ila kuonelea kwamba Maagano yote mawili, la kale na Jipya, yalitabiri ujaji wa Nabii baada ya Yesu, atakayeiongoza dunia nzima "kwenye ukweli wote", na ambaye atasimika jina la Mungu humu ardhini milele na milele. Madai yetu ni kwamba kufunuliwa kwa Kurani na ujaji wa Mtume Mtukufu vinabainisha kutimilizwa kwa ile bishara iliyomo ndani ya Kumbukumbu la Torati. Kweli zifuatazo zathibitisha jambo hili:

(i) Mtukufu Mtume Muhammad[saw] alikuwa mzao wa Ismaeli. Wazao wa Ismaeli walikuwa ni ndugu wa wazao wa Isaka, amabo ndio Waisraeli.

(ii) Mtume Muhammad[saw] ndiye peke yake anayedai kuwa yu Nabii mfano wa Musa. Tunayo maneno haya katika Kurani (Sura Al-Muzzammil, 73:16):

> "Hakika Sisi tumewatumieni Mtume aliye shahidi juu yenu, kama tulivyompeleka Mtume kwa Firauni".

Kurani bila shaka yamfananisha Mtume Mtukufu[saw], na Nabii Musa[as].

(iii) Bishara yamwelezea yule Mwahidiwa kuwa ni Nabii. Mtume Mtukufu[saw] alidai kuwa Nabii tu. Upande mwingine, Yesu, tuambiwavyo, hakudai kuwa Nabii. Twasoma katika Marko (8:27-30):

> Akawauliza wanafunzi wake, akasema, Watu huninena mimi kuwa ni nani? Wakamjibu, Yohana Mbatizaji; wengine, Eliya, wengine, Mmojawapo wa manabii. Naye akawauliza, Na ninyi mnasema ya kuwa mimi ni nani? Petro akamjibu, akamwambia, Wewe ndiwe Kristo. Akawaonya wasimwambie mtu habari zake.

Ndio kusema kwamba, Yesu yuakataa kuwa yeye ni Yohana Mbatizaji, au Eliya, au mmojawapo wa Manabii. Lakini ile bishara ya Kumbukumbu la Torati yamzungumzia yule Mwahidiwa kuwa ni Nabii kama Musa. Bishara hii hivyo basi yamwafiki Nabii wa Islam wala sio Yesu.

(iv) Bishara yazungumzia "maneno nitakayoyatia kinywani mwake".

Injili hazina maneno yoyote sampuli hiyo. Kinyume chake, Mtume Mtukufu wa Islam[saw] alileta duniani Kurani ambayo tangu mwanzo hadi mwishoni ni neno tupu la Mwenyezi Mungu, ambalo Mungu alilitia kinywani mwake. Kurani yajielezea yenyewe kuwa ni neno la Mungu (Sura Al-Baqara, 2:76).

(v) Bishara ilisema kwamba Huyo Mwahidiwa atasema yote atakayoamrishwa. Tumezikariri Injili kuthibitisha kwamba Yesu hakufikisha kila alichopokea toka kwa Mwenyezi Mungu, na kwamba alikuwa aje mwingine baadaye kufanya hivyo. Mtume Mtukufu[saw] wa Islam yuayaafiki kabisa maelezo haya. Tunayo maneno haya katika Kurani (Sura Al-Maaida, 5:68) "Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako". Aya hii ni kama inayosema kwamba, "Ewe Mtume, ipo bishara ya kale kukuhusu wewe iliyosema kwamba utakapokuja humu duniani utaipatia ukweli wote ulioupokea toka kwa Mungu wako. Hivyo basi, hubiria ulimwengu chochote kile kifunuliwacho kwako, wanadamu wakipende au wasikipende". Vivyo hivyo, ile aya iliyofunuliwa kulipohitimika kufunuliwa kwa Kurani yasema:

Leo nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema Yangu, na nimewapendeleeni Islam iwe dini yenu (Sura Al-Maaida, 5:4).

Hii ndio kusema kwamba, "Kwa njia ya wahyi wa Kurani, dini imetimilizwa na hiba ya mwongozo imekamilishwa kwa ajili yenu, na amani na utulivu vimechaguliwa kama dini yenu". Basi, ni Mtume Mtukufu[saw] wa Islam aliyefundisha kila kitu na hakusaza chochote. Wakati wa Yesu, watu hawakuwa tayari kupokea na kuamini kila kitu kilichokuwa na manufaa. Lakini wakati wa Mtume Mtukufu[saw] wa Islam mwanadamu alikuwa amezipitia hatua zote za mabadiliko ya kiroho na wakati ulikuwa umewadia wa ukweli wote kufunuliwa kwa wanadamu.

(vi) Bishara yazungumzia "maneno atakayoyasema katika jina langu".

Sehemu hii ya bishara nayo pia ilitimia katika dhati ya Mtume Mtukufu [saw] wa Islam. Yeye peke yake ndiye aliyeongea katika jina la

Mwenyezi Mungu, kwa sababu kila Sura ya Kitabu hicho kilichofunuliwa alichokuja nacho yeye yaanza kwa maneno: "Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema Mwingi wa ukarimu". Ishara hii kubwa, iliyotiliwa barabara ndani ya Kurani, pia yathibitisha kwamba hatua za mwisho za maendeleo ya kiroho ya mwanadamu, zilizotabiriwa na Nabii Musa[as], zilifikiwa kwa ujaji wa Mtume Mtukufu[saw] wa Islam.

(vii) Bishara iliweka kigezo muhimu ikisema:

> Lakini nabii atakayenena neno kwa kujikinai kwa jina langu, ambalo sikumwagiza kulinena, au atakayenena katika jina la miungu wengine, nabii yule atakufa (Kumbukumbu la Torati, 18:20).

Katika maneno haya dunia ilifundishwa jinsi ya kumpambanua Yule Mwahidiwa mbali na wale itakaowabidi kusingizia tu ya kuwa eti wanatimiza bishara hii. Ilikuwa ni lazima ya kwamba kigezo bayana kiwekwe. Mwahidiwa huyo alikuwa atwishwe jukumu la misheni muhimu ya kuanzisha hatua ya mwisho kabisa katika maendeleo ya kiroho ya mwanadamu. Kama watokee wadai bandia kwenye cheo hiki, basi dunia ingelikuwa hatarini. Ili kuepushilia mbali hatari hizi, Mwenyezi Mungu akaweka hiki kigezo ya kwamba mdai wa bandia ataonjeshwa adhabu ya kimbinguni na kukumbwa na kifo na ushinde. Mtume Mtukufu[saw] wa Islam alitoa madai ya wadhifa huu mapema sana katika kazi yake, tena kwa njia iliyo wazi fika. Zama alipotangaza madai yake, yeye hakuwa na rafiki na alikuwa mtu mnyonge. Maadui zake walikuwa wengii tena wenye nguvu, na walifanya chini juu kukwamisha ujumbe wake na kazi yake wala kwao wao hapakuwa na jambo lililokuwa gumu katika jitihada zao za kumuulia mbali. Watawala wenye nguvu hali kadhalika walijitokeza dhidi yake lakini ilikuwa ni wao, wala siye Mtume Mtukufu, waliopata fedheha. Mtume Mtukufu[saw], alifariki akiwa na ufanisi mkubwa. Alipofariki, Arabuni nzima tayari ilikuwa imemwamini; na baada ya kifo chake Makhalifa wake wa awali katika muda wa miaka michache

tu wakazagaza Islam katika dunia yote iliyojulikana wakati ule.

Musa alikuwa Nabii mkweli. Ile bishara ya Kumbukumbu la Torati ilikuwa ni wahyi toka kwa Mwenyezi Mungu. Lakini je, Mtume Mtukufu[saw], ilikuwa ni sharti afanikiwe vile alivyofanikiwa? Na je, wale maadui zake, waliokazania kifo chake, walikuwa ni sharti kutofaulu vile ambavyo hawakufaulu? La hasha, ufaulu wa Mtume Mtukufu[saw], na kutofaulu kwa maadui zake hayakuwa mambo ya bahati. Kwa upande mwingine, yaonekana kwamba Kurani ilikuwa ikitilia maanani masharti ya ile bishara ya Kumbukumbu la Torati ilipotangaza machoni pa Arabuni nzima tena mapema kabisa katika kazi ya Mtume Mtukufu[saw] ikisema:

> "Na Mwenyezi Mungu atakulinda dhidi ya watu" (Sura Al-Maaida, 5:68).

Vivyo hivyo, ikiwatangazia maadui za Mtume[saw], Kurani ilisema:

Yeye yu Mjuzi wa siri, wala Hamdhihirishii yeyote siri Yake, isipokuwa Mtume Aliyemridhia; basi hakika Yeye Humwekea mlinzi mbele yake na nyuma yake (Sura.Al-Jinn, 72:27-28).

Hivi ni Kusema kwamba, Mtume[saw], akiwa amepatiwa wajibu muhimu, hatakosa kulindwa. Maadui katu hawataweza kumuua.

Aya hizi zilithibitisha kwamba ule ufanisi Mtume Mtukufu[saw] alioupata halikuwa jambo la kutotazamiwa na la kibahati tu. Yeye alitangaza mapema, kwa njia ya wahyi uliopokewa naye kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kurekodiwa hadi leo ndani ya Kurani, ya kwamba Mungu atamlinda dhidi ya maadui zake na umwagaji damu. Yeye aliionya dunia hii ya kwamba kwa vile yeye hakuwa mwenye kujisingizia bali alikuwa ni Yule Nabii aliyeahidiwa katika Kumbukumbu la Torati, basi hatauawa asilani.

Kwa neno zima, miaka elfu moja na mia tisa kabla ya ujaji wa Mtume[saw] wa Islam, Nabii Musa[as] akatangaza kwamba Sheria yake yeye mwenyewe haikuwa, katika mpango wa kimbinguni, Sheria ya mwisho; kwamba dunia ilikuwa ipate Sheria timilifu zaidi hapo

baadaye; na kwamba, kwa ajili ya Sheria hiyo, Mwenyezi Mungu ataleta katika Siku za Mwisho Mtume Wake mwingine. Mtume huyu alikuwa afundishe kweli zote; ilikuwa ni yeye Mtume huyu ambaye angelikuwa ni kikomo cha mwisho katika maendeleo ya kiroho ya mwanadamu. Dunia ilikuwa isubiri Kitabu kingine na Nabii mwingine. Hivyo, kama Kurani na Mtume Mtukufu[saw] kaja baada ya Biblia na baada ya Manabii Musa na Yesu, na kama Kurani na Mtume Mtukufu[saw] anadai kwamba amekuja toka kwa Mwenyezi Mungu kama mwongozo kwa ajili ya mwanadamu, basi madai haya ya Kurani na Mtume Mtukufu[saw] hayana budi kuchukuliwa kuwa ni ya haki na ya kweli. Hayana budi madai haya kuchukuliwa kuwa ndiko kutekelezwa kwa bishara za kale. Wahyi wa Kurani haukuwa kazi bure, usiokuwa na kazi pakiwepo na huo wahyi wa kale. Ama kusema kweli, kama Kurani isingelikuwa imefunuliwa, basi zile ahadi zilizofanywa na Mwenyezi Mungu kwa njia ya Mitume Wake zingelikuwa zimekosa kutimilizwa, na dunia ingelifikwa na tashwishi na kutoamini.

PARANI – SEHEMU YA ARABUNI

Katika Kumbukumbu la Torati (33:2) tunayo maneno haya:

> Akasema, Bwana alitoka Sinai, Akawaondokea kutoka Seiri; Aliangaza kutoka kilima cha Parani, Akaja na elfu kumi za watakatifu. Upande wa mkono wake wa kuume palikuwa na sheria ya moto-moto kwao.

Katika mstari huu Musa yuaahidiwa madhihirisho matatu ya shani ya Mwenyezi Mungu. La kwanza la madhihirisho haya lilitokea kutoka Sinai, ambalo juu yake kidokezo kinafanywa katika kitabu cha Kutoka (19:20) kwa maneno haya:

> Bwana akashukia mlima, juu ya kilele cha mlima; Bwana akamwita Musa aende hata kilele cha mlima; Musa akapanda juu.

Dhihirisho hili la shani ya kiungu lilitokea wakati wa Nabii Musa[as]. Dunia ilishuhudia baraka zilizokuja nalo. Muda ukapita. Dhihirisho la

pili lililoahidiwa katika bishara ilikuwa litokee huko Seiri. Seiri ni lile eneo la dunia ambako huko ilitendeka miujiza ya Yesu. Hivyo basi, maneo haya "akawaondokea kutoka Seiri" yanaashiria ujaji wa Yesu. Wafasiri wa Biblia wa Kikristo wanaitambulisha Seiri na Sinai lakini hili ni kosa. Seiri ni sehemu ya nchi ya Palestina. Jina lenyewe lina mitindo mingi ghafi. Mtindo mmojawapo wa jina hili watumika kama jina la watu ambao ni wazao wa Nabii Yakubu[as] na ambao wanajulikana kama Banu Asher. Mwingine watumika kuwa ni jina la sehemu ya kaskazini magharibi ya nchi ya Palestina. Hivyo basi, Seiri, ndiyo ishara ya dhihirisho la pili la shani ya kiungu, yaani, lile lenye kuhusikana hasa na nchi ya Palestina. Kuitambulisha Seiri na Sinai na kumnasibishia Nabii Musa[as] madhihirisho yote mawili ni kosa pia kwani Nabii Musa[as] hakuingia nchi ya Kanaani. Yeye alifia mahali ambapo aliweza kuona tu mipaka ya nchi ya Kanaani. Baada ya Nabii Musa[as] na kabla ya Yesu hapakutokea dhihirisho la shani ya kiungu lingeliloweza kufanana na lile la Sinai. Kwa hivyo, "Kuwaondokea kutoka Seiri" kunamaanisha ujaji wa Yesu uliotokea ndani kabisa ya nchi ya Kanaani, na ambao kwa njia yake, kama ilivyokuwa, Mungu kaonyesha uso Wake kwa mara ya pili. Dhihirisho la tatu la shani ya kiungu lilikuwa lichomoze kutoka Parani, na Paran (Kiarabu Faran) ndilo jina la vile vilima vilivyopo baina ya Makka na Madina. Wanajiografia wa Kiarabu daima waliliita eneo hili Faran. Mahali pa kupumzikia kwenye njia kuu itokayo Makka kwenda Madina panaitwa Bonde la Fatima. Misafara ipitapo, watoto toka maeneo jirani hukutana nayo na kuwauzia maua. Wakiulizwa yatokako maua yale, watoto hujibu wakisema: "Barriyyatu Faran" (Faslul-Khitaab), yaani, yanatoka kwenye jangwa la Faran. Hivyo basi, Faran, ni sehemu ya Arabuni; bali Hijaz hasa. Kulingana na Agano la Kale, Ismaeli aliishi kwenye maeneo haya. Ndiposa katika Kitabu cha Mwanzo (21:20-21) tunayo maneno haya:

> Mungu akawa pamoja na huyo kijana (Ismaeli), naye akakua, akakaa katika jangwa, akawa mpiga upinde. Akakaa katika jangwa la Parani; mama yake akamtwalia mke katika nchi ya Misri.

WAKUREISHI NI WAZAO WA HADHRAT ISMAELI[AS]

Maelezo ya Biblia ya eneo hili la Paran kwa kiasi yanahitilafiana na yale ya wanajiografia wa Kiarabu. Kulinga na na Biblia, Parani ni nchi inayopakana na Kanaani. Lakini nchi iliyo ya miti na milima ni sharti liwe ni eneo kubwa mno, wakati mwingine likiwa ni lenye kusambaa masafa ya maili elfu nyingi. Haiwezi ikawa ni kijipande cha ardhi kilichomo ndani ya nchi nyingine au mipakani mwake. Yale maelezeo ya Biblia yanaweza tu yakamaanisha ya kwamba misitu na vilima vya nchi ya Parani vyachomoza kwenye eneo fulani pembezoni mwa nchi ya Kanaani. Bali hayawezi yakamaanisha kwamba Parani ni eneo la kusini la nchi ya Kanaani. Biblia, hata hivyo, yakiri kwamba Nabii Ibrahim[as] alikuwa na mwana aliyeitwa Ismaeli na kwamba mwana huyo aliishi Parani. Ushahidi wa wana wa Ismaeli wenye kuikalia nchi hiyo, hauna budi kuwa wa maana zaidi. Waisraeli ni sharti wasiwe na mengi ya kusema juu ya jambo hili. Ujuzi wao wa historia na jiografia haukuwa mzuri. Wao hata hawakuweza kutoa maelezo ya kutosha ya njia waliyoifuata katika ile safari yao wenyewe kutoka Misri kwenda Kanaani. Basi, wao wangewezaje kutangaza juu ya ukweli wa mambo ya kijiografia ya nchi zingine? Ni jamii moja tu leo hii inayonasibisha ukoo wao na Nabii Ismaeli[as] na hao ndio Wakureishi. Wanaishi nchini Arabuni, na Makka ndio mji wao mkuu. Kama madai ya Wakureishi ni uwongo, basi inakuwa vigumu kupata matilaba yake. Madai yenyewe yasingeliweza kunyanyua hadhi yao, kwani Waisraeli bado waliwadharaulia mbali. Hapana kitu kingelichowafanya watu wa jangwani kunasibisha ukoo wao na Nabii Ismaeli[as] isipokuwa nasaba yenyewe iwe ni kweli tupu.

Hali kadhalika, kama madai ya Waarabu ni uwongo, basi ni wapi wazao wa Nabii Ismaeli[as] walikopotelea? Sawa na Biblia, Ismaeli alikuwa na wana kumi na wawili, na tena sawa na Biblia, hawa kumi na wawili walikuwa waongezeke, sana.

Na hapo katika kitabu cha Mwanzo (21:13) tunayo maneno haya:

> Naye mwana wa mjakazi nitamfanya kuwa taifa, maana huyu

naye ni uzao wako.

Tena katika Mwanzo (21:18) tunayo maneno haya:

"Ondoka, ukamwinue kijana, ukamshike mkononi mwako, kwa kuwa nitamfanya kuwa taifa kubwa".

Tena katika Mwanzo (17:20) Mungu yuamwambia Nabii Ibrahimu[as] hivi:

Na kwa habari za Ismaeli nimekusikia, nitamzidisha, nami nitamwongeza sana sana. Atazaa maseyidi kumi na wawili, nami nitamfanya awe taifa kuu.

Yaani, wazao wa Nabii Ismaeli[as], wataongezeka sana sana na kuwa taifa kubwa. Kama madai ya Waarabu ya wao kuwa ni wazao wa Nabii Ismaeli[as] yakiwa ni uwongo mtupu, basi hizi bishara za Biblia nazo hazina budi ziwe ni uwongo. Kwani hapana taifa jingine duniani linalonasibisha ukoo wake na Nabii Ismaeli[as]. Ni pale tu madai ya Waarabu yanapokubaliwa, ambapo zile bishara za Biblia kuhusikana na Nabii Ismaeli[as] ziwezapo kuthibitika kuwa za kweli; kwani zote zahusikana na Waarabu.

Ushahidi wa kihistoria ulio mzito kupita wote ni desturi madhubuti za kitaifa. Kwa mamia ya miaka jamii imejihesabu kuwa ni wazao wa Nabii Ismaeli[as] na hapana jamii nyingine duniani iliyojihesabu kuwa hivyo. Ushahidi bora zaidi ya huu hauwezi ukawepo.

Sawa na Biblia, Waismaeli waliishi Parani, na hii Parani kulingana na wanajiografia wa Kiarabu, ni ile nchi inayoenea kutoka Makka hadi mipaka ya kaskazini ya Arabuni. Hii Parani, kwa hiyo, ni sehemu ya nchi ya Arabuni kikwelikweli kama vile Wakureishi walivyo wazao wa Nabii Ismaeli[as]. Hivyo, ile taadhima ya kiungu iliyokuwa ichomoze kutoka Parani ilikuwa ichomoze kutoka Arabuni.

Ukweli kwamba Waismaeli walikuwa wakikaa Arabuni wathibitishwa na ushahidi zaidi kutoka ndani ya Biblia. Katika kitabu cha Mwanzo (25:13-16) tunayo majina ya wale wana kumi na wawili wa Nabii Ismaeli[as] kama ifutavyo:

1. Nebayothi. 2. Kedari. 3. Abdeeli. 4. Mibsamu. 5.Mishma. 6. Duma. 7. Masa. 8. Hadadi. 9. Tema. 10. Yeturi. 11. Nafishi. 12.Kedema.

Sawa na desturi za kale, yatupasa kutarajia wazao wao kuitwa kwa majina ya mababu zao. Wazao kwa Nabii Yakub[as], kwa mfano, wangeitwa kwa jina la mkale wao. Nchi hali kadhalika zimeitwa kwa majina ya watu wao. Kufuatana na desturi hizi uchunguzi wa wakazi wa nchi ya Arabuni waonesha kwamba majina ya wale wana kumi na wawili wa Nabii Ismaeli[as] yanakutwa yakizagaa sehemu mbalimbali za nchi ya Arabuni. Wazao wa Nabii Ismaeli[as] wanayajaza mapana na marefu yote ya nchi hiyo.

Mwana wa kwanza wa Nabii Ismaeli[as] alikuwa ni Nebayothi. Eneo linalokaliwa na wazao wake, sawa na maoni ya wanajiografia wa Kiarabu, ni baina ya digrii thalathini upande wa Kaskazini na baina ya digrii thalathini na sita na thalathini na nane upande wa Mashariki (wa Arabuni). Padri Katripikari (Khutbaat Ahmadiyya) yuaukubali ukweli huu na kusema kwamba wazao wa Nebayothi walikalia nchi baina ya Palestina na Yambuu‘, iliyo bandari ya mji wa Madina.

Kedari alikuwa ni mtoto wa pili. Wazao wake nao pia ni sehemu ya wakazi wa Arabuni. Kiasili maana ya neno Kedari ni “wa ngamia”, inayoashiria ukazi wao wa Kiarabuni. Hawa wanapatikana katika eneo baina Hijazi na Madina. Akina Ptolemy na Pliny, wakati wa maelezo yao ya watu wa Hijazi, wanazungumzia makabila ya Kedari na Gedori (jina Gedori laelekea kuwa ubetuaji wa jina Kedari). Kunao Waarabu hivi leo wanaodai kuwa wazao wa Kedari.

Mwana wa tatu alikuwa ni Abdeeli. Sawa na mwanahistoria Josephus, hawa Waabdeeli nao pia waliishi katika eneo hili hili la Arabuni. Wa nne alikuwa ni Mibsamu. Hatuwezi kupata alama za kabila hili katika vitabu vya kawaida vya jiografia. Lakini yawezeka kwamba jina lao limegeuzwa kiasi cha kutoweza kutambulikana. Mwana wa tano alikuwa ni Mishma, na Wamishma wanapatikana huku Arabuni hadi hivi leo. Wa sita alikuwa ni Duma. Mahali pamoja maarufu huko Arabuni bado panaitwa Dumah, na wanajiografia wa Kiarabu

wanamnasibishia jina hili yule mwana wa sita wa Nabii Ismaeli[as]. Wa saba alikuwa ni Masa, ambaye jina lake lapatikana vivyo hivyo katika kabila moja la Kiyemeni. Bali hata masalia ya magofu yao ya kale yanaweza yakaoneshwa. Padri Katripikari anagusia ukweli huu. Mwana wa nane alikuwa ni Hadadi ambaye kufuatia jina lake tunao ule mji mashuhuri wa Hudaida nchini Yemeni.

Mwana wa tisa alikuwa ni Tema. Kutoka sehemu ya Najd hadi Hijaz eneo hili laitwa Tema na linakaliwa na wazao wa Tema. Kusema kweli yaonekana wao wamesambaa hadi Ghuba la Uajemi (Persian Gulf).

Mwana wa kumi alikuwa ni Yeturi (yaani, Yatur kwa Kiarabu). Hawa Wayaturi nao pia wanaweza wakapatikana nchini Arabuni na wanajulikana kama Wajeduri. Mara nyingi sauti za herufi "j" na "y" hupokezana kama vile zinzvyopokezane sauti za herufi "t" na "d".

Mwana wa kumi na moja alikuwa ni Nafishi, na Bwana Foster afikiria kwamba msimamo wa Bwana Josephus na ule wa Agano la Kale waunga mkono hii rai kwamba wazao wa huyu Nafishi walikaa katika jangwa la Arabuni.

Mwana wa kumi na mbili alikuwa ni Kedema. Makazi ya wazao wa Kedema yafahamika, sawa na maoni ya mwanajiografia mashuhuri, Mas'ud, kuweko huko Yemeni. Lile kabila lijulikanalo kama As'habur Rass na linalotajwa ndani ya Kurani ni wazao wa Nabii Ismaeli[as], nao walikuwa ni makabila mawili, moja liitwalo Kedama na jingine Yamini. Sawa na rai zingine hilo la pili liliitwa Ra'wil, wala sio Yamini.

Hivyo basi, ushahidi wa kihistoria na ule wa kijiografia, hivyo basi, waonesha ya kwamba wazao wa Nabii Ibrahim[as] wameishi huko Arabuni. Wote waliupatia heshima kubwa mji wa Makka na Nyumba ya Kaaba, na kutokana na ukweli huu yaonekana kwamba Hadhrat Ismaeli[as] kwanza kabisa alikaa mjini Makka, na hili ndilo eneo ambalo, sawa na kumbukumbu za Waarabu na hata zile za Agano la Kale, linaitwa Parani (au Faran kwa Kiarabu) Ushuhuda wa ufunuo wa Nabii Isaya[as] waunga mkono rai hii hii kama unavyosema katika kitabu cha Isaya (21:13-14):

> Ufunuo juu ya Arabuni. Ndani ya mwitu wa Arabuni mtalala, Enyi misafara ya Wadedani. Waleteeni wenye kiu maji, Enyi wenyeji wa nchi ya Tema; Nendeni kuwalaki wakimbiao na chakula chao. Kwa maana wanakimbia mbele ya panga, Upanga uliofutwa, na upinde uliopindwa, Na mbele ya ukali wa vita. Kwa sababu Bwana ameniambia hivi, Katika muda wa mwaka, kama miaka ya mtu mwenye kuajiriwa, utaangamia utukufu wote wa Kedari. Na mabaki ya hesabu ya wavuta pinde, hao mashujaa wa Kedari watakuwa wachache; maana Bwana, Mungu wa Israeli, amenena neno hili.

Maneno haya ya kitume ni picha hasa ya vita vya Badr vilivyofanyika takriban mwaka mmoja baada ya Mtume Mtukufu[saw] kuhama kutoka Makka kwenda Madina. Katika vita hivi wana wa Kedari, watu wa Makka na maeneo jirani, walionjeshwa ushinde mkubwa na Waislamu. Huku wakishindwa kukabiliana na ukali wa wapiganaji wa Kiislamu wa panga na mishale, watu wa Makka wakaambulia ushinde ufedheheshao. Hebu yatilieni maanani yale maneno ambayo kwayo kifungu hiki cha maneno kinaanzia: "Ufunuo juu ya Arabuni". Humo ndani Tema na Kedari vinazungumziwa kimoja kama eneo la nchi ya Arabuni na kingine kama kabila Ia Kiarabu. Sawa na maneno haya, aliyofunuliwa Nabii Isaya[as] miaka mia saba na kumi na minne kabla ya Yesu, wazao wa Nabii Ismaeli[as] waliishi huko Hijaz.

Kwa neno zima, kutoka upande wowote ule tuwezao kulitalii suala hili, upo ushahidi chungu nzima ya kwamba Makureshi walikuwa wazao wa Nabii Ismaeli[as] na kwamba Parani ile Parani ya Kibiblia (Faran, kwa Kiarabu) ndiyo ile nchi walikoishi. Lile dhihirisho la shani ya kiungu lililokuwa lifanyike huko Farani lilikuwa ni ujaji wa Mtume Mtukufu Muhammad[saw], uliotabiriwa na Nabii Musa[as].

MTUME MTUKUFU[SAW] KATAJWA KATIKA KITABU CHA HABAKUKI

Ujaji huu ulitabiriwa pia katika kitabu cha Habakuki (3:3-7) miaka mia sita na ishirini na sita kabla ya Yesu. Ndiposa tunayo maneno haya:

> Mungu alikuja kutoka Temani, Yeye aliye mtakatifu kutoka mlima Parani. Utukufu wake ukazifunika mbingu, Nayo dunia ikajaa sifa yake. Mwangaza wake ulikuwa kama nuru; Alikuwa na mishale ya nuru ubavuni mwake; Ndipo ulipofichwa uwezo wake. Akasimama, akaitetemesha dunia; Akatazama, akawasitusha mataifa; Na milima ya zamani ikatawanyika; Vilima vya kale vikainama; Miendo yake ilikuwa kama siku za kale. Niliziona hema za Kushani katika taabu; Mapazia ya nchi ya Midiani yakatetemeka.

Hapa kupo kutajwa kwa Tema na Mtakatifu kutoka Parani. Kutokana na utabiri wa Nabii Musa[as] na Habakuki ni dhahiri kwamba ujaji wa Yesu haukuwa uwe ndicho hatua ya mwisho ya maendeleo ya kiroho ya mwanadamu. Ujaji wenyewe ulikuwa ufuatiwe na Nabii mwingine kuadhimisha dhihirisho la tatu la shani ya kiungu. Nabii huyu alikuwa aje kudhihirisha vyote viwili Uzuri na Ujalali wa Mungu na kuleta Sheria moto-moto duniani, sio eti Ujumbe tu wa kusameheana.

Yule Mtakatifu wa kudhihiri kutoka nchi ya Tema na Mlima Parani ndiye Mtume Mtukfu Muhammad[saw], na Sheria yake moto-moto ndiyo Kuran yenye sifa ya kuteketezelea mbali ule uchafu ambao kwao madhambi na njama za Kishetani hutengenezewa. Ama kwa hakika Nabii Musa[as] alisema kuwa Yule Mwahidiwa, aangazaye kutoka Parani, ataandamana na elfu kumi za watakatifu. Kama ulimwengu mzima unavyojua, alikuwa ni Mtume Mtukufu[saw] wa Islam aliyeinuka huko Parani na akaingia mjini Makka pamwe na wafuasi elfu kumi. Je, Yesu anaweza akasemwa kuwa alitimiza bishara hii kuu au Nabii Daudi[as] au Nabii Musa? Je, yupo mmoja wao aliyedhihiri kutoka Parani? Je, yupo mmoja wao aliyeenda kwenye ushindi akifuatana na wafuasi watakatifu elfu kumi? Yesu alikuwa na wanafunzi kumi na wawili tu, ambao mmoja wao akamwuza Yesu kwa hela chache. Na mwingine akamlaani Yesu akiogopa kuteswa. Kumi wakabakia waaminifu, lakini, isemavyo Injili, hao pia walijiendea zao zama Yesu alipowambwa Msalabani. Ingelikuwa wao

kusimama bega kwa bega na Bwana wao, hata hapo uandamaji wa watu kumi usingelikuwa sawa na uandamanaji wa watu elfu kumi. Na halafu bishara hiyo ya Biblia yasema kwa uwazi kwamba hao elfu kumi wangekuwa pamoja na yule Nabii Mwahidiwa. Lakini Injili yatuambia kwamba wale wanafunzi kumi waliobakia walimkimbia alipotundikwa Msalabani.

Sawa na kitabu cha Habakuki, ishara moja ya huyo Nabii Mwahidiwa ilikuwa iwe ni kiasi cha sifa azisifiwazo. Ndiposa Habakuki (3:3) kasema: "Nayo dunia ikajaa sifa yake".

Haionekani kwetu sisi kuwa ni jambo la kibahati tu ya kwamba Nabii Mtukufu[saw] wa Islam aliitwa Muhammad (jina ambalo kiasili maana yake ni Msifiwa). Maadui zake walipomkataa, waliihofia hali ya uendaji kinyume unayomaanishwa na kumkataa yule Msifiwa. Hivyo basi, wao wakaligeuza jina lake la Muhammad kuwa Mudhammam wakimpindua kutoka Msifiwa hadi Mkataliwa. Masahaba wa Mtume[saw] walipokasirishwa na kule kukataliwa kwa Mtume na matusi waliyomtupia, yeye alikuwa akitamka na kuwaambia, "Fanyeni subira; hawanitusi mimi bali mtu mwingine aitwaye Mudhammam" Ni yule tu mwenye jina zuri jinsi ilivyo sura na tabia yake angeliyeyaafiki yale maelezo aliyokuwa ameyatoa Habakuki ya Yule Mwahidiwa. Pia hapana budi kutilia maanani ile desturi ya uandikaji wa beti za kumsifu ambayo imemea mizizi katika Islam, na ambayo imezaa lile tawi muhimu la Ushairi uandikwao na Waislamu wa nchi zote.

Habakuki pia yuasema kwamba:

> "Mbele zake ilikwenda tauni, na makaa ya moto yakatoka miguuni pake". (3:5)

Ishara hii ya Yule Mwahidiwa nayo pia ilitimilizwa katika dhati ya Nabii[saw] wa Islam. Kweli kabisa, bishara hii yazungumzia janga la maradhi ya kuambukiza, maradhi yaliyosambaa sana. Lakini ni uharibifu mkubwa na vifo visababavishwavyo na janga vinavyozungumziwa hapa. Kwa kuwa maadui wa Mtume Mtukufu[saw] walikumbwa na uharibifu mkubwa na vifo kwenye mapambano yao dhidi yake, yeye anaweza

akasemewa alitimiza hata sehemu hii ya bishara hiyo.

Kisha kitabu cha Habakuki (3:6) chasema:

> "Akisimama, akaitetemesha dunia: Akatazama akasitusha mataifa"

Hii sehemu ya bishara hii, chambileche zile sehemu zingine, haiwezi ikamwafiki Musa wala Yesu. Nabii Musa[as] alifariki huku akipigana na maadui zake, ambapo Yesu aliwambwa Msalabani. Yule Nabii aliyetazama na kuyashtusha mataifa alikuwa ni Nabii[saw] wa Islam. Na kweli kabisa yeye mwenyewe alijielezea akisema, "Kuwepo kwangu mimi kwatia hofu, na ilivyonisaidia si haba. Watu wanaogofyewa nami mwendo wa safari ya mwezi mzima" (Bukhari).

Na tena:

> "Na milima ya zamani ikatawanyika; Vilima vya kale vikainama (Habakuki, 3:6).

Hii sehemu ya bishara hii nayo pia yahusikana na Nabii[saw] wa Islam. Kwani maadui zake walifagiliwa mbali. Milima na Vilima vyamaanisha tu mataifa makubwa makubwa.

Na tena tunayo maneno haya katika Habakuki (3:7):

> "Niliziona hema za Kushani katika taabu; Mapazia ya nchi ya Midiani yakatetemeka".

Sehemu hii ya bishara yaonesha kwa uwazi kwamba yule Nabii Mwahidiwa alikuwa atokane na mahali pengine nje ya nchi ya Siria. Kwani ni makundi ya wafidhuli nchini Kushani na Midiani yatayoadhibiwa na kupatwa na hofu yatakapojitokeza majeshi ya Yule Mwahidiwa. Maelezo haya hayawezi kuhusikana na Nabii Musa wala Yesu[as]. Yahusikana na Nabii[saw] wa Islam peke yake. Wakati jeshi lake dogo, zama za Khalifa wake wa kwanza Hadhrat Abu Bakar[ra], lilipoikabili Palestina, licha ya ukweli kwamba nchi ya Kanaani wakati ule ilikuwa chini ya himaya ya Kaisari wa Urumi, mtawala wa nusu nzima ya dunia iliyojulikana wakati ule, majeshi yenye nguvu ya Kaisari yalikomolewa na wanajeshi wanyonge wa Kiislamu. Naam,

"Hema za Kushani zilikuwa katika taabu na mapazia ya nchi ya Midiani yakatetemeka, kwa hakika". Wakazi wa nchi hizi wakaambulia usalama wao kwa kusalimu amri ya watumishi wa Mtume Mtukufu Muhammad[saw].

UJAJI WA MTUME MTUKUFU[SAW] ULITABIRIWA NA NABII SULEIMAN[AS]

(a)Katika Wimbo ulio Bora (5:10-16) kunazo habari hizi:

> Mpendwa wangu ni mweupe, tena mwekundu, mashuhuri miongoni mwa elfu kumi; kichwa chake ni kama dhahabu safi sana, nywele zake ni za ukoka, nyeusi kama kunguru; Macho yake ni kama hua penye vijito, wakioga kwa maziwa, wakiikalia mito iliyojaa; Mashavu yake ni kama matuta ya rihani, ambayo hufanyizwa manukato; Midomo yake ni kama nyinyoro, inadondoza matone ya manemane; mikono yake ni kama mianzi ya dhahabu, iliyopambwa kwa zabarajadi; Kiwiliwili chake kama kazi ya pembe, iliyonakishiwa kwa yakuti samawi; Miguu yake ni kama nguzo za marimari, zilizowekwa juu ya misingi ya dhahbu; Sura yake ni kama Lebanoni, Ni bora mfano wa mierezi; Kinywa chake kimejaa maneno matamu, Ndiye mzuri sana pia pia. Ni huyu mpendwa wangu, ni huyu rafiki yangu, Enyi binti za Yerusalemu.

Bishara hii yaahidi ujaji wa Nabii atakayekuwa mbora zaidi ya wengine, na atakayekuwa na cheo cha juu zaidi ya wengine. Sisi twasema haya kwa sababu yale maelezo ya kiashiki katika Wimbo Ulio Bora yanakuja kama majibu ya hili swali:

> "Mpendwa wa namna gani ni mpendwa wako?" (Wim.5:9).

Twaambiwa kwamba mpendwa huyu atasimama chambileche beramu miongoni mwa waja elfu kumi. Kwa kuwa beramu hutambulisha jeshi, hivyo maelezo hayo yahusikana na tukio kuu ambapo huyu mpendwa atasimamia ufuasi wa watu elfu kumi.

Pia twaambiwa kwamba:

> "Midomo yake ni kama nyinyoro, inadondoza matone ya manemane (5:13).

Sasa manemane ni aina fulani ya utomvu, wenye ladha chungu lakini harufu nzuri na wenye manufaa makubwa, sumu ya virusi na kichanganyio cha dawa za kuulia virusi, na katika kutibu vijeraha na katika kutegeneza marashi na manukato.

Pia twaambiwa kuwa yeye "ni mzuri sana pia pia" (zingatia jina Muhamaddim kwa lugha ya Kiebrania). Hili lamaanisha kwamba dhati yake na tabia yake vitakuwa vya namna ambayo kwamba itachochea upendo na hali ya kustaajabia.

Bishara hii kwa uwazi kabisa yamuafiki Mtume Mtukufu[saw] wa Islam.

Alikuwa ni yeye aliyeongoza watakatifu elfu kumi na akajitokeza kibingwa kutoka miinuko ya Parani hadi kwenye bonde la Makka, sawa kabisa na vile ilivyokuwa imetabiriwa na Nabii Musa[as]. Alikuwa ni yeye ambaye mafundisho yake yalihakiki kuwa kama manemane kwa ulimwengu, yenye ladha chungu lakini mazuri mno katika athari zake. Yalikuwa na kanuni na maamrisho ambayo yote yalinuiwa kunawirisha masilahi ya mwanadamu, na ambayo hata hivyo yalikuwa ni machungu kwa baadhi ya mataifa. Na ni yeye aitwaye (bali aliye sawasawa kabisa na maelezo ya jina) Muhammad.

Waandishi wa Kikristo huelekea kudai kwamba yule mpendwa mwahidiwa katika bishara hii ameitwa Muhammadim na sio Muhammad. Lakini ukinzani huu haufiki popote. Katika Agano la Kale jina lake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni ***Elohim***. Katika lugha ya Kiebrania ni kawaida kuonesha staha kwa kuzungumzia mtu mmoja kwa neno la wingi. Hata sisi hufanya vivyo hivyo katika lugha ya Kiurdu. Msemaji katika lugha ya Kiurdu, huweza kuhitimisha usifiaji wake wa Mtume Mtukufu[saw] kwa kusema "***Yeh hain hamare Muhammad[saw]***," Hawa ndio Muhammad wetu.

(b) Katika Wimbo Ulio Bora, tunayo bishara nyingine kumuhusu Mtume Mtukufu[saw] wa Islam. Hii imo katika kifungu cha 4:9-12.

Katika mistari hii Nabii Suleiman[as] yuamzungumzia mpendwa wake kama umbu na bibi arusi pia (4:9; 4:10; 4:12). Kutumiwa wakati ule ule mmoja kwa njia hizi mbili za kumtaja mpendwa — kuwa ni umbu na pia bibi arusi — si jambo lisilokuwa na maana yake. Mpendwa huyo kuitwa "Umbu" kunaashiria kwamba Nabii Mwahidiwa angelikuwa Mwismaelia, mmoja wa ndugu za Waisraeli; na kuitwa "bibi arusi" kunaashiria kwamba Ujumbe wa huyo Nabii Mwahidiwa hautakuwa kwa ajili ya watu wake peke yao, chambileche ule Ujumbe wa Manabii wote wa Kiisraeli. Bali Ujumbe huo utakuwa kwa ajili ya mataifa mengine pia. Tusipotoshwe na hali ya jinsia ya kike iliyotumiwa katika maneno haya. Maneno yenyewe yamenenwa katika lugha ya kishairi, iliyojaa mafumbo. Mstari wa mwisho wa mlango huu watumia jinsia ya kiume, inayokwenda kinyume kabisa, lakini yenye maana. Ndiposa tunayo maneno haya:

> "Mpendwa wangu na aingie bustanini mwake, akayale matunda yake mazuri" (4:16).

Hivyo basi, bishara hiyo ya (4:9-12) yamhusu Mtume Mtukufu[saw] wa Islam peke yake. Yesu hakuwa mmoja wa ndugu za Waisraeli, wala mafundisho yake hayakuelekezewa mataifa yoyote minghairi ya taifa la Waisraeli.

(c) Pia tunayo katika Wimbo Ulio Bora (1:5-6)maneno haya:

> Mimi ni mweusi-mweusi, lakini ninao uzuri, enyi binti za Yerusalemu, Mfano wa mahema ya Kedari, kama mapazia ya Sulemani. Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi-mweusi.

Kutokana na maelezo haya yaonekana kwamba Nabii Suleimani[as] alitabiri ujaji wa Nabii atakayekuja kutoka upande wa kusini, naye (au watu wake) angelikuwa na ngozi nyeusi-nyeusi ukilinganisha na wazao a Nabii Isihaka[as] Ni ukweli wenye kujulikana sana kwamba watu wa nchi za Siria na Palestina rangi yao ni nyeupe-nyeupe kuliko watu wa nchi ya Arabuni. Nabii[saw] wa Islam alikuwa ni Mwarabu.

(d) Mahali hapo hapo alama nyingine ya huyo Mwahidiwa yatolewa

kama ifuatavyo:

> Wana wa mamangu walinikasirikia; waliniweka niwe mlinzi wa mashamba ya mizabibu; bali shamba langu mwenyewe sikulilinda. (1:6).

Haya ni maelezeo ya watu ambao huyu Mwahidiwa angetokana nao. Waarabu, zama za ujaji wa Nabii[saw] wa Islam, hawakujitakia makuu. Wao walikubali kuwatumikia Warumi na Waajemi, lakini nchi yao wenyewe hawakujali ila kidogo tu. Akaja Mtume Mtukufu[saw] na nchi ya Arabuni ikaamka. Matokeo yake yakawa ni mwendeleo wa kimataifa ukiongozwa na Waarabu ulioipenya kila aina inayofikirika ya maendeleo ya mwanadamu — maendeleo ya kiroho, kifikira na kisiasa. Sasa Waarabu wakawa si tu walinzi wa mashamba ya mizabibu yao, bali mashamha ya mizabibu ya dunia nzima.

(e) Wimbo Ulio Bora la Suleimani unalo pia onyo dhidi ya Waisraeli. Ndiposa tunayo maneno haya katika 2:7 ya kwamba

> Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, kwa paa na kwa ayala wa porini, msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, mpaka yatakapoona vyema yenyewe.

Wito huo huo waendelezwa Wimboni katika kifungu cha 3:5 na 8:4. Maneno ya vifungu hivi yanamaanisha tu ya kwamba ajapo huyo Nabii Mwahidiwa, Mayahudi na Wakristo, matawi mawili ya Israreli, watampinga na kumnyanyasa; lakini kwa kuwa Nabii mwenyewe atakuwa ni Nabii Mchaguliwa wa Mungu, hawatafaulu, bali badala yake watashindwa vibaya sana. Nabii Suleimani kwa sababu hiyo, aliwaonya watu wake akiwaambaia:

> "Nawasihi, msiyachochee mapenzi wala kuyaamsha, mpaka yatakapoona vyema yenyewe".

Waisraeli, wakiwemo Mayahudi na Wakristo, walinasihiwa kutomtenda chochote huyo Nabii Mwahidiwa. Uwezo wake utakapozienea nchi zao, basi na wamkubali. Itakuwa kazi bure kumpinga na kujaribu kuzuia mkumbo wa uwezo wake. Upinzani

utamletea mshindani maangamio yake yeye mwenyewe. Kwani watu waingiliao kazi ya Nabii hufaradhishiwa adhabu ya kimbinguni. Onyo hilo likaja kuwa stahili. Mayahudi na Wakristo walikuja kuwa wanyanyasaji na wakajiletea wenyewe adhabu ya kimbinguni. Kama watu wanajishikia hamsini zao wala hawaoneshi uadui wowote kwa Nabii, basi yeye hachukui hatua kali yoyote dhidi yao bali hujishughulisha tu na kufundisha na kuhubiri. Kwa nadra tu, Nabii hushika upanga, lakini dhidi tu ya wale watanguliao kumchomolea upanga. Yeye huwapiga vita wale tu watanguliao kumpiga vita wakitafuta kuuzima kwa mabavu na uonevu wao ule Ujumbe ulioletwa na Mungu. Mfano wa Mtume Mtukufu[saw] waangazia vizuri rai hii. Ilikuwa ni hatari ifuatanayo na upinzani wa kiholela dhidi ya Ujumbe wa kweli ambao Nabii Suleimani[as] alionya juu yake.

Bishara hizi haziwezi kabisa kumhusu Yesu. Yesu hakudhihiri kutoka upande wa kusini wa nchi ya Palestina. Wala yeye hakuwa mmoja wa ndugu za Waisraeli. Wala hakuwa na uwezo wa kukabiliana na kuvunjilia mbali upinzani wa Israeli. Bishara hizi zamhusu tu Nabii[saw] wa Islam. Yeye ndiye mpendwa wa ule Wimbo wa Nabii Suleimani (Wimbo Ulio Bora). Kusema kweli, Wimbo wenyewe ni maelezeo ya furaha tele ya yule Nabii.

BISHARA ZA NABII ISAYA[AS]

Kitabu cha Isaya nacho pia kimejaa bishara chungu nzima kumhusu Nabii Mtukufu[saw] wa Islam. Zote zinaashiria ujaji wa Nabii mwingine mkuu, mletaji wa amani na maridhiko kwa ajili ya dunia nzima. Hata hivyo, sawa na desturi ya kiungu bishara zenyewe zinayo hali ya kimifano isiyokuwa na budi kufafanuliwa kabla maana za bishara hizo kuweza kutafasiriwa. Kule kutumiwa ndani ya bishara hizo majina kama vile Yerusalemu, Sayuni n.k., ni mifano tu. Lakini waandishi wa Wakristo wamepotoshwa na mifano hii katika kufikiria kwamba bishara hizo zamhusu Yesu. Majina vile yalivyo majina hayawi sehemu yoyote ya bishara hizo. Kama kile kilichomo ndani ya bishara kwa jumla hakimhusu Yesu, basi majina Yerusalemu au

Israeli au Sayuni hayawezi yakahalalisha kunasibishiwa Yesu bishara hizi. Ni kweli kabisa, majina yenyewe nayo pia yana maana, lakini ni maana inayoafikiana na sehemu iliyo kubwa ya kile kinachozungumziwa bisharani. Mambo yakiwa hivyo majina Yerusalemu na Israeli yatamaanisha tu "Pahali pangu patakatifu" au "Watu wangu wateule", wala sio Yerusalemu au Israeli hasa.

(a) Bishara ya awali tunayotaka kuinukuu kutoka kitabu cha Isaya imo katika ya 4:1-3. Nayo ni kama ifuatavyo:

> Na siku hiyo wanawake saba watamshika mtu mume mmoja wakisema, tutakula chakula chetu, na kuvaa nguo zetu wenyewe, lakini tuitwe tu kwa jina lako; utuondolee aibu yetu. Siku hiyo chipukizi la Bwana litakuwa zuri, lenye utukufu, na matunda ya nchi yatakuwa mema sana, na kupendeza, kwa ajili ya Waisraeli wale waliookoka. Tena itakuwa ya kwamba yeye aliyebaki katika Sayuni, na yeye aliyeachwa ndani ya Yerusalemu, ataitwa mtakatifu; yaani, kila mmoja aliyeandikwa miongoni mwa hao walio hai ndani ya Yerusalemu.

Ikikubaliwa tu kwamba majina Sayuni na Yerusalemu katika bishara hii ni mifano tu, basi yote yaliyomo humu bisharani yanaeleweka kuwa yanamhusu Mtume Mtukufu[saw] wa Islam wala si yeyote mwingine. Bishara yasema yule Nabii Mwahidiwa ataleta pamoja naye utajiri na utukufu, kwamba yeye atazimiliki hazina za ardhi, kwamba watu wake wataitwa watakatifu na kwamba kuoa wake wengi itakuwa ni desturi wakati huo. Je ishara hizi zinamhusu Yesu na wanafunzi wake? Je, wao walileta kipindi cha utajiri na utukufu? Je, wao walizimiliki hazina za ardhi? Je, kuoa wake wengi ilikuwa ni desturi miongoni mwa jamii yao? La, hasha. Ishara hizi zahusikana tu na Mtume Mtukufu[saw] wa Islam, wafuasi wake na wakati wake. Yesu yuadhaniwa kuwa aliyekatalia mbali ndoa za wake wengi. Lakini Mtume Mtukufu wa Islam aliziruhusu bali hata alizihimiza katika hali fulani fulani. Ilikuwa ni wakati wake ambapo vita ilibidi vipiganwe kuihami dini na vijana wa taifa ikabidi wayatoe maisha yao. Idadi ya

wajane ikaongezeka na vijana wa kike wakakabiliwa na shida ya kujipatia waume. Mtume Mtukufu, sawa na hali ilivyokuwa, akapendekeza ndoa za wake wengi ili kuzuia uasherati na kukidhia nguvu za wale waliopoteza maisha yao vitani.

(b) Katika Isaya (5: 26-30) tunayo maneno haya:

> Naye atawatwekea bendera mataifa toka mbali, naye atawapigia miunzi tokea mwisho wa nchi; na tazama, watakuja mbio mbio upesi sana. Miongoni mwao hakuna achokaye wala kukwaa; hakuna asinziaye wala kulala usingizi; wala mshipi wa viuno vyao hautalegea, wala ukanda wa viatu vyao hautakatika; mishale yao ni mikali, na pinde zao zote zimepindika; kwato za farasi zao zitahesabika kama gumegume; na gurudumu zao kama kisulisuli; ngurumo yao itakuwa kama ya simba; watanguruma kama wana-simba; Naam, watanguruma na kukamata mateka, na kuyachukua na kwenda zao salama, wala hakuna mtu atakayeokoa. Nao watanguruma juu yao siku hiyo kama ngurumo ya bahari; na mtu akiitazama nchi, ataona giza na dhiki, nayo nuru imetiwa giza katika mawingu yake.

Ulikuwa uje wakati, sawa na bishara hii, ambapo mahali fulani nje ya nchi ya Palestina, mja angelipandisha beramu. Mja huyu angeliyaita mataifa ya dunia ambao wangeitikia mwito wake na upesi-upesi wangemkusanyikia. Wale waliomwitikia wangeepukana na uvivu na uzembe na wangejitolea kufa na kupona katika imani yao. Wangeshiriki katika vita na kwato za farasi wao zingetoa cheche za moto. Mashambulio yao dhidi ya maadui zao yangekuwa kana kwamba ni kisulisuli. Wangewashinda maadui zao kabisa kabisa ambao hangekuwepo wa kuwaokoa. Na ni kwa nini basi wao kufanya haya yote? Kwa sababu wao wataona dunia imejaa giza na mabadiliko makubwa yanatakikana.

Bishara hii nzima yamhusu Mtume Mtukufu[saw] wa Islam. Imedokezewa pia katika Kurani. Sawa na bishara hii, Mtume Mtukufu alidhihiri mbali kabisa na nchi ya Palestina — mjini Makka,

na akapandisha beramu yake mjini Madina; alikuwa yeye aliyeitangazia dunia akisema:

> "Enyi watu, hakika mimi ni Mtume wa Mungu kwenu nyote (Sura Al-A'raaf, 7:159).

Ilikuwa ni sauti yake ambayo wanaume kwa wanawake toka pembe zote za dunia waliitikia kwa shime mno. Katika maisha mazima ya Yesu hata mfuasi mmoja hakupatikana toka nje ya Israeli. Wanafunzi wake wote walitoka kwenye eneo la maili arubaini hadi hamsini. Lakini wamwaminio Nabii[saw] wa Islam walitoka Yemen na Najd na Irani, na miongoni mwao walikuwemo waabuduo masanamu na Mayahudi na Wakristo. Walijitolea kufa na kupona kuitikia wito wa Mtume Mtukufu[saw] na kuutilia shime bila kinyongo hivi kwamba maadui sugu wa Islam wanaona hawana budi kuupongeza moyo wao wa upendo na kujitolea mhanga. Mwenyezi Mungu Mwenyewe yuawapongeza katika Kurani Akisema:

> "Mwenyezi Mungu Amewaridhia, nao pia wamemridhia (Sura, At-Tauba, 9:100).

Na pia:

> "Baadhi yao wamekwisha maliza nadhiri zao, na wako miongoni mwao wanaongojea" (Sura Al-Ahzaab, 33:24).

Wafuasi wa Mtume Mtukufu[saw], hawakuwa na budi kushiriki katika vita na kutumia pinde na mishale. Kwato za farasi wao zilifanana na jiwe la mango litoalo cheche linaposuguliwa au kupigwa, na magurudumu yao kama kisulisuli. Juu ya jambo hili kipo pia kidokezeo kingine katika Kurani inaposemekana:

> Naapa kwa (farasi) wakimbiaji wanaotweta, na kwa wale watoao moto kwa kupiga, tena kwa wale washambuliao wakati wa asubuhi; Basi wao wanapeperusha mavumbi; kisha wanapenya ndani ya kundi (la maadui)" (Sura Al- 'Aadiyaat, 100:2-6).

Haya ndiyo maelezo ya mashujaa wa Islam wa hapo awali, na ama kwa hakika yanaafikiana kabisa na bishara ya Isaya.

Tunayo katika sehemu moja ya bishara hii maneno haya:

> Na mtu akiitazama nchi, ataona giza na dhiki, nayo nuru imetiwa giza katika mawingu yake (Isaya 5:30).

Kurani yaligusia jambo hili katika Sura Ar-Ruum, 30:42 hivi:

"Ufisadi umedhihirika barani na baharini".

Yaani, akili ya mwanadamu na mafundisho ya kiungu vyote viwili vimekuwa na hali ya giza-giza na vyote vyaashiria haja ya Mwalimu mpya, mwenye Ujumbe mpya kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Hali kadhalika katika Sura At-Talaaq 65:11-12 tunayo maneno haya:

> Hakika Mwenyezi Mungu Amewateremshieni Ukmbusho — Mtume anayewasomeeni Aya za Mwenyezi Mungu zinazobainisha, ili kuwatoa wale walioamini na watendao mema kutoka giza na kuwapeleka kwenye nuru.

(c) Katika Isaya (8: 13-17) tunayo maneno haya:

> Bwana wa majeshi ndiye mtakayemtakasa; na awe yeye hofu yenu, na awe yeye utisho wenu. Naye atakuwa ni mahali patakatifu; bali ni jiwe la kujikwaza na mwamba wa kujikwaa kwa nyumba za Israeli zote mbili, na mtego na tanzi kwa wenyeji wa Yerusalemu. Na wengi watajikwaa juu yake, na kuanguka na kuvunjika, na kunaswa na kukamatwa. Ufunge huo ushuhuda, ukaitie muhuri sheria kati ya wanafunzi wangu. Nami nitamngojea Bwana, awafichaye uso wake nyumba ya Yakobo, nami nitamtazamia.

Bishara hii kwa uwazi yatabiri kudhihiri kwa Mja mtakatifu ambaye ujaji wake utahakiki kuwa ni mtihani kwa nyumba zote mbili za Israeli, utakuwa ni mtego na kinasio kwa wakazi wa Yerusalemu, watakaoshindwa na kufedheheshwa endapo watakata shauri kumpinga. Ujaji wake utatambulisha kutwaliwa kwa Sheria ya Nabii Musa[as] na Mungu ataipatia kisogo nyumba ya Yakubu.

Waandishi wa Kikristo wamelinyamazia jambo hili. Labda wao

wanatafsiri nyumba mbili za Israeli kuwa na maana ya yale makundi mawili, ambayo moja liliunga mkono na jingine kuwapinga wana wa Suleimani na kusimika utawala pinzani. Lakini hii si hoja, kwa sababu bishara yazungumzia mtu mtakatifu na mambo yatakayotukia katika zama za ujaji wake. Huyu mja mtakatifu anaweza akawa ni Yesu au mtu mwingine ajaye baada ya Yesu, kwani hapajakuwepo na kiongozi mashuhuri wa kidini baina ya wakati wa Isaya na Yesu ambaye huenda angelikabili Israeli akiwa na Ujumbe muhimu. Lakini je, Yesu aliikabili Israeli na Ujumbe wowote sampuli hiyo? Na je, Israeli ilipata ushinde na fedheha kwa kuupinga Ujumbe huu? Na je, Yesu aliwakomeshea wanafunzi wake Sheria na kutangaza mahali pa Sheria ya Musa kuchukuliwa na Sheria nyingine? Naam, kuhusu jambo hili kauli ya Yesu i wazi kabisa. Yeye alisema:

> Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiza. Kwa maana, Amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka, yodi moja wala nukta moja ya torati haitaondoka, hata yote yatimie (Mat.5 :17-18).

Yesu alilimaliza suala hili si tu kwa ajili ya wakati wake, bali kwa ajili ya siku za usoni pia. Alitamka akisema:

> Walioalikwa arusini wawezaje kufunga maadamu bwana-arusi yupo pamoja nao? Muda wote walipo na bwana-arusi pamoja nao hawawezi kufunga. lakini siku zitakuja watakapoondolewa bwana arusi ndipo watakapofunga siku ile (Mk 2:19-20).

Kutokana na tangazo hili ni dhahiri kwamba, sawa na Yesu, hata baada kifo chake, Sheria ya Musa ilikuwa iendelee kuwa faradhi kwa ajili ya wanafunzi wake. Kama isingelikuwa mambo yawe hivyo, yeye angeliweza kusema kwamba siku za kufunga zilkuwa zimemalizika. Badala yake sio kwamba yeye mwenyewe alifunga tu, bali pia alitabiri kwamba wanafunzi wake wataanza kufunga baada ya yeye (kufariki). Hivyo basi, kukomesha Sheria, hakumaanishi kuitangua au ukataaji wa wazo lenyewe la wajibu thabiti wa kidini. Kwamanisha ya kwamba katika wakati wa yule Mja Mtakatifu Mwahidiwa, Sheria ya

Musa itakuja simamishwa na Sheria mpya itakuja simikwa badala yake. Kama hii tafsiri yetu sio kweli, basi ni kwa nini tuliambiwa kwamba Mungu ataipatia kisogo nyumba ya Yakubu? Je, Yesu hakutokana na nyumba ya Yakubu? Kama hakutokana nayo, basi asingekuwa mzawa wa Daudi[as]. Na kama hakuwa mzawa wa Daudi, basi asingekuwa yule Yesu wa bishara. Kwani Kristo alikuwa awe ni mzawa wa Daudi:

(d) Katika Isaya (9:6-7) tunayo maneno haya:

> Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele Mfalme wa amani. Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe, Katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; Kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo.

Bishara hii yaahidi ujaji wa mfalme atakayekuwa na majina matano au vyeo: Mstaajabiwa. (2) Mshauri. (3) Mungu Mwenye nguvu. (4) Baba wa Milele. (5) Mfalme wa Amani. Ustawi na Amani katika ufalme wake havitakuwa na mipaka; atakalia kiti cha enzi cha Daudi milele na milele na kudumisha jina lake zuri kwa hukumu na uadilifu.

Waelezaje wa Injili wanasema kwenye maelezo ya utangulizi wa mlango huu ya kuwa bishara hii yahusikana na kuzaliwa kwa Yesu. Lakini miongoni mwa alama zinazotajwa katika bishara yenyewe, hata moja haimhusu Yesu. Mathalan, je, yeye alipata kuwa mfalme? Je, yale majina yaliyoorodheshwa katika bishra — kama vile Mstaajabiwa, Mshauri, Mungu Mwenye nguvu, Baba wa Milele, Mfalme wa Amani, aliyanasibishiwa? Yeye huenda aliitwa Mstaajabiwa kwa sababu ya kule kuzaliwa kwake kwa kivyake. Lakini kuitwa hivyo kwenyewe hakuonekani kuwa kumepata kupendekezwa. Waliomkataa walikuchukulia kuzaliwa kwake kuwa uana-haranu, hivyo basi wasingelimwita Mstaajabiwa. Wafuasi wake

kwa upande mwingine, waliitilia shaka nasaba yake. Sawa na baadhi yao yeye alikuwa ni mwana wa Daudi. Tunayo maneno haya:

> Yeye ni mfalme wa Israeli; na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini. Pia wale wanyang'anyi waliosulubiwa pamoja naye walimshutumu vile vile (Mathayo, 27: 42, 44).

Yesu hakufanya maonyesho yoyote yale ya "nguvu" zake, wala hakuelezewa na yeyote yule kuwa "mwenye nguvu". Marafiki pamwe na maadui wote walimkanushia sifa hii. Mambo yasingelikuwa hivi, basi wanafunzi wake wasingelimtoroka na kukimbia. Mathayo (26:56) yatoboa ikisema:

> "Ndipo wanafunzi wote wakamwacha wakakimbia".

Je, mwenye nguvu hupatwa na hayo?

Jina la nne ni Baba wa milele; na hili nalo pia halimhusu Yesu. Kwani, kama vile tulivyokwishaonyesha, yeye alitabiri mwingine angeliyekuja baada yake.

Jina la tano ni Mfalme wa Amani, na hata hili haliwezi likamhusu Yesu. Yeye hakupata katu kuwa mfalme, kwa hiyo asingeliweza abadan kuleta amani duniani. Badala yake, yeye alibakia kuteswa na Mayahudi na hatimaye akawambwa msalabani na watu hao hao.

Bishara yaweka alama, "Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe". Yesu hakuliambulia serikali yoyote na, kwa hiyo, asingeweza asilan kuona ongezeko lake.

Alama nyingine ni, "Katika kiti cha Enzi cha Daudi na ufalme wake, kuuthibitisha, na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele", na hata hii haimhusu Yesu.

Alama hizi zamhusu Mtume Mtukufu[saw] wa Islam. Alikuwa yeye iliyembidi kubeba majukumu ya Serikali na ambaye, kinyume kabisa na matakwa yake, alijikuta akiwa mfalme. Ni kinyume cha mambo ya kwamba Yesu, ambaye kamwe hakupata kuwa mfalme, daima alijihisi kuwa mfalme (Mt. 21:4-5 na Lk. 23:1-3). Mtume

Mtukufu[saw] alikuwa mfalme; lakini hata hivyo yeye alichukia kuwa mfalme, na daima aliwaonya wafuasi wake dhidi ya kuiga desturi za akina Kaisari na Khosro.

Jina moja la Huyo Mwahidiwa ni Mstaajabiwa. Yesu yuakiri kwamba mwenye jina hili alikuwa aje baada yake. Kukuri huku twakupata kwenye ile mithali ya shamba la mizabibu (Mt. 21:33-44). Mithali yenyewe ni hii: Kulikuwa na mtu mwenye nyumba, naye alipanda shamba la mizabibu, akalizungusha ugo, akachimba shimo la shinikizo ndani yake, akajenga mnara, akapangisha wakulima, akasafiri. Halafu akawatuma watumishi wake kuvuna matunda, lakini wale wakulima wakawapiga au kuwaulia mbali au kuwavurumishia mawe wale watumishi mmoja baada ya mwingine. Akatuma watumishi zaidi, lakini nao pia wakatendewa mabaya kama wale wengine. Kisha yeye akamtuma mwanawe, lakini wale wakulima wakamuulia mbali yule mwana. Akisha kusema maneno hayo, hapo Yesu akauliza akisema:

> Basi atakapokuja yule bwana wa shamba la mizabibu, atawatendaje wale wakulima? (Mt.21:40).

Wale waliomsikia wakajibu wakisema:

> Atawaangamiza vibaya wale wabaya: na shamba la mizabibu atawapangisha wakulima wengine, watakaomlipa matunda kwa wakati wake.

Lakini Yesu akatamka tena akisema:

> Hamkupata kusoma katika maandiko, Jiwe walilolikataa waashi, hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni; neno hili limetoka kwa Bwana, nalo ni ajabu machoni petu? Kwa sababu hiyo nawaambia, ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, nao watapewa taifa lingine lenye kuzaa matunda yake. Naye aangukaye juu ya jiwe hilo atavunjika-vunjika; naye ye yote ambaye litamwangukia, litamsaga tikitiki (Mt. 21:42-44).

Yaani, baada ya mwana kuuawa, angekuwepo mwingine mtumwa na

Mwenyezi Mungu, yule ambaye angehakiki "kuwa ni jiwe la pembeni", na angeliyeonekana "wa ajabu" machoni pa Yesu na pa watu wengine wote. Huyo Mstaajabiwa, basi angelikuja baada ya mwana kuuawa. Inaweza ikawa tu Mtume[saw] wa Islam ambaye alidhihiri baada ya Yesu ambaye aliwambwa msalabani.

Jina la tatu la Yule Mwahidiwa ni Mshauri. Jina hili lahusikana vilivyo na Mtume Mtukufu[saw]. Taifa zima lilimtaka ushauri. Naye, kwa upande wake, daima akashauriana na watu wake, na akaifanya kuwa ni faradhi kwa Serikali kushauriana na raia juu ya masuala yote muhimu. Ukweli kwamba Mtume Mtukufu[saw] alikuwa mshauriani wa kupindukia upo kinagaubaga katika Kurani. Tunazo haya hizi:

> Enyi mlioamini mnaposhauriana na Mtume faraghani, basi toeni sadaka kabla ya kushauriana kwenu; hiyo ni bora kwenu na safi sana. Kama hamkupata (cha kutoa) Mwenyezi Mungu ni Msamehevu Mrehemevu (Sura Al-Mujaadila, 58:13).

Hili agizo juu ya kutoa sadaka kabla ya kushauriana, linauweka wazi huu ukweli kwamba desturi ya kushauriana na Mtume[saw] kilikuwa ni kitu cha kawaida, na kanuni ya kutoa ada kwa hiari ilikuwa imewekwa ili kupata hela za kuwasaidia maskini. Kanuni hii ilikusudiwa wale walioimudu. Mtume Mtukufu[saw] ikawa ni mwenye kutafutiwa sana fursa ya kushauriana naye hivi kwamba ilionekana yawezekana bali hata yahitajika kumlipisha mtafuta fursa ada ifaayo. Ada hiyo ilistahili kwani ilibidi wakati wa Mtume Mtukufu[saw] kutumiwa kwa manufaa ya wanadamu wote; endapo watu binafsi waliutaka wakati wake, ilikuwa halali kwamba walipe kitu kidogo katika hazina ya taifa. Hivyo basi, kushauriana na Mtume[saw] ikawa ya kawaida. Yeye Mtume[saw] ndiye anayestahili zaidi ya yeyote yule kuitwa Mshauri. Mtume[saw] pia alifaridhisha desturi ya mashauriano (shura) kuwa ni sharti muhimu la utawala mzuri.

Na yasema Kurani:

> "Na sheria yao ni kushauriana wao kwa wao" (Sura Ash-Shuuraa, 42:39).

Hatua za kawaida na za kitawala zisichukuliwe hadi wawakilishi wa umma watakapokuwa wameshauriwa. Kufuatana na amri hii, Mtume Mtukufu[saw] akayafanya mashauriano kuwa ni jukumu muhimu la Khalifa, au kiongozi mchaguliwa wa Waislamu. Yuaripotiwa kuwa aliyesema kwamba, "Hakuna Ukhalifa bila ya mashauriano (Shura)" (Izalatul-Khifaa 'an Khilafatil-Khulafaa). Nchi inayotawaliwa bila ya mashauriano isingelikuwa ya Kiislamu. Sasa ukilinganisha na haya, ni lipi alilofanya Yesu kama mshauri? Yeye hakufanya mashauriano kwa kiwango chochote kikubwa. Wala hakuhimiza kuwa ni jambo la kidesturi. Hivyo basi, Mtume Mtukufu[saw] ndiye aliyekuwa Mshauri wa ile bishara wala sio Yesu.

Jina la nne katika bishara ile ni Mungu mwenye nguvu. Agano la Kale ladokezea mfanano baina ya Mungu na Musa[as]. Ndiposa katika kitabu cha Kutoka (7:1) tunayo maneno haya:

> "Bwana akamwambia Musa, Angalia, nimekufanya wewe kuwa kama Mungu kwa Farao".

Na tena katika Kutoka (4:16):

> "Nawe utakuwa mfano wa Mungu kwake (Haruni)".

Katika Biblia Yesu yuaitwa mwana wa Mungu na Musa yuaitwa "mfano wa Mungu". Hivyo basi, wakati wowote mwanadamu anapozungumziwa kuwa "mfano wa Mungu", itamaanisha Musa au mwingine afananaye na Musa. Nabii Musa tumeonyesha hapo juu, alitabiri juu ya Nabii mwenye kufanana naye (Kum. 18:18), na huyo si mwingine minghairi ya Mtume Mtukufu[saw] wa Islam, akiwa yeye ndiye mwenye kuafiki maelezo ya ile bishara. Hivyo, ni Mtume[saw] wa Islam awezaye kihalali kabisa kuitwa Mungu au, sawa zaidi, Dhihirisho la Mungu. Tunayo magusio yahusikanayo na jambo hili katika Kurani. Kwenye vita vya Badr, Mtume[saw] alitwaa fumba la mchanga na kulivurumishia maadui. Hili likaashiria kuzuka kwa tufani ya changarawe iliyowapigisha butwaa maadui na kusababisha ushinde wao. Kuhusu jambo hili Mweneyzi Mungu Yuasema na Mtume[saw] Akimwambia:

> "Na hukutupa wewe ulipotupa, walakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyetupa" (Sura Al-Anfaal, 8:18).

Vivyo hivyo, wakati wa kusilimu, waaminio wapya walikuwa wakifanya baiati ya utiifu kwake Mtume[saw]. Akigusia ukweli huu Mwenyezi Mungu Yuasema hivi katika Kurani:

"Bila shaka wanaofungamana nawe kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu (Sura Al-Fat'h, 48:11).

Mtume huhudumu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hivyo, jina Mungu la mle bisharani lamhusu Mtume[saw] badala ya yeyote mwingine; pia hii sifa ya "mwenye nguvu". Kwani ilikuwa ni yeye aliyeweza kuwakunjisha mkia maadui zake katika uhai wake na kuvunjilia mbali upinzani wote.

Jina la tano katika bishara ni Baba wa milele. Hili nalo pia lamhusu Mtume[saw] wala halimhusu mwingine yeyote. Alikuwa ni yeye aliyedai kinagaubaga hali ya kidaima dawamu ya mafundisho yake. Kwani yeye alitabiri ujaji wa mara ya pili wa Kristo, lakini, ujaji wa mara ya pili wa Yesu ulikuwa uwe ni katika dhati ya mmoja wa wafuasi wa Mtume[saw] mwenyewe, wala si wa mwingine ambaye ujaji wake ungelivunjia mbali himaya yake ya kiroho, Akigusia jambo hili Mwenyezi Mungu katamka ndani ya Kurani akisema:

> Na hatukukutuma ila kwa watu wote uwe Mtoaji wa habari njema na Mwonyaji; lakini watu wengi hawajui. Na wanasema: Lini (itatimia) ahadi hii ikiwa mnasema kweli? Sema, Mmepewa miadi ya siku ambayo hamtaiahirisha saa wala hamtaitanguliza" (Sura Saba', 34:29-31).

Maneno haya "watu wote" hapa yanaashiria hali ya kiulimwengu mzima na hali ya kidaima dawamu ya Ujumbe wa Islam. Hauna budi kuhubiriwa mataifa yote katika zama zote. Makafiri wanamkejeli Mtume[saw] juu ya siku inayoahidiwa hapa na wanauliza wakisema itakuwa lini; yaani, ni lini ile hali ya Islam ya kiulimwengu mzima na kidaima dawamu itakapooneshwa humu duniani? Katika kujibu,

Mwemeyzi Mungu yuasema siku yenyewe itafika kama ilivyowekwa.

Siku hiyo halikadhalika inagusiwa katika Sura As-Sajdah, 32:6 kwa maneno haya:

> Hutengeneza jambo toka mbinguni mpaka ardhini; kisha linapanda Kwake siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu mnayotumia katika kuhesabu.

Jambo lililotengenezwa ndiyo Islam. Baada ya muda athari yake itaanza kupungua. Katika muda wa miaka elfu itapanda tena juu mbinguni. Ule msaada maalumu wa kimbinguni iliyoupata hapo mwanzoni utatoweka na hali yake itakuwa chini ya nira ya nguvu za kimaumbile humu duniani. Kutokana na Kurani na pia Hadithi yaonekana kwamba kupanuka kwa Islam kulikuwa kuendelee kwa miaka mia tatu ya awali, ambapo nyumaye ulikuwa uanze wakati wa kudhoofika kwake. Kudhoofika kwenyewe kulikuwa kuendelee kwa muda wa miaka elfu moja. Zinaposomwa pamoja sehemu zote mbili — Sura As-Saba' 34:29-31 na Sura As-Sajda 32:6 — inakuwa wazi kabisa kwamba kwa muda mrefu watu wataendelea kutosadiki hali ya ujumbe wa Islam ya kiulimwengu mzima na ile ya kidaima dawamu, baada ya kupita miaka elfu moja na mia tatu utajitokeza ukweli na hali vitakavyoifanya dunia kutokuwa na tashwishi kabisa juu ya jambo hili. Sehemu hizi za Kurani zisomwapo pamoja zadokezea ujaji wa mara ya pili wa yule Masihi — aliyeahidiwa na vyote viwili, Kurani na Hadithi — na zatukumbusha kwamba huo ujaji wa mara ya pili utatimia katika dhati ya mfuasi wa Mtume[saw] wa Islam. Kwa kuwa ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa ungekuwa pia umetabiriwa na Manabii wengine, kuinuka kwake toka miongoni mwa wafuasi wa Mtume Mtukufu[saw] kungethibitisha barabara ya kwamba miliki ya kiroho ya Mtume wa Islam ilikuwa ya milele, kwamba sasa palikuwa pasitokee tena Waalimu wa kimbinguni isipokuwa kutoka miongoni mwa wafuasi wake. Sheria na Mafundisho ya Mtume Mtukufu[saw] yatabakia bila kung'atuliwa na Sheria au Mafundisho yoyote yale mengine. Isitoshe, katika wakati wa Masihi Aliyeahidiwa itakuwepo shime

motomoto itakayotiliwa wajibu wa kuhubiri, ikileta hatimaye ueneaji wa Islam duniani kote. Jambo hili litakapotendeka, basi ile hali ya Islam ya kiulimwengu mzima na ya kidaima dawamu itahakiki kinagaubaga. Hivyo, yule Baba wa milele wa ile bishara ya Isaya ni Nabii[saw] wa Islam wala si mwinginewe.

Jina la sita katika bishara ni Mwanamfalme wa Amani. Lakabu ya Mwanamfalme pia yamaanisha mfalme; Mwanamfalme ni mfalme, kwa hakika. Hivyo, tunaweza kuyaelewa maneno yenyewe kuwa na maana ya Mfalme wa Amani, na ikiwa hivyo yanaweza yakahusikana tu na Mtume wa Islam. Dini aliyoisimika ni Islam, ambayo kimsemo yamaanisha "amani".

Hatujui ni kwa maana ya kivipi anaweza Yesu akachukuliwa kama Mwanamfalme wa Amani. Basi, Mwanamfalme wa Amani angekuwa mtu mwenye amani katika majaaliwa yake na mwenye kuweza kuwapatia amani watu wengine. Hamna dalili ya jambo hili katika upande wa Yesu. Wala yeye hakupata kuwa na uwezo wa kuwapatia maadui zake msamaha. Naam, ni kweli yeye alihubiri msamaha na kuwafundisha wafuasi wake kugeuza shavu la pili. Lakini kati ya kusema na kufanya ipo tofauti kubwa, na chenye thamani kwa hakika ni kufanya, wala sio kusema. Kuhusu huku kufanya kwa vitendo, tunazo dalili katika Mtume Mtukufu[saw] peke yake. Ni kikatili jinsi gani alivyotendewa na watu wake. Hapana dhuluma ambazo hazikufanywa dhidi yake na wafuasi wake. Wengi miongoni mwa jamaa zake wa karibu na marafiki zake waliuawa kikatili. Mtume mwenyewe binafsi alikuwa shahidi kwa kutendewa ukatili huu. Yeye ndiye aliyekuwa lengo lao katika visa mbalimbali na katika njia nyingi mbalimbali. Ilimbidi kuacha mji wake na kutafuta salama mahali penginepo, kama vile walivyokuwa wamefanya marafiki zake na wafuasi wake. Takriban wote iliwalazimu kuonja machungu ya kutenganishwa na ndugu zao wapenzi. Wengine walichanwa vipande huku wakifungiwa ngamia wawili waliotimuliwa mbio mmoja akielekezwa kulia na mwingine kushoto. Akina mama waliuawa kwa kukitwa mikuki kwenye sehemu zao za siri. Watumwa waliomwamini

Mtume Mtukufu[saw] walivuliwa nguo na kubururwa juu ya mchanga wenye kuunguza na juu ya changarawe. Walitaabishwa wakitakiwa waitangue imani yao. Miili ya Waislamu waliouwa vitani ilikatwakatwa vipande vipande. Kwa neno zima, Waislamu wa hapo awali — wanaume kwa wanawake, wazee kwa vijana, wafu na wazima — iliwalazimu kutaabika vikali na kwa njia mbalimbali. Lakini hatimaye Mwenyezi Mungu akawashindisha. Mtume Mtukufu[saw] akiandamana na wafuasi elfu kumi, akaingia mjini Makka kama mshindi. Yule adui katili alijisalimisha pake miguuni, akiichukulia adhabu yoyote kuwa ni halali kwa ule uovu aliokuwa ameutenda. Lakini hata hivyo aliyowaambia Mtume Mtukufu[saw] yalikuwa ni haya tu, "Hivi leo, nawasameheni nyote" (Hashim). Mtume Mtukufu[saw] alikuwa na uwezo wa kuyalipizia kisasi maovu yote aliyotendewa yeye na wafuasi wake. Lakini yeye akapendelea kusamehe, na kujizuia hata kuwaumiza hisia zao za moyoni. Waislamu walipokuwa wakiujongelea mji wa Makka jenarali wao mmoja alisikika akisema ya kwamba siku hii wao tungewaonyesha watu wa Makka cha mtema kuni (Bukhari). Mtume Mtukufu[saw] alimvulia mbali kilemba yule jenerali, huku akisema; matamshi kama hayo yalikuwa na shabaha ya kuwaumiza watu wa Makka. Sasa je, tunapata mambo sampuli hii katika maisha ya Yesu? Au katika maisha ya wanafunzi wake? Au katika historia nzima ya Kikristo? Hapana shaka ya kwamba hata Wakristo nao pia walionjeshwa machungu mengi na taabu, na walikuwa ni watu wanyonge. Lakini zama ziliwadia wao walipojaaliwa uwezo. Je, waliwatendeaje maadui zao? Je, historia haikufanywa nyekundu kwa damu za maadui zao? Basi anawezaje Yesu kuitwa Mwana-Mfalme wa Amani? Yeye mwenyewe hakuwapatia wengine amani. Wafuasi wake walikuwa na uwezo wa kutoa amani, lakini hawakufanya hivyo. Badala yake wao wakapeana kifo na maangamizo. Mtume[saw] wa Islam alikuwa na uwezo wa kuwaadhibu maadui zake kwa maovu tena ya kikatili mno zaidi ya yale aliyofanyiwa Yesu na Mayahudi. Lakini bado yeye akapendelea kusamehe. Kwa Hiyo Mtume[saw] ndiye aliyekuwa yule Mwana-Mfalme

wa Amani wa ile bishara ya Isaya.

Alama ya saba ya yule Mwahidiwa sawa na Isaya (9 :1) ni kwamba:

> "Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe".

Ishara hii ni wazi yamhusu Nabii[saw] wa Islam na sio Yesu. Yesu hakupata uwezo wowote wa kisiasa. Mtume Mtukufu[saw] alipata uwezo huo wa kisiasa, na wafuasi wake wakawa watawala wa dunia nzima ilivyokuwa ikijulikana wakati ule; nao wakatawala kwa namna nzuri isiyoweza kupatikana mfano wake.

Alama ya nane ilikuwa ya kwamba:

> "Katika kiti cha enzi cha Daudi, na ufalme wake, kuuthibitisha na kuutegeneza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele (Isaya 9:7).

Je, Yesu alipata wakati wowote kukalia kiti cha enzi cha Daudi? Inaweza ikawa alifanya hivyo miaka mia tatu nyumaye, pale Mfalme wa Kirumi alipogeuka kuwa Mkristo. Lakini bishara yenyewe yatabiri kwamba kiti hicho cha enzi ni cha kumilikiwa milele. Umilikaji wa Yesu ulidumu kwa takriban miaka mia tatu ambapo ulipokomea kwa ujaji wa Islam, na sasa kwa muda wa miaka elfu moja na mia tatu, nchi ya Palestina — kiti cha enzi cha Daudi — imekuwa mikononi mwa Waislamu. Sasa ni muda upi unaochukuana zaidi na maana ya neno "milele" lililomo bisharani — miaka mia tatu au ni huu muda wa miaka elfu moja na mia tatu? Hapana shaka kabisa, leo hii nchi ya Kikristo inaishikilia Palestina. Lakini ni jambo la maana kulingana na msimamo wetu ya kuwa hao Waingereza wako huko sio kama watawala bali kama wawakilishi. Ukatizwaji wa muda wa umilikaji wa Waislamu hauwezi ukatangua bishara inayozungumziwa.

Utawala aliousimika Mtume Mtukufu[saw] wa Islam humu duniani kwa njia ya wafuasi wake ulijaa tele hukumu na haki, tukirudia maneno ya ile bishara. Tunao ushahidi wa kihistoria wa kuthibitishia ukweli huu. Wakati wa Hadhrat Umar[ra], Khalifa wa Pili wa Islam, jeshi la

Kiislamu ilibidi liitoke kwa muda nchi ya Kikristo kwa kusukumwa kwa nguvu na majeshi ya Kirumi. Kabla hawajaondoka, waliwakusanya wakazi wa eneo lile na kuwafahamisha kwamba hawakuweza tena kuyalinda maisha na mali zao; na hivyo basi walikuwa wanawarudishia zile pesa zao walizokuwa wamezikusanya kutoka kwao kama kodi. Wakazi wa Kikristo wa mji wa Yerusalemu wakavutiwa na kitendo hiki cha hukumu nzuri na haki hivi kwamba wakatoka pamoja na lile jeshi la Waislamu, huku wakilia na kuombea kurejea kwa haraka kwa Waislamu (The Caliphate; Futuh-ul-Buldan). Basi ni ajabu gani kwamba Isaya yuatabiri juu ya Huyo Mwahidiwa akisema:

> Katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha kuutegemeza kwa hukumu na haki (Isaya, 9:7).

(e) Katika Isaya (19:21-25) tunayo maneno haya:

> Na Bwana atajulikana na Misri, na Wamisri watamjua Bwana katika siku hiyo; maana watamtumikia kwa dhabihu na matoleo, nao watamwekea Bwana nadhiri, na kuzitekeleza. Naye Bwana atapiga Misri, akipiga na kuponya; nao wakirudi kwa Bwana, atakubali maombi yao na kuwaponya. Katika siku hiyo itakuwako njia kuu itokayo Misri na kufika hata Ashuru; Mwashuri atafika Misri, na Mmisri atafika Ashuru, na Wamisri wataabudu pamoja na Waashuri. Katika siku hiyo Israeli atakuwa wa tatu pamoja na Misri na Ashuru, watakuwa baraka kati ya dunia; kwa kuwa Bwana wa majeshi amewabariki, akisema, Wabarikiwe watu wangu wa Misri; na wewe Ashuru, kazi ya mikono yangu; na wewe Israeli urithi wangu.

Bishara hii yazungumzia wakati ambapo Mungu Atajidhihirisha kwa watu wa Misri ambao watakuja kumjua na kumtolea dhabihu na matoleo; Misri na Siria zingeungana, wenyeji wa nchi moja watatembelea ile nyingine; na zote mbili zitajumuika katika ibada ya namna moja.

Bishara hii pia ilitimia katika dhati ya Mtume Mtukufu[saw] wa Islam.

Wenyeji wa Misri kweli walipata kuwa Wakristo, lakini kwa muda mfupi tu wa historia yao. Sasa kwa muda wa miaka elfu moja na mia tatu Wamisri wamekuwa ni Waislamu. Katika kauli ya Isaya, Mungu Yuasema na Wamisri akiwaambia: "Wabarikiwe watu wangu wa Misri'. Wamisri na waseme wenyewe. Je, utiifu wao ni kwa Yesu au kwa Mtume[saw] wa Islam?

Kisha tunayo maneno haya:

"Na wewe Ashuru, kazi ya mikono yangu".

Vivyo hivyo, Waasyria na waseme wenyewe. Je, wanajinasibisha na Yesu au Mtume[saw] wa Islam?

Na tunayo maneno haya:

"Na wewe Israeli urithi wangu".

Nani ana madaraka juu ya Palestina, nchi ya Israeli?

Hapana shaka, chini ya athari za nguvu za Ulaya na Marekani Mayahudi wanaingia Palestina. Lakini Mayahudi sio wafuasi wa Yesu. Na kwa vyovyote vile Waislamu bado ndio walio wengi zaidi katika nchi hii ya Israeli, na Wakristo, bado ndio wachache. Endapo Mayahudi wataishikilia Palestina, huo utakuwa tu ukatikaji wa muda wa umilikaji wa Waislamu, na iwe ni Mayahudi ama Waislamu waishkiliao nchi hiyo, Yesu hawezi akahusikana na hii bishara inayozungumziwa.

Bishara yazungumzia "njia kuu itokayo Misri na kufika hata Ashuru", yaani, dalili ya mawasiliano kemkemu baina ya nchi hizi mbili. Bishara yatoa picha ya wananchi wa nchi mbili hizi wakitembeleana na kusuhubiana na kujumuika pamoja katika ibada ya namna moja. Ni nani aliyeyaleta haya yote; je, ni Yesu? Wakristo wakati mmoja walizimiliki nchi hizi zote mbili, Misri na Siria, na wenyeji wao walio wengi zaidi wa nchi hizi, wakati mmoja, walikuwa ni Wakristo. Lakini katika wakati huo, je, zilitokea zile hali inazozizungumzia bishara hii? Kulingana na bishara, hizi nchi mbili zilikuwa zijenge mawasiliano ya kidugu kiasi hiki kwamba ziwe kama nchi moja zikiwa na lugha moja

na dini moja. Mawasiliano baina ya nchi mbili zinazopakana ni jambo la kawaida ua la kimaumbile. Lakini mawasiliano baina ya Misri na Siria yalitakiwa yawe tofauti; yalikuwa yaziunganishe nchi mbili kuwa moja, na kuwapatia utaifa mmoja. Fungamano sampuli hii baina ya hizi nchi mbili halikupata kutokea zama za utawala wa Kikristo. Chini ya utawala wa Warumi, Misri na Siria yalikuwa maeneo ya himaya moja, lakini njia za utawala katika nchi hizi ziliendelea kuwa tofauti. Misri ilikuwa ni ufalme nusu huru, na Ashuru ilikuwa chini ya Gavana wa Kirumi. Bali hata Kanisa la Misri nalo pia lilitofautiana na Kanisa na Ashuru. Misri chini ya athari za Kanisa la Elexandria, Ukristo ulikuwa umepata sura tofauti na ile ya Kanisa na Ki-Palestina au lile la Kisiria. Wamisri waliabudu katika lugha yao, Kikopti, na Wasiria nao katika mseto wa lugha ya Kiyahudi na Kiyunani. Chini ya Islam hali ikawa tofauti kabisa. Kwa karne nyingi Misri na Siria zilikuwa chini ya utawala mmoja. Zote zikaanza kuongea, bali bado zaendelea kuongea lugha moja. Zote zilichagua na bado zinazingatia namna moja ya ibada. Zote zilijenga mawazo mamoja. Wataalamu wa Kisiria walikwenda Misri na wakaheshimiwa kama wanazuoni wa Kimisri. Wataalamu wa Kimisri wakaenda Siria na wakaheshimiwa kama wanazuoni wa Kisiria. Hata hivi leo, ambapo ulimwengu wa Kiislamu chini ya harakati za kidiplomasia ya Ulaya umetapanyika, Jumuiya ya Waarabu (the Arab League) ni mshikamano wa Wamisri, Wasiria na Wapalestina. Nchi hizi tatu zaonekana kuwa zinashirikiana na kujivunia utaifa mmoja. Hivyo, bishara hii ya Isaya ilitimia katika dhati na kwa njia ya Mtume Mtukufu[saw] wa Islam na wafuasi wake. Kuinasibishia Yesu na Kanisa la Kikristo ndio uzushi mkubwa.

(f) Katika Isaya (62:·2) tunayo maneno haya:

"Nawe utaitwa jina jipya, litakalotajwa na kinywa cha Bwana".

Ni dhahiri kabisa, bishara yatabiri mwendeleo mpya, wenye jina jipya na jina hilo jipya halitakuwa ni jina ulilojichagulia mwendeleo huo, bali litakuwa ni jina ulilolipendekezewa na Mungu katika neno Lake lililofunuliwa. Waelezaji wa Biblia bishara hii wanainasibishia Kanisa

la Kikristo, bila kujali vile inavyojulikana kwamba majina Mkristo na Ukristo, au yale majina mengi ambayo kwayo madhehebu ya Kikristo yanajulikana, kamwe hayakupendekezwa na Mungu katika neno Lake lililofunuliwa bali ni ya watu kujichagulia. Kuna jamii moja tu ya watu katika dunia nzima ambao wana jina walilolipewa na Mwenyezi Mungu, na hao ni Waislamu. Na ndiposa Kurani ikasema:

> "Yeye Aliwaiteni Waislamu tangu zamani na katika (Kurani) hii pia" (Sura Al-Hajj, 22:79).

Haya ni marejeo wazi ya ile bishara ya Isaya. Aya hii ya Kurani yaonekana kama inayosema, "Tulitabiri kuwa jina lenu halitakuwa jina la kujichagulia nyinyi wenyewe. Hivyo basi, sawa na utabiri huo, hivi leo, Twawapeni jina — Waislamu". Jina hili limetokana na ***salam*** ambalo lamaanisha Amani, na hii yaafikiana na lakabu moja ya Yule Nabii Mwahidiwa — "Mwana-Mfalme wa Amani". Ilikuwa ni bishara ya kustaajabisha. Na ndivyo unavyostaajabisha huu ukweli kwamba ni Waislamu peke yao wanaodai wamejipatia jina lao kutoka kwa Mwenyezi Mungu katika neno Lake lililofunuliwa. Nabii Isaya alitabiri kwamba angekuja Nabii ambaye jina la wafuasi wake lingechaguliwa na Mungu na kutangazwa katika Kitabu Chake kilichofunuliwa. Mtume Mtukufu[saw] wa Islam ndiye Nabii huyo; wafuasi wake wameitwa Waislamu na Mwenyezi Mungu, na dini yake Islam.

BISHARA ZA DANIELI

Kulingana na kitabu cha Danieli, mlango wa 2, Nebukadneza, Mfalme wa Babeli aliota ndoto, aliyoisahaulia mbali mara. Hapo akawatolea mwito wajuzi wa zama zake wamwambie ndoto ile na tafsiri yake pia. Hapana mmoja wao aliyeweza kufanya hivyo. Danieli akamwomba Mwenyezi Mungu na akaifunuliwa ile ndoto na tafsiri yake. Ndoto yenyewe ilikuwa kama ifuatavyo:

> Wewe, Ee Mfalme, uliona, na tazama, sanamu kubwa sana. Sanamu hii, iliyokuwa kubwa sana, na mwangaza wake mwingi sana, ilisimama mbele yako; na umbo lake lilikuwa lenye kutisha. Na sanamu hii, kichwa chake kilikuwa ni cha dhahabu

safi; kifua chake na mikono yake ni ya fedha; tumbo lake na viuno vyake ni vya shaba; miguu yake ni ya chuma; na nyayo za miguu yake nusu ya chuma na nusu ya udongo. Nawe ukatazama hata jiwe likachongwa bila ya mkono, nalo jiwe hilo likaipiga sanamu miguu yake, iliyokuwa ya chuma na udongo likaivunja vipande vipande. Ndipo kile chuma, na ule udongo, na ile shaba, na ile fedha, na ile dhahabu, vilivunjwa vipande vipande pamoja, vikawa kama makapi ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari; upepo ukavipeperusha, hata pasionekane mahali pake; na lile jiwe lililoipiga hiyo sanamu likawa mlima mkubwa, likaijaza dunia yote. (Danieli 2: 31-35).

Tafsiri Danieli aliyoifanyia ndoto ile ilikuwa hii ifuatayo:

Wewe, Ee mfalme, u mfalme wa wafalme, na Mungu wa mbinguni amekupa ufalme, na uwezo, na nguvu, na utukufu; na kila mahali wakaapo wanadamu, wanyama wa kondeni na ndege wa angani amewatia mkononi mwako, naye amekumilikisha juu ya hao wote; wewe u kichwa kile cha dhahabu. Na baada ya zamani zako utainuka ufalme mwingine, mdogo kuliko wewe; na ufalme mwingine wa tatu wa shaba, utakaoitawala dunia yote. Na ufalme wa nne utakuwa na nguvu mfano wa chuma; kwa maana chuma huvunja vitu vyote na kuvishinda; na kama chuma kisetavyo vitu hivi vyote, ndivyo utakavyovunjavunja na kuseta. Na kama vile ulivyoziona hizo nyayo za miguu na vidole vyake, kuwa nusu udongo wa mfinyanzi, na nusu chuma, ufalme ule utakuwa ufalme uliogawanyika; lakini ndani yake zitakuwako nguvu za chuma, kama vile ulivyoona kile chuma kimechanganyika na udongo wa matope. Na kama vidole vya zile nyayo vilikuwa nusu chuma na nusu udongo, kadhalika ufalme ule utakuwa nusu yake una nguvu, na nusu yake umevunjika. Na kama vile ulivyokiona kile chuma kimechanganyika na udongo wa matope, watajichanganya nafsi zao kwa mbegu za wanadamu; lakini hawatashikamana, kama vile chuma kisivyoshikamana na udongo. Na katika siku za

> wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele. Na kama vile ulivyoona ya kuwa jiwe lilichongwa mlimani bila kazi ya mikono, na ya kuwa lilivunjavunja kile chuma, na ile shaba, na ule udongo, na ile fedha, na ile dhahabu; basi Mungu aliye mkuu anamjulisha mfalme mambo yatakayokuva baadaye; na ndoto hii ni ya hakika, na tafsiri yake ni thabiti (Danieli 2:37-45).

Katika tafsiri ya Nabii Danieli[as] kichwa cha dhahabu ndiye mfalme wa Babeli; kifua cha fedha na mikono, falme za Uajemi na Midiani zilizoibuka baada ya ufalme wa Babeli, viuno vya shaba vyawakilisha ufalme wa Kigiriki chini ya Alexanda, uliopata kubobea baada ya ule wa Uajemi na Midiani; na miguu ya chuma yawakilisha Ufalme wa Kirumi. Kuhusu huu ufalme wa mwisho, ndoto yasema:

> "Miguu yake (yaani miguu ya ile sanamu) nusu ya chuma na nusu ya udongo" (Danieli 2:33).

Maelezo haya yanaashiria huu ukweli kwamba ufalme wa Kirumi utazienea sehemu za Ulaya na za bara la Asia. Miguu ya chuma yaonesha sehemu ya Ulaya ya Ufalme wa Kirumi na kuashiria nguvu ya utaifa mmoja na dini moja. Lakini miguu yenyewe, isemavyo ndoto, ilikuwa nusu ya chuma na nusu ya udongo. Hii yamaanisha kwamba utawala huo wa Kizungu ulikuwa uzitiishe sehemu za bara la Asia na hivyo basi kuwa ni dola la kifalme. Madola ya kifalme hutawala maeneo makubwa makubwa na chungu nzima ya rasilimali, lakini huwa na unyonge wa kiasili utokanao na utovu wa mshikamano miongoni mwa watu wao. Ndoto hii ni dhahiri yamaanisha kwamba katika miaka ya aheri Himaya ya Kirumi ingeanza kufifia kwa sababu ya huu utovu wa mshikamano. Lakini hata hivyo, ndoto yaendelea kusema mambo muhimu:

> Nawe ukatazama hata jiwe lilakchongwa bila kazi ya mkono, nalo jiwe hilo likaipiga sanamu miguu yake, iliyokuwa ya chuma

> na udongo, likaivunja vipande vipande. Ndipo kile chuma, na ule udongo, na ile shaba, na ile fedha, na ile dhahabu vilivunjwa vipande vipande pamoja, vikawa kama makapi ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari; upepo ukavipeperusha, hata pasionekane mahali pake; na lile jiwe lililoipiga hiyo sanamu likawa mlima mkubwa, likaijaza dunia yote (Danieli 2: 34-35).

Hapa tunao utabiri wa ujaji wa Islam. Islam ya awali kwanza kabisa ilikwaruzana na Urumi kisha na Iran (Uajemi). Ilipokwaruzana na Urumi, wakati huo Urumi ilikuwa imeushinda Dola la Alexandria la Ugiriki na sasa ilikuwa imezidi kuwa na nguvu kuliko hapo mwanzo; na walipokwaruzana na Iran, wakati huo nchi ya Iran ilikuwa imefikisha utawala wake hadi Babeli. Kukwaruzana kwao kulipoleta matokeo ya kuangamia kwa himaya zote mbili za Urumi na Iran, basi hapo ndipo kile chuma, na ule udongo, na ile shaba, na ile fedha, na ile dhahabu vilipovunjika vipande vipande vyote pamoja, vikawa kama makapi ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari. Ule mfuatano wa matukio katika ile ndoto na ule uaguzi wake na Danieli haviachi tashwishi yoyote juu ya maana zake.

Kila mtu yuajua kwamba Babeli ilitwaliwa na Iran na Midiani, na himaya za Iran na Midiani zikavunjiliwa mbali na himaya ya Alexanda, na himaya ya Alexanda mahali pake pakachukuliwa na ile ya Urumi ambayo kutoka makao yake makuu ya Mashariki mjini Konstantina ilisimika msingi wa himaya ya Kizungu-Kiasia yenye nguvu. Hii himaya ya Kirumi ya Kiasia ilishindwa na kuangamizwa na Mtume Mtukufu[saw] na masahaba wake. Safari moja iliporipotiwa kwamba majeshi ya Kirumi yalipanga kuwahujumu Waislamu, Mtume Mtukufu[saw] aliongoza yeye mwenyewe jeshi la kujihami hadi kwenye mpaka wa nchi ya Siria. Lakini safari hiyo hapakutokea mapigano. Lakini hata hivyo mapigano madogo ya hapa na pale pamoja na uvamizi vikaendelea hadi vilipoanza vita vya kawaida wakati wa Hadhrat Abu Bakr[ra] yaliyosababisha kutiwa komesha na kuvunjiliwa mbali kwa Himaya ya Kirumi wakati wa Hadhrat Umar[ra], Khalifa wa Pili, ambapo Himaya ya Iran nayo pia ilishindwa na majeshi ya

Waislamu. Hivyo basi, himaya hizi zilizokuwa wakati mmoja madola yenye nguvu yakafifia na kuwa vijinchi na vijisirikali koko.

Tunayo magusio ya hili "jiwe" la bishara ya Danieli katika Isaya na Mathayo. Katika Isaya 8:14 twasoma maneno haya kumhusu Huyo Mtakatifu:

> Naye atakuwa ni mahali patakatifu; bali ni jiwe la kujikwaza na mwamba wa kujikwaa kwa nyumba za Israeli zote mbili, na mtego na tanzi kwa wenyeji wa Yerusalemu.

Na katika Isaya 8:15 tunayo maneno haya:

> Na wengi watajikwaa juu yake, na kuanguka, na kuvunjika, na kunaswa na kukamatwa.

Na kutoka Injili ya Mathayo 21, yaonekana kuwa Yule Mwahidiwa — lile jiwe la ile bishara — si Yesu, bali mwingine anayekuja baada ya Yesu, na katika Mathayo 21:44 tunayo maelezo safi ya jiwe lenyewe:

> Naye aangukaye juu ya jiwe hilo atavunjika-vunjika; na ye yote ambaye litamwangukia, litamsaga tikitiki.

Vivyo hivyo katika Zaburi 118:22 tunayo maneno haya:

> "Jiwe walilolikataa waashi limekuwa jiwe kuu la pembeni".

Kuhusu jambo hili yako pia magusio katika Mathayo (21:42):

> Yesu akawaambia, Jiwe walilolikataa waashi, hilo limekuwa Jiwe kuu la pembeni; neno hili limetoka kwa Bwana, nalo ni ajabu machoni petu.

Kama vile tulivyoona, Yesu mwenyewe yuakanusha kuhusikana kwake na bishara hii yenye kumhusu anayekuja baada ya mwana kuuawa. Wakristo leo hii kwa shauku kubwa wanainasibishia Kanisa lao. Lakini jitihada hii haitafua dafu. Sawa na Danieli, viuno vya ile sanamu vilikuwa shaba, miguu (yaani, ufalme wa Kirumi) vilikuwa vya chuma na udongo; jiwe likaipiga sanamu miguu yake. Ndio kusema Islam ya hapo mwanzo ilikuwa ipigane na maeneo ya

mipakani ya ile sehemu ya Ki-Asia ya himaya ya Kirumi na kuivunjilia mbali vipande vipande. Himaya ya Kirumi ndiyo iliyokuwa kielelezo cha kidunia cha Kanisa la Kikristo. Hivyo basi, lile jiwe la mle bisharani lilikuwa lipigane na Kanisa. Jiwe lisingeliweza kuwa eti ndilo Kanisa kwani Kanisa lisingelipigana na Kanisa. Wala jiwe hilo lisingeliweza kuwa ni Yesu. Kwani Yesu alikuja miaka mingi kabla ya ule utawala wa Mashariki wa himaya ya Kirumi. Yeyote yule aliyevunjilia mbali Himaya ya Kirumi alitimiza bishara hii. Hivyo basi, bishara hii yamhusu Mtume Mtukufu[saw] wa Islam na wafuasi wake, wala si mwinginewe.

Bishara yaendelea kutoboa ikisema:

> Na lile jiwe lililoipiga hiyo sanamu likawa mlima mkubwa, likaijaza dunia yote (Danieli 2: 35).

Hivi ndivyo ilivyotendeka kwa hakika. Mtume Mtukufu[saw] na kundi la wafuasi wake walimshinda Kaisari (wa Urumi) na Khosro (wa Iran), na Waislamu wakawa watawala wa dunia nzima ilivyojulikana wakati ule. Ama kusema kweli, jiwe lilikuwa mlima mkubwa kwa hakika; kwa miaka elfu moja kuyaelekeza mambo ya dunia kukabakia mikononi mwa Waislamu.

BISHARA KATIKA AGANO JIPYA

Sasa twazigeukia bishara kumhusu Mtume Mtukufu[saw] wa Islam ambazo zimerekodiwa ndani ya Agano Jipya. Katika Mathayo (21:33-46) twasoma maneno haya:

> Sikilizeni mfano mwingine. Kulikuwa na mtu mwenye nyumba, naye alipanda shamba la mizabibu, akalizungusha ugo, akachimba shimo la shinikizo ndani yake, akajenga mnara, akapangisha wakulima, akasafiri. Wakati wa matunda ulipokuwa karibu, akawatuma watumwa wake kwa wale wakulima, wapokee matunda yake. Wale wakulima wakawakamata watumwa wake, huyu wakampiga, na huyu wakamwua, na huyu wakampiga kwa mawe. Akawatuma tena watumwa wengine

> wengi kuliko wa kwanza, wakawatenda vile vile. Mwishowe akamtuma mwanawe kwao, akisema, Watamstahi mwanangu. Lakini wale wakulima walipomwona yule mwana, wakasemezana wao kwa wao, Huyu ni mrithi; haya na tumwue, tuutwae urithi wake. Wakamkamata, wakamtupa nje ya shamba la mizabibu, wakamwua. Basi atakapokuja yule bwana wa shamba la mizabibu, atawatendaje wale wakulima? Wakamwambia, Atawaangamiza vibaya wale wabaya; na shamba la mizabibu atawapangisha wakulima wengine, watakaomlipa matunda kwa wakati wake. Yesu akawaambia, hamkupata kusoma katika maandiko, Jiwe walilolikataa waashi, hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni; neno hili limetoka kwa Bwana, nalo ni ajabu machoni petu? Kwa sababu hiyo nawaambia, Ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu, nao watapewa taifa jingine lenye kuzaa matunda yake. Naye aangukaye juu ya jiwe hilo atavunjika-vunjika; naye ye yote ambaye litamwangukia, litamsaga tikitiki. Wakuu wa makuhani na Mafarisayo, waliposikia mifano yake, walitambua ya kuwa anawanenea wao. Nao walipotafuta kumkamata, waliwaogopa makutano, kwa maana wao walimwona kuwa nabii.

Bishara hii tumeishaitaja hapo mbeleni. Katika mithali hii nzuri Yesu katoa muhtasari wa historia ya Manabii. Fungu hili la maneno halina tashwishi ya kwamba shamba la mizabibu lamaanisha dunia; wakulima wamaanisha wanadamu kwa jumla; matunda aliyotaka kuyapokea mwenye nyumba yanamaanisha wema, unyofu na kujitupa kwa Mwenyezi Mungu; watumishi wamaanisha Manabii ambao wamekuwa wakija humu duniani mmoja baada ya mwingine; mwana yuamaanisha Yesu aliyedhihiri baada ya msururu mrefu wa Manabii. Mwana alidhalilishwa na kuuawa na wale wakulima. Baada ya kusema maneno haya, Yesu yuaendelea akizungumzia "jiwe walilolikataa waashi, hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni". Jiwe lililokuwa limekataliwa ni wazao wa Ismaeli, ambao wana wa Isihaka walizoea kuwadharaulia mbali. Kulingana na ile bishara, ilikuwa adhihiri

mmoja kutoka miongoni mwa wana wa Ismaeli na kuwa jiwe la pembeni, "Muhuri wa Manabii", chambileche vile ilivyomwelezea Kurani — si Nabii wa kawaida, bali Nabii angeliyeleta Sheria timilifu na ya mwisho kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Ujaji wa Mwismaeli kwa minajili ya hayo madaraka makuu ungelikuwa jambo geni. Lakini hata hivyo (asemavyo Yesu) Mungu angeondolea mbali ufalme Wake kutoka kwa Waisraeli na kuwapatia Waismaeli, wangeliohakiki kuwa ni taifa lenye kuzaa matunda ya lile shamba la mizabibu, yaani, taifa lingelilodumisha ibada ya Mungu duniani. Bila shaka kila mmoja anaweza kutambua kwamba Nabii mashuhuri wa pekee aliyekuja baada ya Yesu na angeliyeweza kusemwa yuaafikiwa na maelezo haya ni Mtume Mtukufu[saw] wa Islam. Yeye ndiye aliyekuwa na mapambano na dini ya Mayahudi na Ukristo na kuvunjilia mbali athari za dini hizi zote mbili. Ni yeye ambaye taifa lake lilichukiwa. Ni kumhusu yeye tu iwezekanapo kusemwa kwa hakika kwamba, "Yeyote aliyeanguka juu yake alivunika-vunjika na yeyote aliyeangukiwa naye alisagika tikitiki".

(b) Katika Mathayo (23: 38-39) tunayo maneno haya:

> Angalieni, nyumba yenu imeachwa hali ya ukiwa. Kwa maana nawaambia, Hamtaniona kamwe tangu sasa, hata mtakaposema, Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana.

Mistari hii yamaanisha kwamba Yesu atawatoka watu wake na watu wake hawataweza kumwona tena, hadi pale watakapotangaza wakisema:

> "Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana".

Hapa pana bishara ya ujaji maradufu. Ujaji mmoja baada ya kuondoka kwa Yesu; huu ulikuwa uwe kana kwamba ni ujaji wa Mungu (Mwenyewe). Mwingine ni ujaji wa mara ya pili wa Yesu mwenyewe. Inasemwa wazi kwamba hadi pale yule "ajaye kwa jina la Bwana" atakapokuwa amefika, ujaji wa Yesu wa mara ya pili hautatokea kamwe. Tumethibitisha hapo juu kwamba ajaye katika jina la Bwana ni yule anayefanana na Musa.

Bishara ya Yesu na ukweli uliohakiki wa ujaji wa Islam na Mtume[saw] wake Mtukufu havibakizi tena tashwishi ya kwamba katika mpango wa kimbinguni ujaji wa Yesu haukunuiwa uashirie ile hatua kuu ya mwisho ya maendeleo ya kiroho. Hatua hiyo ya mwisho ilikuwa iashiriwe na yule ajaye "katika jina la Bwana". Haiwezi ikasemewa kwamba nyuma yake Yesu aje tena, hivyo ile hatua ya mwisho katika maendeleo ya kiroho bado itatekelezwa na Yesu. Jambo hili lafafanuliwa na Yesu mwenyewe. Je, yeye hakutamka akisema:

> Hamtaniona kamwe tangu sasa hata mtakaposema, amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana (Mt. 23:39).

Wale watakaokuwa wamemkubali na kumtambua yule "mfano wa Musa" ndio peke yao watakaomwona, kumpokea na kumkubali ajapo mara ya pili.

Mwenye kumkatalia mbali yule "mfano wa Musa" hataweza kumtambua Yesu ajapo mara ya pili. Na kulikoni basi? Kwa sababu Yesu ajapo mara ya pili atapatikana miongoni mwa wafuasi wa yule "mfano wa Musa". Yesu hivyo basi, ajapo mara ya pili, hatakuwa ni Mwalimu wa kujitegemea. Yeye atakuwa mfuasi shupavu na kivuli cha yule "mfano wa Nabii Musa[as]". Hivyo basi, hatua ya mwisho katika maendeleo ya kiroho itaashiriwa na huyu. "mfano wa Nabii Musa[as].", wala si mwinginewe.

(c) Twasoma katika Yohana (1: 20-21) ya kuwa watu walimwendea Yohana Mbatizaji, na wakamwuliza kama yeye ndiye aliyekuwa Kristo wa bisharani naye akawajibu akiwaambia, La. Kisha wao wakamwuliza wakimwambia, Ni nini basi? U Eliya wewe? Akasema mimi siye (1:21).

Halafu wakamwuliza:

> "Wewe u nabiii yule? Akajibu la" (1:21).

Baadaye wao wakasema:

> Mbona basi wabatiza, ikiwa wewe si Kristo, wala Eliya wala nabii yule? (1:25) .

Ni wazi kabisa kutokana na maneno haya kwamba bishara tatu zilikuwa zikivuma wakati wa Yesu: (i) ujaji wa mara ya pili wa Eliya; (ii) kuzaliwa kwa Yesu; (iii) na ujaji wa Nabii yule, yaani Yule Mwahidiwa wa ile bishara ya Kumbukumbu la Torati. Na hao watatu waliaminiwa kuwa watu watatu mbalimbali.

Sasa Yesu amemtangaza Yohana mwenyewe kuwa ndiye Nabii Eliya. Na ndiposa katika Mathayo (11:14) tunayo maneno haya:

> "Na ikiwa mnataka kukubali, yeye ndiye Eliya atakayekuja".

Kutokana na Luka (1:17) pia yaonekana kwamba kabla ya kuzaliwa kwa Yohana, babake Zakaria alipokea ufunuo huu:

> "Naye atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya, na nguvu zake".

Halafu katika Marko (9 :13) twamkuta Yesu akitangaza akisema: "Eliya amekwisha kuja".

Na tena katika Mathayo (17:12) Yesu yuasema:

> Ila nawaambia, ya kwamba Eliya amekwisha kuja, wasimtambue, lakini wakamtenda yote waliyotaka.

Kutokana na maneno haya yote, ni dhahiri kwamba sawa na Injili, ujaji wa mara ya pili wa Eliya ulikuwa umetimia kwa dhati ya Yohana. Na ama kumhusu Kristo, yakubaliwa kwamba yeye si mwingine minghairi ya yule Yesu wa Agano Jipya. Bado "Nabii yule" tu. Yeye si Yohana wala Yesu, kwani yuatofautiana na hawa wote, yeye ni wa tatu. Pia yafahamika kwamba huyo "Nabii yule" alikuwa bado hajadhihiri hadi zama za Yesu. Ni wazi hivyo basi, ya kwamba huyo "Nabii yule" wa Biblia alikuwa adhihiri, sawa na ushuhuda wa Injili, wakati fulani baada ya Yesu. Baada ya Yesu, hapana mmoja ambaye amedai kuwa ndiye "Nabii yule" na kwa hakika hapana mmoja aonekanaye kana kwamba yuaziafiki zile ishara anazonasibishiwa huyo "Nabii yule" isipokuwa Mtume Mtukufu[saw] wa Islam.

(d) Katika Luka (24:49) tunayo maneno haya:

> Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu.

Kutokana na mstari huu pia yaonekana kwamba baada ya Yesu palikuwa pawe na mwingine. Na ni nani huyo minghairi ya Mtume Mtukufu[saw]? Mwingine minghairi yake hajapata kutoa madai hayo.

(e) Katika Yohana (14:26) tunayo maneno haya:

> Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisheni yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.

Bishara hii nayo pia inahakiki tu panapo na dhati ya Mtume[saw] wa Islam. Bishara yasema "ambaye baba atampeleka katika jina langu". Lakini haya maneno "katika jina langu" yanaweza tu yakamaanisha kwamba, "yeye atauyakinisha ukweli wangu". Mtume Mtukufu aliyakinisha ukweli wa Yesu kuwa yeye alikuwa mja wa kimbinguni na Mwalimu mheshimiwa na Nabii na kuwatangaza kuwa waliokosea na kupotoka wale waliomchukulia Yesu kuwa mlaaniwa. Bishara yasema dhahiri shahiri, "Yeye atawafundisha yote". Maneno yenyewe ni ukumbusho wa yale yaliyotumiwa katika ile bishara ya Kumbukumbu la Torati. Maelezeo yanamwafiki Mtume Mtukufu[saw] peke yake; ni mafundisho yake yaliyoiletea dunia faraja.

(f) Katika Yohana (16:7-14) tunayo maneno haya:

> Lakini mimi nawaambiya iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke; kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu. Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari za dhambi, na haki, na hukumu. Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini mimi; kwa habari ya haki, kwa sababu mimi naenda zangu kwa Baba, wala hamnioni tena; kwa habari ya hukumu, kwa sababu ya yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa. Hata bado ningali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. Lakini yeye

> atakapokuja, huyo Roho wa kweli atawaongozeni awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake. Yeye atanitukuza mimi; kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari.

Bishara hii yaagizia kwamba yule Msaidizi [Biblia ya Kiingereza ni Comforter, yaani Mfariji] atakuja baada ya Yesu kuiaga dunia hii. Msaidizi atakapokuja ataulaumu ulimwengu wa madhambi na wa ukweli na haki. Wa madhambi, kwa sababu yeye atawalaumu Mayahudi kwa kutomwamini Yesu. Wa ukweli, kwa sababu yeye ataikosoa imani ya kimakosa ya kufufuka kwa Yesu, na kwa kuwa yeye atauhakikishia ulimwengu ya kwamba Yesu wa Nazarethi — yule Mwalimu aliyeidhihirikia Israeli — hatarejea tena humu duniani yeye mwenyewe. Wa haki, kwa sababu yeye atazitia komesha juhudi zote za kishetani. Bishara halikadhalika yasema kwamba huyo Roho wa kweli atakapokuja, atawaongoza na kuwatia kwenye kweli yote, kwamba kitabu alichokifunuliwa hakitakuwa na maneno ya kibinadamu, kwamba atatabiri mambo yatakayokuja baadaye, na kwamba yeye atamtukukuza Yesu na kumwondolea lawama zote.

Bishara hii bila shaka yamhusu Mtume Mtukufu[saw]. Yasema kinagaubaga kwamba isipokuwa Yesu awe ameondoka, yule Msaidizi (Mfariji)hawezi kuja. Kutokana na Matendo (3: 21-22) pia yaonekana kwamba yule Nabii anayeahidiwa katika Kumbukumbu la Torati (18:18) atakuwa mwenye kudhihiri wakati fulani baina ya kung'atuka kwa Yesu na ujaji wake wa mara ya pili. Msaidizi huyo, hivyo basi, si mwingine minghairi ya yule Mwahidiwa katika Kumbukumbu la Torati (18:18). Bishara yasema kwamba huyo Mwahidiwa atawalaumu wanaomkataa Yesu. Mwahidiwa mweyewe hawezi akawa ni Mkristo. Bali ni jambo la kawaida kwa wafuasi kuwalaumu wale wanaomkataa Nabii wao. Bishara hii haina budi kumhusu mja angeliyetokana na taifa jingine lisilokuwa na uhusiano wa kidini wala wa kitaifa na Yesu lakini akiwa mkweli na Aliyetumwa na Mungu, imbidi kuheshimu makusudio ya Manabii

wote wa kweli na kuwazidishia wote heshima na staha. Nabii[saw] wa Islam alikuwa Mwismaeli, si Mkristo wala Myahudi. Lakini ameihami jinsi gani heshima ya Yesu. Ikiwagusia Mayahudi, Kurani (Sura An-Nisaa, 4:158-161) yasema:

> Na kusema kwao: Hakika tumemwua Isa mwana wa Mariamu, Mtume wa Mungu; hali hawakuumwua wala hawakumfisha msalabani, bali alifananishwa kwao (kama maiti). Na kwa hakika wale waliohitilafiana kwalo, yakini wana shaka nalo, nao hawalijui hakika yake isipokuwa wanafuata dhana. Na kwa yakini wao hawakumwua — Bali Mwenyezi Mungu Alimnyanyua Kwake, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima. Na hakuna yeyote katika watu wa Kitabu ila ataliamini kabla ya kifo chake, naye (Masihi) Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao. Basi kwa dhuluma ya Mayahudi Tuliwaharamishia vitu vizuri walivyohalalishiwa, na kwa sababu ya kuzuilia kwao wengi njia ya Mwenyezi Mungu.

Upitaji kiasi wa Mayahudi ulikuwa ni utovu wao wa imani, lawama zao za kikatili dhidi ya Mariamu, na madai yao ya uwongo kabisa kwamba walikuwa wamemwulia mbali Isa, Mtume wa Mungu[as]. Ukweli wa madai yenyewe ni kwamba hawakuwa wamefanikiwa kumwua Nabii Isa[as] si kwa upanga wala kwa kusulubisha. Walikuwa na dhana kabambe tu ya kwamba Yesu alikuwa amefia Msalabani. Lakini hii ilikuwa ni dhana tu wala haikuwa imani yao thabiti. Wao wenyewe waliendelea kubishana kati yao wala hawakuwa na maoni ya pamoja juu ya kile kilichotendeka kwa Yesu kwa hakika. Wakiwa hawanayo yakini ya jambo lenyewe, basi wao wakakisiakisia tu. Lakini ni kweli kabisa kwamba hawakufaulu katika njama zao za kumwulia mbali Nabii Isa[as]. Allah, kwa upande mwingine, alimnusuru dhidi ya kifo cha laana msalabani na kumwingiza katika kundi la vipenzi Vyake, na Allah ni Mwenye nguvu na Mwenye hekima pia. Kila mfuasi wa Kitabu ataendelea kung'ang'ania imani yake juu ya kifo cha Yesu msalabani, lakini Siku ya Hukumu Yesu atajitenga nao wote na kuwalaumu kwa kung'ang'ania uwongo mtupu. Kwa sababu ya hizi

hali za upitaji kiasi za Mayahudi, Mwenyezi Mungu akawaondolea mbali zile baraka za kimbinguni ambazo hapo kabla zilionekana kana kwamba ni urithi wao. Fungu hili la maneno lajielelezea lenyewe.

Alama ya pili katika bishara ya Yohana (16:7-14) ni hii ya kwamba huyo Mwahidiwa ataikosoa itikadi ya kimakosa juu ya kufufuka kwa Yesu na kuthibitisha kwamba Yesu, Mwisraeli, hatarudi tena duniani. Jukumu hili lilitekelezwa vilvyo na Mtume Mtukufu[saw] wa Islam; yeye alilifichua hili kosa ya kwamba Yesu alifufuka toka wafu na kupaa mbinguni alikokuwa yungali hai. Kurani katika (Sura Al-Maaida, 5:117-119) yasema:

> Na Mwenyezi Mungu Atakaposema: Ewe Isa bin Mariam: Je, wewe uliwaambaia watu: Nishikeni mimi na mama yangu kuwa waungu wawili badala ya Mwenyezi Mungu? Atasema: Wewe ndiwe Mtakatifu, hainipasi mimi kusema ambayo sina haki (ya kusema); kama ningalisema bila shaka Ungalijua; Unayajua yaliyomo nafsini mwangu, lakini mimi siyajue yaliyomo nafsini Mwako; hakika Wewe ndiwe Ujuaye sana mambo ya ghaibu. Sikuwaambia lolote ila yale Uliyoniamuru: ya kwamba Mwabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu; na nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa kati yao, lakini Uliponifisha Wewe Ukawa Mchungaji juu yao, na Wewe ni Shahidi juu ya kila kitu. Ikiwa Utawaadhibu, basi bila shaka hao ni watu Wako; na kama Ukiwasamehe basi kwa hakika Wewe ndiwe Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

Kipindi hiki cha maswali na majibu kitatokea Siku ya Hukumu. Aya hizi zatangaza kwamba Yesu amekufa na hayuko hai huko mbinguni; ni wafuasi wake tu waliomtwisha uungu alipokuwa amefariki na kuaga dunia. Kupaa mbinguni kuna maana hii tu ya kwamba akiwa ametekeleza wadhifa wake yeye alikuwa amekwenda kwa Muumba wake hali akiheshimiwa na mwenye kufaulu.

Bishara hiyo (Yohana 16 :7-14) pia ilisema kwamba Shetani na jitihada za kishetani zitatiwa komesha kwa mkono wa huyo

Mwahidiwa. Miongoni mwa mitume wote, Mtume[saw] wa Islam ni wa kileleni katika kuanzisha vikwazo dhidi ya jitihada zote za kishetani na athari zake mbaya na kwa ajili ya kusogeza mbele unyofu na ucha-Mungu maishani mwa mtu. Hatuwezi kuzamia tafsili za mambo sampuli hii hapa. Msomaji atakutana nayo katika sehemu nyinginezo za kitabu hiki. Twaweza kusema tu ya kwamba kwa akali dalili moja machoni petu ya madai haya yetu kwa niaba ya Mtume Mtukufu[saw] ni ile dua ya kulindwa dhidi ya athari mbaya ya Shetani ambayo Mtume Mtukufu[saw] aliwafundisha wafuasi wake, na aliyosisitizia matumizi yake ya mara kwa mara, yaani, ***Najikinga na Mwenyezi Mungu dhidi ya shetani***, mkataliwa. Dua yenyewe yatumiwa na Waislamu kwa kuizoelea. Hatujui cho chote mfano wake katika mafundisho ya Manabii wengine. Waislamu wamekaa chonjo zaidi ya mataifa mengine yote katika wajibu wao wa kila siku wa kuzitilia komesha njama za shetani. Wao wamefundishwa wajibu huu zaidi ya mataifa mengine yote. Wao wanaistahili zaidi ahadi iliyomo ndani ya ile bishara kuliko mataifa mengine. Nabii[saw] wao hivyo basi, atasemekana ya kuwa ameitimiliza bishara yenyewe. Kumuua Shetani, hata hivyo, sio kumaliza kabisa kabisa kiasi cha athari zake mbaya kutosalia duniani. Jambo hili halijatukia wala halitatukia asilan. Athari mbaya ya Shetani ni sharti zibakie. Bila ya athari hizo imani itakosa thamani. Hivyo basi, kummulia mbali Shetani ni kupunguza athari mbaya na matamanio hadi yasalie kidogo tu, na kujenga athari njema na tabia hadi kiwango cha kileleni. Kanisa haliwezi likadai bishara hii kwani Kanisa hilo hilo limeitangaza Sheria kuwa ni laana na kulipatia tashwishi wazo lenyewe la wema na ubaya. Haya maneno katika bishara hiyo — "atawaongozeni awatie kwenye kweli yote" — tayari tumeisha yaelezea katika mazungumzo yetu juu ya ile bishara iliyomo katika Kumbukumbu la Torati (18:18).

Ama kuhusu maneno haya — "na mambo yajayo atawapasha habari zake" — hatuna la kuongezea ila kusema tu ya kwamba hapana Nabii mwingine ambaye ameitabiria dunia mambo yatakayokuja kwa kiasi kikubwa kuliko Nabii[saw] wa Islam.

Na kuhusu hii alama — "kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayosikia atayanena" — yatubidi kusema kwamba maelezo yanaweza yakamwafiki Nabii[saw] wa Islam peke yake. Agano jipya na la Kale havina hata kitabu kimoja ambamo maneno ya watu hayakuchanganywa na maneno ya Mungu. Kurani si kinginecho minghairi ya maneno ya Mwenyezi Mungu toka mwanzo hadi mwisho. Hapana hata neno moja hata lile la Mtume Mtukufu[saw] mwenyewe lipatikanalo ndani yake, achilia mbali neno la mtu mwingine.

Alama ya mwisho katika bishara hiyo — "Yeye atanitukuza mimi" — nayo pia yamhusu Mtume Mtukufu[saw]. Kwani, ni yeye aliyemwondolea Yesu masingizio, ya kwamba eti, kwa vile alidai uungu, Yesu alikuwa na hatia ya kumkaidi na kutomwamini Mungu; na yale masingizio mengine batili ambayo Mayahudi walikuwa wamemzulia.

(g) Katika kitabu cha Matendo (3: 21-24) tunayo maneno haya:

> Ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni hata zije zama za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha Manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu. Kwa maana Musa kweli alinena kwamba, Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii, katika ndugu zenu, kama mimi; msikieni yeye katika mambo yote atakayonena nanyi. Na itakuwa ya kwamba kila mtu asiyemsikiza nabii huyo ataangamizwa na kutengwa na watu wake. Naam, na manabii wote tangu Samweli na wale waliokuja baada yake, wote walionena, walihubiri habari za siku hizi.

Mistari hii yazungumzia bishara iliyomo katika Kumbukumbu la Torati na inacho hiki kidokezeo cha waziwazi kwamba isipokuwa yule Nabii mwenye kuahidiwa katika Kumbukumbu la Torati awe amefika, ujaji wa Yesu wa mara ya pili hauwezi kukafanyika. Ile bishara ya Kumbukumbu la Torati ilisema kwamba yule Nabii Mwahidiwa ataleta Sheria mpya. Kudokezewa kwa jambo hili katika Matendo

kwamaanisha kwa uwazi kwamba mafundisho ya Yesu mahali pake patachukuliwa na mafundisho ya Yule Mwahidiwa. Haya maneno 'Sheria mpya' hayawezi yakawa na maana nyingine. Hivyo, Nabii mwenye kuahidiwa katika bishara ya Kumbukumbu la Torati (na katika maneno haya yanayotokana na kitabu eha Matendo) ilikuwa awe ndiye ishara ya ngazi ya mwisho katika maendeleo ya kiroho ya mwanadamu. Kwani yeye alikuwa aje achukue mahali pa Musa na Yesu na kuupatia ulimwengu Mafundisho mapya na Sheria mpya.

Haya maneno ya Matendo yanadokezea alama nyingine yenye maana ya Yule Mwahidiwa. Yanasema hivi:

> Na manabii wote tangu Samweli na wale waliokuja baada yake, wote walionena, walihubiri habari za siku hizi (3:24).

Bishara ya Musa tayari tumeishaitaja. Kwa kuwa Yesu alikuja baada ya Samweli, mstari huu utokao katika Matendo unaweza ukawa na maana hii tu ya kwamba kutoka Musa hadi Yesu kila Nabii ametabiri ujaji ya Nabii mmoja, jambo linalomaanisha kwamba hadi pale Nabii huyu atakapofika ile misingi ya kiroho mwanadamu asiyokuwa na budi kujenga juu yake itakuwa haijawekwa kikamilifu. Kwa kuwa Nabii huyu, sawa na alama za Biblia, si mwingine minghairi ya Mtume Mtukufu[saw] wa Islam, hatuna budi kuungama ya kuwa Mtume Mtukufu[saw] wa Islam ndiye Yule Mwahidiwa wa Manabii wote na Sheria yake ndiyo Sheria iliyotabiriwa na Manabii wote. Sasa ni nani awezaye kusema kwamba ijapo liwepo Agano Jipya na la Kale humu duniani Kurani haihitajiki? Manabii wote wa hapo mbeleni wameelezea haja ya Kurani na wakaitabiri. Hapana hoja ya maana inayoweza ikatolewa hivi sasa na wafuasi wa Manabii hao dhidi ya Kurani. Tunaweza ta tukasema kwamba kama wao watakanusha haja ya Kurani, basi watautilia doa na tashwishi ukweli wa Manabii wao wenyewe na ukweli wa zile bishara walizobashiri. Je, Musa hakutamka akisema:

> Atakaponena nabii kwa jina la Bwana, lisifuate jambo lile wala kutimia, hilo ndilo neno asilolinena Bwana; kwa kujikinai amelinena huyo nabii, usimwogope.

MTUME MTUKUFU[SAW] — MUHTASARI WA MAISHA YAKE

Sasa tumeishalijibu swali kuhusu haja ya wahyi wa Kurani pakiwepo na dini zingine. Na sasa tungependa kutoa muhtasari wa maisha ya Mtume Mtukufu[saw]. Fungamano la wahyi na mpokeaji wake ni la karibu sana, hatuwezi tukatumainia kukielewa kimoja bila ya kile kingine.

Mwanafalsafa yuaweza kukitenganisha kile mtu anachosema na yule anayekisema na kukifikiria kila kimoja mbali kabisa na kile kingine. Methali ya Kiarabu yakichukulia kile mtu anachosema kuwa chenye maana zaidi kuliko yule anayekisema. Lakini idadi iliyo kubwa zaidi ya watu wa kawaida hawatofuatishi baina ya hivyo viwili na huvichukulia vyote viwili kuwa ni muhimu. Kuhusu kitabu kilichofunuliwa yaonekana hususan kuwa muhimu ya kwamba tukisomapo ni sharti tuyatilie maanani maisha na tabia za yule mtu aliyekipokea kitabu chenyewe toka kwa Mwenyezi Mungu na kukifikishia watu wa zama zake. Mafundisho ya kidini, japo kama yatolewe hoja kabambe jinsi gani, hayakubaliwi na watu isipokuwa yawavutie sana kwa wito wenye nguvu. Hii ni kwa sababu Sheria ya kidini yatofautiana kimadhumuni na sheria za kidunia. Serikali huzingatia uthabiti na utengamano. Hudhamiria kujenga utiifu wa dhahiri; kwa minajili ya jambo hili yatosha kuwa nazo sheria zenye kuwezesha kupatikana kwa tabia nzuri ya dhahiri. Nia ya mtu haitiliwi maanani mradi hapana ukiukaji wa sheria unaoonekana. Nia mbaya haziadhibiwi na mahakama yoyote isipokuwa ziishilizie na tabia mbaya. Lakini katika upande wa dini, nia ni muhimu kama yalivyo yale matendo mabaya yanayotokana nazo. Bali nia ni muhimu zaidi. Matendo pia ni muhimu — hayo ndiyo ishara na alama za nia zisizoonekana. Lakini uimarikaji wa matendo yanayoonekana silo hakikisho la uimarifu katika nia zisizoonekana. Hata hivyo, uimarifu wa nia zisizoonekana, ni hakikisho la uimarifu katika matendo yaonekanayo. Moto bila ya joto haiwezekani; na ndivyo usafi wa moyo usivyowezekana pasi na usafi wa tabia. Kupitiliwa na uzembe huenda vikawepo; lakini kwa kawaida, usafi wa moyo ni sharti uishilize na usafi wa tabia.

Sasa basi, usafi wa moyo hukuzwa vizuri zaidi na mifano thabiti. Sheria nzuri huzipendeza fahamu na akili zetu; lakini mfano mzuri huzipendeza azma zetu na maono yetu. Sheria nzuri hutuchochea kufikiri, lakini mfano mwema hutuchochea kutenda. Mawazo yanaposafika, yanaweza au kutoweza kuishilizia na kusafika kwa tabia zetu za kimwili na za kiroho. Yanaweza yakaishilizia na mshtuko tu wa tabia njema — wala sio kuishilizia na tabia madhubuti na imara. Jambo hili laelelezewa na tofauti baina ya tabia ya kawaida tu ya kuwapendelea wengine na ile tabia ya kuwapendelea wengine itokanayo na silika ya kimaumbile kama vile silika ya mama mzazi. Moja kwa kiasi kikubwa hutokana na akili, na ile tabia nyingine kwa kiasi kikubwa hutokana na maono. Tabia itokanayo na hali ya kiakili tu haiwezi ikashindana na ile tabia inayotokana na hali ya maono au hali ya dhamira itokanayo na maono.

Mapenzi ya mama na kumjali kwake mwanawe ni hali itokanayo na maono au kutokana na azma itokanayo na maono. Hali ya mwanafalsafa kujali jirani zake hutokana na hali ya tabia ya kiakili ya kuwapendelea wengine. Tabia ya hali ya kiakili tu ya kuwapendelea wengine sio thabiti wala aminifu, kwani fikra mara nyingi huelekea kughafilika na ukweli wote upasikanao hauwezi ukakumbukwa daima kabla ya kuamulia tendo. Hali ya kusitasita na kufikirifikiri, iliyo ya lazima katika tabia ya mtu itokanayo na mawazo ya kiakili, nayo pia huelekea kuzidi kurefuka. Lakini tabia ya mtu itokanayo na maono au kutokana na maelekeo yenye kufanyizwa na maono ni ya papo hapo, isiyobadilikabadilika tena thabiti. Mama huenda aonekane yuajitolea kupita kiasi, lakini kumnasihi kwa busara hakuwezi kukambetua kando ya yale majaaliwa aliyoyawekewa na maumbile. Mtoto anapopatwa na shida, yeye hatajikalia tu na kusitasita, bali ataanza mara moja kufanya kile anachokifikiria kuwa chamfaa mtoto wake. Akili yake nzima itashughulikia kitu hiki. Hivyo basi, yaonekana kwamba masuala ya ufufuzi wa tabia njema hayatafanikiwa isipokuwa kama watu binafsi wanaweza kuzoeshwa kutenda kutokana na maelekeo na nia zitokanazo na maono yao na hamu zao. Inapotokea

haja ya kutenda jambo, basi uchukuaji wa hatua na usicheleweshwe na hali ya kusitasita isiyokuwa na maana. Uchukuaji wa hatua ni sharti utokeze mara moja kutoka nafsini mwa kila mmoja wala usiwe na budi kulazimishwa kutoka nje kwa kuanza kuupimia kiakili.

Ni kweli kabisa kwamba kwa kawaida maono hupewa nafasi ya pili baada ya akili. Lakini hii ni kwa sababu sisi twafikiria maono yasiyonidhamishwa na mapotovu. Tabia inayokuja husikana na maono peke yake hufupisha au kuondolea mbali ule muda wa kusitasita na kufikirifikiri wa katikati baina ya haja ya kuchukua hatua na hatua yenyewe. Kuondolewa mbali kwa huu muda wa kusitasita ni kwa lazima iwapo uchukuaji wa hatua utakuwa wa upesi na mwingi. Mtu mwenye kusitasita sana au mwenye kusitasita mara nyingi hupoteza bure ule wakati usiokuwa na budi kutumiwa katika kuchukua hatua. Lakini yule mtu mwenye kujua ukweli na kisha kuufanya maono hasitisiti asilan kuchukua hatua popote pale itokeapo haja ya kuchukua hatua. Mtu sampuli hiyo hawezi akashindwa na mtu mwenye tabia ya kusitasita. Ngwe yake ni mara ishirini zaidi ya ngwe ya yule mtu mwingine. Hali yake ya hamu na hima yake haiwezi ikadunisha thamani ya matendo yake. Kwani yeye hajitendei tu hivi hivi; bali hutafakari na kujulia njia ya kutendea na matokeo yake. Hali hii ya kujulia mambo yeye huifungamanisha na maono yake. Yeye hutenda mara huku akionekana bila hata kufikiri, lakini matendo yake yana msingi wa busara na ni matokeo ya kutafakari. Kwake yeye peke yake kutafakari pale kunapotimia, hakuna haja ya kurudiwa tena na tena. Kufikiria kupita kiasi au kufikiria tena na tena hakuwezi kukawa na hekima. Hivyo basi, uadilishaji wa kidunia nzima au ujengaji upya wa dunia hii hauna budi kusubiri, sio kusubiri ueleweke kwa uwazi kiakili na uwajibikaji wa kiakili, bali hauna budi kuambatanishwa na maono ya mwanadamu ya kawaida na hamu yake. Hata tuelewe kiakili kwa kiasi kikubwa kilioje, hicho hakiwezi kutuondolea shaka na tashwishi. Pana njia moja ya kuepukana na tashwishi, nayo ni kuushika ukweli na kisha kuuchanganya na hulka zetu. Hili litakapofanyika, kwetu sisi ukweli

hauwi tena kitu cha kufahamiwa au kufurahikiwa, bali hutumika kama ishara na miongozo kwa ajili ya utendaji na ufaulu. Kwa mtu wa kawaida kuingiza ukweli huu kwenye tabia ya kila siku hakuwezekani isipokuwa iwe ni chini ya athari nzuri za mifano mizuri. Hoja yaweza kuamsha uelewa wetu; haiwezi kuamsha hali ya mtu kujikinai nafsi yake anakokuweza tu mtoaji mfano mzuri wa kujikinai na kujitolea. Maneno yatumiwayo katika sala yanaweza yakawa mwafaka na maombelevu, lakini hapana kitu kitakacholeta kuzama kunakohitajika katika sala kuliko kumwona msalihina hasa aliyezama katika sala.

Lakini yafaa tusieleweke vibaya. Mfano unaweza ukapotosha na kuwa na hatari. Ni sharti udadisiwe kabla haujaruhusiwa kutuathiri. Isipokuwa uwe umedadidiwa na kukutwa ni wenye kutuliza, kuuiga mfano huo kutakuwa tu na matokeo ya watu wanaotaliwa na tabia na jamii iliyotawaliwa na desturi tunachohitaji ni vyote viwili, mafundisho yenye busara na mtoaji nadhifu wa mfano mzuri. Alhamdu lillahi, Vitabu vilivyofunuliwa naye vimefunuliwa Manabii, wala havikudondoshwa kutoka juu. Vitabu huvutia uelewa wetu, Manabii huzivutia nyoyo zetu. Haishanagazi ya kuwa Manabii huacha humu duniani athari zenye vina vya ndani zaidi ya vile wafanyavyo wanafalsafa; wao hufaulu pale wanafalsafa wakosapo kufua dafu. Wanafalsafa hutafuta kufafanua mawazo yetu, sio kutubadilisha kwa njia ya mfano wao mzuri. Lakini Manabii huyafanya haya yote mawili. Wao hutuchangamsha akili zatu kwa njia ya Vitabu vyao na nyoyo zetu kwa njia ya mfano wao mwema. Mafundisho yao yaliyoandikwa hutunoa uelewa wetu, ambapo ishara za kuwepo kwa Mwenyezi Mungu zinazoshuhudiwa katika utu wao husitawisha yakini, imani na shauku.

Hivyo basi, yaonekana kwetu sisi ya kwamba katika hiki Kifungua Mlango yatubidi tutoe habari za maisha na tabia za Mtume Mtukufu[saw] wa Islam.

MAISHA YA MTUME[SAW] NI KITABU KILICHO WAZI

Maisha ya Mwanzilishi Mtukufu[saw] wa Islam ni kama kitabu kilicho wazi ambacho sehemu yake yoyote mtu anaweza akaitalii na kukuta humo tafsili za kuvutia. Hapana maisha ya Mwalimu au Nabii mwingine yaliyoandikwa vilivyo na ambyo yanaweza kutaliika kama vile yalivyo maisha ya Mtume Mtukufu[saw]. Kweli kabisa, hii chungu nzima ya mambo yaliyorekodiwa juu ya maisha ya Mtume Mtukufu[saw] imewapatia wadadisi wakorofi fursa yao. Lakini pia ni kweli ya kwamba shutuma zenyewe zinapokuwa zimechunguzwa na kutupiliwa mbali, ile hali ya imani na mapenzi ijitokezayo haiwezi ikatiliwa moyoni na maisha mengineyo. Maisha yaliyofichama hukwepa shutuma lakini hukosa kuleta hali ya uhakika na Imani katika waumini wao. Hali ya kutoridhika pamwe na ugumu ni sharti itabakia pale pale. Lakini maisha yaliyorekodiwa sana kama yale ya Mtume Mtukufu[saw] huhamasisha tafakuri na kisha hali ya kusadiki. Wakati shutuma na hali ya kuyaelewa mambo visivyo vinapokuwa vimefutiliwa mbali, maisha kama hayo ni sharti yatatufanya tuyapende kikamilifu tena daima dawamu.

Hata hivyo, yafaa idhihirike kwamba masimulizi ya maisha yaliyo wazi sana mno tena yaliyofurika hayawezi yakaelezeka hata kwa ufupi. Kuyatupia jicho tu ndiko kunakowezekana. Lakini hata huko kuyatupia jicho kwenyewe kuna thamani kubwa. Kitabu cha kidini, kama tusemavyo, kinaweza kuvutia kidogo tu isipokuwa usomaji wake uwe unaweza ukatiliwa fora na hali ya watu kumjua Mwalimu wake. Ukweli huu umezipiga chenga dini nyingi. Dini ya Kibaniani, kwa mfano, yavitegemea vitabu vya Veda, lakini kuhusu wale viongozi (Marishii) wanaosemekana walivipokea vitabu hivyo kutoka kwa Mungu haiwezi kutuambia chochote. Haja ya kuutilia fora ujumbe kwa maelezo juu ya mjumbe haionekani kwamba iliwawajibikia mashabiki wa dini ya Kibaniani. Wanachuoni wa Kiyahudi na wa Kikristo, kwa upande mwingine, hawajali kuwalaumu Manabii wao wenyewe. Wao wanasahau ya kwamba wahyi usiomwongoa mpokeaji wake hauwezi ukawa na faida kubwa kwa watu wengine. Kama mpokeaji mwenyewe

akiwa ni mkaidi, hapo swali linazuka, kwa nini Mwenyezi Mungu akamchagua? Je, ilimbidi kufanya hivyo? Yote haya mawili hayaingii akilini. Kufikiria kwamba wahyi hukosa kumwongoa mpokeaji wake ni jambo lisiloingia akilini chambileche fikara kwamba Mwenyezi Mungu Hana jingine ila kuchagua wapokiaji dhaifu kwa ajili ya baadhi ya wahyi Wake. Lakini hata mawazo sampili hii yamejipenyeza katika dini mbalimbali, aghlabu kwa sababu ya ule muda mrefu ambao sasa hivi unazitenganisha na Waanzilishi wao au kwa sababu akili ya mwanadamu, hadi kufikia ujaji wa Islam, haikuweza kuliona kosa la mawazo haya. Ni muhimu na ni kitu cha maana kiasi gani kufungamanisha Kitabu na Mwalimu wake ni jambo lililotambulikana mapema sana katika Islam. Mmojawapo wa wake watakatifu wa Mtume Mtukufu[saw] alikuwa ni Hadhrat Aisha[ra]. Yeye alikuwa wa umri wa miaka kumi na mitatu au kumi na minne zama alipoolewa na Mtume Mtukufu[saw]. Kwa takriban miaka minane yeye aliishi naye katika ndoa. Mtume[saw] alipofariki yeye alikuwa na umri takriban wa miaka ishirini. Alikuwa bado yu mchanga na hakujua kusoma wala kuandika. Lakini juu ya hayo yeye alijua kwamba mafundisho hayawezi yakatenganishwa na mwalimu wake. Alipoulizwa juu ya tabia ya Mtume Mtukufu[saw], yeye alijibu mara moja akisema, tabia yake ndiyo Kurani (Abu Dawud). Yale aliyoyafanya ndio iliyoyafundisha Kurani; yale Kurani iliyoyafundisha hayakuwa kingine minghairi ya yale aliyoyafanya yeye. Inamletea Mtume Mtukufu[saw] heshima kubwa ya kwamba mwanamke kijana asiyejua kusoma na kuandika kufahamu ukweli uliowakwepa wataalamu wa Kibaniani, Kiyahudi na Kikristo.

Hadhrat Aisha[ra] alielezea ukweli mkubwa na wenye maana sana katika kajisentesi kadogo: haiwezekani kwa mwalimu halisi na mkweli kufundisha kitu kimoja na huku yuatenda kitu kingine, au kutenda jambo moja na kufundisha jingine. Mtume Mtukufu[saw] alikuwa ni Mwalimu halisi na mkweli. Hivi ndivyo Hadhrat Aisha[ra] alivyotaka kusema, kwa hakika. Alitenda yale aliyofundisha na kufundisha yale aliyoyatenda. Kumjua yeye ndiko kuijua Kurani na kuijua Kurani ndiko kumjua yeye.

HALI YA ARABUNI ZAMA ALIPOZALIWA MTUME MTUKUFU[SAW]

Mtume Mtukufu[saw] alizaliwa mjini Makka mwezi wa Agosti mwaka 570 A.D. Akapewa jina la 'Muhammad' lenye maana ya 'Msifiwa'. Ili kuyaelewa maisha na tabia yake ni sharti tuwe na picha ya hali iliyokuweko nchini Arabuni wakati wa kuzaliwa kwake.

Alipozaliwa, Arabuni nzima — isipokuwa hapa na pale — iliamini dini ya miungu wengi. Waarabu hufungamanisha nasaba yao na Hadhrat Ibrahimu[as]. Walijua kwamba Hadhrat Ibrahinu[as] alikuwa ni Mwalimu aliyehubiri Mungu Mmoja. Licha ya hayo, wao walishikilia imani za miungu wengi na ibada za miungu wengi. Wakijitetea wao walidai kwamba baadhi ya wanadamu walikuwa ni wa kileleni katika fungamano lao na Mwenyezi Mungu. Uombezi wao kwa niaba ya wengine ulikubaliwa na Mungu. Mungu Yuko juu na Mtukufu. Kumfikia lilikuwa jambo gumu kwa watu wa kawaida. Watu watimilifu peke yao ndio wanaoweza kumfikia. Hivyo basi, wanadamu wa kawaida ni sharti wapate wengine wafanye uombezi kwa niaba yao kabla hawajaweza kumfikia Mwenyezi Mungu na kupata radhi Yake na msaada Wake. Kwa msimamo wao huu waliweza kujumuisha heshima yao kwa Hadhrat Ibrahimu[as], yule muumini wa Mungu Mmoja, pamoja na itikadi zao za miungu wengi. Wao walisema Hadhrat Ibrahim[as] alikuwa ni mtu mtakatifu. Yeye aliweza kumfikia Mungu bila ya uombezi. Lakini wakazi wa kawaida wa Makka wasingeweza kumfikia Mungu bila ya uombezi wa watu wengine watakatifu na watawa. Katika kutafuta uombezi huu, watu wa Makka walikuwa wametengeneza sanamu za watu wengi watakatifu na watawa, na hawa waliwaabudu na kwao hawa walitoa sadaka ili wampendeze Mwenyezi Mungu kwa njia ya watu hawa. Msimamo huu ulikuwa ni wa kishenzi na usiokuwa na maana. Ulijawa na dosari na kasoro chungu nzima. Lakini watu wa Makka hawakuzijali. Kwa muda mrefu wao walikuwa hawajapata Mwalimu mwenye kuamini Mungu Mmoja, na itikadi ya miungu wengi, mara tu inapomea mizizi katika jamii yoyote, basi huzagaa kote kote. Idadi ya miungu huanza kuongezeka. Wakati alipozaliwa Mtume Mtukufu[saw],

yasemekana kwamba ndani ya Kaaba peke yake, Msikiti Mtakatifu wa Islam nzima na nyumba ya ibada iliyojengwa na Hadhrat Ibrahimu[as] na mwamawe Hadhrat Ismaeli[as], yalikuwemo masanamu mia tatu na sitini. Yaonekana kwamba kwa kila siku ya mwaka wa kimwezi watu wa Makka walikuwa na sanamu moja. Kwa mahali kwengineko na katika vituo vikubwa vikubwa yalikuweko masanamu mengine, hivi kwamba tunaweza tukasema ya kuwa kila sehemu ya Arabuni ilikuwa imezama katika imani ya miungu wengi. Waarabu walikuwa wakizingatia sana ufasaha wa lugha. Walitilia maanani sana usemaji wa lugha yao na kushughulikia mno ukuzaji wake. Hata hivyo, tamaa zao za kujiendeleza kiakili zilikuwa haba mno. Wao hawakujua chochote juu ya taaluma za Historia, Jiografia, Hisabati, n.k. Lakini kwa kuwa walikuwa ni watu wa jangwani na ilikuwa ni lazima wajue njia za kwenda huko na huko jangwani bila msaada wa viongoza njia vya ardhini, wao walikuwa wamejikuzia sana elimu ya nyota. Haikuweko hata shule moja Arabuni nzima. Yasemekana kwamba mjini Makka watu wachache tu waliweza kusoma na kuandika.

Katika uwanja wa tabia njema Waarabu walikuwa ni watu wendao kinyume kabisa. Walikuwa na ubovu wa kupindukia wa tabia zao lakini tena wao walikuwa na baadhi ya sifa za kuvutia. Walikuwa walevi wa kupindukia. Kuwa mlevi na kupayuka kwa sababu ya ulevi kwao wao ilikuwa ni sifa kubwa, wala sio ufasiki. Kwao wao muungwana alikuwa ni yule mtu asiyekuwa na budi kuwaburudisha marafiki na majirani zake katika tafrija za ulevi. Kila mtu tajiri angeliandaa burudani za ulevi kwa akali mara tano kila siku. Kamari ilikuwa mcheze wao wa kitaifa. Lakini wao walikuwa wameusanii kuwa ni sanaa. Wao hawakucheza kamari ili kujitajirisha. Washindi walitakiwa kuwaburudisha masahibu zao. Katika nyakati za vita, pesa zilikusanywa kwa njia ya kamari. Hata hivi leo tunayo desturi ya watu kucheza michezo ya bahati nasibu kuchangisha pesa za kugharamia vita. Desturi hii imejadidishwa katika wakati huu wetu na watu wa Ulaya na Marekani. Lakini ni sharti wakumbuke kwamba katika mbinu hii wao wanawaiga Waarabu. Vita vilipozuka, makabila ya

Waarabu wangelikutana na kuwa na tafrija ya kamari. Yeyote aliyeshinda alikuwa agharamie sehemu kubwa ya matumizi ya vita.

Na kuhusu vifaa vya maisha ya kistaarabu, Waarabu hawakujua chochote. Utovu huu wao waliufidia kwa ulevi na kucheza kamari. Kazi yao kubwa ilikuwa ni biashara, na katika uwanja huu wao walipeleka misafara yao hadi maeneo ya mbali. Kwa njia hii, wao walifanya biashara na Uhabeshi, Siria na Palestina. Walikuwa na uhusiano wa kibiashara hata na nchi ya India. Matajiri miongoni mwao walikuwa ni wenye kuvutiwa sana na upanga wa India. Kwa kiasi kikubwa mahitaji yao ya nguo yalitoshelezwa na nchi za Yemeni na Siria. Vituo vya kibiashara vilikuwa ni mijini. Sehemu iliyosalia ya Arabuni, isipokuwa Yemeni na baadhi ya maeneo ya kaskazini, kulikuwa ni Ubeduini. Hapakuwepo na maskani ya kudumu, wala makazi ya kudumu. Makabila mbalimbali yalikuwa yameigawanya nchi miongoni mwao hivi kwamba watu wa kabila moja walizunguka huko na huko wakiwa ni watu huru katika eneo lao la nchi. Wakati maji yalipoadimika katika sehemu fulani, wao wangeguria sehemu nyingine na kukaa pale. Rasilimali yao ilikuwa ni kondoo, mbuzi na ngamia. Kutokana na manyoya, wao walitengeneza nguo, na kutokana na ngozi wakatengeneza mahema. Vilivyobakia waliviuza sokoni. Dhahabu na fedha havikuwa vitu visivyojulikana, lakini viliadimika mno, kwa hakika. Maskini na watu wa kawaida walijitengenezea mapambo kutokana na kauri na vitu vyenye harufu nzuri. Mbegu za matikiti zilisafishwa, zikakaushwa na kutengenezwa mikufu. Wizi ulikuwa ni kitu cha akali lakini unyang'anyi ulizagaa. Kushambuliana na kupokonyana lilikuwa ni jambo la faradhi. Lakini, wakati huo huo, wao walitimiza ahadi zao kuliko watu wenginewe. Angetoka mtu kumwendea kiongozi mwenye nguvu au kabila na kutaka apatiwe hifadhi, basi kiongozi yule au kabila lile lisingelikuwa na budi kumlinda mtu yule. Kama pangekosekana kufanywa hivyo, basi lile kabila lingedharuliwa Arabuni nzima. Washairi walipewa heshima kubwa. Walipewa heshima kuwa kama ni viongozi wa kitaifa. Viongozi walitakikana kuwa wasemaji fasaha na hata kuweza

kutunga mashairi. Ukarimu ulikuwa umekuja kuwa ni sifa ya kitaifa. Msafiri hohehahe alipowasili penye makao makuu ya kabila alikaribishwa kama mgeni mheshimiwa. Yeye alichinjiwa wanyama bora zaidi na kuonyeshwa takrima kubwa mno. Wao hawakujali mgeni mwenyewe ni mtu wa aina gani. Ilitosha tu ya kwamba mgeni alikuwa amewasili. Ugeni ulimaanisha kuongezeka kwa hadhi ya lile kabila mwenyeji. Basi, ikawa wajibu wa lile kabila kumpatia mgeni yule heshima. Kwa kumpatia yeye heshima likajiletea lenyewe heshima. Wanawake nchini Arabuni hawakuwa na hadhi wala haki. Miongoni mwa Waarabu lilifikiriwa kuwa ni tendo la heshima kumuulia mbali mtoto wa kike. Hata hivyo, ni kosa kudhania kwamba desturi ya kuwaulia mbali watoto wa kike ilifuatwa nchini kote. Desturi hatari sampuli hiyo isingeliweza kuenea nchi nzima. Jambo hilo lingemaanisha kuangamia kwa taifa zima. Ukweli wenyewe ni kwamba huko Arabuni, au tuseme nchini India au katika nchi yoyote ile ambako kumewahi kupatikana hii desturi ya kuwaua watoto wa kike, imekuwa ni desturi ya familia fulani fulani tu. Zile familia za Waarabu walioshikilia desturi hii ama walikuwa na hali ya kujivunia kupita kiasi hadhi yao ya kijamii au walikuwa wamebanwa kwa njia nyingine. Pengine hawakuweza kujipatia vijana wanaofaa kuwaoa mabinti zao; na kwa kufahamu hivyo kimbele wao wakawaulia mbali watoto wao wa kike. Ubaya wa desturi hii umo katika unyama wake na ukatili wake, wala haumo katika matokeo unaoyasababisha katika suala la idadi ya wakazi nchini. Mbinu mbalimbali zilitumiwa kuwaulia mbali watoto wa kike, miongoni mwao ilikuwa ni kuwazika wazima au kwa kuwakaba koo shingoni.

Mama mzazi tu ndiye aliyehesabiwa kuwa ni mama katika jamii ya Waarabu. Mama wa kambo hawakuhesabiwa kuwa ni mama na hapakukatazwa kijana kumwoa mamake wa kambo kufuatia kifo cha babake. Ndoa za wake wengi zilizagaa mno wala hapakuwepo na kikomo cha idadi ya wanawake mtu alioweza kuwa nao. Madada zaidi ya mmoja pia wangeweza kuolewa na mume mmoja kwa wakati mmoja.

Kutendeana vibaya kupindukia kulifanywa na pande mbili zinazopigana vita. Palipokuwa na uadui mkubwa, wao hawakusita kutumbua miili ya majeruhi, kutwaa sehemu za vya ndani na kuzila mtindo wa wala watu. Hawakusita kuzikatakata maiti za maadui zao. Kuwatema watu pua zao au masikio, au kung'olea mbali jicho ulikuwa ni ukatili wa kawaida walioufanya. Utumwa ulienea sana. Makabila dhaifu yalitiwa utumwani. Mtumwa hakutambulikana. Kila mfuga watumwa aliwatendea watu wake jinsi alivyotaka. Hapakuwa na hatua iliyoweza kuchukuliwa dhidi ya mfuga watumwa aliyewatendea watumwa wake visivyo. Mfuga watumwa angeweza kumuulia mbali mtumwa wake bila kuwajibika kwa kitendo chake hiki. Kama mfuga mtumwa fulani angemuua mtumwa wa mtu mwingine, hata hivyo asingeliadhibiwa kwa kifo. Alichotakiwa kufanya ilikuwa ni kumlipa fidia inayofaa yule mwenye mtumwa. Watumwa wa kike walitumiwa kutulizia ashiki za kimwili. Watoto waliotokana na unyama huu nao pia walitendewa kama watumwa. Watumwa wa kike waliopata kuwa mama wazazi walibakia kuwa watumwa tu. Ukipima kwa mizani ya ustaarabu na maendeleo ya kijamii Waarabu walikuwa ni taifa lililo nyuma sana. Kuhurumiana na kutendeana wema vilikuwa vitu visivyojulikana. Wanawake walikuwa na hali mbovu zaidi. Pamoja na hayo Waarabu walikuwa na uzuri wao. Ushujaa wa mtu, kwa mfano, wakati mwingine ulifikia ngazi ya kileleni.

Ilikuwa ni katika watu sampuli hii ambamo Mtume Mtukufu[saw] wa Islam alizaliwa. Babake mzee Abdulla, alifariki kabla ya kuzaliwa kwake. Kutokana na hali hii, yeye na mamake bi Aamina, ikawa wapatiwe huduma na babuye, mzee Abdul Muttalib. Mtoto Muhammad alinyonyeshwa na mama mmoja wa mashambani aliyeishi mahali karibu na mji wa Ta'if. Ilikuwa ni desturi huko Arabuni siku zile kuwatoa watoto kwa akina mama wa mashambani, ambao jukumu lao lilikuwa ni kuwalea watoto wale, kuwazoesha lugha safi na kuwapatia msingi bora kiafya. Mtume[saw] alipokuwa na umri wa miaka sita, mamake alifariki alipokuwa safarini toka Madina kwenda Makka na ikabidi azikwe njiani. Mtoto akaletwa Makka na

mtumishi wa kike na kukabidhiwa babuye. Alipotimu umri wa miaka minane, babuye naye pia akafariki, ambapo baadaye ami ya mjombake, mzee Abu Talib, akawa mlezi wake, huu ukiwa ni wasia uliousiwa na babuye. Mtume[saw] alikuwa na fursa mbili au tatu za kusafir nje ya Arabuni. Fursa moja ilijitokeza wakati alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili alipokwenda nchini Siria akiandamana na mzee Abu Talib. Yaonekana, kwamba safari hii ilimfikisha tu kwenye miji ya kusini mashariki mwa Siria, kwani katika kumbukumbu za kihistoria za safari hii hamtajwi humo mahali kama vile Yerusalemu. Kuanzia hapo hadi alipopevuka na kufikia ujana yeye aliishi mjini Makka. Tangu utotoni yeye alikuwa na mazoea ya kufikiri na kutafakari. Kwenye ugomvi na mizozo ya wengine yeye hakujiingiza, isipokuwa iwe ni kwa shabaha ya kuilainisha. Yasemekana kwamba makabili yaliyoishi mjini Makka na maeneo yaliyoizunguka, huku yakichoshwa na patashika zisizokuwa na mwisho, yaliamua kuanzisha chama ambacho madhumuni yake yalikuwa ni kusaidia manusura wa chokochoko za watu na dhuluma. Mtume Mtukufu[saw] alipopata habari hii, alijiunga nao kwa furaha. Wanachama wa chama hiki walijitwisha jukumu lifuatalo:

> Wao watawasaidia wale wanaodhulumiwa na watawarejeshea haki zao, mradi bado wangali hai. Na wakosapo kufanya hivyo, watawafidia hao manusura toka kwa mali zao wao wenyewe. (Ar-Raudhul-Unuf cha Imam Suhaili).

Yaonekana kwamba hapana mwanachama mwingine wa chama hiki aliyewahi kutakiwa atimize ile ahadi iliyoahidiwa kwa dhati na wanachama wa chama hiki. Lakini fursa ilimfikia Mtume Mtukufu[saw] alipokuwa ametangaza Wadhifa wake. Adui wake mkubwa alikuwa ni Abu Jahl, chifu wa Makka. Huyu Abu Jahl alieneza ususiaji na kudhalilishwa kwa Mtume. Takriban wakati ule ule mkazi wa nje ya Makka alifika mjini. Alikuwa alipwe pesa zake na Abu Jahl, lakini Abu Jahl alikataa katakata kumlipa. Mtu huyu aliwaelezea watu wa Makka taabu zake. Baadhi ya vijana, kwa kutia fitina tu, wakamshauri amwendee Mtume[saw]. Walifikiri kwamba Mtume[saw] atakataa kufanya

lolote kwa hofu ya upinzani wa kila mtu na hususan hofu ya upinzani wa Abu Jahl. Kama akikataa kumsaidia huyu mtoka nje ya Makka, basi atasemekana amevunja ahadi yake kwa kile chama. Na kwa upande mwingine, kama aamue kumfuata Abu Jahl kumtaka alipe mkopo wa wenyewe, basi bila shaka Abu Jahl angemfukulizia mbali kwa dharau. Yule mtu akamwendea Mtume na kumnung'unikia dhidi ya Abu Jahl. Mtume[saw] bila kusita akainuka na kufuatana na yule mtu hadi kwa Abu Jahl na kubisha mlango wa Abu Jahl. Abu Jahl akatoka nje na kukuta kwamba mdai wake yuasimama pamoja na Mtume[saw]. Mtume[saw] akagusia lile deni na kutaka lilipwe. Abu Jahl akashtuka, na bila ya kutoa udhuru wowote akalipa mara moja. Wakati machifu wengine wa Makka waliposikia kisa hiki walimlaumu Abu Jahl, wakimuambia vile alivyokuwa mtu mnyonge na kigeugeu. Yeye alieneza ususiaji wa Mtume, na kumbe yeye mwenyewe akasalimu amri ya Mtume[saw] na kulipa deni kwa kuhimizwa naye. Katika kujitetea, Abu Jahl aliapa kwamba hata mtu mwinginewe angelifanya vivyo hivyo. Aliwaambia kwamba pale nilipomwona Mtume[saw] akisimama, pale mlangoni, mimi pia niliona ngamia wawili wakali upande wa kuume na kushoto wa Muhammad[saw] wakiwa tayari kunishambulia. Hatuwezi tukasema hiki kilikuwa ni kituko cha aina gani. Je, lilikuwa ni onyesho la kimuujiza lililonuiwa kumhofisha Abu Jahl au ilikuwa ni hofu ya kuwepo kwa Mtume[saw] iliyochora ndoto sampuli hii? Mja mwenye kupingwa na mji mzima alijasiri kwenda peke yake kwa jumbe wa mji na kutaka ulipaji wa deni. Pengine ni huku huku kuwepo kwa Mtume[saw] kusikotazamiwa kulikomtia kiwewe Abu Jahl na kwa muda akasahau yale aliyoapa kumtendea Mtume, na kukamfanya atende vile alivyotaka Mtume (Hisham).

NDOA YA MTUME MTUKUFU[SAW] NA HADHRAT KHADIJA[RA]

Mtume[saw] alipokuwa na umri wa takriban miaka ishirini na mitano, sifa yake ya uaminifu na huruma ilikuwa imeenea mji mzima. Watu wakawa wanamwelekezea kidole kwa kuvutika huku wakitamka wakisema, hapa pana mtu awezaye kuaminiwa. Sifa hii ikamfikia mjane mmoja tajiri aliyemwendea ami yake Mtume[saw], mzee Abu

Talib, kumtaka amruhusu Mtume aongoze msafara wake wa kibiashara hadi nchini Siria. Mzee Abu Talib akamfikishia Mtume[saw] ombi hili naye akalikubali. Msafara huu ukapata ufanisi mkubwa na kuleta faida isiyotazamiwa. Yule mjane, Bi Khadija, akawa na hakika kwamba ule ufaulu wa msafara haukuwa tu sababu ya hali ya soko nchini Siria, bali pia kwa sababu ya uaminifu na uhodari wa kiongozi wake. Bi Khadija akamhoji mtumwa wake, Maisara, juu ya jambo hili, na Maisara akamuunga mkono rai yake na akamwambia kwamba ile hali ya uaminifu na huruma ya huyu kijana kiongozi wa msafara aliyoitimiza shughuli zako haiwezi ikaonyeshwa na mtu mwingine. Bi Khadija akavutiwa sana na repoti hii. Alikuwa na umri wa miaka arubaini na tayari alikuwa ameisha kuwa mjane mara mbili. Akamtuma mwanamke mmoja rafikiye akatafute uwezekano wa kumfanya Mtume[saw] amuoe. Huyu mwanamke akamwendea Mtume[saw] na kumwuliza kwa nini hajaoa. Mtume[saw] kajibu akisema kwamba yeye alikuwa bado hajawa tajiri kuweza kufanya hivyo. Yule mgeni akapendekeza iwapo yeye Mtume angeliridhia, endapo angelipatikana mwanamke tajiri tena mheshimiwa angeliyeweza kumwoa. Mtume akadadisi akiuliza huyo angelikuwa mwanamke yupi, na yule mama mgeni akajibu akisema kwamba huyo ni Bi Khadija. Mtume[saw] akamtake radhi akimwambia kwamba Bi Khadija alikuwa wa ngazi ya juu sana kwake. Yule mama mgeni akaahidi kufagilia mbali vikwazo vyote. Kama ni hivyo, akasema Mtume, basi yeye hakuwa na jingine la kusema ila kukubali. Hapo Bi Khadija akampelekea amiye Mtume ujumbe. Ndoa baina ya Mtume na Bi Khdija ikakubaliwa na kuhitimishwa. Sasa mtu maskini aliyetiwa uyatimani utotoni akajionea utajiri kwa mara ya kwanza. Akawa tajiri. Lakini vile alivyoutumia utajiri wake ni somo kubwa kwa wanadamu wote. Baada ya ndoa ile Bi Khadija alionelea kwamba yeye alikuwa tajiri ilihali Mtume alikuwa maskini na kwamba tofauti hii baina yao isingelileta furaha. Hivyo basi yeye akapendekeza ampatie Mtume mali zake na watumwa wake. Mtume, akiwa amejihakikishia kwamba Bi Khadija amekazania uamuzi wake, alitangaza kwamba mara baada

ya yeye kupewa watumwa wowote wa Bi Khadija, atawachilia huru. Na hivyo ndivyo alivyofanya. Isitoshe, sehemu iliyo kubwa zaidi ya ile mali aliyopata kutoka kwa Bi Khadija yeye aliigawia maskini. Miongoni mwa watumwa aliowachilia huru alikuwa ni Zaid. Yeye alionekana mwenye maarifa na busara zaidi ya wengine. Alitokana na familia yenye kuheshimika, alikuwa ametekwa nyara na kuuzwa huko na huko hadi alipofika Makka. Kijana Zaid, mwachiliwa huru, alitambua mara moja kwamba ilikuwa ni afadhali kusahaulia mbali uhuru wake kwa ajili ya kumtumikia Mtume. Mtume alipowaachilia huru watumwa, Zaid alikataa kuachiliwa huru na akataka aruhusiwe kuendelea kukaa na Mtume. Lakini wakati huo huo babake Zaid na amiye walikuwa wakimtafuta na mwishowe walifika Makka. Mjini Makka wakamgundua nyumaani kwa Mtume. Walifika kwa Mtume na wakataka uhuru wa Zaid na wakawa tayari kumlipia fidia kiasi atakachotaka Mtume. Mtume akasema kwamba Zaid alikuwa yu mtu huru na angeweza kufuatana nao kama alivyopenda. Akamwita Zaid na akamwonesha babake na amiye. Baada ya wao kukutana na kujifuta machozi yao babake Zaid akamwambia kwamba alikuwa ameachiliwa huru na bwana wake mwenye huruma na kwa kuwa mamake alikuwa amekondeshwa mno na kule kutengana kwao ni afadhali arejee makwao. Zaid akajibu akisema, "Baba, ni nani asiyewapenda wazazi wake? Moyo wangu umefurikwa na mapenzi yako na mama. Lakini mimi nampenda sana mtu huyu Muhammad kiasi hiki kwamba siwezi kutamani kuishi mahali pengine minghairi ya alipo yeye. Mimi nimekutana nawe na nimefurahika sana. Lakini kutengana na Muhammad mimi sikuwezi". Baba na amiye Zaid wakafanya chini juu wakimbembeleza aandamane nao makwao lakini Zaid akakataa katakata. Kuona hivyo, Mtume Mtukufu[saw], akatamka akisema, "Zaid tayari alikuwa yu mtu huru, lakini kuanzia hivi leo yeye atakuwa mwanangu". Kuona hali hii ya kupendana baina ya Zaid na Mtume[saw], baba na amiye Zaid wakajiendea zao na Zaid akasalia na Mtume[saw] (Hisham).

MTUME[SAW] APOKEA WAHYI WAKE WA KWANZA

Mtume[saw] alipokuwa na umri wa zaidi ya miaka thalathini, mapenzi yake ya kumpenda Mwenyezi Mungu na ya kumwabudu Yeye yalizidi kumwongezekea. Huku akichukizwa na vitimbi, makosa na maovu mengi ya watu wa Makka, yeye alijichagulia mahali takriban maili mbili au tatu toka Makka, pa kujitulizia na kutafakari. Mahali hapa palikuwepo juu ya mlima, mithili ya pango lililochimbika kwenye jabali. Mkewe Bi Khadija[ra], ikawa amtayarishia chakula cha kutosha siku kadha, naye kwenda nacho hadi lile pango la Hiraa. Mle pangoni, akawa yeye akimwabudu Mwenyezi Mungu mchana na usiku. Alipokuwa na umri wa miaka arubaini, akaona njozi. Ilikuwa ni katika pango hili hili. Aliona mtu akimwamrisha asome. Mtume akajibu akisema sijui kusoma. Yule mtu akamkazania na mwishowe akamsomesha Mtume[saw] hizi aya zifuatazo:

> Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba, Alimuumba mwanadamu kwa tone la damu iliyoganda. Soma, na Mola wako yu Mkarimu sana, ambaye Alifundisha (kuandika) kwa kalamu. Alimfundisha mwanadamu asiyoyajua (Sura Al-'Alaq, 96:2-6).

Aya hizi, za mwanzo kabisa kufunuliwa kwa Mtume[saw], zikaja kuwa sehemu ya Kurani chambileche zile zingine zilizofunuliwa baadaye. Aya hizi zina maana kuu. Zinamwamrisha Mtume[saw] asimame na kuwa tayari kutangaza jina la Mungu Mmoja, Yule Muumba Mmoja — wa Mtume[saw] na wengineo wote — Ambaye amemtengeneza mwanadamu na akapanda katika maumbile yake mbegu ya mapenzi Yake Yeye Mwenyewe na mbegu ya mapenzi juu ya wanadamu wengine. Mtume[saw] aliamriwa kutangaza Ujumbe wa Mungu Huyu, na akaahidiwa msaada na ulinzi Wake katika utangazaji wa Ujumbe huu. Aya hizi zilitabiri zama ambapo dunia itafundishwa aina zote za elimu kwa njia ya kalamu, na itafundishwa mambo ambayo kamwe hayakusikika hapo kabla. Aya hizi ni muhtasari wa Kurani. Chochote kile ambacho Mtume[saw] alikuwa aje kufundishwa katika wahyi wa baadaye kimo mithili ya mbegu katika aya hizi. Msingi ulijengwa

ndani ya aya hizi wa maendeleo makubwa yasiyojulikana hapo kabla katika hali ya ukuaji wa kiroho wa mwanadamu. Maana na maelezo ya aya hizi vitapatikana mahali pao katika Maelezo haya. Twavikariri hapa kwa kuwa kufunuliwa kwa mambo haya linakuwa ni tukio kubwa mno katika maisha ya Mtume[saw]. Mtume[saw] alipopokea wahyi huu, aliingiwa na hofu ya lile jukumu ambalo Mwenyezi Mungu alikuwa ameamua kumkabidhi. Mtu mwingine yeyote angelijivunia hali hii ya Mtume[saw] — angejihisi kwamba sasa amekuwa mtu mkubwa. Mtume[saw] alikuwa tofauti. Angeweza kujipatia ufaulu mkubwa lakini kutoweza kujivunia ufaulu wake. Baada ya tukio hili kuu Mtume[saw] alifika nyumbani kwake akiwa mwenye hofu na uso wake kuhuzunika. Alipoulizwa na Bi Khadija[ra] akamsimulia kisa chote na akamfupishia hofu kwa kumwambia, "Mtu mnyonge kama mimi, nawezaje kutekeleza ule wajibu anaotaka Mwenyezi Mungu kunikabidhi". Hadhrat Khadija[ra] akajibu mara moja akisema:

> Wallahi, Yeye Hakukuletea Neno hili kusudi usifue dafu na kuwa usiyefaa, ili Akutupilie mbali. Anawezaje Mwenyezi Mungu kufanya hivyo, hali wewe u mkarimu na mwenye kuwahurumia ndugu zako, wawasaidia maskini na mafukara na kuwaondolea shida zao? Wewe waurejesha ule wema uliokuwa umetoweka nchini mwetu. Wawaheshimu wageni na kuwasaidia wale walio na dhiki. Je, waweza kutiwa mitihanini na Mwenyezi Mungu? (Bukhari).

Baada ya kusema hayo, Hadhrat Khadija[ra] alimpeleka Mtume[saw] kwa binamu yake, aliyeitwa Waraqa bin Naufal, aliyekuwa Mkiristo. Aliposikia kisa kile, Waraqa akatamka akisema:

> "Yule malaika aliyemshukia Musa, nina hakika, amekushukia wewe" (Bukhari)

WAISLAMU WA AWALI

Ni dhahiri Waraqa alikariri ile bishara ya Kumbukumbu la Torati 18:18. Habari hii ilipomfikia Zaid yule Mtumwa wa Mtume[saw] aliyeachiliwa huru, aliyekuwa sasa na umri wa takriban miaka

thalathini, na binamu wa Mtume[saw], Ali, aliyekaribia umri wa miaka kumi na mmoja, wote wawili walisilimu. Bwana Abu Bakr, rafiki yake wa utotoni, alikuwa nje ya mji. Alipokuwa akirud akaanza kusikia hii habari ya kisa kilichokuwa kimempata Mtume[saw]. Aliambiwa kwamba rafikiye alikuwa ameshikwa na wazimu na alikuwa ameanza kusema kwamba malaika walimletea ujumbe toka kwa Mungu. Bwana Abu Bakr alikuwa akimwamini Mtume[saw] kabisa. Hakuwa na shaka hata kidogo, kwamba ni sharti Mtume[saw] awe yuasema kweli — alikuwa akimfahamu kuwa mtu mwenye akili zake na mwaminifu. Alibisha hodi mlangoni pa Mtume[saw] na baada ya kukaribishwa ndani na wakawa pamoja akamwuliza Mtume[saw] kilichotendeka. Mtume[saw] kwa kuhofia huenda Bwana Abu Bakr amwelewe visivyo, akaanza kutoa maelezo marefu. Bwana Abu Bakr akamkatiza, na kurudia kusema kwamba alichotaka kujua ni kama kweli malaika alikuwa amemshukuia toka kwa Mungu na kumpatia Ujumbe. Mtume[saw] akataka kuelezea tena, lakini Bwana Abu Bakr akasema hakutaka kusikia maelezo yoyote. Alitaka jibu ya kuwa kweli alikuwa amepata Ujumbe kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mtume[saw] akasema, "Naam", na mara moja Bwana Abu Bakar akasilimu. Huku akiwa amesilimu akatamka akisema, kubishana kungelishusha hadhi ya imani yangu. Alikuwa amemjua Mtume[saw] kwa muda mrefu tena na kwa karibu sana. Yeye asingeweza kumtilia shaka, wala hakutaka hoja yoyote kumhakikishia ukweli wake. Hiki kikundi kidogo cha waaminio wakati huo ndio waliokuwa waaminio wa kwanza wa Islam: mwanamke mzee, kijana wa miaka kumi na mmoja, mtumwa mwachiliwa huru aliyekiishi ugenini, kijana rafiki na Mtume mwenyewe[saw]. Hili ndilo lililokuwa kundi lililokata shauri kimoyomoyo kusambaza nuru ya Mwenyezi Mungu duniani kote. Watu na viongozi wao walipopata habari hizi, wakaangua kicheko na kutangaza kwamba watu hawa walikuwa ni wendawazimu. Hapakuwa na cha kuogopa wala cha kutilia wasiwasi. Lakini kadiri muda ulivyopita, ukweli ulianza kudhihirika na chambileche alivyotabiri Nabii Isaya (28:13) hapo zamani sana, amri juu ya amri, amri juu ya amri; kanuni juu ya kanuni, kanuni juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo; zilianza kumshukukia Mtume[saw].

WAAMINIO WATESWA

Mungu alianza kuzungumza na Muhammad[saw] katika "lugha nyingine". Vijana wa nchi wakaanza kushangaa. Wale waliokuwa wakitafuta ukweli wakapata shauku. Toka katikati ya kejeli na dharau pakatokea hali ya ukubalifu na uvutiwaji. Watumwa, vijana, na wanawake maskini wakaanza kujikusanaya karibu na Mtume[saw]. Katika Ujumbe wake na mafundisho yake mlikuwemo na tumaini kwa ajili ya wanyonge, waliokandamizwa na vijana. Wanawake waliona kwamba ule wakati wa kurejeshewa haki zao umewadia. Watumwa wakaona kwamba wakati wao wa kupata uhuru ulikuwa umefika na vijana wakaona kwamba fursa za maendeleo sasa zinaelekea kuwekwa peupe kwa ajili yao. Pale dharau zilipoanza kugeuka na kuwa ukubalifu na hali ya kutojali kugeuka kuwa upendo, hapo machifu wa Makka na wasimamizi wakaanza kutishika. Wakakusanyika na kushauriana. Wakaamua kwamba kejeli tupu hazikuwa mbinu tosha za kukabiliana na tishio hili. Rekebisho kabambe zaidi lilihitajika. Mkumbo huu mpya ni sharti ukomeshwe kwa mabavu. Iliamuliwa kwamba mateso na namna fulani ya msusio havina budi kuanzishwa. Mara haya yote yalianzwa kutekelezwa kwa vitendo, na Makka ikakabiliana na Islam katika mzozo mkubwa. Mtume[saw] na wafuasi wachache hawakuchukuliwa tena kuwa ni wendawazimu, bali mkumbo unaokua ambao, endapo utaachiliwa kustawi bila ya kizuizi, utakuja kuwa hatari kwa dini, hadhi, desturi na mapokeo ya watu wa Makka. Islam ilitishia kung'olea mbali mapangilio ya zamani ya jamii ya Makka na kujenga upya, ili kuunda mbingu mpya na ardhi mpya, ambavyo ujaji wao ni sharti umaanishe kupotelea mbali kwa mbingu ya zamani ya Arabuni na dhati yake ya kale. Watu wa Makka hawakuweza tena kuicheka Islam. Hili sasa lilikuwa ni swali la kufa na kupona kwa ajili yao. Islam ilikuwa ndiyo changamoto yenyewe na watu wa Makka wakakalia chonjo changamoto hii, jinsi maadui za Manabii ambavyo daima wamezikalia chonjo changamoto za Manabii wao. Waliamua kutoikabili hoja kwa hoja bali kuchomoa upanga na kuyanyamazisha mafundisho hatari

kwa mabavu; wala sio kujibu mfano mzuri wa Mtume[saw] na wafuasi wake kwa mifano yao wenyewe, wala kujibu kwa kauli njema mfano wake, bali kuwadhulumu na kuwatukana wale waliotoa kauli ya huruma. Kwa mara nyingine tena humu duniani upinzani ukaanza baina ta dini na ukafiri, majeshi ya Shetani yakawatangazia malaika vita. Waaminio, wakiwa bado ni wachache, hawakuwa na nguvu za kukabiliana na mashambulio na ukali wa makafiri. Harakati za kikatili kupindukia zikapamba moto. Wanawake wakauawa bila soni zozote. Wanaume wakauawa. Watumwa waliosema wanamwamini Mtume[saw] walibururwa kwenye mchanga wenye moto na juu ya mawe. Ngozi za miili yao zikapatwa na hali ya kuwa sugu chambileche zile za wanyama. Muda mrefu baadaye ilipokuwa Islam imestawika maeneo ya mbali na karibu, mmoja wa hawa Waislamu wa awali aliyeitwa Hadhrat Khabbaab bin Al-Aratt[ra] aliwaonyesha mwili wake. Marafiki zake waliona ngozi yake ikiwa hali sugu chambileche ile ya wanyama na wakamuuliza ilkuwa-kuwaje. Hadhrat Khabbaab[ra] akatabasamu na akasema si lolote wala si chochote, bali kumbukumbu tu ya zile zama ambapo watumwa waliosilimu walibururwa kwenye barabara za Makka juu ya mchanga wenye moto na mawe (Musnad, J. 5, uk. 110)

Watumwa waliosilimu walitokana na jamii zote. Hadhrat Bilal[ra] alikuwa Mwafrika, Hadhrat Suhaib[ra] alikuwa ni Mgiriki. Walikuwa wafuasi wa dini mbalimbali. Hadhrat Jabr na Suhaib[ra] walikuwa Wakristo, Hadhrat Bilal na Ammaar[ra] walikuwa ni waabuduo masanamu. Bilal alilazwa juu ya mchanga wenye moto, akalundikiwa mawe na vijana wakaambiwa warukeruke juu ya kifua chake, na mfugaji wake kwa jina Umayya bin Khalf alimtesa vile na kisha akamwamuru kumkana Allah na Mtume Wake[saw] na kuitukuza miungu ya watu wa Makka, Laat na Uzza. Lakini Bilal akashikilia tu kusema *Ahad, Ahad...* (Mungu ni Mmoja).

Kwa ghadhabu kubwa, Umayya akamtoa Hadhrat Bilal[ra] kwa wahuni wa mabarabarani, akiwaambia wamtie kamba shingoni na kumburura katika barabara za mji kwenye mawe. Mwili wa Hadhrat Bilal[ra] ukavuja damu, lakini yeye akazidi kutamka *Ahad, Ahad...* Nyumaye, wakati

Waislamu walipokaa mjini Madina na wakaweza kuishi na kuabudu katika mazingara kidogo yenye amani, Mtume Mtukufu[saw] alimfanya Hadhrat Bilal[ra] kuwa Mwadhini, yaani mwitaji rasmi wa wasalihina kwenye Sala. Akiwa Mhabeshi, Hadhrat Bilal[ra] hakuweza kutamka ile herufi (h) ya neno la Kiarabu Ash-hadu (nashuhudia). Waislamu wa Madina wakamcheka kwa taksiri ya matamshi yake, lakini Mtume[saw] akawakaripia na kuwaambia ni jinsi gani Hadhrat Bilal[ra] alivyokuwa kipenzi cha Mwenyezi Mungu kwa ile Imani thabiti aliyoonesha chini ya mateso ya watu wa Makka. Hadhrat Abu Bakr[ra] alimkomboa Hadhrat Bilal[ra] na watumwa wengine wengi na kusababisha kuachiliwa kwao huru. Miongoni mwao alikuwa ni Hadhrat Suhaib[ra], mfanyabiashara tajiri, ambaye Makureishi waliendelea kumtaabisha hata baada ya kukombolewa kwake. Wakati Mtume Mtukufu[saw] alipouhama mji wa Makka kwenda kuishi Madina, Hadhrat Suhaib[ra] alitaka kuandamana naye. Lakini watu wa Makka walimkataza. Walitoa pingamizi wakisema kwamba hawezi kuchukua utajiri aliouchumia Makka. Hadhrat Suhaib[ra] akakata shauri kuachilia mbali utajiri wake wote na mali na akawauliza watu wa Makka kama wangelikubaliana naye na kumruhusu ahamie Madina. Watu wa Makka wakakubali. Hadhrat Suhaib[ra] alifika Madina akiwa mikono mitupu na akaonana na Mtume[saw] aliyesikiza kisa chake na kumpongeza sana, akimwambia, "Hiyo ndiyo biashara bora zaidi maishani mwako".

Wengi wa watumwa hawa waliosilimu waliendelea kuwa thabiti nje na ndani katika kuiamini dini. Lakini baadhi yao walikuwa na nyoyo dhaifu. Safari moja Mtume Mtukufu[saw] alimkuta Hadhrat 'Ammaar[ra] akilia kwa maumivu huku akijipangusa machozi. Alipokabiliwa na Mtume[saw], Hadhrat 'Ammar[ra] alisema kwamba alikuwa amepigwa na kulazimishwa kuritadi. Mtume[saw] akamwuliza., "Lakini je, wewe mwenyewe ulikuwa umeamini kwa dhati?" Hadhrat 'Ammaar[ra] akasema naam, na hapo Mtume[saw] akamwambia kwamba Mwenyezi Mungu angelimsamehe udhaifu wake.

Hadhrat Yaasir na Hadhrat Sumayya, wazazi wake Hadhrat 'Ammaar, nao pia waliteswa na makafiri. Safari moja katika kisa cha

mateso hayo, ikatokea kwamba Mtume[saw] alikuwa akipita karibu nao. Akiwa na huzuni, Mtume[saw] akatamka akisema, "Enyi familia ya Yaasir, stahamilini kwani Mwenyezi Mungu amewaandalieni Pepo". Kauli hii ya kitume ikatimia punde tu baadaye. Hadhat Yaasir[ra] akafa kwa mateso yale, na baadaye kidogo Abu Jahl akamuua Hadhrat Sumayya kwa mkuki.

Mjakazi Zunaira akapoteza macho yake kwa kuteswa kikatili na makafiri. Hadhrat Abu Fukaih[ra] mtumwa wa Safwan bin Umayya, alilazwa kwenye mchanga wenye moto huku kifuani mwake amewekelewa mawe mazito yenye moto, na kutokana na uzito huo ulimi wake akachomoka nje.

Watumwa wengine waliteswa vivyo hivyo.

Ukatili huu haukuvumilika. Lakini waaminio wa hapo awali waliuvumilia kwa sababu nyoyo zao ziliimarishwa kwa matumainisho yaliyopokelewa kila siku toka kwa Mwenyezi Mungu. Kurani ilimshukia Mtume[saw], lakini matumainisho ya kauli ya Mwenyezi Mungu yaliwashukia waaminio wote. Kama isingelikuwa hivyo, waaminio wasingeliweza kuustahimilia ule ukatili waliofanyiwa. Wakiwa wamegomewa na wanadamu wenzao, marafiki na ndugu, wao hawakuwa na yeyote pamoja nao ila Mwenyezi Mungu, nao hawakujali kama walikuwa na yeyote mwingine. Kwa sababu Yake Yeye, ukatili wote haukuonekana kuwa ni chochote, matusi yakasikika kana kwamba ni dua na mawe kuonekana kana kwamba ni hariri.

Hata wananchi waungwana waliosilimu hawakupunguziwa ukatili. Wazee wao na machifu waliwaudhi kwa njia nyingine. Hadhrat Uthman[ra] alikuwa na Umri wa miaka arubaini na alikuwa tajiri; hata hivyo wakati Makureishi walipoamua kuwafanyia Waislamu ukatili kwa jumla, ami yake Hakam, alimtia kamba na akampiga. Hadhrat Zubair bin al-'Awwaam[ra], kijana shujaa ambaye baadaye alikuja kuwa jemadari mkubwa, alikunjiwa ndani ya jamvi na ami yake, akafukizwa moshi na kuteswa kwa kutopata hewa safi. Lakini yeye hakuritadi abadan. Naam, alikuwa amegundua Ukweli wala hakutaka kuutupilia mbali.

Hadhrat Abu Dharr[ra], wa kabila la Ghifaar, alisikia habari za Mtume[saw] na akaenda Makka kufanya uchunguzi. Watu wa Makka wakamshawishi, wakisema kwamba wao walimfahamu Muhammad vizuri sana na kwamba Jumuiya yake ilikuwa ni kujitafutia makuu tu. Hadhrat Abu Dharr[ra] hakuridhika; hapo akafululiza moja kwa moja hadi kwa Mtume[saw] kasikia Ujumbe wa Islam kutoka kwake mwenyewe na akasilimu. Hadhrat Abu Dharr[ra] akataka kujua kama angeweza kulificha kabila lake imani yake. Mtume[saw] akasema angeweza kufanya hivyo kwa siku chache. Lakini alipokuwa akitembea kwenye barabara za Makka akasikia kundi la machifu wa Makka wakimtusi Mtume Mtukufu[saw] na kumfanyia shutuma mbaya. Hakuweza kuficha imani yake, na akatangaza mara moja akisema: "Nashuhudia kwamba hapana Mungu ila Allah, na kwamba hapana afananaye na Allah; na Muhammad ni Mtumishi na Mtume Wake". Tangazo hili lililotolowa katika mkusanyiko wa makafiri lilionekana kwao kuwa ni ufidhuli mtupu. Waliinuka kwa hasira na kumpiga vibaya hadi akaanguka chini akizirai. Amiye Mtume[saw], Abbas, akiwa bado hajasilimu, akapita karibu nao na kuanza kuwaonya kwa niaba ya mshambuliwa wao akiwaambia, "Misafara yenu ya vyakula hupitia kwenye kabila la Abu Dharr, na wakikasirishwa na vile mlivyomtendea wanaweza wakawafanyeni mfe kwa njaa". Keshoye Hadhrat Abu Dharr[ra] akashinda nyumbani kwao. Lakini siku iliyofuatia akarudi tena kwenye mkusanyiko ule ule na akawakuta wakimtukana Mtume Mtukufu[saw] kama pale juzi. Alikwenda hadi kwenye Kaaba na akakuta watu wakifanya vivyo hivyo. Hakuweza kustahamili, alisimama na akapiga ukelele akitangaza imani yake. Kwa mara ya tena akapigwa sana. Ilitokea vivyo hivyo mara ya tatu, na Hadhrat Abu Dharr akarudi kwa kabila lake.

Mtume Mtukufu[saw] mwenyewe hakubakizwa nje ya mateso makali waliyoonjeshwa Waaminio. Safari moja alikuwa salani. Genge la makafiri likamzungushia shuka shingoni mwake na kumburura; macho yake yakawa kwamba yanajichomoa nje. Hadhrat Abu Bakr[ra] akatokea kufika mahali pale na akamwokoa, huku akitamka akiwaambia,

"Mwataka kumuua, eti kwa sababu yuasema, "Mungu ndiye Bwana wangu?" Safari nyingine alipokuwa akisujudu katika sala nao wakamwekelea mgongoni kondo ya nyuma ya ngamia aliyezaa. Mtume[saw] hakuweza kuinuka hadi uzito ule ulipoondolewa mbali. Bali safari nyingine alikuwa akijipitia kwenye barabara na genge la vijana likamfuata. Wakaendelea kumchapa shingoni huku wakiwaambia watu kwamba anajiita Nabii. Hivyo ndivyo lilivyokuwa wingu la chuki na uhasama dhidi yake, na hivyo ndivyo ulivyokuwa upweke wake.

Nyumba ya Mtume[saw] ilivurumishiwa mawe kutoka nyumba za jirani. Takataka na uchafu wa wanyama waliochinjwa vilitupwa mwake jikoni. Mara nyingi sana alirushiwa mavumbi alipokuwa akisali hivi kwamba ilimbidi atafute mahali salama pa kusalia sala zake za jamaa.

Ukatili uliotendwa dhidi ya kundi lisilokuwa na makosa pamwe na Kiongozi wao mwaminifu, mwenye nia safi lakini bila ya msaidizi, haukupotezwa bure. Watu waungwana waliyaona haya yote na ikawa wao kuvutiwa kwenye Islam. Safari moja Mtume[saw] alikuwa akijipumzikia kwenye kilima cha Safaa kilicho karibu na Kaaba. Abu Jahl, chifu wa Makka na adui mkubwa wa Mtume[saw], akapita karibu na pale na kuanza kumtupia matusi machafu. Mtume[saw] hakusema chochote na akajiendea zake nyumbani. Mjakazi mmoja wa nyumbani kwake aliyashuhudia haya yote. Hamza, amiye Mtume[saw], mtu shujaa aliyeogopewa mjini na wakazi wenzake, akatokea kurejea nyumbani kutoka mbugani alikokwenda kuwinda na kuingia kwa vishindo nyumbani mwake, huku upinde wake ukimning'inia begani. Yule mama mjakazi alikuwa bado hajasahau kilichotendeka asubuhi. Akaudhika kwa kule kumwona Hamza akiingia nyumbani kwa vishindo sampuli ile. Basi akamtania, akimwambia, 'Unajifikiria kuwa mtu shujaa na kutembea na silaha lakini hufahamu kile Abu Jahl alichomtendea hapo asubuhi mpwao asiyekuwa na makosa." Hamza akasikia habari za kile kisa cha asubuhi. Japo hakuwa mwaminio, lakini alikuwa mwungwana mwenye tabia njema. Pengine alikuwa amevutiwa na Ujumbe wa Mtume[saw], lakini sio sana kiasi cha kujiunga naye kidhahiri shahiri. Aliposikia ukorofi huu wa Abu Jahl,

hakuweza kuvumilia. Hali yake ya kuusitiasitia ule Ujumbe mpya ikamtoka. Akaanza kuona kwamba hadi kufikia pale hakuwa akiutilia maanani vilivyo. Akafululiza moja kwa moja hadi kwenye Kaaba, ambako machifu wa Makka walipenda sana kukutana na kubarizi. Akashika upinde wake na kumchapa nao Abu Jahl. Akatamka akimwambia, "Tangu leo nihesabu miongoni mwa wafuasi wa Muhammad[saw]. Ulimtukana leo asubuhi kwa vile yeye asingelisema chochote. Kama u mwanaume, basi inuka na tupambane". Abu Jahl akafungwa kinywa. Marafiki zake wakasimama kutaka kumsaidia, lakini Abu Jahl kwa kumwogopa Hadhrat Hamza[ra] na kabila lake, akawazuia, akichelea kwamba vita sampuli hiyo vingelikuwa hasara tupu. Akakiri kwamba yeye ndiye aliyestahili lawama kwa kile kisa cha asubuhi (Hisham na Tabari).

UJUMBE WA ISLAM

Upinzani ulizidi kupamba moto. Wakati huo huo Mtume[saw] na wafuasi wake walikuwa wakifanya chini juu kuwabainishia watu wa Makka Ujumbe wa Islam. Ulikuwa ni Ujumbe wenye pande nyingi tena uliokuwa na maana kuu hapo hatimaye, sio kwa Waarabu tu bali kwa ajili ya dunia nzima. Huo ulikuwa ni Ujumbe utokao kwa Mwenyezi Mungu. Nao ulisema hivi:

> Muumba wa dunia ni Mmoja. Hapana mwingine apasaye kuabudiwa. Manabii daima wamemwamini kuwa yu Mmoja, na kuwafundisha wafuasi wao vivyo hivyo. Watu wa Makka hawana budi kuachilia mbali vinyago vyao na masanamu yao. Je, hawakuona kwamba masanamu yenyewe hata hayakuweza kufukuza nzi waliovamia zile sadaka zilizolundikwa pao miguuni? Ingekuwa washambuliwe, wasingeweza kujitetea. Ingekuwa waulizwe swali, wasingeweza kujibu. Ingekuwa waombwe msaada, wasingemudu lolote. Lakini Yule Mungu Mmoja aliwasaidia wale waliomwomba msaada Wake, aliwajibu wale waliomwomba katika sala, aliwadhalilisha maadui Zake, na kuwanyanyua wale walionyenyekea mbele Yake. Ilipokuja nuru

kutoka Kwake, iliwang'arisha waumnini Wake. Basi ilikuwaje watu wa Makka kutomjali na kugeukia vitu visivyokuwa hai na masanamu na kupoteza maisha yao? Je, hawakuona kwamba utovu wao wa imani juu ya Yule Mungu Mmoja wa Kweli ulikuwa umewafanya wawe washirikina wa kupindukia wasiomudu kitu? Hawakuweza kujua kilichokuwa safi na kilichokuwa kichafu, kunako wema na ubaya. Hawakuwastahi mama zao. Waliwatendea kishenzi dada zao na mabinti zao, na kuwanyima haki zao. Hawakuwatendea wake zao vilivyo. Waliwatesa wajane, kuwadhulumu mayatima, maskini na wanyonge, na kutafuta kujipatia utajiri wao kutokana na maangamio ya wengine. Kusema uwongo na kudanganya hawakukuonea aibu, wala kuiba na kupora mali za wengine. Kamari na ulevi ndizo zilizokuwa sherehe zao. Masilahi ya utamaduni na maendeleo ya kitaifa wao hawakuyajali. Ilikuwa waendelee kwa muda gani kumkatalia mbali Yule Mungu Mmoja wa Kweli, na kuzidi kuhasirika na tena kuhasirika, na kuzidi kuumia tena na tena? Si ilikuwa ni afadhali wajirekebishe? Je, haikuwa ni afadhali wao kuachilia mbali aina zote za kudhulumiana, watoe haki kwa wanaozistahili, watumie utajiri wao katika mahitaji ya kitaifa kuwasaidia waliokuwa maskini na wanyonge, wawachukulie mayatima kuwa ni kabidhi na kuwahifadhi kuwa ni jukumu lao, wawasaidie wajane na kuanzisha na kuipatia changamoto miradi mizuri katika umma wote, na kuhimiza sio tu kupatikana kwa haki na uadilifu, bali pia upendano na huruma? Inabidi maisha katika dunia hii kuzalisha wema. Ujumbe wa Islam ukaendelea kuhimiza ukiwaambia, "Acheni nyuma amali njema", kusudi zipate kuzaa matunda baada ya nyinyi kuitoka dunia hii. Wema halisi umo katika kuwapa wengine, wala sio katika kupokea kutoka kwao wao. Kuweni na tabia ya kujisalimisha kusudi muwe karibu na Mungu wenu. Jikinaini nafsi zenu kwa ajili ya wanadamu wenzenu, ili kwamba mjiongezee mizani yenu kwa Mwenyezi

> Mungu. Naam, Waislamu ni wanyonge, lakini nyinyi msiufuatilie unyonge wao, Ukweli utashinda. Huu ndio uamuzi wa mbinguni. Kwa njia ya Mtume[saw] kipimo kipya na kigezo kipya cha wema na ubaya, haki na batili, kitasimikwa duniani. Maadili na huruma vitazagaa. Hamtaruhusiwa karaha katika mambo ya dini, wala kujitia kati. Ule ukatili ambao wanawake na watumwa wameutendewa utafutiliwa mbali. Ufalme wa Mungu utasimikwa mahali pa ufalme wa Shetani".

Ujumbe huu ulipohubiriwa watu wa Makka, watu wenye nia njema na wenye kutafakari miongoni mwao walianza kuvutiwa nao, wakuu wa Makka wakayakalia chonjo yale yaliyokuwa yakitendeka. Wakatuma wajumbe kwa amiye Mtume[saw], Mzee Abu Talib, na wakamwabia hivi:

> Wewe u mmoja wa machifu wetu na kwa ajili yako hadi hivi sasa tumemwacha mpwao, Muhammad. Lakini sasa wakati umefika ambapo hatuna budi kuikomesha hatari hii ya kitaifa, ushindani huu miongoni mwetu. Twakutafadhalisha na kutaka kwamba aache kuyasema chochote masanamu yetu. Na aendelee tu kutangaza kwamba Mungu ni Mmoja, lakini asiseme chochote dhidi ya masanamu yetu. Akiyakubali haya, basi upinzani wetu na ubishi wetu na yeye utakwisha. Twakutafadhalisha wewe uende ukambembeleze. Lakini kama huwezi kufanya hivyo, basi mojawapo la haya mawili halina budi kutendeka. Ama itakubidi wewe umkatalie mbali mpwao, au sisi, watu wako, tukukatalie mbali wewe (Hisham).

Mzee Abu Talib akakabiliwa na chaguo gumu. Kumkatalia mbali mpwawe ilikuwa vigumu. Bali lilikuwa pia jambo gumu kwa yeye kukataliwa mbali na watu wake. Waarabu walikuwa na utajiri haba wa pesa. Hadhi yao ilikuwemo kwenye uongozi wao. Waliishi kwa ajili ya watu wao, hao nao wakaishi kwa ajili yao. Mzee Abu Talib alihuzunika sana. Akamwita Mtume[saw] na kumwelezea yale matakwa yaliyowasilishwa na wakuu wa Makka. Huku machozi

yakimlengalenga, Mzee Abu Talib akatamka akimwambia Mtume[saw], "Usipokubali, basi itanibidi mimi nikukatalie mbali la sivyo watu wangu watanikatalia mbali". Bila shaka Mtume[saw] alimhurumia ami yake. Machozi yalimlengalenga na akatamka akimwambia:

> "Mimi sikuambii uwaachilie mbali watu wako. Nakutaka usiniunge mkono. Badala yake, wewe nikatalie mbali na kuwaunga mkono watu wako. Lakini Yule Mungu Mmoja wa Pekee ni shahidi wangu ninaposema ya kwamba hata kama wanikabidhi jua mkono wangu wa kuume na mwezi mkono wa kushoto, mimi sitaacha asilan kuhubiri ukweli wa Yule Mungu Mmoja. Ni sharti niendlee kufanya hivyo hadi nitakapokufa. Wewe fanya utakavyo (Hisham na Zurqani).

Jibu hili, thabiti, halisi na nyofu, likayafumbua macho ya Mzee Abu Talib. Akatafakari sana. Ijapokuwa yeye hakuwa na ushujaa wa kuweza kusilimu, lakini yeye akajifikiria kuwa mwenye bahati kuweza kuishi na kujionea onesho hili tukufu la imani na uwajibikaji. Akamgeukia Mtume[saw] na akatamka akimwambia:

> "Ewe mpwa wangu, nenda zako. Tekeleza wajibu wako. Watu wangu wakinikataa, potelea mbali. Mimi niko pamoja nawe (Hisham).

KUHAMIA UHABESHI

Dhuluma zilipopindukia, Mtume[saw] aliwakusanya wafuasi wake, na huku akiashiria upande wa magharibi akawaelezea juu ya nchi ya ng'ambo ya pili ya bahari ambako watu hawauawi kwa sababu ya kubadili dini, wanakoweza kuabudu bila kubughudhiwa, na ambako kuna mfalme mwadilifu. Basi, na waende kule; huenda kubadili maskani kukawaletea faraja. Hapo kufuatana na nasaha hii, kundi la watu wake kwa waume na watoto, wakaenda Uhabeshi. Huu ulikuwa ni uhamiaji wa kiasi kidogo cha watu na wenye dhiki kubwa. Waarabu walijihesabu kuwa wao ndio walinzi wa Kaaba, na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Kuihama Makka kulikuwa kwao wao ni maumivu makubwa, hapakuwa na Mwarabu wa kuweza kufikiria kufanya hivyo

isipokuwa kama kuishi mjini Makka liwe lilikuwa ni jambo lisilowezekana abadan. Wala watu wa Makka hawakuwa tayari kuvumilia uhamaji sampuli hiyo. Wasingeliwaachilia wasumbuliwaji wao watoroke na kuwa na fursa angalau kidogo ya kuishi mahali pengine. Hivyo basi, wahamaji wale ikabidi wayaweke siri maandilizi ya safari yao na kuondoka bila ya kuagana na marafiki na ndugu zao. Hata hivyo, kuondoka kwao kumbe kulifahamiwa na baadhi ya watu bila kukosa kuwatia ngoa. Umar, ambaye baadaye alikujakuwa Khalifa wa pili wa Islam, alikuwa bado yu kafiri, adui mkali na mtesi wa Waislamu. Kwa bahati tu, akakutana na baadhi ya wahamaji hawa. Mmoja wa hawa alikuwa ni mwanamke, Hadhrat Ummi Abdullah[ra]. Umar alipoona vyombo vya nyumbani vimefunganywa na kutwishwa wanyama, alijua mara moja kwamba hao walikuwa ni watu waliokiihama Makka na kutafuta hifadhi penginepo. Akatamka akimwambia, "Ndio mwenda zenu hivyo?" Hadhrat Umm Abdallah[ra] akajibu akimwambia, "Naam, Wallahi twahamia nchi nyingine, kwa sababu nyinyi mwatutesa sana hapa. Sasa hatutarudi tena hadi pale Allah atakapokuwa radhi kuturahisishia jambo hili". Umar akaathirika na akatamka akiwaambia, "Mungu awe pamoja nanyi". Sauti yake ilikuwa na mahangaiko. Kisa hiki cha kimyakimya kilimhuzunisha. Watu wa Makka walipojua jambo hili, wakatuma genge la wasakaji. Genge hili likafikia ufuo wa bahari lakini wakakuta kwamba Waislamu tayari walikuwa wako merikebuni. Waliposhindwa kuwapata wakatuma genge hadi Uhabeshi wende kumchochea mfalme dhidi ya wale wahamiaji na kumshawishi awarudishe tena kwa watu wa Makka. Mmoja wa wajumbe hawa alikuwa ni Amr bin al-'Aas, ambaye baadaye alisilimu na akaiteka Misri. Ujumbe huu wa Makka ukafika Uhabeshi, ukakutana na mfalme na kuwachochea mawaziri wake. Lakini yule mfalme akatokea kuwa thabiti na, licha ya kushurutishwa na wale wajumbe wa Makka na mawaziri wake, yeye alikatalia mbali kuwarudisha Waislamu kwa watesaji wao. Ule ujumbe ukarejea Makka ukiudhika, lakini mjini Makka punde baadaye wakala njama mpya ya kulazimisha kurejeshwa kwa Waislamu kutoka huko

Uhabeshi. Miongoni mwa misafara iendayo Uhabeshi wakazagaza uvumi kwamba Makka nzima ilikuwa imesilimu. Uvumi huu ulipofika Uhabeshi, Waislamu wengi kwa furaha walirejea makwao huko Makka, lakini walipowasili wakagundua kwamba ule uvumi uliowafikia nchini Uhabeshi ni porojo tupu. Baadhi ya Waislamu wakarudi tena Uhabeshi lakini wengine wakakata shauri kukaa. Miongoni mwa walioamua kukaa alikuwemo Hadhrat Uthman bin Maz'uun[ra], mwana wa chifu mkubwa wa Makka. Hadhrat Uthman[ra] alipatiwa hifadhi na rafiki wa babake, Walid bin Mughira, na akaanza kuishi kwa amani. Lakini akawaona Waislamu wengine wakiendelea kutaabika kwa mateso ya kikatili. Jambo hili lilimhuzunisha sana. Akaenda kwa Walid na kutangua hifadhi yake. Alionelea kwamba yeye hakustahili kujipatia hifadhi kama ile ilihali Waislamu wengine waliendelea kuteseka. Walid akawatangazia watu wa Makka jambo hili.

Safari moja Labid, malenga mashuhuri wa Arabuni, aliketi pamoja na machifu wa Makka, akiwasomea beti zake. Akasoma mstari mmoja uliomaanisha neema zote mwishowe ni sharti zikome. Hadhrat Uthman[ra] kwa ujasiri mkubwa akamkosoa, na akatamka akimwambia, "Neema za peponi zitakuwa za milele". Yule mshairi Labid, ambaye hakuwa amezoea udadisi sampuli hii, akakasirika na akasema, "Imekuaje nyinyi Makureishi, wageni wenu hawakutusiwa kiasi hiki hapo mbeleni. Ulianzia wapi mtindo huu?" Ili kumtuliza Labid, mtu mmoja miongoni mwa wasikilizaji akasimama na kusema, "Endelea na usimjali huyu mpumbavu". Hadhrat Uthman[ra] akakazania kusema kwamba yeye hakuwa amesema chochote cha kipumbavu. Hili liliwakasirisha sana Makureishi waliomrukia Hadhrat Uthman[ra] na kumpiga dharuba moja kali iliyomng'olea mbali jicho moja. Walid alikuwepo pale. Yeye alikuwa ni rafiki wa karibu sana wa babake Hadhrat Uthman. Hakuweza kuvumilia kitendo cha namna ile kwa mtoto wa marehemu rafikiye Lakini Hadhrat Uthman[ra] hakuwa tena chini ya hifadhi yake na desturi za Kiarabu zilimzuia kuingilia kati. Hivyo basi, hakuwa na la kufanya. Akiwa na hasira na uchungu, alimgeukia Hadhrat Uthman[ra] na akasema, "Mtoto wa rafiki yangu,

ungenusurika hili jicho lako, kama usingetangua hifadhi yangu. Yakupasa uishukurie sana".

Hadhrat Uthman[ra] akajibu akisema:

> "Nimelitamani sana tukio hili. Mimi siombolezei kung'olewa jicho, kwani hili jingine lasubiri hayo hayo. Kumbuka, anapotaabika Mtume[saw], sisi hatutaki amani" (Halabiyya, J. 1, uk. 348).

UMAR YUASILIMU

Takriban wakati huu huu tukio jingine muhimu lilitukia. Umar, ambaye baadaye alikujakuwa Khalifa wa Pili wa Islam, alikuwa bado ni mmoja wa maadui wakali na walioogopewa sana wa Islam. Yeye alionelea kwamba zilikuwa bado kuchukuliwa hatua kabambe dhidi ya hii Jumuiya mpya na akakata shauri kumuulia mbali Mtume[saw]. Akashika upanga wake na kuelekea kwa Mtume[saw]. Rafiki yake mmoja akastaajabu kwa kumwona akienda vile na kumwuliza alikokuwa kaenda na alikuwa na shabaha gani. Umar akajibu akisema, "Naenda kumuulia mbali Muhammad".

Lakini yule rafikiye akadadisi akisema, je, wewe utakuwa salama kutokana na kabila lake baada ya hayo? Lakini je, wajua uhakika wa jinsi mambo yanvyokwenda? Je, wajua kwamba dadako na mumewe wamesilimu?"

Habari ilimjia Umar kana kwamba ni kipigo cha radi na kumkasirsha sana. Akakata shauri kwanza kwenda kuwamalizia mbali dadake na mumewe. Alipokuwa akikaribia nyumbani kwao akasikia kisomo kikiendelea mle ndani. Sauti yenyewe ilikuwa ni ile ya Hadhrat Khabbab[ra] aliyekuwa akiwafundisha Kitabu Kitakatifu. Umar akajipenyeza ndani haraka. Hadhrat Khabbab[ra] kwa kugutuashwa na vile vishindo tayari alikuwa amejificha. Dadake Umar, Hadhrat Fatima[ra] akazificha zile nyaraka za Kurani. Huku akiwakabili na mumewe, Umar akatamka akiwaambia, "Naskia mmeiacha dini yenu wenyewe", aliposema hivyo, akainua mkono wake ampige yule mume, aliyekuwa binamuye. Hadhrat Fatima[ra] akajiingiza kati baina

ya Umar na mumewe; na hivyo basi mkono wa Umar ukashukia usoni mwa Hadhrat Fatima[ra] na kumtwanga puani, mlimovuja damu mara moja. Dharuba yenyewe ikamzidisha Hadhrat Fatima[ra]'' ushujaa. Akasema, "Naam, sasa hivi tu Waislamu na tutadumu kuwa hivyo; fanya utakavyo". Umar alikuwa ni mtu shujaa licha ya kuwa mkali. Ule uso wa dadake uliojaa damu aliyoitiririsha kwa mkono wake yeye mwenyewe, ulimtia majuto. Punde si punde akabadilika. Akataka aoneshwe zila nyaraka za Kurani walizokuwa wakizisoma. Hadhrat Fatima[ra] akakataa kumwonesha akihofia huenda akazichanilia mbali. Umar akaahidi kutofanya hivyo. Lakini Hadhrat Fatima[ra] akamwambia hakuwa safi. Umar akakata shauri kuoga. Kisha huku akiwa safi na aliyepoa moto, akazishika zile nyaraka za Kurani mkononi mwake. Zilikuwa na sehemu ya Sura Twaa Haa. Na akafikia ile aya isemayo:

> "Kwa yakini Mimi ndiye Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye ile Mimi, basi uniabudu na usimamishe Sala kwa kunitaja. Bila shaka saa ile inakuja — karibu Nitaidhihirisha — ili kila nafsi ilipwe kwa yale iliyoyafanyia bidii (Twaa Haa, 20:15- 16).

Kule kutiliwa mkazo kwa kuwepo kwa Mwanyezi Mungu, ile ahadi bayana ya kuwa Islam hivi karibuni itasimika ibada halisi badala ya ile ibada iliyokuweko Makka — haya pamwe na mawazo mengine chungu nzima yanayohusikana nayo, bila shaka yalimvutia sana Umar. Hakuweza tena kujizuia. Imani ilimjaa moyoni na katamka akisema, "Yastaajabisha jinsi gani, yatumainisha kiasi gani!"; Hadhrat Khabbab[ra] akatoka mafichoni pake, na akatamka akisema, "Wallahi, ni jana tu nilipomsikia Mtume[saw] akiombea kusilimu kwa Umar au 'Amr ibn Hisham. Kubadilika kwako ni matokeo ya dua ile". Umar alikuwa ameshaikata shauri. Akataka kujua alikokuwa Mtume[saw] na akamfuata moja kwa moja kule Dari Arqam, huku upanga wake uliochomolewa ukiwa bado u mkononi. Alipokuwa akibisha hodi Masahaba wa Mtume waliweza kumwona Umar kupitia nyufa. Wakahofia asije akawa na dhamira mbaya. Lakini Mtume[saw] akasema, "Mwacheni aingie". Umar akaingia ndani, upanga mkononi.

Mtume[saw] akamwuliza akimwabia, "Ni nini kilichokuleta hapa?" "Ewe Mtume wa Mungu", Umar akajibu, "Mimi nimekuja hapa kusilimu". Mtume[saw] akapaaza sauti ya ***Allahu Akbar***. Masahaba nao wakaitikia kwa ***Allahu Akbar***. Vilima vya Makka vikavumisha Takbira hii. Habari za kusilimu kwa Hadhrat Umar[ra] zikasambaa haraka mno na tokea hapo yule Umar, mtesaji wa Waislamu aliyeogopewa, mwenyewe akaanza kuteswa pamoja na Waislamu wengine. Lakini Umar[ra] sasa alikuwa amebadilika. Akayafurahia kuteswa sasa kama vile alivyofurahia kutesa. Akapitisha maisha mjini Makka hali ya kuwa mtu aliyeteswa sana.

MATESO YAZIDI KUPAMBA MOTO

Mateso yalizidi kuwa makali na yakazidi kutovumilika. Waislamu wengi walikuwa wamehama Makka. Wale waliosalia nyuma ikawa wateseke kuliko wakati wowote hapo nyuma. Lakini katu Waislamu hawakutetereka hata chembe kutoka ile njia walioichagua. Nyoyo zao zilikuwa thabiti kama siku zote, imani yao shupavu. Mapenzi yao kwa Mungu Mmoja yalikuwa yanazidi na ndivyo zilivyokuwa zinazidi chuki zao dhidi ya yale masanamu ya kitaifa ya Makka. Upinzani ukawa mkali kuliko wakati wowote hapo nyuma. Watu wa Makka wakaitisha mkutano mwingine mkubwa. Katika mkutano huu wakaamua kuwasusia kabisa Waislamu. Watu wa Makka hawakuwa wafanye shughuli zozote zile na Waislamu. Hawakuwa wanunune chochote kutoka kwao wala kuwauzia chochote. Mtume[saw], ahali zake na baadhi ya nduguze ambao, ingawaje hawakuwa Waislamu bado walishirikiana naye, wakalazimika kwenda kutafuta hifadhi mahali pa upweke, miliki ya Mzee Abu Talib. Wakiwa bila ya pesa, bila njia yoyote wala akiba, familia ya Mtume[saw] na nduguze wakakumbwa na dhiki kubwa chini ya msusio huu. Kwa muda wa miaka mitatu ukashikiliwa uzi ule ule. Kisha hatimaye, waungwana watano miongoni mwa maadui wakakaidi hali hii. Wakaenda kwa familia iliyosusiwa na wakajitolea kuutangua ule msusio, na kuitaka ijitokeze. Mzee Abu Talib akajitokeza na kuwalaumu watu wake. Ukaidi wa wale watu watano ukajulikana Makka nzima, lakini nia njema

ikajitokeza tena, na watu wa Makka wakaamua kuumalizia mbali ule msusio. Msusio ukawa umekwisha, lakini sio athari zake. Baada ya siku chache Hadhrat Khadija[ra] mke mwaminifu wa Mtume[saw], akaaga dunia, na mwezi mmoja baadaye Mzee Abu Talib, amiye Mtume[saw] naye pia akafariki.

Mtume Mtukufu[saw] sasa akawa amepoteza uenzi na msaada wa Hadhrat Khadija[ra], na yeye pamoja na Waislamu wakawa wamepoteza wema wa Mzee Abu Talib. Kufa kwao pia kwa jumla kukawa na matokeo ya kupungukiwa na hali ya kuonewa huruma. Abu Lahab, ami mwingine wa Mtume[saw], mwanzoni alionekana kuwa tayari kushirikiana na Mtume[saw]. Majonzi ya kifo cha nduguye na hali ya kujali wasia wake ni mambo ambayo bado yalikuwa mapya moyoni mwake. Lakini punde si punde watu wa Makka wakafaulu kumhasimisha. Walitumia vile vivutio vya kawaida. Mtume[saw] alifundisha kwamba kutoamini Umoja wa Mungu lilikuwa ni kosa, lenye kuadhibika huko Ahera; mafundisho yake yalitofautiana na kila kitu walichokuwa wamejifunza kutoka kwa wakale wao, n.k.w.k. Hapo Abu Lahab akaamua kumpinga Mtume[saw] kuliko hapo awali. Uhusiano baina ya Waislamu na watu wa Makka ulikuwa umezorota. Msusio wa miaka mitatu na mazingiwa yalikuwa ni mambo yaliyozidisha kutengana kwao. Kukutana na kuhubiri yakaonekana kuwa ni mambo yasiyowezekana. Mtume[saw] hakuzijali dhuluma na mateso; haya yalikuwa si chochote mradi yeye alikuwa na fursa ya kukutana na watu na kuwahutubia. Lakini sasa ilionekana kwamba hakuwa na fursa kama hiyo mjini Makka. Achilia mbali uhasama wa kawaida, Mtume[saw] sasa alikiona ni kitu kisichowezekana kwake yeye kuonekana kwenye barabara yoyote au hadharani. Ikiwa alifanya hivyo basi wao walikuwa wakimtifulia mavumbi na kumrudisha tena kwake nyumbani. Safari moja alirejea nyumbani, kichwa kikimjaa mavumbi. Bintiye akalia alipokuwa akiyapangusa. Mtume[saw] akamwambia asilie kwani Mwenyezi Mungu Yu pamoja naye. Dhuluma hazikumuudhi Mtume[saw]. Bali yeye alizifurahia kama dalili ya watu kuvutiwa na Ujumbe wake. Siku moja, kwa mfano, watu wa

Makka kwa kula njama zao za kawaida hawakumsemesha chochote wala kumdhulumu kwa njia yoyote. Mtume[saw] alirejea nyumbani hali ya kuwa mtu aliyeudhika, hadi sauti ya Mungu yenye kutumainisha ilipomfanya awarejelee tena watu wake.

MTUME[SAW] YUAENDA TA'IF

Ilionekana kwamba mjini Makka sasa hakuwepo wa kumsikiliza na jambo hili lilimuhuzunisha. Alijihisi kuwa yuakwama. Hivyo, akaamua kwenda mahali pengine akahubiri Ujumbe wake, na akachagua Ta'if, mji mdogo takriban maili sitini kusini mashariki mwa mji wa Makka na uliokuwa mashuhuri kwa matunda yake na ukulima wake. Uamuzi huu wa Mtume[saw] uliambatana na suna ya Mitume wote. Naam, Nabii Musa[as] mara alimwendea Firauni, mara Waisraeli, na mara Wamidiani. Naye Yesu hali kadhalika, mara aliigeukia Galilaya, mara maeneo ya ng'ambo ya pili ya mto wa Yordani, na mara mji wa Yerusalemu. Kwa hiyo Mtume Mtukufu[saw] wa Islam, kuona kwamba watu wa Makka watatesa na sio kusikiza, akaigeukia Ta'if. Katika uwanja wa kuamini miungu wengi, mji wa Ta'if haukuwa nyuma ya mji wa Makka. Yale masanamu yaliyopatikana ndani ya Kaaba hayakuwa hayo tu, wala sio kwamba yaliyokuwa peke yao masanamu muhimu, nchini Arabuni. Sanamu moja mashuhuri, lililoitwa al-Lat, lilipatikana pia huko Ta'if; kwa sababu yeke mji wa Ta'if nao pia ulikuwa ni mahali pa haji ya makafiri. Wakazi wa Ta'if walikuwa ndugu moja na watu wa Makka; na mashamba mengi baina ya Ta'if na Makka yalimilikiwa na watu wa Makka. Alipowasili Ta'if, Mtume[saw] alitembelewa na machifu wa kule lakini hakuwepo hata mmoja wao aliyeonesha ishara za kukubali Ujumbe wake. Wakazi wote wakubwa kwa wadogo waliwatii viongozi wao na kuyakatalia mbali mafundiaho yake kwa dharau. Hili halikuwa jambo lisilokuwa la kawaida. Watu walioziinamia shughuli za kidunia daima huchukulia Ujumbe sampuli hiyo kana kwamba ni kuingilia mambo yao na hata kuwa kana kwamba ni uhalifu wenyewe. Kwa kuwa Ujumbe hauna msaada wa kidhahiri — kama vile majeshi na silaha — wao pia hujiona kwamba wanaweza wakaukatalia mbali

kwa dharau. Mtume[saw] wala hakuwa tofauti. Habari zake tayari zilikuwa zimefika Ta'if, na sasa yeye mwenyewe alikuwa huko huko, bila ya silaha wala wafuasi, mtu mmoja akiandamana na mwenzake mmoja, Hadhrat Zaid[ra]. Wakazi wa mjini wakamchukulia kuwa udhia mtupu usiokuwa na budi kukomeshwa, huenda machifu wakafurahi. Wakawaamrishia wahuni na machokora wao wa mjini waliompiga mawe na kumtupa nje ya mji. Hadhrat Zaid[ra] akajeruhiwa na Mtume[saw] akaanza kuvuja damu nyingi. Lakini ukimbizaji haukukoma hadi wanyonge hawa wawili walipokuwa maili kadha nje ya Ta'if. Mtume[saw] alijawa na majonzi na kuhuzunika sana alipomshukia malaika na kumuuliza kama angelitaka watesaji wake waangamizwe. Mtume[saw] akasema, "La hasha". "Natumainia kwamba watazaliwa kutokana na washambuliaji hawa hawa wale watu watakaomwabudu Mungu Mmoja" (Bukhari. Kitab Bad'ul-Khalq).

Akiwa mchovu na aliyejawa na huzuni, akasimama katika shamba moja la mizabibu, mali ya watu wawili wa Makka waliokuwepo. Walikuwa ni miongoni mwa watesaji wake mjini Makka lakini safari hii wakawa na huruma. Je, ilikuwa ni kwa sababu mwenyeji mwenzao wa Makka katendewa mabaya na watu wa Ta'if, au ilikuwa kwa sababu nuru ya huruma ya kibinadamu ilikuwa kwa ghafla imewapenya nyoyoni? Walimpelekea Mtume[saw] sinia iliyojaa zabibu iliyobebwa na mtumwa Mkristo, jina lake Addaas, aliyekuwa mtu wa Ninawi. Addas akampatia ile sinia Mtume[saw] na mwenzake. Alipokuwa akiwatazama kwa matumaini, udadisi wake ukazidi kuliko hapo mwanzo alipomsikia Mtume[saw] akisema, "Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu". Ukristo wake ukahuika na akajiona kana kwamba yu mbele ya Nabii wa Kiebrania. Mtume[saw] akamuuliza alikotoka na akasema Ninawi, na hapo Mtume[saw] akatamka akisema; "Yunus, mwana wa Amittai, mwenyeji wa Ninawi, alikuwa ni mtu mtakatifu, Nabii kama mimi". Mtume[saw] pia akmwelezea Addas Ujumbe wake yeye mwenyewe. Addas akavutika na kukubali mara moja. Akamkumbatia Mtume[saw] huku machozi yakimlengalenga na kuanza kumbusu kichwani, mikononi

na miguuni. Kukamalizika kukutana kwao, na Mtume[saw] akamgeukia Allah kwa mara ya tena na akatamka akisema:

> Ee Allah, maombolezo yangu nayaelekeza Kwako. Mimi ni mnyonge wala sina uwezo. Watu wangu wananidharau. Wewe ndiwe Mola wa wanyonge na maskini na Wewe ndiwe Mola wangu. Utaniachia akina nani — watu tusiozoeleana nao wanaonizoza au yule adui anitaabishaye kwetu mjini? Kama Wewe hukunikasirikia, basi mimi simjali adui yangu. Huruma Yako na iwe juu yangu. Najikinga kwenye nuru ya uso Wako. Ni Wewe tu Uwezaye kuliondolea mbali giza duniani na kuwapatia wote amani, hapa na ahera. Na isinishukie hasira Yako wala adhabu Yako. Wewe hughadhabiki isipokuwa uwe mara unafurahika. Na hapana nguvu wala hifadhi ila Kwako (Hisham na Tabari).

Baada ya kuomba dua hii, akashika njia kurudi Makka. Njiani akasimama kwa siku kadha mahali paitwapo Nakhla na akashika njia tena. Sawa na desturi za watu wa Makka yeye hakuwa tena mwenyeji wa Makka. Alikuwa ameihama Makka kwa sababu aliichukulia kuwa ni adui na asingeliweza kurudi kule bila ya ruhusa ya watu wa Makka. Hivyo basi, akapeleka ujumbe kwa Mut'im bin 'Adii — chifu mmoja wa Makka, kutaka kujua kama watu wa Makka wangemruhusu kurejea. Huyu Mut'im ingawaje alikuwa mkali kama adui mwinginewe, alikuwa na utu wa moyo. Akawaita wanawe na jamaa zake. Wakiwa wamejihami kwa silaha zao, wakaenda Kaaba. Akisimama kwenye uwanja wa Kaaba akatangaza akisema kwamba yeye anamruhusu Mtume arejee. Hapo Mtume[saw] akarejea na akaitawafu Kaaba. Hapo Mut'im, wanawe na jamaa zake, panga zao zimechomolewa, wakampeleka Mtume[saw] nyumbani kwake. Hiyo haikuwa ni ile hifadhi ya desturi ya Kiarabu Mtume[saw] aliyokuwa amepatiwa na Mut'im. Mtume[saw] aliendelea kutaabishwa na Mut'im hakumlinda. Alivyofanya Mut'im ilikuwa kutangaza ruhusa rasmi kwa Mtume[saw] kurejea. Safari ya Mtume[saw] ya huko Ta'if imeleta sifa hata kutoka kwa maadui wa Islam. Sir William Muir akielezea safari hii

katika kitabu chake kiitwacho "Life of Muhammad" (Maisha ya Muhammad) yuaandika akisema:

> Imo fahari na ushujaa katika safari hii ya Muhammad ya kwenda Ta'if; mtu mpweke, aliyedhrauliwa na kukataliwa na watu wake, kusafiri kwa ujasiri katika jina la Mungu, chambileche Yona kwenda Ninawi, na kuutolea wito mji uabuduo masanamu utubu na kuunga mkono wadhifa wake. Yaonesha wazi uthabiti wa imani yake juu ya chimbuko la kimbinguni la wadhifa aliokuwa nao (Life of Muhammad by Sir W. Muir, toleo la 1923, uk.112-113).

Makka ikarejelea uhasama wake wa zamani. Mji huu wa nyumbani wa Mtume[saw] ukawa moto tena kwa ajili yake. Lakini yeye aliendelea kuwaambaia watu wake Ujumbe wake. Ile shahada ya kuwa "Mungu ni Mmoja", ikaanza kusikika hapa na pale. Kwa mapenzi na makini, na kwa moyo wa kidugu, Mtume[saw] akakazania uelezeaji wa Ujumbe wake. Watu walimpa kisogo lakini yeye akawahutubia tena na tena. Akatangaza imani yake, haidhuru watu wakimjali au wasimjali, na kukazana kwake kukaelekea kuzaa matunda. Kile kikundi cha Waislamu waliokuwa wamerejea kutoka Uhabeshi na ambao walikuwa wameamua kuendalea kukaa Makka, kisirisiri wakahubiria marafiki zao, majirani na ndugu zao. Baadhi ya hawa walishawishiwa kujitangaza hadharani na kutaabika pamoja na Waislamu wengine. Lakini wengi, ingawaje walishawishika nyoyoni, hawakuwa na ujasiri wa kukiri hadharani; wakingojea ufalme wa Mungu ushuke ardhini.

Wakati huo huo wahyi uliopokewa na Mtume[saw] ulianza kudokezea uwezekano wa hivi karibuni wa kuhajiri kutoka Makka. Fununu za pale mahali ambapo walikuwa wahajirie pia nazo akafikishiwa. Ulikuwa ni mji wenye visima na viunga vya mitende. Mtume[saw] ukaudhania mji wa Yamama. Lakini punde si punde fikara hiyo ikatoweka. Kisha yeye akasubiri akiwa na hili hakikisho kwamba popote pale wangeilipokwenda basi bila shaka hapo pangekuwa ni kitovu cha Islam.

ISLAM YAENEA HADI MADINA

Haji ya kila mwaka ikakaribia, na kutoka kila pembe ya Arabuni mahujaji wakaanza kuwasili Makka. Mtume[saw] akaenda kila alipoona kikundi cha watu, kawaeleza imani ya Mungu Mmoja na kuwanasihi watupilie mbali aina zote za upitaji kiasi na kujiandaa kwa Ufalme wa Mungu. Baadhi yao walimsikiliza na wakavutika. Wengine walitaka kumsikiliza lakini wakafukuziliwa mbali na watu wa Makka. Wengine ambao tayari walikuwa wamekata shauri wakaacha kudhihaki. Mtume[saw] alikuwa kwenye bonde la Minaa alipoona kikundi cha watu sita au saba. Akagundua kwamba wao walikuwa ni wa kabila la Khazraj, lililokuwa na urafiki na Mayahudi. Akawauliza kama wangesikiza atakachokisema. Wao walikuwa wamepata habari zake na walivutiwa; hivyo wakakubali. Mtume[saw] akatumia muda fulani akiwaambia kwamba Ufalme wa Mungu ulikuwa umewadia kwamba masanamu yatatoweka, kwamba imani ya Mungu Mmoja itapata ushindi, na unyofu na uaminifu ulikuwa ni hali zitakazostawi kwa mara ya tena. Je, wao huko Madina, wasingeliupokea Ujumbe huo? Kikundi kile kikavutika sana. Wakaupokea Ujumbe, na wakaahidi watakaporejea Madina, kuzungumza na wengine na kuripoti mwakani kama Madina itakuwa tayari kupokea Waislamu wahamiaji kutoka Makka. Wakarejea makwao na kushauriana na marafiki na jamaa zao. Huko Madina wakati ule, yalikuweko makabila mawili ya Waarabu na matatu ya Mayahudi. Makabila ya Waarabu yalikuwa ni Aus na Khazraj na yale ya Mayahudi yalikuwa ni Banu Quraidha, Banu Nadhiir, na Banu Qainuqaa‘. Makabila ya Aus na Khazraj yalikuwa na vita. Makabila ya Quraidha na Nadiir yalikuwa marafiki wa kabila la Aus na lile la Qainuqaa‘ lilikuwa na urafiki na Khazraj. Wakiwa wamechoshwa na vita visivyokuwa na mwisho, walielekea kutafuta amani. Mwishowe wakakubaliana kumtambua chifu wa kabila la Khazraj, Abdullah bin Ubayy bin Salul, kama Mfalme wa Madina. Watu wa makabila ya Aus na Khazraj walikuwa wamesikia kutoka kwa Mayahudi, bishara katika Biblia. Walikuwa wamesikia visa vya Kiyahudi juu ya kupotea kwa fahari ya Israel na juu ya ujaji

wa Nabii "mfano wa Musa". Ujaji huu ulikuwa umewadia, ndivyo Mayahudi walivyokuwa wakisema. Ulikuwa waja kuashiria kurejeshwa Israeli mamlakani na kuangamizwa kwa maadui zao. Watu wa Madina waliposikia habari za Mtume[saw] waliingiwa na shauku na wakaanza kutaka kujua kama huyu Mtume wa Makka hakuwa ni yule Nabii waliyekuwa wamemsikia kutoka kwa Mayahudi. Vijana wengi wakamwamini mara moja. Haji iliyofuatia watu kumi na wawili kutoka Madina walikuwa Makka kujiunga na Mtume[saw]. Kumi miongoni mwao walitoka katika kabila la Khazraj na wawili kutoka kabila la Aus. Walikutana na Mtume[saw] katika bonde la Minaa na, huku wakiushika mkono wa Mtume[saw] wakaeleza kwa makini imani yao juu ya Umoja wa Mungu na nia yao ya kujiepusha na maovu yote ya kawaida, pamoja na kuwaua watoto wachanga, na kutupiana lawama zisizokuwa za kweli. Pia wakaamua kwamba watamtii Mtume[saw] katika mambo yote mema. Waliporejea Madina, wakaanza kuwapasha wengine habari za Imani yao Mpya. Jazba zikaongezeka. Masanamu yakachomolewa nje ya vishubaka vyao na kutupiliwa mbali mabarabarani. Wale waliozoea kuinamia vinyago sasa vichwa vikawasimama wima. Wakakata shauri kutomwinamia yeyote minghairi ya Mungu Mmoja. Mayahudi wakashangaa. Karne nyingi za urafiki, kuelezeana pamwe na mijadala hazikuwa zimefaulu kuleta yale mabadiliko aliyoyaleta huyu Mwalimu wa Makka katika siku chache tu. Ikawa watu wa Madina kuwaendea Waislamu miongoni mwao na kuuliza maswali juu ya Islam. Lakini wale Waislamu wachache hawakuweza kukabiliana na maswali chungu nzima, wala hawakujua Islam vya kutosha. Hivyo basi, wakakata shauri kumtafadhalisha Mtume[saw] awapelekee mtu akafundishe Islam. Mtume[saw] akakubali kumtuma Hadhrat Mus'ab[ra], mmoja wa wale Waislamu waliokuwa wamekwenda Uhabeshi. Hadhrat Mus'ab[ra] ndiye aliyekuwa mbashiri wa kwanza wa Islam kwenda nje ya Makka. Takriban wakati huu huu, Mtume[saw] alipata ahadi kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Aliona njozi ambapo alijikuta akiwa huko Yerusalemu na Manabii walikuwa wamejiunga nyuma yake katika sala

ya jamaa. Yerusalemu ilimaanisha Madina tu, ambao utakuja kuwa kitovu cha ibada ya Mungu mmoja. Manabii wengine kujiunga nyuma ya Mtume[saw] ilkuwa ni ishara iliyomaanisha kwamba watu wawafuatao Manabii mbalimbali watajiunga na Islam na Islam kuwa dini ya dunia nzima.

Hali mjini Makka sasa ilikuwa ni hatari kupindukia. Mateso yalikuwa yamegeuka na kuwa ya namna mbaya iwezekanavyo. Watu wa Makka waliidhihaki njozi hii wakiita eti tamaa tupu. Wao hawakuwa na habari kwamba misingi ya ile Yerusalemu mpya tayari ilikuwa imeisha simikwa. Mataifa ya Mashariki na Magharibi yalikuwa na hamu. Yalitaka kusikia Ujumbe wa Mwisho wa Mwenyezi Mungu. Katika siku zile zile Kaisari wa Urumi na Khosro wa Irani walipigana. Khosoro akashinda. Nchi za Siria na Palestina zikatekwa na majeshi ya Irani. Yerusalemu Ikaangamizwa. Misri na nchi za Asia ya Magharibi zikatawaliwa. Kwenye mlango wa bahari ya Bosfora, maili kumi tu kutoka mji wa Constatina, majenerali wa Irani waliweza kupiga mahema yao. Watu wa Makka wakafurahia ushindi wa Iran na wakasema eti hukumu ya Mungu ilikuwa imetolewa — waabuduo masanamu wa Irani walikuwa wamewashinda Watu wa Kitabu. Kwenye wakati ule ule Mtume[saw], alipokea wahyi ufuatao:

> Warumi wameshindwa katika nchi iliyo karibu; nao baada ya kushindwa kwao, watashinda katika miaka michache; Amri ni ya Allah kabla na baadaye; na siku hiyo waaminio watafurahi kwa msaada wa Allah; Humsaidia amtakaye; naye ni Mwenye nguvu, Mwenye rehema. (Hii ni) ahadi ya Allah. Allah havunji ahadi Yake, lakini watu wengi hawajui (Sura Ar-Ruumi, 30:3-7).

Bishara hii ilitimia katika muda wa miaka michache. Warumi wakawakomoa Wairani na kujinyakulia tena yale maeneo yaliyokuwa yamepotelea kwao. Ile sehemu ya bishara hii iliyosema., "siku hiyo waaminio watafurahi kwa msaada wa Allah", nayo pia ikatimia. Islam ilianza kupiga hatua. Watu wa Makka waliamini kwamba wao walikuwa wameitia komesha kwa kuwashawishi watu wasiwategee

sikio Waislamu bali waoneshe uadui mkali badala yake. Katika wakati huu huu Mtume[saw] alipokea kwenye wahyi wake habari za ushindi kwa ajili ya Waislamu, na kuangamizwa kwa watu wa Makka. Mtume[saw] akatangaza hizi aya zifuatazo:

> Na wanasema: Kwa nini hakutuleta Ishara kutoka kwa Mola wake? Je, haikuwafikia dalili wazi ya yale yaliyokuwa katika Vitabu vya kale? Na lau kama Tungaliwaangamiza kwa adhabu kabla yake (Mtume), wangesema: Ee Mola wetu, mbona hukutuletea Mtume tukazifuata Aya Zako kabla sisi kudhilika na kufedheheka? Sema: Kila mmoja anangoja, basi nanyi pia ngojeni; hivi karibuni mtajua ni nani mwenye njia iliyo sawa na ni nani aliyeongoka (Sura Twaa Haa, 20: 134-135).

Watu wa Makka walilalamikia utovu wa Ishara. Wakajibiwa wakiambiwa kwamba zile bishara juu ya Islam na Mtume[saw] zilizorekodiwa ndani ya vitabu vya hapo awali na ziwatoshe. Kama watu wa Makka wangeliangamizwa kabla ya Ujumbe wa Islam kuelezewa kwao, wangelilalamikia kutopatikana kwa fursa ya kuzitafakaria Ishara (za Mungu).

Ni sharti, hivyo basi, watu wa Makka wangoje.

Wahyi unaowaahidia waaminio ushindi na ushinde wa makafiri ulikuwa ukipokelewa kila siku. Watu wa Makka walipoangalia nguvu zao na utajiri, na unyonge na umaskini wa Waislamu, na kisha kusikia kila siku kwenye wahyi wa Mtume[saw] ahadi za msaada wa kimbinguni na ushindi wa Waislamu, wakashangaa na kushangaa. Je, wenyewe walikuwa wendwazimu au ni Mtume[saw] aliyekuwa mwehu? Walikuwa wakitumainia kwamba mateso yangewalazimisha kutupilia mbali imani yao na kurejea kwa watu wa Makka, na kwamba mwenyewe Mtume[saw] na wafuasi wake shupavu zaidi wangeanza kuingiwa na shaka juu ya madai yake. Lakini badala yake ikawa wao kusikiliza mahakikisho thabiti kama haya yafuatayo:

> Basi naapa kwa mnavyoviona na msivyoviona kwa hakika hii ni kauli ya Mtume mwenye heshima. Wala hiyo si kauli ya mshairi;

> ni kidogo tu mnayoyaamini; wala si kauli ya kahini; ni kidogo tu mnayoyajali. Ni uteremsho kutoka kwa Mola wa viumbe vyote. Na kama (Mtume) angelizua juu Yetu baadhi ya maneno, bila shaka tungelimshika kwa mkono wa kuume kisha kwa hakika tungelimkata mshipa mkubwa (wa moyo). Na hapana mmoja wenu ambaye angeweza kutuzuia naye. Kwa hakika (kauli hii) ni mauidha kwa wamchao Mungu. Na kwa yakini Tunajua ya kuwa miongoni mwenu wamo wanaokadhibisha. Lakini kwa kweli ni sikitiko juu ya wanaokataa. Na hasa hii ni haki kwa yakini. Basi litukuzwe jina la Mola wako Aliye Mkuu (Sura Al-Haaqqa 69:39-53).

Watu wa Makka walionywa kwamba matumaini yao yote ya moyoni yatavunjiliwa mbali. Mtume[saw] hakuwa mshairi, wala hakuwa kahini wala hakuwa mwenye kujifanya kuwa Mtume. Kurani ilikuwa ni kisomo kwa ajili ya wacha-Mungu. Naam, ilikuwa na wakataaji wake. Lakini ilikuwa pia na waridhiaji wake wa siri, wale walioyaonea wivu mafundisho yake na ukweli wake. Zile ahadi na bishara zilizomo ndani yake zote zitatimia Mtume[saw] aliambiwa kutojali upinzani wote na aendelee kumtukuza Mungu wake Mweza.

Haji ya tatu ikawadia. Miongoni mwa mahujaji kutoka Madina lilikuwemo kundi kubwa la Waislamu. Kwa sababu ya upinzani wa watu wa Makka, hawa Waislamu kutoka Madina wakataka kumwona Mtume[saw] kwa faragha. Mtume mwenyewe[saw] mawazo yake yalikuwa yakiigeukia Madina zaidi na zaidi, kama mahali pawezekanapo kuhamia. Akawajulisha jambo hili jamaa zake wa karibu, lakini wao walijaribu kumshawishi dhidi ya mawazo yote sampuli hii. Wakamtafadhalisha wakimwambia kwamba ijapokuwa Makka palikuwa pamejaa uadui, lakini pia palipatikana msaada wa jamaa zake kadha wenye uwezo. Matumainio ya Madina yote yalikuwa ya tashwishitashwishi, na endapo Madina patakuwa mahali hasimu kama vile Makka, ndugu zako wa Makka watawezaje kukusaidia? Hata hivyo, Mtume[saw] alikuwa na hakika kwamba hijira ya Madina ilikuwa imeamrishwa. Kwa hiyo, yeye aliukatalia mbali ushauri wa jamaa zake na akahajiri Madina.

AHADI YA KWANZA YA ‘AQABA

Baada ya usiku wa manane, Mtume[saw] alikutana tena na wale Waislamu kutoka Madina katika bonde la ‘Aqaba. Waislamu hao idadi yao ilikuwa watu sabini na watatu, ambao watu sitini na wawili miongoni mwao walikuwa wa kabila la Khazraj na kumi na mmoja kabila la Aus. Kundi hilo lilikuwa na wanawake wawili, mmoja akiwa ni Hadhrat Ummi Ammaara[ra] wa kabila Banu Najjar. Walikuwa wamefundishwa Islam na Hadhrat Mus‘ab[ra], nao walijaa imani na ushupavu. Wote wakatokea kuwa miamba ya Islam. Hadhrat Ummi ‘Ammaara[ra] ndio mfano wenyewe. Yeye aliingiza nyoyoni mwa watoto wake uaminifu usiokoma juu ya Islam. Mmoja wa wanawe, kwa jina Habib[ra], alichukuliwa mateka na Musailima kadhabu katika vita baada ya kufariki Mtume[saw]. Musailama akajaribu kufutilia mbali imani ya Hadhrat Habib[ra]. Akamwuliza akimwambia, “Wamwamini Muhammad kuwa ni Mtume wa Mungu? Hadhrat Habib[ra] akajilbu akisema, “Naam”. Musailama akamwuliza, “Je, waniamini mimi kuwa ni Mtume wa Mungu?” Jibu likawa “La hasha”. Kusikia hivyo, Musailama akatoa amri akatwe kiungo chake kimoja. Kilipokatwa, Musailama akamwuliza tena Hadhrat Habib[ra] akimwambia, “Wamwamini Muhammad kuwa ni Mtume wa Mungu?” Hadhrat Habib[ra] akajibu akisema, “Naam”. “Na mimi je, waniamini kuwa ni Mtume wa Mungu?” Jawabu likawa “La”. Musailama akaamrisha kikatwe kiungo kingine cha Hadhrat Habib[ra]. Basi kiungo baada ya kiungo kikakatwa kwa njia hii na mwili wa Hadhrat Habib[ra] ukageuzwa kuwa vipande chungu nzima. Naam, yeye alikufa kifo cha kikatili, lakini aliacha nyuma mfano usiosahaulika wa ushujaa wa kibinafsi na kujitoa kafara kwa ajili ya imani ya dini (Halabiyya, J. 2, uk. 17).

Hadhrat Ummi ‘Ammaara[ra] aliandamana na Mtume[saw] kwenye vita kadha.

Kwa neno zima, kundi hili la Waislamu wa Madina lilijichumia sifa kubwa kwa uaminifu wao na imani. Wao walikuja Makka lakini sio kwa ajili ya kujipatia utajiri, bali kwa ajili ya kujichumia imani; nao

wakajichumia imani maridhawa.

Mzee Abbas huku akiwa ameingiwa na huruma za kidugu na hali ya kujiona kuwa yeye ndiye mlinzi halali wa Mtume[saw], alisema na lile kundi la Waislamu wa Madina akiwaambai:

> Enyi Wakhazraj, huyu jamaa yangu hapa yuaheshimiwa na watu wake. Sio wote Waislamu, lakini hata hivyo wao wanamlinda. Lakini hivi sasa yeye amechagua kutuacha sisi na kwenda kwenu nyinyi. Nyie Wakhazraji, je, mwajua kitakachofanyika? Arabuni nzima itawahasimu. Kama nyinyi mwaitambua ile hatari iliyomo ndani ya huu mwaliko wenu, basi mchukueni; kama hatari hiyo hamuioni basi acheni nia yenu na kumwacha akae papa hapa.

Kiongozi wa lile kundi, Hadhrat Al-Baraa' kwa kumhakikishia alimjibu:

> Tumesikia. Sisi tuna dhamira thabiti. Maisha yetu tumempatia Mtume wa Mungu. Sisi tumekaa chonjo, na twangojea uamuzi wake tu (Halabiyya, J. 2, uk. 18).

Mtume[saw] akatoa maelezo zaidi ya Islam na mafundisho yake. Akilielezea jambo lenyewe, yeye aliliambia lile kundi la Waislamu wa Madina ya kwamba angekwenda Madina kama wangekuwa wao kuithamini Islam jinsi wawathaminivyo wake zao na watoto wao. Hata kabla hajamaliza kusema, lile kundi la waaminio sabini na watatu kwa pamoja lilipaaza sauti likisema, "Naam, Naam". Katika shauku yao wao hata walisahaulia mbali ile hatari ya kwamba huenda wakasikiwa. Mzee Abbas akawanasihi wapunguze sauti zao. Lakini kundi lile lilikuwa limefurikwa na Imani. Kifo sasa hakikuwa kitu chochote machoni mwao. Mzee Abbas alipowanasihi, mmoja wao alitamka kwa sauti kubwa akisema, "Sisi hatuogopi, Ewe Mtume wa Mungu. Hebu tupatie ruhusa, na twaweza kuwakabili watu wa Makka sasa hivi na kulipiza zile taabu walizokuonjesha." Lakini Mtume[saw] akasema kwamba yeye bado alikuwa hajaamriwa kupigana.

Kisha kundi lile likachukua ahadi ya baiati na mkutano ukamalizika.

Watu wa Makka wakawahi kupata habari za mkutano huu. Wakaenda

kwenye kambi ya watu wa Madina na wakawalalamikia machifu wao dhidi ya wageni wale. Abdullah bin Ubbay bin Salul — Chifu wa machifu — hakuwa na habari za yaliyotendeka. Aliwahakikishia watu wa Makka ya kwamba bila shaka huo ulikuwa ni uvumi tu waliousikia. Alisema watu wa Madina walikuwa wamemkubali yeye kuwa kiongozi wao na wasingeliweza kufanya kitu chochote bila ya yeye kukijua na bila ya ruhusa yake. Yeye hakujua kumbe watu wa Madina walikuwa wameutupilia mbali utawala wa Shetani na kukubali utawala wa Mungu badala yake.

HIJRA

Lile kundi lilirejea Madina, na Mtume[saw] na wafuasi wake wakaanza maandalizi ya kuhajiri. Familia baada ya familia wakaanza kutoweka. Waislamu huku wakiwa na hakika kwamba Ufalme wa Mungu ulikuwa umewadia, walikuwa na hima sana. Wakati mwingine kichochoro kizima kingetoweka kwa usiku mmoja tu. Asubuhi yake ingekuwa watu wa Makka kuona nyumba zimekomelewa kufuli na kujua kwamba wenye nyumba walikuwa wamehamia Madina. Athari inayoongezeka ya Islam iliwashangaza.

Mwishowe Mwislamu hata mmoja hakusalia isipokuwa watumwa na waumini wachache, mwenyewe Mtume[saw], Hadhrat Abu Bakr[ra] na Ali[ra]. Watu wa Makka wakatambua kwamba windo lao lilikuwa karibu kuponyoka. Machifu wao wakakutana tena na kuamua kwamba sasa Mtume ni sharti auawe. Ilikuwa ni kwa mpango maalumu wa kimbinguni, yaonekana, ambapo ile siku waliyopanga kumuua Mtume[saw] ikawa ni siku hiyo hiyo aliyopangiwa kuondoka kwake. Walipokuwa watu wa Makka wakikusanyana mbele ya nyumba ya Mtume[saw]kwa nia ya kumuulia mbali, Mtume[saw] naye alikuwa akiondoka katika giza la usiku. Watu wa Makka ni lazima wawe walihofia kutarajiwa kwa mpango wao mwovu na Mtume[saw]. Walifanya mambo yao kwa tahadhari kubwa na wakati Mtume[saw] mwenyewe alipopita, wao walimdhania kuwa mtu mwingine, na wakajimbanza mbali wasije wakatambuliwa. Hadhrat, Abu Bakar[ra],

rafiki mkubwa zaidi wa Mtume[saw], alikuwa ameishajulishwa mpango wa Mtume[saw] siku iliyotangulia. Akajiunga naye ilivyotakikana na wote wawili wakaitoka Makka, na kujificha katika pango liitwalo Thaur, takriban maili tatu au nne hivi kutoka mjini Makka juu ya kilima. Watu wa Makka walipogundua kuponyoka kwa Mtume[saw], wakakutana na kutuma kundi la wasakaji. Wakiongozwa na msakaji stadi, walifika kwenye pango la Thaur. Yule msakaji huku akisimama mlangoni mwa lile pango ambamo Mtume[saw] na Hadhrat Abu Bakr[ra] walikuwa wakijificha, akasema kwamba Muhammad yumo humu pangoni, la sivyo amepaa mbinguni. Hadhrat Abu Bakr[ra] akayasikia maneno haya na moyo ukamdunda. Akamnong'onezea Mtume[saw] akimwambia, "Maadui wako karibu kututia mbaroni". Mtume[saw] akamwambia, "Usiogope, Mungu yu pamoja nasi". Abu Bakr[ra] akaendela akisema kwamba, "Mimi sihofii nafsi yangu", bali nakuhofia wewe". Kwani kama nikifa, mimi ni mtu tu wa kawaida; lakini kama wewe ukifa, itamaanisha kufa kwa dini na roho pia" (Zurqani). Mtume[saw] akamtuliza akimwambia, "Hata hivyo usiwe na haja ya kuogopa", Mtume[saw] akamhakikishia, "Hatuko wawili humu pangoni. Tunaye wa tatu − Mungu" (Bukhari).

Udhalimu wa Makka ulikuwa umalizike. Islam ilikuwa ipate fursa ya kustawi. Wale wasakaji wakakatwa chenga. Wakayazomea maoni ya yule msakaji mwenzao. Wakamsuta wakimwambia kwamba hili ni pango wazi mno na mtu yeyote hawezi kujificha humo, kwani nyoka na nge wanalikosesha usalama ndani yake. Lakini kama wasakaji wangechungilia kidogo tu ndani ya pango, basi wangeweza kuwaona wale waja wawili. Lakini wao kamwe hawakufanya hivyo, na huku wakimkatalia mbali yule msakaji hodari, wakarejea Makka.

Kwa muda wa siku mbili Mtume[saw] na Hadhrat Abu Bakr[ra] wakasubiri mle pangoni. Usiku wa tatu sawa na maandalizi, ngamia wawili wa msafara waliletwa kule pangoni, mmoja kwa ajili ya Mtume[saw] na kiongozi wa msafara, na mwingine kwa ajili ya Hadhrat Abu Bakr[ra] na mtumishi wake aliyetwa 'Aamir bin Fuhaira.

SURAKA AMSAKA MTUME[SAW]

Kabla ya kushika njia, Mtume[saw] aliutazama mji wa Makka. Huzuni ikamjaa moyoni. Makka palikuwa mahali pake alipozaliwa. Alikuwa ameishi pale kama mtoto na mtu mzima na alikuwa amepewa Utume pale pale. Pale ndipo palipokuwa mahali ambapo wakale wake waliishi na kufanikiwa tangu zama za Hadhrat Ishmaili[as]. Akiwa na maono haya akapatupia jicho kwa mara ya mwisho na akatamka akisema, "Makka, mimi nakuthamini kuliko mahali penginepo duniani, lakini watu wako hawakuniacha nikae hapa". Kusikia hivyo Hadhrat Abu Bakr[ra] akatamka, akisema, "Mahali hapa pamemfukuza Mtume wake, hapa panangojea maangamio yake." Watu wa Makka, baada ya kutofaulu kwa usakaji wao, walizitolea zawadi shingo za hawa wakimbizi wawili. Waliahidi kwamba yeyote atakayetia mbaroni na kumrejeshea watu wa Makka Mtume[saw] au Hadhrat Abu Bakar[ra] mzima au maiti, alikuwa apewe zawadi ya ngamia mia moja. Tangazo hili lilifanyiwa makabila yaliyoizunguka Makka. Akishawishika kwa zawadi ile, Suraka bin Malik, chifu mmoja wa Kibedui, alianza kusaka msafara ule na mwisho akawaona kwenye njia ya Madina. Aliona ngamia wawili waliopandwa, na huku akiwa na hakika kwamba walikuwa wakimbeba Mtume[saw] na Hadhrat Abu Bakr[ra], alimtoa farasi wake shoti. Yule farasi akainua miguu yake ya mbele na kuanguka kabla hajaenda mbali, na Suraka, akaanguka naye. Ama ni jambo la kuchangamsha anavyokisimulia Suraka mwenyewe kisa hiki. Yuasema:

> Baada ya kuanguka farasini, mimi nikapiga ramli ya desturi ya kishirikina ya Waarabu kwa kupiga mishale. Mishale ikaonyesha ndege mbaya. Lakini tamaa ya ile zawadi ilikuwa kubwa. Nikampanda tena farasi wangu kuwafuatilia na nusura niwafikie. Mtume[saw] alisafiri kwa utulivu, wala hakutazama nyuma. Lakini Abu Bakr[ra] alitazama nyuma mara kwa mara (bila shaka kwa kuhofia usalama wa Mtume[saw]). Nilipokuwa nikiwakaribia farasi akanyanyua tena miguu yake ya mbele, nami nikadondoka chini. Nikaigeukia ramli ya mishale; nayo kwa mara ya tena ikaonesha ndege mbaya. Kwato za farasi wangu

> zilizama ndani ya mchanga. Kumpanda tena na kuanza usakaji likaonekana jambo gumu. Hapo nikatambua kwamba ule msafara ulikuwa chini ya kivuli cha ulinzi wa kimbinguni. Nikawaita nikiwasihi wasimame. Nilipowakaribia vya kutosha nikawatobolea nia yangu mbaya na kughairi kwangu. Nikawaambia mimi naachilia mbali kuwasaka na narudi nyuma. Mtume[saw] akaniachilia, lakini akanitaka niahidi kutomwambia yeyote waliko. Nikawa na yakini kwamba Mtume[saw] alikuwa mkweli, asiyekuwa na budi kufaulu. Nilimwomba Mtume[saw] aniandikie dhamana ya amani inifaidi zama yeye atakapokuwa mkuu. Mtume[saw] akamwambia 'Aamir bin Fuhaira aniandikie hati, naye akafanya hivyo. Nilipokuwa nikijitayarisha kurudi nayo, Mtume[saw] alipata wahyi kuhusu siku za usoni na akatamka akisema, "Suraka, utajisikiaje ukiwa umezivaa bangili za Khosro mkononi mwako?" Mimi nikiwa nimeshangazwa na bishara ile nikamwuliza, "Khosro yupi"? Je, Khosro bin Hurmuz, Mfalme wa Iran?" Mtume[saw] akasema, "Naam". (Usudul Ghaba).

Miaka kumi na sita au kumi na saba baadaye bishara hii ikatimia. Suraka alisilimu na akaenda Madina. Mtume[saw] akafariki, na baadaye, kwanza Hadhrat Abu Bakr[ra], na kisha Hadhrat Umar[ra] akawa Khalifa wa Islam. Athari ya Islam iliyokuwa ikiongezeka ikawatia husuda Wairani na ikawafanya wawashambulie Waislamu, lakini badala ya kuwatiisha Waislamu, Wairani wenyewe wakaoneshwa cha mtema kuni. Mji Mkuu wa Irani ukatekwa na Waislamu waliozishika hazina zake, zikiwemo bangili za dhahabu alizokuwa Khosro akizivaa kwenye sherhe za Kitaifa. Baada ya kusilimu, Suraka alizoea kusimulia kisa chake cha kumsaka Mtume[saw] na wenziwe na kueleza kilichotukia baina yake na Mtume[saw]. Wakati mali iliyotokana na vita dhidi ya Wairan ilipowekwa mbele ya Hadhrat Umar[ra], akaziona zile bangili za dhahabu na kukumbuka Mtume[saw] alivyokuwa amemwambia Suraka. Ama kwa hakika hii ilikuwa ni bishara kuu iliyobashiriwa wakati wa unyonge mtupu. Hadhrat Umar[ra] akaamua kuweka peupe kutimizwa kwa bishara hiyo. Hivyo basi, yeye

akamwita Suraka na kumtaka azivae bangili zile za dhahabu. Suraka akalalamika akisema kwamba kuvaliwa kwa dhahabu na wanaume kulikuwa kumekatazwa na Islam. Hadhrat Umar[ra] akatamka akimwambia, hiyo ilikuwa ni sawa lakini hiki kilikuwa ni kisa tofauti. Mtume[saw] alikuwa ameishaziona kimbele hizi bangili mikononi mwa yeye Suraka; hivyo basi, sasa hakuwa na budi kuzivaa hata iwe ni kwa maumivu ya kitubio. Suraka alikuwa akidinda akichelea uendaji kinyume na mafundisho ya Mtume[saw] waila yeye alikuwa na shauku kama mtu mwingine ya kuainisha dalili inayoonekana ya kutimizwa kwa ile bishara tukufu. Basi akazivaa zile bangili na Waislamu wakaiona bishara imetimia. (Usudul-Ghaba). Nabii mzozwaji akawa mfalme. Yeye mwenyewe hakuwa tena humu duniani. Lakini wale walioshikilia mahali pake wakaweza kushuhudia kutimizwa kwa maneno yake na njozi yake.

MTUME[SAW] YUAWASILI MADINA

Hebu sasa natukirudie kisa chetu cha Hijira. Baada ya Mtume[saw] kumbetua Suraka aliendilea na safari yake ya Madina salama salimini. Alipowasili Madina, Mtume[saw] aliwakuta watu wakimsubiri kwa hamu. Isingeliweza kutokea kwao siku tukufu kuliko hiyo. Kwani, lile jua lililokuwa limechomozea Makka badala yake lilikuwa limekuja kung'aria Madina.

Habari za kuwa Mtume[saw] alikuwa ameitoka Makka zilikuwa zimewafikia, hivyo basi wao walikuwa wakitumainia kufika kwake. Baadhi yao walisafiri masafa marefu nje ya Medina kwenda kumwangalia. Walikwenda asubuhi na jioni wakarejea makwao bila ya kufanikiwa. Hatimaye alipokuwa sasa ameingia Madina, aliamua kusimama kwa muda huko Qubaa, kijiji kilichokuwa karibu. Myahudi mmoja alikuwa amewaona wale ngamia wawili na akawa na uhakika kwamba wanyama wale walikuwa wakimbeba Mtume[saw]na Masahaba zake. Akapanda kilimani na kupiga ukelele akisema, "Enyi wana wa Qaila, yule mliyemsubiri amefika". Kila mmoja aliyesikia ukelele huu katika eneo la Madina alikwenda upesi Qubaa, wakati ambapo wakazi

wa Qubaa, wakiwa na ndremo kwa kuwasili kwa Mtume[saw] miongoni mwao waliimba nyimbo za kumsifu.

Hali ya Mtume[saw] ya kutojitakia makuu yadhihirishwa na kisa kimoja kilichotukia wakati huu pale Qubaa. Watu wa Madina walio wengi zaidi walikuwa hawajamwona Mtume[saw] hapo kabla. Walipouona msafara wake ukiketi chini ya mti, wengi wao walimdhania Hadhrat Abu Bakr[ra] kuwa ndiye Mtume[saw]. Ingawaje Hadhrat Abu Bakr[ra] ailikuwa na umri mdogo, lakini yeye alikuwa na ndevu nyeupe zaidi na alivalia vizuri zaidi kuliko Mtume[saw]. Basi wakamwendea yeye na kuketi mbele yake baada ya wao kumwonyesha heshima zao zenye kumstahili Mtume[saw]. Hadhrat Abu Bakr[ra] alipoona kuwa yeye alikuwa akidhaniwa kuwa ndiye aliyekuwa Mtume[saw], akasimama na kushika kashida yake na kumfanyia kivuli Mtume[saw] na akatamka akisema, "Ewe Mtume wa Mungu, uko juani. Mimi nakutilia kivuli (Bukhari). Kwa hekima na staha yeye aliwaonyesha wageni wa Madina makosa yao. Mtume[saw] alisimama Qubaa kwa siku kumi, ambapo baadaye watu wa Madina walimpeleka kwao mjini. Alipoingia mjini akakuta kwamba watu wote, waume kwa wanawake na watoto, walikuwa wamejitokeza kumlaki. Miongoni mwa nyimbo walizoimba ulikuwa ni wimbo huu:

> Mwezi arubatashara umetuchomozea kutoka nyuma ya Al-Wadaa. Maadamu tunaye miongoni mwetu mja atuitaye kwa Mwenyezi Mungu, yatupasa tumshukuru Mungu. Kwako, ewe uliyetumwa kwetu na Mwenyezi Mungu, twafikisha wetu utiifu (Halabiyya).

Mtume[saw] hakuingia Madina toka upande wa mashariki. Watu wa Madina walipomwelezea kuwa yeye alikuwa ni "mwezi wa usiku wa arubatashara", walikuwa na maana ya kwamba wao walikuwa wakiishi gizani kabla Mtume[saw] hajaja kuwamulikia nuru. Ilikuwa ni Jumatatu Mtume[saw] alipoingia Madina. Ilikuwa Jumatatu alipolitoka pango la Taur, na − hata istaajabishe kiasi gani − ilikuwa ni Jumatatu yeye alipouteka mji wa Makka miaka kumi baadaye.

HADHRAT ABU AYYUB ANSARI[RA] AWA MWENYEJI WA MTUME[SAW]

Mtume[saw] alipokuwa mjini Madina, kila mmoja alitamani kupata heshima ya kuwa mwenyeji wake. Ngamia wake alipokuwa akipita mtaa mmojawapo, ilikuwa familia kupanga mlolongo kumkaribisha. Ikawa wao kutamka wakisema, "Sisi pamoja na majumba yetu, na mali zetu na uhai wetu tuko hapa kukupokea na kukupatia ulinzi wetu. Njoo ukae nasi". Ikawa wengi kuonesha jazba kubwa zaidi, wakichomoza na kushika hatamu za ngamia wa Mtume[saw] wakimkazania ashuke na kuingia mwao nyumbani. Ikawa Mtume[saw] kukataa na kuwaambia kwa upole, "Mwacheni ngamia wangu. Yuaongozwa na Mwenyezi Mungu; atasimama pale Mwenyezi Mungu amtakapo asimame". Mwishowe ngamia akasimama kwenye kiwanja kilichokuwa mali ya mayatima wa kabila la Banu Najjar. Mtume[saw] akashuka na akatamka akisema, "Yaonekana kwamba hapa ndipo Mwenyezi Mungu anapopataka tusimame". Akafanya uchunguzi. Mdhamini wa mayatima wale akajitokeza na kumpatia Mtume[saw] kiwanja kile. Mtume[saw] akajibu akisema kwamba yeye asingelikubali toleo hilo isipokuwa iwe ataruhusiwa kukigharamia. Basi wakaridhiana bei na Mtume[saw] akaamua kujenga pale msikiti na nyumba kadha. Kiwanja kikiwa kimenunulika, Mtume akataka kujua ni akina nani waliokiishi karibu zaidi na kiwanja kile. Hadhrat Abu Ayyub Ansari[ra] akajitokeza na akasema kwamba nyumba yake ndiyo iliyokuwa karibu zaidi naye huduma zake zilikuwa miguuni pa Mtume[saw]. Mtume[saw] akamwambia amtayarishie chumba. Nyumba ya Hadhrat Abu Ayyub[ra] ilikuwa na ghorofa. Akakata shauri kumwacha Mtume[saw] aende ghorofani. Lakini Mtume[saw] akapendelea chumba cha chini akichelea wageni watakaomtembelea.

Yale mapenzi watu wa Madina waliyokuwa nayo juu ya Mtume[saw] yakajitokeza kwa mara ya tena. Hadhrat Abu Ayyub[ra] akaridhia Mtume[saw] akae chumba cha chini, lakini akakataa katakata kulala katika chumba ambacho chini yake kuliishi Mtume[saw]. Yeye na mkewe waliiona kuwa ni utovu wa adabu kufanya hivyo. Ikatokea gudulia la maji kuvunjika kwa ajali na maji kusambaa sakafuni.

Hadhrat Abu Ayyub[ra], akihofia yasije maji yakavujia chumbani mwa Mtume[saw], alichukua mfarishi wake na kuyapangulia mbali kabla hayajadondokea chumba cha chini. Asubuhi yake akafika kwa Mtume[saw] na akamsimulia kisa kizima cha usiku uliopita, kusikia hivyo Mtume[saw] akakubali kuhamia ghorofani. Hadhrat Abu Ayyub[ra] akawa akiandaa makuli na kuyapeleka ghorofani. Mtume[saw] alikula chochote alichotaka na Hadhrat Abu Ayyub[ra] akala makombo yoyote yaliyosalia. Baada ya siku chache watu wengine wakataka nao wapate fungu la kumhudumia Mtume[saw]. Hadi kufikia pale Mtume[saw] alipokuwa sasa yuaishi katika nyumba yake yeye mwenyewe na kujipangia mambo yake alikarimiwa kwa zamu na watu wa Madina. Mama mmoja mjane alikuwa na mtoto mmoja tu aitwaye Anas, wa umri wa miaka minane au tisa hivi. Alimleta mtoto huyu kwa Mtume[saw] na kumtoa amtumikie Mtume. Huyu Hadhrat Anas[ra] akagandama katika historia ya Islam. Alielimika sana na akawa mtu tajiri. Alijaaliwa umri wa zaidi ya miaka mia moja na katika zama za Makhalifa yeye aliheshimiwa sana na kila mtu. Hadhrat Anas[ra] yuaripotiwa kuwa alisema kwamba licha ya yeye kwenda kumtumikia Mtume[saw] akiwa yu mtoto na kukaa naye hadi Mtume[saw] alipofariki, hakupata hata mara moja Mtume[saw] kumsemesha kwa ukali, wala hakupata kumkemea, wala hakupata hata mara moja kumpatia kazi asiyoiweza. Wakati wa kuishi kwake mjini Madina, Mtume[saw] alikuwa na Hadhrat Anas[ra] tu. Hivyo basi, ushuhuda wa Hadhrat Anas[ra] ni picha ya tabia ya Mtume[saw] kadri ilivyoimarika katika zile zama nguvu zake na ufanisi wake ulikuwa ukiongezeka huko Madina.

Baadaye, Mtume[saw] alimtuma Hadhrat Zaid[ra] kwenda kuwaleta familia yake na nduguze. Watu wa Makka walikuwa wameshangazwa na maandalizi ya ajabu ya kuondoka kwa ghafla kwa Mtume[saw] na wafuasi wake. Hivyo, kwa muda kadha wao hawakumfanyia chochote cha kumuudhi. Wakati familia ya Mtume[saw] na ile ya Hadhrat Abu Bakr[ra] walipoitoka Makka hawakuwafanyia rabsha. Familia hizi mbili ziliwasili Madina salama salimini. Wakati huo huo Mtume[saw] aliweka msingi wa msikiti katika kile kiwanja

alichokinunulia mradi huu. Baada ya hayo, akajenga nyumba kwa ajili yake na Masahaba zake. Takriban miezi saba ilitumika kuzikamilisha.

MAISHA YAWA HATARI MADINA

Kwenye muda wa siku chache baada ya Mtume[saw] kuwasili Madina, wapagani wa Kiarabu wa sehemu zila walivutiwa na Islam na walio wengi zaidi wakasilimu. Wengi, ambao hawakuwa wameridhika nyoyoni, pia wakasilimu. Kwa njia hii pakawa na kundi lililosilimu ambao nyoyoni hawakuwa Waislamu, kwa hakika. Watu hawa walikuja kutekeleza njama hatari katika histotia ya baadaye. Baadhi yao walitokea kuwa Waislamu waaminifu. Wengine waliendelea kutokuwa waaminifu na wakaendesha hujuma dhidi ya Islam na Waislamu. Baadhi yao walikataa kusilimu kabisa, Lakini hawakuweza kukabiliana na ufanisi uliokuwa ukiongozeka wa hii Dini Mpya, hivyo wao wakaitoka Madina na kuhamia Makka. Madina ukawa ni mji wa Waislamu. Humo ikasimikwa ibada ya Mungu Mmoja. Hapakuwepo na mji wa pili duniani wakati ule ungelioweza kufanya madai sampuli hii. Hii haikuwa furaha ndogo kwa Mtume[saw] na marafiki zake ya kwamba siku chache tu baada ya kuhajiri kwao mji mzima ulikuwa umekubali kutupilia mbali ibada ya masanamu na kusimamisha badala yake ibada ya Mungu Mmoja Asiyeonekana. Lakini bado hapakuwepo na amani kwa Waislamu. Madina kwenyewe kundi moja la Waarabu lilikuwa limesilimu kijuujuu tu. Ndani kwa ndani, wao walikuwa ni maadui wakali wa Mtume[saw]. Tena palikuwepo na Mayahudi ambao wakati wote walipanga njama dhidi yake. Mtume[saw] alizijua hatari hizi zote. Yeye alikuwa wima na akawashauri marafiki zake wakae chonjo. Mara nyingi yeye alikesha akiwa macho (Fat-hul-Bari, J. 6, uk. 60). Akiwa amechoka kwa kukesha macho, safari moja yeye akatamani kujinyosha. Punde si punde akasikia sauti ya silaha. Akauliza akisema, "Ni nini hicho?" Akajibu Sahaba wake akimwambia, "Huyu ni Sa'd bin Waqqas, Ewe Mtume wa Mungu, aliyekuja kufanya zamu ya kukulinda" (Bukhari na Muslim). Watu wa Madina waliufahamu sana wajibu wao mkubwa. Wao walikuwa wamemwalika Mtume[saw] aje aishi miongoni mwao na sasa lilikuwa ni

jukumu lao kumlinda. Makabila yakashauriana na wakaamua kuilinda nyumba ya Mtume[saw] kwa zamu.

Katika hali ya kukosekana kwa usalama wake yeye mwenyewe na kukosekana kwa amani kwa ajili ya wafuasi wake, hapakuwepo na tofauti baina ya maisha ya Mtume[saw] mjini Makka na maisha yake mjini Madina. Tofauti ya pekee ilikuwa ni hii ya kwamba mjini Madina Waislamu waliweza kuabudu hadharani ndani ya ule msikiti waliokuwa wameujenga katika jina la Mwenyezi Mungu. Waliweza kukusanyika kwa shabaha hii mara tano kwa siku bila ya shida wala kizuizi.

Ikapita miezi miwili au mitatu. Watu wa Makka wakaondokewa na kiwewe chao na wakaanza kupanga njama za kuwachokoza Waislamu. Mara wakatambua kwamba halikutimia lengo lao kwa kuwasumbua tu Waislamu mjini Makka na pembezoni mwake. Ilikuwa ni lazima kumshambulia Mtume na wafuasi wake kule Madina na kuwatimua kutoka hifadhi yao mpya. Sawa na shabaha hii, wao wakamwandikia barua Abdullah bin Ubayy bin Salul, kiongozi mmoja wa Madina, ambaye kabla ya kuwasili kwa Mtume[saw] alikuwa amechaguliwa na makundi yote kuwa ni mfalme wa Madina. Katika barua hii wao wakasema kwamba walikuwa wamesikitishwa na Mtume kuwasili Madina na kwamba lilikuwa ni kosa kwa upande wa watu wa Madina kumpatia hifadhi. Mwisho wa barua hiyo wakasema:

> Sasa kwa kuwa nyinyi mmemkaribisha adui yetu huko kwenu, twaapa kwa Mungu na kutangaza kwamba sisi, watu wa Makka, tutajiunga katika kuishambulia Madina isipokuwa nyinyi, watu wa Madina, mkubali kumtupa nje ya Madina au kumpiga vita vya shirika. Tutakaposhambulia Madina, tutawaulia mbali watu wazima wote na kuwatia wanawake wote utumwani. (Abu Dawud, Kitab al-Kharaaj).

Abdullah bin Ubayy bin Salul akafikiri barua hii imeletwa na Mungu. Akashauriana na wanafiki wenzake mjini Madina na kuwashawishi ya kwamba kama wao watamruhusu Mtume kuishi kwa amani miongoni mwao, basi watajivutia uadui wa watu wa Makka. Hivyo, walikuwa

wanapaswa kumpiga vita Mtume, angalau ni kwa sababu ya kuwapendeza watu wa Makka. Mtume[saw] akazijua njama hizi. Akamwendea Abdullah bin Ubayyy bin Salul na kujaribu kumnasihi ya kwamba njama kama hizo zitakuwa ni chambileche kujitia kitanzi shingoni. Watu wengi mjini Madina walikuwa wamesilimu na walikuwa tayari kujitoa uhai wao kwa ajili ya Islam. Kama Abdullah akitangaza vita dhidi ya Waislamu, basi watu wa Madina walio wengi zaidi watapigana upande wa Waislamu. Hivyo basi, vita sampuli hiyo vingemletea gharama kubwa na kuwa chanzo cha maangamizi yake. Ushauri huu ukiwa umemkolea, Abdullah akatupilia mbali njama zake.

Wakati huu Mtume[saw] akachukua hatua nyingine muhimu. Aliwakusanya Waislamu na akapendekeza kwamba kila Waislamu wawili wafungamane kama ndugu wawili. Pendekezo hili likapokelewa vyema. Mwana-Madina akamchukuwa Mwana-Makka kuwa nduguye. Chini ya huu udugu mpya, Waislamu wa Madina walikata shauri kugawana mali zao na Waislamu wa Makka. Mwislamu mmoja wa Madina akaamua kumtaliki mmoja wa wakeze wawili na kumwacha aolewe na nduguye wa Makka. Waislamu wa Makka wakadinda kukubali ukarimu wa Waislamu wa Madina wakitilia maanani haja za ndugu zao wa Madina. Lakini Waislamu wa Madina wakawakazania, na suala hili likapelekewa Mtume[saw]. Waislamu wa Madina wakashikilia kwamba Waislamu wa Makka walikuwa ni ndugu zao; hivyo basi hawakuwa na budi kugawana nao mali zao. Naam, Waislamu wa Makka hawakujua kuishughulikia ardhi. Lakini wanaweza wakagawanyiwa mazao ya ardhi ikiwa si ardhi yenyewe. Waislamu wa Makka wakalikataa kwa shukrani toleo hili la ukarimu usio na kifani, na wakachagua kuendelea na kazi zao za kibiashara. Waislamu wengi wa Makka wakawa matajiri tena. Lakini Waislamu wa Madina daima walikumbuka toleo lao la kagawana mali zao na Waislamu wa Makka. Mara nyingi alipofariki Mwislamu wa Madina, wanawe waligawana mali zake na ndugu zao wa Makka. Kwa miaka mingi, desturi hii ikaendelea mpaka Kurani ilipoikomesha kwa mafundisho yake kuhusu ugawaji wa mirathi (Bukhai na Muslim).

MAPATANO BAINA YA MAKABILA MBALIMBALI YA MADINA

Pamoja na kufungamanisha Waislamu wa Makka na Waislamu wa Madina katika udugu, Mtume[saw] alianzisha mapatano baina ya watu wote wa Madina. Kwa njia ya mapatano haya, Waarabu na Mayahudi wakaunganishwa katika uraia mmoja na Waislamu. Mtume[saw] akawaelezea Waarabu na Mayahudi ya kwamba kabla Waislamu hawajajitokeza kama kundi moja mjini Madina, humu mjini yalikuwemo makundi mawili tu, lakini kwa kuwepo Waislamu sasa, yalikuwepo makundi matatu. Ilikuwa sawa kabisa kwamba wafanye mapatano yatakayokuwa ni pingu kwao wote, na yatakayowahakikishia kiasi fulani cha amani. Hatimaye yakafikiwa mapatano. Mapatano yenyewe yakasema:

> Kati ya Mtume wa Mungu na Waaminio kwa upande mmoja, na wale wote kwa upande mwingine, wanaokubali kwa hiari kuingia (mapatanoni). Kama Mwislamu yeyote wa Makka atauawa, wenyewe Waislamu wa Makka itakuwa ni juu yao. Pia utakuwa ni juu yao wajibu wa kuwezesha kuachililiwa huru kwa mahabusu wao. Waislamu wa Madina nao hali kadhalika yatakuwa ni juu yao maisha yao na mahabusu wao. Yeyote atakayeasi na kuleta fujo atahesabiwa kuwa ni adui wa wote. Itakuwa ni wajibu wa wengine wote kumpiga vita, hata kama awe ni mwana au ndugu wa karibu. Kama kafiri akiuawa vitani na Mwislamu, nduguze Waislamu hawatajilipiza kisasi. Wala hawatawasaidia makafiri dhidi ya waaminio. Mayahudi wenye kushiriki katika mapatano haya watasaidiwa na Waislamu. Mayahudi Hawatapatishwa taabu yoyote. Maadui zao hawatasaidiwa dhidi yao. Hapana kafiri atakayemkaribisha mtu yeyote kutoka Makka. Hatakuwa mdhamini wa mali yoyote ya mtu wa Makka. Kwenye vita baina ya Waislamu na makafiri yeye hatashiriki. Kama Mwislamu akidhulumiwa bila sababu, Waislamu watakuwa na haki ya kuwapiga vita wale wanaodhulumu. Kama adui ya wote akiishambulia Madina, Mayahudi watashirikiana na Waislamu na kugawana gharama za

vita vile. Makabila ya Kiyahudi yenye mapatano na makabila mengine ya Madina yatakuwa na haki sawa na zile za Waislamu. Mayahudi watafuata dini yao na Waislamu dini yao. Haki zile walizonazo Mayahudi pia wafuasi wao watakuwanazo. Raia wa Madina hawatakuwa na haki ya kutangaza vita bila ya ruhusa ya Mtume. Lakini hii haitatangua haki ya mtu yeyote binafsi kujilipizia kisasi kosa la kibinafsi. Mayahudi watagharamia kundi lao wenyewe na Waislamu kundi lao wenyewe. Lakini vikiwepo vita, basi watashughulika kwa umoja. Mji wa Madina utachukuliwa na wale wenye kusaini mapatano haya kuwa mji mtakatifu usichafulike. Wageni wapatao ulinzi wa wakazi wake watahesabiwa kuwa ni wakazi. Lakini watu wa Madina hawataruhusiwa kumpatia mwanamke uraia wa mji bila ya ruhusa ya nduguze. Ubishi wote utaachiwa uamuzi wa Mungu na Mtume. Washiriki wa mapatano haya hawatakuwa na haki ya kufanya mapatano yoyote na watu wa Makka au marafiki zao. Ni hivyo kwa sababu washiriki wa mapatano haya wanakubaliana katika kuwakabili maadui walio wao. Washiriki hawa watakuwa na mshikamano katika amani na katika vita. Kundi lolote halitaamua kupigana vita peke yake wala kufanya mapatano ya amani binafsi. Lakini hapana mshirika atakaye-lazimika kushiriki vitani. Lakini hata hivyo, mshiriki atakayepita kiasi, atakabiliwa na faini. Kweli kabisa Mungu ndiye mlinzi wa watawa na Waaminio na Muhammad ni Mtume Wake (Hashim).

Haya ndiyo mapatano kwa ufupi. Yametayarishwa kutoka dondoo zipatikanazo kwenye rekodi za kihistoria. Mapatano haya bila shaka yanasisitiza ya kuwa katika usuluhishaji wa mizozo na ubishi kati ya makundi yaliyokuweko Madina, kanuni-tawala zilikuwa ni uaminifu, ukweli na uadilifu. Wenye kutenda upitajikiasi walikuwa waandamwe kwa upitajikiasi wao. Mapatano yanaainisha kwamba Mtume[saw] wa Islam alikuwa akinuia kuwatendea kwa utu na huruma wakazi wa Madina, na kuwatilia maanani na kuwachukulia kuwa ni ndugu. Kama ugomvi na ubishi ulikuja kuzuka baadaye, hiyo ilikuwa ni juu ya Mayahudi.

Kama tulivyokwisha sema, miezi miwili au mitatu ilipita kabla watu wa Makka hawajarejelea uadui wao ulionuiwa dhidi ya Islam. Fursa ikatolewa na Sa'd bin Mu'adh, chifu wa kabila la Aus la Madina, aliyewasili Makka kuizunguka Kaaba. Abu Jahl alimwona akifanya hivyo na akatamka akimwambia, "Baada ya nyinyi kumpatia hifadhi huyu kafiri Muhammad, mnadhani mnaweza mkaja Makka na kuizunguka Kaaba kwa amani? Je, mnadhani mnaweza kumlinda na kumnusuru? Wallahi, kama isingelikuwa kwa sababu ya Abu Sufyan, wewe usingeliweza kurudi salama kwa ahali zako."

Sa'd bin Mu'adh akamjibu akimwabia, "Amini usiamini, mimi nakuambia kama nyinyi watu wa Makka mkitukataza kuzuru na kuizunguka Kaaba, basi hamtakuwa na amani kwenye njia yenu ya kwenda Siria". Wakati huo huo chifu mmoja wa Makka, Walid bin Mughira, akawa mgonjwa sana. Alihisi kwamba mwisho wake umewadia. Machifu wengine wa Makka walikuwa wameketi karibu. Walid hakuweza kujizuia na alianza kulia. Wale machifu wenzake wakashangaa na kumwuliza ni nini kilichomliza. Akiwajibu aliwaambia, "Mwafikiri mimi naogopa kifo? La, hasha; kifo mimi sikiogopi. Niogopacho ni kwamba isije hii dini ya Muhammad ikaenea na hata Makka kuwa chini yake." Abu Sufyan akamhakikishia kwamba mradi wao wako hai watazuia kwa damu zao kuenea kwa Dini hii (Khamis, J. 1).

WATU WA MAKKA WAJIANDAA KUSHAMBULIA MADINA

Kutokana na huku kuelezewa kwa matukio ni dhahiri kwamba kupoa kwa uadui wa watu wa Makka kulikuwa ni kwa muda tu. Waila viongozi wa Makka walikuwa wakiandaa kuanzishwa tena kwa mashambulio dhidi ya Islam. Machifu wanaokufa waliwalisha warithi wao kiapo cha uadui dhidi ya Mtume[saw], na wakawachochea kwenye vita dhidi yake na wafuasi wake.

Watu wa Medina walishauriwa wajihami dhidi ya Waislamu na wakaonywa ya kwamba, kama watakataa kufanya hivyo, basi watu wa Makka na marafiki zao wataishambulia Madina, wawaulie mbali

wanaume wao na kuwatia utumwani wanawake wao. Kama Mtume[saw] angejisimamia kando na kutoufanyia chochote ulinzi wa Madina, angekabiliwa na jukumu hatari. Hivyo basi, Mtume alianzisha mpango wa upelelezi. Aliwatuma watu kwenye maeneo yaliyoizunguka Makka waje wamripotie dalili zozote za maandalizi ya vita. Mara kwa mara, ikatokea visa — mikwaruzano na mapigano — baina ya watu hawa na watu wa Makka. Waandishi wa Ulaya wadai kwamba visa hivi vilichochewa na Mtume, na hivyo katika vile vita vilivyofuatia, yeye ndiye aliyekuwa mchokozi. Lakini sisi tunayo machoni petu ile miaka kumi na mitatu ya udhalimu wa watu wa Makka dhidi ya Waislamu, pamoja na vile vitisho vya kushambuliwa kwa Madina yenyewe. Hapana mtu akumbukaye haya yote awezaye kumwekelea Mtume[saw] lawama za kuchochea visa hivi. Kama yeye alipeleka vikundi vya Waislamu kwa minajili ya upelelezi, basi huko kulikuwa ni kujihami. Miaka kumi na mitatu ya udhalimu ilikuwa ni sababu tosha ya kujiandaa kwa Waislamu katika kujihami. Kama vita vilifuatia baina yao na maadui wao wa Makka, basi hiyo haikuwa juu ya Waislamu.Vile vijisababu ambavyo leo hii mataifa ya Kikristo hutangaziana vita vyajulikana sana. Ingelitokea nusu tu ya yale watu wa Makka waliyowatendea Waislamu leo hii kutendewa taifa la Ulaya, wao wangeliona ni halali kuanzisha vita. Inapokuwa watu wa taifa moja kupanga mauaji makubwa ya watu wa taifa jingine, inapokuwa watu wa taifa moja kuwafanya watu wa taifa jingine wayaache majumba yao, je, hii haiwapatii watu wanaotendewa hivyo sababu za kuzusha vita? Baada ya Waislamu kuwa wamehamia Madina, hakikuhitajika tena kisingizio kingine cha kuwatangazia vita watu wa Makka. Lakini Mtume[saw] hakutangaza vita. Yeye alionesha ustahamilivu na mbinu zake za kujihami za kupeleleza. Watu wa Makka, hata hivyo, waliendelea kuwachokoza na kuwasumbua Waislamu. Wao waliwachochea watu wa Madina dhidi yao na kuingilia haki yao ya kuhiji. Walibadilisha njia za kawaida za misafara yao na kuanza kupitia maeneo ya makabila yaliyoizunguka Madina, kusudi wayachochee makabila hayo dhidi ya Waislamu. Amani ya Madina ilihatarishwa; hivyo basi, ulikuwa ni wajibu dhahiri wa

Waislamu kuvikabili vile vitisho vya vita walivyokuwa watu wa Makka wakiwafanyia kwa miaka kumi na minne. Katika hali kama hii hapana mtu angeliyeweza kutilia shaka haki ya Waislamu ya kukabiliana na vitisho hivyo.

Mtume[saw] alipokuwa akijishughulisha na upelelezi, yeye hakua mwenye kuyasahaulia mbali mahitaji ya kawaida na ya kiroho ya wafuasi wake mjini Madina. Idadi iliyo kubwa zaidi ya watu wa Madina walikuwa wamesilimu, kwa kauli na pia kwa imani ya ndani ya moyo. Baadhi yao walikuwa wamesilimu kwa kauli tu. Kwa hiyo, Mtume[saw] alianza kusimika aina ya serikali ya Kiislamu miongoni mwa wafuasi wake wachache. Katika siku za awali, Waarabu walikuwa wakisuluhisha ugomvi wao kwa upanga na kwa ukali wa mtu binafsi. Mtume[saw] akaanzisha utaratibu wa mahakama. Wakachaguliwa mahakimu kuamua mashtaka ambayo mtu au makundi ya watu walishtakiana. Bila ya hakimu kutangaza madai kuwa ni ya haki na ya kweli, hayakukubaliwa. Katika siku za zamani kazi za kielimu zilikuwa zimedharauliwa. Mtume[saw] alichukua hatua za kusitawisha ujuzi wa kusoma na kuandika na watu kutaka kuelimika. Wajuzi wa kusoma na kuandika walitakiwa wawafundishe wengine fani hizo. Dhuluma na ukatili vikatiwa komesha. Haki za wanawake zikasimikwa. Matajiri wakawa wagharamie mahitaji ya maskini na huduma za kijamii mjini Madina. Wafanyakazi wakalindwa dhidi ya unyanyasaji. Ukafanywa mpango wa kuwachagulia wadhamini wale warithi waliokuwa wanyonge na wasiomudu mambo yao. Shughuli za ukopaji zikaanza kurekodiwa kimaandishi Umuhimu wa kutekeleza ahadi zote ukaanza kusisitiziwa. Ukatili uliofanyiwa watumwa ukapigwa marufuku. Elimusiha na huduma za usafi wa jamii vikaanza kutiliwa maanani. Watu wakahesabiwa. Njia na barabara zikatakikana kupanuliwa, na hatua zikachukuliwa za kuziweka katika hali ya usafi. Kwa neno zima, ziliundwa sheria kwa minajili ya kujenga familia bora na maisha ya kijamii yanayofaa. Ikawa washenzi wa Kiarabu kwa mara ya kwanza katika maisha yao kufunzwa tabia ya upole na maisha ya kistaarabu.

VITA VYA BADR

Huku Mtume[saw] akipanga utaratibu wa utekelezwaji wa sheria ambazo hazikuwa zisihudumie zama zake yeye mwenyewe za Waarabu tu bali wanadamu wote na wakati wote, watu wa Makka walifanya plani zao za vita. Mtume[saw] aliplania sheria iliyokuwa iwaletee watu wake yeye mwenyewe na wengineo wote amani, heshima na maendeleo; ambapo maadui zake wa Makka waliuplania uvunjaji wa sheria hiyo. Plani za watu wa Makka hatimaye zikawa na matokeo ya vita vya Badr. Huo ulikuwa ni mwezi wa kumi na nane baada ya Hijra. Msafara wa kibiashara chini ya uongozi wa Abu Sufyan ulikuwa ukirejea kutoka Siria. Kwa kisingizio cha kuuhami msafara huu, watu wa Makka wakaunda jeshi kubwa na kuamua kulipeleka Madina. Mtume[saw] alipata habari za maandalizi haya. Pia alipokea wahyi uliosema kwamba wakati wa kumlipiza adui kisasi ulikuwa umewadia. Akatoka nje ya Madina na baadhi ya wafuasi. Wakati ule hapana mtu aliyejua kama kundi hili la Waislamu ingelibidi likabiliane na ule msafara uliokuwa ukija kutoka Siria au lile jeshi lililokuwa likija kutoka Makka. Lile kundi la Waislamu lilikuwa la watu takriban mia tatu. Msafara wa kibiashara zama zile haukuwa na ngamia tu waliobeba bidhaa. Bali pia walikuwa nao watu wenye silaha waliouhami msafara na kuusindikiza safari yake nzima. Kwa kuwa chokochoko zilikuwa zimezuka baina ya watu wa Makka na Waislamu wa Madina, machifu wa Makka walikuwa wameanza kuchukua tahadhari maalumu kuhusiana na ushikaji silaha wa walinzi wa misafara. Historia yarekodi habari za misafara mingine miwili iliyopitia njia hii hii muda mchache hapo kabla. Kwenye mmoja wa misafara hii, watu mia mbili walikuwemo humo kama walinzi na wasindikizaji, na katika ule mwingine watu mia tatu. Ni kosa kudai, kama vile wanavyodai waandishi wa Kikristo, ya kwamba Mtume[saw] alichukua wafuasi mia tatu na kwenda kushambulia msafara wa kibiashara usiokuwa na ulinzi. Madai haya ni uchochezi mtupu wala hayana msingi. Ule msafara ambao sasa ulikuwa unakuja kutoka Siria ulikuwa ni msafara mkubwa na, ukiangalia ukubwa wake na ile idadi

ya walinzi wenye silaha ambao misafara mingine ilipatiwa, haliwi tena jambo la kutokubalika kufikiria kwamba walinzi takriban mia nne hadi mia tano ni sharti wawe walipewa kazi ya kuusindikiza msafara ule. Kudai kwamba kundi la Waislamu mia tatu wenye silaha duni waliongozwa na Mtume[saw] kwenda kuushambulia msafara uliojihami vikali kwa silaha eti kwa tamaa za kuuporea mali zake, ni madai ya kidhalimu kupindukia. Ni chuki mbaya tu na husuda ya makusudi iwezayo kuleta fikara sampuli hiyo. Kama lile kundi la Waislamu lilijitokeza kukabiliana na msafara huu tu, basi kujitokeza kwao kungeliweza kuelezewa kuwa ni kujitokeza kivita, vita vya kujilinda, kwani lile lilikuwa ni kundi dogo la Waislamu toka Madina tena lililokuwa na silaha duni, ambapo ule msafara wa watu wa Makka ulikuwa mkubwa uliojihami kwa silaha nzuri, na muda mrefu walikuwa wameendeleza harakati za uadui dhidi ya Waislamu wa Madina.

Kusema kweli hali amabayo kwayo kundi hili dogo la Waislamu lilijitokeza nje ya Madina ilikuwa ya hatari zaidi. Kama vile tulivyosema, wao hawakujua kama walikuwa wapambane na ule msafara kutoka Siria au na lile jeshi kutoka Makka. Hali hii ya Waislamu ya kutokuwa na hakika yadokezewa ndani ya Kurani. Lakini Waislamu wale walikuwa tayari kwa vyote viwili. Hali ya kutokuwa na hakika ambayo kwayo Waislamu walijitokeza kutoka Madina yaitilia fora imani yao na uaminifu wao mkubwa. Ilikuwa ni baada ya wao kusafiri masafa kadha nje ya Madina ambapo Mtume[saw] aliwafahamisha kwamba hawatakuwa na budi kukabiliana na lile jeshi kubwa kutoka Makka wala sio ule msafara kutoka Siria.

Habari zilikuwa zimewafikia Waislamu juu ya ukubwa wa jeshi la Makka. Makisio ya wastani zaidi ya ukubwa wa jeshi lile yalikuwa ya askari elfu moja, wote wakiwa ni askari wenye uzoefu mpevu wa mbinu za vita. Idadi ya walioandamana na Mtume[saw] ilikuwa ni watu mia tatu na kumi na watatu, na miongoni mwao wengi hawakuwa na maarifa wala uzoefu wa vita, na wengi zaidi walikuwa na silaha duni. Idadi yao kubwa zaidi walitembea kwa miguu, au kupanda ngamia. Kulikuweko na farasi wawili tu katika kundi zima. Kundi hili

lililokuwa na silaha duni za kivita sambamba na vile lilivyokuwa changa kiuzoefu, ikabidi likabiliane na jeshi kubwa mara tatu zaidi yake, lililokuwa na idadi kubwa zaidi ya wapiganaji wenye uzoefu. Kilikuwa dhahiri kitu cha hatari zaidi kupata kufanyika katika historia. Mtume[saw] alifanya maarifa kuhakikisha kwamba hapana aliyeshiriki humo bila kujua na bila ya hiari yake na kupenda kwake. Aliwaambia wenzake kwa uwazi kwamba haukuwa ule msafara waliokuwa wakabiliane nao bali lile jeshi kutoka Makka. Akawataka ushauri wao. Na mmoja baada ya mwingine, wafuasi wake wa kutoka Makka walisimama kumhakikishia Mtume[saw] uaminifu wao na jazba, na uamuzi wao wa kuwapiga vita maadui wa Makka waliokuja kuwashambulia Waislamu wa Madina kwao majumbani. Kila mara Mtume[saw] aliposikia Mwislamu wa Makka, alitaka ushauri zaidi na zaidi. Waislamu wa Madina walikuwa wamenyamaza kimya. Wachokozi walikuwa wanatoka Makka, wakiwa na uhusiano wa damu na wengi wa wale Waislamu waliokuwa wamehajiri Madina pamoja na Mtume[saw] na ambao sasa walikuwemo kwenye kundi hili dogo. Waislamu wa Madina walihofia usije mori wao wa kutaka kupigana ukawakera ndungu zao watokao Makka. Lakini Mtume[saw] alipokazania ushauri zaidi, mmojawapo wa Waislamu wa Madina alisimama na akatamka akisema, "Mtume wa Mungu, wapata ushauri wote unaotaka, lakini bado wazidi kutaka ushauri zaidi. Labda waashiria upande wetu, sisi Waislamu wa Madina. Je, ni hivyo?"

Mtume[saw] akasema, "Naam".

Yule Ansari[ra] akasema, "Wataka ushauri wetu ukifikiria kwamba labda ulipokuja kwetu, sisi tulikubali kupigana upande wako pale tu itakapotokea kwamba wewe na wahajiri wenzako wa Makka mnashambuliwa ndani ya mji wa Madina. Lakini sasa yaonekana kwamba tumetoka nje ya Madina, na wawe wafikiria kwamba mapatano yetu hayahusikani na hii hali ambayo tunajikuta nayo hivi leo. Lakini Ewe Mtume wa Mungu, pale tulipofanya mapatano yale sisi hatukujua jinsi tunavyokujua hivi sasa. Sasa twafahamu ni daraja ya juu iliyoje uliyonayo. Hatujali tulichokipatania. Sisi sasa tuko

pamoja nawe, vyovyote vile utakavyotuamrisha. Wala hatutafanya kama wafuasi wa Musa waliosema, "Enenda wewe na Mungu wako mkapigane na maadui, sisi tutabakia hapa hapa nyuma". Ikiwa ni sharti tupigane, basi tutapigana kuumeni kwako, kushotoni kwako, mbele yako na nyuma yako. Naam, adui ataka kukufikia. Lakini sisi twakuhakikishia kwamba yeye hatafua dafu bila ya kutukanyaga maiti zetu. Mtume wa Mungu, watutaka tupigane. Sisi tuko tayari kufanya cha ziada. Hapa karibu nasi pana bahari. Ukituamrisha tujitumbukize ndani, sisi hatutasitasita" (Bukhari, Kitabul Maghazi, na Muslim).

Huu ndio uliokuwa moyo wa imani na kujitolea waliouonyesha Waislamu wa hapo awali, na ambao hauwezi ukapatikana katika historia ya dunia nzima. Mfano wa wafuasi wa Nabii Musa[as] umekaririwa hapo juu. Ama kuhusu wafuasi wa Yesu, twajua kwamba wao walimtoroka wakati wa hatari. Mmoja wao alimsaliti kwa tamaa ya hela chache. Mwingine akamlaani na kumi waliosalia wakamkibia. Waislamu waliojiunga na Mtume[saw] kutoka Madina walikuwa wamekaa katika usahibu wake kwa mwaka mmoja na nusu tu. Lakini wao walikuwa wamejijengea imani pevu kiasi hiki kwamba ingelikuwa Mtume[saw] kuamrisha tu, basi wao wasingelisita kujitosa baharini moja kwa moja. Naam, Mtume alifanya mashauri lakini yeye hakuwa na shaka yoyote iwayo kuhusu uaminifu wa wafuasi wake. Yeye alifanya mashauri kusudi agundue waoga na awaondolee mbali. Lakini akakuta kwamba Waislamu wa Makka na Madina walishindana wao kwa wao katika kudhihirisha uaminifu wao. Wote walikuwa wameamua kwamba hawatamgeuzia adui migongo yao, hata kama adui aliwazidi mara tatu na awe na vifaa bora zaidi, silaha na uzoefu. Ilikuwa ni afadhali kutegemea ahadi za Mwenyezi Mungu, kuionyeshea lslam heshima zao, na kutoa uhai wao katika kuihami.

Mtume[saw] akiwa amehakikishiwa uaminifu huu na Waialamu wote wa Makka na Madina, akasonga mbele. Alipofika mahali paitwapo Badr, akakubali pendekezo la mfuasi wake mmoja na kuamrisha watu wake wapige kambi karibu na kijito cha Badr. Waislamu waliitwaa chemchemi hii ya maji, lakini ile ardhi walimokita kambi yao ilikuwa

ni mchanga mtupu, na hivyo kutofaa kwa harakati za wapiganaji vita. Wafuasi wa Mtume[saw] wakaonyesha wasiwasi wa kawaida juu ya kasoro hii. Mwenyewe Mtume[saw] akawa na wasiwasi huo huo wa wafuasi wake na akakesha akiomba. Akakariri tena na tena akisema:

> Mungu wangu, juu ya uso mzima wa ardhi hivi sasa kunao hawa watu mia tatu tu wanaokuamini Wewe na kuazimia kusimika ibada Yako. Mungu wangu, kama hawa watu mia tatu wakifa hivi leo kwa kushambuliwa na maadui zao katika vita hivi, atabakia nani kulitukuza jina Lako? (Tabari).

Mwenyezi Mungu akatakabali dua ya Mtume[saw] Wake. Usiku kukanyesha mvua. Kule kulikokuwa na mchanga walikopiga kambi Waislamu kukawa ni mchanga ulioshikamana. Kule kulikokuwa na udongo ulioshikamana walikopiga kambi maadui kukawa ni matope na utelezi. Maadui wa Makka huenda waliichagua sehemu hii ya uwanja wa vita na kuwaachia Waislamu kule mchangani kwa sababu jicho lao lenye uzoefu mkubwa lilipendelea udongo mkavu kuzatiti upiganaji wa wanajeshi wao na farasi. Lakini mambo yakafanywa chini juu na takdiri inayofaa ya Mwenyezi Mungu. Ile mvua iliyonyesha usiku kucha iliifanya ile sehemu yenye mchanga ya uwanja wa vita walikokuwa Waislamu kuwa ardhi madhubuti na ile sehemu walikokuwa watu wa Makka kuwa utelezi mtupu. Usiku Mtume[saw] alipata ishara wazi kutoka kwa Mwenyezi Mungu ya kuwa watu mashuhuri wa hao maadui watakumbana na mauti yao. Bali hata majina yao yalifunuliwa kwake. Mahali watakapofia pia akaoneshwa. Watu hao wakafa kama vile walivyotajwa na wakafia katika sehemu zilizotabiriwa.

Katika vita vyenyewe lile kundi dogo la Waislamu lilionesha ushujaa mkubwa na uaminifu. Kisa kimoja chahakikisha ukweli huu. Mmoja wa majenerali wachache wa hili jeshi la Waislamu liliokuwa nao alikuwa ni Hadhrat ‘Abdur-Rahman bin ‘Auf[ra], mmoja wa machifu wa Makka na mwanajeshi mpevu kwa upande wake. Vita vilipoanza, yeye alitazama kulia na kushoto kuona ni akina nani waliokuwa

wakimhami. Kwa mshangao mkubwa akakuta ni machipukizi wawili tu kutoka Madina waliokuwa huku na huku. Moyo ukamtaharuki na akajiambia, "Kila jemadari yuahitaji ulinzi huku na huku. Hususan kwangu mimi hivi leo. Lakini nina machipukizi wawili tu. Naweza kufanya nao kitu gani hawa?" Hadhrat Abdur-Rahman bin 'Auf[ra] yuasimulia kwamba ilikuwa ni kabla yeye hajamaliza kujiambia maneno haya ambapo mmoja wa wale vijana alimgusa ubavuni kwa kiko cha mkono wake. Alipokimtega sikio, yule kijana akatamka akisema, "Mzee, tumesikia mtu aitwaye Abu Jahl aliyekuwa akimnyanyasa na kumtaabisha Mtume[saw]. Mzee, mimi nataka kupambana naye; niambie alipo." Hadhrat Abdur-Rahman bin 'Auf[ra] alikuwa bado hajamjibu kijana, ambapo aliulizwa vivyo hivyo na yule kijana mwingine. Hadhrat Abdur-Rahman bin 'Auf[ra] hakuustaajabia kidogo ujasiri na ushujaa wa vijana hawa wawili. Askari mpevu, hakufikiria kwamba hata yeye mwenyewe angechagua jemadari wa maadui kupigana naye. Hadhrat 'Abdur-Rahman bin 'Auf[ra] akanyosha kidole chake akiwaonesha Abu Jahl — silaha zikimjaa tele huku akisimama nyuma ya safu za askari akilindwa na majemadari wawili wapevu, walioshika majambia. Hadhrat Abdur-Rahman bin 'Auf[ra] alikuwa bado hajauteremsha mkono wake, ambapo wale vijana wawili waliwafyatukia maadui upesi chambileche furukombe, wakimlenga Abu Jahl. Shambulio hili lilikuwa la ghafla. Wale wanajeshi na walinzi wakapigwa na butwaa. Hapo wakawashambulia wale vijana. Mmoja wao akakatwa mkono. Lakini hawakugutuka wala kushindwa. Walimshambulia vikali Abu Jahl kiasi hiki kwamba jemadari huyu mkubwa alidondoka chini, akiwa amejeruhiwa vibaya. Kutokana na huku kujitolea mhanga kwa hawa vijana wawili, mtu anaweza akaelewa ni kiasi gani nyoyo za wafuasi wa Mtume[saw], wazee kwa vijana, zilivyokuwa zimechomeka kwa yale mateso ya kikatili waliyokuwa wameonjeshwa. Sisi twayasoma katika historia tu, hata hivyo twashtuka sana. Watu wa Madina walipata habari za mateso haya kutoka kwa watu waliyoyashuhudia kwa macho. Ule uchungu ambao ni sharti uliwaingia nyoyoni, unaweza ukaeleweka. Kwa

upande mmoja walisikia habari za ukatili wa watu wa Makka na kwa upande mwingine wakasikia habari za subira ya Mtume[saw]. Basi haliwi tena jambo la kushangaza ya kwamba walichemkwa na mori wa kulipizia kisasi dhuluma alizofanyiwa Mtume[saw] pamwe na Waislamu wa Makka. Walitafuta tu nafasi kuwaambia watesaji wa Makka kwamba kama Waislamu hawakujilipiza kisasi, haikuwa kwa sababu eti wao hawakuwa na nguvu; bali ilikuwa ni kwa sababu hawakuwa wameruhusiwa na Mwenyezi Mungu kufanya hivyo. Hali ya kujitolea ya jeshi hili dogo la Waislamu ya kufa kiume, yaweza ikapimwa kwa mizani ya hiki kisa kingine. Vita vilikuwa bado havijaingiliwa ambapo Abu Jahl alimtuma chifu mmoja wa Kibedui kwenda upande wa Waislamu ili aje amripotie ukubwa wa jeshi la Waislamu. Yule chifu akaleta ripoti akisema kwamba Waislamu walikuwa ni mia tatu au zaidi. Abu Jahl na wafuasi wake wakafurahi. Waliwachukulia wale Waislamu kuwa ni windo lao rahisi. Hapo yule chifu akatamka akisema, "Lakini nasaha yangu ni kwamba: "Nyinyi msipigane na watu hawa, kwa sababu yaonekana kila mmoja wao amedhamiria kufa. Mimi sikuona watu ila mauti juu ya ngamia". (Tabari na Hisham). Chifu yule wa Kibedui alisema kweli — wale walio tayari kufa hawafi kwa urahisi.

BISHARA KUU YATIMIA

Wakati wa vita ukawadia. Mtume[saw] akachomoza nje a kibanda alimokuwa akiomba, na akatangaza akisema;

"Watu hawa bila shaka watashindwa na kutimuliwa".

Haya yalikuwa ni maneno aliyoyafunuliwa Mtume[saw] mjini Makka wakati fulani hapo kabla. Ni dhahiri yalidokezea vita hivi. Wakati ukatili wa Makka ulipofurika, na Waislamu wakawa wanahamia mahali wanakoweza kujipatia amani, Mtume[saw] alifunuliwa aya hii na Mwenyezi Mungu:

> Na kwa kweli Waonyaji waliwafikia watu wa Firauni. Wakakadhibisha Ishara Zetu zote. Kwa hiyo, Tukawakamata kwa mkamato wa Mwenye nguvu, Mwenye uwezo. Je, makafiri

> wenu ni bora kuliko hao? Au je, yameandikwa vitabuni kwamba nyinyi mtaachwa? Au je wamesema, sisi ni jamii ya watu tuwezao kulipiza kisasi? Watu hawa bila shaka watashindwa na kutimuliwa. La, bali Saa ile ndio wakati wao walioahidiwa; na Saa hiyo itakuwa ni nzito sana na chungu sana. Kwa hakika wakosevu wamo katika mahangaiko na moto uwakao. Siku watakapokokotwa motoni kifudifudi na itasemwa kwao, Onjeni mguso kwa Jahanamu" (Sura Al-Qamar, 54:42-49).

Aya hizi ni sehemu ya Sura Al-Qamar na Sura hii, sawa na ripoti zote, ilfunuliwa huko Makka. Waandishi wa Kislamu wanaiwekea tarehe ya ufunuzi wake wakati fulani baina ya mwaka wa tano na wa kumi baada ya Mtume[saw] kudai Utume yaani, kwa akali miaka mitatu kabla ya Hijra (ndio kusema mwaka wa kuhajiri Mtume[saw] kutoka Makka hadi Madina). Yaelekea zaidi, ilifunuliwa miaka minane hapo kabla. Waandishi wa Ulaya wana maoni hayo hayo. Sawa na rai ya Noldeke, Sura hii nzima ilifunuliwa baada ya mwaka wa tano wa Utume wa Mtume[saw]. Lakini mwenzake Wherry yuaichukulia tarehe hii kuwa ni mapema sana. Sawa na rai yake, Sura hii ni ya mwaka wa sita kabla ya Hijra au saba baada ya Utume wa Mtume[saw]. Kwa neno zima, waandishi wote Waislamu na wasiokuwa Waislamu wanakubali kwamba Sura hii ilifunuliwa miaka mingi kabla ya Mtume[saw] kwenda kuhajiri kutoka Makka kwenda Madina. Hali ya kibishara ya aya hizi za Makka haitiliki shaka. Katika aya hizi kimo kidokezo kilicho wazi cha kile kitakachowapata watu wa Makka kwenye uwanja wa vita wa Badr. Maafa waliyokuwa watakuja kuyapata yanabashiriwa waziwazi. Wakati Mtume[saw] alipojitokeza nje ya kibanda chake, alikariri haya maelezeo ya kibishara yaliyomo ndani ya Sura hii iliyoshuka Makka. Ni sharti awe alikumbushwa aya hizi za Makka, wakati wa maombi yake mle kibandani. Kwa kusoma mojawapo ya aya hizi Mtuma[saw] aliwakumbusha wafuasi wake kwamba ile Saa iliyoahidiwa kwenye wahyi wa Makka sasa ilikuwa imewadia.

Na Saa yenyewe ilikuwa imewadia kwa hakika. Nabii Isaya[as] (Isaya 21:13-17) alikuwa ameitabiri saa hii hii. Vita vikapamba moto,

ingawaje Waislamu hawakuwa tayari navyo na wasiokuwa Waislamu walikuwa wamenasihiwa kutopigana. Waislamu mia tatu na kumi na watatu, wengi wao kurutu na wasiokuwa na uzoefu wa kivita, na takriban wote bila ya zana, wakalikabili jeshi kubwa mara tatu, na wote wanajeshi wapevu. Baada ya masaa machache, machifu wengi mashuhuri wa Makka wakafikwa na mwisho wao. Kama vile tu alivyokuwa ametabiri Nabii Isaya[as], utukufu wa Kedari ukaangamia. Jeshi la Makka likakimbia mbio wakiziacha nyuma maiti zao na mahabusu pia. Miongoni mwa mahabusu alikuwemo amiye Mtume[saw], Mzee Abbas, ambaye kwa kawaida alisimama pamoja na Mtume[saw] katika siku za Makka. Mzee Abbas alikuwa amelazimishwa kuungana na watu wa Makka na kumpiga vita Mtume[saw]. Mateka mwingine wa kivita alikuwa ni Abul 'Aas, mkwe wa Mtume[saw]. Miongoni mwa waliokufa alikuwemo Abu Jahl, Jemadari Mkuu wa jeshi la Makka na, sawa na masimulizi yote, adui mkubwa wa Islam.

Ushindi ukapatikana, lakini ukamletea Mtume[saw] maono tamu-chungu. Alifurahia kutimia kwa ahadi za kimbinguni, zilizorudiwarudiwa katika miaka kumi na minne iliyokuwa imepita, ahadi ambazo pia zilikuwa zimerekodiwa katika baadhi ya maandiko ya kidini ya awali sana. Lakini wakati huo huo yeye alihuzunishwa na mkasa wa watu wa Makka. Ulikuwa ni mwisho wa kuhuzunisha kiasi gani uliowakumba! Kama ushindi huu angeliupata mtu mwingine badala yake, basi huyo angerukaruka kwa furaha. Lakini kuwaona wafungwa wa kivita mbele yake, wamekazwa kamba na kutiwa pingu, kuliyatiririsha machozi macho ya Mtume[saw]na sahibu yake mwaminifu, Hadhrat Abu Bakr[ra]. Hadhrat Umar[ra] aliyeshika hatamu za uongozi kama Khalifa wa Pili wa Islam baada ya Hadhrat Abu Bakr[ra], aliliana jambo hili lakini hakulielewa. Imekuwaje, Mtume[saw] na Aba Bakr[ra] kutolea ushindi machozi.? Hadhrat Umar[ra] alishangaa. Hivyo basi ikawa kumwuliza Mtume[saw] akimwambia, "Mtume wa Mungu, niambie ni kwa nini walia ilihali Mwenyezi Mungu kakupatia ushindi mkubwa kaiasi hiki? Kama yatubidi tulie, mimi nitalia nawe, au angalau kuonesha uso wa kilio." Mtume[saw] akakumbusha hali ya

kusikitisha ya wale mahabusu wa Makka. Haya ndiyo yaliyaletwa na kumwasi Mwenyezi Mungu.

Nabii Isaya[as] aliuzungumzia tena na tena uadilifu wa Mtume huyu, aliyekuwa ameambulia ushindi kutokana na vita hatari sana. Ama katika kisa hiki kilikuweko kielelezo kikubwa cha uadilifu huo. Alipokuwa akirejea Madina, Mtume[saw] alipumzika njiani usiku mmoja. Wafuasi waaminifu waliomwangalia wakamwona akigeuka ubavu huu na ubavu huu na hakuweza kupata usingizi. Mara wakapata wazo kwamba alikuwa amesikia kite kilichopigwa na amiye Mzee Abbas, aliyekuwa amelazwa karibu naye, akiwa amekazwa kamba kama mfungwa wa kivita. Basi wao wakamlegeza kamba Mzee Abbas. Mzee Abbas akaacha kupiga kite. Mtume[saw] pakiwa sasa hapana cha kumkera, akapata usingizi. Baadaye akaamka na akashangaa kwa kutosikia tena kite cha Mzee Abbas. Akadhani labda Mzee Abbas alikuwa amezirai. Lakini wale Masahaba waliokuwa wakimlinda Mzee 'Abbas wakamwambia kwamba walikuwa wamemlegeza kamba Mzee 'Abbas ili yeye (Mtume[saw]) apate kulala bila msukosuko. Mtume[saw] akasema "Hapana, hapana; pasiwepo na ubaguzi. Kama 'Abbas ni jamaa yangu, hao mahabusu wengine nao ni jamaa za watu wengine. Walegezeni kamba wote au 'Abbas naye mkazeni kamba". Masahaba wakausikia ushauri huu na wakaamua kuzilegeza kamba za mahabusu wote, na wao wenyewe kuwa na jukumu la ulinzi wao. Miongoni mwa hao wafungwa wa kivita, wale waliokuwa wasomi waliahidiwa kuachiliwa huru ikiwa kila mmoja wao atachukua jukumu la kuwafundisha vijana kumi wa Makka kusoma na kuandika — hii ikiwa ndiyo fidia yao ya kujikombolea. Wale ambao hawkuwa na yeyote wa kuwalipia fidia, walijipatia uhuru wao kwa mataradhio. Wale waliokuwa na uwezo wa kulipa fidia waliachiliwa huru baada ya kuwa wamekwishalipa. Kwa kuachilia huru wafungwa kwa njia hii, Mtume akakomesha desturi ya kikatili ya kuwageuza wafungwa wa kivita kuwa watumwa.

VITA VYA UHUD

Wakati jeshi la Makka lilipotimka kutoka Badr walitangaza kwamba wataushamblilia tena mji wa Madina na kuwalipiza kisasi Waislamu kwa yale yaliyowakumba watu wa Makka katika vita vya Badr, na mwaka mmoja tu baadaye waliushambulia tena mji wa Madina kwa nguvu zao zote. Walijiona wametiwa aibu na kufedheheshwa na ushinde ule kiasi hiki kwamba Machifu wa Makka waliwakataza jamaa za waliofia Badr kuwaomboleza wale waliouawa katika vita hivyo. Pia waliweka sharia kwamba faida zitokanazo na misafara ya kibiashsra zitageuzwa kuwa ni hazina ya kivita. Kwa maandalizi kamili hivyo basi, jeshi la watu elfu tatu chini ya uongozi wa Abu Sufyan likaushambulia mji wa Madina. Mtume[saw] akafanya mashauri na akawauliza wafuasi wake kama wao wangelipendelea kupambana na adui mjini Madina au nje yake. Yeye mwenyewe alipendelea hilo wazo lililotangulia. Alipendelea kuwaacha Waislamu wakae Madina na kumwacha adui aje awashambulie majumbani mwao. Mbinu hii yeye aliifikiria ya kwamba ingelimwekelea adui lawama ya uchokozi. Lakini kwenye mashauriano haya walikuwemo Waislamu wengi ambao hawakuwa wamepata fursa ya kushiriki katika vita vya Badr, na ambao sasa walitamani kupigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Wakakazania kuwepo na vita waziwazi na wakakazania kujipatia nafasi ya kufa wakipigana. Mtume[saw] akalikubali shauri la wote. (Tabari).

Ajenda hii ilipokuwa ikijadiliwa, Mtume[saw] alisimulia ruya yake. Alisema, "Mimi niliona ruya. Niliona ng'ombe, na nikaona upanga wangu ncha yake imevunjika. Nikamwona yule ng'ombe akichinjwa, na kwamba mimi nilikuwa nimeuingiza mkono wangu ndani ya deraya. Pia mimi nilijiona nimepanda juu ya kondoo dume". Masahabu wakamwuliza Mtume[saw] aliitafasiriaje ruya hii.

Mtume[saw] akasema, "kuchinjwa kwa yule ng'ombe kwaonyesha kwamba baadhi ya Masahaba wangu watauawa katika vita hivyo. Ncha iliyovunjika ya upanga wangu yaonesha kwamba mtu fulani mashuhuri miongoni mwa jamaa zangu atafikwa na mauti, au

pengine mimi mwenyewe yatanifika maumivu au aina fulani ya jeraha. Kuingiza mkono wangu ndani ya deraya yaonekana kunamaanisha kwamba kama tukikaa hapa hapa Madina itakuwa ni bora kwetu. Jambo hili kwamba nimejiona nimepanda juu ya kondoo dume lamaanisha kwamba tutamshinda jemadari wa makafiri, na kwamba tutamuulia mbali (Bukhari, Hisham na Tabari).

Ilibainishwa na ruya hii na tafsiri yake kwamba ilikuwa ni heri Waislamu kukaa mjini Madina. Lakini Mtume[saw] hata hivyo, hakukukazania kufanya hivyo, kwa kuwa tafsiri ya ile ruya ilikuwa ni yake yeye mwenyewe, na sio sehemu ya elimu iliyofunuliwa. Yeye alikubaliana na maoni ya wengi na akaamua kujitokeza nje ya Madina kwenda kumkabili adui. Alipokuwa akishika njia, sehemu iliyokuwa na kiherehere zaidi ya wafuasi wake wakiwa wametambua kosa lao, walimsogelea Mtume[saw] na wakasema, "Mtume wa Mungu, mbinu unayoipendekeza yaonekana kuwa bora zaidi. Ni afadhali tukae hapa hapa mjini Madina na kupambana na adui mwetu barabarani."

Mtume[saw] akasema, "Sio hivyo tena. Sasa Mtume wa Mungu amevaa deraya yake. Hata ikitokea nini, sasa tutasonga mbele. Mkiwa na subira na uvumilivu, Mwenyezi Mungu atawasaidieni" (Bukhari na Tabari). Baada ya kusema hivyo, akashika njia akiwa na jeshi la watu elfu moja. Wakalala njiani mahali ambapo hapakuwa mbali nje ya mji wa Madina. Ilikuwa ni desturi ya Mtume[saw] kuwapumzisha wanajeshi wake kwa muda kabla ya kupambana na maadui. Wakati wa sala ya alfajiri, yeye alikagua kambi. Akakuta kwamba baadhi ya Mayahudi nao pia walikuwa wameungana na Waislamu. Walisingizia kwamba wao walikuwa na mapatano ya kirafiki na makabila ya Madina. Kwa kuwa Mtume[saw] alikuwa akizifahamu njama za Mayahudi, akawafukuzilia mbali wale Mayahudi. Mara baada ya kufanya hivyo, chifu wa wanafiki, Abdullah bin Ubayy bin Salul, akajiondoa pamwe na wafuasi wake mia tatu. Akasema jeshi la Waislamu sasa lilikuwa ni tumbaku ya kunusa kwa maadui zao. Kupigana katika vita hivi sasa ndiyo mauti pasipo shaka. Kwani Mtume alikuwa amekosea kwa kuwafukuza marafiki zake yeye mwenyewe. Matokeo ya utoro huu

wa saa ya mwisho yakawa kwamba walibakia Waislamu mia saba tu chini ya uongozi wa Mtume[saw]. Hawa mia saba wakasimama dhidi ya jeshi kubwa mara nne, na lililowapita mara nyingi kwa zana na silaha. Katika jeshi la Makka walikuwemo wapiganaji mia saba waliovalia deraya; katika jeshi la Waislamu wapiganaji mia moja tu. Watu wa Makka walikuwa na askari wapanda-farasi mia mbili, Waislamu walikuwa na wawili tu. Mtume[saw] akafika Uhud. Huko akaweka askari hamsini juu ya ujia wa kupitia baina ya vilima, wakiwa na jukumu la kuulinda dhidi ya shambulio lolote la maadui au jaribio lolote la kuuteka. Mtume[saw] aliwabainishia wajibu wao kwa uwazi. Ilikuwa wao wasimame pale pale walipowekwa, na kutoondoka pale hadi watakapoamriwa kufanya hivyo, hata kitokee kitu gani kwa Waislamu. Akiwa na wale mia sita na hamsini waliosalia, Mtume[saw] alijitokeza kupambana na jeshi la ukubwa takriban mara tano zaidi. Lakini, kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, muda si muda wale Waislamu mia sita na hamsini wakawatimua askari elfu tatu wa Makka wenye uzoefu mkubwa wa kivita. Waislamu wakawakimbiza. Ule ujia wa vilimani kulikowekwa askari hamsini ulikuwa upande wa nyuma wa uwanja wa vita. Wale walinzi wakamwambia kiongozi wao, "Adui ameshindwa. Sasa ni wakati wetu nasi kupigana na kujichumia malipo yetu ya huko ahera". Kiongozi wao akawakataza, akiwakumbusha amri waziwazi za Mtume[saw]. Lakini wao wakamwambia kwamba amri ya Mtume ilikuwa ichukuliwe kama alivyonuia wala si kama alivyotamka. Haikuwa na maana tena kuendelea kuulinda ujia ule wakati maadui walipokuwa wakitimka kuokoa roho zao.

USHINDI WAFANYWA USHINDE

Wakiwa wanabishana hivyo wakauachilia mbali ule ujia na kujitosa vitani. Lile jeshi la Makka lililokuwa likikimbia ndani yake alikuwemo Khalid bin Walid, alitokea baadaye kuwa jemadari mashuhuri wa Kiislamu. Akauona ule ujia ukiwa haulindwi vya kutosha. Khalid akamwita jemadari mwenzake wa Makka, 'Amr bin al-'Aas, na akamtaka autupie jicho ule ujia uliokuwa nyuma yao. 'Amr akafanya hivyo na akaona hii ndiyo nafasi yake ya mwaka. Majemadari hawa

wote wawili wakawasimamisha watu wao na kupanda kilimani kulikokuwa na Waislamu. Wakawaua wale Waislamu wachache ambao bado walikuwa wakiulinda ule ujia na kutoka pale mahali palipoinuka wakaanzisha shambulio dhidi ya jeshi la Waislamu. Kusikia ukelele wao wa kivita lile jeshi la Makka lililokuwa limetawanyika likajikusanya na kurudi tena kwenye uwanja wa vita. Shambulio dhidi ya Waislamu lilikuwa la ghafla. Katika jitihada zao za kulitimua jeshi la Makka wao walikuwa wametapanyika uwanja mzima wa mapigano. Ngome ya upinzani wa Waislamu dhidi ya shambulio hili la maadui haikuweza tena kuundika. Waislamu mmoja mmoja tu ndio walioonekana wakipambana na maadui hawa. Wengi wao wakafa huku wakipigana kiume. Wengine, wakarudi nyuma. Wachache wakajenga ukuta kumzunguka Mtume[saw]. Hawa wasingeweza kuwa zaidi ya ishirini kwa jumla. Jeshi la Makka liliushambulia vikali ukuta huu. Mmoja baada ya mwingine, Waislamu hawa waliomjengea Mtume[saw] hifadhi ya ukuta wakaangushwa na dhoruba za panga za wanajeshi wa Makka. Kutoka kule juu kilimani, askari wapigaji upinde wakanyesha mvua ya mishale. Wakati ule Hadhrat Talha[ra], mmoja wa Makureishi wa Makka aliyehajiri Madina, akaona kwamba kumbe mishale yote ya maadui ilikuwa ikilenga uso wa Mtume[saw]. Akanyoosha mkono wake mbele ya uso wa Mtume[saw]. Mshale baada ya mshale ukafuma mkono wa Hadhrat Talha[ra], lakini hata hivyo haukubanduka ulipokuwa, licha ya kwamba kila mshala uliupenya hadi upande wa pili. Hatimaye mkono ukachanika kabisa. Hadhrat Talha[ra] akapoteza mkono wake na kusalia na kikono maisha yake mazima. Wakati wa Khalifa wa Nne wa Islam[ra] ulipokuwa umejitokeza ugomvi miongoni mwa Waislamu, Hadhrat Talha[ra] alishutumiwa na adui mmoja akaitwa Talha-Kikono. Rafiki yake Hadhrat Talha[ra] akasema, "Kweli yeye ni kikono, lakini je, wewe wajua ni wapi alikoupotezea mkono wake? Ni katika vita vya Uhud ambako yeye aliinua mkono wake kuunusuru uso wa Mtume dhidi ya mishale ya adui."

Muda mrefu baada ya vita vya Uhud, marafiki wa Hadhrat Talha[ra]

walimwuliza wakimwambia, "Kwani mkono wako haukugutuka kwa kufumwa na mishale na uchungu kukudondoshsa machozi?" Hadhrat Talha[ra] akajibu akisema, "Naam, mkono uliniuma na nusura nitokwe na machozi, lakini mimi hayo yote nikayavumilia kwa sababu nilijua kwamba kama mkono wangu ukitikisika kidogo tu, utaufungulia uso wa Mtume mishale ya maadui". Wale watu wachache waliobaki pamoja na Mtume[saw] wasingeliweza kufua dafu mbele ya lile jeshi walilolikabili. Kikosi kimoja cha maadui kilisonga mbele na kuwasukuma kando. Hapo Mtume[saw] akasimama peke yake kama ukuta, na punde si punde jiwe likampiga kwenye paji la uso na kumjeruhi vibaya. Pigo jingine likabonyeza kofia yake ya chuma na kuvizamisha vipande vyake ndani ya panja zake. Mishale ilipokuwa imechacha na Mtume[saw] kujeruhiwa yeye aliomba akisema, "Mola wangu, wasamehe watu wangu kwani wao hawajui wafanyalo" (Muslim). Mtume[saw] akaangukia miili, miili ya wale waliokufa wakimlinda. Waislamu wengine wakachomoza mbele kumnusuru Mtume[saw] dhidi ya mashambulizi zaidi. Hao pia wakafa wakipigana. Mtume[saw] akalala chini akizirai miongoni mwa maiti hizi. Maadui walipoona hivyo, wakamchukulia kuwa yu maiti. Wakasongea kando wakiwa na uhakika wa ushindi na kuanza kujipanga tena milolongo. Miongoni mwa wale Waislamu waliokuwa wakimlinda Mtume[saw] na ambao walikuwa wamesukumwa mbali na patashika ya maadui, alikuwemo Hadhrat 'Umar[ra]. Uwanja wa vita ulikuwa sasa umeachwa mtupu. Hadhrat 'Umar[ra] aliyeshuhudia haya yote, alikuwa na hakika kwamba Mtume[saw] alikuwa amekufa. Hadhrat 'Umar[ra] alikuwa mtu shujaa. Alithibitisha ushujaa wake mara nyingi; kielelezo bora zaidi ni katika kuzipiga vita kwa wakati mmoja himaya mbili kubwa za Urumi na Iran. Hakuwa amepata kutishika penye patashika. Huyu 'Umar aliketi juu ya jiwe akijawa na huzuni, huku akilia kama mtoto. Ndipo alipokuja Mwislamu mwingine, Hadhrat Anas bin Nadhr[ra], akiwa yuajizungukia akiamini kwamba Waislamu walikuwa wameshinda vita. Alikuwa amewaona wakiwashinda nguvu maadui lakini, yeye akiwa hajala riziki yoyote tangu usiku uliotangulia, alikuwa

ameondoka kwenye uwanja wa vita, akiwa na tende chache mkononi. Mara tu alipomwona Hadhrat 'Umar[ra] yualia, alisimama akishangaa na akauliza akisema, "Umar, una nini, badala ya kushangilia ushindi uliofana walioupata Waislamu, wewe walia?".

Hadhrat 'Umar[ra] akajibu akimwambia, "Anas, wewe hujui kilichofanyika. Uliona mwanzo tu wa vita. Hujui kwamba maadui waliiteka ile sehemu ya maana sana kule vilimani na kutushambulia vikali. Waislamu walikuwa wametawanyika, wakiamini wameshinda. Hapakuwepo na upinzani dhidi ya shambulio hili la maadui. Mtume peke yake na walinzi wachache walikabiliana na jeshi zima la maadui na wote wakafa wakipigana."

Hadhrat Anas[ra] akasema, "Kama ni kweli, basi inafaida gani kuketi hapa na kulia? Kule alikokwenda Kiongozi wetu mpendwa, nasi hatuna budi twende hukuhuko pia".

Hadhrat Anas[ra] tende yake ya mwisho alikuwa nayo mkononi. Na alikuwa karibu aitie mdomoni lakini, badala yake, aliitupilia mbali akisema, "Ewe tende, ni kipi kingine isipokuwa wewe kilichopo baina ya Anas na Pepo?"

Kusema hivyo, akachomoa upanga wake na kujitosa ndani ya jeshi la maadui, mtu mmoja kupamba na watu elfu tatu hakuweza kufua dafu, lakini nafsi moja yenye kuamini ni bora kuliko nyingi. Akiwa yuapigana kishujaa, Hadhrat Anas[ra] mwishowe aliangunka chini akiwa amejeruhiwa, lakini akaendelea kupigana. Kuona hivyo, umati wa maadui ukamrukia kikatili. Yasemekana kwamba vita vilipomalizika na waliokufa kutambulikana, mwili wa Hadhrat Anas[ra] haukuweza kutambulikana. Ulikuwa umekatwakatwa vipande-vipande. Hatimaye dadake Hadhrat Anas[ra] akiutambua kwa alama ya kidole-gutu alitamka akisema, "Huu ni mwili wa kakangu" (Bukhari).

Wale Waislamu waliokuwa wamefanya ukuta kuzunguka Mtume[saw] lakini wakasukumwa nyuma na maadui, walichomoza mbele tena mara tu walipoona maadui wakiondoka. Wakaunyanyua mwili wa Mtume[saw] kutoka miongoni mwa maiti. Hadhrat Abu 'Ubaida bin

Jarrah[ra] akitumia meno yake alivichomoa vile vipande vya chuma vilivyokuwa vimemjeruhi Mtume[saw] panjani mwake, ikawa naye kupoteza meno yake mawili alipokifanya hivyo.

Punde si punde, Mtume[saw] akapata fahamu. Wale walinzi waliokimzunguka wakaeneza ujumbe kuwataka Waislamu wajikusanye tena. Jeshi lililotapanyika likaanza kujikusanya. Wakaenda na Mtume[saw] hadi chini ya kilima. Kuona masalia hawa wa Waislamu, Abu Sufyan, jemadari wa maadui, akapiga ukelele akisema, "Tumemuulia mbali Muhammad." Mtume[saw] aliusikia ukelele huo na majidai, lakini akawanasihi Waislamu kutoujibu, isije maadui wakagundua ukweli wa mambo yalivyo na kushambulia tena na Waislamu waliochoka na kujeruhiwa vibaya kulazimika kupigana tena na kundi hili la kikatili. Alipokosa jawabu kutoka kwa Waislamu, Abu Sufyan akawa na yakini kwamba Mtume[saw] alikuwa amekufa. Hapo ukulele wake wa mwanzo akauongezea wa pili akisema, "Pia tumemuulia mbali Abu Bakr". Mtume[saw] akamnashi Hadhrat Abu Bakr[ra] kutojibu. Huyu Abu Sufyan akaongeza ukelele wa tatu, na akasema, "Tumemuulia mbali 'Umar". Mtume[saw] akamnasihi Hadhrat 'Umar[ra] naye pia kutojibu. Kuona hivyo, Abu Sufyan akatangaza kwamba walikuwa wamewaulia mbali wote watatu. Sasa Hadhrat 'Umar hakuweza kujizuia tena na akapiga ukelele akisema, "Sisi sote tu wazima na kwa fadhili za Mwenyezi Mungu tayari kabisa kuwapiga vita na kupasulia mbali vichwa vyenu." Ikawa Abu Suyfan kutoa wito wao wa kitaifa akisema, "Atukuzwe Hubal. Atukuzwe Hubal. Kwani Hubal kaitia Islam komesha." (Hubal ndilo lililokuwa sanamu la kitaifa la watu wa Makka). Mtume[saw] hakuweza tena kuvumilia majidai haya dhidi ya Yule Mungu Mmoja tu, Allah, Ambaye kwa ajili yake yeye na Waislamu walikuwa tayari kutoa kila walichonacho. Yeye alikuwa amekataa kukosoa tangazo la kifo chake. Alikuwa amekataa kukosoa tangazo na kifo cha Hadhrat Abu Bakr[ra] na cha Hadhrat 'Umar[ra] kimaarifa tu. Ni manusura wachaehe tu wa jeshi lake dogo waliokuwa wamesalia. Jeshi la maadui lilikuwa kubwa na zima. Lakini sasa adui alikuwa amemtukana Allah. Mtume[saw]

hakuweza kuvumilia matusi sampuli hiyo. Dhati yake ilichemka. Aliwatupia jicho kali wale Waislamu waliomzunguka na akasema, "Mbona mwasimama kimya na hamtoi jibu lolote dhidi ya haya matusi anayotusiwa Allah, Mungu wa Pekee?"

Waislamu wakauliza wakisema, "Tusemeje, Ewe Mtume". Kasema, "Semeni, Allah peke yake ndiye Mkuu na Mwenye Nguvu. Allah peke yake ndiye Mkuu Mwenye Nguvu. Yeye peke yake ndiye Aliye juu Aheshimiwaye. Yeye peke yake ndiye Aliye juu Aheshimiwaye."

Waiaslamu wakapiga ukelele vivyo hivyo. Ukelele huu ukawapumbaza maadui. Wakasimama wakishangazwa na hili wazo kwamba kumbe Mtume hakuwa amekufa. Mbele yao kuliweko na Waislamu wachache, majeruhi na wachovu. Kuwamalizia mbali lilikuwa ni jambo rahisi mno. Lakini maadui wakaogopa kushambulia tena. Wakitosheka na ile namna ya ushindi waliojipatia, walirudi makwao na ndaro chungu nzima.

Kwenye vita vya Uhud, ushindi wa Waislamu ulipata kugeuzwa ushinde. Lakini hata hivyo, vita vyenyewe vyatoa dalili za ukweli wa Mtume[saw]. Kwani katika vita hivi zilitimia zile bishara Mtume[saw] alizokuwa amebashiri kabla ya kwenda vitani. Waislamu walipata ushindi hapo mwanzo. Ami mpendwa wa Mtume[saw], Hadhrat Hamza[ra] alikufa akipigana. Jemadari wa maadui aliuawa mapema kwenye mapigano. Mtume mwenyewe[saw] alijeruhiwa na Waislamu wengi kuuawa. Haya yote yalifanyika sawa na vile yalivyokuwa yamebashiriwa na Mtume[saw] katika ruya yake.

Pamoja na kutimia kwa yale mambo yaliyotabiriwa kimbele vita hivi vina dalili nyingi za uaminifu na kujitolea kwa Waislamu. Nidhamu yao ilikuwa bora kiasi hiki kwamba haiwezi historia ikatoa mfano wake. Baadhi ya matukio ya kuthibitishia ukweli huu sisi tayari tumekwisha kuyazungumzia. Tukio moja zaidi lastahili kuelezewa. Laonesha hali ya uhakika wa imani na kujitolea kulikooneshwa na Masahaba wa Mtume[saw]. Mtume[saw] alipokwenda kujipumzisha chini ya kilima pamoja na Waislamu wachache, alituma baadhi ya Masahaba wake waende wakawahudumie majeruhi waliobwagika kwenye uwanja

wa vita. Sahaba mmoja baada ya kutafuta-tafuta, alimpata Mwislamu mmoja wa Madina. Alikuwa akikaribia kufa. Yule Sahaba akainama na kumwambia, "Assalaamu Alaikum." Yule Mwislamu majeruhi akamnyooshea mkono wa kutetemeka, na huku akishika mkono wa yule Sahaba akatamka akisema, "Nilikuwa nikisubiri patokee mtu".

Yule Sahaba akamwambia, "Uko hali mahututi, je, una ujumbe wa kupelekewa nduguzo?"

Yule mwnajeshi majeruhi akasema, "Naam, naam. Waambie ndugu zangu Asslaamu Alikum na uwaambie kwamba hapa mimi ninapokufa, naacha nyuma amana yenye thamani ya kulindwa nao. Amana hiyo ni Mtume[saw] wa Mungu. Ni matumaini yangu kwamba ndugu zangu watamlinda kwa uhai wao na kukumbuka haya matakwa yangu ya pekee ya kuagia dunia" (Muwatta na Zurqani).

Wanaokufa huwa na mengi ya kuwaambia ndugu zao, lakini hawa Waislamu wa hapo awali, hata katika gharighari ya mauti, hawakuwafikiria ndugu zao, wana, mabinti au wake, wala mali zao, bali Mtume[saw]. Waliyakabili mauti wakiwa na yakini kwamba Mtume[saw] alikuwa ni mwokozi wa dunia nzima. Watoto wao kama wakinusurika, watapata ufanisi haba tu. Wakifa wakimlinda Mtume, watakuwa wamewatumikia wote wawili, Mungu na mwanadamu. Waliamini kwamba katika kuzitoa kafara jamaa zao, waliwahudumia watu na Mola wao. Katika kujitakia kifo, wao wakawapatia watu wote uhai wa milele.

Mtume[saw] akakusanya majeruhi na maiti. Majeruhi wakafanyiwa huduma ya kwanza na maiti zikazikwa. Hapo Mtume[saw] akafahamu kwamba maadui walikuwa wamewatendea Waislamu kinyama mno, walikuwa wamezikatakata maiti za Waislamu na huyu wakimkata pua na yule kumkata sikio. Mmojawapo wa maiti waliokatwakatwa alikuwa ni wa Hadhrat Hamza[ra], amiye Mtume[saw]. Mtume[saw] akashtuka sana na akatamka akisema, "Matendo haya ya makafiri sasa yanastahilisha kule kutendewa ambako sisi hadi sasa tumekuona hakustahili." Alipokisema hivyo, akaamriwa na Mwenyezi Mungu kuwaacha makafiri na kuendelea kuwaonesha upendo.

UVUMI WA KIFO CHA MTUME[SAW] WAFIKA MADINA

Uvumi wa kifo cha Mtume[saw] na kutapakanywa kwa jeshi la Waislamu ulifika Madina, kabla masalia ya jeshi la Waislamu kuweza kuwasili mjini. Wanawake na watoto walipiga mbio ovyo kwenda Uhud. Wengi wao walijulishwa ukweli wenyewe na askari watokao Uhud na wakarudi makwao. Mama mmoja wa kabila la Banu Dinar alifuliza hadi Uhud. Mama huyu alikuwa amempoteza mumewe, babake na kakake vitani. Sawa na wasimulizi wengine, alikuwa pia amempoteza mwanawe. Askari mmoja atokaye vitani akamwambia kwamba babake amekufa. Katika kujibu akasema, "Simjali babangu; nipe habari za Mtume". Yule askari alijua Mtume[saw] yuko hai, hivyo hakumjibu swali lake mara moja, bali akazidi kumpatia tanzia ya kakake na mumewe ambao pia walikuwa wamekufa. Akatokea kutogutushwa na ripoti hizi na akazidi kuuliza akisema, "Mtume wa Mungu kafanya nini? Ilikuwa ni kauli ya kushangaza kuitumia, lakini tunapokumbuka kwamba ni mwanamke aliyeitumia, haionekani tena ya kushangza. Maono ya mwanamke ni mazito. Mara nyingi mwanamke humzungumzia mtu aliyekufa kana kwamba yu hai. Mtu yule kama akitokea kuwa jamaa wa karibu, basi mwanamke huwa na tabia ya kumnung'unikia na kuuliza ni kwa nini anamkimbia na kumwacha nyuma bila ya mlezi na mtunzaji. Ni jambo la kawaida kwa wanawake kuomboleza ndugu zao kwa njia hii. Basi maneno aliyoyatumia mama huyu ni stahili kwa mwanamke aombolezaye kifo cha Mtume[saw]. Mama huyu alimthamini sana Mtume[saw] na akakataa katakata kwamba alikuwa amekufa hata baada ya yeye kusikia kwamba alikuwa amekufa. Wakati huo huo yeye hakuikataa ile ripoti bali akazidi kusema katika huzuni hasa ya kike, "Mtume[saw] wa Mungu kafanya nini?" Kwa kusema hivyo yeye alifanya kana kwamba Mtume[saw] alikuwa hai, na kunung'unika kwamba kiongozi mwaminifu kama yeye alikuwa amechagua kuwapatia hiyo chungu nzima ya huzuni za kwaheri.

Alipotambua yule askari mtoka-vitani kwamba huyu mama hakujali kifo cha babake, kakake na mumewe, akaelewa uzito wa mapenzi

yake kwa Mtume[saw] na akatamka akimwambia, "Ama kuhusu Mtume, yeye yuko vile unavyotaka, mzima kabisa." Yule mama akamtaka amwonyeshe Mtume aliko. Akamwelekeza upande mmoja wa uwanja wa vita. Yule mama akaharakia upande ule na kufika kwa Mtume[saw] akamshika kashida yake, akaibusu na akasema, "Baba na mama watolewe sadaka kwako, Ewe Mtume wa Mungu, wewe ukiwa mzima, mimi sijali ni nani anayekufa."(Hisham).

Kwa hiyo, tunaweza tukaona ni aina gani ya subira na kujitolea Waislamu — wake kwa waume — waliyoonyesha katika vita hivi. Waandishi wa Kikristo husimulia kwa kujionea fahari kisa cha Mariamu Magdalene na wenzake na kutuelezea kujitolea kwao na ushujaa wao. Yasemekana asubuhi na mapema wao walijipenyeza kati ya Mayahudi na kufulizia kwenye kaburi la Yesu. Lakini hiki ni kitu gani kikilinganishwa na haya mapenzi ya huyu mama wa kabila la Dinar?

Mfano mwingine zaidi umerekodiwa historiani. Baada ya kuwa maiti wamekwisha zikwa na Mtume[saw] kuwa yuarejea mjini Madina, aliona wanawake na watoto waliokuwa wamejitokeza nje ya Madina kuja kumlaki. Hatamu za ngamia wake zilikuwa zikishikiliwa na Hadhrat Sa'd bin Mu'adh[ra], chifu wa Madina. Hadhrat Sa'd[ra] alikuwa akimwongoza yule ngamia kwa vishindo. Alikuwa kana kwamba yuaitangazia dunia kwamba licha ya yaliyotukia, hatimaye Waislamu walikuwa wamefanikiwa kumrejesha Mtume[saw] Madina akiwa mwenye nguvu na afya zake. Alipokisonga mbele akamwona mamake mzazi aliyekuwa katika hali ya uzee akija kuwalaki Waislamu waliokuwa wakirejea kutoka vitani. Mama huyu mzee alikuwa hawezi kuona sawasawa. Hadhrat Sa'd[ra] akamtambua na akimgeukia Mtume[saw] akatamka akisema, "Huyu ndiye mamangu, Ewe Mtume".

Mtume[saw] akasema, "Mwache aje huku mbele."

Yule mama akasongea mbele na kwa mtazamo usioashiria chochote akajaribu kuona uso wa Mtume[saw]. Hatimaye akaweza kuuona na kufurahi. Kumwona yule mama Mtume[saw] akatamka akisema, "Mama nahuzunishwa na kifo cha mwanao".

Yule mama mwenye imani kubwa akajibu akisema, "Lakini baada ya kukuona mzima, mimi nimeyameza machungu yangu." Maneno ya Kiarabu aliyoyatumia ni kwamba "Machungu yangu mimi nimeyaoka nikayala" (Halabiyya, J. 2 uk. 210). Ni upendaji wa dhati kiasi gani matamshi haya yanaouonesha. Kwa kawaida huzuni humpunguza mtu turuhani, na hapa alikuwepo huyu mama mzee aliyekuwa amempoteza mwanawe, tegemeo lake la uzeeni. Lakini yeye akasema kwamba badala ya kuyaruhusu majonzi yake yamtoe turuhani, yeye alikuwa ameyamezelia mbali machungu yake. Akimaanisha kwamba ule ukweli ya kwamba mwanawe alikuwa amekufa kwa ajili ya Mtume[saw] utamtosheleza maisha yake yote.

Mtume[saw] alifika Madina. Katika vita hivi Waislamu wengi waliuawa na wengi kujeruhiwa. Hata hivyo haviwezi vikasemwa kwamba vilikuwa vimemalizikia ushinde wa Waislamu. Vile visa ambavyo tumevitaja hapo juu vyathibitisha kinyume cha mambo yalivyokuwa. Vyathibitisha kwamba vita vya Uhudu vilikuwa ni ushindi mkubwa kwa Waislamu kama ushindi mwinginewe. Waislamu wazifunuao kurasa za historia yao ya awali wanaweza wakajipatia changamoto na hima kutokana na vita vya Uhud.

Baada ya kurejea Madina, Mtume[saw] alirejelea wadhifa wake. Alijishughulisha tena katika ulezi na ufundishaji wa wafuasi wake. Lakini kama ilivyokuwa hapo kabla, kazi yake haikuendelea bila ya kukatizwa. Baada ya vita vya Uhud, Mayahudi walipata ujasiri zaidi, nao wanafiki wakaanza tena chokochoko zao. Walianza kutumainia kwamba kukomesha Islam kulikuwa ndani ya duara la uwezo wao na nguvu zao. Ila tu, ilitaka wafanye juhudi za pamoja. Sawa na fikara hii, Mayahudi wakatumia mbinu mpya za uchokozi. Ikawa wao kutangaza kimashairi, matusi machafu na kwa njia hii kumtusi Mtume[saw] na familia yake. Safari moja Mtume[saw] alitakiwa kuamua ubishi na ikamlazimu aende kwenye ngome ya Mayahudi. Mayahudu waliplani kumwangushia kipande cha jabali na hivyo basi kummalizia mbali. Mtume[saw] akajulishwa njama hiyo kimbele na Mwenyezi Mungu. Ilikuwa ni jambo la kawaida yeye kutahadharishwa hivyo.

Mtume[saw] akaondoka kitini bila ya kutamka lolote. Kisha baadaye Mayahudi wakaungama kula njama yao hii mbaya. Wanawake wa Kiislamu wakawa wanatukanwa ovyo barabarani. Kwenye kisa kimoja cha aina hii Mwislamu mmoja alipoteza maisha yake. Katika kisa kingine Mayahudi walimpiga mawe msichana mmoja wa Kiialamu na akafa kifo chenye maumivu makubwa. Njama hizi za Mayahudi zilivuruga uhusiano wao na Waislamu na ikawa wao kulazimika kuwapiga vita Mayahudi. Lakini Waislamu wakawatimua tu nje ya mji wa Madina. Moja la yale makabila mawili ya Mayahudi lilihamia Siria. Miongoni mwa wale wengine, baadhi yao walikwenda Siria na wengine wakaenda kuishi huko Khaibar, ngome iliyolindwa sana ya Mayahudi, kuelekea kaskazini mwa mji wa Madina.

Kwenye kipindi cha amani baina ya vita vya Uhud na vita vilivyofuatia, dunia ilishuhudia mfano bora kabisa wa athari nzuri ya Islam juu ya wafuasi wake. Twagusia kuharamishwa kwa pombe. Katika kuelezea hali ya jamii ya Waarabu kabla ya Islam, sisi tulisema kwamba Waarabu walikuwa ni walevi wa kupindukia. Kunywa pombe mara tano kwa siku ulikuwa ndio mtindo wa maisha katika nyumba. Mtu kujisahaulia mbali kwa pombe kumjaa kichwani ilikuwa ndiyo desturi yenyewe na kwa Waarabu hii haikuwa aibu hata kidogo. Bali wao waliiona hali hii kuwa ndio utu-bora wenyewe. Mgeni alipowasili, ulikuwa ni wajibu wa mke mwenye nyumba kumwandalia pombe. Kuwaachisha watu sampuli hii tabia yao hii mbaya haikuwa kazi rahisi. Lakini katika mwaka wa nne baada ya Hijira, Mtume[saw] alipokea amri ya kuwa pombe imeharamishwa. Kufuatia kutolewa kwa amri hii, unywaji pombe ulitoweka miongoni mwa Waislamu. Imerekodiwa ya kwamba ulipopokewa wahyi unaoiharamisha pombe, Mtume[saw] alimwita Sahaba wake mmoja na akamwamuru kwenda kuitangaza amri hii mpya kwenye mitaa ya Madina. Katika nyumba ya Ansari mmoja (Mwislamu wa Madina) ilikuwa tayari ikisherehekewa karamu ya kunywa pombe. Watu wengi walikuwa wamealikwa na walikuwa wakibugia makopo ya divai. Mtungi mzima ulikuwa umeshanywewa tayari na wa pili ulikuwa njiani. Wengi

walikuwa chakari, na wengine wengi walikuwa wakikaribia kujisahaulia mbali. Katika hali hii wakamsikia mtu mmoja akitangaza kwamba pombe imeharamishwa na Mtume[saw] kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Mmoja wa wale washerehekeaji akanyanyuka na akasema, "Laonekana kuwa ni tangazo dhidi ya unywaji pombe; hebu tukahakikishe." Mwingine akasimama akaupiga gongo ule mtugi wa pili na kuuvunjia mbali na kisha akasema, "Kwanza tii ndipo ukachunguze. Ni hoja tosha kwamba sisi tumesikia tangazo sampuli hii. Haifai ya kwamba sisi tuendelee na kunywa huku eti tukiwa tunakwenda kulihakikishia. Bali ni wajibu wetu kuimwagilia mbali pombe hii ndipo twende tukalichunguze tangazo hili" (Bukhari na Muslim Kitabul Ashriba). Kauli ya Mwislamu huyu ilikuwa sawa kabisa. Kwani kama pombe ilikuwa imeharamishwa, wao wangelikuwa na kosa ingekuwa wao kuendelea kunywa; kwa upande mwingine kama pombe haikuwa imeharamishwa, basi hawatakosa mengi kama ingewabidi hii safari moja tu kuiachilia mbali ile pombe iliyo mitungini mwao itiririke mabarabarani. Ulevi ulitoweka kabisa miongoni mwa jamii ya Waislamu baada ya tangazo hili. Hapana jitihada zozote kabambe zilizohitajika kuleta mabadiliko haya ya kimapinduzi. Waislamu walioisikia amri hii na wakaona vile ilivyotiiwa mara moja kwa moyo mkunjufu waliishi miaka sabini au hata thamanini. Hapajulikani kisa cho chote cha Mwislamu ambaye baada ya yeye kusikia katazo hili alionesha udhaifu wa kulihalifu. Na kama palikuwepo na kisa chochote sampuli hii, basi ni sharti iwe kilikuwa ni kisa cha yule mtu ambaye hakupata fursa ya kuishi chini ya athari tukufu ya Mtume[saw]. Linganisha hali hii na zile jitihada za kukataza ulevi huko Marekani, na zile harakati kabambe za upunguzaji pombe ambazo zimefanywa huko Ulaya miaka nenda miaka rudi. Kwa upande mmoja tangazo moja tu la Mtume[saw] lilitosha kung'olea mbali ushetani uliokuwa umemea mizizi katika jamii ya Waarabu. Na kwa upande mwingine, ukatazaji (ulevi) ukafanywa kwa kutunga sheria maalumu. Kikosi cha polisi na wanajeshi, wakaguzi wa idara ya forodha, wote walijitahidi kama timu

moja na kujaribu kuitia komesha tabia mbaya ya kunywa pombe lakini hawakufua dafu na wakalazimika kukiri ushinde wao. Walevi waliambulia ushindi na ushetani wa kulewa haukukomoleka. Zama hizi zetu zasemekana kuwa ni zama za maendelao ya kijamii. Lakini tunapolinganisha zama zetu na zama za Islam ya hapo awali, twashangaa ni zipi baina ya zama hizi mbili zinazostahili kuitwa hivyo — ni hizi zama zetu au ni zile zama ambapo Islam ilileta haya mapinduzi makubwa ya kijamii?

Kilichofanyika kule Uhud hakikuwa kiweze kusahaulika kwa urahisi. Watu wa Makka walidhani vita vya Uhudu vilikuwa ushindi wao wa kwanza dhidi ya Islam. Waliitangaza habari hii Arabuni nzima na wakaifanya chombo cha kuwachochea makabila ya Waarabu dhidi ya Islam na kuwashawishi kwamba Waislamu sio eti hawapigiki. Kama Waislamu wakiendelea kustawi, hiyo si kwa sababu ya nguvu zao wenyewe bali ni kwa sababu ya udhaifu wa majaaliwa ya Waarabu. Ilikuwa ni kwa sababu ya udhaifu wa Waarabu wenyewe waabuduo masanamu. Kama Waarabu wabudu masanamu wakifanya juhudi za pamoja, basi kuwashinda nguvu Waislamu haikuwa kazi ngumu. Matokeo ya propaganda hii yakawa kwamba uhasama dhidi ya Waislamu ukaanza kuchemka mno. Makabila mengine ya Waarabu yakaanza kuwapita watu wa Makka katika kuwataabisha Waislamu. Wengine walianza kuwashambulia kidhahiri shahiri. Wengine wakaanza kuwatia hasara kwa hila. Katika mwaka wa nne wa Hijira, makabila mawili ya Waarabu, 'Adh na Qara, walituma wajumbe wao kwa Mtume[saw] kwenda kumripotia kwamba watu wao wengi walikuwa wameelekea Islam. Wakamtafadhalisha Mtume[saw] awapelekee Waislamu kadha waijuao vizuri Islam, wakakae nao na kuwafundisha hiyo Dini Mpya. Kusema kweli hii ilikuwa ni njama iliyopangwa na watu wa kabila la Banu Lihyan, maadui wakali wa Islam. Wakawatuma hawa wajumbe wao kwa Mtume[saw] wakiwaahidia zawadi nono. Mtume[saw] alilipokea ombi hili bila ya kulitilia shaka na akawatuma Waislamu kumi kwenda kuwafundisha watu wa makabila yale mafundisho ya Kiislamu. Waislamu hawa walipoingia kwenye

ardhi ya kabila la Banu Layhan, wasindikizaji wao waliwapasha habari hii watu wa kabila lile na kuwashawishi wawakamate Waislamu wale au wawaulie mbali. Kufuatia kishawishi hiki cha kikatili, washika silaha mia mbili wa kabila la Lihyan wakijitokeza kuwaandama wale Waislamu na hatimaye kuwafikia mahali palipoitwa Rajii'. Ikazuka patashika baina ya Waislamu kumi na wale maadui mia mbili. Wale Waislamu walijawa tele na imani. Maadui hawakuwa na hata chembe. Wale watu kumi walipanda kilimani na kuwaita kuja kushindana wale mia mbili. Maadui wakatafuta kuwashinda nguvu kwa hila hatari. Wakasema watawaachilia huru, bora tu washuke chini. Lakini mkubwa wa kikundi kile akawajibu akiwaambia kwamba ahadi za makafiri wao hawakuwa wageni nazo. Kusema hivyo, wakajitupa kwa Mwenyezi Mungu na kuomba dua. Mwenyezi Mungu alikuwa ni mwenye kukifahamu sana kizaazaa chao. Je, haikustahili Amjulishe Mtume[saw] wao? Wale makafiri walipokikuta kile kikundi kidogo cha Waislamu kikisimama imara, wakaanza kukipiga vita. Waislamu wale wakapigana kufa na kupona. Saba wao wakafa wakipigana.

Wale watatu waliosalia, makafiri wakawakariria ahadi yao ya kutowadhuru kama wakiteremka chini ya kile kilima. Hawa watatu wakakubaliana na ahadi ya wale makafiri na kushuka chini. Mara waliposhuka chini, wale makafiri wakawakaza kamba. Mmoja wa wale watatu akatamka akisema, "Huu ni uvunjaji wa kwanza wa ahadi yenu. Mungu tu ndiye anayejua mtafanya kitendo gani baada ya hiki". Kusema hivyo, yeye akakataa katakata kwenda nao. Wale makafiri wakaanza kumpiga na kumbaruta njiani. Lakini wakatishiwa sana na kujizatiti kiume na kukita alikokufanya huyu mtu mmoja kiasi hiki kwamba walimuulia mbali pale pale. Wawili waliosalia wakawachukua na wakaenda kuwauzia Makureishi wa Makka kama watumwa. Mmoja wa hao wawili alikuwa ni Hadhrat Khubaib[ra] na mwenzake Hadhrat Zaid[ra]. Mnunuzi wa Hadhrat Khubaib[ra] haja yake ilikuwa ni kumuulia mbali eti kulipiza kisasi cha babake, aliyekuwa ameuawa katika vita vya Badr. Siku moja, Hadhrat Khubaib[ra] katika hali ya kujikwatuakwatua aliitisha wembe. Wembe ule alipokuwa nao

mkononi, mtoto wa pale nyumbani akamjia katika hali ya kudadisidadisi. Hadhrat Khubaib[ra] akmwinua yule mtoto na kumkalisha juu goti lake. Kuona hivyo, mamake mtoto akagutuka sana. Tangu mwanzo yeye uhasama ulikuwa umejaa tele moyoni, na sasa hapa palikuwa na mtu waliyekuwa watamuulia mbali baada ya siku chache akishika wembe vile karibu na mtoto wao. Alikuwa na hakika kwamba Hadhrat Khubaib[ra] alinuia kumuulia mbali mtoto wao; Hadhrat Khubaib[ra] akiona hofu usoni mwa yule mama na akatamka akisema, "Wadhani nitamuua mtoto wako? Usifikirie hivyo hata kidogo. Siwezi nikafanya kitu kama hicho. Waislamu hawadanganyi." Mwanamke yule akavutiwa sana na uaminifu na tabia ya unyofu ya Hadhrat Khubaib[ra]. Tokea hapo akawa yuaikumbuka daima na alikuwa amezoea kusema kwamba alikuwa hajapata kuona mfungwa kama Khubaib. Hatimaye watu wa Makka wakampeleka Hadhrat Kubaib[ra] kwenye uwanja kwenda kusherekea mauaji yake hadharani. Wakati ulipowadia, Hadhrat Khubaib[ra] alitaka ruhusa asali rakaa mbili. Baada ya kumaliza kusali, akasema kwamba nilitaka kuendelea na sala, lakini sikufanya hivyo wasije wakanifikiria kuwa naogopa kifo. Halafu kwa utulivu akamsarendea muuaji shingo yake. Na alipokuwa akifanya hivyo, akawa yuaimba beti hizi:

> Ninapokufa Mwislamu, kiwiliwili changu sijali kiangukie kulia au kushoto. Potelea mbali! Kifo changu ni katika njia ya Allah; Yeye akipenda, anaweza akakibariki kila kipande cha mwili wangu (Bukhari).

Haikuwa Hadhrat Khubaib[ra] kuzimaliza kabisa beti hizi ilipomshukia shingoni mwake dhoruba ya upanga wa muuaji na kichwa chake kudondoka chini upande mmoja. Wale waliokuwa wamekusanyika ili kushangilia mauaji haya ya hadharani walikuwa ni pamoja na mtu mmoja aliyeitwa Sa'id bin 'Amir ambaye baadaye alisilimu. Mtu huyu yuasemekana kwamba kila yalipotajwa mauaji ya Hadhrat Khubaib[ra] akiwepo, alikuwa anazirai. (Hisham). Yule mahabusu mwingine, Hadhrat Zaid[ra], naye pia alipelekwa nje kwenda kuuawa. Miongoni mwa watazamaji wa mauaji yake alikuwemo Abu Sufyan, chifu wa

Makka. Basi Abu Sufyan akamgeukia Hadhrat Zaid[ra] na kutamka akimwuliza, "Si ungependa Muhammad awe hapa badala yako? Si ungeona heri wewe kuwa nyumbani salama salimini, huku Muhammad akiwa mikononi mwetu?"

Hadhrat Zaid[ra] kwa shauku akamjibu akimwambia, "Eti nini, Abu Sufyan? Wasema nini? Wallahi, ni afadhali mimi nifilie mbali kuliko yeye Mtume[saw] kuchomwa na hata kajimwiba katika barabara za Madina". Abu Sufyan hakuwa na jingine ila kuathiriwa sana na kina hiki cha upendo. Akamtazama Hadhrat Zaid[ra] kwa mshangao na bila kusita akatangaza, lakini kwa sauti ya kupimia, akisema, "Haki ya Mungu, mimi sijamjua mtu yeyote kumpenda mwingine sawa na vile Masahaba wa Muhammad wanavyompenda Muhammad" (Hisham, J. 2).

Takriban wakati huu huu baadhi ya watu wa Najd nao pia walimwendea Mtume[saw] awatume Waislamu wende wawafundishe Islam. Mtume[saw] akateua mahafidhi wa Kurani sabini. Kundi hili lilipofika mahali paitwapo Bi'r Ma'uuna, mmoja wao, kwa jina Hadhrat Haraam bin Milhaan[ra] akaenda kwa chifu wa kabila la 'Aamir (mpwawe Baraa) kumfikishia ujumbe wa Islam. Kidhahiri Hadhrat Haraam[ra] alipokewa kwa moyo mkunjufu na watu wa kabila lile. Lakini alipokuwa akisema na yule chifu mtu mmoja alichomoka toka upande wa nyuma na kumpiga mkuji. Hadhrat Haram[ra] akafa pale pale. Ule mkuki alipokuwa ukimkita shingoni Hadhrat Haraam[ra] alisikika akisema, "Mungu ni Mkubwa. Mola wa Kaaba ni shahidi wangu, mimi nimefikia shabaha yangu" (Bukhari). Baada ya kumuua Hadhrat Haraam[ra] kwa njia hii ya kijambazi, viongozi wa kabila lile wakawachochea watu wa kabila lao wawashambulie wale waalimu Waislamu waliosalia. Wakajibu wale watu wakisema, "Jamani, Abu Baraa, chifu wetu, alijitolea kuwa mdhamini; hawa sisi hatuwezi tukawashambulia." Hapo wale machifu wa kikabila, kwa msaada wa yale makabila mawili yaliyokuwa yamekwenda kwa Mtume[saw] kutaka waalimu Waislamu pamwe na makabila mengineyo, wakawashambulia wale Waislamu. Ombi lao la kiutu wakisema, Jamani, "Sisi tumekuja mahubirini na ukufunzini", halikufaa kitu.

Watu wale walianza kuwaua. Wote sabini ila watatu wakauliwa mbali. Mmoja wa wale manusura alikuwa ni kiwete na alikuwa ameishakwea kilimani kabla haijaanza patashika. Wengine wawili walikuwa wamekwenda vichakani kulisha ngamia zao. Waliporudi wakawakuta wenzao sitini na saba wakiwa maiti. Hapo wakashauriana. Mmoja akasema, "Twende tukamripotie Mtume[saw] janga hili". Mwingine akasema, "Mimi siwezi nikapabanduka pale mahali ambapo mkubwa wa kundi letu, ambaye Mtume[saw] wetu amemteua kiongozi wetu, ameuliwa mbali." Kusema hivyo, akawarukia wale makafiri peke yake na akafa akipigana. Yule mwingine akachukuliwa mateka lakini baadaye akaachiliwa katika kutimiza ahadi aliyokuwa ameifanya chifu wa kabila lile. Miongoni mwa wale waliouawa alikuwemo Hadhrat 'Aamir bin Fuhaira[ra] mwachiliwa huru wa Hadhrat Abu Bakr[ra]. Muuaji wake alikuwa ni mtu mmoja aitwaye Jabbar ambaye alikuja kusilimu baadaye. Huyu Jabbar alinasibisha kusilimu kwake na haya mauaji ya kinyama ya Waislamu hawa.

Jabbar yuasimulia akisema, "Mimi nilipoanza kumuua 'Aamir, nilimsikia akisema, "Wallahi nimefikia shabaha yangu". Nikamwuliza mtu fulani mbona Mwislamu asema hivyo anapokuwa akifa. Mtu huyo akasema kwamba Waislamu hukihesabu kifo katika njia ya Allah kuwa ni baraka na ushindi." Jabbar alivutiwa sana na jibu hili kiasi hiki kwamba alianza utalii kabambe wa Islam, na hatimaye akasilimu (Hisham. na Usdul-Ghaba).

Habari za visa hivi viwili vya kusikitisha, ambamo takriban Waislamu thamanin walipoteza maisha yao kama matokeo ya hila mbaya, zilifika Madina sawia. Hawa hawakuwa watu wa kawaida waliouawa. Walikuwa ni mahafidhi wa Kurani. Hawakuwa wamefanya kosa lolote wala kumdhuru yeyote. Hawakuwa wakishiriki kwenye vita vyovyote vile. Walikuwa wamenasishwa mikononi mwa maadui kwa uwongo uliotolewa kwa jina la Allah na dini. Visa hivi vilithibitisha kwa nguvu kwamba uadui dhidi ya Islam ulikuwa umemea tena mpevu. Kwa upande mwingine shauku ya Waislamu kwa ajili ya Islam nayo pia ilikuwa imemea na kupevuka.

MAPAMBANO NA KABILA LA BANU MUSTALIK

Baada ya vita vya Uhud, ilitokea njaa kali Makka. Bila kujali uadui wote waliomfanyia watu wa Makka na bila kujali njama zote walizokuwa wakizifanya kueneza chuki dhidi yake kote nchini, Mtume[saw] alifungua mfuko kuwasaidia maskini wa Makka katika hii hali yao ya dhiki kubwa. Watu wa Makka wakaendelea kutovutiwa hata na ishara hii ya nia njema. Uadui uliendelea bila kupungua. Kusema kweli ulizidi kuwa mbaya. Makabila ambayo hadi kufikia hapo yalikuwa na mapenzi kwa Waislamu nayo pia yakawa maadui. Mojawapo la makabila hayo lilikuwa ni hili kabila la Banu Mustalik. Wao walikuwa na uhusiano mwema na Waislamu. Lakini sasa walikuwa wameanza kuandaa shambulio dhidi ya Madina. Mtume[saw] alipopashwa habari za maandalizi yao, alituma watu kwenda kujua ukweli wa mambo yalivyo. Watu wale wakarudi na kuthibitisha ripoti za hapo awali. Mtume[saw] akaamua kwenda kupambana na hili shambulio jipya. Ndipo yeye alipokusanya jeshi na kuliongoza hadi eneo la kabila la Banu Mustalik. Jeshi la Waislamu lilipokutana na maadui, Mtume[saw] alijaribu kuwanasihi maadui wajiendee zao bila kupigana. Wakakataa. Vita vikapamba moto na baada ya masaa machache maadui wakashindwa.

Kwa vile makafiri wa Makka walikuwa wamekazania chokochoko na makabila rafiki yalikuwa yakigeuka maadui, wanafiki miongoni mwa Waislamu nao pia safari hii walikuwa wamejiingiza kwenda kupigana upande wa Waislamu. Pengine wao walifikiria huenda wakapata fursa ya kufanya uharibifu. Mapambano dhidi ya Banu Mustalik yakamalizika baada ya masaa kidogo. Hivyo wanafiki hawakupata nafasi yoyote ya kufanya madhara wakati wa mapambano yale. Hata hivyo, Mtume[saw] aliamua kukaa katika mji wa Banu Mustalik kwa siku kadha. Katika huu muda wa kukaa kwake ubishi ulizuka baina ya Mwislamu wa Makka na wa Madina wakigombania utekaji maji ya kisima. Yule Mwislamu wa Makka akatokea kuwa ni mtumwa mwachiliwa huru. Akamchapa yule wa Madina, aliyepiga makelele akiwalilia wenzake wa Madina — wajulikanao kama Ansari au

Wasaidizi. Yule wa Makka naye pia akawalilia wenzake wa Makka — wajulikanao kama Muhajirina au Wahamiaji. Mori ukawapanda. Hapana aliyeuliza, kulikoni. Vijana wa pande zote mbili walichomoa panga zao. Hapo Abdullah bin Ubayy bin Salul akaiona hii kuwa ndiyo nafasi ya mwaka. Akaamua kuzidisha fitina. Ule moto wa mori yeye akaumwagilia mafuta kwa kuwachochea Waislamu wa Madina kwa kuwaambia, "Nyinyi mmewatendekeza sana hawa Muhajirina. Ukarimu wenu umewafurisha vichwa, na sasa wao wanajaribu kuwatawaleni kwa kila njia." Maneno haya huenda yangelikuwa na ile athari aliyoitumainia 'Abdullah. Ubishi huu huenda ungelizaa patashika kubwa. Lakini mambo hayakuwa hivyo. 'Abdullah aliikisia visivyo athari ya haya maneno yake ya kichochezi. Hata hivyo, akidhania pengine Maansari walikuwa wameshawishika alijasiri kuendelea akisema:

> Wacha turudi Madina. Ndipo yule aheshimiwaye zaidi miongoni mwa wakazi wake atamtimulia mbali yule mdharauliwa zaidi (Bukhari).

Kwa hii kauli yake ya 'mkazi muheshimiwa zaidi' alijimaanisha yeye mwenyewe, na 'mdharauliwa zaidi' alimaanisha Mtume[saw]. Mara aliposema hivyo, Waaminio Waislamu wakaweza kutambua, wakasema kumbe ni fitina yenyewe. Wakasema kumbe hawakuwa wamesikiliza kauli njema, bali kauli ya Shetani aliyekuwa amekuja kuwapotosha. Akasimama kijana mmoa na akamripotia Mtume[saw] kupitia amiye. Mtume[saw] akamwita Abdullah bin Ubayy ibn Salul na marafikize na akawauliza kilichotokea. Abdullah na marafiki zake wakakanusha kuwa walikuwa wamefanya chochote kama kile wanachokinasibishiwa katika kisa hiki. Mtume hakusema lolote. Lakini ukweli wa mambo ulianza kuzagaa. Muda si muda mwanawe mwenyewe Abdullah bin Ubayy ibn Salul, kwa jina Hadhrat Abdullah[ra] ilimfikia habari hii. Hadhrat Adullah[ra] akamwona Mtume[saw] mara moja, na akasema, "Ewe Mtume, babangu amekutusi. Adhabu yake ni kifo. Ukiamua hivyo, basi mimi ningeona ni afadhali uniamuru mimi niende nikamuulie mbali babangu. Kama

ukimuamuru mtu mwingine, na babangu kuuawa na mtu yule, huenda mimi nikashawishika kulipiza kisasi kwa kumuulia mbali mtu yule. Pengine najichumia hasira za Allah kwa njia hii."

Mtume[saw] akatamka akisema, "Lakini mimi siko huko. Mimi nitamshughulikia babako kwa huruma na upole." Hadhrat Abdullah[ra] alipozilinganisha dharau za babake na hii huruma na upole wa Mtume[saw], alielekea Madina hali akifunukiza hasira zilizomjaa dhidi ya babake. Njiani akamsimamisha babake na akamwambia sitakuruhusu kusonga mbele hadi uitangue kauli yako dhidi ya Mtume. "Mdomo ule ule uliosema eti 'Mtume ni mdharauliwa na wewe ndiwe muheshimiwa', sasa ni sharti useme, 'Mtume ni muheshimiwa na wewe u mdharauliwa.' Mimi sikupishi njia mpaka useme hivyo." Abdullah bin Ubayy ibn Salul akapigwa na butwaa na akashtuka na hapo aksema, "Nakubali mwanangu, ya kuwa Muhammad ni mheshimiwa na kwamba mimi ni mdharauliwa." Ndipo Hadhrat Abdullah[ra] akampisha njia babake (Hisham, J. 2).

Mbeleni tumeyataja makabila mawili ya Mayahudi yaliyobidi kutimuliwa toka Madina kwa sababu ya fitina zao za kichochezi na mauaji. Moja la makabila hayo mawili, Banu Nadhiir, baadhi yao walihamia Siria na wengineo Khaibar, kaskazini mwa mji wa Madina. Khaibar ilikuwa ni ngome madhubuti ya Mayahudi nchini Arabuni. Wale Mayahudi waliokuwa wamehamia kule walianza kuwachochea Waarabu dhidi ya Waislamu. Watu wa Makka tayari walikuwa ni maadui wakali wa Islam. Hapana uchochezi mpya uliohitajika kuwachemsha watu wa Makka dhidi ya Waislamu. Watu wa kabila la Ghatafan wa eno la Najd, kwa sababu ya uhusiano wao mzuri na watu wa Makka, nao pia walikuwa wakiwahasimu Waislamu. Wale Mayahudi wahamiaji ambao sasa walikuwa wanakaa Khaibar wakawatumainia Makureishi wa Makka pamwe na kabila la Ghatafan la upande wa Najd. Isitoshe, walipanga kuyachochea makabila ya Banu Slaim nia Banu Asad dhidi ya Islam. Pia wakawashawishi watu wa kabila la Banu Saad, waliokuwa na urafiki na Mayahudi, waungane na watu wa Makka nguvu moja dhidi ya

Islam. Baada ya njama za muda mrefu ukaundwa muungano wa majeshi ya Waarabu kuwapiga vita Waislamu. Kwenye muunagno huu walikuwemo watu wa Makka, makabila yaliyokuwa yakikaa katika maeneo yaliyozunguka Makka. Makabila ya Najd, na yale yaliyokuwa yakiishi kaskazini mwa mji wa Madina.

VITA VYA HANDAKI

Lilikusanywa jeshi kubwa katika mwaka wa tano wa Hijira. Ukubwa wa jeshi hili umekadiriwa na wanahistoria kuwa maaskari baina ya elfu kumi na elfu ishirini na nne. Lakini muungano wa majeshi ya Waarabu uliokusanywa kutokana na haya makabila mbalimbali usingeliweza kuwa wa eti askari elfu kumi. Elfu ishirini na nne inakuwa idadi iliyo sawa. Bila shaka yawezekana ulikuwa na idadi wa maaskari baina elfu kumi na nane na elfu ishirini. Mji wa Madina ambao majeshi haya yalinuia kuushamabulia ulikuwa ni wa kadiri tu, usioweza kabisa kukabiliana na shambulizi la Arabuni nzima. Idadi ya wakazi wake wakati huo ilikuwa imizidi kidogo wanaume elfu tatu (wakiwemo wazee, vijana na watoto). Kupiga vita watu hawa, maadui walikuwa wamekusanya jeshi la maaskari baina ya elfu ishirini na ishirini na nne, wajuao vita; na (kwa vile walikuwa wamekusanywa kutoka sehemu mbalimbali za Arabuni) wao walikuwa ni jeshi lililokuwa na wanajeshi spesheli. Kwa upande mwingine, idadi ya wakazi wa Madina, wangelioweza kutakikana kupambana na jeshi hili kubwa ilikuwa ni pamoja na wanaume, wa umri wote (wakubwa kwa wadogo). Mtu anaweza akajiamulia mwenyewe ilikuwa ni shari kiasi gani iliyowabidi Waislamu wa Madina kupambana nayo. Hili lilikuwa ni pambano lililoyapita yote kwa kutokuwa nguvu sawa. Maadui walikuwa ni elfu ishirini hadi elfu ishirini na nne katika idadi yao, huku Waislamu wakiwa kama elfu tatu tu wakiwemo, kama tulivyosema, wanaume wote wa mjini, wazee kwa watoto. Mtume[saw] aliposikia maandalizi makubwa ya maadui, alifanya mkutano na akataka ushauri. Miongoni mwa wale waliotakwa ushauri alikuwemo Hadhrat Salman Mwajemi[ra], akiwa ni mtu wa kwanza kusilimu kutoka nchi ya Uajemi. Mtume[saw] akamwuliza Hadhrat Salman[ra] vile

walivyokuwa wakifanya kwao Uajemi ilipowabidi kuuhami mji dhidi ya jeshi kubwa. Hadhrat Salman[ra] akajibu akisema, "Kama mji haukuzungushiwa ngome, na jeshi la pale ni dogo, desturi ya nchi yetu ni kuchimba handaki kuuzunguka na kuuhami tukiwa ndani." Mtume[saw] akakubaliana na rai hii. Mji wa Madina umezungunkwa na vilima upande mmoja. Hiki ni kinga ya asili kwenye eneo hili la mji. Upande mwingine uliojawa na vijibarabara ulijawa na wakazi wengi. Upande huu wa mji usengiliweza kushambulika kwa ghafla. Upande wa tatu ulikuwa na nyumba na mashamba ya mitende, mbali kidogo ilikuweko ngome ya kabila la Mayahudi la Banu Quraidha. Watu wa Banu Quraidha walikuwa wamefanya mkataba wa amani na Waislamu. Hivyo basi, upande huu nao pia ulihesabiwa kuwa salama dhidi ya mashambulio ya maadui. Upande wa nne ulikuwa ni ardhi wazi na ilikuwa ni kutoka upande huu shambulio la maadui lilikokuwa na uwezekano mkubwa zaidi kufanyika na lilikotarajiwa zaidi. Hivyo basi, Mtume[saw] akaamua kuchimba handaki upande uliokuwa wazi kuwazuia maadui wasishambulie kwa ghafla. Kazi iligawanywa miongoni mwa Waislamu — watu kumi wachimbe yadi kumi za handaki. Kwa jumla handaki la maili moja, la upana na kina cha kutosha, lilibidi kuchimbwa.

Kazi ya kuchimba ilipokuwa imepamba moto, wakafikia mwamba ambao Waislamu wachimba handaki waliuona usiowezekana. Ripoti ikafikishiwa Mtume[saw] aliyefika mahali pale mara moja. Akishika sururu Mtume[saw] alilitwanga vikali jiwe lile. Zikatoka cheche, na Mtume[saw] akatamka kwa sauti kubwa akisema, "Allahu Akbar." Akaupiga dharuba nyingine. Pakatokea tena cheche na Mtume[saw] aksema tena, "Allahu Akbar." Akaufuatilia na dharuba ya tatu. Cheche zikatoka tena, na Mtume[saw] akasema, Allahu Akbar na ule mwamba ukawa umevunjika vipandevipande. Masahaba wakamwuliza Mtume[saw] mambo haya yote. Mbona alirudiarudia kusema, "Allahu Akbar?" Mtume[saw] akasema:

> "Mimi niliupiga mwamba huu dharuba tatu za hii sururu, na nikaona mara tatu ikifunuliwa kwangu taadhima ya Islam ya

> siku zijazo. Katika mwako wa cheche za kwanza niliona majumba ya Kifalme ya huko Siria ya Himaya ya Kirumi. Nikawa mimi nimepewa funguo za majumba yale. Safari ya pili nikaona majumba ya kifalme yenye mwangaza ya Himaya ya Uajemi mjini Madain, na nikawa nimepewa funguo za Ufalme wa Uajemi. Safari ya tatu nikaona milango ya San'aa na nikawa nimepewa funguo za Ufalme wa Yemeni. Hizi ni ahadi za Mwenyezi Mungu nami natumaini mtakuwa na matumaini nazo. Maadui hawawezi kuwadhuruni (Zurqani, J. 2)

Kwa sababu ya uhaba wa nguvu-kazi, lile handaki waliloweza kuchimba Waislamu lisingeliweza kuwa handaki zuri kwa upande wa mbinu za kijeshi lakini ilionekana kana kwamba lilikuwa linakinga angalau uingiaji mjini wa maadui kwa ghafla. Na ukweli ya kwamba halikuwa lisilovukika wathibitishwa vya kutosha na visa vya baadaye ndani ya vita vile. Hapana upande mwingine uliofaa maadui kufanyia mashambulio yao ya mji wa Madina.

Hivyo ikawa kwamba lile jeshi kubwa la makabila ya Waarabu kuanza kuisogelea Madina kutoka upande huu wa handaki. Kusikia hivyo, Mtume[saw] akajitokeza kuihami Madina akiandamana na kikosi cha watu elfu moja na mia mbili akiwa amewatuma watu wengine kwenda linda sehemu zingine za mji.

Wanahistoria wanatoa makadirio mbalimbali ya idadi ya wale waliojitokeza kulilinda lile handaki. Wengine wanasema ni watu elfu tatu, na wengine wanasema ni kati ya watu elfu moja mia mbili hadi elfu moja mia tatu, na baadhi yao wanawakisia kuwa walikuwa ni watu mia saba tu. Makisio haya yanatofautiana na yanaonekana ni vigumu kuyapatanisha. Lakini, baada ya kuchunguza ushahidi, sisi tumefikia uamuzi kwamba makisio haya yote matatu ya idadi ya Waislamu waliojishughulisha kulilinda handaki yako sawa. Yanahusikana na nyakati mbalimbali za vita vile.

VITA VISIVYOSHINDIKA

Tumekwishakubaliana kwamba, baada ya kujiondoa kwa wanafiki vitani Uhud, idadi ya Waislamu waliosalia vitani ilikuwa ni mia saba. Vita vya Handaki vilifanyika miaka miwili tu baada ya Vita vya Uhud. Katika miaka miwili hii hapakuwepo na kusilimu kwingi kunakorekodiwa hisroriani. Katika wakati huu haliwezi likatarajiwa ongezeko la wapiganaji Waislamu kutoka mia saba hadi elfu tatu. Wakati huo huo haielekei kwamba hapakuwepo na ongezeko la Waislamu wapiganaji baina ya Vita vya Uhud na Vita vya Handaki. Idadi ya Waislamu iliendelea kuongezeka baina ya vita hivyo viwili. Kutokana na fikara hizi mbili, yaelekea kuwepo na uwezekano kwamba yale makisio yanayoifanya idadi ya wapiganaji Waislamu katika Vita vya Handaki kuwa elfu moja na mia mbili ni sawa. Swali la pekee la kujibiwa ni, mbona wengine wanarekodi wapiganaji elfu tatu na wengine mia saba. Jibu letu kwa swali hili ni kwamba tarakimu hizo mbili zahusikana na nyakati mbili tofauti za vita vyenyewe. Vita vya Uhud vilipiganwa katika sehemu tatu. Tulikuwa na sehemu ya kwanza kabla maadui hawajaja karibu na Madina, na Waislamu walikuwa wakishughulikia uchimbaji wa handaki. Katika wakati huu, tunaweza tukafikiria kwamba kwenye kazi ya kuusomba kando udongo uliochimbwa, watoto na kwa kiasi fulani pengine hata wanawake ni sharti wawe walifika kusaidia. Hivyo, kwenye uchimbaji wa handaki tunaweza tukaechukulia kwamba kwa jumla watu elfu tatu walitumika upande wa Waislamu. Idadi yenyewe ilijumisha watoto na akina mama. Watoto waliweza kusaidia katika usombaji wa udongo, wanawake ambao daima walishindana na wanaume katika kuzisaidia harakati za Waislamu, ni sharti wawe walitumiwa kufanya kazi mbalimbali zilizohusikana na uchimbaji. Upo ushahidi wa kuungia mkono rai hii. Uchimbaji ulipoanza, hata watoto walitakiwa wajitokeze. Kwa kweli wakazi wote walijumuika kwenye uchimbaji. Lakini mara tu maadui walipofika na vita kuanza, Mtume[saw] aliwaamuru vijana wa chini ya umri wa miaka kumi na mitano kuondoka kwenye uwanja wa vita. Wale waliozidi umri huo

waliruhusiwa kupigana ikiwa walitaka (Halabiyya, J. 2). Kutokana na jambo hili yaonekana kwamba wakati wa uchimbaji, idadi ya Waislamu ilikuwa kubwa kuliko wakati vita vilipoanza. Wakati wa vita watoto wote wadogo walikuwa wamejiondokea. Yale makadirio yanayoifanya idadi ya Waislamu kwenye vita vile kuwa elfu tatu yanahusikana na zama za uchimbaji tu, na yale yanayoifanya idadi hiyo kuwa elfu moja na mia mbili yanahusikana na wakati wa vita vyenyewe ambapo watu wazima peke yao ndio waliopigana. Makadirio ya pekee ambayo sisi hatukuyaelezea ni yale yanayoifanya idadi hiyo kuwa watu mia saba. Hata makadirio haya tuonavyo sisi ni sawa. Makadirio haya yamewasilishwa na mtu mwenye kutegemeka akiwa ni Ibn Isihak, anayeungwa mkono na Ibn Hazm. Ni vigumu kuyadadisi makadirio haya. Kwa bahati nzuri, tunapozisarifu habari zingine za vita hivi, hata makadirio haya nayo pia yanakuwa sawa. Upo ushahidi kuonesha kwamba pale watu wa kabila la Banu Quraidha, kinyume na ahadi yao, walipoungana na maadui, na kuamua kuishambulia Madina kutoka upande wa nyuma, Mtume[saw] akiwa amefahamishwa nia yao hatari, aliamua kuweka walinzi kwenye ule upande wa mji uliokabiliwa na mashambulizi ya watu wa kabila hilo la Banu Quraidha. Upande huu wa mji mwanzoni ulikuwa umeachwa bila ya ulinzi kwa kuwa kabila hili la Banu Quraidha lilikuwa likielewana na Waislamu. Na ilikuwa ikitarajiwa kwamba wasingeliwaruhusu maadui kushambulia mji wa Madina kutoka upande wao. Yafahamika kwamba usaliti wa kabila la Banu Quraidha uliporipotiwa Mtume[saw] na ikawa dhahiri kwamba wanawake wa Kiislamu, waliohesabiwa kuwa ni salama katika upande huu wa mji kwa sababu ya kule kuelewana kulikokuwepo, hawakuwa tena salama, Mtume[saw] aliamua kupeleka vikosi viwili, vya watu mia mbili na mia tatu, kulinda sehemu mbili tofauti za ile sehemu ya mji ambayo sasa haikuwa tena usalama. Mtume[saw] akawaagiza kila mara wapige ukelele wa "Allahu Akbar", kusudi jeshi zima la Waislamu lipate kujua kwamba akina mama Waislamu wako salama salimini. Yale makadirio ya Ibn Isihak, hivyo basi, yanayoifanya idadi ya wapiganaji katika vita

vya Handaki kuwa ni mia saba, nayo pia ni sawa. Ikiwa watu mia tano kutoka miongoni mwa watu elfu moja na mia mbili walipelekwa kulinda upande wa nyuma wa mji, basi hapana budi walisalia mia saba tu. Ndiposa makadirio yote matatu ya ukubwa wa jeshi la Waislamu katika vita vya Handaki yanakuwa ni sawa.

Hivyo basi, katika kulilinda handaki Mtume Mtukufu[saw] alikuwa na watu mia saba tu. Naam, handaki lilikuwa limechimbwa tayari. Lakini kulihami na kuzuilia jeshi kubwa kama lile maadui walilokuwanalo, hata kwa msaada wa handaki lile lilionekana kuwa ni bamba gumu lisilowezekana. Lakini kama kawaida yao Waislamu walimtegemea Mola wao na kutumainia msaada Wake. Jeshi lao dogo lilikaa chonjo likawangojea maadui, ambapo wanawake na watoto walikuwa wamepelekwa sehemu mbili za mji zilizoonekana kuwa ni salama. Maadui walipofika handakini, walitaharuki kwa sababu mbinu hii ya kivita haikuwa imepata kutumiwa hapo kabla katika vita vyovyote vya Waarabu. Hivyo basi wakaamua kupiga kambi kwenye upande wao wa handaki na kupanga mbinu za kushambulia na kuingilia Madina. Upande mmoja wa Madina ulikuwa ukilindwa na lile handaki. Upande wa pili ulikuwa na vilima vilivyokuwa ulinzi wa kimaumbile. Upande wa tatu ulikuwa na nyumba za mawe na viunga vya miti. Haikuwezekana kwa maadui kuufanyia shambulio la ghafla upande wowote wa mji. Majemadari wa maadui wakashauriana pamoja na kuamua kwamba ilibidi kulishawishi kabila la Banu Quraidha, ambao walikuwa Mayahudi waliokuwa wakali wakiishi Madina, dhidi ya maelewano yao na Waislamu na kuwataka wajiunge na lile genge la majeshi ya Waarabu katika shambulio hili muhimu dhidi ya mji wa Madina. Ni hawa Banu Quraidha peke yao wangelioweza kuwapatia mwanya kuingilia Madina. Hatimaye Abu Sufyan akamteua Huyai bin Akhtab, chifu wa lile kabila lililotimuliwa la Banu Nadhiir na mchochezi mkubwa wa Waarabu dhidi ya Madina, akamwidhinisha aende kula njama na kabila la Banu Quraidha papatikane uwezekano wa kuushambulia mji kutoka upande wa nyuma. Huyai bin Akhtab akaenda kwenye ngome ya wale Mayahudi kuonana na kiongozi wa

kabila lile. Mwanzoni walikataa kuonana naye. Lakini alipofafanua kwamba hii ndiyo iliyokuwa nafasi hasa ya kuwakomolea mbali Waislamu, akafanikiwa kumvutia mtu mmoja wa kabila lile, kwa jina Ka'b. Alizidi kuelezea kwamba Arabuni nzima ilikuwa imejitokeza kuwaangamiza Waislamu. Jeshi lililokuwa limepiga kambi upande wa pili wa handaki halikuwa ni jeshi kwa hakika, bali ilikuwa ni bahari nzima ya watu wenye nguvu ambao isingeliwezekana kwa Waislamu kuwashinda. Hatimaye ikakubaliwa kwamba mara tu baada ya jeshi la maadui kufaulu kulivuka handaki watu wa kabila la Banu Quraidha wataishambulia ile sehemu ya Madina ambayo Mtume Mtukufu alikuwa amewapeleka wanawake na watoto ili wapate kusalimika. Ukatokea mpango huu kuaminika kwamba ungelizima kabisa upinzani wa Waislamu, na kuwatumbukiza watu wao wote kwenye janga la mauti — wanaume, wanawake na hata watoto. Kama mpango huu ungejipatia nafasi ya kufua dafu hata ile ndogo kiasi gani, ingeliwatia hasara kubwa Waislamu na kuvuruga mambo kabisa kwa ajili yao. Wasingelikuwa na mwanya wa kuliepukia janga hili.

USALITI WA KABILA LA BANU QURAIDHA

Kama tulivyosema, kabila la Banu Quraidha lilikuwa na maelewano na Waislamu. Hata kama wasingelijitia vitani upande wa Waislamu, ilikuwa ikitarajiwa kwamba wao kwa akali upande wa kwao wangeliwafungia njia maadui. Hivyo, ikawa Mtume[saw] kuuacha upande ule bila ya ulinzi kabisa. Kabila hili lilijua kwamba ahadi yao Waislamu waliiamini. Basi walipoamua kuungana na jeshi la Waarabu, ikakubaliwa kwamba hawatajiunga nalo kiwaziwazi wasije Waislamu wakawa macho na kuchukua hatua za kuihami ile sehemu ya mji kuliko kuweko na kabila la Banu Quraidha. Njama hii ilikuwa hatari sana.

Ilipokubaliwa kwamba Waislamu wawe watashambuliwa kutoka pande mbili, jeshi la Waarabu lilianza kulivamia handaki. Hata hivyo, ilipita siku kadha, bila chochote kufanyika. Hapo wakapata wazo la kuwaweka washikapinde wao kilimani na kuwataka wavishambulie

vikosi vya Waislamu viliivyokuwa vikililinda lile handaki. Wanajeshi hawa wakasimama ukingoni mwa kilima wakitengana kwa hatua chache. Mara Waislamu walipoonesha alama ya kulegea, makafiri wakawa wanajaribu kulivuka handaki kwa msaada wa wapanadafarasi wao hodari. Waliamini kwamba endapo ushambulizi sampuli hii utarudiwarudiwa, basi wao wangelijitekea sehemu katika upande wa Waislamu wa lile handaki wangeliyoweza kupitishia majeshi yao tayari kuushambulia mji kwa nguvu zao zote. Hivyo basi, ikawa kufanyika shambulio baada ya shambulio. Walindaji handaki wa Kiislamu ikabidi wapigane bila ya kupumzika. Siku moja walishughulika sana na uzimaji wa mashambulio haya kiasi hiki kwamba baadhi ya sala za kila siku hazikuweza kusalika katika wakati wake. Jambo hili lilimuudhi sana Mtume[saw] na akatamka akisema, "Mwenyezi Mungu waadhibu makafiri hawa, wametuvurugia sala zetu." Kisa hiki chaonesha vile yalivyokuwa makali mashambulio ya maadui. Lakini pia chaonesha kwamba jambo la kwanza na la mwisho alilolitaka Mtume[saw] ilikuwa ni ibada ya Allah. Mji wa Madina ulikuwa umezingirwa pande zote. Sio tu wanaume, bali hata wanawake na watoto walikabiliwa na kifo kisichoepukika. Mji mzima ulikuwa kwenye kilindi cha mahangaiko. Lakini hata hivyo Mtume[saw] alitilia maanani haja ya kusali sala za kila siku katika wakati wake. Waislamu hawamwabudu Mwenyezi Mungu mara moja tu kwa wiki chambileche Wakristo na Mabaniani. Waislamu wanatakiwa kuabudu mara tano kila siku. Wakati wa vita, kusali hata sala moja inakuwa ni vigumu, achilia mbali kusali sala za jamaa mara tano kila siku. Lakini Mtume[saw] alisalisha hizi sala tano kila siku hata wakati wa vita. Kama ilitokea moja ya sala hizi kuvurugwa na mashambulio ya maadui, basi hili lilimuhuzunisha sana.

Tukirudia uwanja wa vita, maadui walikuwa wakishambulia kutoka upande wa mbele, watu wa kabila la Banu Quraidha walikuwa wakijiandaa kushambulia kutoka upande wa nyuma lakini kwa njia isingeliyoweza kuwafanya wakazi Waislamu wawe macho. Wao walikusudia kujipenyeza mjini kutoka upande wa nyuma na kuwaulia

mbali akina mama na watoto waliositiriwa kule. Siku moja watu wa kabila la Banu Quraidha walituma jasusi kuona iwapo kulikuwa kumewekwa ulinzi kwa ajili ya wanawake na watoto, na kama kunao walinzi, basi wajue ni wanagapi. Palikuwepo na nyumba maalum pamoja na kiwanja chake kwa familia maadui walizozifikiria kuwa ndizo hasa windo lao maalumu. Yule jasusi akaja na kuanza kuivinjari sehemu hii kwa njia yenye kutiika shaka. Alipokuwa akifanya hivyo, Hadhrat Safiyya[ra] shangaziye Mtume[saw], akamwona. Ikatokea kwamba ni mwanamume mmoja tu ndiye aliyekuwa akishika doria wakati ule bali alikuwa mgonjwa. Hadhrat Safiyya[ra] akamripotia alichokiona na akamtaka amtie mbaroni jasusi huyu kabla hajaweza kuwajulisha maadui vile wanawake na watoto walivyokuwa hawana ulinzi katika sehemu ile ya mji. Mwislamu huyu mgonjwa akakataa kufanya chochote ambapo Hadhrat Safiyya[ra] alishika gongo na kuanza kumshambulia yule mtu asiyetakikana. Kwa msaada wa akina mama wengine akafanikiwa kumshinda nguvu na kumuulia mbali. Baadaye ikafahamika kwamba mtu huyu alikuwa kweli jasusi wa Banu Quraidha. Waislamu wakashtuka na kuanza kutazamia mashambulio mengine kutoka ule upande uliokuwa wao wameufikiria kuwa salama salimini. Lakini mashambulio ya upande wa mbele yalikuwa ni makali kiasi hiki kwamba jeshi zima la Waislamu lilihitajika kupambana nayo. Hata hivyo, Mtume[saw] aliamua kubandua sehemu ya jeshi kwa ajili ya usalama wa wanawake na watoto. Kama vile tulivyosema katika maelezo yetu ya idadi ya Waislamu katika vita hivi, kutoka watu elfu moja mia mbili, Mtume[saw] alipeleka mia tano kwa ajili ya ulinzi wa akina mama mle mjini. Kwa hiyo, watu mia saba peke yake ndio waliobakia kulihami handaki dhidi ya jeshi la watu baina ya elfu kumi na nane na ishirini. Waislamu wengi kushtushwa na kutowezekana kwa mapambano waliyotakiwa kukabiliana nayo. Wakamwendea Mtume[saw] na kumripotia vile hali ilivyokuwa ya kutowezekana, na vile ilivyoonekana kutowezekana kuuokoa mji wa Madina. Walimtafadhalisha Mtume[saw] aombe. Aidha walimtaka awafundishe dua maalumu ya wakati wa kizaazaa hiki. Mtume[saw]

akajibu akiwaambia, "Msiogope. Muombeni tu Mwenyezi Mungu awalindeni dhidi ya udhaifu wenu, awaimarishe nyoyo zenu, na kuwaondolea mahangaiko." Mtume mwenyewe akaomba dua kwa maneno yafuatayo:

> Mwenyezi Mungu, Wewe umeniletea Kurani. Wewe huchelei kumsuta yeyote. Hili genge lililokuja kutushambulia, lipatie ushinde. Mwenyezi Mungu, narudia kukuomba: Washinde, tushindishe juu yao, zipindukize shabaha zao zote mbaya (Bukhari).

Na tena:

> Mwenyezi Mungu, Wewe huwasikiza wale wanaokulilia wakiwa taabani na katika dhiki. Wewe huwatakabalia wale walioshikwa na taharuki. Niondolee huzuni yangu, taharuki yangu na uhofiaji wangu. Wewe wajua ni hatari gani inayonikabili mimi na Masahaba wangu (Zurqani).

Wanafiki walishtuka zaidi kuliko wengine katika jeshi la Waislamu. Hawakuchelea tena heshima ya jeshi lao na usalama wa mji wao, wanawake wao na watoto. Lakini hawakutaka kufedheheka machoni pa wenzao. Hivyo basi, wao walianza mmoja baada ya mwingine kuwatoroka Waislamu kwa visingizio visivyokuwa na maana. Kurani yaligusia jambo hili katika aya isemayo:

> Na kundi jingine miongoni mwao likaomba ruhusa kwa Mtume kwa kusema: "Hakika nyumba zetu zimeachwa pweke" lakini hazikuwa zimeachwa pweke, hawakutaka ila kutoroka tu (Sura Al-Ahzaab, 33:14).

Hali ya vita ya wakati ule, na hali waliyokuwemo Waislamu yaelezewa katika Kurani kwenye aya zisemazo:

> Walipowajieni (kuwashambulieni) kutoka juu yenu na kutoka chini yenu; na macho yaliponywea na mioyo ikapanda kooni, nanyi mkaanza kumdhania Mwenyezi Mungu dhana mbalimbali. Hapo waaminio walijaribiwa na wakatetemeshwa

> kwa tetemeko kali. Na waliposema wanafiki na wale wenye maradhi mioyoni mwao, Mwenyezi Mungu na Mtume Wake hawakutuahidi ila udanganyifu mtupu. Na taifa moja miongoni mwao liliposema: Enyi watu wa Yathrib! Hapa si mahali pa kukaa nyinyi, basi rudini (Sura Al-Ahzaab, 33: 11-14).

Hapa Waislamu wanakumbushwa vile walivyoshambuliwa kutoka upande wa mbele na majeshi ya muungano wa Waarabu, na kutoka upande wa nyuma na Mayahudi. Wanakumbushwa vile walivyokuwa taabani wakati ule. Macho yao yaliwanywea na nyoyo zao kufikia kooni. Bali wao hata walianza kumshuku Mwenyezi Mungu. Hapo waaminio walikuwa mtihanini. Wote walitetemeshwa. Wanafiki na wale wenye maradhi nyoyoni mwao wakaanza kusema, "Tumedanganyika kwa ahadi za uongo tulizopewa na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake!" Kundi moja miongoni mwao hata likaanza kuwashtusha Waislamu likiwaambia, "Sasa hapa hapana vita. Hapana la kufanya ila kurudi nyumbani."

Vile waaminio wa kweli walivyofanya katika vita hivi nalo pia ni jambo linaloelezewa ndani ya Kurani katika aya zisemezo:

> Na waamiinio walipoyaona majeshi, walisema, "Haya ndiyo aliyotuahidi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake; Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wamesema kweli; na haikuwazidishia ila imani na utii. Wapo watu miongoni mwa waaminio waliotimiza ahadi waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu: hivi baadhi yao wamekwisha maliza nadhiri zao, na wako miongoni mwao wanaongojea, wala hawakubadilika hata kidogo (Sura Al-Ahzaab, 33:23-24).

Ndio kusema kwamba waaminio halisi walitofutiana na wanafiki na wenye imani dhaifu. Walipoona majeshi chungu nzima ya maadui, yaliwakumbusha walichokuwa wameambiwa tayari na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hili shambulio nguvu-moja la makabila ya Waarabu lilikuwa ni dalili tu ya ukweli wa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake[saw]. Waaminio halisi hawakutikisika. Bali walizidi katika

hali yao ya utiifu na jazba ya imani. Waaminio halisi walishikilia ahadi yao na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao walikuwa tayari wamefikia shabaha ya maisha yao kwa kufa wakipigana. Wengine walikuwa wakisubiri tu wafe katika njia ya Allah na kufikia shabaha yao.

Maadui walilishambulia handaki tena na tena vikali mno. Wakati mwingine walifaulu kulivika. Siku moja, majemadari wakuu wa maadui walifaulu kulivuka handaki. Lakini wakashambuliwa kishujaa na Waislamu kiasi hiki kwamba iliwabidi kurudi nyuma. Katika mapigano haya, Naufal, kiongozi mkubwa wa maadui, aliaga dunia. Huyu alikuwa ni kiongozi mkubwa kiasi hiki kwamba makafiri walidhani wasingeliweza kuvumilia mwili wake kufanyiwa maovu. Hivyo basi, wakampelekea ujumbe Mtume[saw] wakisema kwamba wao wangelipa dinari elfu kumi. Hii ilikuwa ni bei kubwa kulipia kurudishwa kwa maiti yule. Hili lilikuwa ni ombi walilolifanya kutokana na makosa yao. Makafiri wenyewe walikuwa wamezikata-kakata maiti za Waislamu katika vita vya Uhud na sasa wakahofia kwamba Waislamu nao wangelifanya vivyo hivyo. Islam iliharamisha moja kwa moja ukatakataji wa maiti. Mtume[saw] alipopata ombi hili na toleo la malipo, yeye alitamka akisema, "Kwani sisi tuna kazi gani na maiti huyu? Tutawarejeshea bure. Mkipenda mwaweza mkamchukua" (Zurqani, J. uk. 114).

Sehemu ya kitabu cha Bwana Muir kwa jina ***Life of Muhammad*** (kilichotolewa mjini London mwaka wa 1878, uk. wa 322) yaelezea ukali wa mashambulizi dhidi ya Waislamu. Wala hatujutii kuikariri hapa:

> Asubuhi yake, Muhammad akakuta zimekusanywa nguvu zote za makabila yaliyoungana dhidi yake. Kilitakikana kibarua kikali na usimeme wa kupindukia kwa upande wake kuzima mashambulio ya maadui. Ikawa mara maadui kutishia kushambulia wote kwa pamoja; na mara kujigawa vikosi vikosi na kuwa wenye kushambulia sehemu mbalimbali kwa wepesi wa kutisha; na mwishowe, huku wakijitafutia nafasi nzuri, wakawa wenye kukusanya vikosi vyao kulenga sehemu isiyolindwa sana,

> na, wakiwa chini ya kivuli cha ufyatuaji wa mishale uumizao na wenye kuendelea, kujaribu kulivamia handaki. Tena na tena jaribio la kishujaa lilifanywa kupenya mjini, na kulifikia hema la Muhammad, na viongozi wasifika kama vile akina Khalid na 'Amr; na majaribio haya yote yakazimwa tu kwa mbinu za kipinzani na ufyatuaji wa mishale usiokoma. Moto huu wa vita uliendelea kuwaka mchana kutwa; na kwa vile jeshi la Muhammad lilitoshea tu ulinzi wa urefu wa handaki, hawakuwa na wa kubadilishana nao. Hata wakati wa usiku Khalid na kikosi madhubuti cha wapanda farasi, aliendelea kutishia, na huku akihatarisha ulinzi, alilazimisha kuwepo na ulinzi wa doria wa mara kwa mara. Lakimi jitihada zote za maadui hazikufua dafu. Handaki halikuvukika.

Vita vilikuwa vimepiganwa siku mbili. Lakini bado hapakuwa pametokea mapigano ya mkono kwa mkono, hapakuwepo na umwagikaji mkubwa wa damu. Saa ishirini na nne za mapigano zilikuwa tu na matokeo ya vifo vitatu kwa upande wa maadui na vitano kwa upande wa Waislamu. Hadhrat Sa'd bin Mu'adh[ra], chifu wa kabila la Aus, na mtu mwenye kumpenda sana Mtume[saw], alijeruhiwa. Hata hivyo, kushambuliwa kwa handaki kwa mara kwa mara kulisababisha uharibifu, na huu ulirahisisha mashambulio zaidi. Pakashuhudiwa matuko makubwa ya ushujaa na uaminifu. Ulikuwa ni usiku wenye baridi kali, pengine wa baridi kali zaidi Arabuni nzima. Twasikia kutokana na kauli ya Hadhrat Aisha[ra], mke mtakatifu wa Mtume[saw] ya kuwa Mtume[saw] aliamka usingizini mara kwa mara kwenda linda sehemu ya handaki iliyoharibiwa. Akachoka sana. Akarudi kitandani lakini kisaha baada ya kusikia joto kidogo, alirudi tena kulilinda handaki. Siku moja alikuwa amechoka mno hivi kwamba alionekana kutoweza kujimudu. Hapo akasema kwamba alitamani laiti angelitokea Mwislamu mmoja wa dhati kubadilishana naye zamu ya kulinda handaki katika baridi ya usiku. Mara akasikia sauti. Ilikuwa ni Hadhrat Sa'd bin Waqqas[ra]. Mtume[saw] akamwuliza amefuata nini. Hadhrat Sa'd[ra] akajibu akisema, "Nimekuja kukulinda wewe."

Mtume[saw] akasema, "Hapana haja ya kunilinda. Sehemu moja ya handaki imeharibiwa. Nenda ukailinde ili Waislamu wawe salama." Hadhrat Sa'd[ra] akaenda kule, na Mtume[saw] akaweza kupata usingizi. (Lakini mwenye bahati habahatishi. Kwani wakati Mtume[saw] alipowasili Madina na hatari dhidi ya maisha yake kuwa kubwa, hata wakati ule ilikuwa ni Hadhrat Sa'd[ra] aliyejitolea kumlinda). Safari nyingine katika huu wakati mgumu, Mtume[saw] alisikia sauti ya silaha. Akauliza akisema, "Ni nani huyo?" Jawabu likawa, "Ni mimi Abbad bin Bishr," Mtume akauliza,"Una mtu mwingine?" Hadhrat Abbad[ra] akasema, "Naam. Masahaba kadha. Tutalinda hema lako".

"Msijali hema langu. Makafiri wanajaribu kuvuka handaki, Nendeni mkawapige vita." (Halabiyya, J. 2).

Kama vile tulivyosema hapo mbele, Mayahudi walijaribu kuingia mjini kwa hila. Jasusi wa Kiyahudi alikufa katika jaribio lao hili. Walipogundua kwamba njama zao zilikuwa zimefichulika, walianza kuyasaidia majeshi ya mwungano wa Waarabu kwa uwazi zaidi. Hata hivyo, shambulio la pamoja la upande wa nyuma halikujaribiwa, kwa sababu uwanja sehemu hii ulikuwa ni finyu na kule kupelekwa kwa walinzi wa Kiislamu katika sehemu ile kulikuwa kumelifanya shambulio kubwa kutowezekana. Lakini siku kadha baadaye, Mayahudi na ule mwungano wa majeshi ya wapagani waliamua wote wawashambulie Waislamu kwa wakati mmoja na kwa ghafla.

MAJESHI YA MWUNGANO WA WAARABU YAFUMUKANA

Lakini, mpango huu hatari ukavurugwa na Mwenyezi Mungu kwa njia ya ajabu. Ulivurugwa hivi. Mtu mmoja aitwaye Nu'aim, wa kabila la Ghatafan, aliitokea kuvutiwa na Islam. Yeye alikuwa ameandamana na majeshi ya makafiri lakini akatafuta mwanya wa kuwasaidia Waislamu. Yeye peke yake asingeliweza kufua dafu. Lakini alipoona kwamba Mayahudi walikuwa wameungana na Waarabu na Waislamu wakawa wanakabiliwa na kifo kisichoepukika na maangamio, Nu'aim alikata shauri kufanya awezavyo kuwanusuru Waislamu. Akawaendea Banu Quraidha na kuongea na machifu wao. Ikitokea majeshi ya

Waarabu kukimbia, wao walidhani Waislamu wangefanya nini? Mayahudi wakiwa na mapatano na Waislamu, je, haiwabidi kuwa tayari kutiwa ile adhabu inayowastahili wale wanaokwenda kinyume na mapatano? Udadisi huu uliwashtusha wale viongozi wa Kiyahudi. Wakamwuliza iliwabidi wafanye nini. Nu'aim akawashauri kudai wapewe wapagani sabini kama dhamana. Kama mwungano huu wa wapagani wa Kiarabu kweli unathamini watilia maanani mashambulio ya pamoja basi ombi hili hawatalikatalia mbali. Na waseme kwamba hawa sabini watalinda sehemu zao muhimu, wakati wao Mayahudi wenyewe wawashambuliapo Waislamu kutoka upande wa nyuma. Baada ya mazungumzo haya na Mayahudi, alikwenda kwa viongozi wa wapagani. Akawauliza wangelifanya kitu gani kama ingelitokea Mayahudi kuhalifu mkataba wao; kama wao, ili kuwaridhisha Waislamu wangeitisha wapagani kadha kuwa kama dhamana na kisha kuwakabidhi Waislamu. Je, haikuwa muhimu kwao wao kupima uaminifu wa Mayahudi na kuwataka washiriki upesi kwenye hili shambulio la pamoja? Machifu wa kipagani wakavutiwa na ushauri huu. Wakiwa wameutilia maanani, waliwapelekea Mayahudi ujumbe wakiwauliza kama sasa hawataushambulia mji kutoka upande wa nyuma kwa vile sasa wao (majeshi ya mwungano) wamejiandaa tayari kwa lile shambulio liliopangwa. Mayahudi wakajibu wakisema kwamba kesho yake ni sabato yao na wasingeliweza kupigana siku hiyo. Aidha, wakadai wakisema kwamba wao walikuwa ni wakazi wa Madina, na majeshi yote ya mwungano yalikuwa ni ya watu waliotoka nje ya Madina. Je, ikitokea Waarabu kukimbia vitani, sisi Mayahudi tutafanya nini? Kwa hiyo, Waarabu na wawatoe dhamana watu sabini. Ndipo Mayahudi watakuwa tayari kutekeleza sehemu yao ya ushambulizi. Kutiliana shaka kulikuwa tayari kumezuka. Waarabu walilikatalia mbali ombi la Mayahudi. Kama Mayahudi walikuwa na uaminifu katika mkataba wao na Waarabu, hapakuwepo na maana yoyote ya aina ya mapendekezo waliyokuwa wameyafanya. Kwa kuwa shuku huvunja moyo, majeshi ya Waarabu yakapotelewa na mori wao, na usiku ulipoingia, yakaenda kulala yakilemewa na shuku

na shida. Majemadari na askari wote wakaenda kwao mahemani kwa moyo mzito. Kisha muujiza ukafanyika, msaada kutoka mbinguni ukawajia Waislamu. Upepo mkali ulianza kuvuma. Mahema yakang'olewa mbali. Vyungu vikatekuliwa mafigani. Mioto ikazimika. Wapagani walikuwa na desturi ya kuwacha moto uwake usiku kucha. Kwao wao moto unaowaka ulikuwa ni ndege mzuri na uliozima ulikuwa ni ndege mbaya kisirani. Ilipotokea moto wa mbele ya hema kuzimika, wenye hema huku wakikichukulia kuwa ni kisirani, basi ilikuwa wao kujiondoa vitani siku ile, na kujiunga tena baadaye. Viongozi wa wapagani tayari walikuwa wameingiwa na shuku. Wakati baadhi ya wapigakambi walipofunga virago vyao, wenzao wengine walifikiria kwamba Waislamu walikuwa wamefanya shambulio la usiku. Fikara ikazagaa. Wote wakaanza kufunga virago na kuondoka kwenye uwanja wa vita. Abu Sufyan yuasemekana kwamba alikuwa usingizini hemani mwake. Zikamfikia habari za kutimka kwa ghafla kwa vikosi vya wapagani. Akaamka kwa hamaki, na katika hali ya mahangaiko, akapanda ngamia aliyekazwa ukambaa. Akamchochea yule mnyama, lakini mnyama hakuweza kwenda. Marafiki zake wakamtanabahisha, wakamfungua ngamia, na Abu Sufyan na kundi lake wakaweza kuutoka uwanja wa vita.

Theluthi tatu za usiku zilikuwa zimepita. Uwanja wa vita tayari ulikwa mweupe kabisa. Jeshi lenye baina ya elfu ishirini na ishirini na tano za askari na wafuasi lilitoweka, likiacha nyuma mbuga tupu. Wakati ule ule Mtume[saw] akapokea wahyi ya kwamba lile jeshi limetimka kama matokeo ya kudura ya Mwenyezi Mungu. Ili kupata kujua kilichokuwa kimefanyika, Mtume[saw] alitaka kumtuma mfuasi wake mmoja kwenda kuchungua uwanja wa vita na aje kuleta ripoti. Kulikuwa na baridi kali. Haishangazi ya kwamba Waislamu waliokuwa hawakujisitiri vizuri walikuwa wakitetemeka kwa baridi. Baadhi yao walisikia sauti ya Mtume[saw]. Wakataka kuitikia, lakini hawakuweza. Kulikuwa na baridi kupita kiasi. Ilikuwa ni Hadhrat Hudhaifa[ra] pekee aliyeweza kuitikia kwa sauti kubwa akisema, "Labeka, Ewe Mtume wa Mungu, watuamrisha tufanye kitu gani?"

Mtume[saw] akaita tena. Na kwa mara ya tena hapana aliyeweza kuitika kwa jinsi baridi ilivyokuwa kali. Ni Hadhrat Hudhaifa[ra] peke yake aliyeweza kuitikia tena. Mtume[saw] akamwambia Hadhrat Hudhaifa[ra], 'uende ukausaili uwanja wa vita kwani Mwenyezi Mungu Amenijulisha ya kuwa maadaui wamekimbia.' Hadhrat Hudhaifa[ra] akaenda karibu na handaki na kutoka sehemu ile akaona kwamba maadui walikuwa wameutoroka uwanja wa vita. Hawakuwepo askari wala wafuasi. Hadhrat Hudhaifa[ra] akarudi kwa Mtume[saw], akapiga Shahada na akaripoti kwamba maadui walikuwa wamekimbia. Keshoye Waislamu nao wakavunja kambi na kuanza kufunga safari ya kurudi mjini. Mtihani mgumu ulioendelea kwa takriban siku ishirini ulikuwa umemalizika.

KABILA LA BANU QURAIDHA LAADHIBIWA

Waislamu wakaweza kurudia tena hali ya amani. Lakini bado walikuwa na hili kabila la Banu Quraidha la kuoneshwa cha mtema kuni. Hili kabila la Banu Quraidha lilikuwa limehalifu mkataba wao na Waislamu na uhalifu huu, na hii isingeliweza kusameheka. Mtume[saw] akakusanya wanajeshi wake wachovu na kuwaambia kwamba bado hapakuwa na mapumziko. Kabla jua halijatua, ni sharti wakawapige vita watu wa kabila la Banu Quraidha kwao ngomeni. Kisha alimtuma Hadhrat Ali[ra] kwa kabila hili la Banu Quraidha kwenda kutaka kujua ni kwa nini walivunja mapatano. Kabila hili halikuonesha moyo wa kujutia kitendo chao wala kusema kunradhi. Badala yake, wao wakamtusi Hadhrat 'Ali[ra] na wajumbe wengine wa Waislamu na kuanza kuwatupia matusi machafu Mtume[saw] na akina mama wa familia yake. Wakasema eti hawakumjali Muhammad wala hawakuwa wamefanya naye mkataba wowote. Hadhrat 'Ali[ra] aliporudi kuliripoti jawabu la Mayahudi, akamkuta Mtume[saw] na Masahaba wakielekea kwenye ile ngome ya Mayahudi. Mayahudi walikuwa wakimtusi Mtume[saw], wakeze na mabintize. Hadhrat 'Ali[ra] akihofia kwamba jambo hili lingemuudhi sana Mtume[saw], akashauri kwamba hapakuwepo na haja ya Mtume[saw] kuwepo ndani ya vita hivi kwani Waislamu wenyewe wangeweza kuwakomolea mbali

Mayahudi. Mtume[saw] akamwelewa Hadhrat Ali[ra] na akatamka akisema, "Mimi hunitaki nisikie matusi yao, sivyo? Hadhrat Ali[ra] akasema "Naam". Mtume[saw] akauliza, "Lakini kulikoni, Ewe Ali?" Musa alikuwa ni jamaa yao hasa. Hata hivyo wao walimuudhi kuliko vile ambavyo wamenifanya mimi". Mtume[saw] alizidi kusonga mbele. Mayahudi wakajizatiti na kuanza kupigana. Wanawake wao nao pia wakajumuika nao. Baadhi ya Waislamu walikuwa wakiketi chini ya ukuta. Kuona hivyo, mwanamke mmoja wa Kiyahudi akawadondoshea jiwe, na kumuua mmoja wao, aitwaye Khallad. Ngome ya Mayahudi ikaendelea kuzingirwa kwa siku kadha. Mwishowe Mayahudi wakaona mambo yamewachachia. Ndipo machifu wao wakampelekea Mtume[saw] ujumbe wakimwomba awapelekee Hadhrat Abu Lubaba[ra], Mwislamu Ansari aliyekuwa chifu wa kabila la Aus, lililokuwa na urafiki na Mayahudi. Haja yao ilikuwa ni kumtaka ushauri juu ya kupatikana suluhisho. Mtume[saw] akawapelekea Hadhrat Lubaba[ra] waliyemwuliza kama ilikuwa vyema wao kuangusha silaha zao na kukubali toleo la Mtume[saw]. Hadhrat Lubaba[ra] akawaambia wafanye hivyo. Lakini wakati huohuo yeye akazungusha kidole chake shingoni akionesha ishara ya kifo. Mtume[saw] hakuwa amemwambia yeyote lolote juu ya jambo hili. Lakini Hadhrat Abu Lubaba[ra], akihofia huenda ule uhalifu wa Mayahudi ulistahili kifo, yeye bila kujua akafanya ishara hii, iliyotokea kuwa ndege mbaya kwa Mayahudi. Ikatokea wao kutoukubali ushauri wa Abu Lubaba[ra] na kukatalia mbali toleo la Mtume[saw]. Kama wangelilikubali toleo la Mtume[saw], basi adhabu ya mwisho ingelikuwa wao kutimuliwa toka Madina. Lakini kama ilivyo mkosa bahati kutobahatika, wao walilikataa toleo la Mtume[saw]. Wakasema kwamba badala ya Mtume[saw], wao watakubali uamuzi wa Sa'd bin Mu'adh, chifu wa kabila rafiki yao la Aus. Watakubali adhabu yoyote atakayoipendekeza. Pia ulizuka ubishi miongoni mwa Mayahudi. Baadhi yao walianza kudai kwamba kwa kweli watu wao walikuwa wamehalifu mkataba wao na Waislamu. Kile walichofanya Waislamu kwa upande mwingine, kilionesha kwamba wao walikuwa waaminifu

na wakweli na kwamba dini yao ni ya kweli. Wale waliofikiria hivi wakasilimu. Mmoja wa machifu wa Kiyahudi, aitwaye Amr bin Sa'di, akawalaumu watu wake akiwaambia, "Mmefanya kosa la kutangua maelewano na kuvunja ahadi yenu. Njia ya pekee mliyonayo sasa hivi ni nyinyi kusilimu ama mtoe jizya".

Wakasema, "Sisi hatutasilimu wala kutoa *jizya*, kwani kufa ni bora kuliko kulipa *jizya*". 'Amr akajibu akisema kwamba kama ni hivyo, basi yeye hakuwa hatiani, na kwa maneno haya yeye akaihama ngome. Akatokea kuonekana na Hadhrat Muhammad bin Maslama[ra], kamanda wa kikosi cha Waislamu, aliyetaka kujua yeye alikuwa nani. Baada ya kujua alikuwa nani, Hadhrat Muhammad bin Maslama[ra] akamwachilia ajiendee zake kwa amani, na yeye mwenyewe (Hadhrat Muhammad bin Maslama[ra]), akapaaza sauti akiomba:

> "Mwenyezi Mungu, siku zote nijaalie uwezo wa kusitiri makosa ya wanyofu".

Alichomaanisha ni kwamba Myahudi huyu alikuwa ameyajutia na kuyasikitikia makosa ya watu wake. Ilikuwa, hivyo basi, faradhi kwa Waislamu kusamehe watu sampuli hii. Katika kumwachilia aende zake, yeye alikuwa amefanya kitu cha maana, na aliomba ya kwamba Mwenyezi Mungu amjazi fursa ya kufanya matendo mema kama hayo mara kwa mara. Mtume[saw] alipojua kile Hadhrat Muhammad bin Maslama[ra] alichokuwa amekifanya, hakumkaripia kwa kumwachilia kiongozi huyu wa Mayahudi aponyoke. Bali aliridhia vile mambo yalivyokwenda.

Nia ya kutaka amani na kukubali uamuzi wa Mtume[saw] ilikuwa imeoneshwa tu na Myahudi mmoja mmoja. Lakini wao kama taifa, walizidi kudinda na kukatalia mbali uamuzi wa Mtume[saw] na kutaka, badala yake, uamuzi wa Sa'd bin Mu'adh (Bukhari, Tabari na Khamis). Mtume[saw] akayakubali matakwa yao na kumpelekea habari Sa'd, aliyekuwa majeruhi akijinyosha, akimtaka aje atoe uamuzi juu ya kuvunja mapatano kwa Mayahudi. Mara tu rai ya Mtume[saw] ilipotangazwa, watu wa kabila la Aus waliokuwa marafiki wa Banu

Quraidha kwa muda mrefu walimkimbilia Sa‘d na kuanza kumhimiza atoe uamuzi wake akiwapendelea Banu Quraidha. Wakizidi kumhimiza walisema kwamba watu wa kabila la Khazraj walikuwa daima wamejaribu kuwanusuru Mayahudi waliokuwa na urafiki nao. Basi ilikuwa ni juu ya Sa‘d kuwanusuru Mayahudi walio marafiki wa kabila lake. Sa‘d akawaendea watu wa Kabila la Banu Quraidha. Watu wa kabila lake wakamfuatilia huku na huku wakimtaka asiwaadhibu watu wa Banu Quraidha. Katika kuwajibu Sa‘d aliwaambia tu kwamba mtu iliyembidi kutoa uamuzi, huwa anao wajibu. Hakuwa na budi kutekeleza wajibu kwa unyofu”. Hivyo basi, mimi nitatoa uamuzi wangu, huku nikitilia maanani kila kitu, na bila ya woga wala mapendeleo”. Sa‘d alipofika kwenye ngome ya Banu Quraidha, akawakuta watu wa Banu Quraidha wamejipanga mlolongo kuegemea. ukuta wa ngome yao, huku wakimsubiri yeye. Upande mwingine walikuwepo Waislamu. Sa‘d alipowakaribia akawauliza, “Je, mtakubali uamuzi wangu?” Wakasema, “Naam”.

UAMUZI WA SA‘D[RA] WAAFIKIANA NA BIBLIA

Sa‘d[ra] akawageukia Banu Quraidha na kuwauliza swali lile lile, nao pia wakakubali. Kisha kwa adabu akageukia upande alikokuweko Mtume[saw] na akauliza ikiwa nao pia watafuata uamuzi wake. Kusikia hivyo, Mtume[saw] akajibu akisema, “Naam” (Tabari na Hisham). Hapo Sa‘d[ra] akatoa uamuzi wake kulingana na hii amri ya Biblia inayofuata:

> Utakaposogea karibu na mji kwenda kupigana juu yake, ndipo utakapowapigia ukelele wa amani. Itakuwa utakapokujibu kwa amani, na kukufungulia, ndipo watu wote watakaoonekana humo watakufanyia kazi ya shokoa, na kukutumikia. Na kwamba kama hautaki kufanya amani nawe, lakini utafanya vita juu yako, ndipo uuhusuru; na Bwana, Mungu wako, autiapo mkononi mwako, mpige kila mume aliyemo kwa makali ya upanga; lakini wanawake na watoto, na wanyama wa miji, na vilivyo mjini vyote, navyo ni nyara zake zote, uvitwae viwe mateka kwako; nawe utakula nyara za adui zako alizokupa

> Bwana, Mungu wako. Utaifanyia vivyo miji yote iliyo mbali sana nawe, isiyokuwa miji ya mataifa haya. Lakini katika miji ya mataifa haya akupayo Bwana, Mungu wako, kuwa urithi, usihifadhi kuwa hai kitu cho chote kipumzikacho; lakini uwaangamize kabisa, Mhiti na Mwamori, na Mkanaani, na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi, kama alivyokuamuru Bwana, Mungu wako; wasije wakawafunza kufanya mfano wa machukizo yao yote waliyoifanyia miungu yao; hivyo itakuwa ni makosa juu ya Bwana, Mungu wako (Kum. 20:10-18).

Kulingana na mafundisho ya Biblia, kama Mayahudi wangeshinda na Mtume[saw] kushindwa, basi Waislamu wote — wanaume kwa wanawake na watoto — wangeuliwa mbali. Twajua historiani kwamba hili hasa ndilo lililokuwa ni lengo la Mayahudi. Cha mwisho Mayahudi wangelichoweza kufanya ilikuwa ni kuwaulia mbali wanaume, kuwatia utumwani wanawake na watoto na kupora mali za Waislamu, hii ikiwa ndiyo amri inayofaradhishwa ndani ya Kumbukumbu la Torati dhidi ya mataifa adui yanayoishi katika sehemu za mbali za dunia. Sa'd[ra] alikuwa rahimu kwa watu wa Banu Quraidha. Kabila lake lilikuwa na maelewano na kabila lao. Alipoona kwamba Mayahudi walikuwa wamekataa kukubali uamuzi wa Mtume[saw] na hivyo basi kukataa adhabu nafuu inayopendekezwa katika Islam kwa kosa kama hilo, aliamua kuwapatia Mayahudi ile adhabu ambayo Nabii Musa[as] alikuwa ameiweka. Jukumu la uamuzi huu halimo mikononi mwa Mtume[saw] au mikononi mwa Waislamu, bali li mikononi mwa Nabii Musa[as] na mafundisho yake na Mayahudi waliokuwa wamewatendea Waislamu kikatili jinsi ile. Walikuwa wamependekezewa ule ungeliokuwa uamuzi wa huruma. Lakini badala ya kuubali huu, wao wakang'ang'ania kutolewa uamuzi na Sa'd[ra]. Sa'd[ra] akaamua kuwaadhibu Mayahudi kulingana na Sheria ya Nabii Musa[as]. Lakini Wakristo hadi wa leo wanaendelea kumlaumu Mtume wa Islam[saw] na wanadai yeye alikuwa mkatili kwa Mayahudi. Kama Mtume[saw] alikuwa mkatili kwa Mayahudi, basi ni kwa nini hakuwa mkatili kwa watu wengine katika visa vingine? Kulikuweko

na visa vingi ambapo maadui wa Mtume[saw] walijitupa mikononi mwake, na haikutokea kabisa wao kuomba msamaha wakanyimwa. Katika kisa hiki maadui walimkazania mtu minghairi ya Mtume[saw] kutoa uamauzi. Mchaguliwa huyu wa Mayahudi, akiwa yu mwamuzi baina yao na Waislamu, hadhrani alimwuliza Mtume[saw] na Mayahudi ikiwa wao watakubali uamuzi wake. Ilikuwa ni baada ya pande zote mbili kuwa zimeridhika, ndipo yeye alipoutangaza. Na uamuzi wenyewe ulikuwa ni kitu gani? Haukuwa chochote ila utumiaji wa Sheria ya Nabii Musa[as] kwenye kosa la Mayahudi. Basi ingelikuwaje wao kuukatalia mbali? Je, wao hawakujihesabu miongoni mwa wafuasi wa Nabii Musa[as]? Kama palitumiwa ukatili, basi huo ulitumiwa na Mayahudi juu ya Mayahudi. Myahudi walikatalia mbali kuridhia uamuzi wa Mtume[saw] na wakataka badala yake itumike sheria yao ya kidini kwenye hili kosa lao. Basi ukatili kama ulitumiwa, huo ulitumiwa na Nabii Musa[as] aliyeiweka adhabu hii juu ya adui mzingirwa na kuitia kitabuni mwake kwa amri ya Mungu. Waandishi wa Kikristo na wasimvurumishie moto wa hasira zao Mtume[saw] wa Islam. Na wamlaumu Nabii Musa[as] aliyeweka adhabu hii ya kikatili au Mungu wa Nabii Musa[as] aliyemwamuru kufanya hivyo.

Vita vya Handaki vikiwa vimemalizika, Mtume[saw] akatangaza kwamba tokea siku ile kwenda mbele, wapagani kamwe hawatawashambulia Waislamu; sasa badala yake, Waislamu watawashambulia wapagani. Mambo yatageuka. Waislamu watayachukulia hatua yale makabila na makundi ambayo hadi kufikia pale yalikuwa bila sababu yoyote yakiwashambulia. Aliyoyasema Mtume[saw] havikuwa vitisho vitupu. Katika vita vya Handaki ule mwungano wa majeshi ya Waarabu haukuwa umepata kipigo chochote cha maana. Walikuwa wamewapoteza watu wachache tu. Katika muda wa chini ya mwaka mmoja wao wangeliweza kurudi na kuushambulia tena mji wa Madina wakiwa wamefanya maandalizi bora zaidi. Badala ya jeshi la askari elfu ishirini wao wangeliweza kukusanya jeshi la askari elfu arubaini hata hamsini kwa ajili ya hili shambulio jipya. Jeshi la idadi ya askari laki moja au laki moja na elfu hamsini lisingekuwa vigumu

kwao kuweza kulikusanya. Lakini sasa kwa muda wa miaka ishirini na mmoja, maadui wa Islam walikuwa wamefanya chini juu kuangamiza Islam na Waislamu. Kuendelea kutofaulu kwa plani zao kulikuwa kumewababaisha. Walikuwa wameanza kuhofia kwamba yale aliyoyafundisha Mtume[saw] yalikuwa ni kweli, na kwamba miungu yao ya kitaifa ilikuwa ni bandia, kwamba Muumbaji alikuwa ni Yule Mungu Mmoja Asiyeonekana aliyemfundisha Mtume[saw]. Hofu ya kwamba Mtume[saw] alikuwa kwenye haki na wao kwenye batili ilikuwa imeanza kuwapenya. Lakini hapakuwepo na ishara yoyote ya kidhahiri ya hofu hii. Kwa kuonekana, makafiri waliendesha shughuli zao kama walivyokuwa wakifanya siku zote. Waliyaendea masanamu yao na kuyaomba sawa na desturi zao. Lakini walikuwa wamevunjika moyo. Kidhahiri waliishi maisha ya wapagani na makafiri ; lakini kwa ndani nyoyo zao zilikuwa kana kwamba zinapeperusha ule wito wa Waislamu zikisema, "Hapana Mungu ila Allah".

Baada ya Vita vya Handaki, kama vile tulivyotangulia kusema, Mtume[saw] alitangaza kwamba tangu sasa makafiri katu hawatawashambulia Waislamu bali badala yake Waislamu watawashambulia makafiri. Uvumilivu wa Waislamu ulikuwa umefikia kikomo chake. Sasa mambo yatabadilika, (Bukhari, Kitabul Maghazi).

JE, MTUME[SAW] ALINUIA KUENDELEZA VITA?

Katika vile vita ambavyo kufikia pale vilikuwa vimepiganwa, Waislamu walikuwa ama wamebakia mjini Madina au kwenda nje kidogo ya mji kupambana na uchokozi wa makafiri. Waislamu hawakuanzisha mapambano haya, na hawakuonesha nia ya kuyaendeleza baada ya kuanzishwa. Kwa kawaida uadui mara uanzwapo, unaweza ukasitishwa kwa njia mblili tu — mkataba wa amani au upande mmoja kusalimu amri ya mwingine. Katika mapigano baina ya Waislamu na makafiri hadi kufikia pale haikutokea kuwepo na tetesi ya amani wala upande mmoja kupata kusalimu amri ya mwingine. Naam, kulikuwepo na kunyamaa kwa vita, lakini hapana aliyeweza kusema kwamba vita baina ya Waislamu

na makafiri vilikuwa vimekwisha. Sawa na kanuni za kawaida, Waislamu wangeliweza kuyashambulia makabila adui na kuwalazimisha kusalimu amri. Lakini Waislamu hawakufanya hivi. Maadui walipoacha kupigana, Waislamu nao waliacha. Waliacha kupigana kwa sababu wao waliamini huenda pakawa na mazungumzo ya amani. Lakini ilipodhihirika kwamba mazungumzo ya amani na makafiri hayakuwepo, wala kuwepo na nia ya makafiri kusalimu amri, Mtume[saw] akaona kwamba wakati ulikuwa umewadia wa kumaliza vita ama kwa mapatano ya amani au kwa njia ya upande mmoja kusalimu amri ya upande mwingine. Vita havikuwa na budi kumalizika kama palitakiwa pawepo na amani. Hivyo, baada ya Vita vya Handaki ilionekana kuwa Mtume[saw] aliamua kupata mojawapo la haya mawili; amani au kusalimu amri. Na kwa Wailsmu kusalimu amri ya makafiri ilikuwa haiwezekani kabisa. Ushindi wa Islam dhidi ya watesaji wake ulikuwa umeahidiwa na Mwenyezi Mungu. Matangazo yenye kumaanisha hivyo yalikuwa yametolewa na Mtume[saw] katika maisha yake ya Makka. Harakati za amani zinaweza zikaanzishwa ama na wenye nguvu au na upande wa wanyonge. Wakati upande wa wanyonge unapotafuta amani hauna budi kusalimisha, kwa muda au daima dawamu, sehemu ya himaya yake au sehemu ya mapato yake; au haina budi kwa wanyonge kukubali masharti mengine wanayolundikiwa na maadui. Inapokuwa upande wenye nguvu kupendekeza amani hufahamika kwamba haunuii maangamizo ya kabisa kabisa ya upande mnyonge lakini uko tayari kuuruhusu ubakie na uhuru kamili au nusunusu ukifaidia masharti fulani fulani. Kwenye vile vita vilivyokuwa vimepiganwa baina ya Waislamu na makafiri ilikuwa imetokea makafiri kuonjeshwa ushinde baada ya ushinde. Lakini hata hivyo nguvu yao haikuwa imevunjiliwa mbali. Walikuwa wameshindwa tu katika jitihada zao za kuwaangamiza Waislamu. Kushindwa kumwangamiza mwingine hakumaanishi ushinde. Kwamaanisha jambo hili moja tu ya kwamba chokochoko bado hazijafaulu, mashambulio ambayo hayakufaulu yanaweza yakarejelewa. Hivyo basi, watu wa Makka hawakuwa

wameshindwa; ila tu chokochoko zao dhidi ya Waislamu hazikuwa zimefua dafu. Katika uwanja wa kijeshi, bila shaka Waislamu ndio waliokuwa upande mnyonge. Naam, ulinzi wao ulikuwa bado wasimama chonjo, lakini wao ndio waliokuwa wachache zaidi na wachache ambao, ingawaje walikuwa wameweza kukabiliana na chokochoko za walio wengi, hawakuwa wameweza kuanzisha mapigano. Kwa hiyo, Waislamu walikuwa bado kusimika uhuru wao. Kama wangelikuwa wamependekeza amani, ingelimaanisha kwamba ulinzi wao umevunjika, na kwamba wao sasa walikuwa tayari kukubaliana na masharti ya makafiri. Ingetokea wao kunyosha mkono wa amani hilo lingelikuwa na madhara makubwa kwa Islam. Lingelimaanisha kujiangamiza. Lingempatia maisha mapya adui aliyevunjwa moyo na ushinde wa mara kwa mara. Hisia za ushinde zinazozidi kuongezeka sasa zingelitoa nafasi kwa tumaini jipya na tamaa. Makafiri wangelifikiria kwamba ingawaje Waislamu walikuwa wameinusuru Madina kumbe wao bado walikuwa wakiutilia shaka ushindi wao dhidi ya makafiri. Kwa hiyo, pendekezo la amani lisingeweza kutokana na upande wa Waislamu. Lingetokana na upande wa Makka, au upande wa tatu, ingetokea kupatikana upande wa tatu. Lakini upande wa tatu haukuweza kupatikana. Katika patashika iliyokuwa imezuka Madina ilikuwa imepiganishwa dhidi ya Arabuni nzima. Hivyo basi, ilikuwa ni makafiri waliostahili kutafuta amani, na hapakuwa na ishara ya jambo hili. Ndio maana vita baina ya Waislamu na Waarabu huenda vingeliendelea milele na milele. Waislamu wasingeliweza, na Waarabu hawakuweza kupendekeza amani. Hivyo basi, ghasia za raia nchini Arabuni hazikuonekana kuwa na mwisho, pengine hata kwa miaka mingine mia moja.

Palikuwa na njia moja tu iliyokuwa wazi kwa Waislamu ikiwa wao walitaka kumalizia mbali mizozo hii. Wao hawakuwa tayari kusalimisha dhamira yao kwa Waarabu, yaani kutangua haki yao ya kutangaza, kufuata na kuhubiri walichotaka; na hapakuwepo na harakati za kutaka amani kutoka upande wa makafiri. Waislamu walikuwa wameweza kupambana na chokochoko za tena na tena.

Hivyo basi, ilikuwa ni juu yao kuwalazimisha Waarabu kusalimu amri au kutaka amani. Mtume[saw] aliamua kufanya hivyo.

Je, ilikuwa ni vita alivyotaka Mtume[saw]? La hasha, haikuwa vita bali ni amani aliyotaka kuleta. Kama asingelifanya chochote wakati huu, basi nchi ya Arabuni ingelibakia kwenye mapigano ya raia zake. Hatua alizochukua zilikuwa ni njia ya pekee kuleta amani. Vimekuwepo vita vya muda mrefu historiani. Vita vingine viliendelea kwa muda wa miaka mia moja na vingine miaka thalathini au takriban muda kama huo. Vita vya muda mrefu daima vimetokana na pande zinazohusika kutotenda kitendo chenye kuzima vita. Kitendo cha kuzima vita, kama vile tulivyosema, kinaweza kikawa cha aina mojawapo tu ya hizi mbili — kusalimu amri kabisa au mapatano ya amani.

Je, Mtume[saw] angeweza kutojali? Je, angeweza kwenda yeye na jeshi lake dogo la Waislamu kujikalia nyuma ya ukuta wa Madina na kuacha kila kitu kijiendeshe chenyewe? Hii haikuwezekana. Makafiri ndio waliokuwa wameanzisha chokochoko. Kutojali kusingelimaanisha mwisho wa vita, bali kuendelea kwake, kwa hakika. Ingelimaanisha kwamba makafiri wangeweza kuwashambulia Waislamu wakati wowote waliotaka. Wangeliweza kushambulia walipotaka na kuacha walipotaka. Vita kutulia haikumaanisha mwisho wa vita. Ilimaanisha kuwa mbinu tu ya kimaarifa.

MAFUNDISHO YA KIYAHUDI NA YA KIKRISTO JUU YA VITA

Lakini sasa swali hili linazuka — Je, kweli inaweza ikasihi kuipigania dini? Basi hebu na tuligeukie swali hili. Mafundisho ya dini juu ya suala zima la vita yanakuwa na sura mbalimbali. Mafundisho ya Agano la Kale, tumeyakariri hapo juu. Nabii Musa[as] yuaamriwa aiingie nchi ya Kanaani kwa mabavu, kuwashinda wakazi wake na kuwakalisha watu wake yeye mwenyewe (Kum. 20:10-18). Licha ya mafundisho haya katika kitabu cha Nabii Musa[as], na licha ya kutiliwa shime kwake kwa mfano wa vitendo wa Manabii Yoshua, Daudi na wengine, Mayahudi na Wakristo huzidi kuwaheshimu na kuvichukulia vitabu vyao kuwa ni vitabu vya Mungu.

Mwishoni mwa hayo mafundisho ya Musa, tulikuwa naye Yesu aliyefundisha akisema:

> Lakini mimi nawaambia, msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili (Mt. 5:39).

Wakristo mara nyingi wameyataja mafundisho haya na kudai kwamba Yesu alipinga vita. Lakini ndani ya Agano Jipya tunayo mistari inayoonekana yafundisha kinyume kabisa na hivyo. Kwa mfano, sehemu moja yasema hivi:

> Msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; la! sikuja kuleta amani bali upanga (Mt.10: 34).

Na nyingine yasema:

> Akawaambia, lakini sasa mwenye mfuko na auchukue, na mkoba vivyo hivyo; naye asiye na upanga, na auze joho lake akanunue (Lk. 22:36).

Katika hiyo mistari mitatu ile miwili ya mwisho yaupinga wa kwanza. Kama Yesu alikuja kwa ajili ya vita, basi ni kwa nini yeye akafundisha watu wageuze shavu la pili? Yaonekana hapa hatuna budi ama tukubali hitilafu katika Agano Jipya, au tulielezee kwa njia inayofaa mojawapo ya mafundisho yanayohitilafiana. Sisi hapa hatumo katika swali la kama kweli inawezekana kugeuza shavu la pili au la. Tumo tu katika kusema kwamba ndani ya muda mzima wa historia yao ndefu hapana taifa la Kikristo ambalo limewahi hata mara moja kukawia kuanzisha vita. Wakristo walipopata nguvu kwa mara ya kwanza huko Roma, walishiriki katika vita vya kujihami na vya kiuchokozi. Leo hii wao ndio nguvu kubwa duniani, na wanazidi kushiriki katika vita vya kujihami na vile vya kiuchokozi. Ila tu hivi leo ule upande unaoshinda hutakatishwa na Wakristo wengine duniani. Ushindi wao husemekana kuwa ni ushindi wa ustaarabu wa Kikristo. Ustaarabu wa Kikristo umekuja kutokea kumaanisha chochote kile kinachoelekea kuwa na nguvu na ufaulu. Zinapopigana madola mawili ya Kikristo, kila moja hudai kuwa ndiyo mtunzaji wa maadili ya Kikristo. Dola

lenye kushinda hutakatishwa kuwa eti ndiyo hasa nguvu ya Kikristo. Lakini ni kweli kwamba tangu zama za Yesu hadi hizi zama zetu, ulimwengu wa Kikristo umehusikana na vita — na ishara zaonyesha kwamba utazidi kuhusikana na vita. Hukumu ya kidhahiri ya mataifa ya Kikristo, hivyo basi, ni kwamba vita ndiyo mafundisho halisi ya Agano Jipya, na kwamba kugeuza shavu la pili yalikuwa ni mafundisho yaliyofaa zama zake yaliyotolewa na hali ya kinyonge ya Wakristo wa hapo awali, au ni mafundisho kwa ajili ya Wakristo mmoja mmoja tu, sio kwa ajili ya nchi wala mataifa ya Kikristo.

Pili, hata tukimfanya Yesu kwamba alifundisha amani na sio vita, haiwi kwa sababu hiyo kwamba wasiolitekeleza agizo hili si watakatifu au waheshimiwa. Kwani ulimwengu wa Kikristo siku zote umeheshimu mashabiki wa vita kama vile Musa, Yoshua na Daudi. Si hayo tu, Kanisa lenyewe limewatakatifisha mashujaa wa kitaifa waliofia vitani. Walifanywa watakatifu na Mapapa.

MAFUNDISHO YA KURANI JUU YA VITA NA AMANI

Mafundisho ya Islam ni tofauti na mafundisho haya yote mawili. Yanaweka wastani baina ya hayo mawili. Islam haifundishi mabavu alivyofanya Musa[as]. Wala haihubiri mahitilafiano kama vile ufanyavyo Ukristo (yamkini uliochafuliwa) wa hivi leo. Haututaki tugeuze shavu la pili na papo hapo kuuza nguo zetu tukanunue upanga. Mafundisho ya Islam yanalingana na tabia za kimaumbile za mwanadamu, na kujenga amani kwa njia ya pekee inayowezekana.

Islamu yakataza uchokozi, lakini yatutaka tupigane endapo kutopigana kutahatarisha amani na kuchoehea vita. Ikiwa kutopigana kwamaanisha kukomeshwa kwa uhuru wa dini na uhuru wa kutafuta ukweli, basi ni wajibu wetu kupigana. Haya ndiyo mafundisho ambayo juu yake amani hatimaye inaweza ikajengwa, na haya ndiyo mafundisho ambayo juu yake Mtume[saw] aliweka kanuni zake na matendo yake. Mtume[saw] aliendelea kuteseka tena bila kikomo huko Makka lakini yeye kamwe hakupambana na dhuluma alizokuwa windo lake lisilokuwa na makosa. Alipoponyokea Madina, maadui

wakanuia kuiangamiza Islam; hivyo basi, ilikuwa ni lazima kuwapiga vita maadui katika kutetea ukweli na uhuru wa dini.

Twakariri hapa chini aya za Kurani zinazohusikana na suala la vita.

(i) Katika Sura Al-Hajj 22:40-42, tunayo maagizo haya:

> Imeruhusiwa (kupigana) kwa wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa; na kwa yakini Allah anao uwezo wa kuwasaidia — waliotolewa majumbani mwao pasipo haki ila tu kwa sababu wanasema: Mola wetu ni Allah. Na kama Allah asingeliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangelivunjwa mahekalu na makanisa, na nyumba za ibada na misikiti ambamo jina la Allah hutajwa kwa wingi, na bila shaka Allah humsaidia yule anayemsaidia Yeye. Hakika Allah ni Mwenye nguvu, Mshindi — Wale ambao tukiwaimarisha katika ardhi watasimamisha Sala na watatoa Zaka na wataamrisha yaliyo mema na watazuia yaliyo mabaya. Na kwa Allah ndiko mwisho wa mambo yote.

Aya zenyewe zina maana ya kusema kwamba ruhusa ya kupigana imepewa wale wanaodhulumiwa bure. Mwenyezi Mungu aweza kabisa kuwasaidia wadhulumiwa — wale ambao wametolewa majumbani mwao kwa sababu ya imani zao. Ruhusa hii ni yenye hekima kwa sababu, Mwenyezi Mungu asingeliwazuia makatili kwa msaada wa watawa, basi kusingekuwepo na uhuru wa dini na ibada duniani. Hapana budi Mwenyezi Mungu kuwasaidia wanaosaidia kuleta uhuru na ibada. Basi kwa sababu hiyo mapigano yanaruhusiwa inapokuwa watu kutaabika kwa muda mrefu kwa dhuluma za bure — ambapo mdhalimu mwenyewe hakuwa amepata udhuru wa kudhulumu na yuatafuta kuingilia dini ya mdhulumiwa wake. Wajibu wa mdhulumiwa, ikiwa anao uwezo na atakapotokea kuwa na uwezo, ni kuleta uhuru wa dini na kulinda dini zote na mahali pote pa ibada. Uwezo wake usiwe utatumiwa kujifaharisha yeye mwenyewe, bali utumiwe kuwahudumia maskini, maendaleo ya nchi na uimarishaji wa amani kwa jumla. Mafundisho haya ni safi kabisa kama yalivyo

wazi halisi. Aya yatangaza kwamba Waislamu wa hapo awali walipigana vita kwa sababu walilazimika kufanya hivyo. Vita vya kichokozi vilikatazwa na Islam. Waislamu wanaahidiwa uwezo wa kisiasa, lakini wanaonywa kwamba uwezo huu usiwe utatumiwa kujitakia makuu, bali utumiwe kwenye ustawishaji wa maskini na uimarishaji wa amani na maendeleo kwa jumla.

(2) Katika Sura Al-Baqara 2: 191-194, tunayo maagizo haya:

> Na piganeni katika njia ya Allah na wale wanaowapigeni, wala msiruke mipaka. Kwa hakika Allah hawapendi warukao mipaka. Na waueni popote mwakutapo, na kuwatoa popote walipowatoeni; kwani mateso ni mabaya zaidi kuliko kuua. Wala msipigane nao karibu na Msikiti Mtakatifu mpaka wawapigeni humo. Na wakiwapigeni, basi nanyi wapigeni; hayo ndiyo malipo kwa makafiri. Lakini kama wakiacha, basi hakika Allah ni Msamehevu, Mrehemevu. Na wapigeni mpaka yasiwepo mateso, na dini iwe kwa ajili ya Allah tu; na kama wakiacha, basi usiweko uadui ila kwa wadhalimu.

Mapigano na yawe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, sio kwa ajili yetu sisi wenyewe au kusababishwa na hasira tu au kujitakia makuu, na hata mapigano nayo pia ni sharti yasiwe na urukaji wa mipaka, kwani urukaji mipaka humkasirisha Mwenyezi Mungu. Mapigano ni baina ya makundi ya wapiganaji wanaopigana. Kuwashambulia watu mmoja mmoja kumekatazwa. Mateso dhidi ya dini ni sharti yakabiliwe na upinzani mkali, kwani mateso kama hayo ni mabaya zaidi ya kuua. Waislamu wasipigane karibu na Msikiti Mtakatifu, isipokuwa shambulio kwanza lifanywe na maadui. Mapigano ya karibu na Msikiti Mtakatifu huingilia uhuru wa watu wa kuhiji. Lakini kama maadui wakishambulia, basi Waislamu wako huru kujibu mashamblio hayo; haya yakiwa ndiyo malipo yaliyohakiki juu ya uchokozi. Lakini kama maadui wakiacha, basi Waislamu nao ni sharti waache mapigano, na kusamehe na kusahau yaliyopita. Mapigano na yaendelee mradi dhuluma za kidini zinaendelea na uhuru wa dini haupatikani. Dini ni

kwa ajili na Mwenyezi Mungu. Utumiaji wa mabavu au ulazimishaji katika dini ni makosa. Kama makafiri wakiacha vita na dini kuiachiliwa huru, basi Waislamu na waache kuwapiga vita makafiri. Silaha na washikiwe wale wenye kuruka mipaka. Urukaji mipaka ukomapo, basi mapigano nayo pia na yakome.

Kinagaubaga, tunaweza tukasema, aya zenyewe zinafundisha hizi kanuni zifuatazo:

(i) Vita vipiganwe kwa ajili ya Mwenyezi Mung wala si kwa ajili ya nia yoyote ya kujitakia makuu, si kwa ajili ya kujitafutia masilahi mengineyo.

(ii) Tunaweza tu kupigana vita dhidi ya yule atanguliaye kutushambulia.

(iii) Twaweza kuwapiga vita wale tu wanaotupiga vita. Hatuwezi kupigana vita dhidi ya wale wasiokuwemo vitani.

(iv) Hata baada ya maadui kuanzisha vita, ni faradhi kwetu sisi kuviweka vita ndani ya mipaka yake. Kupanua vita, iwe kimaeneo au ubadilishaji wa silaha zinazotumiwa, ni makosa.

(v) Tupigane tu na lile jeshi la kawaida lililoamriwa na maadui kupigana upande wao. Na tusiwapige wengineo wa upande wa maadui.

(vi) Katika harakati za vita kuwepo kutohusishwa kwa haki za kidini na ibada. Maadui wasiposhambulia mahali shughuli za kidini zinakofanyika, basi Waislamu nao pia ni sharti wasipigane kwenye maeneo kama hayo.

(vii) Kama maadui wakitumia mahali pa ibada kama kituo cha mashambulio yao, basi Waislamu wanaweza wakayajibu mashambulio hayo. Lawama haitakuwa juu yao kama wakifanya hivyo. Mapigano hayaruhusiwi hata pembezoni mwa mahali pa ibada. Kushambulia mahali pa ibada na kupaangamiza au kapafanyia madhara yoyote imekatazwa kabisa. Mahali pa ibada patumiwapo kama kituo cha harakati za kivita panaweza pakavutia mashambulio

ya kujilipiza. Hapo lawama juu ya uharibifu wowote unaofanyiwa kituo hicho itwaendea maadui, wala sio Waislamu.

(viii)Maadui wanapoitambua hatari na kosa la kupatumia mahali pa ibada kuwa kituo, na kubadilisha makao yao ya kivita, Waislamu ni sharti wayaafiki mabadiliko hayo. Ukweli huu kwamba maadui walianzisha mashambulio kutoka mahali pa ibada na usitumiwe kuwa ni kisingizio cha kupashambulia mahali pale. Kwa kupastahi mahali pale Waislamu ni sharti nao wahamishe uwanja wa vita mara tu baada ya maadui kufanya hivyo.

(ix) Mapigano na yaendelee tu mradi kuingiliwa kwa uhuru wa dini kunaendelea. Dini inapoachiliwa huru kuiingilia kunapokuwa hakuruhusiwi na maadui kutangaza na kuanza kutenda sawa na wanavyotangaza, basi pasiwe tena na vita, hata kama ni maadui wanaovianzisha.

(3) Katika Sura Al-Anfaal 8:39-41 tunayo maagizo haya:

> Waambie wale waliokufura, kama wataacha watasamehewa yaliyopita na kama wakirudia, basi umekwishapita mfano wa watu wa kwanza. Na piganeni nao mpaka yasiwepo mateso, na dini iwe kabisa kwa ajili ya Allah. Lakini wakiacha, basi hakika Allah anayaona wanayoyatenda. Na kama wakigeuka, basi jueni kwamba Allah ndiye Mola wenu: ni Mola Mwema na Msaidizi Mwema.

Hivi ndio kusema kwamba vita vimelazimishiwa Waislamu. Lakini kama maadui wakiacha, basi ni wajibu wa Waislamu nao pia kuacha mapigano, na kusamehe yaliyopita. Lakini kama maadui hawaachi na wanawashambulia Waislamu tena na tena, basi yawapasa kukumbuka yaliyowapata maadui wa Manabii wa hapo awali. Waislamu na wapigane, yanapoendelea mateso ya kidini, na mradi dini si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu peke Yake na uingiliaji kwenye mambo ya kidini hautupiliwi mbali. Mdhalimu anapoacha, Waislamu nao pia na waache mapigano. Na wasiendlee na vita kwa sababu eti maadui wanaamini dini ya bandia. Thamani ya imani na matendo aijua sana

Mwenyezi Mungu naye Ataijazi malipo kama anavyopenda. Waislamu hawana haki ya kuingilia dini ya watu wengine hata kama dini ile ionekane kwao kuwa ni ya bandia. Ikiwa baada ya toleo la amani, maadui wanazidi kuwasha moto wa vita, basi Waislamu na wawe na uhakika wa kupata ushindi hata kama idadi yao ni ndogo. Kwani Mwenyezi Mungu atawasaidia, na ni nani awezaye kusaidia vizuri zaidi ya Mwenyezi Mungu?

Aya hizi zilifunuliwa kuambatana na vita vya Badr. Vita hivi ndivyo vilivyokuwa mapigano rasmi ya kwanza baina ya Waislamu na makafiri. Katika vita hivi Waislamu ndio walikuwa wadhulumiwa wa dhuluma za bure bilashi. Maadui walikuwa wamekata shauri kuvuruga amani ya Madina na ya maeneo yanayoizunguka. Licha ya haya yote, ushindi uliwaendea Waislamu na viongozi wakubwa wa maadui kuuawa. Hatua ya kulipiza dhuluma za bure kama hizi inaonekana kuwa ni ya kawaida, ya haki na ya lazima. Lakini licha ya hayo Waislamu wanafundishwa kuacha vita mara tu maadui wanapoviacha. Yote anayotakiwa adui kuruhusu ni uhuru wa dini na ibada.

(4) Katika Sura Al-Anfaal 8:62-63 tunayo maagizo haya:

> Na kama wakielekea kwenye amani nawe pia uielekee, na mtegemee Allah. Hakika Yeye ndiye Asikiaye Ajuaye. Na kama wakitaka kukuhadaa, basi Allah atakutoshelezea. Yeye ndiye aliyekusaidia kwa nusura Yake na kwa waaminio.

Hivi ndio kusema kwamba ikiwa wakati wa mapigano maadui wakati wowote watataka amani, basi Waislamu na wawakubalie mara moja na kuwanyooshea mkono wa amani. Waislamu na wafanye hivyo hata panapokuwa na hatari kuweza kudanganywa. Wao na wamtegemee Mwenyezi Mungu. Udanganyifu hautafaa dhidi ya Waislamu wanaotegemea msaada wa Mungu. Ushindi wao si kwa sababu ya wao wenyewe bali kwa sababu ya Mwenyezi Mungu. Katika nyakati za huzuni na shida kubwa, Mwenyezi Mungu amekuwa pamoja na Mtume[saw] na wafuasi wake. Na ndivyo atakavyokuwa pamoja nao dhidi ya wadanganyifu. Toleo la amani na

likubaliwe. Na lisikataliwe kwa huu udhuru kwamba huenda ikawa ni hila ambayo kwayo maadui wanajitafutia muda wa kuandaa mashambulio mapya.

Usisitizaji wa amani katika aya hizi si kwamba hauna maana. Ni usisitizaji unaotarajia yale mapatano Mtume[saw] aliyoyatia saini kule Hudaibiya. Mtume[saw] yuanasihiwa kwamba utakuja wakati ambapo maadui watataka amani. Toleo la amani na lisikataliwe kwa sababu eti maadui ndio waliokuwa wachokozi na walikuwa wameruka mipaka, au ya kuwa maadui hawawezi wakaaminika. Njia iliyo sawa inayowekwa na Islam yamtaka Mwislamu kukubali toleo la amani. Unyofu na hata kanuni vyote vyaufanya moyo wa kukubali toleo la amani kuwa kitu kinachotakikana.

(5) Katika Sura An-Nisaa 4:95 tunayo maagizo haya:

> Enyi mlioamini, mtakaposafiri katika njia ya Allah, basi pelelezeni sawasawa, wala msimwambie yule aliyewatoleeni salamu (ya kwamba) wewe si muumini; mnataka mafao ya maisha haya, lakini Allah anavyo vizuri vingi. Mlikuwa hivyo hapo kabla, lakini Allah akawafanyieni hisani, basi chunguzeni sawasawa; hakika Allah anazo habari za (yale) mnayoyafanya.

Hivi ndio kusema kwamba Waislamu wanapojitokeza kupigana, na wahakikishe kwamba kutofaa kwa vita kumefahamishwa maadui na kwamba wao (maadui) bado wanataka vita. Hata ikiwa hivyo, ikitokea mtu kufanya mapendekezo ya amani au kundi la watu, basi Waislamu na wasilikatalie mbali kwa kuleta udhuru kwamba eti hayaaminiki. Kama Waislamu wakikataa mapendekezo ya amani basi wao hawatakuwa wakipigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, bali kwa ajili ya kujifaharisha na kujitakia mafao ya dunia. Kama vile tu dini hutoka kwa Mungu, faida ya kidunia na fahari navyo pia hutoka kwake Yeye. Kuua kusiwe ndiko shabaha yenyewe, Yule tunayemtaka kumuua leo, kesho huenda akaongoka. Je, wangeweza Waialamu kuwa Waislamu kama wasingepatiwa nusura? Waislamu na waepukane na kuua kwa sababu wale waliopatiwa nusura wanaweza wakatokea kuwa ndio watu

walioongoka. Mwenyezi Mungu yuayajua sana yale watu wayafanyayo na ni kwa kadiri gani na madhumuni gani.

Aya yafundisha kwamba hata baada ya vita kuwa vimeanza, ni wajibu wa Waislamu kuwa na uhakika kwamba kweli maadui wamekazania uchokozi. Mara nyingi hutokea kwamba sio ugomvi unaodhamiriwa bali kutokana na taharuki na hofu maadui wameanza kujiandaa kwa vita. Isipokuwa Waislamu wamekuwa na uhakika kwamba shambulio la kichokozi limeandaliwa na maadui, na wasiingie vitani. Ikigunduliwa, au kama maadui wakitangaza kwamba maandilizi yao ni ya kujihami tu, basi Waislamu na wayakubali madai hayo na kujizuia kupigana vita. Na wasidadisi kwamba yale maandilizi ya maadui hayadhamirii chochote minghairi ya uchokozi; huenda alidhamiria uchokozi, lakini nia yake imebadilika. Nia na dhamiri si vinaendelea kugeukageuka? Je, Maadui wa Waislamu hawakuja kuwa marafiki?

(6) Juu ya kutohalifika mikataba Kurani yasema hivi:

> Isipokuwa wale mlioahidiana nao miongoni mwa washirikina kisha hawakuwapunguzieni chochote, wala hawakuwasaidia wowote dhidi yenu, basi watimizieni ahadi yao mpaka muda wao; hakika Allah huwapenda waogopao (Sura At-Tauba, 9:4).

Wapagani, wanaofanya mikataba na Waislamu, waheshimuo mikataba wala hawawasaidii maadui dhidi ya Waislamu, basi na wafanyiwe vivyo hivyo na Waislamu. Unyofu wataka kwamba Waislamu watimize upande wao wa mkataba kama ulivyoandikwa na kama inavyotakikana.

(7) Juu ya adui anayepigana na Waislamu anayetaka kuutalii Ujumbe wa Islam, Kurani yaamrisha ikisema:

> Na, kama mmoja wa washirikina akikuomba ulinzi, basi mlinde. ili apate kusikia maneno ya Allah, kisha mfikishe mahali pake pa usalama. Hayo ni kwa sababu ya kuwa hao ni watu wasiojua (Sura At-Tauba 9:6).

Hii ndio kusema kwamba ikiwa yeyote yule miongoni mwa wale

wanaopigana na Waislamu yuataka kimbilio kwa Waislamu kusudi ajifunze Islam na kuutafakaria Ujumbe wake; basi na wapatiwe kimbilio na Waislamu kwa muda unaoonekana kuwa ni wa kutosha kwa madhumuni hayo.

(8) Juu ya wafungwa wa kivita, Kurani yafundisha ikisema:

> Haimpasi Nabii kuwa na mateka mpaka apigane na kushinda katika nchi. Mnataka vitu vya dunia, hali Allah anataka Akhera. Na Allah ni Mwenye nguvu Mwenye hekima (Sura Al-Anfaal, 8:68).

Hivi ndio kasema kwamba haimpasi Nabii kuwafanya maadui mahabusu isipokuwa iwe ni matokeo ya vita vilivyomwaga damu nyingi. Ile desturi ya kuyafanya mahabusu makabila ya maadui bila ya vita vyovyote wala kumwagika kwa damu iliyotumika hadi kufikia zama za Islam — bali na hata baada ya ujaji wa Islam — yaharamishwa hapa. Kushikwa mahabusi kunaweza tu kukafanyiwa wapiganaji kisha baada ya kuwepo mapigano.

(9) Masharti ya kufunguliwa kwa wafungwa pia yamewekwa. Ndipo tunapoambiwa:

> Tena waachilieni kwa hisani au kwa kujikomboa mpaka vita vitue mizigo yake (Sura Muhammad, 47:5).

Kilicho bora, sawa na mafundisho ya Islamu, ni kuwaachilia wafungwa bila ya kutaka fidia. Na kwa kuwa kitu hiki hakiwi kinachowezekana wakati wote, imeruhusiwa pia njia ya uachiliaji huru kwa kulipa fidia.

(10) Ipo kanuni kwa ajili ya wale wafungwa wa kivita wasiokuwa na uwezo wa kujilipia wenyewe, na ambao hawana yeyote awezaye kuwalipia au ambaye atalipia uachiliwaji wao. Mara nyingi ndugu huwa wanaweza kulipa, lakini hawalipi, kwa sababu wao wanaona ni afadhali ndugu zao waendelee kuwa wafungwa — labda kwa sababu za njama za kutaka kuwaporea mali zao wakiwa hawapo karibu. Kanuni yenyewe imo ndani ua Kurani inaposema:

> Na wale wanaotaka mkataba wa kuachiliwa huru toka miongoni

> mwa wale inayowamiliki mikono yenu ya kuume, basi waandikieni, kama mkiona wema kwao. Na wapeni katika mali ya Allah aliyowapeni (Sura An-Nur 24:34).

Ndio kusema hivi, wale wafungwa wa kivita wasiostahili kuachiliwa huru bila ya fidia lakini ambao hawana mtu wa kuwalipia — kama hata hivyo wanaomba uhuru wao — wanaweza wakaupata kwa kujisainia mkataba ya kwamba wakiruhusiwa kufanya kazi na kupata mshahara, watalipa fidia zao. Hao waruhusiwe kufanya hivyo ikwa tu ustadi wao wa kuchapa kazi na kujichumia ujira waelekea kutumainika. Ustadi wao ukihakikika, basi hata na wapatiwe msaada wa kifedha na Waislamu katika juhudi zao za kufanya kazi na kujichumia kipato. Wale Waislamu wenye uwezo wa kufanya hivyo na walipe; au, na pafunguliwe mfuko wa kitaifa wa kuwainulia wafungwa hawa maskini.

Maneno yatokayo Kuranini tulioyakariri hapo juu yamo ndani yake mafundisho ya Islam kuhusu suala la vita na amani. Yanatuambia ni katika hali za namna gani, kulingana na Islam, endapo yajuzu kuingia vitani na ni mipaka ipi ya kutiliwa maanani na Waislamu wawapo vitani.

MAAGIZO YA MTUME[SAW] JUU YA VITA

Mafundisho ya Waislamu hayana tu maagizo yatolewayo katika Kurani. Bali mafundisho haya yanayo pia maagizo na mifano ya Mtume[saw]. Kile alichofanya au kile alichofundisha nayo pia ni sehemu muhimu ya mafundisho ya Islam. Twanukuu hapa chini baadhi ya maneno ya Mtume[saw] kuhusu suala la vita na amani.

(i) Waislamu wanakatazwa kabisa wasichanechane miili ya wafu (Muslim).

(ii) Waislamu wanakatazwa kabisa wasitumie udanganyifu (Muslim).

(iii) Watoto na wasiuawe, wala wanawake (Muslim).

(iv) Makasisi na wafanyakazi wa dini pamwe na viongozi wa kidini hawapaswi kuingiliwa (Tahawi).

(v) Vikongwe na wasiojiweza na wanawake na watoto wasiuawe. Uwezekano wa kupatikana amani ni sharti utiliwe maanani (Abu Dawud).

(vi) Waislamu wanapoingia nchi ya maadui, na wasiwatese raia wa kawaida. Na wasiruhusu dhuluma yoyote kwa watu wa kawaida (Muslim).

(vii) Jeshi la Waislamu na lisipige kambi mahali linapoweza kuwa ni msukosuko kwa raia wa kawaida. Linaposonga mbele ni sharti liwe angalifu lisifunge njia au kuwaletea shida wapita njia wengine.

(viii) Kuharibu sura za nyuso za watu na kusiruhusiwe (Bukhari na Muslim)

(ix) Maadui na watiwe hasara ndogo inavyowezekana (Abu Dawud).

(x) Wafungwa wa kivita wanaposalimishwa chini ya ulinzi, basi wale wa ukoo mmoja na wawekwe karibukaribu (Abu Dawud).

(xi) Wafungwa na wawekwe katika hali njema. Waislamu hawana budi kujali hali za wafungwa kuliko hali zao wao wenyewe (Tirmidhi).

(xii) Mabalozi na wajumbe kutoka nchi zingine ni sharti waheshimiwe. Makosa yoyote au dharau wafanyazo na yapuuziliwe mbali (Abu Dawud, Kitabul Jihad).

(xiii) Mwislamu akifanya kosa la kumfanyia vibaya mfungwa wa kivita, basi dhabihu yake na ifanywe kwa kumwachilia huru yule mfungwa bila kutolewa fidia.

(xiv) Mwislamu anapomweka mfungwa wa kivita, basi mfungwa huyo ni sharti alishwe na kuvishwa sawa kabisa na Mwislamu mwenyewe (Bukhari).

Mtume[saw] aliyasisitizia sana masharti haya kwa jeshi linalopigana kiasi hiki kwamba alitangaza ya kuwa yule ambaye hakuyafuata masharti haya hatakuwa akipigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu bali kwa ajili ya nafsi yake dhalili (Abu Dawud).

Hadhrat Abu Bakr[rh], Khalifa wa Kwanza wa Islam[ra], aliyaongezea maamrisho haya ya Mtume[saw] kwa yake kadha. Mojawapo ya haya kama linavyonukuliwa hapa chini nalo pia ni sehemu ya mafundisho ya Waislamu:

(xv) Majumba ya umma na miti ya matunda (na mimea ya chakula) na visiharibiwe (Muwatta).

Kutokana na maneno ya Mtume[saw] na maamrisho ya Khalifa wa Kwanza wa Islam[ra] ni dhahiri kwamba Islam imeweka hatua zenye athari ya kuepusha au kusitisha vita au kupunguza maovu yake. Kama vile tulivyosema hapo kabla, zile sera inazozifundisha Islam sio maagizo kiutawa tu; bali ni sera zilizo na vielelezo vyao vya matendo katika dhati ya Mtume[saw] na Makhalifa wa Islam wa awali. Kama dunia nzima ijuavyo, Mtume[saw] sio tu alifundisha sera hizi, bali yeye alizitimiliza kwa matendo na kusisitiza zifuatwe.

Tukigeukia zama zetu sisi wenyewe, hatuna budi kusema kwamba hapana mafundisho mengine yanayoelekea kusuluhisha matatizo ya vita na amani. Mafundisho ya Musa[as] yako mbali kabisa na picha yetu ya maadili na haki. Wala haiwezekani leo hii kutekeleza mafundisho hayo. Mafundisho ya Yesu hayafuatiki na yamekuwa hivyo tangu na tangu. Wakristo katika historia yao katu hawakujaribu kuyatimiza mafundisho haya. Ni mafundisho ya Islam peke yake yafuatikayo; mafundisho ambayo yamehubiriwa na kutekelezwa na wafuasi wake, na ambayo kutekeleza kwayo kunaweza kukaleta na kudumisha amani duniani.

Katika hizi siku zetu, Bwana Gandhi yaonekana kafundisha kwamba hata kama vita vikilazimishwa kwetu na tusipigane. Na tusipigane. Lakini mafundisho haya hayakutumiwa wakati wowote katika historia ya dunia. Hayajajaribiwa. Haiwezekani, hivyo basi, kusema ni thamani gani mafundisho haya yanaweza yakawa nayo katika suala zima la vita na amani. Bwana Gandhi aliishi vya kutosha akaweza kuona chama cha Indian Congress kikishikilia hatamu za uhuru wa kisiasa. Lakini hata hivyo Serikali ya chama cha Congress

haikulivunjilia mbali jeshi wala makundi mengine ya askari wa India. Inafanya tu mipango ya kulifanya jeshi liwe ni jeshi la Kihindi. Pia inayo plani ya kuwarejesha kazini wale maofisa wa Kihindi waliojifanya wenyewe kuwa ni Jeshi la Taifa la India (na walioachishwa kazi na utawala wa Kiingerza) pale Wajapani walipozishambulia nchi za Burma na India katika hatua za mwisho za Vita Vikuu vya hivi majuzi. Yeye mwenyewe Bwana Gandhi amepata mara nyingi kulalamika akitaka yasilaumiwe sana makosa ya kuzusha fujo na kusisitika kuwaachia huru waliofanya ghasia. Hii kwa akali yaonesha kwamba mafundisho ya Bwana Gandhi hayawezi yakatumika na kwamba Bwana Gandhi mwenyewe yuaujua ukweli huu pamwe na wafuasi wake wote. Hapajatolewa kwa akali mfano wa matendo kuonesha dunia vile wito huu wa 'kutotumia nguvu' inavyoweza ukatumika pale ubishi wa kushikiana silaha unapozuka baina ya taifa na taifa na baina ya nchi na nchi, au vile wito huu wa kutotumia nguvu uwezavyo kuepusha au kukomesha vita. Kuzungmzia mbinu ya kusitishia vita, lakini kisha kukosa kabisa kutoa kielelezo cha kimatendo cha mbinu yenyewe kwaonesha kwamba mbinu hiyo haitekelezeki. Hivyo basi, itaonekana ya kuwa uzoefu wa kibinadamu na hekima ya kibinadamu vyaashirla mbinu moja tu ya kuzuilia au kusitishia vita; na mbinu yenyewe ilifundlishwa na kutumiwa na Mtume[saw] wa Islam.

MAKAFIRI WAFANYA MASHAMBULIO YA HAPA NA PALE

Yale majeshi ya muungano wa Waarabu yalirejea kutoka Vita vya Handaki yakiwa yameshindwa na kuhuzunika, lakini wakiwa hawajaamini kabisa kwamba uwezo wao wa kuwanyanyasa Waislamu umekwisha. Ingawaje walikuwa ni washinde, walijua kwamba wao bado ndio waliokuwa wengi zaidi. Wangeweza kwa urahisi kusumbua Mwislamu mmoja mmoja, kuwapiga na hata kuwaulia mbali. Kwa huku kuwatesa Waislamu mmoja mmoja makafiri walitumainia kujiondolea majonzi yao ya ushinde. Hivyo si muda mrefu baada ya vile vita, wao wakanza kushambulia Waislamu pembezoni mwa mji wa Madina. Baadhi ya wapanda ngamia wa kabila la Faraza

walishambulia Waislamu karibu na Madina. Wakapora ngamia waliopatikana kule, wakateka nyara mwanamke na kutorokea makwao. Yule mwanamke aliwahi kuwaponyoka, lakini wale watu wa kabila la Faraza wakafaulu kutorosha idadi kadha ya wanyama. Mwezi mmoja baadaye, kundi moja la kabila la Ghatafan lilishambulia kutoka upande wa kaskazini kwenye jaribio la kuwapokonya Waislamu ngamia zao. Mtume[saw] akamtuma Hadhrat Muhammad[ra] bin Maslama na Masahaba kumi wapanda rikabu kwenda kupeleleza na kulinda wanyama wa Waislamu. Lakini maadui wakakivizia kikundi hiki cha Waislamu na wakakishambulia kikatili, na kuwawacha maiti. Lakini, Hadhrat Muhammad[ra] bin Maslama hakuwa maiti bali alikuwa amezirai tu. Alipopata fahamu alijikokota na kurudi mjini Madina na akatoa ripoti. Siku chache baadaye, mjumbe wa Mtume[saw] akiwa njiani kwenda kwa mji mkuu wa Kirumi alishambuliwa na kunyang'anywa na watu wa kabila la Jurham. Mwezi mmoja baadaye, watu wa kabila la Banu Faraza walishambulia msafara wa Waislamu na kukimbia na mali nyingi. Yawezekana kwamba shambulio hili halikusababishwa na uadui wa kidini. Watu wa hili kabila la Banu Faraza walikuwa ni wezi waliozoea kupora mali na kuua. Mayahudi wa huko Khaibar, waliokuwa kipengele kikuu kwenye Vita vya Handaki, nao pia walikuwa wamekata shauri kulipiza kisasi cha ule ushinde mbaya walioonjeshwa katika mapigano yale. Walizunguka wakichochea wanavijiji vya kikabila na maofisa wa kiserikali kwenye mipaka ya himaya ya Warumi. Hivyo basi, viongozi wa Waarabu huku wakiwa hawawezi kuifanyia Madina shambulio la moja kwa moja, walikuwa wakila njama na Mayahudi kufanya maisha yawe magumu kwa Waislamu. Mtume[saw], hata hivyo, alikuwa bado hajayafanyia maamuzi mapigano komesha. Yeye alifikiri huenda viongozi wa Waarabu wakafanya mapendekezo ya amani, na hivyo basi ugomvi wa raia kumalizika.

MTUME[SAW] YUASAFIRI MAKKA NA MASAHABA 1500

Katika wakati huu Mtume[saw] akaona njozi inayotajwa hivi katika Kurani:

> Kwa hakika Mwenyezi Mungu amemyakinishia Mtume Wake njozi kwa haki; Bila shaka nyinyi mtaingia kwenye Msikiti Mtukufu ***Insha Allah*** kwa salama, mkinyoa vichwa vyenu na kupunguza nywele, hamtaogopa, na kabla ya haya (Yeye) aliwapeni ushindi ulio karibu (Sura Al-Fat'h 48:28).

Hivi ndio kusema kwamba, Mwenyezi Mungu alikuwa ameamua kuwaruhusu Waislamu waingie kwenye Kaaba kwa amani, wakiwa vichwa vimenyolewa na nywele kupunguzwa (hizi zikiwa ni alama za nje za wanaohiji kwenye Kaaba), na bila ya hofu. Lakini Waislamu hawakujua vile hasa Mwenyezi Mungu atakavyolifanya jambo hili kutendeka. Isitoshe, kabla Waislamu kutimiza haji yao kwa amani, wao walikuwa wapate ushindi mwingine, kitangulizi cha ushindi ulioahidiwa katika ile njozi.

Katika njozi hii Mwenyezi Mungu alitabiri ushindi wa Waislamu unaokuja, kuingia kwao mjini Makka kwa amani na kutekwa kwa mji wa Makka bila kutumia silaha. Lakini Mtume[saw] akafahamu utabiri wenyewe kuwa na maana ya kwamba Waislamu walikuwa wameamriwa na Mwenyezi Mungu waende mara moja kuizunguka Kaaba. Huu ukoseaji wa Mtume[saw] wa tafsiri ya njozi ile ukawa kuwa kisababisho cha ule ushindi ulio karibu unaoahidiwa na njozi yenyewe. Hivyo, kwa kukosea Mtume[saw] akaplani kusafiri kuelekea kwenye Kaaba. Aliwatangazia Waislamu njozi yake na vile yeye ailivyoielewa na akawataka wajiandae. Akawaagiza akisema, "Nyinyi mtakwendazunguka Kaaba tu. Hivyo basi, na pasiwepo na maonesho dhidi ya maadui". Kuelekea mwisho wa mwezi wa Februari 628, hivyo basi, mahujaji elfu moja mia tano[3] wakiongozwa na Mtume[saw]

[3] Katika haji hii uliyoandaliwa mwaka mmoja baada ya Vita vya Handaki, watu elfu moja mia tano tu ndio walioandamana na Mtume[saw]. Idadi ya wapiganaji Waislamu kwenye Vita vya Handaki ingeliweza kuwa chini lakini sio zaidi ya hii idadi ya watu elfu moja na mia tano. Wanahistoria wanaoifanya idadi ya wapiganaji Waislamu katika vita vya Handaki kuwa elfu tatu, hivyo basi, wamekosea. Idadi yenyewe inaweza kwa kweli kufanywa watu elfu moja na mia mbili.

walianza safari kuelekea Makka. Walinzi ishirini wapanda rikabu walitangulia mbele masafa kadha kwenda kuwatahadharisha Waislamu endapo maadui wataonesha ishara za mashambulio.

Upesi watu wa Makka wakapata fununu za msafara huu. Utamaduni wa siku zile ulikuwa imeifanya desturi ya kuizunguka Kaaba kuwa ni haki ya wote. Haki hii kwa kweli wasingeliinyimwa Waislamu. Wao walikuwa wametangaza kinagaubaga kwamba madhumuni ya safari yao ilikuwa ni kuzunguka Kaaba, sio zaidi. Mtume[saw] alikuwa amekataza maringo ya aina yoyote. Ilikuwa pasiwepo na ubishi, udadisi au kujinaki. Licha ya haya yote, watu wa Makka walianza maandalizi kana kwamba ni mapigano ya silaha. Waliweka ulinzi pande zote, wakayaita upande wao makabila yaliyokiizunguka Makka na kuonekana wamekata shauri kupigana. Mtume[saw] alipofika karibu na Makka, alijulishwa kwamba Makureishi walikuwa tayari kwa vita. Walikuwa wamevalia ngozi za simba marara, walikuwa na wake na watoto wao na walikuwa wameapa kutowaruhusu Waislamu kupita. Ngozi za simba marara zililkuwa ni ishara ya kijangili ya kuamua kupigana vita. Punde baadaye, kundi la watu wa Makka likitembea mbele ya jeshi lao liliwakabili Waislamu. Ikawa sasa Waislamu wasingeweza kwenda mbele isipokuwa kwa kuchomoa panga zao. Hata hivyo, Mtume[saw] hakuwa amekata shauri kufanya jambo lolote kama hilo.

Yeye alimwajiri mwongoza-njia kuuonesha ule msafara wa Waislamu njia nyingine kupitia jangwani. Mwongoza-njia huyu akamfikisha Mtume[saw] na Masahaba wake huko Hudaibiya, mahali palipo karibu sana na Makka.

Ngamia wa Mtume[saw] akasimama na kukataa kwenda mbele.

Akatamka Sahaba mmoja akimwambia Mtume[saw], "Ewe Mtume wa Mungu, mnyama huyo yuaonekana mchovu. Yafaa ubadilishe mwingine".

Mtume[saw] akajibu akisema, "La hasha, huyu mnyama si mchovu. Inaonekana ni kwamba huenda Mwenyezi Mungu yuatutaka

tusimame hapa na kutokwenda mbele. Mimi, hivyo basi, napendekeza ya kwamba tupige kambi hapahapa na tuwaulize watu wa Makka ikiwa wao watataruhusu kufanya Haji. Mimi binafsi, nitakubaliana na masharti yoyote watakayotaka kuyaweka" (Halabiyya, J. 2, uk. 13).

Wakati huu jeshi la Makka halikuweko mjini Makka. Lilikuwa limesafiri masafa kadha kwenda kabiliana na Waislamu kwenye njia kuu ya kwenda Madina. Angelitaka Mtume[saw], basi yeye angeliweza kuwaongoza wale watu wake elfu moja na mia tano hadi mjini Makka na kuuteka mji ule bila ya upinzani. Lakini yeye alinuia kujaribu kuizunguka Kaaba, na pia kwa kibali cha watu wa Makka. Yeye angelikabiliana na kupigana na watu wa Makka endapo tu watu wa Makka walikuwa ndio wa kwanza kushambulia Waislamu. Kwa hiyo, yeye aliiacha njia kuu na kupiga kambi huko Hudaibiya. Punde si punde habari zikamfikia jemadari wa Makka, ambaye aliwaamuru watu wake kuondoka na kwenda karibu na Makka. Hapo watu wa Makka wakamtuma chifu, kwa jina Budail, aende akashauriane na Mtume[saw]. Mtume[saw] akamwambia Budail kwamba yeye na wale Waislamu wengine walitaka tu kuizunguka Kaaba; lakini kama watu wa Makka walitaka kupigana, basi Waislamu walikuwa tayari. Hapo 'Urwa, mkwewe Abu Sufyan, jemadari wa watu wa Makka, akaja kwa Mtume[saw]. Huyu akaonesha dharau kubwa. Akawatusi Waislamu akiwaita takataka za umma na kusema watu hawatawaruhusu kuingia mjini Makka. Watu wa Makka wakazidi kuja kuzungumza na la mwisho walilosema ni kwamba kwa akali mwaka ule wasingeliwaruhusu kufanya hata angalau kuizunguka Kaaba. Watu wa Makka watafedheheswa endapo wataruhusu izungukwe Kaaba mwaka huu. Mwaka ujao huenda wakafanya hivyo.

Baadhi ya makabila marafiki wa watu wa Makka waliwashauri viongozi wa Makka wawaruhusu Waislamu kuizunguka Kaaba. Walichotaka Waislamu ilikuwa ni haki yao ya kuizungmka tu. Palikuwa na maana gani wao kukatazwa hata kitu kama hiki? Lakini watu wa Makka wakadinda. Hapo ndipo viongozi wa kikabila

waliposema, kumbe watu wa Makka hawakuwa na haja na amani na kutishia kujitenga nao. Kutokana na hofu, watu wa Makka wakalazimika kujaribu kufikia mapatano na Waislamu. Mara tu baada ya Mtume[saw] kupata habari hii, alimtuma Hadhrat Uthman[ra] (aliyekuwa baadaye Khalifa wa Tatu wa Islam) aende kwa watu wa Makka. Hadhrat Uthman[ra] alikuwa na nduguze wengi mjini Makka. Wakajitokeza na kumzunguka, na wakakubali kumruhusu aizunguke Kaaba, lakini wakatangaza kwamba wasingelimruhusu Mtume[saw] kufanya hivyo hadi mwaka wa kesho. Lakini Hadhrat Uthman[ra] akawajibu akiwaambia, "Mie katu sitaizunguka Kaaba isipokuwa niandamane na Bwana wangu". Mazungumzo ya Hadhrat Uthman[ra] na machifu wa Makka yakatokea kuwa marefu. Kwa kutia fitina ukazushwa uvumi ya kwamba yeye alikuwa ameuawa. Uvumi huo ukamfikia Mtume[saw]. Kusikia hivyo Mtume[saw] akawakusanya Masahaba na akatamka akisema, "Maisha ya balozi yanaheshimiwa miongoni mwa mataifa yote. Mimi nimesikia kwamba watu wa Makka wamemuua Uthman. Hii ikiwa kweli, basi ni lazima tuingie Makka hata kukitokea kitu gani." Nia ya Mtume[saw] ya hapo awali ya kuingia Makka kwa amani ikabidi igeuzwe, katika hii hali iliyogeuka. Mtume[saw] akaendelea kutamka akisema, 'Wale wenye kuahidi kwa dhati kwamba ikiwa ni lazima wasonge mbele, basi hawatarudi nyuma ila kama washindi, na wajitokeze wale kiapo juu ya mkono wangu". Kabla Mtume[saw] hajamaliza kusema, wale Masahaba wote elfu moja na mia tano walinyanyuka na kujisukuma mbele kuushika mkono wa Mtume[saw] na kula kiapo kile. Kiapo hiki kina umuhimu maalumu katika historia ya Islam ya hapo awali. Chaitwa "kiapo cha Mtini". Kilipoliwa kiapo hiki, Mtume[saw] alikuwa akiketi chini ya mti. Kila mmoja wa wale waliokila kiapo hiki, kikawa ni kitu cha kujivunia maisha yake mazima. Miongoni mwa wale elfu moja na mia tano hapana hata mmoja wao aliyesitasita. Wote waliahidi kwamba ikiwa yule balozi wa Waislamu alikuwa ameuawa, basi wao hawatarudi nyuma. Ama wangeiteka Makka kabla ya magharibi, au wawe wote watakufa wakipigana. Ulaji wa kiapo haukuwa umemalizika akajitokeza

Hadhrat Uthman[ra]. Aliripoti kwamba watu wa Makka hawakuwa wamekubali kuwaruhusu Waislamu kuizunguka Kaaba hadi mwaka wa kesho. Walikuwa wameteua wajumbe wao waje wasaini mapatano na Waislamu. Punde tu, Suhail, chifu mmoja wa Makka akafika kwa Mtume[saw]. Mapatano yakafikiwa na mkataba ukaandikwa.

MKATABA WA HUDAIBIYA

Mkataba huu uliandikwa kama ifuatavyo:

Kwa jina la Mwenyezi Mungu. Haya ndiyo masharti ya amani baina ya Muhammad, mwana wa Abdullah, na Suhail ibn 'Amr, mjumbe wa Makka. Hayatakuwepo mapigano kwa miaka kumi. Yeyote yule mwenye kutaka kujiunga na Muhammad na kufanya naye mapatano yoyote yuko huru kufanya hivyo. Yeyote yule mwenye kutaka kujiunga na Makureish na kufanya mapatano nao yuko huru kufanya hivyo. Barobaro, au yule ambaye babake yu hai, akienda kwa Muhammad bila ruhusa ya babake au mlezi wake, atarejeshwa kwa babake au mlezi wake. Lakini akitokea mtu kwenda kwa Makureish, basi huyo hatarejeshwa. Mwaka huu Muhammad atarudi bila ya kuingia Makka. Lakini mwaka ujao yeye na wafuasi wake wanaweza wakaingia Makka, kukaa siku tatu na kuizunguka Kaaba. Katika siku hizi tatu Makureishi watatoka kwenda vilimani. Muhammad na wafuasi wake watakapoingia Makka, hawatakuwa na silaha isipokuwa zile panga za ndani ya ala, wasafiri wa Arabuni wanazokuwanazo wakati wote (Bukhari).

Palitukia mambo mawili ya kukumbukwa wakati wa kusainiwa kwa mkatabu huu wa amani. Baada ya masharti kuwa yameafikiwa, Mtume[saw] alianza kuandikisha mkataba na kusema, "Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa ***rehema***, Mwingi wa ***ukarimu***."

Suhail alipinga akisema, "Mwenyezi Mungu twamjua na twamwamini, lakini ni mambo gani haya ya 'Mwingi wa ***rehema*** na Mwingi wa ukarimu?' Huu mkataba ni baina ya pande mbili. Kwa hiyo imani ya kidini ya pande zote mbili ni sharti iheshimiwe."

Mtume[saw] akakubali mara moja na akmwelekeza mwandishi wake akimwambia, "Andika, 'Kwa jina la Mwenyezi Mungu', basi". Sasa Mtume[saw] akaanza kuandikisha masharti ya mkataba. Sentensi ya kwanza ilikuwa, 'Haya ndiyo masharti ya amani baina ya watu wa Makka na Muhammad, Mtume wa Mungu'. Suhail akapinga tena akisema, "Ingetukia sisi kukufikiria wewe kuwa u Mtume wa Mungu, basi tusingelikupiga vita." Mtume[saw] ubishi huu pia akaukubali. Badala ya Muhammad, Mtume wa Mungu, yeye akapendekeza Muhammad mwana wa Abdullah. Kwa kuwa Mtume[saw] alikuwa akikubaliana na kila walichokipendekeza watu wa Makka, Masahaba wakaiona hii kuwa ni fedheha iliyowakasirisha sana. Damu zikaanza kuwachemka, na Hadhrat Umar[ra], aliyepandwa na mori kupita wote, akamwendea Mtume[saw] na akauliza akisema, "Ewe Mtume wa Mungu, kwani sisi sio wa msimamo wa sawa?" Mtume[saw] akasema "Naam, sisi tu wa msimamo wa sawa". Hadhrat Umar[ra] akauliza akisema, "Na kwani hatukuambiwa na Mwenyezi Mungu kwamba mtaizunguka Kaaba?"

Mtume[saw] akasema, "Naam."

"Basi ni ya nini mapatano haya na ni ya nini haya masharti haya yenye kufedhehesha?"

Mtume[saw] akasema, Mwenyezi Mungu alitabiri kweli kwamba tungeliizunguka Kaaba kwa amani lakini Yeye hakusema ni lini. Mimi kweli nilifikiri itakuwa mwaka huu. Lakini naweza kuwa nimekosea. Kwani ni sharti iwe mwaka huu?

Hadhrat Umar akanyamazishwa.

Hapo Masahaba wengine nao wakaleta pingamizi zao. Baadhi yao wakataka kujua itakuwaje kukubali kumrejesha kwa babake au mlezi wake barobaro ambaye angesilimu, bila ya sisi kuwa na masharti hayo hayo kwa ajili ya Mwislamu ambaye angejiunga au kutokea kuwaendea watu wa Makka. Mtume[saw] akasema hapo hapakuwa na madhara yoyote. Akizidi kuelezea, Mtume[saw] alisema, 'Kila mwenye kusilimu hufanya hivyo kwa sababu yuazikubali itikadi na desturi

zinazofundishwa na Islam. Yeye hawi Mwislamu kusudi ajiunge na kundi na kufuata mila zake. Mtu sampuli hiyo atahubiri Ujumbe wa Islam popote aendapo, na kuwa kama chombo cha kuenezea Islam. Lakini mtu mwenye kuiritadi hana faida kwetu sisi. Ikiwa moyoni yeye haamini tena yale tunayoyaamini, basi si mwenzetu tena. Ni afadhali aende kwingineko." Jawabu hili la Mtume[saw] liliwatuliza wale waliokuwa na shaka msimamo uliochukuliwa na Mtume[saw]. Jawabu hili na liwasute hivi leo wale wote wenye kudhania kwamba katika Islam adhabu ya kuritadi ni kifo. Kama mambo yangelikuwa hivyo, basi Mtume[saw] angelisisitizia kurejeshwa na kuadhibiwa kwa wale walioiacha Islam.

Mkataba ulipokuwa umekwisha kuandikwa na kutiwa saini na pande zote mbili, mara kikatokea kisa kilichoupatia majaribio uaminifu wa pande zote mbili. Mwana wa Suhail, mwakilishi wa watu wa Makka, alitokea mbele ya Mtume[saw] akiwa amekazwa kamba, kujeruhiwa na mchovu. Akamwangukia Mtume[saw] miguuni na kutamka akisema, "Ewe Mtume wa Mungu, mimi ni Mwislamu kwa moyo, na kwa sababu ya imani yangu imekuwa mimi kufikiwa na mashaka haya kwa mkono wa babangu. Babangu alikuwa nawe hapa. Hivyo basi, mimi nikaweza ponyoka na kufika kwako." Mtume[saw] hakuwa amesema chochote, Suhail alipoingilia kati na kusema kwamba mkataba ulikuwa umesainiwa na hapakuwa na budi aende naye. Abu Jandal — likiwa hili ndilo lililokuwa jina la yule kijana — akawa kasimama mbele ya Waislamu, ndugu wa nduguze, akiwa yu mwenye kukatishwa tamaa na mateso ya babake. Kulazimika kumrejesha alikotoka ulikuwa ni wajibu wasioweza kuuvumilia. Wakachomoa panga zao na kuonekana kuwa tayari kufa au kumwokoa huyu ndugu. Kijana Abu Jandal mwenyewe akamsihi Mtume[saw] amwache akae. Iweje yeye kumrejesha kwa wale wadhalimu ambako alikuwa amefanikiwa kukutoroka. Lakini Mtume[saw] alikuwa ameishaamua. Akamwambia Abu Jandal, "Manabii hawetangui kauli zao. Sisi sasa tumesaini huu mkataba. Ni juu yako kufanya uvumilivu na kumtegemea Mwenyezi Mungu. Bila shaka Yeye Atajaalia uhuru wako na uhuru wa vijana wengine chipukizi kama wewe." Mkataba

ulipokuwa umesainiwa, Mtume[saw] alirejea Madina. Punde si punde, kijana mwingineo aliyesilimu kutoka Makka, kwa jina Abu Basiir, alifika Madina. Lakini kulingana na masharti ya yale mapatano, yeye pia akarejeshwa na Mtume[saw]. Njiani, yeye na walinzi wake wakazushiana purukushani ambapo yeye alimuulia mbali mmoja wao na hivyo kuweza kuponyoka. Watu wa Makka wakaenda tena kwa Mtume[saw] na kumlalamikia. Mtume[saw] akasema akiwaambia, "Lakini sisi tumewapeni mtu wenu. Yeye sasa ameiponyoka mikono yenu. Si jukumu letu tena kumpata na kuwarejesheeni tena. Siku chache baadaye, mwanamke mmoja alitorokea Madina. Baadhi ya nduguze wakamfuata na kutaka arejeshwe. Mtume[saw] akafafanua akisema kwamba ule mkataba ulikuwa ni kuwahusu wanaume, sio kuwahusu wanawake; hivyo yeye akakataa kumrudisha mwanamke huyu.

BARUA ZA MTUME[SAW] KWA WAFALME MBALIMBALI

Baada ya kukaa Madina aliporudi kutoka Hudaibiya, Mtume[saw] alianzisha plani mpya kuzagaza Ujumbe wake. Alipowatajia Masahaba plani hii, baadhi yao waliojua desturi na nidhamu zilizofuatwa katika mabaraza ya wafalme wakamwambia Mtume[saw] kwamba wafalme hawapokei barua zisizokuwa na muhuri wa wanaoziandika. Mambo yakiwa hivyo Mtume[saw] akatengenezesha muhuri uliokuwa na maneno, Muhammad Rasulullah.

Kwa sababu ya heshima, jina Allah liliandikwa juu, chini yake Rasul na chini zaidi Muhammad.

Katika mwezi wa Muharram, mwaka 628, wajumbe walikwenda miji mikubwa mbalimbali, kila mmoja wao akiwa na barua kutoka kwa Mtume[saw], ikiwaita watawala waikubali Islam. Wajumbe walikwenda kwa Herakla, Mfalme wa Rumi, Wafalme wa Iran, Misri (Mfalme wa Misri zama zile alikuwa ni gavana wa Kaisari) na Uhabeshi. Pia walikwenda kwa wafalme na watawala wengine. Barua iliyoandikiwa Kaisari ilipelekwa na Hadhrat Dihya Kalbi[ra] aliyeagizwa kwanza amwendee Gavana wa Basra. Hadhrat Dihya[ra] alipomwona yule Gavana, kumbe Kaisari mwenyewe alikuwemo nchini Siria akiwa

katika ziara ya kuitembelea himaya yake. Hadhrat Dihya[ra] alipofika kwenye baraza la mfalme, aliambiwa kwamba yeyote akubaliwaye kukutana na Kaisari ni lazima amsujudie. Hadhrat Dihya[ra] akakataa kufanya hivyo, akisema kwamba Waislamu hawamsujudii mwanadamu yeyote. Hivyo basi, Hadhrat Dihya[ra] akajikalia mbele ya Kaisari bila ya sijida iliyotakikana. Kaisari akaisomewa barua ile na mkalimani na akataka kujua kama mjini kulikuwemo na msafara wa Waarabu. Alisema kwamba yeye alitaka kumhoji Mwarabu kuhusu huyu Nabii wa Kiarabu aliyekuwa amemletea mwaliko wa kuikubali Islam. Ikatokea kwamba Abu Sufyan alikuwemo mjini akiwa na msafara wa kibiashara. Maofisa wa baraza la mfalme wakampeleka kwa Kaisari. Abu Sufyan akasimamishwa mbele ya Waarabu wengine waliokuwepo, waliotakiwa kumkosoa endapo ataongopa au kusema visivyo. Kisha Kaisari akaanza kumhoji Abu Sufyan. Mazungumzo yao yamerekodiwa historiani hivi:

Herakla: Wamjua mtu huyu adaiye kuwa ni Nabii na aliyenitumia barua? Waweza kusema yuatokana na ukoo wa aina gani?

Abu Sufyan: Yuatokana na ukoo mtukufu na ni mmoja wa ndugu zangu.

Herakla: Je, wamekuwepo Waarabu kabla yake ambao wametoa madai kama yake?

Abu Sufyan: La.

Herakla: Je, watu wako walipata kumwita mwongo kabla ya kutangaza madai yake

Abu Sufyan: La.

Herakla: Je, amepata kuwemo mfalme au mtawala miongoni mwa wakale wake?

Abu Sufyan: La.

Herakla: Waufikiriaje uwezo wake wa kawaida na kipawa chake cha maamuzi?

Abu Sufyan: Hatujapata dosari yoyote katika uwezo wake na kipawa chake cha maamuzi.

Herakla: Wafuasi wake wakoje? Je, ni watu wakubwa na wenye uwezo au wao ni watu maskini na wanyonge?

Abu Sufyan: Wengi wao ni maskini na wanyonge na chipukizi.

Herakla: Je, idadi yao huelekea kuongezeka au kupungua?

Abu Sufyan: Kuongezeka.

Herakla: Je, wafuasi wake hupata wakati wowote kurejelea imani zao za kale?

Abu Sufyan: La.

Herakla: Je, amepata wakati wowote kuvunja ahadi?

Abu Sufyan: Hadi hivi sasa, la. Lakini tumefanya naye mkataba mpya hivi majuzi. Wacha tuangalie afanyavyo juu yake.

Herakla: Je, mmpata kupigana naye hadi hivi sasa?

Abu Sufyan: Naam.

Herakla: Kukawa na matokeo gani?

Abu Sufyan: Leo sisi kesho yeye, twabadilishana naye ushindi na ushinde. Mathalan, katika vita vya Badr, ambavyo mimi sikuwemo, yeye aliweza kutushinda. Katika vita vya Uhud, ambavyo mimi niliongoza upande wetu, sisi tuliwatoa jasho. Tuliwapasua matumbo yao na masikio na pua.

Herakla: Lakini yuafundisha nini?

Abu Sufyan: Kwamba sisi tumwabudu Yule Mungu Mmoja na tusimhusishe na chochote. Yuahubiri dhidi ya masanamu waliyoyaabudu wakale wetu. Yuatutaka sisi, badala yake, tumwabudu Mungu Mmoja wa Pekee, kusema kweli tupu na daima tujitenge na maovu yote na matendo ya kifisadi. Yuataka tufanyiane wema na kuidumisha ahadi zetu na wajibu wetu.

Mazungumzo haya ya kukumbukwa yakakatika na kisha Kaisari akatamka akisema:

> Kwanza mimi nilikuuliza juu ya ukoo wake na ukasema yeye alitokana na ukoo mtukufu. Kwa kweli, Manabii daima hutokana na ukoo Mtukufu. Kisha nikakuuliza ikiwa mtu yeyote, kabla yake alikuwa amefanya madai kama haya na ukasema, La. Swali hili nilikuuliza kwa sababu mimi nilifikiria kwamba ikiwa zamani za hivi majuzi mtu fulani alikuwa amefanya madai sampuli hii, basi mtu anaweza akasema kwamba huyu Nabii yuaigiza madai yale. Mimi kisha nikakuuliza kama yeye alikuwa amepata wakati wowote kuitwa mwongo kabla haya madai yake hayajatangazwa na ukasema, La. Hapa nilichokimaanisha ni kwamba mtu asiyeongopea watu hatamwongopea Mungu. Nikafuatia kukukuliza kama amepata kuwepo mfalme miongoni mwa wakale wake na ukasema La. Hapo mimi nilifahamu kwamba madai yake hayawezi yakawa ni hila za kuunyakulia tena ufalme. Kisha nikakuuliza kama watu anaojichumia wengi zaidi ni watu wakubwa, matajiri na wenye uwezo au maskini na wanyonge. Na katika kujibu ukasema kwamba kwa jumla ni watu maskini na wanyonge, sio watu wakubwa wenye kujivuna, na hivyo ndivyo walivyo wafuasi wa awali wa Nabii. Mimi kisha nikakuuliza kama wafuasi wake wanaongezeka ama kupunguka na ukasema wanaongezeka. Hapa mimi nilikumbuka ya kwamba wafuasi wa Nabii huzidi kuongezeka mpaka yule Nabii ahitimishe lengo lake. Halafu nikakuuliza kama wafuasi wake hutokea kuachana naye kutokana na kuchukizwa au kutopata walichokitumainia, na ukasema, La. Hapo mimi nikakumbuka kwamba wafuasi wa Nabii kwa kawaida huwa imara. Wanaweza wakalegalega kwa sababu zingine, lakini sio kwa kukirihishwa na imani yao. Baadaye mimi nikakuuliza kama yamepata kuwepo mapigano kati yenu na yeye, na kama ni hivyo, yamekuwa na matokeo gani. Na ukasema kwamba nyinyi na wafuasi wake

> mlibadilishana ushindi na ushinde, na Manabii ndivyo walivyo. Mwanzoni wafuasi wao huoneshwa cha mtema kuni, lakini mwishowe wao hushinda. Halafu nikakuuliza kile anachofundisha na ukasema yeye yuafundisha kumwabudu Mungu Mmoja, kusema kweli, wema na umuhimu wa kutimiza ahadi na kutekeleza majukumu. Pia mimi nilikuuliza kama yeye wakati wowote huwa ni mdanganyifu, na ukasema, La. Na hiyo ndiyo tabia ya watu wema. Hivyo basi kwangu mimi, inaonekana kwamba madai yake ya kuwa Nabii wa Mungu ni ya kweli. Kidogo mimi nilikuwa nikitazamia kudhihiri kwake katika wakati huu wetu, lakini sikujua atakuja kuwa Mwarabu. Kama vile ulivyoniambia ni kweli, basi mimi nadhani athari zake na himaya yake vitazienea nchi hizi (Bukhari).

Matamshi haya yaliwaudhi maofisa wa baraza la kifalme na wakaanza kumlaumu yule Mfalme kwa kumsifu Mwalimu wa taifa jingine. Yakazuka malalamiko. Kisha maofisa wa baraza la mfalme wakamwondoa pale Abu Sufyan na wenzake. Barua yenyewe Mtume[saw] aliyomwandikia Kaisari yapatikana katika rekodi za kihistoria. Yasema hivi:

> Kutoka kwa Muhammad, Mtumishi wa Mungu na Mtume Wake. Kwa Chifu wa Urumi, Herakla. Yeyote mwenye kukanyaga njia yenye mwongozo, amani iwe juu yake. Baada ya hayo, Ewe Mfalme, mimi nakukaribisha katika Islam. Silimu. Mungu atakunusuru dhidi ya maafa yote, na kukulipa maradufu. Lakini kama ukipinga na kuukatalia mbali Ujumbe huu basi hutatwisha madhambi ya ukataaji wako tu, bali ya ukataaji wa rai zako yatakuwa juu yako. Enyi watu wa Kitabu: Njooni kwenye neno lililo sawa baina yenu na baina yetu, ya kwamba tusimwabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, na kwamba tusimshirikishe na chochote, na kwamba baadhi yetu wasiwafanye wengine miungu badala ya Mwenyezi Mungu. Lakini wakikengeuka, basi sema: 'Shuhudieni ya kwamba sisi tu Waislamu' (Zurkani).

Huu wito kwenye Islam ulikuwa ni wito kuamini ya kwamba Mungu ni Mmoja na Muhammad[saw] ni Mtume Wake. Pale barua inaposema kwamba ikiwa Herakla atasilimu, atalipwa maradufu, kinachoashiriwa ni huu ukweli kwamba Islam yafundisha kuwaamini wote wawili Yesu na Muhammad[saw].

Yasemekana kwamba ile barua iliyopatiwa Mfalme, baadhi ya maofisa wa baraza la kifalme walipendekeza kwamba ichanwechanwe na kutupiliwa mbali. Wakadai wakisema kwamba barua hiyo ilikuwa ni matusi kwa Mfalme. Haikutaja Mfalme kama Mfalme ila tu kama Sahibur Rum, yaani, Chifu wa Urumi. Lakini, hata hivyo, yule Mfame akasema kwamba haikuwa busara kuipasulia mbali barua ile bila ya kuisoma. Aidha yeye akasema kwamba ile anuani, ya 'Chifu wa Urumi', haikuwa na makosa. Kwani Bwana wa Vyote alikuwa ni Mwenyezi Mungu. Mfalme alikuwa ni Chifu tu.

Mtume[saw] alipoambiwa vile barua yake ilivyopokelewa na Herakla, alionekana mwenye kuridhika na kufurahi na akasema kwamba kwa sababu ya mapokezi yule Mfalme wa Urumi aliyoifanyia barua yake, himaya yake itanusurika. Wazao wa Mfalme kwa muda mrefu wataendelea kushikilia Ufalme ule. Hivyo kwa hakika ndivyo ilivyofanyika. Katika vita vilivyofanyika baadaye, sehemu kubwa ya Milki ya Urumi, kulingana na bishara nyingine ya Mtume wa Islam[saw], ilitwaliwa kutoka usimamizi wa Urumi; lakini hata hivyo kwa muda wa miaka mia sita baadaye, ukoo wa Herakla ulishikilia mamlaka huko Constantina. Ile barua ya Mtume[saw] iliendelea kuhifadhiwa kwenye makabadhi ya Serikali kwa muda mrefu. Mabalozi wa Mfalme wa Kiislamu, Mansur Qalaawuun, walitembelea baraza la kifalme la Urumi, na wakaoneshwa barua hiyo ikiwa imehifadhiwa ndani ya kasha. Akiwaonesha barua hiyo Mfalme wa Urumi alisema kwamba ilikuwa imepokelewa na babu yangu wa kale kutoka kwa Nabii wenu na ilikuwa imehifadhiwa kwa uangalifu.

BARUA KWA MFALME WA IRAN

Barua kwa Mfalme wa Irani ilipelekwa kwa mkono wa Hadhrat Abdullah bin Hudhafa[ra]. Yaliyokuwemo ndani yalikuwa haya:

> Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. Barua hii yatoka kwa Muhammad, Mtume wa Mungu, kwake Kisra, Chifu wa Iran. Yeyote mwenye kukubali mwongozo halisi, na kumwamini Allah, na kushuhudia ya kuwa Allah ni Mmoja, wala hakuna aliye sawa naye au mshirika, na kwamba Muhammad ni Mtumishi Wake na Mtume Wake, basi amani na iwe juu yake. Ewe Mfalme, kwa amri ya Mwenyezi Mungu, mimi nakukaribisha kwenye Islam. Kwani mimi nimetumwa na Mungu kama Mtume Wake kwa wanadamu wote, kusudi niwaonye wote walio hai na niwatimizie Ujumbe wangu makafiri wote. Ikubali Islam na ujilinde dhidi ya maafa yote. Kama utaukataa wito huu, basi madhambi ya ukataaji wa watu wako wote yatakuwa juu yako (Zurqani na Khamis).

Hadhrat Abdullah bin Hudhafa[ra] yuasimulia kwamba alipowasili kwenye baraza la kifalme la Kisra yeye aliomba ruhusa ya kufika mbele ya mfalme. Akaitoa barua kwa Mfalme naye Mfalme akamtaka mkalimani aisome na kuelezea yaliyomo. Baada ya kusikiza ujumbe uliokuwemo, Khosro Kisra alighadhabika. Akainyakua barua ile na kuichana vipandevipande. Hadhrat Abdullah bin Hudhafa[ra] akamripotia Mtume[saw] kisa hiki. Kusikia ripoti hiyo, Mtume[saw] alitamka akisema:

> Vile Khosro alivyoifanyia barua yetu ndivyo Mwenyezi Mungu atakavyoifanyia Milki yake (yaani ataivunjavunja).

Ule mori wa ghadhabu aliouonesha Khosro Kisra katika kisa hiki ulikuwa ni matokeo ya propaganda hatari zilizofanywa dhidi ya Islam na Mayahudi waliokuwa wamehamia Iran kutoka nchi ya Warumi. Mayahudi hawa wakimbizi walikuwa kwenye mstari wa mbele katika njama dhidi ya Urumi zilizopangiwa nchini Iran, na walikuwa, hivyo basi, wametokea kuwa ni wapendelewa katika baraza la kifalme la

Iran. Kisra alipandwa na ghadhabu dhidi ya Mtume[saw]. Zile ripoti kumhusu Mtume[saw] Mayahudi walizokuwa wamezipeleka Iran, zikamwia kana kwamba zimethibitishwa na barua ile. Akamfikiria Mtume[saw] kuwa ni mchokozi mtukutu aliyeimezea mate nchi ya Iran. Punde tu baadaye, akamwandikia Gavana wa Yemen kwamba mmoja wa Makureishi huko Arabuni amejitangaza kuwa yu Mtume. Madai yake yamepita kiasi. Yule Gavana alitakiwa kutuma watu wawili waende wakamtie mbaroni Mkureishi huyu na wamlete kwenye mahakama ya Iran. Badhaan, aliyekuwa Gavana wa Yemen chini ya utawala wa Khosro Kisra, akamtuma mkuu wa kijeshi na mpanda rikabu mwenzake kwenda kwa Mtume[saw]. Pia akwapatia barua iliyoandikiwa Mtume[saw], alimwambia kwamba baada ya kuipokea Mtume[saw] aandamane mara moja na wale wajumbe wawili hadi kwenye baraza la kifalme la Iran. Wale wajumbe wawili wakapanga kwanza waje zao Makka. Njiani karibu na mji wa Taif, wakaambiwa kwamba Mtume[saw] alikuwa akiishi Madina. Hivyo wao wakaenda Madina. Walipowasili Madina huyu mkuu wa kijeshi akamwambia Mtume[saw] kwamba Badhaan, Gavana wa Yemen, alikuwa ametakiwa na Khosro Kisra aandae kutiwa nguvuni kwa Mtume[saw] na kusafirishwa Iran. Ikitokea Mtume[saw] kutotii, basi yeye na watu wake ni sharti waangamizwe na nchi yao kuharibiwa. Kwa kumhurumia Mtume[saw], ujumbe huu wa kutoka Yemen ukasisitiza kwamba yafaa Mtume[saw] awe mtiifu na akubali apelekwe Iran. Baada ya kuyategea sikio maneno haya, Mtume[saw] akashauri kwamba wale wajumbe wamwone tena keshoye. Usiku Mtume[saw] alimwomba Mwenyezi Mungu ambaye alimjulisha kwamba ufidhuli wa Khosro ulikuwa umemletea kifo. "Tumemchochea mwanawe dhidi yake, na huyu mwana atamuulia mbali babake Jumatatu tarehe 10, mwezi wa Jumadal Ula mwaka huu". Sawa na ripoti zingine, wahyi huo ulisema, "Mwana amemulia mbali baba usiku huu huu". Yawezekana kwamba usiku ule ule ndio ulikuwa tarehe 10 ya mwezi wa Jumadal Ula. Asubuhi yake Mtume[saw] aliwaita wale wajumbe wa Yemen na kuwaambia yale aliyoyafunuliwa usiku. Kisha akamtayarishia Badhaan

barua ikisema kwamba Khosro Kisra alikuwa auawe siku fulani ya mwezi fulani. Yule Gavana wa Yemen alipoipata barua ile alitamka akisema, "Ikitokea mtu huyu kuwa Nabii wa kweli, basi hata mambo haya yatakuwa vivyo hivyo. Na kama yeye si Nabii mkweli, basi Mungu Amsaidie yeye na nchi yake. Punde si punde, ilifika merikebu kwenye bandari ya Yemen. Ilileta barua kutoka kwa Mfalme wa Iran kwa Gavana wa Yemen. Ile barua ilikuwa na muhuri mpya ambao kutokana nao yule Gavana alifikia uamuzi kwamba ile bishara ya Nabii wa Arabuni imethibitika. Muhuri mpya uilimaanisha mfalme mpya. Akaifungua ile barua. Ilisema:

> Kutoka kwake Kisra Siroes kwa Badhaan, Gavana wa Yemen. Nimemuulia mbali babangu kwa maana utawala wake ulikuwa umefisidika na ukawa wa dhuluma. Yeye aliwaulia mbali watu bora na kuwatendea ukatili rai zake. Mara tu upatapo barua hii, wakusanye maofisa wote na kuwataka wanihakikishie utiifu wao. Ama kuhusu ile amri ya babangu ya kukamatwa kwa Nabii wa Arabuni, wewe ichukulie hiyo kuwa ni amri iliyobatilishwa (Tabari, J. 3, uk. 1572-1574 na Hisham uk. 46).

Badhaan alivutiwa sana na visa hivi kiasi hiki kwamba yeye na marafiki zake wengi walisilimu mara moja na kumjulisha hivyo Mtume[saw].

BARUA KWA NAJASHI

Barua ya Najash, Mfalme wa Uhabeshi, ilipelekwa na Hadhrat 'Amr bin Umayya Dhamri[ra]. Ilisema hivi:

> Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu Muhammad, Mtume wa Mungu, yuamwandikia Najashi, Mfalme wa Uhabeshi. Ewe Mfalme, amani ya Mungu iwe juu yako. Ninamsifu machoni pako Yule Mmoja Aliye Mungu wa Pekee. Hapana mwingine apasaye kuabudiwa. Yeye ndiye Mfalme wa wafalme, chemchemi ya ubora wote aliyeepukana na kasoro zote, huwapatia utulivu watumishi Wake wote na huwalinda viumbe Wake. Nashuhudia kwamba Yesu mwana wa Mariamu alikuwa Mtume wa Mungu aliyekuja katika kutimizwa

> kwa ahadi alizoahidiwa Mariamu na Mwenyezi Mungu. Mariamu maisha yake alikuwa ameyatoa wakfu kwa Mwenyezi Mungu. Nakualika uungane nami katika kujifungamanisha na Yule Mmoja Aliye ni Mungu wa Pekee na katika kumtii Yeye. Nakualika pia unifuate na kumwamini Yule Mungu ambaye amenituma. Mimi ni Mtume Wake. Nakualika wewe na majeshi yako mwingie Dini ya Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu. Ninatimiza wajibu wangu kwa njia hii. Mimi nimekufikishia Ujumbe wa Mwenyezi Mungu, na kukufafanulia maana ya Ujumbe wenyewe. Mimi nimefanya hivyo kwa moyo mweupe, nami natumai utautilia maanani uaminifu ambao umehamasisha ujumbe huu. Yule mwenye kutii mwongozo wa Mwenyezi Mungu huwa mrithi wa baraka za Mungu (Zurqani).

Barua hii ilipomfikia Najashi, aliifanyia staha na heshima kubwa. Aliishikilia mbele ya macho yake, akashuka chini ya kiti cha enzi na akaagiza liletwe kasha la pembe za ndovu. Kisha aliitia ndani na akatamka akisema, "Barua hii inapokuwa salama, basi ufalme wangu u salama". Vile alivyosema ikatokea kuwa kweli kabisa. Kwa muda wa miaka elfu moja majeshi ya Waislamu yalikuwa mbioni kwenye harakati zao za ushindi. Yalielekea pande zote, na yakapitia pembezoni mwa Uhabeshi katika kila upande, lakini hawakuugusa huu ufalme mdogo wa Najashi; na hii yote ilikuwa ni kwa sababu ya kuheshimu matendo mawili ya kukumbukwa ya Najashi — hifadhi aliyowapatia wakimbizi wa Islam ya awali na staha aliyoifanyia ile barua ya Mtume[saw] Ufalme wa Urumi ulivunjiliwa mbali. Khosro Kisra akapoteza himaya yake. Falme za Uchina na India zilitoweka, lakini huu ufalme mdogo wa Najashi ukabakia bila kuvurugika, kwa kuwa mtawala wake alipokea na kuwalinda wakimbizi wa kwanza Waislamu na kuifanyia staha na heshima barua ya Mitume[saw].

Waislamu wakaulipia kwa njia hii ukarimu wa Najashi. Hebu linganisha haya na vile taifa la Kikristo, katika zama hizi za ustaarabu, lilivyoutendea ufalme huu wa Kikristo wa Najashi. Waliinyeshea mabomu kutoka juu angani miji ya Uhabeshi na kuiharibu kabisa.

Familia ya kifalme ikalazimika kutafuta hifadhi mahali pengine mbali na nchi yao kwa miaka kadha. Taifa lile lile limetendewa kwa njia mbili tofauti na mataifa mawili tofauti. Waislamu waliichukulia Uhabeshi kuwa ni nchi ya kuheshimiwa na ya kutofanyiwa chochoko kwa sababu ya ukarimu wa mmoja wa watawala wake. Taifa la Kikristo likaishambulia na kupora rasilimali zake katika jina la ustaarabu. Malinganisho haya yanaonesha ni jinsi gani athari nzuri za mafundisho ya Mtume[saw] na mfano wake zilivyo za kukolea na kudumu. Shukrani za Waislamu kwa ufalme wa Kikristo zilifanya ufalme ule kuwa wa kuheshimika kwa Waislamu. Ulafi Wa Kikristo ukaushambulia ufalme ule ule, bila kujali ni wa Kikristo.

BARUA KWA MTAWALA WA MISRI

Barua iliyoandikiwa Mukaukas ilipelekwa na Hadhrat Hatib ibn Abi Balta'a. Yaliyoandikwa katika barua hii yalikuwa ni sawa kabisa na yale yalioandikiwa Mfalme wa Urumi. Barua kwa Mfalme wa Urumi ilisema kwamba madhambi ya kukataa kusilimu kwa raia wa Urumi angaliyatwishwa yeye. Barua iliyoandikiwa Mukaukas ilisema kuwa madhambi ya kukataa kusilimu kwa Wamisri atayatwishwa mtawala. llisema hivi:

> Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu. Barua hii yatoka kwake Muhammad, Mtume wa Allah, kwake Mukaukas, Chifu wa Wamisri. Amani na iwe kwa yule mwenye kufuata njia ya uadilifu. Mimi nakualika uukubali Ujumbe wa Islam. Silimu nawe utaokolewa na thawabu zako zitakuwa maradufu. Usipoamini, basi madhambi ya kukataa kusilimu kwa Wamisri nayo pia yatakuwa juu yako. Enyi watu wa Kitabu: Njooni kwenye neno lililo sawa baina yenu na baina yetu, ya kwamba tusimwabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, na kwamba tusimshirikishe na chochote, na kwamba baadhi yetu wasiwafanye wengine miungu badala ya Mwenyezi Mungu. Lakini wakikengeuka, basi sema, "Shuhudieni ya kwamba sisi tu Waislamu (Halabiyya, J. 3, uk. 275).

Hadhrat Hatib[ra] alipofika Misri, hakumkuta Mukaukas kwenye mji mkuu. Hadhrat Hatib[ra] akamfuata hadi mjini Alexandria, alikokuwa akibarizi karibu na bahari. Hadhrat Hatib[ra] alisafiri hadi mjini Alexandria kwa merikebu.

Baraza la kifalme lilikuwa likilindwa sana. Hivyo, Hadhrat Hatib[ra] akaionesha barua ile akiwa mbali kidogo na kuanza kuongea kwa sauti kubwa. Mukaukas akataka Hadhrat Hatib[ra] aletwe kwake. Mukaukas akaisoma ile barua na akasema, "Ikiwa mtu huyu ni Nabii wa kweli, basi mbona haombei maangamizo ya maadui zake?" Hadhrat Hatib[ra] akamjiba akimwambia, "Wewe wamwamini Yesu. Yeye alifanywa vibaya na watu wake, lakini hata hivyo hakuwaombea maangamizo." Yule mfalme akampongeza Hadhrat Hatib[ra] akimwita mwakilishi mwenye busara wa mtu mwenye busara. Alikuwa ameyajibu vizuri maswali aliyoulizwa. Kusikia hivyo, Hadhrat Hatib[ra] akazidi kuongea. Akatamka akisema: Kabla yako palikuweko na mfalme mwenye majivuno, fedhuli na katili. Ndiye yule Firauni aliyemtesa Nabii Musa. Mwishowe alionjeshwa adhabu ya kimbinguni. Kwa hivyo usiwe na majivuno. Amini huyu Nabii wa Mungu. Wallahi Nabii Musa hakumtabiri Yesu kwa uwazi kama vile Yesu alivyomtabiri Muhammad[saw]. Twakuita kwa Muhammad[saw], Mtume wa Mungu, kama vile tu nyinyi Wakristo mnavyowaita Mayahudi kwa Yesu. Kila Nabii anao wafuasi wake. Wafuasi ni sharti wamtii Nabii wao. Kwa kuwa sasa Nabii amedhihiri katika wakati wako, ni jukumu lako kumwamini na kumfuata. Bali kumbuka dini yetu haikutaki wewe umkane au kutomtii Yesu. Dini yetu yamtaka kila mmoja kumwamini Yesu.

Kusikia hivyo, Mukaukas akafumbua kwamba yeye alikuwa amepata fununu ya mafundisho ya Nabii huyu na akaonelea kwamba hakufundisha chochote kibaya wala kukataza chochoe kizuri. Yeye pia alikuwa amachunguza na kugundua kwamba huyu hakuwa mchawi wala mpiga ramli. Alikuwa amezisikia baadhi ya bishara zake zilizokuja kuwa kweli. Kisha akaagizia kasha la pembe za ndovu na kuitia humo ile barua ya Mtume[saw], akaifungia ndani na

kumpatia mjakazi kasha lile liende likahifadhiwe. Halikadhalika akaandika barua kumjibu Mtume[saw]. Yaliyoandikwa humo yamerekodiwa historiani. Yasema hivi:

> Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa Ukarimu. Kutoka kwake Mukaukas, Mfalme wa Wamisri, kwake Muhammad, mwana wa Abdullah. Amani na iwe juu yako. Baada ya hayo, mimi nasema kwamba nimeisoma barua yako na kuyatafakaria yaliyomo na ile imani unayonialikia. Mimi najua kwamba Manabii wa Kiyahudi wametabiri kuja kwa Nabii katika wakati huu wetu. Lakini mimi nilidhani kwamba yeye angelidhihiri nchini Siria. Nimepokea mjumbe wako kwa heshima, na nimetoa kwake zawadi ya dinari elfu moja na majoho matano na nakuleta wasichana wawili wa Kimisri kuwa zawadi kwako. Raia yangu Wamisri wanawaheshimu sana wasichana hawa. Mmoja wao ni Mariamu na yule mwingine ni Siriin. Aidha mimi nakuletea mavazi ishirini yaliyotengenezwa kwa aina bora ya kitani cha Misri. Pia nakuletea baghala[4] mmoja. Nikimaliza, mimi naomba tena ya kwamba uipate amani toka kwa Mwenyezi Mungu (Zurqani na Khamis).

Kutokana na barua hii ni dhahiri kwamba, ingawaje Mukaukas aliifanyia staha barua ile yeye hakusilimu.

BARUA KWA CHIFU WA BAHRAIN

Mtume[saw] pia alimwandikia barua Mundhir Taimii, Chifu wa Bahrain. Barua hii ilipelekwa na Hadhrat 'Alaa ibn Hadhramii[ra]. Maneno yaliyokuwa ndani yake yamepotea. Ilipomfikia Chifu huyu, alisilimu, na akamwandikia Mtume[saw] akisema kwamba yeye na marafiki zake na wafuasi wake wengi wameamua kusilimu. Lakini baadhi yao wameamua kusalia nje. Halikadhalika yeye alisema kwamba wapo Mayahudi na Wamajusi wanaoishi chini yangu. Je, hao ningeliwafanyaje?

[4] Baghala ni mnyama mkubwa anayezaliwa kutokana na mchangyanyiko wa punda na farasi. Pia anaitwa nyumbu.

Mtume[saw] akamwandikia tena Chifu huyu akimwambia hivi:

> Mimi nimefurahia na kusilimu kwako. Wajibu wako ni kuwatii wajumbe na matarishi ambao sina budi kuwaleta kwako. Yeyote mwenye kuwatii yuanitii mimi. Yule tarishi aliyekuletea barua yangu alikusifu kwangu, na akanihakikishia dhati ya imani yako. Mimi nimewaombea Mungu watu wako. Basi, wewe jaribu kuwafundisha nidhamu na desturi za Islam. Zilinde mali zao. Usimruhusu yeyote kuwa na zaidi ya wake wanne. Madhambi yaliyopita yamesamehewa. Maadamu mtu mwema na mwadilifu, utaendlea kuwatawala watu wako. Ama kuwahusu Mayahudi na Ma-majusi, hao wanatakiwa kulipa kodi tu. Hivyo, usifanye madai yoyote mengine juu yao. Na kuwahusu raia kwa jumIa, wale wasiokuwa na ardhi ya kutosheleza mahitaji yao na wapewe kila mmoja dirhamu nne na nguo za kuvaa (Zurqani na Khamis).

Halikadhalika Mtume[saw] alimwandikia Mfalme wa 'Uman, Chifu wa Yamama, Mfalme wa Ghassan, Chifu wa Bani Nahd, kabila la Yemen, Chifu wa Hamdaan, kabila jingine la Yemen, Chifu wa Bani 'Aliim na Chifu wa kabila la Hadhramii. Wengi wao wakasilimu.

Barua hizi zaonesha ni jinsi gani ilivyokuwa thabiti Imani ya Mtume[saw] juu ya Mwenyezi Mungu. Pia, zinaonesha ya kwamba tokea hapo awali Mtume[saw] aliamini kuwa yeye sio kwamba ametumwa na Mwenyezi Mungu kwa taifa lolote moja au nchi moja, bali kwa watu wote duniani. Ni kweli kwamba barua hizi zilipokelewa na wale waliozipelekewa kwa njia mbalimbali. Baadhi yao walisilimu mara moja., Wengine walizifanyia adabu barua zile, lakini hawakusilimu. Wengine walipokea kwa njia ya kawaida tu. Bali wengine walionyesha dharau na majivuno. Lakini ni kweli kabisa na historia ni shahidi ya ukweli wenyewe ya kuwa wapokeaji wa barua hizi au watu wao walifikiwa na hatima kulingana na vile walivyozitendea barua hizi.

KUTEKWA KWA MJI WA KHAIBAR

Kama vile tulivyosema hapo juu, Mayahudi na wapinzani wengine wa Islam sasa walikuwa wakijitahidi kuyachochea makabila dhidi ya

Waislamu. Wao sasa walikuwa na hakika kwamba Arabuni haiwezi kukabiliana na nguvu zinazozidi za Islam na kwamba makabila ya Waarabu hayawezi kuishambulia Madina. Hivyo basi, Mayahudi walianza kula njama na makabila ya Kikristo yaliyoikalia sehemu ya kusini ya mpaka wa Ufalme wa Kirumi. Wakati huo huo walianza kuwaandikia wenzao nchini Iraki dhidi ya Mtume[saw]. Kwa propaganda ya chuki iliyoendeshwa kwa njia ya barua wakataka kumchochea Khosro wa Iran dhidi ya Islam. Kutokana na fitina za Kiyahudi, Khosro akaihasimu Islam, na hata akatoa amri kwa Gavana wa Yemen ya kwenda kumkamata Mtume[saw]. Ilikuwa ni kutokana na kudura maalumu ya kimbinguni na fadhili ya kwamba Mtume[saw] alibakia salama salimini, na plani hatari ya Mfalme wa Irani kupanguliwa. Haina budi kuwa wazi ya kwamba, thama na msaada wa kimbinguni uliomfikia Mtume[saw] katika wadhifa wake wote, jumuiya changa ya Islam ya awali ingelitiwa komesha chini ya uadui na upinzani wa Wafalme wa Urumi na Iran. Wakati Khosro alipoamrisha kukamatwa kwa Mtume[saw] ikatokea kwamba kabla haijatekelezwa amri yenyewe yule Mfalme akapinduliwa na kuuawa na mwanawe na amri yake ya kukamatwa kwa Mtume[saw] ikafutiliwa mbali na mtawala mpya. Wakuu wa kiserikali nchini Yemen walivutiwa sana na muujiza huu; kwa hivyo mkoa wa Yemen bila kusita ukawa ni sehemu ya Miliki ya Kiislamu. Zile njama dhidi ya Waislamu na mji wao Madina, ambazo Mayahudi walizidi kuziendeleza zililazimisha kwamba wao wasukumwe mbali zaidi na mji wa Madina. Kama wangeliachwa waendelee kuishi karibu na Madina zisingelikosa njama zao kusababisha umwagaji damu zaidi na zaidi na hata ghasia. Mtume[saw] aliporejea kutoka Hudaibia, alisubiri miezi mitano na kisha akakata shauri kuwatimulia mbali kutoka Khaibar. Mji wa Khaibar ulikuwa masafa machache tu kutoka Madina na kutoka hapa Mayahudi waliona ni rahisi kuendeleza njama zao. Akiwa na shabaha hii Mtume[saw] (wakati fulani katika mwezi wa Agosti 628 A.D.) akauendea mji wa Khaibar. Aliandamana na watu elfu moja mia sita. Khaibar, kama tulivyosema, ulikuwa ni mji

uliozungushiwa boma madhubuti. Pande zote ulikuwa umezungukwa na majabali ambayo juu yao zilijengwa ngome ndogo ndogo. Kuteka mahali sampuli hii kwa jeshi dogo kama lile, haikuwa kazi rahisi. Vituo vidogo vidogo pembezoni mwa mji wa Khaibar vilitekwa baada ya kupigana kidogo. Lakini pale Mayahudi walipojikusanya kwenye ngome kuu ya mji ule, mashambulio yote dhidi ya ngome ile na aina zote za mbinu za kivita zilizotumiwa zilionekana kana kwamba hazifui dafu. Siku moja Mtume[saw] alilpokea wahyi kwamba mji wa Khaibar utatekwa kwa mkono wa Hadhrat Ali[ra]. Asubuhi yake Mtume[saw] aliwatangazia wafuasi habari hii na akatamka akisema, "Leo, mimi nitaitoa beramu nyeusi ya Islam kwake yule aliye kipenzi cha Mungu, Mtume wake na Waislamu wote. Mwenyezi Mungu amekadiria kwamba ushindi wetu wa Khaibar upatikane kwa mkono wake." Kesho yake akamwita Hadhrat Ali[ra] na kumkabidhi yeye ile beramu. Hadhrat Ali[ra] hakuzubaa. Aliongoza watu wake na kushambulia ile ngome kuu. Licha ya ukweli kwamba Mayahudi walikuwa wamejikusanya wote pamoja ndani ya ngome hii, Hadhrat Ali[ra] aliweza kuiteka kabla ya usiku. Ukasainiwa mkataba wa amani. Masharti yake yalikuwa kwamba Mayahudi wote, wake zao na watoto, wataihama Khaibar na kwenda kuishi mahali pengine pa mbali sana na Madina. Mali zao na virago vyao vichukuliwe na Waislamu. Yeyote yule atakayejaribu kuficha mali zake zozote au akiba yake, au kufanya udanganyifu, hatapatiwa hifadhi ya mkatabu huu. Hatakuwa na budi kulipa ile faini iliyowekwa dhidi ya kuvunja mapatano.

Visa vitatu vya kukumbukwa vilitukia katika kuzingirwa huku kwa Khaibar. Kimoja ni Ishara ya Mwenyezi Mungu na vile viwili ni vielelezo vya tabia bora kabisa ya Mtume[saw].

Mjane wa Kinana, Chifu wa Khaibar, aliolewa na Mtume[saw] Mtume[saw] akauona uso wake ukiwa na alama, kana kwamba ni alama ya kuchapwa kibao. Mtume[saw] akamwuliza akimwambia, "Umefanywa nini usoni, ewe Safiyya?"

Hadhrat Safiyya[ra] akaelezea akisema, "llitokea hivi, mimi niliona

ndotoni mwezi ukiniangukia mapajani. Nikamwambia mume wangu ndoto hii. Hata kabla sijamaliza mume wangu akanichapa dharuba kali ya kibao cha usoni huku akisema, "Wataka kuolewa na Mfalme wa Arabuni" (Hisham). Mwezi ndio uliokuwa ni nembo ya kitaifa ya watu wa Arabuni. Mwezi wa mapajani ilimaanisha hali ya usuhuba wa karibu na Mfalme wa Arabuni. Mwezi uliopasuka au mwezi unaodondoka ulimaanisha vurugu katika ufalme wa Kiarabu au kuangamizwa kwake.

Hii ruya ya Hadhrat Safiyya[ra] ni ishara ya ukweli wa Mtume[saw]. Bali pia ni ishara ya huu ukweli kwamba Mwenyezi Mungu huwafunulia siku za usoni watumishi Wake kwa njia ya ndoto. Uhondo huu waaminio wanao mwingi zaidi kuliko makafiri. Hadhrat Safiyya[ra] alikuwa ni Myahudi alipopata ruya hii. Mumewe alitokea kuuawa kwenye hii patashika ya kuzingiriwa kwa mji wa Khaibar. Patashika yenyewe ilikuwa ni adhabu kwa Wayahudi kwa sababu ya wao kuhalifu mkataba. Safiyya alishikwa mateka, na mateka walipogawanywa yeye akapatiwa Sahaba mmoja. Hapo ikagunduliwa kwamba kumbe yeye ni mjane wa chifu. Hivyo basi, ikaonelewa kwamba ingelingana zaidi na hadhi yake kama ingelikuwa yeye kuishi na Mtume[saw]. Lakini Mtume[saw] akachagua kumwoa, naye akakubali. Kwa njia hii ruya yake ikatimia.

Palikuwa na visa vingine viwili. Kimoja kilihusikana na mchungaji kondoo wa chifu wa Kiyahudi. Mchungaji kondoo huyu alisilimu. Baada ya kusilimu akasema na Mtume[saw] akimwambia, "Ewe Mtume wa Mungu, mimi sasa siwezi kurudi kwa watu wangu. Nifanye nini na hawa kondoo na mbuzi wa mwajiri wangu?"

"Hawa wanyama nyuso zao zielekeze upande wa Khaibar kisha uwasukume. Mwenyezi Mungu atawarejeshea mwenyewe", ndivyo alivyosema Mtume[saw]. Yule mchungaji akafanya kama alivyoambiwa, na wale wanyama wakafika hadi ngomeni kwa Mayahudi. Walinda ngome wakawapokea (Hisham, J. 2, uk. 191). Kisa hiki chaonesha ni kwa dhati kiasi gani Mtume[saw] alivyolichukulia suala la haki za mtu binafsi na ilikuwa muhimu jinsi gani, sawa na maoni yake, kwa

mlinda haki kutimiza wajibu wake. Kwenye vita mali ya washinde kihalali hutekwa na washindi. Hizi zama zetu ni za ustaarabu na utamaduni, lakini je, twaweza kuonesha mfano wowote wa tendo hili la Mtume[saw]. Je, imepata kutokea wakati wowote ambapo aliyefukuziliwa mbali aliacha nyuma mali zake ambazo washindi walizirejeshea wenyewe? Katika hiki kisa cha hivi sasa wale mbuzi walikuwa mali ya mpiganaji wa upande wa maadui. Kurejeshwa kwa wale mbuzi kulikuwa na maana ya kuwarejeshea maadui chakula cha kuwalisha kwa miezi kadha wa kadha. Wakiwa na chakula hiki maadui wangeliweza kupambana kwa muda mrefu dhidi ya ngome yao. Hata hivyo Mtume[saw] aliruhusu wale mbuzi warudishwe, ilimradi amwoneshe yule Mwislamu mpya umuhimu wa kutimiza wajibu.

Kisa cha tatu chahusikana n mwanamke wa Kiyahudi aliyejaribu kumtilia sumu Mtume[saw]. Yeye aliwauliza Masahaba akitaka kujua ni sehemu ipi ya nyama Mtume[saw] aliyopenda sana kula. Akaambiwa kwamba yeye alipendelea sana nyama ya mkono wa mbuzi au kondoo. Yule mwanamke, akachinja mbuzi na kukaanga vipande vya nyama juu ya mawe ya moto. Kisha akavichanganya na sumu kali, hususan vile vipande vilivyokatwa toka nyama ya mkono, akiamini kwamba Mtume[saw] angevipendelea.

Mtume[saw] alikuwa akirejea hemani kwake akiwa amesalisha sala ya magharibi. Akamwona mwanamke huyu akimsubiri karibu na hema lake na akamwulilza akimwambia, "Naweza kukufanyia chochote, bibiye?"

Yule mama akasema, "Naam, Abul Kasim, waweza kuikubali zawadi yangu". Mtume[saw] akamwambia Sahaba mmoja apokee chochote alichokileta yule mama. Mtume[saw] aliketi chini kula chakula alicholetewa na hii zawadi pia ya nyama choma. Mtume[saw] akatia kipande cha nyama mdomoni. Sahaba mmoja Hadhrat Bishr Ibn al-Baraa ibn al-Ma'ruur[ra] naye pia akawahi kipande kimoja. Masahaba wengine waliokuwepo maakulini wakanyoosha mikono wapate kula nyama. Lakini Mtume[saw] akawakataza akisema, yeye yuaona ile nyama

imetiwa sumu. Kusikia hivyo Hadhrat Bishr[ra] akasema kwamba hata yeye alihisi vivyo hivyo. Alitaka kuiitupilia mbali nyama ile lakini akasita akichelea kutomuudhi Mtume[saw]. Akasema "mimi kukuona tu ukila kipande, nami pia nikajilia kipande, lakini mara nikaanza kutamani laiti usingelikila kipande chako asilani." Punde si punde Hadhrat Bishr[ra] alijisikia vibaya na, sawa na baadhi ya ripoti, akafa pale pale. Sawa na ripoti zingine alifariki baada ya kutojiweza kwa muda fulani. Hapo Mtume[saw] akaitiwa yule mwanamke na akamwuliza kama ile nyama alikuwa ameitia sumu. Mwanamke yule akamwuliza Mtume[saw] vile alivyoweza kujua habari hii. Mtume alikuwa na kipande kimoja mkononi mwake, na akatamka akisema, "Mkono wangu uliniambia hayo, akimaanisha kwamba ladha ya nyama ilimjulisha. Mwanamke yule akakiri alichokuwa amekifanya. Mtume[saw] akamwuliza, "ni kitu gani kilichokuchochea kufanya hivyo?" Akijibu, yule mwanamke akasema, "Mlikuwa mkipigana na watu wangu na ndugu zangu wakauawa katika mapigano haya, mimi nikaamua kukutilia sumu, nikiamini kwamba kama ulikuwa mzushi utafilia mbali nasi tuwe salama, lakini kama wewe ulikuwa Nabii, basi Mungu angekunusuru."

Kusikia maneno haya Mtume[saw] akamsamehe yule mwanamke licha ya ukweli kwamba alikuwa amejiletea mwenyewe adhabu ya kifo (Muslim).

NJOZI YA MTUME[SAW] YATIMIA

Katika mwaka wa saba wa Hijra, kwenye mwezi wa Februari 629, Mtume[saw] alitazamia kusafiri Makka kwenda kuizunguka Kaaba. Hili walikuwa wamelikubali viongozi wa Makka. Wakati wa kuondoka Mtume[saw] ulipofika, yeye alikusanya wafuasi elfu mbili na kushika njia kuelekea Makka. Alipofika Marradh-Dhahraan, kituo kilichokuwa karibu na mji wa Makka, akawaamuru wafuasi wake wabwage silaha zao. Hizi zilikusanywa mahali pamoja. Sambamba kabisa na masharti ya yale mapatano yaliyosainiwa kule Hudaibiya, Mtume[saw] na wafuasi wake waliingia ndani ya Uwanja Mtakatifu, wakiwa wamebeba panga

za alani peke yake. Kurejea mjini Makka baada ya kuzuilika nje kwa muda wa miaka saba hakikuwa kitu cha kawaida kwa watu elfu mbili kuingia Makka. Waliyakumbuka mateso waliyokuwa wameteswa katika siku zao mjini Makka. Wakati huo huo, waliona ni kiasi gani Mwenyezi Mungu alivyokuwa mkarimu kwa kuwaacha warejee na kuizunguka Kaaba kwa amani. Hasira zao hazikuwa ila sawa na furaha yao. Watu wa Makka walikuwa Wametoka nje ya majumba yao na kujipachika juu vilimani kuwatazama Waislamu. Waislamu walijawa na jazba na shauku na kuona fahari. Walitaka kuwaambia watu wa Makka ya kwamba zile ahadi Mwenyezi Mungu alizokuwa amewaahidi zote zilikuwa zimetimia. Hadhrat Abdullah bin Rawaha[ra] alianza kuimba nyimbo za vita, lakini Mtume[saw] akamkanya akimwambia "Hakuna nyimbo za vita. Sema tu, Hapana wa kuabudiwa ila Mungu Mmoja. Ni Mwenyezi Mungu aliyemsaidia Mtume[saw] na kuwanyanyua waaminio kutoka udhaifuni hadi heshimani na Ambaye aliwatimulia mbali maadui" (Halabiyya, J. 3, uk. 73).

Baada ya kuizunguka Kaaba na kukimbia baina ya vilima vya Safaa na Marwah, Mtume[saw] na Masahaba wake walikaa mjini Makka siku tatu. Hadhrat Abbas[ra] alikuwa na shemejiye mjane, Hadhrat Maimuna[ra], na akapendekeza kwamba Mtume[saw] amuoe. Mtume[saw] akakubali. Siku ya nne watu wa Makka wakawataka Waislamu waondoke. Mtume[saw] akatoa amri ya kuondoka na akawaambia wafuasi wake kuanza kurejea Madina. Yeye aliyatekeleza mapatano kwa uaminifu na kuwa muaminifu kutambua maoni ya watu wa Makka kwa kiasi hiki kwamba bi-arusi wake mpya alimwacha nyuma mjini Makka. Akampangia kuja kuungana naye akiwa pamoja na kikundi cha ule msafara kilichokuwa kinabeba virago vya wale mahaji. Mtume[saw] akapanda ngamia wake na punde si punde akatoka nje ya eneo takatifu. Njiani Mtume[saw] alipumzika mahali paitwapo Sarif, na hapo ndipo alipoungana tena na mkewe Hadhrat Maimuna[ra].

Tungelitokea kukiachia hiki kisa kidogo nje ya hii historia fupi ya Maisha ya Mtume[saw], lakini kisa hiki kinalo jambo moja muhimu, nalo ndilo hili. Mtume[saw] ameshutumiwa na waandishi wa Ulaya kwa

sababu eti alikuwa na wake wengi. Wao wanafikiria kwamba kuoa wake wengi ni dalili ya uzembe, na kupenda anasa. Lakini maoni haya juu ya ndoa za Mtume[saw] yanasutwa na ule uaminifu na mapenzi ya kupindukia wakeze Mtume waliyokuwa nayo juu yake. Uaminifu na mapenzi yao vilithibitisha kwamba unyumba wa Mtume[saw] ulikuwa safi kabisa, usio na ubinafsi tena wa kiroho. Huu ulikuwa ni unyumba wa kipekee hivi kwamba hapana mtu awezaye kusemekana alikuwa amemtendea mke wake mmoja vizuri kama vile Mtume[saw] alivyowatendea wakeze wengi. Ungelitokea unyumba wa Mtume[saw] kuhamasishwa na anasa, basi bila shaka ungelitokea kuwafanya wakeze kuwa wazembe na hata kumhasimu. Lakini ukweli wenyewe ni kinyume na hayo kabisa. Wake wote wa Mtume[saw] walimpenda sana, na upendo wao ulikuwa ni kwa sababu ya mfano wake wa kujali masilahi ya wengine na unyofu. Kuitikia mfano wake wa kuyajali masilahi ya wengine na unyofu wao walijibu kwa upendo wa kupindukia. Jambo hili lathibitishwa na visa vingi vilivyorekodiwa historiani. Kisa kimoja kinamhusu Hadhrat Maimuna[ra] mwenyewe. Yeye kwa mara ya kwanza kabisa alikutana na Mtume[saw] hemani huko jangwani. Kama uhusiano wao kinyumba ungelikuwa ni ghafi, ingelikuwa Mtume[saw] kuwapendelea wakeze wengine kuliko wenzao kwa sababu ya uzuri wao, basi asingeliweza Hadhrat Maimuna[ra] kukufanya kukutana kwake na Mtume[saw] kwa mara ya kwanza kuwa ni kumbukumbu muhimu ya maishani. Kama ndoa yake na Mtume[saw] ingelitokea kuchanganyikana na kumbukumbu za mambo yenye kuudhi na ya kizembe, basi yeye angelikisahaulia mbali kisa hiki. Hadhrat Maimuna[ra] aliishi sana baada ya kufariki Mtume[saw]. Alifariki katika hali ya uzee lakini hakuweza kusahau ilikuwa imemmaanishia kitu gani ndoa yake na Mtume[saw]. Siku iliyotangulia kifo chake akiwa na umri wa miaka thamanini, zinapokuwa zimesahaulika raha zote za kimwili, ambapo yale tu yenye kuthaminika milele na wema huuvutia moyo, aliusia azikwe mwendo wa siku moja kutoka Makka, mahali pale pale alipokuwa Mtume[saw] amepiga kambi kwenye safari yake ya kurejea Madina, na ambapo baada ya ndoa yake yeye alikuwa

amekutana naye kwa mara ya kwanza. Dunia yajua habari za ndoa nyingi za kweli na bandia, lakini haina habari za ndoa yoyote yenye kuvutia kama hii.

Punde tu haada ya huku kuzungukwa kwa Kaaba kwa kihistoria, majemadari wawili maarufu wa maadui walisilimu. Wakatokea kuwa majemadari mashuhuri wa Islam. Mmoja wao alikuwa ni Hadhrat Khalid bin Walid[ra] ambaye uhodari wake na ushujaa vilitikisisha misingi ya Himaya ya Kirumi na ambaye chini ya ujemadari wake nchi baada ya nchi ilijumlishwa na Waislamu katika himaya yao. Mwingine alikuwa ni Hadhrat 'Amr bin al-Aas[ra] mtekaji wa nchi ya Misri.

VITA VYA MU'TA

Aliporejea kutoka safari ya kwenda kuhiji, Mtume[saw] alipata ripoti ya kuwa makabila ya Kikristo kwenye mpaka wa Siria yakichochewa na Mayahudi na wapagani, yalikuwa yakijiandaa kushambulia Madina. Kwa hiyo, yeye akatuma kikosi cha watu kumi na watano kwenda kujua ukweli wa mambo yalivyokuwa. Waliwaona maadui wakijikusanya kwenye mpaka wa Siria. Badala ya kurejea Madina mara moja na kupiga ripoti wao walikawia. Jazba yao ya kutaka kutangaza Islam ikawachelewesha, lakini matokeo ya nia njema ya jazba yao yakatokea kwenda kinyume kabisa na vile walivyokuwa wakitamani na kutarajia.

Tunapoyachunguza mambo hivi sasa, tunaweza tukaona kwamba wale ambao, chini ya uchochezi wa maadui, walikuwa wakijiandaa kushambulia nchi ya Mtume[saw] hawawezi kutarajiwa watende kivingine. Badala ya kusikiliza yale maelezo juu ya Islam, wao walishika pinde zao na kuanza kukinyeshea mvua ya mishale kikosi cha watu kumi na watano. Hata hivyo, kikosi kile hakikugeuka. Walifumwa mishale kama majibu ya hoja zao, lakini kamwe hawakubanduka. Walisimama kiume watu kumi na watano dhidi ya maelfu, wakafa wakipigana.

Mtume[saw] akapanga msafara wa kwenda kuwaadhibu Wasiria kwa sababu ya huu ukatili wao wa makusudi, lakini wakati huo huo

akapokea habari ya kwamba yale majeshi yaliyokuwa yakijikusanya kwenye mpaka wa Siria yalikuwa yametawanyika. Hivyo basi, yeye akaahirisha mpango wake.

Hata hivyo, Mtume[saw] alimwandikia barua Mfalme wa Urumi (au Chifu wa kabila la Ghassan aliyekuwa akiitawala Busra kwa niaba ya Urumi). Tunaweza tukatazamia, Mtume katika barua hii alilalamikia maandalizi ambayo yalikuwa yameonekana kwenye mpaka wa Siria na yale mauaji ya kinyama yasiyokuwa na sababu ya wale Waislamu kumi na watano aliokuwa amewatuma wende kuleta ripoti ya hali ya mpakani. Barua hii ilipelekwa na Hadhrat al-Harth[ra], Sahaba wa Mtume[saw]. Njiani yeye alisimama huko Mu'ta alikokutana na Shurahbil, Chifu wa kabila la Ghassan aliyekishikilia mamlaka kama ofisa wa Urumi. Huyu chifu akamwuliza Hadhrat al-Harth[ra] akimwambia, "Wewe u mjumbe wa Muhamad?" Alipojibiwa "Naam", akamkamata Hadhrat al-Harth[ra], kumtia kamba na kumpiga hadi akafa. Labda chifu huyu huyu wa kabila la Ghassan ndiye aliyekuwa kiongozi wa lile jeshi lililokuwa limewapiga vita na kuwaulia mbali wale Waislamu kumi na watano waliokuwa wamejaribu kuhubiri. Ukweli kwamba yeye alisema na Hadhrat al-Harth[ra] akimwambia, "Labda unao ujumbe kutoka kwa Muhammad" waonesha kwamba yeye alichelea yasije malalamiko ya Mtume[saw] ya kuwa kabila moja raia wa Kaisari lilikuwa limewashambulia Waislamu yakamfikia Kaisari mwenyewe. Alichelea asije akatakiwa kuelezea kisa kilichokuwa kimetendeka. Akadhani njia salama ililkuwa ni kumuulia mbali mjumbe wa Mtume[saw]. Hakupata aliyoyatarajia. Mtume[saw] alipashwa habari za mauaji haya. Ili kuyalipizia kisasi mauji haya na yale ya hapo awali ya Waislamu kumi na watano, akakusanya jeshi la watu elfu tatu na kulipeleka Siria chini ya uongozi wa Hadhrat Zaid bin Harith[ra], mtumwa mwachiliwa huru wa Mtume[saw], tuliyemtaja katika habari zetu za maisha yake ya Makka. Mtume[saw] akamteua Hadhrat Ja'far ibn Abi Talib[ra] kuwa mwandamizi wa Hadhrat Zaid[ra] endapo Hadhrat Zaid[ra] atauawa, na Hadhrat Abdullah bin Rawaha[ra] kama akiuawa Hadhrat Ja'far[ra]. Akitokea kuuawa Hadhrat 'Abdullah

bin Rawaha[ra] hapo Waislamu na wajichagulie kiongozi wao. Myahudi mmoja aliyesikia matamshi haya ya Mtume[saw] akatamka akisema, "Ewe Abul Kasim, kama wewe u Nabii kweli, basi hawa maofisa uliowataja hawana budi kufa; kwani Mungu hutekeleza kauli ya Nabii." Akigeukia Hadhrat Zaid[ra] akasema, "Mimi nakwambia kama kweli Muhammad ni Nabii, basi wewe hurudi mzima". Hadhrat Zaid[ra] akiwa Mwis1amu halisi, akaajibu akimwambia," Mimi nife nisife, Muhammad[saw] kweli ni Mtume wa Mungu." (Halabiyya, J. 3, uk.75).

Keshoye jeshi la Waislamu likaanza safari yao ndefu. Mtume[saw] pamwe na Masahaba wakalisindikiza masafa kadha. Mbeleni jeshi kubwa muhimu kama hili lilikuwa halijapata kujitokeza bila ya Mtume mwenyewe[saw] kuliongoza. Mtume[saw] alipokuwa akienda kuagana na jeshi lile, alishauriana na kutoa maelekezo. Alipofika mahali ambapo kwa kawaida watu wa Madina huagana na marafiki na jamaa zao wanaokwenda Siria, Mtume[saw] akasimama na kutamka akisema:

> Nawakumbusheni kumwogopa Mwenyezi Mungu na kwatendea haki Waislamu mnaofuatana nao. Endeni vitani kwa jina la Allah na kupigana na maadui nchini Siria ambao ni maadui zenu na maadui za Allah. Mtakapokuwa huku Siria, mtawakuta wale wenye kumkumbuka sana Mwenyezi Mungu katika nyumba zao za ibada. Msiwe na ugomvi nao, wala msiwabughudhie. Katika nchi ya maadui msiwaue wanawake wowote wala watoto, wala vipofu wala wakongwe; msikate mti wowote, wala kubomoa nyumba yoyote (Halabiyya, J. 3).

Baada ya kusema hayo, Mtume[saw] akarudi, na jeshi la Waislamu likasonga mbele. Hili lilikuwa ndilo jeshi la kwanza la Waislamu lililopelekwa kupigana aa Wakristo. Waislamu walipofika kwenye mpaka wa Siria, wakasikia kwamba Kaisari mwenyewe alikuwa kwenye uwanja wa vita akiwa na askari laki moja wake wenyewe na wengine laki moja waliosajiliwa vitani kutoka makabila ya Kikristo ya Arabuni. Wakiwa wamekabiliwa na idadi kubwa kama hiyo ya maadui, Waislamu nusu walitaka kusimama njiani na kumjulisha

Mtume[saw] mjini Madina. Kwani pengine angeliweza kujazilia idadi yao au kutoa maagizo mapya. Viongozi wa kijeshi waliposhauriana, Hadhrat Abdullah bin Rawaha[ra] akasimama huku akipandwa na mori na akatamka akisema "Ndungu zangu, nyinyi mmetoka majumbani mje mfe kama mashahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu, na sasa ambapo ushahidi wenyewe unanukia yaonekana mnasitasita. Hadi hivi leo sisi hatujapata kabisa kupigana kwa kuwa eti tulikuwa na ubora zaidi kuliko majeshi ya maadui zetu katika wapiganaji au silaha. Tegemeo letu kubwa limekuwa ni imani yetu. Adui akitokea kutuzidi mara nyingi kwa idadi na vifaa, hii ina maana gani? Ni sharti tupate zawadi moja baina ya hizi mbili. Ama sisi tushinde au tufe kama mashahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu." Jeshi likamskia Hadhrat Ibn Rawaha[ra] likaathirika sana. Wote wakatamka kwa sauti moja wakisema, "Leo ni Leo". Jeshi likasonga mbele. Walipokuwa wakisonga mbele wakaliona jeshi la Warumi, likiwasogelea. Hivyo basi, huko Mu'ta jeshi la Waislamu lilijipanga na vita vikapamba moto. Punde si punde Hadhrat Zaid[ra], jemadari wa jeshi la Waislamu, akauawa na hapo binamuye Mtume[saw], Hadhrat Ja'far ibn Abi Talib[ra] akashikilia beramu ya uongozi wa jeshi Ia Waislamu. Alipokuta msukumo wa maadui ukizidi kuongezeka huku Waislam, kwa sababu ya nguvu zao haba kabisa, hawakuwa wanafua dafu, alimshuka farasi wake na kumkata miguu. Tendo hili lilimaanisha kwamba kwa akali yeye hatakimbia vita; angependelea kifo kuliko kukimbia.

Mtu kumkata farasi wake miguu ilikuwa ni desturi ya Waarabu ya kuepushia kimbio la ghafla na taharuki. Hadhrat Ja'afar[ra] akakatwa mkono wake wa kuume, lakini yeye akashikilia beramu kwa mkono wa kushoto. Mkono wake wa kushoto nao pia ukakatwa na hapo yeye akashikilia beramu kwa kuikandamiza kifuani mwake kwa vigutu vya mikono yake. Sawa kabisa na ahadi yake akafa akipigana. Hapo Hadhrat Abdullah bin Rawaha[ra], sawa na amri ya Mtume[saw], akaichukua beramu pamwe na uongozi wa jeshi la Waislamu. Naye pia akafa akipigana. Amri ya Mtume[saw] sasa ilikuwa ni kwa Waislamu washauriane na kuchagua jemadari. Lakini hapakuwepo na wakati wa

kufanya uchaguzi; Waislamu wangeweza kujisalimisha kwa ile idadi iliyokuwa kubwa mno ya maadui. Lakini Hadhrat Khalid[ra] bin Walid, akatokea kukubali pendekezo la rafiki yake, akachukua beramu na akaendelea na vita hadi jioni. Keshoye Hadhrat Khalid[ra] akajitokeza tena uwanjani na jeshi lake lililoumizwa na kuchoka sana, lakini yeye akatumia mbinu ya kivita. Yeye aliwabadilishia wanajeshi wake, nafasi zao — wa upande wa mbele wakabadilishana na waliokuwa nyuma na wa kulia wakabadilishana na wa kushoto. Pia wakazua wito wa kutiliana shime. Maadui wakifikiria kwamba Waislamu wameletewa askari zaidi wakati wa usiku wakatimka mbio kwa woga. Hadhrat Khalid[ra] akawaokoa manusura wake na kurejea Madina. Mtume[saw] alikuwa amepashwa habari hizi kwa njia ya wahyi. Yeye akawakusanya Waislamu msikitini. Alipokuwa akisimama kuwahutubia machozi yalikuwa yakimlengalenga. Akatamka akisema:

> Nigependa kuwapasheni habari za lile jeshi lililoondoka hapa kwenda mpakani mwa Siria. Lilikabiliana na maadui na kupambana nao. Zaid alikuwa wa kwanza kushika beramu halafu Ja'far na kisha 'Abdulla bin Rawaha. Wote watatu wakafa wakipigana kishujaa. Waombeeni hao wote. Baada ya hawa beramu ikashikiliwa na Khalid bin Walid. Alijichagua yeye mwenyewe. Yeye ni upanga miongoni mwa panga za Mwenyezi Mungu. Ndipo akaliokoa jeshi la Waislamu na kurejea (Zadul Ma'ad, J. 1, na Zurqani).

Vile Mtume[saw] alivyomwelezea Hadhrat Khalid likatokea kuwa jambo maarufu. Hadhrat Khalid[ra] akatokea kujulikana kuwa 'Upanga wa Mungu'.

Hadhrat Khalid[ra] akiwa ni miongoni wa waliosilimu nyuma, yeye alikuwa mara nyingi akidhihakiwa na Waislamu wengine. Safari moja yeye na Hadhrat Abdur Rahman bin 'Auf[ra] waligombania kitu fulani. Hadhrat Abdur-Rahman[ra] akapeleka mashitaka kwa Mtume[saw] dhidi ya Hadhrat Khalid[ra]. Mtume[saw] akamkaripia Hadhrat Khalid[ra] na akasema, "Khalid, imekuwaje kumuudhi mtu ambaye amekuwa akiihudumia

Islam tangu wakati wa Badr. Mimi nakuambia wewe hata utoe dhahabu ya uzani wa Uhud katika kuihudimia Islam, hutakuwa mwenye kustahili thawabu za kiungu kama vile Abdur-Rahman."

Hadhrat Khalid[ra] akajibu akisema, "Lakini wao wananidhihaki-dhihaki, na ni sharti niwajibu."

Kusikia hivyo Mtume akawageukia wengine na kutamka akisema, "Msimchezee Khalid. Yeye ni upanga miongoni mwa panga za Mungu zinazokaa zikichomolewa dhidi ya makafiri."

Vile Mtume[saw] alivyomwelezea Hadhrat Khalid[ra] ikaja kuwa hivyo hivyo miaka michache baadaye.

Aliporejea Hadhrat Khalid na lile jeshi la Waislamu, ikatokea Waislamu wengine kuwaelezea warejeaji hao kuwa ni washinde wasiokuwa na ari. Lawama yenyewe ilikuwa kwamba ingefaa wote wafe wakipigana. Mtume[saw] akawakaripia wenye kulaumu. Yeye akasema kwamba Khalid na wanajeshi wake hawakuwa washinde au wasiokuwa na ari. Wao walikuwa ni askari waliorudi tena na tena kwenye mashambulio. Kauli hii ilikuwa na undani wake. llimaanisha vita Waislamu watakavyopigana na Siria.

MTUME[SAW] YUAIANDAMA MAKKA NA WAFUASI WAKE ELFU KUMI

Kwenye mwaka wa nane wa Hijra katika mwezi wa Ramadhani (Desemba 629 A.D.) Mtume[saw] alishika njia kwenye ule msafara wa kivita wa mwisho ulioisimika Islam kihalisi nchini Arabuni.

Kule Hudaibiya ilikubaliwa baina ya Waislamu na makafiri ya kwamba makabila ya Waarabu yaruhusiwe kujiunga na makafiri na pia kujiunga na Mtume[saw]. Aidha ilikubaliwa ya kwamba kwa muda wa miaka kumi Waislamu na makafiri hawatapigana isipokuwa kama upande mmoja ukivunja masharti ya mapatano kwa kuushambulia ule mwingine. Chini ya mkatabu huu, kabila Banu Bakr liliungana na watu wa Makka, ambapo watu wa kabila la Khuza'a walifanya maelewano na Waislamu. Makafiri wa Kiarabu hawakuheshimu vilivyo masharti ya mikataba, hususan mikataba na Waislamu.

Ilitokea kwamba makabila ya Banu Bakr na Khuza'a kumbe yalikuwa na mzozo wa kale. Watu wa kabila la Banu Bakr wakashauriana na watu wa Makka juu ya kuwalipiza kisasi watu wa kabila la Khuza'a. Walileta chokochoko wakidai kwamba ulikuwa umesainiwa mkataba wa Hudaibiya. Na kabila la Khuza'a lilijiona kuwa salama salimini kwa sababu ya mkataba wao na Waislamu. Hivyo basi, sasa ndio uliokuwa wakati wa kuwashambulia watu wa kabila la Khuza'a. Watu wa Makka wakakubali. Sawa na njama hii wao na watu wa kabila la Banu Bakr wakashirikiana katika shambulizi la usiku juu ya kabila la Khuza'a na kuwaulia mbali wengi wa watu wao. Watu wa kabila la Khuza'a wakatuma Madina wapanda ngamia wao arubaini kwenda kumripotia Mtume[saw] uvunjaji huu wa mapatano uliofanyiwa. Walivyosema ni kwamba ilikuwa ni juu ya Waislamu kuuendea mji wa Makka kuyalipizia kisasi mashambulio haya. Wale wajumbe wakakutana na Mtume[saw] naye akawaambia kinagaubaga kwamba yeye ameuchukulia msiba huu wao kama msiba wake. Mtume[saw] akawaonesha wingu la mvua lililokuwa linazuka juu angani na akatamka akisema, "Vile mnavyoyaona yale matone ya mvua kule, ndivyo wanajeshi wa Kiislamu watakavyoshuka kuwasaidieni". Watu wa Makka walifadhaishwa na habari za kwenda Madina kwa ujumbe wa kabila la Khuza'a. Upesi wakamtuma Abu Sufyan aende Madina akawazuie Waislamu wasije wakafanya mashambulizi. Abu Sufyan akafika Madina na kuanza kutangaza ubish akisema kwamba kwa vile yeye hakuweko Hudaibiya, ni sharti sasa mkataba mpya ufanywe. Mtume[saw] akafikiria hapakuwa na busara ya kujibu ubishi huu. Abu Sufyan akapandwa na mori, akaenda msikitini na kutangaza akisema:

"Enyi watu, kwa niaba ya watu wa Makka, mimi nawakaririeni tena thibitisho letu la amani" (Zurqani).

Kumbe watu wa Madina hawkuyaelewa haya. Hivyo basi, wao wakajichekea tu. Mtume[saw] akamwambia Abu Suyfan, "Kauli yako ni ya upande mmoja nasi hatuwezi tukakubaliana nayo". Wakati ule ule Mtume[saw] alikuwa ameyapelekea makabila yote ya Waislamu ujumbe. Wakiwa wamemhakikishia kwamba wao walikuwa wamekaa chonjo

na wako njiani, yeye akawataka Waislamu wa Madina kujihami kwa silaha na kujiandaa. Tarehe mosi Januari, jeshi la Waislamu likawa safarini. Mahali mbalimbali njiani, makabila mengine ya Waislamu yakajiunga nao. Ilikuwa imefanyika safari ya siku chache tu, ambapo jeshi hili liliziingia nyanda ya Faran. Idadi yake — sawa kabisa na alivyokuwa Nabii Suleiman[as] ametabiri zamani — sasa ilikuwa imefikia watu elfu kumi. Lilipokuwa jeshi hili likipiga hatua kuisogelea Makka, hali ya shuari iliyosambaa kote kote ilizidi kuwatia kiwewe watu wa Makka. Wakamshawishi Abu Sufyan atoke nje kwa mara ya tena kwenda kuijulia mipango ya Waislamu. Alikuwa amesafari mwendo usiozidi wa siku moja alipoona wakati wa usiku sehemu nzima ya nyanda iking'aa kwa mioto ya kambini. Mtume[saw] alikuwa ameitaka kila kambi iwashe moto. Athari za mioto hii katika utulivu wa giza la usiku zilitisha mno. Abu Sufyan akawauliza wenzake akisema, "Ni mambo gani haya? Kwani limeshuka jeshi kutoka mbinguni? Mimi sijui jeshi lolote la Waarabu kubwa jinsi hii." Wakamtajia makabila fulani, na kwa kila jina Abu Sufyan akakariri akisema, "Hakuna kabila la Waarabu au taifa liwezalo kuwa na jeshi kubwa hivi." Abu Sufyan na marafiki zake walikuwa bado wamepumzika sauti gizani ikisema, "Abu Handhala"! (yaani, Babake Handhala! — Abu Sufyan mwanawe alikuwa akiitwa Handhala)

Abu Sufyan akajibu akisema, "Abbas uko hapa?"

Hadhrat Abbas[ra] akasema "Naam, jeshi la Mtume liko karibu. Fanya haraka au ukabiliwe na fedheha na ushinde."

Hadhrat Abbas[ra] na Abu Sufyan walikuwa ni marafiki wa zamani. Hadhrat Abbas[ra] akamsisitizia Abu Sufyan aende naye juu ya nyumbu mmoja hadi kwa Mtume[saw]. Akamkamata mkono Abu Suyfan, akamvuta na kumpandisha nyumbuni. Akamtoa shoti yule nyumbu na punde si punde wakafika kambini kwa Mtume[saw]. Hadhrat Abbas[ra] alikuwa akichelea asije Hadhrat Umar[ra] aliyekuwa akilinda hema la Mtume[saw] akamtia vifumbani Abu Sufyan na kumuulia mbali. Lakini Mtume[saw] alikuwa amekwisha chukua tahadhari akitangaza kwamba

ikitokea yeyote kumkuta Abu Sufyan, basi na asijaribu kumuua. Mkutano huu ulimvutia sana Abu Sufyan. Alishangazwa na ustawi uliokuwa umeishukia hali ya Islam. Alikuwepo hapa yule Mtume[saw] waliyekuwa wamemfukuzilia mbali watu wa Makka akiwa hana yeyote ila rafiki mmoja tu. Hata miaka saba ilikuwa haijamalizika sawasawa tangu wakati ule, na sasa alikuwa akiibishia hodi milango ya Makka akiwa na wafuasi elfu kumi. Mambo yalikuwa yamebadilika kabisa. Yule Nabii mkimbizi ambaye miaka saba hapo kabla ilimbidi autoke mji wa Makka kwa kuhofia maisha yake, sasa alikuwa amerejea Makka, na Makka haikuthubutu tena kumzuilia.

KUTEKWA KWA MJI WA MAKKA

Abu Sufyan ni sharti awe alikuwa akitafakari kwa ghadhabu. Haya si ni mabadiliko makubwa yaliyotokea katika miaka saba? Na sasa yeye kama kiongozi wa watu wa Makka, atafanya nini? Je, atoe upinzani, au asalimu amri? Akikerwa na mawazo sampuli hii, alionekana mwenye kufadhaika kwa wale waliomtazama. Mtume[saw] alimwona huyu kiongozi mshtuliwa. Akamwambia Hadhrat Abbas[ra] amchukue aende akae naye usiku ule, huku akiahidi kuonana naye keshoye. Abu Sufyan akaenda kulala pamoja na Hadhrat Abbas[ra]. Asubuhi wakafika kwa Mtume[saw]. Ulikuwa ni wakati wa sala ya alfajiri. Ile kukurukakara aliyoishuhudia Abu Sufyan alfajiri vile ilikuwa ni jambo geni mno maishani mwake. Hakuwa amepata kujua — hakuwa na mtu wa Makka aliyekuwa amepata kujua — watu wenye kuamka mapema kama vile Waislamu walivyokuwa wamezoelea chini ya nidhamu ya Islam. Aliwaona Waislamu wote kambini wamejitokeza kwa ajili ya sala yao ya Alfajiri. Wengine walipitapita wakitafuta maji ya kutawadhia, na kupangisha safu waumini tayari kwa sala. Abu Sufyan hakuielewa kukurukakara hii ya alfajiri na mapema. Akashikwa na hofu. Pana plani mpya ya kumtetemesha zaidi, au vipi?

Kwa hofu kubwa akauliza akisema, "Ni mambo gani haya?" Hadhrat: Abbas[ra] akamjibu akimwambia, "Usiwe na wasiwasi, wanajiandaa tu kusali sala ya alifajiri."

Hapo Abu Sufya akaona maelfu ya Waislamu wakipanga safu nyuma

ya Mtume[saw], huku wakitenda kila lililofaradhishwa salani — wakirukuu, kusujudu, na kusimama wima tena, n.k. kufuatia kauli ya Mtume[saw]. Hadhrat Abbas[ra] alikuwa akishika doria, kwa hiyo yeye alikuwa na nafasi ya kuzungumza na Abu Sufyan.

Abu Sufyan akazidi kuuliza akisema, "Wanafanya nini sasa?" Hadhrat Abbas[ra] akamwambia, "Kila kitu anachokifanya Mtume[saw] wote wanakifanya;"

"Ni nini kinachokutia mshawasha? Hii, Abu Sufyan, ni sala tu ya asubuhi. Waislamu wangefanya chochote wakiamrishwa na Mtume[saw] — kuacha kula na kunywa, kwa mfano."

Abu Sufyan akakiri akisema, "Ni kweli kabisa. Mimi nimekuweko kwenye mabaraza makubwa makubwa ya kifalme. Nimeyaona mabaraza ya kifalme ya akina Khosro na Kaisari, lakini mimi sijaona watu wenye kumpenda kiongozi wao kama vile Waislamu wanavyompenda Mtume wao". (Halabiyya, J. 2, uk. 90).

Akiwa amejawa na hofu na hatia, Abu Sufyan aliendelea kumwuliza Hadhrat Abbas[ra] akitaka kujua kama asingelimtafadhalisha Mtume[saw] awasamehe watu wake — akimaanisha watu wa Makka.

Ikawa sala ya alfajiri imemalizika, sasa Hadhrat Abbas[ra] akampeleka Abu Sufyan kwa Mtume[saw]. Akatamka Mtume[saw] kumwambia Abu Sufyan, "Bado hujatambua kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah?"

Abu Sufyan akajibu akisema, "Na watolewe kafara kwako babangu na mamangu. Wewe daima umewahurumia na kuwasaidia nduguzo. Hivi sasa mimi nina hakika kwamba kama angelikuweko mwingine apasaye kuabudiwa, basi tungekuwa tumepatiwa na huyo msaada dhidi yako."

"Pia bado hujatambua kwamba mimi ni Mtume wa Allah?".

Abu Sufyan akasema, "Na watolewe kafara kwako babangu na mamangu, hapa mimi bado nina wasiwasi."

Huku Abu Sufyan akisitasita kumtambua Mtume[saw] kuwa ni Mjumbe wa Mungu, wanzake wawili waliokuwa wamesafiri naye kutoka Makka kuja kuwapelelezea watu wa Makka, walisilimu. Mmoja wao alikuwa ni Hadhrat Hakiim bin Hizaam[ra]. Nyumaye, Abu Sufyan naye pia akasilimu, lakini yaonekana kusilimu kwa ndani ya moyo wake kulikuwa kumeahirishwa hadi baada ya kutekwa kwa mji wa Makka. Hadhrat Hakiim bin Hizaam[ra] akamwuliza Mtume[saw] kama Waislamu watawaangamiza ndugu zao.

Mtume[saw] akajibu akisema, "Watu hawa wamekuwa wakatili mno. Wamefanya uovu wa kupindukia na kujifanya wasioaminika. Wamehalifu mkataba wa Hudaibiyya na kulishambulia kikatili kabila la Khuza'a. Wamemwaga damu mahali palipofanywa patakatifu na Mwenyezi Mungu."

Hadhrat Hakiim[ra] akakubali akisema kwamba watu wetu wamefanya kweli hivyo unavyosema Ewe Mtume wa Mungu, lakini nyinyi badala ya kuuandama mji wa Makka si mngewashambulia watu wa kabila la Hawazin.

Akimjibu, Mtume[saw] alitamka akisema, "Watu wa kabila la Hawazin halikadhalika wamekuwa wakatili na wauaji. Ni matumaini yangu kwamba mwenyezi Mungu ataniwezesha kufikia haya malengo yote matatu: Kutekwa kwa mji wa Makka, ushindi wa Islam na kushindwa kwa kabila la Hawazin".

Abu Sufyan, aliyekuwa ametega sikio, sasa akamwuliza Mtume[saw] akisema, "Wakitokea watu wa Makka kutochomoa panga zao, je, watapata amani?

Mtume[saw] akamjibu, "Naam, kila mmoja ajifungiaye ndani atakuwa salama."

Hapo Hadhrat Abbas[ra] akadukiza akisema, "Lakini, Ewe Mtume wa Mungu, huyu Abu Sufyan yuajihofia yeye mwenyewe binafisi. Yuataka kujua kama cheo chake na hadhi yake miongoni mwa watu wa Makka vitatambuliwa."

Mtume[saw] akatamka akisema, "Barabara: Yeyote atakayejisalimisha nyumbani mwa Abu Sufyan atakuwa salama. Yeyote atakayeingia Msikiti Mtakatifu akuwa salama. Wale watakaoweka silaha zao chini watakuwa salama. Wale watakaofunga milango yao na kubakia ndani watakuwa salama. Wale watakaokaa nyumbani mwa Hakiim bin Hizaam watakuwa salama."

Kusema hivyo, akamwita Hadhrat Abu Ruwaiha[ra] na akamkabidhi beramu ya Islam. Hadhrat Abu Ruwaiha[ra] alikuwa amepangiana udugu na Hadhrat Bilal, Mwafrika[ra]. Alipokipeana ile beramu, Mtume[saw] alitamka akisema, "Yeyote mwenye kusimama chini ya beramu hii atakuwa salama."

Wakati ule ule, akamtaka Hadhrat Bilal[ra] kutangulia mbele ya Hadhrat Ruwaiha[ra] na kuwatangazia wote ya kuwa palikuwepo na usalama chini ya beramu iliyoshikwa na Ruwaiha.

MTUME[SAW] YUAINGIA MAKKA

Mpangilio huu ulijaa hekima. Wakati Waislamu walipoteswa mjini Makka, Hadhrat Bilal[ra], mmoja wa windo lao, alibururwa barabarani kwa kamba alizofungiwa miguuni. Mji wa Makka haukumpatia usalama Hadhrat Bilal[ra], isipokuwa machungu tu, dhila na fedheha. Ni kadri gani ya jazba ya kujilipizia kisasi huenda Hadhrat Bilal[ra] alikuwa nayo katika hii siku ya ukombozi wake. Kumwacha aulipizie kisasi ule ukatili wa kinyama aliouonjeshwa mjini Makka lilikuwa ni jambo la lazima, lakini kisasi chenyewe kitawaliwe na kanuni zilizowekwa na Islam. Sawa na kanuni hizo, Mtume[saw] hakumruhusu Hadhrat Bilal[ra] kuchomoa upanga na kuwaulia mbali watesaji wake wa zamani. Hilo lingekuwa ni kinyume na Islam. Badala yake, Mtume[saw] alimkabidhi nduguye Hadhrat Bilal[ra] beramu ya Islam, na Hadhrat Bilal[ra] mwenyewe kumpatia jukumu la kuwapatia salama na amani watesaji wake wote wa zamani chini ya beramu iliyobebwa na nduguye. Ama kwa hakika, mlikuwemo na uzuri na mvutio katika kisasi hiki. Yatubidi kumtazama kimawazo Hadhrat Bilal[ra] akipiga hatua mbele ya nduguye na akiwatolea maadui zake wito wa usalama

na amani. Hamu yake ya kujilipizia kisasi isingeliweza kukaa. Ni sharti iwe ilitoweka kadri alivyosonga mbele akiwaitia watu wa Makka salama na amani chini ya beramu iliyonyanyuliwa na nduguye.

Pindi Waislamu walipokuwa wakiusogelea mji wa Makka, Mtume[saw] alimtaka Hadhrat Abbas[ra] kumpeleka Abu Sufyan na marafiki zake mahali watakapoweza kulitazama vizuri jeshi la Waislamu, nidhamu yake na sura yake. Hadhrat Abbas[ra] akafanya hivyo na kutoka mahali pazuri Abu Sufyan na wenzake wakayaona yakipita yale makabila ya Waarabu ambayo kwa miaka hii yote watu wa Makka walikuwa wakizitumainia nguvu zao katika chochoko zao dhidi ya Islam. Naam, siku ile wao walisonga mbele sio kama wanajeshi wa ukafiri bali kama wanajeshi wa imani. Sasa walikuwa wakitoa wito wa Islam wala sio wito wa siku zao za upagani. Walikuwa wanapiga hatua kinidhamu, sio kwenda kuyakomesha maisha ya Mtume[saw], bali kwenda kuyatoa maisha yao wenyewe wayanusuru yake; sio kwenda kumwaga damu, bali kumwaga damu yao wao wenyewe kwa ajili yake. Hamu yao siku ile haikuwa kupinga Ujumbe wa Mtume[saw] na kunusuru umoja wa kijuujuu wa watu wao. Nia yao ilkuwa ni kuzifikishia sehemu zote za dunia Ujumbe ule ule ambao hadi kufikia pale walikuwa wameukatalia mbali. Ilikuwa ni kusimika umoja na mshikamano wa wanadamu. Kikosi baada ya kikosi kikapita hadi kabila la Ashja‘ likafika machoni pa Abu Sufyan. Uaminifu wao kwa Islam na jazba yao ya kujitoa mhanga iliweza kuonekana nyusoni mwao, na kusikika katika nyimbo na miito yao.

Akauliza Abu Sufyan akisema, “Hawa ni akina nani?” Akaambiwa, “Hawa ni watu wa kabila la Ashja‘.”

Abu Sufyan akaonekana mwenye kushangaa na akatamka akisema, “Hakukuweko Arabuni nzima waliowazidi hawa kwa chuki dhidi ya Muhammad.” Hadhrat Abbas[ra] akamwambia kwamba kwetu sisi, hii ilikuwa ni fadhili ya Mwenyezi Mungu. Yeye alikuwa akizigeuza roho za maadui wa Islam mara Aonapo inafaa.

Mwisho kabisa akaja Mtume[saw] akizingirwa na vikosi vya Ansar na

Muhajirin. Ni sharti walikuwa takriban watu elfu mbili, wakivalia mavazi ya deraya. Shujaa Hadhrat Umar[ra] alikuwa akiwapigisha hatua. Mandhari hii ikatokea kuwa yenye kuathiri sana zaidi. Uaminifu wa Waislamu hawa, ari yao na jazba yao ilionekana kana kwamba ilikuwa ikifurika. Abu Sufyan alipowaona, akasarenda kabisa.

Akauliza akisema, "Ni akina nani hawa?"

Akajibu Hadhrat Abbas[ra] akimwambia, "Hawa ndio Ansar na Muhajirin wakimzunguka Mtume[saw].

Abu Sufyan akasema, "Hapana nguvu ardhini iwezayo kukabiliana na jeshi hili, na kisha, akimzungumzia hususan Hadhrat Abbas[ra] akatamka akisema, "Wewe Abbas mpwao katokea kuwa mfalme mwenye nguvu zaidi duniani." Hadhrat Abbas[ra] akamjibu akimwambia, "Umekosea sana, Abu Sufyan, yeye si mfalme; yeye ni Mtume, Mjumbe wa Mungu."

Ikawa Abu Sufyan kuropoka akisema, "Naam, naam, na awe hivyo unavyosama, Mtume, sio mfalme."

Lilipokuwa jeshi Ia Waislamu likipiga hatua kupitia alipokuwa Abu Sufyan, jemadari wa Ansar, Hadhrat Sa'd bin 'Ubada akatokea kumwona Abu Sufyan na kutoweza kujizuia kusema kwamba leo Mwenyezi Mungu amewahalalishia kuingia Makka kwa nguvu na kwa Makureishi wangeoneshwa cha mtema kuni.

Mtume[saw] alipokuwa akipita, Abu Sufyan akapaaza sauti yake akisema kumwambia Mtume[saw], "Je, umeruhusu kuangamizwa kwa nduguzo? Mimi nimemsikia jemadari wa Ansar, Sa'd na wenzake wakisema hivyo. Walisema hii ni siku ya mauaji. Utakatifu wa Makka hautazuia damu kumwagika na Makureishi watadhalilishwa. Mtume wa Mungu, wewe ndiwe mbora, msamehevu zaidi, na mwenye huruma kuliko watu wote. Je, hutasamehe na kukisahaulia mbali chochote kilichofanywa na watu wako?"

Kilio cha Abu Sufyan kilisikika. Waislamu wale wale waliozoea kutukanwa na kupigwa katika barabara za mji wa Makka, ambao

walikuwa wamepokonywa na kufukuzwa toka majumba yao, walianza kuwaonea huruma wateasaji wao wa zamani. Ikawa kauli kuwatoka ikisema, "Mtume wa Mungu, habari walizozisikia Ansar za ukatili wa kupindukia tuliofanyiwa na watu wa Makka, zinaweza zikawafanya watake kulipiza kisasi. Hatujui watafanya nini".

Mtume[saw] akaielewa kauli hii. Akimgekia Abu Sufyan alitamka akisema "Alivyosema Sa'd ilikuwa visivyo. Hii siyo siku ya mauaji. Hii ni siku ya msamaha. Makureishi na Kaaba Ataviheshimu Mwenyezi Mungu."

Halafu akamwita Hadhrat Sa'd[ra], na kumtaka kumkabidhi beramu ya Ansar mwanawe, Hadhrat Qais (Hisham, J. 2). Usimamizi wa kikosi cha Ansar ulimtoka Hadhrat Sa'd kwenda kwa Hadhrat Qais[ra]. Ilikuwa ni hatua ya busara. lliwafurahisha watu wa Makka na kuwaepushia Ansar kinyongo. Hadhrat Qais[ra], kijana mnyofu, aliaminiwa sana na Mtume[saw]. Kisa kimoja cha siku zake za mwisho chaonesha unyofu wa tabia yake. Akiwa mahututi kitandani, Hadhrat Qais[ra] aliwaalika kwake marafiki zake. Wengine wakaja na wengine hawakuja. Hili halikumwingia akilini na akataka kujua ni kwa nini baadhi ya marafiki zake hawakuwa wamekuja kumuamkua. Akimjibu, mmoja wao akatamka akimwambia, "Ukarimu wako ni mkubwa, Umekuwa ukiwasaidia wanyonge kwa mikopo yako. Kuna watu wengi mjini wenye madeni yako. Wengine huenda hawakuja wakichelea usije ukawataka wakurudishie mikopo yako".

"Basi nimewafanya mimi kutokuja. Tafadhali tangaza ukisema kwamba sasa hapana mwenye kudaiwa chochote na Qais." Baada ya tangazo hili, Hadhrat Qais[ra] aliamkuliwa na watu wengi katika siku zake za mwisho kiasi hiki kwamba vipandio vya nyumbani kwake vilibomoka.

Jeshi la Waislamu lilipokuwa limekwishapita, Hadhrat Abbas[ra] alimwambia Abu Sufyan kwa haraka afike Makka na kuwatangazia watu wa Makka ya kwamba Mtume amekuja na kuwaelezea vile wote wanavyoweza kupata salama. Abu Sufyan alifika Makka na ujumbe

huu wa amani kwa ajili ya mji wake, lakini mkewe, aliyeitwa Hind, maarufu kwa uhasama wake dhidi ya Waislamu, akakumbana naye. Kafiri mkubwa, lakini hata hivyo alikuwa mwanamke shujaa. Alimshika ndevu Abu Sufyan na kuwaita watu wa Makka waje wamuulie mbali mumewe mwoga. Badala ya kuwahamasisha wanamji wake wajitolee kufa na kupona katika kuhami mji wao, yeye alikuwa akiwaita kwenye usalama na amani.

Abu Sufyan alifahamu kwamba Hind alikuwa akifanya ujinga. Akatamka akimwambia, "Leo sio jana". Rudi nyumbani na ukajifungie ndani. Mimi nimeliona jeshi la Waislamu. Hata Arabuni nzima sasa haiwezi kukabiliana nalo".

Baadaye akawaelezea watu wa Makka masharti ambayo Mtume[saw] alikuwa amewaahidia usalama. Kusikia hivyo watu wa Makka wakakimbilia maeneo yaliyokuwa yametajwa katika tangazo la Mtume[saw]. Kwenye tangazo hili la kupata salama na amani wanaume kumi na mmoja na wanawake wanne walikuwa wameachwa kando. Uhalifu waliokuwa wameufanya ulikuwa mkubwa mno. Kosa lao halikuwa kwamba eti hawakuwa wamesilimu wala kuwa eti walikuwa wameshiriki katika vita dhidi ya Islam; wao walikuwa wamefanya udhalimu ambao haukuweza kusameheka. Hata hivyo ukweli wenyewe ni kwamba watu wanne tu waliuawa.

Mtume[saw] alikuwa amemtaka Hadhrat Khalid bin Walid[ra] kutoruhusu mapigano yoyote isipokuwa kama wakishambuliwa na kama ikitokea watu wa Makka kuwa wa kwanza kuanzisha mashambulio. Ule upande wa mji alikoingilia Hadhrat Khalid[ra] haukuwa umeyasikia yale masharti ya kujipatia salama na amani. Watu wa Makka waliokuweko upande ule wakamtolea mwito Hadhrat Khalid[ra] wakimtaka apigane. Ikazuka patashika ambapo watu kumi na wawili au kumi na watatu waliuawa. (Hisham, J. 2, uk. 217). Hadhrat Khalid[ra] alikuwa ni mtu mkali. Mtu mmoja aliyegutushwa na tukio hili, akafuliza hadi kwa Mtume[saw] na kumwomba amkanye Hadhrat Khailid[ra]. Akizidi kumlalamikia Mtume[saw] yule mtu akasema kwamba ikiwa Khalid

hataacha kupigana, basi watu wote wa Makka huenda wakauawa.

Upesi Mtume[saw] akamwita Hadhrat Khalid[ra] na kumhoji akimwambia, "Mimi sikukataza kupigana?" Akajibu Hadhrat Khalid[ra] akisema, "Naam, umenikataza, Ewe Mtume wa Mungu, lakini jamaa hawa ndio waliozusha vita na kuanza kuturushia mishale. Kwa muda kadha mimi sikuwafanya chochote na niliwajulisha kwamba sisi hatukuwa na haja na vita. Lakini wao hawakujali wala kuacha chokochoko zao. Hivyo basi, mimi nikawajibu na kuwatimua mbio."

Kisa hiki kisichofaa ndicho kilichokuwa cha pekee kutokea wakati huu. Kwa hiyo, kutekwa kwa mji wa Makka kulitekelezwa bila ya umwagaji damu.

Mtume[saw] akaingia Makka. Wakamwuliza angelikotaka kusimama. Akajibu akiwaambia, "Je, 'Aqil amenibakizia nyumba yoyote ya kuishi?" Huyu 'Aqil alikuwa ni binamuye Mtume[saw], mtoto wa amiye. Kwenye miaka ya ukimbizi wa Mtume[saw] Madina, nduguze walikuwa wameziuzilia mbali mali zake zote. Hapakubakia nyumba yoyote ambayo Mtume[saw] angeliiita mali yake. Hivyo basi, Mtume[saw] akatamka akisema, "Mimi nitasimama kule Khaif Banii Kinana." Hapa palikuwa uwanjani. Safari moja watu wa makabila ya Kureish na Kinana walikusanyika pale na wakaapa kwamba isipokuwa watu wa makabila ya Banu Hashim na Banu 'Abdul Muttalib wamsalimishe Mtume[saw] kwao wamfanye watakavyo, basi watayasusia haya makabila mawili. Wasingeliwauzia chochote wala kununua kwao chochote. Ilikuwa ni kutokana na tangazo hili ambapo Mtume[saw], amiye Mzee Abu Talib, familia yake na wafuasi wake, ilibidi wakimbilie katika bonde la Abu Talib na kukabiliwa na hali mbaya ya kutengwa na kususiwa iliyoendelea kwa muda wa miaka mitatu.

Kwa hiyo, pale mahali Mtume[saw] alipopachagua pawe makao yake, palikuwa na undani mwingi. Naam, safari moja watu wa Makka walikuwa wametokea kukusanyana papa hapa na kula kiapo na wakisema kwamba isipokuwa Mtume[saw] asalimishwe kwao, basi wao wasingelikuwa na amani na kabila lake. Sasa Mtume[saw] alikuwa

amejitokeza mahali pale pale. Ilikuwa kana kwamba yeye alikuwa amekuja kuwaambia watu wa Makka: "Hapa ndipo mliponitaka. Sasa mimi nipo hapa. Lakini sio kama vile mlivyotaka. Mlinitaka kama mateka wenu, wa kufanya nami mtakavyo. Lakini hapa mimi niko mamlakani. Sio tu watu wangu, bali Arabuni nzima iko pamoja nami. Mliwataka watu wangu wanisalimishe kwenu. Lakini badala yake wao wamewasalimisheni nyinyi kwangu." Siku hii ya ushindi ilikuwa ni Jumatatu. Siku Mtume[saw] na Hadhrat Abu Bakr[ra] walipoondoka kwenye pango la Thaur wakiwa safarini kwenda Madina nayo pia ilikuwa ni Jumatatu. Siku hiyo, Mtume[saw] akiwa juu ya mlima Thaur, aliutazama mji wa Makka na akatamka akisema, "Ewe Makka! Mimi nakuthamini kuliko mahali penginepo lakini watu wako hawakuniacha nikae hapa."

Mtume[saw] alipoingia Makka, akipanda ngamia wake, Hadhrat Abu Bakr[ra] alifuatana naye akishikilia kikuku cha mnyama yule. Alipokipiga hatua, Hadhrat Abu Bakr[ra] alisoma zile aya za Sura Al-Fat'h ambamo kutekwa kwa mji wa Makka kulikuwa kumetabiriwa miaka mingi hapo kabla.

MASANAMU YAVUNJILIWA MBALI

Mtume[saw] alifululiza moja kwa moja hadi kwenye Kaaba na kuizunguka mahali patakatifu mara saba, akiwa juu ya ngamia wake. Akishika gongo mkononi, sasa akaizunguka ile nyumba iliyokuwa imejengwa na Hadhrat Ibrahim[as] na mwanawe Hadhrat Ismaeli[as] kwa ajili ya ibada ya Mungu Mmoja wa Pekee, lakini ambayo ilikuwa imeachiliwa na wazao wao wapotovu kudunika kiasi cha kuwa ni hifadhi ya masanamu. Moja baada ya jingine, Mtume[saw] akayavunjilia mbali yale masanamu mia tatu na sitini mle ndani ya nyumba. Kila lilipoporomoka chini sanamu moja, ikawa Mtume[saw] kusoma ile aya ya Kurani isemayo "Ukweli umefika na uwongo umetoweka; hakika uwongo ndio wenye kutoweka (Sura Banii Israaiil, 17:82). Aya hii ilifunuliwa kabla Mtume[saw] hajaondoka Makka kwenda Madina na ni sehemu ya Sura Banii Israaiil. Katika Sura hii mlibashiriwa hijra ya Mtume[saw] na kutekwa kwa mji wa Makka. Banii Israaiil ni Sura

iliyoshuka Makka, jambo linalokubaliwa na hata waandishi wa Ulaya. Aya zilizo na bishara ya hijra ya Mtume[saw] kutoka Makka na baadaye kutekwa kwa mji wa Makka zasema hivi:

> Na sema: Mola wangu, ufanye kuingia kwangu kuwe kuingia kuzuri, na kutoka kwangu kuwe kutoka kuzuri. Na utujaalie nguvu kutoka Kwako isaidiayo. Na ukweli umefika na uwongo umetoweka; hakika uwongo ndio wenye kutoweka (Sura Banii Israaiili 17:81-82).

Kutekwa kwa mji wa Makka kwabashiriwa hapa katika sura ya dua aliyofundishwa Mtume[saw]. Mtume[saw] yuafundishwa aombee uingiaji wake wa Makka na utokaji wake uwe mzuri; na aombe msaada wa Mungu katika kuhakikisha ushindi na hatimaye wa ukweli dhidi ya batili. Bishara yenyewe ilikuwa imetimia sawasawa. Kusomwa kwa aya sampuli hii na Hadhrat Abu Bakr[ra] ilikuwa sawa kabisa. Ziliwatilia shime Waislamu, na kuwakumbusha watu wa Makka upuuzi wao mtupu wa kupigana na Mwenyezi Mungu na kuwaonesha ukweli wa ahadi zilizofanywa na Mwenyezi Mungu kwa Mtume[saw].

Mji wa Makka ukiwa umetekwa, sasa Kaaba ikawa kurejeshwa tena kwenye yale matumizi ambayo kwa ajili yake ilikuwa imewekwa wakfu na Hadhrat Ibrahim[as] miaka mingi hapo kabla. Kaaba ikawekwa wakfu tena kwa ajili ya ibada ya Mungu Mmoja wa Pekee! Masanamu yalivunjiliwa mbali. Hubal likiwemo miongoni mwao. Mtume[saw] alipolivunjilia mbali kwa gongo lake, na likaanguka chini likiwa limevunjikavunjika, Hadhrat Zubair[ra] alimtupia jicho Abu Sufyan na huku akijizuia kucheka akamkumbusha kisa cha vita vya Uhud akimwambia, "Wakumbuka ile siku waliposimama Waislamu majeruhi na wachovu nawe ukazidi kuwatonesha kwa kupiga ukelele ukisema, "Atukuzwe Hubal, Atukuzwe Hubal"? Je, ilikuwa ni huyu Hubal aliyewapatieni ushindi siku ile? Kama ilikuwa ni huyu Hubal, basi waweza ukajionea mwisho wake leo."

Abu Sufyan akavutika, na akakiri akisema ni kweli kabisa kwamba kama pangelikuwepo na Mungu minghairi ya Mungu wa

Muhammad[saw], basi pengine wao wangeepushiwa ile fedheha ya ushinde walioonjeshwa siku hii ya leo.

Kisha Mtume[saw] akataka zifutiliwe mbali picha zote zilizokuwa zimechorwa kwenya kuta za Kaaba. Akishasema hivyo Mtume[saw] akasali rakaa mbili za shukrani kwa Mwenyezi Mungu. Kisha akatoka nje uwanjani na akasali rakaa zingine mbili. Kazi ya kuzifutilia mbali picha ilikuwa imepewa Hadhrat Umar[ra]. Alizifutilia mbali picha zote isipokuwa ile ya Hadhrat Ibrahim[as]. Mtume[saw] aliporudi kukagua na kuikuta pale picha hii, alimwuliza Hadhrat Umar[ra] ni kwa nini hakuwa ameifutilia mbali hii nayo. Je, yeye hakukumbuka ushuhuda wa Kurani ya kuwa yeye Ibrahim hakuwa Myahudi wala Mkristo, bali Mwislamu muongofu na mtiifu (Sura Aali-Imraan 3:68).

Ilikuwa ni kuitusi kumbukumbu ya Hadhrat Ibrahim[as], mtangazaji mkubwa wa Umoja wa Mungu, kuwa na picha yake kwenye kuta za Kaaba. Ilikuwa kana kwamba Hadhrat Ibrahim[as] angeliweza kuabudiwa sambamba na Mwenyezi Mungu.

Hii ilikuwa ni siku ya kukumbukwa, siku iliyojawa na Ishara za Mungu. Ahadi zilizofanywa na Mwenyezi Mungu kwa Mtume[saw] wakati ambapo kutimilizwa kwazo lilionekana jambo lisilowezekana, hatimaye zilikuwa zimetimilizwa barabara. Mtume[saw] alikuwa ni changamoto ya uaminifu na imani. Katika dhati yake na kwa njia ya dhati yake, Mwenyezi Mungu alikuwa amejidhihirisha, na kuonesha kama ilivyokuwa, uso Wake kwa mara ya tena. Mtume[saw] akaitisha maji ya Zamzam. Mengine akayanywa na mengine akatawadhia. Waislamu walimpenda sana Mtume[saw], hata haikuwa wao kuliacha tone la maji haya lidondoke ardhini. Waliyakinga maji haya vifumbani mwao na kujipaka miilini; waliyafanya hivyo kwa unyenyekevu mkubwa. Wapagani walioshuhudia matukio haya ya upendo mkubwa walikariri tena na tena wakisema kwamba hawajapata asilan kuona mfalme wa kidunia ambaye watu wake walimpenda jinsi hii (Halabiyya, J. 3, uk. 99).

MTUME[SAW] YUAWASAMEHE MAADUI ZAKE

Wajibu na yaliyowajibika yakiwa yamefanyika, Mtume[saw] aliwahutubia watu wa Makka na akatamka akisema: "Mmeona vile ahadi za Mwenyezi Mungu zilivyotokea kuwa kweli. Hebu sasa niambieni ni adhabu gani mnayopaswa kupewa kwa ule ukatili na uadui mliowafanyia wale ambao kosa lao la pekee ni kwamba wao waliwanasihini kuabudu Mungu Mmoja wa Pekee."

Kujibu kauli hii ya Mtume[saw] watu wa Makka wakatamka wakisema, "Twataraji utatutendea vile Yusufu alivyowatendea nduguze wakosefu."

Ajabu ni kwamba, katika ombi lao la msamaha watu wa Makka walitumia maneno yale yale aliyokuwa ameyatumia Mwenyezi Mungu katika Sura Yusuf, iliyofunuliwa miaka kumi kabla ya kutekwa kwa mji wa Makka. Katika Sura hii Mtume[saw] aliambiwa kwamba angeliwatendea watesaji wake wa Makka kama vile Nabii Yusuf[as] alivyokuwa amewatendea nduguze. Kwa kuomba kwao kwamba watendewe vile Nabii Yusuf[as] alivyokuwa amewatendea nduguze, watu wa Makka walikiri kwamba Mtume wa Islam[saw] alikuwa ni mfano wa Nabii Yusuf[as] na kama vile Nabii Yusuf[as] alivyopewa ushindi juu ya nduguze na Mtume[saw] alikuwa amepewa ushindi dhidi ya watu wa Makka. Kusikia ombi hili la watu wa Makka, Mtume[saw] mara moja akatamka akisema, "Wallahi, leo hamtapatiwa adhabu wala hamna lawama" (Hashim).

Alipokuwa Mtume[saw] akishughulika kumshukuru Mwenyezi Mungu na kufanya ibada zingine kwenye Kaaba, na wakati alipokiwahutubia watu wa Makka akiwatangazia uamuzi wake wa kusahaulia mbali yaliyopita, ilizuka dukuduku miongoni mwa Ansari, Waislamu wa Madina. Baadhi yao hawakupendezwa ilivyokuwa hali ya kurudi nyumbani na ya kuwiana radhi waliyoiona pale. Waislamu wa Makka waliporejea Makka. Je, Mtume[saw] alikuwa akitengana nao, marafiki zake wa zama za dhiki walioipatia Islam makao yake ya awali? Je, sasa Mtume[saw] alikuwa ataishi Makka, mji aliokuwa ameuhama akihofia

maisha yake? Dukuduku sampuli hii haikuonekana kuwa kitu cha kutotazamiwa wakati huu ambapo Makka ilikuwa imetekwa na kabila lake mwenyewe kusilimu. Huenda Mtume[saw] akataka kuishi hapa. Mwenyezi Mungu akamjulisha Mtume[saw] dukuduku hii ya Waislamu wa Madina. Akainua kichwa chake, akwatazama Ansari na kutamka akisema, "Mwaonekana kufikiria kwamba Muhammad ameathirika kwa upendo wa mji wake, na udugu unaomfungamanisha na kabila lake." Ansari wakajibu wakisema, "Naam", hayo tuliyafikiria."

Mtume[saw] akasema, "Je, mwanijua mimi ni nani? Mimi ni Mtumishi wa Mungu na ni Mjumbe Wake. Nawezaje kuachana nanyi? Nyinyi mlishikamana nami, mkayatoa maisha yenu dhabihu wakati Dini ya Mungu ilipokuwa haina usaidizi wa kidunia. Nawezaje kuachana nanyi nikaishi kwengineko? La hasha, Enyi Ansari, hili haliwezekani. Mimi niliutoka mji wa Makka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na siwezi kurudi tena. Mimi nitaishi na kufa nanyi."

Waislamu wa Madina wakachomwa nyoyo na hii kauli ya upendo na uaminifu. Wakasikitikia kutomtegemea kwao Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, wakatirikwa na machozi na kuomba msamaha. Wakaeleza wakisema kwamba wao wasingekuwa na amani yoyote angetokea Mtume[saw] kuuhama mji wao kwenda kuishi kwengineko. Mtume[saw] akawajibu akiwaambia kwamba wasiwasi wao ni wa kueleweka na kwamba baada ya maelezo waliyotoa, Mwenyezi Mungu na Mtume Wake walikuwa wametosheka na usafi wao na wanatambua unyofu wao na utiifu wao.

Watu wa Makka walijifikiriaje wakati huu. Ni kweli wao hawakutiririkwa na machozi ya uaminifu lakini ni sharti nyoyo zao ziwe zilijawa na masikitiko na majuto. Je, hawakuwa wameitupilia mbali kwa mikono yao wenyewe hii johari iliyokuwa imepatikana mjini mwao? Bali wao walikuwa na ziada ya sababu za kulisikitikia hili kwani Mtume, baada ya kuwa amerejea Makka, alikuwa ameamua kuitoka tena na kwenda zake Madina.

IKRIMA YUASILIMU

Miongoni mwa wale waliokuwa wameharamishiwa msamaha, kuna baadhi yao waliosamehewa kufuatana na mapendekezo ya Masahaba. Miongoni mwa wale waliosamehewa kwa njia hii alikuwemo huyu Ikrima, mwana wa Abu Jahl. Mkewe Ikrima moyoni alikuwa ni Mwislamu. Akamlilia Mtume[saw] amsamehe mumewe. Mtume[saw] akamsamehe. Ikrima mwenyewe wakati ule alikuwa akipanga kutorokea Uhabeshi. Mkewe akamfuatilia na akamkuta akikaribia kupanda jahazini. Akamsuta. Akatamka akimwambia, "Je, wamtoroka mtu mpole na raufu kama vile Mtume[saw]?".

Ikrima akapigwa na butaa na akamwuliza kama kweli alimtarajia Mtume[saw] kumsamehe. Mkewe akamhakishia kwamba hata Ikrima mwenyewe angesamehewa na Mtume[saw]. Bali tayari yeye alikuwa ameishapata fununu toka kwake. Ikrima akaupangulia mbali mpango wake wa kutorokea Uhabeshi na kurejea Makka kumwona Mtume[saw]. Akasema kumwambia Mtume[saw], "Nimeambiwa na mke wangu kwamba wewe umesamehe hata mtu kama mimi".

Mtume[saw] akasema, "Mkeo amesema kweli. Mimi nilikusamehe kitambo".

Ikawa Ikrima kuamua kwamba mwenye kuweza kumsamehe adui wake mkubwa jinsi hii hawezi akawa mwongo. Hivyo basi, yeye akaikubali Islam. Akatangaza akisema, "Mimi nashuhudia kwamba Mungu ni Mmoja wala hana mshirika na nashuhudia kwamba wewe u Mtumishi Wake na Mtume Wake." Kusema hivyo, Hadhrat Ikrima[ra] kichwa kikamwinama kwa kuona haya. Mtume[saw] akamfariji. Yeye akatamka akimwambia, "Ikrima, mimi sio kwamba nimekusamehe tu, bali kama thibitisho la vile ninavyokuthamini, nimeamua kukuruhusu uniombe chochote kile ninachoweza kukitoa."

Hadhrat, Ikrima[ra] akajibu akisema, "Hapana cha ziada au kilicho bora cha kukuomba wewe kuliko kukutafadhalisha ya kwamba uniombee msamaha wa Mwenyezi Mungu kwa dhuluma na maovu yoyote yale niliyokufanyia."

Kusikia mataradhio haya, mara moja Mtume[saw] akaomba akisema, "Ee Mwenyezi Mungu, usamehe huu uadui Ikrima aliokuwa nao dhidi yangu. Msamehe yale matusi yaliyomtoka kinywani."

Kisha Mtume[saw] akasimama na akamfunika Hadhrat Ikrima[ra] kashida yake na akatamka akisema, "Yeyote ajaye kwangu, akimwamini Mwenyezi Mungu, tu kitu kimoja. Nyumba yangu ni yake kama ilivyo yangu."

Kusilimu kwa Hadhrat Ikrima[ra] kulitimiza bishara aliyokuwa ameifanya Mtume[saw] miaka mingi hapo kabla. Safari moja Mtume[saw] alipokiwahutubia Masahaba wake alikuwa ametamka akisema, "Mimi niliona njozi ambamo nilijiona nikiwa Peponi. Kule niliona shazi la zabibu. Nilipouliza zabibu zile ni za nani, jamaa mmoja alijibu akisema; 'Ni za Abu Jahl.' Akigusia njozi hii kwenye kisa hiki cha kusilimu kwa Hadhrat Ikrima[ra], Mtume[saw] alisema mwanzoni yeye hakuielewa njozi yenyewe. Itokeeje Abu Jahl, adui wa waaminio, kuingia Peponi na itokeeje shazi la zabibu kuwekewa yeye. Mtume[saw] akasema, "Lakini hivi sasa, njozi yangu naielewa; lile, shazi la zabibu alilitunukiwa Ikrima. Ila tu, badala ya Ikrima mimi nilioneshwa babake, ambacho ni kitu cha kawaida katika njozi na ndoto" (Halabiyya, J. 3, uk. 104).

Miongoni mwa wale waliokuwa wamehukumiwa kukatwa kichwa kwa kuaharamishiwa msamaha wa jumla alikuwemo mtu mmoja aliyekuwa ni msababishi wa kuuawa kinyama kwa Hadhrat Zainab[ra], binti ya Mtume[saw]. Huyu alikuwa ni Habbar. Mtu huyu alikuwa amezikatilia mbali kamba za matandiko ya ngamia wa Hadhrat Zainab[ra] ambapo Hadhrat Zainab[ra] alianguka chini na, kwa vile alikuwa ni mjamzito, mimba ikaharibika. Muda si muda naye pia akaaga dunia. Huu ulikuwa ni mmojawapo wa ukatili aliokuwa ameufanya na ambao kutokana nao yeye alistahili adhabu ya kifo. Mtu huyu sasa akamjia Mtume[saw] na akasema, "Mtume wa Mungu, mimi nilikukimbia na nikaenda Iran, lakini ikanijia fikara ya kuwa Mungu alikuwa ametuondolea mbali imani zetu za kipagani na

kutuokoa dhidi ya kifo cha kiroho. Badala ya mimi kuwaendea watu wengine na kutafuta hifadhi toka kwao kwa nini mimi nisimwendee Mtume mwenyewe, kukiri makosa yangu na kumwomba msamaha?"

Mtume[saw] akamhurumia na akatamka akisema, "Habbar, kama Mwenyezi Mungu kakutilia moyoni mwako mapenzi ya Islam, mimi nawezaje kukataa kukusamehe? Nakusamehe kila ulichofanya hapo kabla."

Hawezi mtu kuelezea kwa marefu na mapana uovu mkubwa waliokuwa wameufanya watu hawa dhidi ya Islam na Waislamu. Hata hivyo, ni kwa upesi kiasi gani Mtume[saw] alivyowasamehe! Moyo huu wa usamehevu uliwageuza maadui wakali sana kuwa wafuasi wa mstari wa mbele wa Mtume[saw].

VITA VYA HUNAIN

Kuingia kwa Mtume[saw] mjini Makka kulikuwa kwa ghafla. Makabila ya pembezoni mwa Makka, hususan upande wake wa kusini, waliendelea kutokuwa na habari za kisa hiki hadi muda fulani baadaye. Walipopata habari zake, walianza kukusanya majeshi yao na kujiandaa kwa vita dhidi ya Waislamu. Hawa walikuwa ni watu wa makabila mawili ya Waarabu, Hawazin na Thakiif, ambao kwa kawaida walijivunia desturi zao za kishujaa. Walishauriana pamoja na baada ya kuambizana wakamchagua Maalik ibn 'Auf kuwa kiongozi wao. Kisha wao wakayaita makabila yaliyowazunguka yaungane nao. Miongoni mwa yale makabila yaliyoitwa walikuwemo watu wa kabila la Banu Sa'd. Hadhrat Halima[ra], mama aliyemnyonyesha Mtume[saw] alitokana na kabila hili na utotoni Mtume[saw] alikuwa ameishi miongoni mwao. Wanaume wa kabila hili walijikusanya katika jeshi na wakajitokeza kuelekea Makka wakichukua familia zao na virago vyao. Walipotakiwa kueleza sababu ya kufanya hivyo, wakajibu wakisema mbinu hii ilikuwa ni kwa sababu ya kuwa askari wawe wataonywa ya kwamba ikiwa watageuka kwa visigino vyao na kutoroka, basi wake zao na watoto wangeshikwa mateka na mali zao kuporwa — uliwawaka kiasi gani mori wao wa kuwapiga vita na kuwaangamiza Waislamu. Jeshi hili

likateremka kwenye bonde la Autaas — mahali bora kabisa pa kupigania vita, penye kivuli cha miti, malisho na maji mengi, na wasaa wa kuwatoa shoti farasi. Mtume[saw] alipopata habari hii, alimtuma Hadhrat Abdullah bin Abi Hadrad[ra] aende kuleta ripoti kamili. Hadhrat Abdullah[ra] akaripoti kwamba sehemu zile kulikuweko na mikusanyiko ya kivita na mori wa kutaka kuua au kuuawa. Kabila hili lilijulikana sana kwa ustadi wao wa kupiga mishale, na pale mahali walipokuwa wamepachagua paliwafaa sana. Mtume[saw] akamwendea Safwan, chifu wa Makka mwenye mali nyingi kwenda kukopa deraya na silaha. Chifu Safwan akajibu akisema, "Yaonekana mwazidi kunishurutisha na kudhania kwamba mimi nitatishiwa na kuzidi kwa nguvu zenu na kuwapatieni chochote mtakacho?"

Mtume[saw] akajibu akimwambia, "Hatuna nia ya kukunyang'anya chochote. Tunachotaka ni kukopesha vitu hivi tu, na tuko tayari kukuwekea mdhamana unaostahili."

Hapo chifu Safwan akaridhika na akakubali kuanzisha vitu walivyotaka. Kwa jumla yeye alitoa deraya mia moja na idadi ifaayo ya silaha. Mtume[saw] akaazima mikuki elfu tatu kutoka kwa binamuye, Naufal bin Harith, na dinari takriban elfu thalathini kutoka kwake Abdullah bin Rabi'a (Muwatta', Musnad na Halabiyya). Jeshi la Waislamu lilipokuwa likielekea Hunain, watu wa Makka walitangaza nia yao ya kutaka kupigana upande wa Waislamu. Wao hawakuwa ni Waislamu lakini walikuwa wamekubali kuishi chini ya serikali ya Kiislamu. Sawa na nia hii yao, watu wa Makka elfu mbili wakajumuika na Waislamu. Njiani, wakafikia mahali pajulikanapo penye mzimu mashuhuri wa Waarabu paitwapo Dhat Anwaat. Hapa palikuwepo na mkunazi wa zamani ambao kwa Waarabu ulikuwa ni mti mtakatifu. Waliponunua zana mpya Waarabu ilikuwa ni desturi yao kwanza kabisa kufika huko Dhat Anwaat kwenda kuzitundika zile silaha juu ya mti ule ili kuzipatia baraka zake. Jeshi la Waislamu lilipopitia kwenye mzimu huu baadhi ya askari wakatamka wakisema, "Mtume wa Mungu, na pawepo na Dhat Anwat kwa ajili yetu sisi pia."

Mtume[saw] akakataa na akasema, "Imekuwa nyinyi kusema chambileche wafuasi wa Musa. Alipokuwa Musa akielekea Kanani, njiani wafuasi wake waliwaona watu waabuduo masanamu, na wakasema, "Ewe Musa, nasi tutengenezee mungu kama vile walivyo na miungu" (Sura Al-A'raaf 7:139).

WITO WA "MTUME WA MUNGU ANAWAITENI"

Mtume[saw] aliwanasihi Waislamu daima wakumbuke kwamba Allah ni Mkubwa na kumwomba Yeye awaepushe na ushirikina wa watu wa awali. Kabla jeshi la Waislamu halijafika Hunain, kumbe wapiganaji wa kabila la Hawazin na washirika wao tayari walikuwa wameandaa mavizio kadha wa kadha ya kuwashambulia Waislamu kama mahandaki ya maoteo na kamafleji ya silaha inavyotumiwa katika vita mamboleo. Vituo hivi walikuwa wamevizunguushia kuta. Nyuma ya zile kuta walijibanza askari kuwaotea Waislamu. Waislamu walibakiziwa bonde jembamba la kupitia baina ya vilima viwili. Sehemu ya Jeshi iliyo kubwa zaidi iliwekwa kwenye vituo hivi vya maoteo, wakati idadi ndogo ya askari ilipangishwa mlolongo mbele ya ngamia wao. Ikatokea Waislamu kuifikiria idadi ya maadui kutokuwa zaidi ya wale askari walioweza kuwaona. Hivyo basi, wao walisonga mbele kushambulia. Walipokuwa wamesonga mbele zaidi na maadui waliojificha kutosheka kwamba sasa wangeweza kushambulika kwa urahisi sana, askari walijipanga mbele ya ngamia na kushambulia sehemu ya katikati ya jeshi la Waislamu wakati washika pinde wao waliponyesha mishale yao kuliani na kushotoni mwa jeshi la Waislamu. Wale jamaa wa Makka, waliokuwa wamejiingiza jeshini kusudi wapate fursa ya kuonyesha ushujaa wao, wakatokea kutoweza kuvumilia huu ushambulizi maradufu. Wakatimka kurudi Makka. Waislamu walikuwa wamezoeleana na hali za kufa na kupona, lakini pale askari elfu mbili wapanda farasi na ngamia walipojipenyeza kwenye jeshi la Waislamu, wanyama wa Waislamu nao pia walishtuka. Ikazuka taharuki katika jeshi lao. Moto wa vita ukawawakia kutoka pande tatu, uliosambaza mauaji. Kwenye tahruki hii, Mtume[saw] peke yake pamwe na Masahaba kumi na wawili

hawakutikisika. Sio kwamba Masahaba wote walikuwa wameukimbia uwanja wa vita. Takriban wenzao mia moja bado walikuweko uwanjani, lakini wao walikuwa mbali kidogo na alipokuwa Mtume[saw]. Masahaba kumi na wawili tu waliendelea kumzunguka Mtume[saw]. Sahaba mmoja yuwasimulia kwamba yeye na marafiki zake walifanya chini juu kuwaelekeza wanyama wao kwenye uwanja wa vita. Lakini wale wanyama walikuwa wameshtushwa na vurugu la wanyama wa watu wa Makka. Hapana jitihada iliyoonekana ikifua dafu. Wakawavuta hatamu zao lakini wanyama wale wakakataa kugeuka. Wakati mwingine wakawa wanavipindua vichwa vya wanyama wale kiasi cha hata kukaribia kugusana na mikia yao. Lakini walipojaribu kuwatoa shoti kuelekea vitani ikawa wanyama wale kukataa kwenda. Badala yake, ikawa wanazidi kurudi nyuma. "Nyoyo zikatuenda mbio kwa kuhofia usalama wa Mtume[saw]", yuwaripoti Sahaba huyu, "lakini hatukuwa na la kufanya" Hivyo ndivyo walivyoadhirika Masahaba wa Mtume[saw]. Mwenyewe Mtume[saw] akawa chonjo na watu wachache, pande tatu akiwa yu peupe kunyeshelezewa mvua ya mishale ya maadui. Ulikuwepo upenyenye mdogo tu nyuma yao ambao watu wachache tu wangeweza kuupitia kwa wakati mmoja. Wakati ule akatokea Hadhrat Abu Bakr[ra] kushuka rikabuni na huku akishikilia hatamu za farasi wa Mtume[saw] akatamka akisema, "Mtume wa Mungu, hebu na tujiondoe kidogo kuliwezesha jeshi la Waislamu lijikusanye tena."

Mtume[saw] akajibu, Abu Bakr[ra], ziache hatamu za farasi wangu." Kusema hivyo, akamtoa shoti farasi wake kwenye ule ujia wa milimani ambao mitemkoni mwake ndimo mlimokuwa na vile vituo vya maoteo washika pinde wa maadui walikokuwa wakivurumishia mishale yao. Huku akimtoa shoti farasi wake, Mtume[saw] alitamka akisema, "Mimi ni Mtume; hii sio uongo. Mimi ni mwana wa Abdul Muttalib" (Bukhari). Maneno haya yaliyotamkwa wakati wa hatari kubwa kwa dhati yake binafsi yana maana kubwa. Yanasisitizia ukweli kwamba Mtume[saw] alikuwa Mtume kweli, Mjumbe hasa wa Mwenyezi Mungu. Kwa kusisitizia ukweli huu, yeye alimaanisha

kwamba hakujali mauti wala kutofaulu kwa wadhifa wake. Lakini kama, licha ya kuzidiwa na washika pinde, yeye alibakia salama salimini, basi Waislamu na wasimvishe sifa zozote za kiungu. Kwani yeye ni mwanadamu tu, mwana wa Abdul Muttalib. Ni jinsi gani Mtume[saw] alivyokuwa mwangalifu daima kuwafafanulia wafuasi wake tofauti baina ya imani na ushirikina. Baada ya kutamka haya maneno ya kukumbukwa, Mtume[saw] akamwita Hadhrat Abbas[ra]. Hadhrat Abbas[ra] alikuwa na sauti kubwa mno. Mtume[saw] akamwambia, "Abbas, paaza sauti yako na uwakumbushe Waislamu kile kiapo walichokula chini ya mti kule Hudaibiya, na kile walichofundishwa wakati wa kufunuliwa kwa Sura Al-Baqara. Waambie, Mtume wa Mungu anakuiteni." Hadhrat Abbas[ra] akapaaza sauti yake kubwa. Wito wa Mtume[saw] ukasikika masikioni mithili ya ngurumo za radi, na hayakuwa masikio viziwi bali masikio yenye shauku kubwa. Ulikuwa na athari ya kushutusha. Masahaba wale wale waliotokea kutokuwa na uwezo wa kuwaelekeza wanyama wao vitani, wakaanza kuhisi kana kwamba hawakuwa tena humu duniani bali huko akhera, wakiwa mbele ya Mwenyezi Mungu katika Siku ya Hukumu. Ile sauti ya Hadhrat Abbas[ra] haikusikika kuwa ni sauti yake bali sauti ya malaika ikiwataka kutoa hesabu ya matendo yao. Basi hapo hapakuwa na chochote cha kuwafanya kutorejea tena kwenye uwanja wa vita. Wengi wao waliwashuka wanyama wao na wakiwa na panga na ngao peke yake na kwa upesi wakarejea vitani, wakiwaacha wanyama wao kwenda watakako. Wengine waliwashuka wanyama wao, wakawakatilia mbali vichwa vyao na kukimbia kwa miguu kumrejelea Mtume[saw] Yasimuliwa kwamba siku hiyo Ansari walimkimbilia Mtume[saw] kwa kasi kama vile ngamia jike au ng'ombe amkimbiliavyo mtotowe baada ya kusikia kilio chake. Muda si muda Mtume[saw] akazungukwa na Masahaba idadi kubwa zaidi wakiwa Ansari. Ikawa adui kushindwa kwa mara ya tena.

Siku hiyo kuwepo kwa Abu Sufyan upande wa Mtume[saw] ilikuwa ni ishara kabambe ya kimbinguni, ilikuwa kwa upande mmoja ishara ya uwezo wa Mwenyezi Mungu na upande mwingine ilikuwa ni ishara

ya mfano wenye kutakasa wa Mtume[saw]. Siku chache tu hapo kabla, huyu Abu Sufyan alikuwa ni adui mwenye kiu ya damu ya Mtume[saw], mkuu wa jeshi katili lililoapa kuwafutilia mbali Waislamu. Lakini hapa, katika siku hii Abu Sufyan yule yule alisimama ubavuni mwa Mtume[saw], akiwa ni rafiki, mfuasi na Sahaba. Ngamia wa maadui waliposhtuka, Abu Sufyan akiwa jemadari mpevu mwenye maarifa, alitambua kwamba huenda farasi wake naye pia akapata mshtuo. Kwa upesi alishuka chini, na huku akishikilia kikuku cha nyumbu wa Mtume[saw] akaanza kutembea kwa miguu. Upanga mkononi, Abu Sufyan alipiga hatua karibu na Mtume[saw] akinuia kutomruhusu yeyote kumkaribia Mtume[saw] isipokuwa kwanza amshambulie yeye mwenyewe na kumuulia mbali. Mtume[saw] akatazama kwa furaha na mshangao kubadilika huku kwa Abu Sufyan.

Akatafakaria huu ushahidi mpya wa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Siku kumi au kumi na tano tu hapo kabla, mtu huyu alikuwa akikusanya jeshi kuiangamizilia mbali Jumuiya ya Islam. Lakini yalikuwa yameingia mabadiliko. Jemadari wa hapo awali wa jeshi la maadui sasa alisimama karibu na Mtume[saw] akiwa kama askari wa kawaida, akishikilia kikuku cha nyumbu wa Bwana wake, huku akiwa tayari kufa kwa ajili yake. Hadhrat Abbas[ra] akatokea kuona mshangao kwenye mtazamo wa Mtume[saw]na akatamka akisema, "Mtume wa Mungu, huyu ndiye Abu Sufyan, mtoto wa amiyo, na hivyo basi, nduguyo. Je, humfurahikii?"

Mtume[saw] akajibu akisema, "Mimi nimejawa na furaha na ninaomba iwe Mwenyezi Mungu atamsamehe makosa yote aliyofanya". Na kisha akimgeukia Abu Sufyan mwenyewe, akasema, "Binamu!" Abu Sufyan hakuweza kustahimili upendo uliokichemka moyoni mwake. Aliinama na kubusu mguu wa Mtume[saw] kwenye kile kikuku cha nyumbu alichokuwa akikishikilia (Halabiyya).

Baada ya vita vya Hunain, Mtume[saw] akazirudisha zile zana za vita alizokuwa amezikopa. Alipokuwa akiwarejeshea zana zao wakopeshaji aliwaongezea sana malipo yao. Wale wakopeshaji wakaathiriwa sana na

uangalifu na huruma Mtume[saw] aliyotokea kuonesha katika kuwarejeshea zana zao na katika kuwalipa wakopeshaji. Wakamchukulia Mtume[saw] kwamba yeye si mtu wa kawaida, bali ni mtu ambaye mfano wake wa kitabia ulikuwa ni wa juu sana kuliko watu wengine. Si ajabu ya kwamba Safwan alisilimu mara moja.

ADUI MKUBWA AWA MFUASI MWAMINIFU

Vita vya Hunain daima vyawakumbusha wanahistoria kisa kingine cha kuvutia kilichotendeka vilipokuwa vimepamba moto. Mkazi mmoja wa Makka kwa jina Shaiba, aliyekuwa pia mtumishi wa Kaaba, alishiriki mle vitani kwenye upande wa maadui. Yeye yuwasema kwamba shabaha yake ilikuwa ni moja tu katika vita hivi — ya kuwa yatakapokuwa yakipambana majeshi haya mawili, atatafuta wasaa wa kumuulia mbali Mtume[saw]. Alikuwa na nia imara kwamba hata kama dunia nzima ikiungana na Mtume (achilia mbali Arabuni nzima), yeye angekaa chonjo na kuendelea kupinga Islam. Vita vilipozidi kupamba moto, Shaiba alichomoa upanga wake na kuanza kumsogelea Mtume[saw]. Alipozidi kumsogelea, akawa mwoga. Ari yake ikaanza kulainika. Shaiba yuwasema, "Nilipokuwa karibu sana na Mtume[saw], mimi nikawa kana kwamba naona mwali wa moto ukitishia kuniteketeza. Hapo nikasikia sauti ya Mtume[saw] ikisema, "Shaiba, njoo karibu nami". Nilipomkaribia, Mtume[saw] alipitisha mkono wake kifuani mwangu kwa mapenzi makubwa. Alipokuwa akifanya hivyo yeye akawa akisema, "Mwenyezi Mungu, mwondolee Shaiba mawazo yote ya kishetani." Kwa athari ya kuguswa vile Shaiba akabadilika kabisa. Chuki na uadui wake vikatoweka, na tangu wakati ule Shaiba alimpenda Mtume[saw] kuliko kinginecho duniani. Shaiba alipokibadilika, Mtume[saw] alimtaka ajitokeze kupigana vitani. Yuwasema Hadhrat Shaiba[ra], "Wakati ule mimi nilikuwa na shabaha moja tu, nayo ilikuwa ni kufa kwa ajili ya Mtume[saw]. Hata babangu kama angenijia mbele yangu, nisingelisita hata mara moja kumchoma upanga wa kifua (Halabiyya).

Kisha Mtume[saw] akauendea mji wa Taif, uliompiga mawe na kumfukuzilia mbali. Mtume[saw] akauzingira mji ule, lakini kwa kukubali ushauri wa baadhi ya rafikize akaacha kuuzingira. Nyumaye, watu wa Taif wote walisilimu.

MTUME[SAW] YUWAGAWA MATEKA

Baada ya kutekwa kwa mji wa Makka na ushindi wa vita Hunain, Mtume[saw] alikabiliwa na kazi ya ugawaji wa pesa na mali zilizotolewa kama fidia au zilizoachwa vitani na maadui. Kama ingelikuwa imefuatwa desturi, basi pesa na mali hizi ingelibidi kugawiwa askari Waislamu walioshiriki katika vita vile. Lakini katika kisa hiki, badala ya kuigawa miongoni mwa Waislamu, Mtume[saw] aliigawa miongoni mwa watu wa Makka na wale walioishi pembezoni mwake. Watu hawa walikuwa bado hawajaonesha maelekeo kwenye Imani. Wengi walikuwa ni wakataaji sugu. Wale waliokuwa wametangaza imani yao bado walikuwa wachanga humo. Hawakujua ni jinsi gani watu wawezavyo kuwa ni wenye kujinyima baada ya kuwa wao wameikubali Islam. Lakini, badala ya kunufaika na ile hali ya kujinyima na kujitolea waliyoiona, badala ya kuwatendea wengine wema kama vile walivyotendewa na Waislamu, wao walizidi kuwa akina tamaa-mbele na walafi kupindukia. Tamaa zao zikaanza kuchemka. Wakamzingira Mtume[saw] na kumsukuma hadi chini ya mti huku kashida yake ikiwa imepasuliwa kuanzia mabegani. Mwishowe Mtume[saw] akaiambia halaiki ile ya watu akisema, "Mimi sina kingine cha kuwapeni. Kama ningelikuwa nacho, basi ningeliwapeni. Mimi si bahili wala mchoyo." (Bukhari, mlango wa Faraduhl-Khums).

Kisha baada ya kwenda kwenye ngamia wake na kumchopoa usinga mmoja, akaiambia halaiki ya watu, "Kutoka kwa pesa na mali hizi mimi sitaki chochote kile, hata kidogo kama usinga huu. Ila tu, ni sharti nipate sehemu ya tano, na hiyo ni kwa ajli ya Utawala. Hilo ndilo fungu ambalo daima desturi za Waarabu zimelikubali kuwa ni haki na sawa. Sehemu hiyo ya tano haitatumiwa kwangu mimi. Itatumiwa kwenu nyinyi na mahitaji yenu. Kumbukeni ya kwamba

mwenye kunyakua au kutumia vibaya mali ya umma, atakuja kudhalilishwa machoni pa Mwenyezi Mungu Siku ya Hukumu".

Imedaiwa na wadadisi wenye husuda ya kwamba Mtume[saw] alitamani kuwa mfalme na kuwa na himaya. Lakini hebu mpige picha akizingirwa na halaiki ya watu walafi, huku yeye tayari akiwa ni mfalme. Kama alikuwa ametamani kuwa mfalme na kuwa na himaya, je, kweli yeye angeliweza kulitendea genge omba-omba kama vile alivyolitendea hili genge la watu wa Makka? Je, kweli yeye angeruhusu kuzingirwa kwa vyovyote vile? Je, angetoa hoja na kutoa maelezo? Ni Mitume tu na Wajumbe wa Mwenyezi Mungu wawezao kutoa mfano sampuli hiyo. Mateko yote, pesa, na vitu vya maana vya kugawanywa vilivyokuwepo vilikuwa vimeshagawanywa miongoni mwa wanaostahili na maskini. Lakini hata hivyo walikuwepo wale waliokuwa bado kuridhika, waliomzingira Mtume[saw], wakilalamikia ugawaji na kudai Mtume[saw] hakutenda haki.

Mmoja wao, kwa jina Dhul Khuwaisira, alimsogelea Mtume[saw] na akatamka akisema, "Muhammad, mimi nakiona unachokifanya."

Mtume[saw] akmwuliza, "Nami nafanya nini?"

Akatamka yule mtu akisema, "Wewe wafanya dhuluma."

Mtume[saw] akamjibu akimwambia, "Ole wako. Kama mimi naweza kufanya dhuluma, basi hapana yeyote juu ya uso wa ardhi awezaye kuwa mwadilifu". (Muslim, Kitabuz Zakaat).

Waaminio halisi walikasirika sana. Mtu huyu alipojiendea zake baadhi yao wakasema, "Huyu yuwastahili kuuawa. Utaturuhusu tukamuulie mbali?"

Mtume[saw] akjibu akiwaambia, "La hasha." Kama yeye atashika sheria zetu na kutofanya makosa ya dhahiri, twawezaje kumuulia mbali?"

Walioamini wakasema, "Lakini kama mtu akisema na kufanya kitu kimoja kumbe yuwaamini na kutamani kitu kingine kabisa, asingestahili kutendewa vivyo hivyo?"

"Mimi siwezi nikawatendea watu sawa na yaliyomo nyoyoni mwao. Mwenyezi Mungu hakunipatia jukumu hili. Ninaweza nikawatendea sawa na wanavyotamka na kutenda."

Mtume[saw] akaendelea kuwaambia waaminio kwamba siku moja mtu huyu na wenzake kama yeye wangezusha maasi katika Islam. Kauli hii ya Mtume ilitokea kuwa kweli. Kwenye wakati wa Hadhrat Ali[ra], Khalifa wa Nne wa Islam, mtu huyu na marafiki zake waliongoza maasi dhidi yake na akatokea kuwa kiongozi wa kundi mlaaniwa katika Islam, akina Khawarij.

Baada ya kuwanyamazisha watu wa kabila la Hawazin, Mtume[saw] alirejea Madina. Ikawa tena sikukuu kwa watu wa Madina. Siku nyingine kuu ilikuwa pale Mtume[saw] alipowasili Madina akiwa mkimbizi kutokana na dhuluma za watu wa Makka. Katika sikukuu hii, Mtume[saw] aliingia tena Madina, akijawa na furaha na akijua kabisa dhamira yake na ahadi ya kuifanya Madina makao yake.

NJAMA ZA ABU 'AAMIR

Sasa hatuna budi kugeukia njama za mtu mmoja kwa jina Abu 'Aamir Madanii. Yeye alikuwa ni mtu wa kabila la Khazraj. Kutokana na kuzoeleana kwa muda mrefu na Mayahudi na Wakristo alikuwa na tabia ya kutafakari kimya kimya na kukariri majina ya Mwenyezi Mungu. Kwa sababu ya hii tabia yake, kwa kawaida alijulikana kama Abu 'Aamir, Mpweke. Hata hivyo, yeye kidini hakuwa Mkristo. Mtume[saw] alipokwenda Madina baada ya Hijra, huyu Abu 'Aamir alitoroka Madina kwenda Makka. Pale hatimaye ambapo Makka nayo pia ilisalimu athari inayoongezeka ya Islam, yeye alianza kuandaa njama mpya dhidi ya Islam. Yeye aligeuza jina lake na mazoea ya kivazi chake na akaenda kukaa huko Qubaa, kijiji kilichokuwa karibu na Madina. Yeye alikuwa amekaa mbali kwa muda mrefu na kubadilika sura na mavazi yake, watu wa Madina hawakumtambua. Walimtambua wanafiki wale tu ambao kisiri alikuwa na uhusiano nao. Yeye aliwatilia maanani sana wanafiki wa Madina na kwa kupatana nao akapanga kwenda Siria kuitaharukisha na kuwachochea

watawala wa Kikristo na Waarabu Wakristo waishambulie Madina. Alipokuwa akishughulikia harakati zake hatari huko upande wa kaskazini, yeye alikuwa ameandaa kuzagazwa chuki mjini Madina. Wenzake, wale wanafiki, walikuwa waeneze uvumi kwamba Madina ilikuwa yaja kushambuliwa na majeshi ya Siria. Kama matokeo ya njama hizi za pande mbili Abu 'Aamir alitumainia kwamba Waislamu na Wakristo wa Siria wangepambana katika vita. Endapo njama hizi zake hazikufaulu, yeye aliwatarajia Waislamu wenyewe wangepandwa na mori wa kuishambulia Siria. Hata kwa njia hii vita vingetokea baina ya Waislamu na Siria ambapo Abu 'Aamir angelipata kitu cha kusherehekea. Kumaliza tu mipango yake, akaelekea Siria. Alipokuwa hayuko wanafiki mjini Madina — sawa na plani yao — walianza kueneza uvumi ya kwamba misafara ilikuwa imeonekana iliyokuwa ikija kushambulia Madina. Ilipokosa kuonekana misafara, wao walitoa udhuru huu au ule.

MSAFARA WA KIJESHI KWENDA TABUK

Uvumi huu ukazidi kuvuma kiasi hiki kwamba Mtume[saw] aliona yafaa aongoze yeye mwenyewe jeshi la Waislamu dhidi ya Siria. Huu ulikuwa ni wakati mgumu. Arabuni ilikuwa imekumbwa na njaa kubwa. Mavuno ya mwaka jana yalikuwa machache na palikuwepo na uhaba wa nafaka na matunda. Musimu wa mavuno mapya ulikuwa haujafika. Ilikuwa ni kwenye mwisho wa mwezi wa Septemba au mwanzoni mwa mwezi wa Oktoba alipokwenda Mtume[saw] katika safari hii. Wanafiki walifahamu kwamba uvumi wenyewe ulikuwa ni vituko vyao. Pia walifahamu kwamba shabaha yao ilikuwa ni kuwachochea Waislamu washambulie Wasiria endapo Wasiria hawatawashambulia Waislamu. Katika haya yote mawili, kupambana na himaya kubwa ya Kirumi kulikuwa kuishilizie na kuangamizwa kwa Waislamu. Kisa cha Mu'ta kilikuwa mbele ya macho yao. Huko Mu'ta Waislamu iliwabidi wakabiliane na jeshi kubwa hivi kwamba ilikuwa ni kwa dhiki kubwa kwamba wao walifanikiwa kulirudisha nyuma. Wanafiki walitarajia kuzusha vita vya pili vya Mu'ta ambamo Mtume mwenyewe[saw] pengine angepoteza maisha yake. Walipokuwa

wanafiki wakishughulika na kueneza uvumi juu ya shambulio la Wasiria dhidi ya Waislamu, wao pia walifanya chini juu kuwahofisha Waislamu. Eti wangeweza Wasiria kukusanya jeshi kubwa mno wasiloweza Waislamu kukabiliana nalo. Wao hivyo wakawanasihi Waislamu eti wasishiriki kwenye mzozo huu na Siria. Plani yao ilikuwa, kwa upande mmoja, kuwachochea Waislamu waishambulie Siria, na kwa upande mwingine kuwavunja moyo wasijitokeze kwa wingi. Walitaka Waislamu wapigane vita na Wasiria na bila shaka kuonjeshwa ushinde. Lakini mara tu baada ya Mtume[saw] kutangaza nia yake ya kuongoza msafara huu, shauku ilichemka miongoni mwa Waislamu. Walijitokeza wakiwa wamejitoa dhabihu kwa ajili ya dini yao. Waislamu hawakuwa na zana kwa ajili ya vita vikubwa jinsi hii. Hazina yao ilikuwa tupu. Ni wale Waislamu matajiri zaidi tu ndio waliokuwa na uwezo wa kugharamia vita vile. Mwislamu huyu na yule wakashindana katika moyo wa kujitolea kwa ajili ya dini yao. Yasemekana kwamba wakati msafara ulipokuwa maandalizini na Mtume[saw] kuitisha pesa, Hadhrat Uthman[ra] alitoa sehemu iliyo kubwa zaidi ya utajiri wake. Mchango wake wasemekana kuwa uliofikia takriban dinari za dhahabu elfu moja, zilizo sawa na takriban rupia elfu ishirini na tano. Waislamu wengine nao pia walitoa michango sawa na uwezo wao. Waislamu maskini nao pia wakapewa wanyama wa kusafiria, panga na mikuki. Jazba ikashika kasi. Mlikuwemo mjini Madina wakati ule kikundi cha Waislamu waliokuwa wamehama kutoka Yemen. Hawa walikuwa ni maskini hohehahe. Baadhi yao walifika kwa Mtume[saw] na wakajitolea kwa ajili ya msafara huu. Wakasema, "Ewe Mtume wa Mungu, tuchukue pamoja nawe. Hatuhitaji cha zaidi ya vifaa vya kusafiria." Kurani yawazungumzia Waislamu hawa na toleo lao kwa maneno yafuatayo:

> Wala (si kosa) juu ya wale waliokufikia ili uwapandishe (juu ya wanyama), ukasema: Sina cha kuwapandisheni juu yake; wakarudi hali macho yao yanachuruzika machozi kwa huzuni ya kukosa kupata cha kutoa (Sura At-Tauba 9:92)

Ndio kusema kwamba hawana lawama waliokosa kushiriki kwenye

vile vita kwa kuwa hawakuwa na viwezesho na ambao walitaradhia kwa Mtume[saw] awapatie njia ya kusafiria vitani. Mtume[saw] hakuweza kuwapatia usafiri, hivyo wao wakajiendea zao kwa huzuni wakijiona maskini, na hawakuweza kuchangia vita baina ya Waislamu na Wasiria. Hadhrat Abu Musa[ra] alikuwa ndiye kiongozi wa kundi hili. Alipotakiwa kusema kile walichotaradhia, yeye alijibu akisema, "Sisi hatukutaka ngamia wala farasi. Tulisema tu ya kuwa hatukuwa na viatu na tusingeliweza kumaliza safari hii ndefu miguu mitupu. Laiti tungelikuwa na viatu, basi sisi tungelikwenda kwa miguu na kushiriki kwenye vita tukiwa bega kwa bega na ndugu zetu Waislamu." Kwa kuwa jeshi hili lilikuwa likienda Siria na Waislamu bado walikuwa hawajasahau vile walivyodhikika kule Mu'ta, kila Mwislamu ulimjaa wasiwasi kwa kohofia usalama wa Mtume[saw]. Akina mama wa Madina walitimiza wajibu wao. Waliwahamasisha waume zao na watoto wao kushiriki vitani. Sahaba mmoja aliyekuwa ameenda nje ya Madina alirejea alipokuwa Mtume[saw] tayari ameondoka pamoja na jeshi. Huyu Sahaba aliingia nyumbani mwake na alikuwa akimtarajia mkewe kumsalimia kwa ile shauku ya mwanamke anayekutana na mumewe baada ya muda mrefu. Alimkuta mkewe ameketi uani na akamkaribia amkumbatie na kumbusu. Lakini mkewe akamnyooshea mikono yake na kumsukuma nyuma. Yule mume aliyeshangaa akamtazama mkewe na akatamka akisema, "Haya ndiyo makaribisho kwa yule arejeaye nyumbani baada ya muda mrefu?"

Mkewe akamjibu akisema, "Wewe huoni haya? Mtume wa Mungu atokee kwenda misafara hatari, nawe uwe ukijiburudisha na mkeo? Wajibu wako tangulizi ni kwenda kwenye uwanja wa vita. Yaliyobaki ni juu yetu."

Yasemekana kwamba yule Sahaba alichomoka nje ya nyumba yake mara moja, akakaza kanda za kufungia matandiko ya mnyama wake na akafukuzia kumfuata Mtume[saw]. Kwenye mwendo wa takriban siku tatu akalifikia jeshi la Waislamu. Makafiri na wanafiki huenda walifikiria kwamba kwa kufuatilia uvumi, waliouzusha na kuueneza, Mtume[saw] angeliyarukia majeshi ya Syria bila kujali. Walisahau kwamba Mtume[saw] alizingatia kuviwekea mfano vizazi na vizazi vya wafuasi

wake wa siku zote zijazo. Mtume[saw] alipokaribia Siria, alipiga kambi na akatuma watu wake pande mbalimbali wakalete ripoti za vile mambo yalivyokuwa. Wale watu wakarejea na kuripoti kwamba hakukuweko na mikusanyiko ya majeshi ya Wasiria kokote kule. Mtume[saw] akaamua kurudi alikotoka, lakini akakaa kwa siku kadha wakati ambapo alifanya mapatano na baadhi ya makabila ya mpakani. Hapakuwepo na vita wala mapigano. Safari hii ilimchukua Mtume[saw] takriban miezi miwili u nusu. Walipogundua wanafiki wa Madina kwamba njama zao za kuchochea vita baina ya Waislamu na Wasiria hazikufua dafu na kwamba Mtume[saw] alikuwa akirejea nyumbani salama salimuni, wakahofia kwamba sasa uchochezi wao ulikuwa umejulikana. Waliogopa adhabu ambayo ilikuwa imehakiki juu yao. Lakini hawakusitisha plani zao mbaya. Walilishikisha kundi moja silaha na kuliweka kwenye pande mbili za ujia mwembamba maili kadha kutoka Madina. Ujia huu ulikuwa mwembamba kiasi hiki kwamba watu wangeliweza tu kuupitia wakiandamana katika mlolongo. Mtume[saw] na jeshi la Waislamu lilipopakaribia mahali hapa alitahadharishwa kwa njia ya wahyi kwamba maadui wanamuotea panda zote mbili za ujia ule. Mtume[saw] akawaamrisha Masahaba wake wapeleleze. Walipofika mahali pale wakawaona watu wakijimbanza kuvizia kwa shabaha ya kushambulia. Lakini watu hawa hata hivyo, walitimka mbio mara tu walipowaona wale wapelelezi. Mtume[saw] akaamua kutowakimbiza. Mtume[saw] alipofika Madina, wale wanafiki waliokuwa wamejiondoa kwenye vita hivi walianza kutoa udhuru wao wa kirongorongo. Lakini, Mtume[saw] akawakubalia. Wakati huo huo akaonelea kwamba unafiki wao yafaa uwekwe peupe. Akapata amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu ya kuwa ule msikiti wa Qubaa, ambao wanafiki walikuwa wameujenga kusudi waweze kukutania humo kisiri, yafaa ubomolewe mbali. Ikawa wanafiki kulazimika kusali pamoja na Waislamu wengine. Haikutolewa adhabu nyingine.

Kurejea kutoka Tabuk, Mtume[saw] akakuta kwamba watu wa Taif nao pia walikuwa wamesilimu. Baada ya hayo makabila mengine ya Arabuni yalitaka kusilimu. Muda si muda Arabuni nzima ikawa chini ya beramu ya Islam.

HIJA YA MWISHO

Kwenye mwaka wa tisa wa Hijra, Mtume[saw] alienda kuhiji Makka. Siku ya Hija hii, alipokea wahyi mlimokuwa na ile aya mashuhuri inayosema:

> Leo Nimewakamilishieni dini yenu, na kuwatimizieni neema Yangu, na Nimewapendeleeni Islam iwe dini yenu (Sura Al-Maaida 5:4).

Kimaana hasa aya hii ilisema kwamba ule Ujumbe Mtume[saw] aliokuwa ameuleta kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ambao kwa kauli na matendo yeye alikuwa akiuelezea kwa miaka hii yote, ulikuwa umekamilishwa. Kila sehemu ya Ujumbe huu ilikuwa ni baraka. Ujumbe ambao sasa ulikuwa umekamilishwa ulikuwa na zile baraka za juu zaidi alizoweza mwanadamu kupokea kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Ujumbe wenyewe umefupishiwa katika jina 'al-Islam', limaanishalo kujisalimisha. Kujisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu) ndiko kulikokuwa kuwe ndio dini ya Waislamu, dini ya wanadamu. Mtume[saw] alisoma aya hii katika bonde la Muzdalifa, mahujaji walimokuwa wamekusanyikia. Alipokuwa akirejea kutoka Muzdalifa, Mtume[saw] alisimama huko Minaa. Ilikuwa ni siku ya kumi na moja ya mwezi wa Dhulihija. Mtume[saw] alisimama mbele ya halaiki kubwa ya Waislamu na akatoa hotuba, isifikayo historiani kama hotuba ya kwaheri ya Mtume[saw]. Alipokihutubu Mtume[saw] alitamka akisema:

> Jamani, nisikilizeni kwa makini. Kwani mimi sijui kama nitasimama tena mbele yenu katika bonde hili na kuwahutubieni jinsi ninavyowahutubieni hivi sasa. Maisha yenu na mali zenu Mwenyezi Mungu amevinusurisha na mashambulio ya nyinyi kwa nyinyi hadi Siku ya Hukumu. Mwenyezi Mungu amemkatia kila mmoja fungu katika mirathi. Sasa hapana 'wasia' utakaokubalika unaokwenda kinyume na haki za mrithi halisi. Mtoto mwenye kuzaliwa katika nyumba yoyote atahesabiwa kuwa ni mtoto wa yule baba katika nyumba ile. Yeyote mwenye kupinga nasaba ya mtoto huyu atastahili adhabu chini ya Sheria

ya Islam. Yeyote mwenye kumnasibishia kuzaliwa kwake baba wa mtu mwingine, au kudai kimakosa mtu fulani kuwa ndiye babake, basi Mwenyezi Mungu, malaika Wake na wanadamu wote watamlaani.

Jamani, nyinyi mnazo haki kadha dhidi ya wake zenu; lakini wake zenu nao pia wanazo haki kadha dhidi yenu. Haki zenu dhidi yao ni kwamba wao waishi maisha ya kitawa, na kutoshika mienendo ambayo huenda ikamletea mumewe aibu mbele za watu wake. Endapo wake zenu hawatayazingatia haya, basi mnayo haki ya kuwaadhibu. Mnaweza mkawaadhibu baada ya kufanywa uchunguzi kabambe na walinda-sheria wastahiki, na haki yenu ya kuwaadhibu kuthibitika. Hata hivyo, adhabu katika kisa sampuli hii ni sharti isiwe kali. Lakini kama wake zenu wasipofanya mambo kama haya, na tabia yao si ya kuweza kuwaletea wanaume zao aibu, basi wajibu wenu ni kuwapatia chakula, nguo na nyumba, sawa na kiwango cha maisha yenu. Kumbukeni ni sharti kuwatendea vizuri wake zenu. Mwenyezi Mungu amewapeni jukumu la kuwatunza. Mwanamke ni dhaifu na hawezi kujilindia haki zake. Pale mlipooa, Mwenyezi Mungu aliwafanyeni wadhamini wa haki zile. Mliwaleta wake zenu makwenu chini ya Sheria ya Mwenyezi Mungu. Msiudhihaki, hivyo basi ule mdhamana ambao Mwenyezi Mungu amewakabidhini.

Jamani, nyinyi bado mko nao wafungwa kadha wa kivita. Hivyo basi, nawanasihini mwalishe na kuwavisha kwa njia na mtindo ule ule mnaokula na kujivisha nyinyi wenyewe. Wakikosea kitu chochote msichoweza kukisamehe, basi wahamishieni kwa mtu mwingine. Wao ni sehemu ya viumbe vya Mwenyezi Mungu. Kuwaonjesha maumivu au misukosuko haiwezi ikawa sawa asilan.

Jamani, ninachowaambieni, ni sharti mkisikie na kukikumbuka. Waislamu wote ni kama ndugu wao kwa wao. Nyinyi nyote mko sawa. Watu, hata wawe wametokana na taifa au kabila gani, na hata wawe na cheo gani maishani, wote wako sawa.

Alipokuwa akisema hivyo, Mtume[saw] aliinua mikono yake na kuviweka pamoja vidole vya mkono huu na huu na kisha akasema:

> Kama vile vilivyo sawa vidole vya mikono hii miwili, ndivyo kila mwanadamu alivyo sawa na mwingine. Hapana yeyote mwenye haki yoyote, ubora wowote wa kudai juu ya wengine. Nyinyi ni kama ndugu.

Akiendelea Mtume[saw] alitamka akisema:

> Je, mwajua huu ni mwezi gani? Ni nchi gani tulimo? Ni siku gani ya mwaka hivi leo?

Waislamu wakajibu wakisema, 'Twajua ni mwezi mtakatifu, nchi takatifu na siku ya Hajj.'

Hapo Mtume[saw] akasema:

> Kama vile mwezi huu ulivyo mtakatifu, iheshimikavyo nchi hii, na ilivyo takatifu siku hii, ndivyo ambvyo Mwenyezi Mungu amevifanya vitakatifu maisha, mali na heshima ya kila mtu. Kuangamiza maisha ya mtu au kutwaa mali yake, au kupaka heshima yake matope, ni dhuluma na makosa kama vile kuvuruga utakatifu wa siku hii, mwezi huu na nchi hii. Kile ninachowaamrisheni hivi leo hakikusudiwi kuwa ni cha leo tu. Chakusudiwa kuwa cha daima dawamu. Mwatarajiwa kukikumbuka na kukitimiza hadi mtakapoitoka dunia hii kwenda ile dunia nyingine kukutana na Muumba wenu.

Akimalizia alisema:

> Kile nilichowaambieni, kienezeni pembe zote za dunia. Huenda wale ambao hawakunisikia kikawanufaisha zaidi kuliko wale walionisikia (Sihah Sitta, Tabari, Hisham na Khamiis).

Hotuba ya Mtume[saw] ni muhtasari wa mafundisho yote na kiini kizima cha Islam. Yaonesha ni kwa undani kiasi gani alivyoyajali masilahi ya mwanadamu na amani ya dunia; na pia uzito wa ghera aliyokuwa nayo kwa ajili ya haki za wanawake na zile za viumbe

wengine walio wanyonge. Mtume[saw] alijua kifo chake kilikaribia. Alikuwa amepata ishara kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuhusu kifo chake. Miongoni mwa mambo aliyoyajali na yaliyomtia wasiwasi aliyoyaangazia ilikuwa ni hadhari na wasiwasi wake kuhusu wanawake watendewavyo na wanaume. Alichukua tahadhari ya kuwa asije yeye kuitoka dunia hii kwenda ile nyingine bila ya kuwahakikishia wanawake ile hadhi iliyokuwa ni haki yao. Tangu kuzaliwa kwa mwanadamu, wanawake walikuwa wahesabiwa kuwa ni watumishi wa wanaume. Hili ni moja alilojali Mtume[saw]. Jingine alilolijali lilikuwa ni suala la wafungwa wa kivita. Walichukuliwa visivyo na kutendewa kama watumwa na walitendewa ukatili na uovu wa kila aina. Mtume[saw] alionelea kwamba yeye asiitoke dunia hii bila ya kuwahakikishia wafungwa wa kivita zile haki zilizokuwa ni zao machoni pa Mwenyezi Mungu. Hali ya kukosekana kwa usawa baina ya mtu na mtu mwingine pia ilimchoma moyo Mtume[saw]. Mara kwa mara tofauti zilizingatiwa kwa kiasi kisichovumilika. Baadhi ya watu walitukuzwa na wengine kudunishwa. Zile hali zilizosababisha tofauti hii zilikuwa ni hali zilizosababisha uadui na vita baina ya taifa na taifa na baina ya nchi na nchi. Mtume[saw] alizifikiria shida hizi pia. Isipokuwa shime ya hizi tofauti iuliwe mbali na zile hali zilizowashawishi watu kujinyakulia haki za watu wengine na kupiga vita maisha na mali zao — isipokuwa hali hizi ambazo huwa zinazagaa sana nyakati za ufasiki ziondolewe mbali — amani na maendeleo ya dunia visingeliweza kuwa na uhakika. Yeye alifundisha kwamba maisha ya mwanadamu na mali vina utakatifu ule ule unaoambatana na siku takatifu, miezi mitakatifu na pahali patakatifu. Hapana kabisa mtu aliyewajibikia na kutilia maanani masilahi ya wanawake, haki za wanyonge, na kujali amani kati ya mataifa kama alivyofanya Mtume wa Islam[saw]. Hapana kabisa mtu aliyeshughulika kama vile alivyoshughulika Mtume[saw] kujenga usawa miongoni mwa wanadamu. Hapana kabisa mtu aliyehuzunikia masilahi ya mwanadamu kama vile alivyoyahuzunikia Mtume[saw]. Haliwi tena jambo la kutotazamiwa, kwamba Islam yatambua haki za wanawake

kumiliki na kurithi mali. Mataifa ya Ulaya hayakuiwazia haki hii hadi miaka elfu moja na mia tatu baada ya ujaji wa Islam. Kila mtu mwenye kusilimu anakuwa sawa na mwinginewe, hata kama jamii anayotokana nayo iwe ni duni kiasi gani. Uhuru na usawa ndio mchango wa aina yake kabisa wa Islam katika utamaduni wa dunia hii. Zile picha dini zingine zilizonazo za hili wazo la uhuru na usawa zimeachwa nyuma kabisa ya zile Islam inazozihubiri na kuzionesha kwa matendo. Ndani ya msikiti wa Waislamu, mfalme, kiongozi wa dini na mtu wa kawaida wana vyeo sawa; hapana tofauti kati yao. Kwenye mahali pa ibada pa dini zingine na mataifa mengine ziko tofauti hizi hadi hivi leo ingawaje dini hizo zimefanya mengi kuliko Islam kwa ajili ya uhuru na usawa.

MTUME[SAW] YUWADOKEZEA KIFO CHAKE

Njiani, Mtume[saw] aliwaambia tena Masahaba wake habari za kuwadia kwa kifo chake. Alitamka akisema, "Jamani, mimi ni kama nyinyi tu. Unaweza ukanifikia 'Wito' siku yoyote na ninaweza nikajiendea zangu. Bwana wangu Mwenye Huruma na Mkaa Chonjo amenifahamisha kwamba Nabii huishi hadi kufikia nusu ya miaka ya yule Nabii aliyemtangulia.[5] Nadhani hivi karibuni nitapokea Wito nami nitajiendea zangu. Enyi Masahaba wangu, sitakuwa na budi kwenda kumjibu Mwenyezi Mungu, na nyinyi pia hamtakuwa na budi kwenda kumjibu. Basi mtakwenda kumwambiaje?"Kusikia hivyo Masahaba wakasema, "Sisi tutasema kwamba Uliufikisha vyema Ujumbe wa Islam na ukajitolea maisha yako mazima kuihudumia Dini. Wewe ulikuwa na roho iliyohalisika zaidi kwa ajili ya masilahi ya mwanadamu. Basi sisi tutasema: Allah, mpe malipo bora zaidi."

Hapo Mtume[saw] akauliza akisema, "Je, mwashuhudia kwamba Mungu ni Mmoja, kwamba Muhammad ni Mtumishi Wake na Mtume Wake,

[5] Hii haikuwa ni kanuni ya kawaida. Bali ilimhusu Mtume[saw] tu. Hadithi yautaja umri wa Yesu kuwa miaka mia na ishirini. Kwa kuwa Mtume tayari alikuwa na umri wa miaka sitini na mitatu, basi alifikiria kwamba kifo chake kilikuwa karibu — Edita.

kwamba pepo na Jahanamu ni kweli, kwamba mauti ni hakika, kwamba upo uhai baada ya kifo, kwamba Siku ya Hukumu ni sharti ije, na kwamba wafu wote siku moja watafufuliwa toka makaburini mwao, kuhuishwa na kukusanywa?"

Masahaba wakajibu wakisema, "Naam". "Twaushuhudia ukweli huu wote."

Akimgeukia Mwenyezi Mungu, Mtume[saw] akatamka akisema, "Nawe pia kuwa Shahidi wa haya — ya kuwa nimewaelezea Islam".

Baada ya Hija hii, Mtume[saw] akawa na kazi nyingi akiwafundisha na kuwazoeza wafuasi wake, kujaribu kunawirisha hali ya tabia zao na kunidhamisha na kutakasa mienendo yao. Kifo chake yeye mwenyewe kikawa jambo la kuzungumziwa mara kwa mara na akawaandaa Waislamu kwa ajili yake.

Siku moja, alipokiinuka kuwahutubia Waaminio, alitamka akisema, "Leo mimi nimepokea huu wahyi unaosema:

> Utakapofika msaada wa Mwenyezi Mungu na ushindi, na utawaona watu wakiingia dini ya Mwenyezi Mungu makundi makundi, basi mtukuze Mola wako kwa sifa njema, na umwombe ghofira; hakika Yeye ndiye apokeaye sana toba (Sura An-Nasr 110: 2-4).

Yaani, ulikuwa unakuja wakati ambapo, kwa msaada wa Mungu, makundi kwa makundi ya watu watakuja kuingia katika dini ya Islam. Hivyo basi, ilikuwa ije itukie kuwa ni wajibu wa Mtume[saw] — na wafuasi wake — kumtukuza Mwenyezi Mungu na kumwomba Yeye aondelee mbali vizingiti vyote katika njia ya kuiweka imara Dini.

Safari hii Mtume[saw] alitumia mithali akisema: Mweneyzi Mungu alimwambia mtu mmoja, "Ukipenda, waweza ukarejea Kwangu, au waweza ukaendelea kidogo kuinidhamisha dunia. Yule mtu akasema ningependelea kurejea kwa Mola wangu.".

Hadhrat Abu Bakr[ra] alikuwa miongoni mwa waliomsikiliza. Yeye alikuwa ameisikiliza hii hotuba ya mwisho ya Mtume[saw], kwa shauku

na mahangaiko — shauku ya muumini mkubwa na mahangaiko ya rafiki na mfuasi aliyeweza kuona katika hotuba hii ishara za kifo cha Mtume[saw]. Alipoisikia ile methali, Hadhrat Abu Bakr[ra] hakuweza tena kujizuia. Aliangua kilio. Masahaba wengine, ambao walikuwa wameyachukulia kijuujuu yale waliyokuwa wakiyasikiliza, walishangaa pale Hadhrat Abu Bakr[ra] alipoangua kilio. Wakasema wakimwuliza, umefanywa nini Abu Bakr. Mtume[saw] alikuwa akigusia ushindi unaokuja wa Islam, alihali wewe umetokwa na machozi. Hususan Hadhrat Umar[ra] alitokea kuchukizwa mno na hali ya Hadhrat Abu Bakr[ra]. Mtume[saw] alikuwa akitoa habari njema, lakini mzee huyu yupo kilioni. Lakini, Mtume[saw] peke yake alielewa kilichokuwa kikitendeka. Kwake yeye, ilikuwa ni Hadhrat Abu Bakr aliyekuwa amemuelewa kisawa. Ilikuwa ni Hadhrat Abu Bakr[ra] peke yake aliyekuwa ameng'amua kwamba zile aya zilizoahidi ushindi pia ziliashiria kuwadia kwa kifo cha Mtume[saw].

Mtume[saw] akaendelea kutamka akisema, "Nampenda Abu Bakr. Kama ingalijuzu kumpenda yeyote minghairi ya Mwenyezi Mungu kwa upendo usio na mipaka, ningalimpenda Abu Bakr kwa upendo kama huo. Enyi watu wangu, milango yote inayotazamana na msikiti na ifungwe kuanzia hivi leo isipokuwa mlango wa Abu Bakr."

Hapakuwa na tashwishi yoyote kwamba agizo hili la mwisho liliashiria bishara ya kwamba baada ya Mtume[saw] Hadhrat Abu Bakr[ra] angekuwa Kalifa wa Kwanza. Ili kuwaongoza waaminio katika sala ingelikuwa yeye kuja msikitini mara tano kila siku na, kwa sababu hii, ingekuwa yeye kuacha wazi mlango wa nyumba yake wenye kukabiliana na msikiti. Miaka mingi baadaye, Hadhrat Umar[ra] alipokuwa ni Khalifa, yeye aliwauliza baadhi ya waliokuwepo maana ya ile aya "Utakapofika msaada wa Mwenyeai Mungu na ushindi". Bila shaka yeye aliikumbuka ile hali ambamo Mtume[saw] aliwafundisha Waislamu aya hii na zile zinazofuatia. Ni sharti awe pia alikuwa amekumbuka kwamba alikuwa ni Hadhrat Abu Bakr peke yake aliyeelewa maana ya aya hizi. Hadhrat Umar[ra] alikuwa akiutahini ujuzi wa Waislamu wa aya hizi. Wao Hawakuweza

kuzielewa wakati zilipofunulwa: "Sasa je, mnajua maana ya aya hizi?" Hadhrat Ibn 'Abbas[ra], ambaye bila shaka alikuwa na umri wa miaka kumi au kumi na mmoja wakati zilipofunuliwa na ambaye sasa alikuwa na miaka kumi na saba au kumi na minane, akajitolea kujibu. Akatamka akisema, "Ewe Kiongozi wa Waaminio, aya hizi zilikuwa na bishara ya kifo cha Mtume[saw]. Kazi ya Nabii inapomalizika, basi yeye hatamani tena kuishi duniani. Aya hizi zilizungumzia ushindi usioepukika wa Islam. Ushindi huu ulikuwa na sehemu yake ya huzuni nayo ilikuwa ni kukaribia kwa Mtume[saw] kuitoka dunia hii." Hadhrat Umar[ra] alimuunga mkono Hadhrat Ibn Abbas[ra] na akasema kwamba aya hizi zilipofunuliwa, Abu Bakr peke yake alizielewa maana yake.

SIKU ZA MWISHO ZA MTUME[SAW]

Hatimaye ikakaribia ile siku ambayo kila mwanadamu ni sharti akumbane nayo. Kazi ya Mtume[saw] ilikuwa imekamilika. Yote aliyokuwa Mwenyezi Mungu amfunulie kwa manufaa ya mwanadamu yalikuwa yamefunuliwa. Dhati ya Muhammad[saw] ilikuwa imeleta maisha mapya kwa watu wake. Taifa jipya lilikuwa limezuka, hali ya kuyafikiria upya maisha, na desturi mpya; kwa neno zima, mbingu mpya na ardhi mpya. Misingi ya utaratibu mpya ilikuwa imesimikwa. Nchi ilikuwa imelimwa na kunyunyiziwa maji na kupandwa mbegu kwa ajili ya mavuno mapya. Na sasa mavuno yenyewe yalikuwa yameanza kuonekana. Hata hivyo, haikuwa kazi yake yeye kuyavuna. Kazi yake ilikuwa tu kulima, kupanda na kumwagilia maji. Alikuja kama kibarua, akabakia kibarua na sasa yeye alikuwa amekaribia kuondoka kama kibarua. Hakuona malipo yake katika vitu vya dunia hii bali katika mapenzi na radhi ya Mungu wake, Muumba wake na Bwana wake. Ulipowadia wakati wa mavuno, yeye alipendelea kurejea Kwake, akiwaacha wengine wavune.

Mtume[saw] akawa mgonjwa. Kwa siku kadha akaendelea kwenda msikitini na kuongoza sala. Baadaye akawa dhaifa sana kuweza kufanya hivyo. Masahaba walikuwa wamezoea sana kuwa naye kiasi

hiki kwamba ilikuwa vigumu sana kwao kuamini kwamba Mtume[saw] angelifariki. Lakini yeye alikuwa akiwatajia kifo chake mara kwa mara. Siku moja, akiwa yuwagusia jambo hili hili, alitamka akisema, "Akitokea mtu kufanya kosa, basi ni afadhali alifidie humu humu duniani kusudi yasije yakampata majuto huko ahera. Hivyo basi, mimi nasema, kama nimemkosea chochote mmoja wenu yeyote, hata kama si kwa makusudi, na anitake nilifidie. Hata kama kwa kutokujua mimi nimemdhuru mmoja wenu yeyote, basi na aje ajilipizie kisasi. Mimi sitaki kwenda kuaibishwa nitakaposimama mbele ya Mungu wangu huko ahera." Masahaba nyoyo zikawalainika. Machozi yakawalengalenga. Wakawa wakiwaza kimoyomoyo ni machungu gani yaliyokuwa yeye hakuwa ameyaonja na ni taabu gani zilizokuwa yeye hakuwa amezivumilia kwa ajili yao?

Yeye alikaa na njaa na kiu kusudi watu wengine wapate cha kutosha kula na kunywa. Alijitilia ripea nguo na viatu vyake ili wengine wavalie vizuri. Lakini hata hivyo yeye alikuwa yupo hapa, tayari kufidia hata yale makosa ya kudhania tu ambayo huenda aliwafanyia watu wengine; alizithamini sana haki za wengine.

Masahaba wote wakalipokea kimya kimya toleo hili la Mtume[saw]. Lakini mmoja akajitokeza na akatamka akisema "Ewe Mtume wa Mungu, mimi safari moja uliniumiza. Tulikuwa tukijipanga vitani ulipopitia safu yetu na ulipokuwa ukipita ulinipiga kumbo. Haikufanyika makusudi, lakini wewe umesema twaweza tukayalipizia kisasi hata yale makosa yasiyokuwa ya makusudi. Mimi nataka kulilipizia kisasi kosa hili". Masahaba waliokuwa wamelisikiza toleo la Mtume[saw] kimya kimya, wakajawa na hasira. Walikasirishwa na utovu wa adabu na upumbavu wa mtu huyu aliyekosa kufahamu kabisa dhati ya toleo la Mtume[saw] na uzito wa mambo yaliokuwa. Lakini yule Sahaba akatokea kudinda kabisa — akinuia kumchukulia Mtume[saw] sawa na kauli yake.

Mtume[saw] akasema akimwambia, "Unayo ruhusa ya kujilipiza kisasi." Akamgeuzia mgongo na akamwambia, "Njoo unipige kumbo kama vile nilivyokupiga."

Yule Sahaba akasema, "Lakini, uliponipiga kumbo ubavu wangu ulikuwa uko wazi, kwani siku ile mimi sikuwa nimevaa shati."

Mtume[saw] akasema, "Niinueni shati, na mumwache anipige kumbo." Wakamwinua shati lakini, badala ya kumbo, yule Sahaba akainama huku machozi yakimlengalega na kmbusu mwili wa Mtume[saw].

Mtume[saw] akauliza akisema; "Mambo gani haya?"

Yule Sahaba akasema, "Si ulisema siku za wewe kuwa nasi zilikuwa zimefikia ukingoni? Basi ni fursa zingine ngapi sisi tunazoweza kuwa nazo za kukugusa mwilini na kukuonesha mapenzi yetu na shauku zetu? Kumbo ulinipga kweli, lakini ni nani wa kuilipizia kisasi. Wazo hili lilinijia sasa hivi. Ulituruhusu tujilipizie kisasi. Mimi nikajiambia — hebu nikubusu kwa kisingizio cha kisasi."

Wale Masahaba ambao hadi kufikia hapo hasira zilikuwa zimewajaa wakaanza kutamani laiti nao pia lingeliwajia wazo sampuli hiyo.

MTUME[SAW] YUWAAGA DUNIA

Lakini Mtume[saw] alikuwa ni mgonjwa na ugonjwa wenyewe ulionekana ukimzidi. Ilionekana mauti yalikuwa yakimsogelea karibu zaidi na zaidi, na hali ya huzuni na majonzi ikazishukia nyoyo za Masahaba. Jua liliangaza kama kawaida mjini Madina, lakini kwao Mashaba lilioneka kuzidi kutokuwa na nuru. Mchana ulipambazuka kama kawaida, lakini ulionekana kana kwamba waleta giza, sio nuru. Hatimaye ukafika wakati ambapo roho ya Mtume[saw] ilikuwa iyatoke mazingara yake ya kimwili na kukutana na Muumba wake. Kupumua kwake kukazidi kuwa kwa taabu. Mtume[saw] aliyekuwa akipitisha siku zake za mwisho chumbani mwa Hadhrat Aisha[ra], akamwambia, "Kidogo niinue kichwa ukisogeze kwako. Siwezi kupumua vizuri." Hadhrat Aisha[ra] akafanya hivyo. Aliketi na kumshikilia kichwa. Uchungu wa mauti ulidhihirika. Akikosa utulivu, Mtume[saw] alitazama huku na huku. Akakariri mara kwa mara akisema, "Ole wao Mayahudi na Wakristo. Walitilia maanani kuabudiwa kwa makaburi

ya Manabii wao." Huu, tunaweza tukasema ndio uliokuwa ujumbe wake wa kuagia dunia kwa wafuasi wake. Alipokuwa amelala pale alipofilia, yeye alikuwa kana kwamba yuwawaambia wafuasi wake, "Mtazoea kunitanguliza mbele ya Manabii wengine wote, na kunihesabu mfanikiwa kuliko mmoja wao yeyote. Lakini jihadharini msiligeuze kaburi langu kuwa ni kitu cha kuabudiwa. Kaburi langu na libakie kuwa ni kaburi tu. Wengine wanaweza wakayaabudu makaburi ya Manabii wao na kuyafanya kuwa ni vituo vya hija, mahali wanapoweza kwenda na kujinyima raha, kutoa dhabihu zao na sadaka zao. Wengine wanaweza wakayafanya haya lakini sio nyinyi. Ni sharti muikumbuke shabaha yenu moja tu — yaani, ibada ya Mungu Mmoja wa Pekee.

Baada ya kuwaonya hivyo Waislamu kuhusu wajibu wao wa kulinda Imani ya Mungu Mmoja iliyopatikana kwa damu na wajibu wao kutofautisha baina ya Mungu na Mwanadamu, kope zilianza kumshuka. Macho yakaanza kumfungika. Hapo yote aliyosema yalikuwa haya, "Kwa Rafiki yangu wa Juu zaidi ya walio Juu — kwa Rafiki yangu wa Juu zaidi ya walio Juu", dhahiri akimaanisha kwamba alikuwa akielekea Kwake Mwenyezi Mungu. Alipokuwa akisema hivyo akakata roho.

Habari zikafika msikitini. Masahaba wengi walikuwa wamekusanyika kule, wakiwa wameachilia mbali shughuli zao za kibinafsi. Walikuwa wakitarajia kupata habari njema lakini badala yake wakasikia kifo cha Mtume[saw]. Kilifika mithili ya pigo lisilovumilika. Hadhrat Abu Bakr[ra] hakuwepo. Hadhrat Umar[ra] alikuwemo msikitini, lakini yeye alikuwa ameshikwa na bumbuazi kwa huzuni kubwa. Ikawa yeye kukasirika kama akimsikia mtu akisema kwamba Mtume[saw] kafariki. Hata akatokea kuchomoa upanga wake akitishia kuwaulia mbali wale wangeliothubutu kusema kwamba Mtume[saw] amefariki. Yalikuweko mengi aliyokuwa Mtume[saw] bado ayafanye, kwa hivyo Mtume[saw] asingeliweza kufariki. Kweli, roho yake imeutoka mwili wake, lakini ilikuwa imekwenda kukutana na Muumba wake tu. Ni kama vile tu

Musa alivyokuwa amekwenda kwa muda kukutana na Muumba wake na baadaye kurejea, ni sharti Mtume[saw] arudi kufanya yale ambayo bado hayajafanywa. Walikuweko watu kama vile wanafiki kwa mfano, ambao bado alikuwa apambane nao. Hadhrat Umar[ra] alitembea upanga mkononi chambileche mwenda wazimu. Alipokuwa akitembea akawa akisema: "Yeyote atakayesema Mtume[saw] amefariki atafariki yeye mwenyewe kwa mkono wa Umar. Wakawa Masahaba wametatizika na kuwa karibu kuamini aliyosema Hadhrat Umar[ra]. Mtume[saw] asingeliweza kufariki. Ni lazima pana kosa fulani. Wakati huo huo baadhi ya Masahaba walienda kumtafuta Hadhrat Abu Bakr[ra], wakampata na kumpasha habari hii. Hadhrat Abu Bakr[ra] akafulizia msikitini moja kwa moja na bila ya kuongea na mtu, akaingia chumbani mwa Hadhrat Aisha[ra] na akamwuliza akimwambia, "Je, Mtume[saw] amefariki?" Hadhrat Aisha[ra] akajibu "Naam". Hapo akaenda ulikolazwa mwili wa Mtume[saw], akaufunua uso, akainama na kubusu kipaji cha uso. Machoni alitiririkwa na machozi ya mapenzi na huzuni na ndipo akasema, Wallahi, mauti hayatakujia mara mbili."

Hii ilikuwa ni kauli yenye maana nyingi. Lilikuwa ni jibu la Hadhrat Abu Bakr[ra] la yale Hadhrat Umar[ra] aliyokuwa akisema katika kupayuka kwake kwa huzuni. Mtume[saw] amefariki tu. Hicho kilikuwa ni kifo chake cha kimwili — kifo cha lazima kila mmoja kufa. Lakini asingelitokea kuwa na kifo cha pili. Pasingelitokea kuwa na kifo cha kiroho — hapana kifo kwa zile imani alizokuwa amezijenga katika wafuasi wake na ambazo kwa ajili ya ujenzi wake yeye alikuwa amepata taabu kupindukia. Moja ya imani hizo — moja ya zile imani muhimu zaidi — alizokuwa amezifundisha ilikuwa kwamba hata Manabii walikuwa ni wanadamu na hata wao hawakuwa na budi kufariki. Hawakuwa Waislamu watokee kuisahaulia mbali imani hii mara baada ya kifo cha Mtume[saw]. Baada ya kutamka kauli hiyo nzito penye mwili wa Mtume[saw], Hadhrat Abu Bakr[ra] alitoka nje na huku akijipenyeza kwenye safu za Waaminio, akaenda hadi kwenye mimbari. Alipokuwa akisimama Hadhrat

Umar[ra] alijibanza karibu naye, upanga wake mkononi kama hapo mwanzo, akidhamiria kwamba akitokea Hadhrat Abu Bakr[ra] kusema Mtume[saw] kafariki, basi ni sharti amkatilie mbali kichwa chake. Hadhrat Abu Bakr[ra] alipoanza kunena, Hadhrat Umar[ra] alimvuta shati, akitaka kumkataza asiseme, lakini Hadhrat Abu Bakr[ra] akarekebisha shati lake na kukataa kunyamaza.

Hapo yeye akasoma hii aya ifuatayo ya Kurani:

Na Muhammad ni Mtume tu. Bila shaka wamekwisha fariki kabla yake Mitume. Je, akifa au kuuawa mtarudi nyuma kwa visigino vyenu? (Sura Aali 'Imraan 3:145).

Yaani, Muhammad alikuwa ni mwanadamu akiwa na Ujumbe kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Wamepata kuwepo wanadamu wengine wakiwa na Ujumbe kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na hao wote walikufa. Akitokea Muhammad kufariki, wao wangekitupilia mbali kila kitu walichokuwa wamefundishwa na walichokuwa wamejifunza? Aya ilifunuliwa wakati wa vita vya Uhud. Wakati huo uvumi ulikuwa umeenea kwamba Mtume[saw] alikuwa ameuawa na maadui. Waislamu wengi walikata tamaa na kujiondoa kwenye uwanja wa vita. Hii aya ilikuja kutoka mbinguni kuwatilia shime. Ilikuwa na athari ile ile wakati huu. Baada ya kusoma aya hii, Hadhrat Abu Bakr[ra] aliiongezea maneno yake yeye mwenyewe. Akasema, "Wale miongoni mwenu wanaomwabudu Mwenyezi Mungu, na wajue kwamba Mwenyezi Mungu yungali hai, na atakuwa hai milele. Lakini miongoni mwenu waliomwabudu Muhammad[saw], basi na waelewa kutoka kwangu mimi kwamba Muhammad amefariki." Masahaba wakarekebika kiakili kwa kusikia hotuba hii iliyohitajika. Hadhrat Umar[ra] mwenyewe alibadilika alipomskia Hadhrat Abu Bakr[ra] akisoma aya hii. Akaanza tena kujimudu, na kurejelewa na fahamu zake. Pale Hadhrat Abu Bakr[ra] alipomaliza kusoma aya hii ikawa jicho la kiroho la Hadhrat Umar[ra] kufunguka kabisa. Akaelewa kwamba Mtume[saw] kweli alikuwa amefariki. Lakini mara alipofahamu ukweli wa mambo yalivyokuwa, miguu yake yalianza kutetemeka na kulegea. Akaanguka chini akiwa

mchovu. Yule mtu aliyetaka kumdhuru Hadhrat Abu Bakr[ra] kwa upanga wake alikuwa amefanywa hoi na hotuba ya Hadhrat Abu Bakr[ra]. Masahaba wakatokea kuhisi kana kwamba aya ile ilikuwa imefunuliwa kwa mara ya kwanza siku ile, athari yake ikiwa nzito na mvuto wake ukiwa mpya. Katika ukali wa huzuni wao wakasahau kwamba aya ile ilikuwemo ndani ya Kurani.

Wengi walizielezea huzuni zilizowafunikiza Waislamu kutokana na kifo cha Mtume[saw], lakini kichoma-moyo chenyewe na maombolezo fasaha zaidi ambayo Hassaan, mshairi wa Islam ya awali, alikipatia kifo cha Mtume[saw] bado hadi hivi leo ndiyo bora na ya kudumu zaidi. Yeye alisema, "Ulikuwa ndiwe mboni ya jicho langu. Ukiwa sasa umekufa, jicho langu limepofuka. Mimi sasa sijali ni nani anayekufa. Kwani kifo chako ulikuwa ndio wasiwasi wangu."

Ubeti huu ulielezea maoni ya kila Mwislamu. Kwa miezi mingi katika barabara za Madina wanaume, wanawake na watoto walitembea huku wakiukariri ubeti huu wa Hadhrat Hassaan bin Thabit[ra].

HULKA ZA MTUME[SAW] NA TABIA ZAKE

Baada ya kuelezea kwa kifupi matukio makubwa makubwa katika maisha ya Mtume[saw], sasa na iwe sisi kidogo kupiga picha ya tabia zake. Katika uwanja huu tunao ushahidi wa pamoja wa watu wake yeye mwenyewe walioutoa kuhusu tabia zake kabla hajadai kuwa Mtume. Hadi kufikia wakati ule yeye alijulikana kwa watu wake kama "Mwaminifu" na "Mkweli" (Hisham). Siku zote panaishi idadi kubwa ya watu ambao hazitolewi lawama za udanganyifu dhidi yao. Zipo pia idadi kubwa za watu ambao katu hawakuyakabili majaribio magumu au vishawishi na katika shughuli za kawaida na mambo ya kimaisha wao huwa wanatenda kwa uaminifu na unyofu, lakini hata hivyo hawafikiriwi kuwa wanastahili sifa yoyote maalumu kutokana na mienendo hiyo yao. Sifa maalumu bainifu hutolewa pale tu maisha ya mtu yanapozionesha kwa kiwango kikubwa tabia njema tukufu. Kila mwanajeshi ajitupaye kwenye uwanja wa vita huhatarisha maisha

yake, lakini sio kila mwanajeshi kama huyo wa Kingereza kahesabiwa mwenye kustahili kuzawadiwa nishani ya Victoria Cross, wala sio kila mwanajeshi kama huyo wa Kijarumani kuwa yuwastahili kuzawadiwa nishani ya Iron Cross. Kunao mamia ya maelfu ya watu nchini Ufaransa wanaojishugulisha na fani za kiakili lakini sio kila mmoja wao yuwatunukiwa nishani ya ***Lagion of Honour***. Hivyo basi, ukweli peke yake kwamba mtu ni mwaminifu na mkweli hauoneshi kwamba yeye ana ubora katika nyanja hizi, lakini linapotokea taifa zima kushirikiana kwa pamoja kumtunukia mja mmoja lakabu za "Mwaminifu" na "Mkweli", basi hiyo ni dalili ya yeye kuwa na sifa bora zaidi. Ingelitokea kuwa ni desturi ya watu wa Makka kumpatia mtu fulani sifa sampuli hiyo katika kila kizazi, hata katika hali kama hiyo mtunukiwa kama huyo angelitokea kuhesabiwa mwenye cheo cha juu. Lakini historia ya Makka na Arabuni haina kidokezo chochote ya kuwa ilikuwa ni desturi ya Waarabu lakabu hizi kuzitunukia watu mashuhuri katika kila kizazi. Kinyume chake, ndani ya karne nyingi za historia ya Waarabu twakuta kwamba ilikuwa tu kumhusu Mtume wa Islam[saw] ya kuwa watu wake walizitunukia hizi lakabu za "Mwaminifu" na "Mkweli". Hili ni thibitisho la ukweli kwamba Mtume[saw] alikuwa na sifa hizi kwa kadri iliyo kubwa kiasi hiki kwamba sawa na watu wake walivyofahamu na kukumbuka, hakuweza mtu mwingine kuchukuliwa kuwa sawa naye katika sifa hizi. Waarabu walijulikana sana kwa ukali wa fahamu zao na kile walichokifahamu wao kuwa ni kitu cha nadra ni sharti kiwe kilikuwa ni cha nadra na cha kipekee.

Mtume[saw] alipotakiwa na Mwenyezi Mungu kuchukua wajibu na jukumu la Utume, mkewe, Hadhrat Khadija,[ra], alitoa ushahidi wa tabia zake tukufu — kisa ambacho kimeelezewa kwenye sehemu ya matukio ya kihistoria ya Kifungua Mlango hiki. Sasa tutaanza kuonesha baadhi ya tabia zake tukufu ili kwamba msomaji aweze kuzifahamu hata zile sehemu za tabia zake zisizojulikana sana.

USAFI WA MAWAZO YA MTUME[SAW] NA TABIA ZAKE

Inasimuliwa juu ya Mtume[saw] ya kwamba maneno yake daima yalikuwa safi na kwamba (kinyume na wengi wa watu wa zama zake) yeye hakuzoelea kuapa (Tirmidhi). Hiki hakikuwa kitu cha kawaida kwa Mwarabu. Hatumaanishi kwamba Waarabu katika zama za Mtume[saw] walitokea kutumia lugha chafu, lakini hapana tashwishi ya kwamba wao walikuwa na mazoea ya kutomelea maneno yao kwa 'Wallahi' nyingi, mazoea yanayodumu miongoni mwao hadi leo. Mtume[saw] hata hivyo, aliliheshimu sana jina la Mwenyezi Mungu na hakulitaja kabisa bila ya stahili yake.

Yeye alikuwa mwangalifu sana, hata mstahifu, kuhusu usafi wa kimwili. Yeye alikuwa akipiga mswaki mara kadha kila siku na tabia hii aliipendelea sana hata akawa akisema kwamba kama asingelichelea isije tabia hii ikawa nzito, basi yeye angelimfaradhishia kila Mwislamu kupiga mswaki kabla ya kila moja ya sala tano za kila aiku. Siku zote yeye alinawa mikono yake kabla na baada ya kila maakuli, na baada ya kula kitu chochote kilichopikwa, siku zote yeye alisukutua na akakichukulia kuwa ni kitu kilichotakikana ya kuwa kila mtu aliyekula chochote kilichopikwa awe akisukutua kabla ya kujumuika kwenye mojawapo yoyote ya zile sala tano. (Bukhari).

Katika desturi za Islam msikiti ndipo mahali pa pekee kukusanyika palipopendekezewa Waislamu. Hivyo, Mtume[saw] alitilia usafi wa misikiti mkazo maalumu, hususan katika zile nyakati ambapo watu walitarajiwa kukusanyika humo. Alikuwa ameagiza kwamba nyakati kama hizo misikiti ifukizwe ubani (udi) kusafisha hewa (Abu Dawud). Pia alitoa maagizo kwamba yeyote asifike msikitini wakati wa sala ya jamaa au mkusanyiko baada ya yeye kuwa amekula kitu chochote ambacho huenda kikatoa harufu mbaya (Bukhari).

Alisisitizia barabara kuwekwa safi na kutokuwa na majani, mawe, wala takataka zozote ambazo huenda zikawa vizuizi au kuwaudhu wapita njia. Yeye mwenyewe kila alipokuta vitu au takataka kama hizo zikiwa barabarani alikuwa akiziondolea mbali, na alizoea kusema kwamba kila

anayesaidia kuziweka safi barabara na njia, hujichumia thawabu machoni pa Mwenyezi Mungu. Yuwasemekana pia alitaka kwamba barabara za umma zisitumiwe kwa njia ambayo kwamba zitakuwa ni pingamizi wala vitu vichafu ama vinavyochukiza na visitupwe mahali kunakopitiwa na watu wote, wala barabara na zisichafuliwe kwa njia yoyote iwayo; mambo yote sampuli hiyo yanamchukiza Mwenyezi Mungu. Alisisitiza kwamba maji yote yaliyotengewa matumizi ya wanadamu ni sharti yawekwe safi na mazuri. Kwa mfano, yeye alikataza kitu chochote kutupwa kwenye dimbwi la maji kiwezacho kuyachafua na akiba yoyote ya maji kutumiwa kwa njia itakayoyachafua (Bukhari na Muslim, Kitab al-Birr wa'l-Sila).

MAISHA YA KIKAWAIDA YA MTUME[SAW]

Mtume[saw] alikuwa na tabia ya kikawaida kabisa kuhusu chakula. Hakupata kukitoa makosa chakula kilichopikwa au kutayarishwa visivyo. Alipotokea kuweza kula chakula kama hicho basi yeye alikila tu ilimradi kumwepushia mpishi mahangaiko. Hata hivyo, chakula kilichotokea kutolika, yeye aliepuka tu kukila na wala hakukitia walakini. Alipoketi kula chakula yeye alitilia maanani kile chakula alichoandaliwa na alizoea kusema kwamba alichukia tabia ya kutojali chakula kana kwamba mlaji alikuwa na hali iliyokiuka mambo ya maakuli na maji. Chakula chochote alichokipatiwa yeye sikuzote alikila pamoja na wale waliokuwepo. Safari moja mtu mmoja alimpatia tende. Alitazama huku na huku na baada ya kukadiria idadi ya waliokuwepo akazigawa zile tende sawasawa miongoni mwao, kila mmoja wao akapata tende saba. Hadhrat Abu Huraira[ra] yuwasimulia kwamba hata mkate wa shayiri Mtume[saw] hakupata kabisa kula na akashiba (Bukhari).

Safari moja alipokuwa akipitapita njiani aliwaona watu waliokusanyika kuzunguka mbuzi aliyeokwa wakiwa tayari kumla. Walipomwona Mtume[saw] wakamkarabisha ale pamoja nao, lakini yeye akakataa. Hii haikuwa kwa sababu ya yeye kutopenda nyama-choma bali kwa sababu ya ukweli kwamba hakupendelea watu kufanyia karamu zao peupe wanapoweza kuonwa na watu maskini ambapo

wenyewe hawana chakula cha kutosha. Yaripotiwa juu yake kwamba safari zingine yeye alikula nyama-choma. Hadhrat Aisha[ra] amesimulia kwamba maisha yake mazima Mtume[saw] hakupata wakati wowote kula na kushiba siku tatu mfululizo. Alikuwa mwangalifu sana ya kwamba mtu na asiende kula nyumbani kwa mtu mwingine bila ya kukaribishwa. Safari moja mtu fulani alimwalika kwenda kula chakula na akamwomba ya kuwa angeliweza kuja na watu wengine wanne. Alipowasili nyumbani kwa yule mwenyeji wake akagundua kumbe mtu mwingine wa sita alikuwa amefuatana nao. Yule mwenyeji wake akaja mlangoni kumpokea pamwe na kundi lake na Mtume[saw] akamfahamisha kwamba sasa walikuwa ni watu sita na kwamba ilikuwa ni juu ya yule mwenyeji kuamua kama angemruhusu yule mtu wa sita kula nao au mtu yule ajiendee zake. Naam, bila wasiwasi mwenyeji akamkaribisha yule wa sita pia (Bukhari, Kitabul-At'ima).

Mtume[saw] wakati wowote alipoketi kujipatia riziki, daima alianza kwa kutanguliza jina na Allah na baraka Zake, na mara baada ya kumaliza kula alishukuru kwa maneno haya: "Sifa zote njema ni Zake Allah, Aliyetulisha: Sifa teletele tena za dhati na zinazozidi kuongezeka: Sifa zisizomfanya mtu ajisikie kwamba amesifu vya kutosha bali zinazozusha akilini mwa mtu wazo ya kwamba bado hajasifia vya kutosha na sifa ambazo hazifai kukatizwa na zinazomfanya mtu kuona kwamba kila tendo la kimbinguni lastahili sifa na ni sharti lisifiwe. Ewe Allah! zijaze nyoyo zetu kwa mawazo haya." Wakati mwingine yeye alitumia maneno haya: "Sifa zote njema ni Zake Mwenyezi Mungu Aliyetutuliza njaa na kiu zetu. Na zitokee nyoyo zetu daima dawamu kutamani sifa Zake na kutokosa kabisa kumshukuru" Daima yeye aliwanasihi Masahaba wake kuacha kula kabla ya kushiba na alizoea kusema kwamba chakula cha mtu mmoja chastahili kuwatosha watu wawili. Kila kilipopikwa chakula kizuri nyumbani mwake, yeye alikuwa akipendekeza kwamba sehemu ya chakula hicho wapelekewe jirani zake hidaya; na hidaya sampuli hii za vyakula na vitu vingine zilikuwa zikiendelea kutolewa toka kwake nyumbani kupelekwa nyumba za jirani zake (Muslim na Bukhari, Kitabul-Adab).

Daima yeye alijaribu kusoma nyuso za wale waliokuwa pamoja naye kuona kama yeyote miongoni mwao yuwahitaji riziki. Hadhrat Abu Huraira[ra] yuwasimulia kisa kifuatacho: Safari moja yeye alikuwa hajala kwa zaidi ya siku tatu. Akasimama kwenye mlango wa msikiti na akamwona Hadhrat Abu Bakr[ra] akipita karibu. Akamwuliza Hadhrat Abu Bakr[ra] maana ya aya moja ya Kurani yenye kuhimiza kuwalisha maskini. Hadhrat Abu Bakr[ra] akaelezea maana yake na akajiendea zake. Alipokisimulia kisa hiki Hadhrat Abu Huraira[ra] alikuwa akisema kwa uchungu kwamba hata yeye aliielewa Kurani chambileche Hadhrat Abu Bakr[ra]. Shabaha ya kumwuliza Hadhrat Abu Bakr[ra] aeleze maana ya aya yenyewe ilikuwa kwamba itokee Hadhrat Abu Bakr[ra] kumhisi kuwa na njaa na kutokea kumfanyia mpango wa maakuli. Punde si punde, Hadhrat Umar[ra] akapitia pale na Hadhrat Abu Huraira[ra] akamwuliza huyu naye aelezee maana ya ile aya. Hadhrat Umar naye pia akaelezea maana yake na kuenda zake. Kama ilivyokuwa tabia ya Masahabu wote wa Mtume[saw], Hadhrat Abu Huraira[ra] alichukia kabisa omba-omba za moja kwa moja na baada ya kuhisi kwamba kitendawili cha kuitangaza njaa yake hakikuwa kimefua dafu, alianza kujisikia dhaifu. Ndipo aliposikia likiitwa jina lake kwa sauti nzuri na yenye upendo. Alipotazama ilikotoka sauti akaona kumbe Mtume[saw] alikuwa akimtazama kwenye dirisha la nyumba yake na alikuwa akitabasamu. Akamwuliza Hadhrat Abu Huraira[ra] akimwambia; "Wasikia njaa?' ambapo Hadhrat Abu Huraira[ra] alimjibu akimwambia: "Naam, Ewe Mtume wa Allah! Mimi nasikia njaa."

Mtume[saw] akasema: "Mwetu nyumbani pia hamna chakula, lakini mtu mmoja sasa hivi katuletea kikombe cha maziwa. Hebu nenda kule msikitini ukaangalie kama kunao watu wengine wanaosikia njaa kama wewe." Hadhrat Abu Huraira[ra] yuwaendelea kusimtilia akisema: "Nikajiambia, maziwa ya kikombeni mimi mwenyewe hayanitoshi njaa yangu, huku Mtume[saw] amenitaka niwaite watu wengine ambao huenda wakawa na njaa, ikimaanisha kwamba yale maziwa mimi nitapata kidogo sana. Lakini ilinibidi kutekeleza amri ya Mtume[saw],

basi nilifika msikitini na nikakuta watu sita niliofutana nao hadi mlangoni pa Mtume[saw]. Akampatia mmoja wao kile kikombe cha maziwa na akamwabia anywe. Akiwa ameishakunywa na kukiondoa kikombe mdomoni, Mtume[saw] akamhimiza kunywa tena na tena mpaka aliposhiba. Akamhimiza vivyo hivyo kila mmoja wa wale watu sita kunywa maziwa hadi ashibe. Kila alipomhimiza mtu mmoja kunywa mimi hofu ikanizidi kwamba nitabakiziwa kidogo mno. Wale wote sita walipokwisha kunywa Mtume[saw] akanipa kile kikombe na nikaona bado yalikuwemo maziwa mengi. Nami halikadhalika akanihimiza ninywe hadi nishibe na akanitaka kunywa tena na tena na mwishowe yeye akanywa yaliyosalia na akamshukuru Mwenyezi Mungu na kufunga mlango" (Bukhari, Kitabur-Riqaaq). Huenda shabaha ya Mtume[saw] ya kumfanya Hadhrat Abu Huraira[ra] kuwa wa mwisho kunywa yale maziwa ilikuwa ni kumuonesha kwamba alitakiwa kuvumilia njaa, akimtumainia Mwenyezi Mungu, na haikufaa yeye kuumbua hali yake hata kwa njia ya kitendawili.

Daima yeye alikula na kunywa kwa mkono wa kuume na alipokuwa akinywa daima alikatiza mara tatu kuvuta pumzi. Pengine sababu moja ya kufanya hivyo ilikuwa ni hii ya kwamba ikiwa mtu mwenye kiu atakunywa maji kwa mkupuo mmoja ataelekea kunywa mengi zaidi na hivyo kujidhuru tumboni. Ama juu ya suala la kula kanuni aliyoishika ilikuwa ni hii ya kwamba yeye alikula vitu vyote vilivyokuwa safi na halali lakini sio kwa mtindo wa ponda-mali wala mtindo ungeliowanyima watu wengine fungu lao. Kama ambavyo imeelezewa, chakula chake sikuzote kilikuwa ni chakula cha kawaida tu lakini kama alitokea mtu kumpatia kilichotayarishwa kwa mapishi spesheli yeye hakukikataa. Yeye, hata hivyo, hakujitamania chakula bora, ijapo alipenda sana asali na tende. Kuhusu tende, yeye alikuwa akisema kwamba ulikuwepo uhusiano spesheli baina na Mwislamu na mtende ambao majani yake na magome yake na matunda, mabivu na mabichi, na hata kokwa za matunda yake vyote vinaweza vikawa na matumizi haya au yale na mti ambao hapana sehemu yake isiyoweza kuwa na matumizi yake. Na hivyo ndivyo ilivyo hali ya Mwislamu

halisi. Hapana tendo lake lisilokuwa na manufaa yake na kila anachofanya kinastawisha masilahi ya wanadamu (Bukhari na Muslim).

Mtume[saw] alipendelea nguo za kawaida tu. Nguo zake yeye mwenyewe kwa kawaida zilikuwa ni shati na shuka ya kiunoni, au shati na suruali. Daima yeye alivaa shuka au suruali yake kwa namna ambayo kwamba nguo zenyewe ziliufunika mwili hadi juu kidogo ya vifundo vya miguu. Yeye hakupenda goti au sehemu yoyote ya mwili iliyo juu ya goti kuachwa wazi pasi na dharura kubwa. Yeye alichukia utumiaji, iwe ni kama sehemu ya mavazi au pazia, n.k., wa vitambara vilivyonakshiwa au kuchorwa michoro, hususan, kama michoro yenyewe ilikuwa ni mikubwa na iliyoelekea kufahamiwa kuwa yawakilisha miungu ya kike au ya kiume au vitu vingine vinavyoelekezewa ibada. Safari moja yeye alikuta pazia likining'inia mwake nyumbani lililokuwa na michoro mikubwa mikubwa na akaamuru liondolewe. Lakini hata hivyo, yeye hakuona ubaya wowote katika kutumiwa kwa vitambara vilivyokuwa vijichoro vidogo vidogo ambavyo havikuweza kuleta taswira hiyo. Yeye mwenyewe hakuvaa hariri asilani wala hakuiona hariri kuwa ni halali kuvaliwa na Waislamu wanaume. Yeye kwa shabaha ya kurasimisha barua alizowaandikia watawala fulani kuwataka wasilimu alitengenezesha pete yenye muhuri, lakini akaamuru utengenezwe kwa fedha wala sio dhahabu, kwani aliesma kwamba kuvaa dhahabu kumeharamishiwa Waislamu wanaume (Bukhari na Muslim). Waislamu wanawake wanaruhusiwa kuvaa hariri na dhahabu lakini hata kwao wao amri ya Mtume[saw] ilikuwa kwamba wasipite kiasi. Safari moja yeye aliitisha mchango wa kuwasaidia maskini na mama mmoja akamletea bangili yake moja kama mchango wake. Mtume[saw] akasema naye akimwambia: "Kwani huo mkono wako mwingine haustahili kuepushiwa Moto?" Hapo yule mama aliivua bangili kutoka mkono wake mwingine nayo pia akaitoa katika shabaha aliyokuwa nayo Mtume[saw]. Hapana mmoja wa wakeze aliyekuwa na mapambo ghali na Waislamu wanawake nao pia kwa nadra sana walikuwa na mapambo yoyote. Sawa na mafundisho ya Kurani yeye alikataza kujilundikia pesa au dhahabu, kwani alionelea kwamba jambo hili

lilidhuru masilahi ya maskini katika jamii na lilikuwa na matokeo ya kuchafua uchumi wa jamii na hivyo basi lilikuwa ni dhambi.

Safari moja Hadhrat Umar[ra] alimpendekezea Mtume[saw] ya kuwa kwa vile yeye hakuwa na budi kuwapokea Mabalozi wa dola kubwa kubwa, basi yafaa ashonewe joho la kukata-na-shoka analoweza kuvaa wakati kama huo. Mtume[saw] hakuliridhia pendekezo hili na akasema, "Mwenyezi Mungu hatakuwa radhi mimi kufuata desturi sampuli hii. Mimi nitampokea kila mtu nikivaa nguo zangu za kawaida. Safari moja aliletewa nguo za hariri na moja ya hizo akampelekea Hadhrat Umar[ra] Kuona hivyo, Hadhrat Umar[ra] akasema, "Nawezaje kuvaa nguo hii wakati wewe mwenyewe umekataza uvaaji wa nguo za hariri." Mtume[saw] akamjibu akisema, "Kila zawadi si kwa matumizi ya kibinafsi." Akiwa na maana ya kwamba kwa vile nguo yenyewe ilikuwa ya hariri, basi Hadhrat Umar[ra] angetokea kumpatia mkewe au bintiye au kuitumia kwa njia nyingine. (Bukhari, Kitabul-Libaas).

Malalo ya Mtume[saw] yalikuwa ya kawaida tu. Yalikuwa ni kipande cha ngozi au kipande cha nguo iliyosukwa kwa singa za ngamia. Hadhrat Aisha[ra] yuwasimulia hivi: "Kijitandiko chetu kilikuwa ni kidogo kiasi hiki kwamba Mtume[saw] alipokuwa akiamka usiku kusali mimi nilikuwa nikilalia upande mmoja wa kijitandiko na kunyoosha miguu yangu pale yeye alipokuwa akisimama wima salani na kuikunja tena alipokuwa akitaka kusujudu (Muslim, Tirmidhi na Bukhari, Kitabul At'ima).

Desturi hii ya kutotaka makuu yeye aliitumia katika mpango wa makazi yake. Nyumba yake ilikuwa kwa kawaida ya chumba kimoja na kajiukumbi kadogo. Ukambaa ulikuwa ukifungwa kupitia nusu nzima ya chumba kusudi apatapo wageni iweze, kuangikwa pazia mle ukambaani kuifanya sehemu moja ya chumba kile iwe ni mahali pa mazungumzo mbali na sehemu alikokuweko mkewe. Maisha yake yalikuwa ni maisha ya kujinyima kiasi hiki kwamba Hadhrat Aisha[ra] yuwaripoti ya kuwa mara nyingi wao walikuwa wakiponea tende na maji na kwamba siku alipofariki nyumbani hamkuwa na chakula isipokuwa tende kidogo (Bukhari).

UHUSIANO WAKE NA MWENYEZI MUNGU

Kila jiha ya maisha ya Mtume Mtukufu[saw] yaonekana iliyokuwa imetawaliwa na kuwa na rangi ya mapenzi yake na hali yake ya kujitupa kwa Mwenyezi Mungu.

Licha ya kubeba wajibu mzito aliokuwa ameupewa, sehemu iliyo kubwa ya wakati wake wa mchana na usiku ilipitishwa katika ibada na kumtukuza Mwenyezi Mungu. Ilikuwa yeye kuacha tandiko lake usiku wa manane na kuzama kwenye ibada ya Mwenyezi Mungu hadi ufikapo wakati wa kwenda msikitini kusali sala ya alfajiri. Wakati mwingini yeye aliweza kusimama sana salani kwenye mwisho mwisho wa usiku hadi miguu yake iwe inavimba, na wale waliomwona katika hali ile daima waliadhirika mno. Safari moja Hadhrat Aisha[ra] alimwambia: "Mwenyezi Mungu amekujazi mapenzi Yake na ukaribu Wake. Basi inakuwaje wewe kujipatisha taabu na mashaka sampuli hiyo?" Akajibu: "Kama Mwenyezi Mungu kwa Fadhila na Rehema Zake amenijazi Mapenzi Yake na ukaribu naye, je, hainipasi mimi niwe ni mwenye kumshukuru daima? Shukrani ni sharti ziwe ni zenya kuongezeka kulingana na hisani iliyopatikana (Bukhari Kitabul-Kusuuf).

Yeye hakufanya jambo lolote bila ya amri au kibali cha kiungu. Tayari imeelezewa kwenye sehemu ya utangulizi kwamba licha ya mateso makali aliyoonjeshwa na watu wa Makka yeye hakuutoka mji ule hadi pale alipopokea amri ya Mungu ya kufanya hivyo. Mateso yalipozidi kuwa makali kupindukia naye akawaruhusu Masahaba wake kuhamia Uhabeshi, baadhi yao walionesha nia yao ya kutaka aandamane nao. Yeye akakataa kufanya hivyo kwa sababu hakuwa amepata ruhusa ya Mungu ya kufanya hivyo. Hivyo basi, wakati wa dhiki na mateso ambapo watu kwa kawaida hutaka kuwaweka marafiki na ndugu zao karibu nao, yeye aliwanasihi Masahaba wake wahamie Uhabeshi na yeye mwenyewe akabakia mjini Makka, kwani Mwenyezi Mungu alikuwa bado hajamwamuru kuutoka.

Kila aliposikia neno la Mungu likiwa linasomwa, moyo ulimlainika na machozi kuanza kumlengalenga, hususan anapotukia kusikiza aya zinazosisitizia wajibu wake. Hadhrat Abdullah bin Mas'uud[ra] yuwasimulia kwamba safari moja yeye alitakiwa na Mtume[saw] kumsomea aya za Kurani. Akasema: "Ewe Mtume wa Mungu! Kurani umeifunuliwa wewe. Sasa iweje mimi kukusomea?" Lakini Mtume Mtukufu[saw] akasema: "Mimi hupenda kuisikia ikisomwa na watu wengine pia."

Hapo Hadhrat Abdullah bin Mas'uud[ra] akaanza kusoma Sura An-Nisaa. Aliposoma aya isemayo: "Basi itakuwaje tutakapoleta shahidi katika kila Umati na tutakuleta wewe uwe shahidi juu ya hawa?" (Sura An-Nisaa, 4:42). Mtume Mtukufu[saw] ikamtoka sauti ikisema: 'Basi! Basi! Hadhrat Abdullah bin Mas'uud[ra] akatupa jicho na akaona machozi yakimtiririka Mtume[saw] (Bukhari, Kitab Fadhaa'ilil-Kuran).

Yeye alikuwa mwangalifu sana juu ya kusali sala za jamaa hivi kwamba hata wakati wa kuumwa sana inaporuhusiwa mtu sio tu kusali sala zake chumbani mwake bali hata kusali huku akijilaza kitandani, alitokea kwenda msikitini kusalisha yeye mwenyewe. Safari moja alipotokea kutojiweza kwenda msikitini, alimwamuru Hadhrat Abu Bakr[ra] kusalisha. Hata hivyo mara akajisikia afueni na akataka apelekwe msikitini. Ikawa yeye kuegemea mabega ya watu wawili lakini alikuwa yu hali dhaifu kiasi hiki kwamba, sawa na ripoti ya Hadhrat Aisha[ra], miguu yake ilibururika (Bukhari).

Ni jambo la kawaida kwa mtu kuonesha furaha au kuashiria kitu chochote maalumu kwa kupiga makofi na Waarabu walikuwa wakifuata desturi hii hii. Hata hivyo, Mtume Mtukufu[saw] alipenda sana kumkumbuka Mwenyezi Mungu hivi kwamba kwa ajili ya hali sampuli hii yeye aliingiza utukuzaji wa Mwenyezi Mungu badala ya upigaji wa makofi. Safari moja alipotokea kuwa na shughuli muhimu, wakati wa sala ulikaribia na akaamuru Hadhrat Abu Bakr[ra] asalishe. Punde si punde akaweza kuhitimisha shughuli alizokuwanazo na kwenda msikitin mara moja. Hadhrat Abu Bakr[ra] alikuwa akisalisha

lakini maamuma walipohisi kwamba Mtume Mtukufu[saw] alikuwa amewasili, walianza kupiga makofi kushangilia kufika kwake na pia kumjuza Hadhrat Abu Bakr[ra] ya kuwa Mtume Mtukufu[saw] alikuwa amewasili. Hapo Hadhrat Abu Bakr[ra] akarudi safu ya nyuma na akampatia Mtume Mtukufu[saw] wasaa wa kuongoza sala. Sala ilipomalizika, Mtume[saw] akasema na Hadhrat Abu Bakr[ra] na akamwambia: "Ilikuwaje wewe kurudi safu ya nyuma baada ya kuwa mimi nilikutaka usalishe?" Hadhrat Abu Bakr[ra] akajibu akisema: "Ewe Mtume wa Mungu! Itamstahilije mwana wa Abu Quhafa kusalisha anapokuwepo Mtume wa Allah?" Akiwageukia maamuma Mtume[saw] alitamka akiwauliza: "Mbona mlipiga makofi? Mnapokuwa nyinyi katika hali ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu haifai kupiga makofi. Ikiwa itatokea ya kwamba patolewe ishara wakati wa sala kuhusu kitu fulani, basi badala ya nyinyi kupiga makofi semeni ***Subhaanallah*** kwa sauti. Hii itakuwa ni ishara tosha juu ya kitu chochote kinachotakiwa kutiliwa maanani (Bukhari).

Mtume[saw] hakutaka sala au ibada kutekelezwa kana kwamba ni kitubio au mzigo. Safari moja aliwasili nyumbani na akaona ukambaa umening'inizwa baina ya nguzo mbili. Akata kujua kisa na maana, na akaambiwa kwamba mkewe Hadhrat Zainab[ra] alikuwa amezoea kushikilia ukambaa ule alipokuwa amechoka salani. Mtume[saw] akaamuru ukambaa ule ufuguliwe mbali na akasema ya kwamba sala iwe ikiendelea kusaliwa mradi mtu anapokuwa yuwahisi hall ya urahisi na huku akijisikia mchangamfu na kwamba akitokea mtu kuchoka salani basi na aketi chini. Sala haikuwa ni mzigo, na ikiwa itatekelezwa wakati mwili unapokuwa ni mchovu haitimizi shabaha yake (Bukhari, Kitabul-Kusuuf).

Yeye alichukia kila tendo na desturi yenye dalili hata ndogo jinsi gani ya kuabudu viumbe. Ilipomkurubia hatima yake na kuwa katika hali ya kichomi cha mauti yeye aligeuka huku na huku akisema kwamba: "Na iwafikie laana ya Mwenyezi Mungu wale Mayahudi na Wakristo ambao wameyafanya makaburi ya Manabii wao kuwa ni mahali pa ibada" (Bukhari). Alikuwa akigusia wale Mayahudi na Wakristo

wanaoyasujudia makaburi ya Manabii wao na watakatifu na kuwaomba dua, na akamaanisha kwamba wakitokea Waislamu kushika mila sampuli hiyo basi hawatastahili dua zake bali wao, kinyume chake, ingelikuwa wamejitenga mbali naye.

Hali yake ya kuonea jazba kubwa utukufu wa Mwenyezi Mungu tayari imekwishaelezewa hapo mwanzoni. Watu wa Makka walitafuta kuziwekea shabaha zake kila aina ya vishawishi kumfanya atupilie mbali upinzani wake dhidi ya ibada ya masanamu (Tabari). Amiye Mzee Abu Talib vile vile alijaribu kumshawishi na akaonesha hofu yake ya kwamba kama Mtume[saw] atazidi kulaumu ibada ya masanamu, basi yeye Mzee Abu Talib itambidi kuchagua baina ya kuacha kumpatia ulinzi na upinzani mkali wa watu wake. Jawabu la pekee Mtume[saw] alilompatia amiye katika kisa hiki lilikuwa: "Hata wakitokea watu hawa kuliweka jua mkono wangu wa kuume na mwezi mkono wangu wa kushoto, mimi sitaacha kutangaza na kuhubiri Umoja wa Mungu" (Zurqani). Tena, wakati wa vita vya Uhud yalipomzingira mabaki ya majeruhi ya Waislamu chini ya mlima na ikawa maadui zao wanapiga ukulele wa nderemo zao za kuwashinda Waislamu na kiongozi wao Abu Sufyan kuropoka akisema: "Atukuzwe Hubal (mojawapo ya sanamu yaliyoabudiwa na watu wa Makka). Atukuzwe Hubal!" Mtume[saw] licha ya kutambua kwamba usalama wake na wa kile kikundi cha Waislamu waliokuwa wamemzunguka uliwataka wao wakae kimya hakuweza kujizuia tena na akawataka Masahaba wake kujibu kwa kupiga ukelele wakisema, "Ushindi na utukufu ni wa Allah peke yake! Ushindi na utukufu ni wa Allah peke yake!" (Bukhari).

Lilikuwa ni kosa la kawaida miongoni mwa wafuasi wa dini mbalimbali kabla ya ujaji wa Islam kufikiria kwamba madhihirisho ya kimbinguni na yale ya juu angani yalikuwa yakifanyika ili kuonesha wakati wa furaha na huzuni kwa ajili ya Manabii, watakatifu na watu mashuhuri na kwamba hata kuzunguka kwa sayari za juu kuliweza kusimamiwa na watu hao. Kwa mfano, baadhi yao wanasemekana kwamba walilifanya jua lisimame kwenye mzunguko wake au walisimamisha mzunguko wa mwezi au kukwamisha mtiririko wa

maji. Islam ikafundisha kwamba mawazo sampuli hiyo hayana msingi na kwamba kutajwa kwa mambo kama haya ndani ya Maandiko ya kidini kulikuwa ni kwa kimithali tu ambayo, badala ya kuelezewa katika sura ya hali yake halisi, ilikuwa imezusha ushirikina. Hata hivyo, baadhi ya watu miongoni mwa Waislamu wanaelekea kuwanasibishia Manabii wakubwa wakubwa matokeo sampuli hii. Katika miaka ya mwisho mwisho ya Mtume[saw], mwanawe Ibrahim alifariki akiwa na umri wa miaka miwili u nusu. Jua likapatwa siku hiyo hiyo. Baadhi ya Waislamu mjini Madina wakazusha wazo kwamba jua lilikuwa limetiwa giza kilipotokea kifo cha mwana wa Mtume[saw] kama ishara ya rambirambi za kimbinguni. Wazo hili lilipotajwa kwa Mtume[saw] yeye alionesha hasira kubwa na akalilaumu vikali. Alielezea kwamba jua na mwezi na sayari nyingine za angani vyote vikifuata kanuni na mizunguko yao na madhihirisho yanayoambatana navyo hayana uhusiano wowote na maisha wala kifo cha yeyote yule (Bukhari).

Arabuni ni nchi kavu mno na daima mvua hufurahikiwa mno na hungojewa sana. Waarabu walikuwa wakidhania kwamba kunyesha kwa mvua kulikuwa kukifuatia mizunguko ya nyota. Kila mara mtu alipolileta wazo lile, Mtume Mtukufu[saw] alikuwa akiudhika sana na akawaonya watu wake neema walizopewa ma Mwenyezi Mungu wasizinasibishe na vitu vingine. Alielezea kwamba mvua na mambo mengine ya kimaumbile yote yalifuata kanuni za kimbinguni na kwamba wala hayakuwa yakifuata kupenda au kutopenda kwa mungu mwinginewe wa kike wala wa kiume au nguvu yoyote nyingine (Muslim, Kitabul-Iman).

Alikuwa na hali halisi ya kumtegemea Mwenyezi Mungu ambayo hapana matatizo chungu nzima yaliyoweza kuitikisa. Safari moja adui yake mmoja, akitokea kumpata usingizini na bila ya ulinzi, alisimama kwake kichwani na kutishia kummalizia mbali mara moja. Kabla ya kufanya hivyo akauliza: "Ni nani awezaye kukunusuru humu kilingoni?" Mtume Mtukufu[saw] kwa utulivu mkubwa akajibu: "Allah." Neno hili yeye alilitamka kwa dhati halisi hivi kwamba hata moyo wa

yule adui yake kafiri ulilazimika kukiri hali ya utukufu wa imani yake na jinsi alivyomtegemea Mwenyezi Mungu. Upanga ukamdondoka, na yule mtu ambaye punde tu hapo kabla alinuia mauaji yake, akawa yuwasimama mbele yake kana kwamba ni muhalifu aliyengojea hukumu (Muslim Kitabul-Fadhaa'il, Bukhari, Kitabul-Jihad).

Kwa upande mwingine ilikuwa ni ile hali yake ya unyenyekevu halisi mbele ya Mwenyezi Mungu. Hadhrat Abu Huraira[ra] yuwasimulia: "Siku moja nilimsikia Mtume Mtukufu[saw] akisema kwamba hapana atakayepata wokovu kwa njia ya vitendo vyake vizuri." Hapo mimi nilisema: "Ewe Mtume wa Allah! Bila shaka wewe utaingia Peponi kwa njia ya matendo yako mema," wazo ambalo yeye alilijibu akisema: 'La hasha, hata mimi siwezi kuingia Peponi kwa njia ya matendo yangu mimi mwenyewe ila tu iwe Rehema na Huruma ya Mwenyezi Mungu vitanifunikiza." (Bukhari, Kitabur-Riqaaq).

Daima yeye aliwanasihi watu wateue na kushika njia ya sawa na kutia bidii katika kuzitafuta zile njia ambazo kwazo wanaweza wakapata ukaribu na Mwenyezi Mungu. Alifundisha mtu kutojitakia mauti, kwani akiwa yu mwema yeye kwa kuwa na umri mrefu ataweza kujichumia heri kubwa; na akitokea kuwa mwovu, pengine, akipatiwa muda, ataweza kutubia mienendo yake mibaya na kuanza njia njema. Mapenzi yake juu ya Mwenyezi Mungu na kumwamini kwake kuliainishwa kwa njia nyingi. Kwa mfano, kila wakati baada ya ukame wa muda mrefu matone ya kwanza ya mvua yalipoanza kunyesha, ilikuwa yeye kuchomoa ulimi ajipatie tone la mvua na hapo kutamka akisema: "Hii ni baraka ya sasa hivi kutoka kwa Mola Wangu." Wakati wote alishughulika na kuomba msamaha wa Mwenyezi Mungu na baraka Zake, huku akizidi sana hususan alipotokea kuketi miongoni mwa watu kusudi wale waliokuwa pamoja naye au waliofungamana naye na Waislamu kwa jumla wajiepushie ghadhabu za Mungu na kutokea kuwa ni watu wenye kustahili msamaha wa Mungu. Hisia zake ya kwamba yeye daima yupo mbele ya Mwenyezi Mungu hazikumtoka asilani. Alipotokea kuwa yuwajinyosha kulala, akasema: "Ee Allah! Hebu nijifie (nilale) na jina Lako mdomoni na

niamke na jina Lako mdomoni." Alipoamka, basi ilikuwa yeye kutamka akisema "Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Aliyenihuisha baada ya mauti (usingizi) na sote siku moja tutakusanywa Kwake" (Bukhari).

Wakati wote yeye alitamani ukaribu wa Mwenyezi Mungu, na moja ya dua zake alizozirudiarudia ilikuwa hivi "Ee Allah! Nijaze nuru Yako moyoni na nijaze nuru Yako machoni na nijaze nuru Yako masikioni na niwekee nuru Yako kuumeni na niwekee nuru Yako kushotoni na niwekee nuru Yako juu yangu na niwekee nuru Yako chini yangu na niwekee nuru Yako mbele yangu na niwekee nuru Yako nyuma yangu na Ee Allah, mimi mzima nigeuze nuru Yako" (Bukhari).

Hadhrat Ibn Abbas[ra] yuwasimulia kwamba: "Muda mfupi kabla ya kifo cha Mtume[saw], Musailima (yule kadhabu) alikuja Madina na kutangaza ya kuwa kama Muhammad akitokea kumchagua yeye awe mrithi wa Utume wake basi atakuwa tayari kumwamini. Musailima aliandamana na genge kubwa mno na kabila alilofungamana nalo lilikuwa ndilo kabila kubwa zaidi miongoni mwa makabila ya Arabuni. Alipopashwa habari za kufika kwake, Mtume[saw] alienda kukutana naye, akiandamana na Hadhrat Thabit[ra] bin Qais bin Shams[ra]. Mkononi mwake alikuwa na tawi kavu la mtende. Alipofika kambini kwa Musailima akaenda akajikita mbele yake. Wakati huo baadhi ya Masahaba wake wengine walikuwa wamekwisha jitokeza na kujipanga kumzunguka. Mtume[saw] akitamka kumwambia Musailima alisima, "Imenifikia ya kuwa wewe umesema kwamba ingetokea mimi kukuchagua uwe mwandamizi wangu basi ungekuwa tayari kuniamini, lakini siwezi kukutunukia wewe hata hili kole kavu la mtende kinyume na amri za Mwenyezi Mungu. Wewe utaishilizia vile Mwenyezi Mungu alivyokujaalia. Ukinikataa basi Mwenyezi Mungu atakutia komesha. Mimi naona dhahiri shahiri kwamba Mwenyezi Mungu atakuchukulia ile hatua aliyonifunulia." Kisha akaongeza akimwambia: "Sasa mimi naenda zangu. Ukiwa na chochote cha kuongezea, basi waweza ukasema na Thabit bin Qais bin Shams ambaye atakuwa mwakilishi wangu." Kisha akarudi. Hadhrat Abu

Huraira[ra] pia alikuwepo. Mtu mmoja akamwuliza Mtume[saw] alimaanisha nini aliposema kwamba Mwenyezi Mungu atatokea kumchukulia Musailima ile hatua aliyomfunulia. Mtume Mtukufu[saw] akjibu akisema: "Mimi niliota bangili mbili mikononi mwangu ambazo sikuzipenda. Nikiwa bado ndotoni niliambiwa na Mwenyezi Mungu nizipulizie. Nilipozipulizia, zote mbili zikatoweka. Mimi naiona ndoto hii kuwa na maana ya kwamba patatokea mitume bandia wawili baada yangu" (Bukhari, Kitabul Maghaazi). Kisa hiki kilitokea karibu na mwisho wa maisha ya Mtume[saw]. Kabila la mwisho na kubwa zaidi miongoni mwa makabila ya Waarabu waliokuwa bado kumkubali lilikuwa tayari kumkubali na sharti la pekee walililoliweka lilikuwa ni hili ya kwamba Mtume[saw] amchague chifu wao awe mwandamizi wake. Kama Mtume[saw] angelikuwa yu mwenye kufuata hata kidogo matamanio ya kibinafsi, basi hapakuwa na chochote cha kumzuia asijinyakulie umoja wa Arabuni nzima kwa kumwahidia urithi wake chifu wa kabila kubwa zaidi nchini Arabuni. Mtume[saw] hakuwa na mwana na hapana tamaa yoyote ya kuanzisha silsila ya kifalme ingeliyoweza kuzuia mapatano kama hayo, lakini yeye hakuihesabu hata chembe kuwa ni chembe yake na kuwa iko chini ya idhini yake kabisa. Hivyo basi, asingeliweza kuuchezea uongozi wa Waislamu kana kwamba ulikuwemo ndani ya zawadi yake. Yeye aliuchukulia kuwa ni amana takatifu na aliamini kwamba Mwenyezi Mungu angeikabidhi yeyote atakayemwona kuwa yuwafaa. Kwa hiyo, yeye akalikatalia mbali pendekezo la Musailima na kumwambia kwamba achilia mbali uongozi wa Waislamu, yeye hakuwa tayari kumkabidhi hata kole kavu la mtende.

Kila mara alipozungumzia au kugusia juu ya Mwenyezi Mungu, machoni pa watu ilionekana kana kwamba dhati yake nzima ilikuwa imejawa na mapenzi juu ya Mwenyezi Mungu na hali ya kujitupa kwake.

Daima yeye alisisitizia urahisi katika ibada ya Mwenyezi Mungu. Ule msikiti alioujenga kule Madina na ambao ndani yake yeye siku zote aliongoza sala, ulikuwa sakafu ya udongo tu ambayo haikuwa na

majamvi wala mikeka, na paa lililokuwa limefunikwa kwa matawi na majani makavu ya mtende, lilivuja kila kuliponyesha mvua. Wakati kama huo Mtume Mtukufu[saw] na maamuma wote wangeliloa maji na matope lakini yeye alikuwa akiendelea na sala hadi mwisho wala hakupata wakati wowote kuonesha ishara kuwa ataiahirisha sala au kwenda kusali mahali pengine. (Bukhari, Kitab al-Saum)

Aidha yeye alikuwa yu mwangalifu kuwahusu Mashaba wake. Hadhrat Abdullah bin Umar[ra] alikuwa ni mtu mwenye hali ya unyofu mkubwa na utawa maishani. Kumhusu yeye safari moja Mtume Mtukufu[saw] alitamka akisema: "Abdullah bin Umar angelizidi kuwa mwema kama angetokea kudumisha zaidi sala yake ya *Tahajjud.* Ilipofikishiwa habari hii Hadhrat Abdullah bin Umar[ra] tangu wakati huo hakukosa tena sala hii. Imeandikwa kwamba alipotokea kuwemo nyumbani mwa bintiye Hadhrat Fatima[ra], Mtume Mtukufu[saw] alimwuliza yeye na mkewe Hadahrat Ali[ra], ikiwa wao walidumisha sala ya Tahajjud. Hadhrat Ali[ra] akajibu akisema: "Ewe Mtume wa Allah! Twajaribu kuamka kusali Tahajjud lakini pale anapotaka Mwenyezi Mungu kiasi cha sisi kutoweza kuamka wakati wake basi tunaikosa." Mtume Mtukufu[saw] akaenda zake na njiani akakriri mara kadha aya ya Kurani inayomaanisha kwamba mara nyingi mtu hawi tayari kukiri makosa yake na hujaribu kuyatafutia visingizio (Bukhari, Kitabul Kusuuf). Mtume[saw] alikuwa na maana ya kwamba Hadhrat Ali[ra] asingelimnasibishia makosa yake Mwenyezi Mungu kwa kusema anapotaka Mwenyezi Mungu kwamba wao wasiamke wakati wa Tahajjud wao hawakuwa wakiamka wakati wake, bali yeye angelikiri makosa yake katika jambo hili.

KAKATAZA KITUBIO

Mtume Mtukufu[saw] alikataza sana ada katika jambo hili la ibada na akalaumu mtu kujipatia kitubio kuwa kama aina ya ibada. Yeye alifundisha ya kuwa ibada halisi ilikuwa ni kuvitumia vyema vipawa Mwenyezi Mungu alivyomjazi mwanadamu. Kama Mwenyezi Mungu kampatia mwanadamti macho ya kuonea, isingelikuwa ibada bali

kitubio kuyafumba macho au kuyafanya yang'olewe mbali. Sio matumizi mwafaka ya macho yawezayo kuhesabiwa kuwa ni dhambi, bali ni matumizi yasiyofaa ya kipawa hiki yanayoweza kuwa dhambi. Ingelikuwa ni utovu wa hisani kwa upande wa mtu kujiachilia aondolewe uwezo wa kusikia, ingawaje ingelikuwa ni dhambi kwake yeye kukitumia kipawa hiki kusikilizia masingizio na masengenyo. Kuacha chakula (isipokuwa pale kunapopendezwa au kwa namna fulani kuwe kunafaa) kunaweza kukaishilizia kujiua na hapo kukawa ni dhambi lisilosameheka, ingawaje lingekuwa pia ni dhambi kwa upande wa mtu kushiriki kula na kunywa peke yake au kuingilia ulaji na unywaji wa vitu vilivyoharamishwa au visivyotakikana. Hii ndiyo sera mufti iliyofundishwa na kuhimizwa na Mtume Mtukufu[saw] wa Islam na ambayo haikuwa imefundishwa na Nabii yeyote wa hapo kabla.

Matumizi sawa ya vipawa vya kimaumbile ndio tabia njema hasa; kuvizuilia au kuvipuuzilia mbali vipawa vile ni upumbavu mtupu. Matumizi yasiyofaa ya vipawa hivi ndio ubaya au dhambi. Matumizi yafaayo ni wema. Hiki ndicho kiini cha yale mafundisho ya tabia njema yaliyofundishwa na Mtume Mtukufu[saw] wa Islam. Na kwa ufupi, hii hii pia ndiyo picha ya maisha yake mwenyewe na matendo yake. Hadhrat Aisha[ra] yuwasimulia kwamba: "Wakati wowote Mtume Mtukufu[saw] alipotokea kuwa na nafasi ya kuchagua hili au lile daima yeye alichagua lililo rahisi zaidi baina ya hayo mawili, mradi liwe limeepukana na tashwishi zote na madhambi. Ilipotokea hatua yoyote kuweza kuzusha tashwishi kama hizo, Mtume Mtukufu[saw] miongoni mwa wanaume wote aliikwepa kwa mbali mno". (Muslim, Kitabul Fadha'il). Hii kwa hakika ndiyo njia yenye kuvutia zaidi mwanadamu aliyo nayo. Watu wengi kwa hiari hujionjesha machungu na dhiki, si kwa sababu ya kujipatia radhi ya Mwenyezi Mungu, kwani radhi ya Mwenyezi Mungu haipatikani kwa mtu kujionjesha machungu na dhiki zisizokuwa na maana, kwa sababu tu ya kuwadanganya wanadamu. Watu sampuli hiyo wana wema kidogo tu wa kuzaliwa nao na hutafuta kuziba upungufu huu wao na kujipatia sifa machoni pa wengine kwa kujivisha wema bandia. Lakini

shabaha ya Mtume Mtukufu[saw] wa Islam, ilikuwa ni kufikia wema halisi na kujichumia radhi ya Mwenyezi Mungu. Yeye, hivyo basi, aliepukana kabisa na huu walakini wa kujifanya na kujisingizia. Suala kwamba dunia imwone kuwa mbaya au kumsifu kuwa yu mwema lilikuwa ni kitu yeye asichokijali asilani. Kilichokuwa muhimu kwake yeye ilikuwa ni vile alivyojikuta na vile Mwenyezi Mungu angelivyomuhesabu. Kama pamoja na ushuhuda wa nafsi yake na radhi ya Mwenyezi Mungu alijichumia pia ushahidi halisi wa wanadamu yeye alishukuru, lakini kama watu walimtazama kwa jicho la husuda yeye aliwahurumia wala hakutilia maanani maoni yao.

TABIA YAKE KWA WAKEZE

Yeye alikuwa na huruma sana na mwema kwa wakeze. Kama wakati mwingine mmoja wao yeyote hakujistahi na kuwa na tofauti naye yeye alitabasamu tu na kuyasahaulia mbali. Siku moja alisema na Hadhrat Aisha[ra] akimwambia: "Aisha, kila mara unapoudhika nami daima mimi hayo huyajua." Hadhrat Aisha[ra] akauliza akisema: "Inakuwakuwaje?" Mtume[saw] akasema: "Mimi nimegundua kwamba unaponifurahikia na kwenye mazungumzo wataka kumtaja Mwenyezi Mungu, basi wewe humwita Mola wa Muhammad. Lakini unapokuwa umeudhika name hapo wewe humwita Mola wa Ibrahim." Kusikia hivyo, Hadhrat Aisha[ra] akacheka na kukubaliana naye (Bukhari, Kitabun-Nikah). Hadhrat Khadija[ra] alikuwa ndiye mkewe wa kwanza na alikuwa amejitolea sana kwake. Yeye alikuwa na umri mkubwa kuliko Mtume[saw]. Baada ya kifo chake yeye alioa wachanga lakini hakujiruhusu kumsahau Hadhrat Khadija[ra]. Kila mara rafiki yeyote wa Hadhrat Khadija[ra] alipofika, Mtume[saw] alikuwa akiinuka kumkaribisha (Muslim). Alipotokea kuona kitu chochote kilichokuwa cha Hadhrat Khadija[ra] au kilichohusikana naye, daima yeye alipatwa na huzuni. Miongoni mwa wafungwa waliotekwa na Waislamu katika vita vya Badr alikuwa ni mkewe Mtume[saw]. Hakuwa na chochote cha kujikombolea. Mkewe Zainab (bintiye Mtume[saw]) akapeleka Madina mkufu uliokuwa ni mali ya mamake (Hadhrat Khadija[ra]) na akautoa kama fidia kwa ajili ya mumewe. Mtume[saw] alipouna mkufu ule

akautambua na kuhuzunika sana. Akatamka kwa Masahaba wake akiwaambia: "Mimi sina ruhusa ya kutoa maagizo yangu katika jambo hili, lakini mimi nafahamu sana kwamba mkufu huu wapendwa sana na Zainab kama kumbukumbu ya mwisho ya mamake na ikiwa mko radhi, basi mimi ningesema asipokonywe na mkufu huu arudishiwe." Wakasema hapana jingine la kuwafurahisha zaidi ya hilo na kulikubali pendekezo lake mara moja (Halabiyya, J. 2). Mara nyingi yeye alimsifu Hadhrat Khadija[ra] mbele ya wakeze wengine na kutilia mkazo wema wake na jinsi alivyojitolea katika njia ya Islam. Kwenye kisa kama hiki safari moja Hadhrat Aisha[ra] alisononeka na akatamka akisema: "Ewe Mtume wa Allah, inakuwaje wewe kuendelea kumtaja mama huyo kizee? Mwenyezi Mungu amekujazi wake wachanga na warembo zaidi." Mtume Mtukufu[saw] akajawa na huzuni na akabisha akisema: La, la, Aisha[ra]! Wala hujui ni jinsi gani Khadija alivyokuwa mwema kwangu" (Bukhari).

HULKA ZAKE TUKUFU

Yeye daima alikuwa mvumilivu sana kwenye dhiki. Hakukatishwa tamaa abadan na hali ya dhiki wala hakuruhusu matamanio yoyote ya kibinafsi kumtawala. Tayari imekwisha simuliwa kwamba babake alikuwa amefariki kabla hajazaliwa na mamake alifariki akiwa yeye bado yu mtoto mdogo. Hadi kufikia umri wa miaka minane, yeye alikuwa chini ya ulezi wa babuye, na baada ya kifo cha babuye yeye akawa chini ya ulezi wa amiye, Mzee Abu Talib. Kwa sababu ya mapenzi ya kidugu na pia kwa sababu yeye alikuwa amepewa nasaha maalumu na babake juu ya jambo hili, Mzee Abu Talib daima alimtunza mpwawe kwa makini lakini mkewe mambo haya hayakumwingia sana moyoni. Mara nyingi yeye alitokea kuwagawia kitu watoto wake akimnyima binamu wao. Kama angelitokea Mzee Abu Talib kufika nyumbani wakati wa kisa kama hiki basi angelimkuta mpwawe mdogo akijikalia kando kwa heshima bila ya alama yoyote ya kuhuzunika usoni mwake. Hapo huyu ami huku akihimizwa na mwako wa upendo na kutambua wajibu wake, angelitokea kumwendea mpwawe, kumkumbatia na kutoa mwito

akisema: "Huyu mwanangu naye pia mwangalie! Huyu mwanangu naye pia mwangalie!" Visa sampuli hii sio eti havikuwa vya kawaida na wale waliovishuhudia walikubaliana katika ushahidi wao kwamba mtoto Muhammad hakupata kabisa kuonesha ishara ya kuathiriwa navyo au kwamba aliwaonea mabinamu zake wivu wowote. Baadaye maishani alipokuwa yeye katika hali ya kuweza kufanya hivyo, alichukua jukumu la utunzaji na ulezi wa wana wawili wa binamuye, Ali na Ja'far, na akatimiza wajibu huu kwa njia iliyo bora zaidi.

Mtume Mtukufu[saw] maisha yake mazima, ilimbidi kukabiliana na msururu wa machungu. Yeye alizaliwa yatima, mamake alifariki yeye alipokuwa akali mtoto mdogo, na akapoteza babuye katika umri wa miaka minane. Baada ya kuoa ikambidi kuvumilia vifo vya watoto kadha, mmoja baada ya mwingine, na kisha kifo cha mkewe mpendwa Hadhrat Khalija[ra]. Baadhi ya wakeze aliooa baada ya kifo cha Hadhrat Khadija[ra] walifariki maishani mwake na karibu na mwisho wa uhai wake yeye alilazimika kuvumilia kifo cha mwanawe Ibrahim. Misiba hii yote na maafa yeye akayavumilia kwa uchangamfu, na hapana mojawapo la mambo haya lililoathiri hata chembe azima yake kubwa au hali yake ya utumwema. Huzuni zake za kibinafsi hazikujitokeza hadharani abadani na daima yeye alikutana na kila mtu kwa uso wa huruma na wote akawatendea kwa namna moja kwa ukarimu ule ule. Safari moja alimkuta mama mmoja aliyefiliwa na mtoto wake akiomboleza kwa mayowe kwenye kaburi la yule mtoto. Akamnasihi awe na subira na kukubali kudura ya Mwenyezi Mungu. Yule mama hakuwa na habari kwamba alikuwa akizungumziwa na Mtume Mtukufu[saw] na akajibu akisema: "Wewe ungekuwa umepata kufiliwa na mtoto kama vile nilivyofiliwa mimi, basi ungetambua ni vigumu jinsi gani kuwa mvumilivu katika msiba kama huu." Mtume[saw] akamwambia: "Mimi sikufiliwa na mtoto mmoja tu bali na watoto saba," na akajiendea zake. Isipokuwa pale alipogusia misiba yake yeye mwenyewe kwa njia ya kupitia kando, hakuona haja ya kuieleza sana wala hakuiruhusu misiba hii kuingilia huduma zake za dawamu kwa wanadamu na bashasha yake ya kushirikiana nao katika shida zao.

HALI YA KUJITAWALA NAFSI

Daima yeye aliitawala nafsi yake kabisa. Hata pale alipokuwa ni Mtawala yeye kila mmoja alimtegea sikio kwa makini, na kama ilitokea mtu kumfanyia ufidhuli alimvumilia tu wala hakujaribu kumlipiza kisasi. Pande za Mashariki, njia moja ya mtu kumwonesha heshima yule anayezungumza naye ni kutomwita jina lake mwenyewe. Waislamu walizoea kumwita Mtume Mtukufu[saw] "Ewe Mtume wa Allah", na wasiokuwa Waislamu walimwita "Abu Kasim" (Babake Kasim: Jina Kasim lilikuwa ni la mmoja wa wanawe). Safari moja Myahudi alimjia mjini Madina na kuanza kuongea naye. Wakati wa maongezi yule Myahudi akarudiarudia kumwita "Ewe Muhammad, "Ewe Muhammad", Mtume[saw] hakujali alivyoitwa na Myahudi yule na akaendelea kwa subira kumwelezea jambo walilokimzungumzia. Hata hivyo, Masahaba wake hamaki zilikuwa zikiwachemka kwa ule utovu wa heshima aliokifanyiwa na yule aliyekuwa akizungumza naye hadi mmoja wao, kwa kutoweza kujizuia zaidi, akamwonya yule Myahudi kutoendelea kumwita Mtume[saw] kwa njia ile bali amwite Abul Kasim. Yule Myahudi akasema kwamba atamwitu tu kwa lile jina ambalo wazazi walikuwa wamempatia. Mtume[saw] akatabasamu na akatamka akiwaambia Masahaba wake: "Hakukosea. Nilipozaliwa mimi niliitwa Muhammad na hapana haja ya kuchukizwa na vile anavyoniita."

Wakati mwingine watu walimsimamisha njiani na kuzungumza naye, kuelezea haja zao na kumfikishia matakwa yao. Daima yeye alisimama kwa utulivu akiwaacha wazungumze na hakuondoka mpaka walipomaliza. Wakati mwingine watu walipokuwa wanampa mkono waliushika mkono wake kwa muda na ingawaje huu uliuona ni usumbufu na pia ulipoteza wakati muhimu, lakini yeye hakupata kuwa wa kwanza kuondolea mbali mkono wake. Watu walimwendea bila kizuizi na kumfikishia dhiki zao na shida zao na kumwomba msaada. Alipotokea kuweza kuwasaidia yeye hata mara moja hakukataa kuwasaidia. Wakati mwingine alitiririshiwa maombi na yakasisitiziwa visivyo lakini yeye akaendelea kuyatekeleza kadiri

alivyoweza. Penginepo baada ya kumtimizia mtu ombi lake, alikuwa yeye akimnasihi mhusika kuzidi kumtegemea Mwenyezi Mungu na kuepukana na kuwataka wengine msaada. Safari moja Mwislamu mmoja mwenye ikhlasi alimwomba pesa mara kadha naye akamtimizia haja yake lakini hatimaye akasema: "Ni afadhali kwa mtu kumtegemea Mwenyezi Mungu na kuepukana na omba-omba." Yule mhusika alikuwa ni mtu mwaminifu. Kwa kujali heshima ya Mtume[saw], hakuridhia kurudisha kile alichokuwa amepewa lakini alitangaza kwamba huko mbele yeye hatamtaka msaada yeyote yule hata pakitokea nini. Miaka mingi baadaye, alikuwa akipigana vitani, juu ya mnyama wa vita, na vita vilipopamba moto na ghasia na mwako wa silaha kufikia kileleni naye kuzungukwa na maadui, mjeledi wake ukamdondoka. Askari mmoja Mwislamu aliyekuwa pale chini, kwa kujua tatizo la mwenzake, akainama kumwokotea mjeledi wake lakini huyu askari mpanda mnyama akamkataza na akaruka chini kujiokotea mwenyewe mjeledi wake, huku akimjulisha yule mwenzake kwamba kwa muda mrefu yeye alikuwa amemwahidi Mtume Mtukufu[saw] kwamba hatamtaka yeyote msaada na kama angetokea kumwacha mwenzake amwokotee mjelidi wake basi kwa njia fulani huko kungelikuwa ni kutaka msaada kungelikoweza kumtia kwenye hatia ya kuvanja ahadi aliyomwahidi Mtume Mtukufu[saw].

HAKI NA MAADILI

Waarabu walikuwa wakishikilia sana tabia ya upendeleo nao wao huyu walimtendea hivi na huyu wakamtendea vile. Hata miongoni mwa yale mataifa yasemekanyo eti ni mastaarabu mtu huona pana kusitasita kuwatia mbaroni watu wakubwa wakubwa au wale wenye madaraka makubwa makubwa kuwahoji matendo yao, ingawaje sheria hutumiwa vikali dhidi ya raia wa kawaida. Lakini, Mtume Mtukufu[saw] alikuwa ni mtu wa kipekee kabisa katika kushikilia haki na maadili. Safari moja kesi ilifikishwa kwake ambamo msichana mmoja wa familia tukufu alipatikana na hatia ya wizi. Jambo hili lilizusha hofu kubwa kwani, ingelitokea adhabu kupewa yule kijana wa kike, basi familia yenye kuheshimika ingelitiwa dosari na

kuaibishwa. Wengi walitamani kumtetea kijana yule wa kike mbele ya Mtume[saw] lakini waliogopa kufanya hivyo. Hatimaye Hadhrat Usama[ra] akatwishwa jukumu la kufanya uombezi huo. Hadhrat Usama[ra] alifika kwa Mtume[saw], lakini kusikia tu vile alivyoliwasilisha jambo lenyewe Mtume[saw] akakasirika sana na akatamka akimwambia: "Yafaa ukome. Mataifa yameangamia kwa sababu ya hii desturi ya kuwafanyia mapendeleo watu wakubwa wakubwa huku wakiwabana raia wa kawaida. Islam hairuhusu mambo sampuli hii nami sitafanya hivyo asilini. Wallahi, angelitokea binti yangu mwenyewe, Fatima, kufanya uhalifu mimi nisingelisitasita kutoa adhabu iliyohakiki" (Bukhari, Kitabul Huduud).

Tayari imekwishaelezewa kwamba aliposhikwa mateka katika vita vya Badr, Mzee Abbas, amiye Mtume[saw], yeye kama mateka wengine alitiwa kamba asiweze kuponyoka. Kamba zenyewe zikatokea kukazwa sana hivi kwamba yeye alilia kwa maumivu. Mtume[saw] akamsikia akilia na hakuweza kupata usingizi. Masahaba wa Mtume[saw] wakaing'amua hali hii, na wakalegeza kamba za mzee Abbas. Alipopata habari hii Mtume[saw] akatoa amri wafungwa wote watendewe sawa, akiongeza kwamba hapakuwepo na sababu ya kumfadhili jamaa yake mwenyewe. Akasisitiza kwamba ni sharti wawalegeze kamba mateka wote la sivyo Mzee Abbas wamkaze kamba sawa na mateka wengine. Kwa vile Masahaba wa Mtume[saw] walichelea kutomhangaisha tena kwa sababu ya amiye wakakata shauri mateka wawazidishie ulinzi na wote wawalegeze kamba (Zurqani, J. 3, uk. 279).

Hata katika hali ya vita yeye alikuwa mwangalifu katika kuzitilia maanani kanuni zote zilizokubaliwa na miadi iliyowekwa. Safari moja yeye alituma kikosi cha Mashaba wake kwenye harakati za kushika doria. Wakakumbana na watu kadha wa upande wa maadui kwenye siku ya mwisho ya Mwezi Mtukufu wa Rajab. Ikiwa wao kufikiria kwamba labda ilikuwa hatari kuwaachilia waponyoke na kufikisha Makka habari za walinda doria wa Kiislamu kuja karibu sana, wakawashambulia na katika kindumbwendumbwe kilichofuatia

mmoja wao akauawa. Baada ya kile kikosi cha walinda doria kuwa kimerejea Madina watu wao wakaanza kulalamika ya kuwa wale walinda doria walikuwa wamemuua mmoja wa watu wao katika mwezi Mtukufu wa Rajab. Wenyewe watu wa Makka mara nyingi walikuwa na hatia ya kutangua utukufu wa Miezi Mitukufu dhidi ya Waislamu kila walipopenda, na lingelikuwa kwao wao jawabu tosha kusema kwamba kwa vile watu wa Makka walikuwa wao wenyewe wamevunjilia mbali mapatano kuhusu miezi mitakatifu, basi hawakuwa na haki ya kusisitizia kutiliwa maananni kwa mapatano hayo na Waislamu. Lakini Mtume[saw] hakuchagua jawabu hili. Yeye aliwakaripia vikali walinda doria wale, akakatalia mbali walivyoviteka na kulingana na ripoti zingine hata fidia yeye alimlipia yule mtu aliyeuawa, hadi pale kufunuliwa kwa aya ya 218 ya Sura Al-Baqara kulipouambua ukweli wa mambo yalivyo (Tabari na Halbiyya).

Watu kwa kawaida huwa waangalifu wasiwakasirishe marafiki na ndugu zao lakini Mtume Mtukufu[saw] katika uwanja huu alikuwa mwangalifu hata kuwahusu wale waliokuwa wakimpinga. Safari moja Myahudi alifika kwake akilalamika kwamba Hadhrat Abu Bakr[ra] alikuwa amemwudhi kwa kusema kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa amemtukuza Muhammad kuliko Musa. Mtume[saw] akamwita Hadhrat Abu Bakr[ra] na kumwuliza kilichotokea. Akielezea, Hadhrat Abu Bakr[ra] akasema kwamba yule Myahudi ndiye aliyaanza kwa kusema kwamba naapa kwa Musa ambaye Mwenyezi Mungu alikuwa amemnyanyua zaidi ya wanadamu wote, nami hapo nikamjibu kwa kuapa kwa Muhammad, ambaye Mwenyezi Mungu amemnyanyua zaidi ya Musa. Mtume[saw] akasema: "Haikufaa kusema hivyo kwani maono ya wengine hayana budi kustahiwa. Mtu na asinitukuze kuliko Musa" (Bukhari, Kitabut-Tauhid). Hii haikumaanisha kwamba kwa kweli Mtume Mtukufu[saw] hakuwa na manzili ya juu kuliko Nabii Musa[as] lakini kwamba ukweli kama huu kuambiwa Myahudi ulielekea kumwudhi na ilikuwa ni afadhali kutotamkwa.

KUWAJALI MASKINI

Mtume Mtukufu[saw] daima alikazania sana kunawirisha hali za wale walio maskini katika jamii na kukuza hadhi yao. Safari moja alipokuwa ameketi na Masahaba wake, mtu mmoja tajiri alipitia pale. Mtume[saw] akmwuliza mmoja wa Masahaba wake vile alivyomchukulia tajiri yule. Sahaba akajibu akisema: "Yeye ni tajiri mwenye kujulikana. Kama angetokea kutaka kumposa msichana basi posa hiyo ingekubaliwa na kama angetokea kumfanyia mtu uombezi basi uombezi huo ungekubaliwa." Punde si punde, akapita mtu mwingine aliyeonekana ni maskini na asiyekuwa na chochote. Mtume,[saw] akamwuliza Sahaba yule yule vile alivyomchukulia mtu huyu. Sahaba akajibu akisema: "Ewe Mtume wa Allah! Yeye ni mtu maskini. Kama angetokea kutaka kumposa msichana basi posa hiyo isingekubaliwa na kama angetokea kumfanyia mtu uombezi basi uombzi huo ungekataliwa na kama angetokea kutaka kuzungumza na mtu yeyote basi pasingekuwa na wa kumtilia maanani."

Kusikia hivyo Mtume[saw] akasema: "Huyu mtu maskini thamani yake ni kubwa zaidi ya thamani ya lundo la dhahabu liwezalo kuujaza ulimwengu mzima. (Bukhari, Kitabur-Riqaaq).

Mwanamke mmoja Mwislamu maskini alikuwa akifagia msikiti wa Mtume Mtukufu mjini Madina. Mtume[saw] hakumwona tena msikitini kwa muda wa siku kadha na akataka kujua habari zake. Akaambiwa yule mwanamke alikuwa amefariki. Akasema: "Mbona sikujulishwa alipofariki? Mimi nigelitamani kuwemo katika sala yake ya jeneza," na akazidi kutamka akisema, "Penginepo nyinyi hamkumtilia maanani kwa sababu alikuwa maskini. Na hivyo sivyo. Twendeni mkanioneshe kaburi lake." Hapo yeye akafika kwake kaburini na akamwombea (Bukhari, Kitabus Salaat). Alikuwa akisema kunao akina-manywele wenye miili iliyojaa mavumbi na ambao hawajongelewi na watu matajiri lakini ambao wanathaminiwa sana na Mwenyezi Mungu kiasi hiki kwamba kama, katika kumtegemea Mwenyezi Mungu upaji wake, wao wangetokea kuapa kwa jina Lake

kwamba jambo fulani litaishilizia kitu fulani basi Yeye angeliwaridhia." (Muslim, Kitabul-Birr was-Sila). Safari moja baadhi ya Masahaba wa Mtume Mtukufu[saw] waliokuwa ni watumwa waachiliwa huru walikuwa wameketi pamoja na akatokea kupita karibu yao Abu Sufyan aliyekuwa ni chifu miongoni mwa Makureishi na aliyekuwa amewapiga vita Waislamu hadi kufikia kusarenda kwa mji wa Makka na alikuwa amesilimu tu kwenye tukio hilo. Walipokuwa wakisema naye, hawa Masahaba wakamkumbusha ushindi Mwenyezi Mungu alioipatia Islam. Hadhrat Abu Bakr[ra] naye pia akasikia maneno haya na hakufurahia chifu wa Makuraishi kukumbushwa fedheha zao na akawakaripia wale Masahaba. Kisha akaenda kwa Mtume[saw] na akamsimulia kisa hicho. Mtume[saw] akasema: "Ewe Abu Bakr! Umenitia wasiwasi, huenda wewe umewaudhi hawa watumishi wa Mwenyezi Mungu. Ikiwa ni hivyo, basi anaweza Mwenyezi Mungu kukukasirikia." Mara moja Hadhrat Abu Bakr[ra] akawarudia wale watu na akawauliza akisema: "Ndugu zanguni! Yale niliyoyasema yaliwaudhini?" Ambapo wao walimjibu wakisema: "Hayakutuudhi. Mwenyezi Mungu na akusamehe!" (Muslim, Kitabul-Fadhaa'il).

Ingawaje Mtume[saw] alisisitiza kwamba maskini waheshimiwe na kutoudhiwa na akajitahidi kuwatimizia haja zao, yeye pia alinuia kuwafanya wawe ni watu wenye kujistahi na akawafundisha kutokuwa ombaomba. Sio stahili ya mtu maskini kutaka atosheke na tende moja au mbili au na tonge moja au mawili ya chakula bali kujizuia asiombe, hata ajaribiwe vikali kiasi gani (Bukhari, Kitabul-Kusuuf). Kwa upande mwingine yeye alikuwa akisema kwamba hapana karamu itakayobarikiwa isipokuwa maskini nao pia waalikwe. Hadhrat Aisha[ra] yuwasimulia kwamba mwanamke mmoja maskini alikuja kumtembelea safari moja akiandamana na mabinti zake wadogo wawili. Wakati ule Hadhrat Aisha[ra] hakuwa na chochote ila tende moja ambayo alimpatia yule mama. Naye akaigawanyia mabinti zake wadogo na wote wakaenda zao. Mtume[saw] aliporejea nyumbani Hadhrat Aisha[ra] akamasimulia kisa kile naye akatamka akisema:

"Kama mtu maskini akiwa nao mabinti na anawatendea kwa huruma, basi Mwenyezi Mungu atamwepushia adhabu ya Jahanamu, na akazidi kusema: "Mwenyezi Mungu atamjazi Pepo huyu mama kwa sababu ya huruma aliyowafanyia mabintize" (Muslim). Safari moja aliambiwa kwamba mmoja wa Masahaba wake, Hadhrat Sa'd[ra] aliyekuwa ni mtu tajiri, alikuwa akijigambia maarifa yake mbele za watu wengine. Aliposikia hayo Mtume[saw] akasema: "Mtu na asifikirie kwamba utajiri wake au hadhi au uwezo eti ni matokeo ya jitihada yake au maarifa. Hivyo sivyo ilivyo. Uwezo wako na cheo chako na utajiri wako hivyo vyote huchumwa kwa njia ya maskini." Moja ya dua zake ilikuwa hivi "Ee Mwenyezi Mungu! Nidumishe mnyenyekevu niwapo hai na nidumishe mnyenyekevu nifapo na ufanye ufufuzi wangu hapo Siku ya Hukumu uwe ni miongoni mwa wanyenyekevu" (Trmidhi, Abwabuz-Zuhd).

Safari moja, majira ya kiangazi, alipokuwa akipita njiani alimwona Mwislamu mmoja maskini akisomba mizigo mizito kutoka huku hadi kule. Umbo lake lilikuwa ghafi-ghafi hivi alijawa na jasho na vumbi. Alikuwa na sura ya kuhuzunika. Mtume Mtukufu[saw] akamnyatia kutoka upande wa nyuma na, chambileche vile watoto wanavyotaniana wakati mwingine, akmnyooshea mikono na na kumziba macho yake, akimtarajia kubahatisha huyu alikuwa nani. Yule mtu naye akanyoosha mikono yake kinyumenyume na huku akigusa mwili wa Mtume[saw] akatambua kwamba huyu ndiye Mtume Mtukufu[saw] mwenyewe. Pengine pia zilimjia hisia kwamba asingelitokea mtu mwinginewe kumwonyesha mtu mwenye hali kama yake upendo sampuli ile. Akijawa na furaha na uchangamfu, akazidi kujigandamiza na Mtume[saw] huku mwili wake wenye jasho na mavumbi akiusuglia nguo za Mtume[saw], akitamani pengine kujua ni kwa muda gani Mtume Mtukufu angelitaka kumtania vile. Mtume[saw] akaendelea kutabasamu tu bila kumtaka akome. Yule mtu alipokuwa sasa ni furaha tupu Mtume[saw] akatamka akimwambia: "Mimi nina mtumwa wangu; waona mtu yeyote atataka kumnunua?" Yule

akatambua kwamba pengine hakuwepo yeyote duniani, isipokuwa Mtume Mtukufu mwenyewe[saw] angeliyeweza kumthamini, na kwa kite cha huzuni akajibu akisema: "Ewe Mtume wa Allah! Hapana yeyote humu duniani wa kuwa tayari kuninunua mimi." Mtume[saw] akasema: "Hapana! Hapana! Usiseme hivyo. Wewe una thamani kubwa machoni pa Mwenyezi Mungu (Sharhus-Sunna).

Si tu kwamba yeye mwenyewe alichungulia kwa makini masilahi ya maskini bali wakati wote aliwahimiza watu wengine wafanye vivyo hivyo. Hadhrat Abu Ash'ari[ra] yuwasimulia kwamba kama alitokea mtu maskini kuja kwa Mtume Mtukufu[saw] na kutaka msaada, basi yeye alizoea kuwahimiza wale waliopo akiwaambia, nyinyi pia mwatakiwa kulichangia ombi hili kusudi mpate thawabu kwa kuwa wachangiaji kwenye kuhamasisha tendo jema (Bukhari na Muslim), shabaha yake ikawa ni kwa upande mmoja kuingiza nafsini mwa Masahaba hisia za kiherehere cha kuwasaidia maskini na kwa upande mwingine mwingine kuwafanya maskini wenyewe watambue upendo na huruma wanayofanyiwa na ndugu zao wanaojiweza.

KULINDA MASILAHI YA MASKINI

Wakati Islam ilipoanza kukubaliwa katika sehemu iliyo kubwa zaidi ya Arabuni, mara kwa mara Mtume Mtukufu[saw] alipokea vitu vingi na pesa ambapo yeye kwa upesi alizigawanya miongoni mwa watu maskini. Safari moja bintiye, Hadhrat Fatima[ra], alimjia na, huku akimwonesha vifumba vya mikono yake vilivyokuwa vimefanywa sugu na kazi zake za nyumbani za kusaga nafaka kwa kutumia mawe, akamtafadhalisha kwamba apatiwe mjakazi wa kumsaidia. Mtume[saw] akajibu akisema: "Mimi nitakwambia jambo litakalotokea kuwa ni bora zaidi ya mjakazi. Utakapokwenda kulala basi Mtukuze Mwenyezi Mungu (ukisema Subhaanallah) mara thalathini na tatu, na zitangaze sifa Zake njema (ukisema Alhamdu Lillahi) mara hizo hizo na utangaze ukuu Wake (ukisema Allahu Akbar) mara thalathini na nne. Huu ni uradi utakaokusaidia kwa kiwango kikubwa mno kuliko kuwa na mjakazi (Bukhari).

Safari moja alipokuwa akigawanya pesa, sarafu moja ilimdondoka na ikafichama. Alipomaliza kugawanya alikwenda msikitini na akaongoza sala. Yeye alikuwa na desturi ya kukaa kidogo baada ya sala katika hali ya kumkumbua Mwenyezi Mungu na kisha kutoa fursa kwa watu wamjie kumwuliza maswali au kumfikishia mahitaji yao. Katika kisa hiki mara baada ya sala kumalizika, yeye alisimama mara moja na kuelekea nyumbani kwake. Akaitafuta ile sarafu iliyojificha na baada ya kuipata, akarudi msikitini na kuipatia mtu mmoJa maskini, huku akisema kwamba sarafu yenyewe ilikuwa imemdondoka alipokuwa akigawanya pesa na hili alikuwa amelisahaulia mbali lakini likamjia kwa ghafla alipokuwa akiongoza sala na akahangaishwa na wazo kwamba angetokea yeye kufariki kabla hajaiokota tena ile sarafu na kumpatia yule anayeihitaji, basi mimi ningebebeshwa huu mzigo na Mwenyezi Mungu; hili ndilo lililokuwa limemfanya yeye aondoke haraka msikitini kwenda kuiokota ile sarafu (Bukhari, Kitabu-Kusuuf).

Katika kukazania kwake kulinda kikamilifu masilahi ya maskini na wasiojiweza yeye alipiga hatua kiasi cha kuagiza kwamba isitolewe kabisa sadaka yoyote kwa wazao wake, akichelea wasije Waislamu kwa sababu ya mapenzi yao na uaminifu wao kwake yeye baadaye wakawafanya wazao wake kuwa ni shabah kubwa ya sadaka zao na hivyo basi kuwanyima maskini na wasiojiweza fungu lao halali. Safari moja mtu mmoja alimletea tende kiasi fulani na akazitoa kuwa ni sadaka. Mjuku wake Hadhrat Imam Hasan[ra] ambaye wakati ule alikuwa na umri wa miaka miwili na nusu tu, akatokea kuwa amekaa pamoja na Mtume[saw] Akachukua tende moja na akaitia mdomoni. Mara moja Mtume[saw] akamtia kidole mdomoni na kuichomoa tende ile huku akisema: Sisi, hizi hatuna haki nazo. Hizi ni mali ya maskini miongoni mwa viumbe wa Mwenyezi Mungu" (Bukhari, Kitabul-Kusuuf).

KUWAHURUMIA WATUMWA

Yeye daima aliwanasihi wale waliokuwa na watumwa wawatendee kwa huruma tena kwa njia nzuri. Alikuwa ameweka maagizo kwamba kama akitokea bwana wa mtumwa kumpiga mtumwa wake au

kumtusi, basi kafara ya pekee aliyoweza kutoa kwa kosa lake ilikuwa ni kumwachilia huru yule mtumwa (Muslim, Kitabul-Imaan).

Yeye alianzisha njia za kuhimizia kuachwa huru kwa watumwa, kwa kila kisingizio. Yeye alisema: "Kama mtu mwenye mtumwa akimwachilia huru, basi Mwenyezi Mungu katika thawabu ataiepushia moto kila sehemu ya mwili wake kulingana na kila sehemu ya mwili wa mtumwa yule". Tena, yeye aliweka kanuni ya kwamba mtumwa awe akipewa kazi ile tu anayoweza kuimudu kwa urahisi na kwamba atokeapo kupewa kazi, basi bwana wake na amsaidie kuifanya kusudi mtumwa asijisikie kuwa mnyonge na duni (Muslim, Kitabul-Imaan). Atokeapo bwana kusafiri na mtumwa wake, basi iwe ni faradhi kwake yeye kusafiria mnyama wake (rikabu) na mtumwa wake na iwe kwa wote wawili kupanda kwa wakati mmoja au kwa zamu. Hadhrat Abu Huraira[ra] ambaye baada ya kusilimu alikuwa akipitisha wakati wake wote pamoja na Mtume[saw] na aliyekuwa amesikia mara kwa mara maagizo ya Mtume[saw] kuhusu jinsi ya kuwatendea watumwa, amesema: "Mimi naapa kwa Mwenyezi Mungu Ambaye maisha yangu yamo mkononi Mwake ya kwamba isingelikuwa zile fursa nipatazo kupigana katika jihadi na za kwenda kuhiji na isingelikuwa ukweli kwamba ninazo fursa za kumhudumia mamangu, mimi ningelitamani kufa mtumwa, kwani Mtume[saw] wakati wote alisisitiza kwamba watumwa watendewe vizuri tena kwa huruma" (Muslim). Hadhrat Ma'ruur bin Suwaid[ra] yuwasimulia kwamba: "Mimi nilimwona Abu Dharr Ghifari (Sahaba wa Mtume[saw]) akivaa nguo sawa kabisa na zile zilizovaliwa na mtumwa wake. Nikamwuliza mbona imekuwa hivi naye akasema: 'Mtume Mtukufu alipokuwa hai, mimi safari moja nilitokea kumtania mtu nikimwambia mamake alikuwa amepata kuwa mtumwa. Hapo Mtume Mtukufu[saw] akanikaripia na akatamka akisema: "Yaonekana wewe bado wakumbuka mambo ya kabla ya Islam. Watumwa ni akina nani? Wao ni ndugu zenu na ni msingi wa uwezo wenu. Mwenyezi Mungu kwa hekima Zake anawapatieni mamlaka ya muda juu yao. Yule mwenye mamlaka sampuli hiyo juu ya nduguye basi na amlishe nduguye

chakula kile kile alacho yeye mwenyewe; amvishe nguo zile zile avaazo yeye mwenyewe wala na asimpe kazi ya kumzidi nguvu, na yeye mwenyewe ni sharti amsaidie kazi yoyote anayotakiwa kufanya." Safari nyingine Mtume[saw] alitamka akisema: "Atokeapo mtumishi wako kukupikia chakula na kukuandalia, basi yakubidi umkaribishe aketi ule naye au kwa akali ale sehemu ya chakula kile mkiwa pamoja, kwani yeye amekuwa na haki nacho kwa kule kukipika" (Muslim).

KUWATENDEA WEMA WANAWAKE

Mtume Mtukufu[saw] alikuwa na shauku kubwa ya kuimarisha hali ya wanawake katika jamii na kuwapatia heshima na kutendewa inavyopasa. Islam ilikuwa ndiyo dini ya kwanza kuwapatia wanawake haki ya urithi. Kurani yawafanya mabinti pamoja na wana warithi wa mali zinazoachwa na wazazi wao. Vivyo hivyo mama anafanywa mrithi wa mali za mwanawe na bintiye, na mke anafanywa mrithi wa mali za mumewe. Atokeapo ndugu kuwa mrithi wa mali za marehemu nduguye basi dada naye pia ni mrithi wa mali ile. Hapana dini yoyote kabla ya Islam ambayo kwa uwazi na kwa uthabiti ilikuwa imeweka haki ya mwanamke ya urithi na haki yake ya kumiliki mali. Katika Islam mwanamke ni mmiliki hasa wa mali zake na mumewe hawezi akawa na mamlaka yoyote juu yake eti kwa sababu tu yu mume wake. Mwanamke anao uhuru kamili wa kufanya atakavyo na mali zake.

Mtume Mtukufu[saw] alikuwa mwangalifi mno kuhusu kutendewa wanawake kwa huruma hivi kwamba wale waliokuwa karibu naye ambao hapo kabla hawakuwa wamezoe kuwachukulia wanawake kwa huu msimamo ya kuwa wao walikuwa ni wenzi wasaidizi waliona vigumu kujirekebisha kwenye ule mfano wa juu sana aliotaka Mtume[saw] kuuweka na kuuendeleza. Hadhrat Umar[ra] yuwasimulia kwamba: "Mke wangu wakati mwingine akitaka kujidukiza katika mambo yangu kwa ushauri wake nami huwa nikimkaripia, nikisema kwamba hawajapata Waarabu kuwaruhusu wake zao kujidukiza katika mambo yao. Basi huwa yeye kunijibu akisema: "Hayo yote ni ya kale. Mtume Mtukufu[saw] huwaruhusu wakeze kumshauri katika

mambo yake na hawakatazi. Mbona wewe hufuati mfano wake?" Jibu langu lilikuwa ni kusema kwamba: 'Ama kumhusu Aisha, Mtume[saw] yuwampenda kivyake lakini kumhusu bintiyo (Hafsa), kama akijidukiza hivi basi siku moja hatakuwa na budi kuvuna matokeo ya kimbelembele chake.' Basi ikaja kutokea baadaye kwamba safari moja Mtume Mtukufu[saw], akiwa amechukizwa na jambo fulani, aliamua kukaa kwa muda mbali na wakeze. Nilipopata kujua hivyo nikamwambia mke wangu, 'Kile nilichokihofia sasa kimetendeka. Hapo nikaenda nyumbani kwa binti yangu Hafsa, na nikamkuta akilia. Nikamwuliza kama Mtume[saw] alikuwa amemtaliki. Akasema: Talaka sina habari nayo, lakini Mtume[saw] ameamua kukaa mbali nasi kwa muda.' Nikamwambia: 'Si mimi nilikuonya usimtanie amtaniavyo Aisha, kwani Mtume[saw] anampenda sana lakini yaonekana umejiletea mwenyewe kile nilichokihofia.' Kisha nikaenda kwa Mtume Mtukufu[saw] na nikamkuta akilalia mkeka mgumu. Wakati ule hakuwa amevaa shati na mwili wake ulikuwa na alama-alama za mkeka ule. Nikaketi karibu naye na nikasema: Ewe Mtume wa Allah! Kaisari na Khosro hawastahili hisani yoyote ya Mwenyezi Mungu lakini hata hivyo wao wanapitisha maisha yao katika starehe kubwa na wewe uliye ni Mtume Wake wapitisha siku zako katika taabu sampuli hii. Mtume[saw] akajibu akisema "Sio hivyo. Mitume wa Allah hawatazamiwi kupitisha wakati wao stareheni. Maisha sampuli hiyo yawafaa tu watawala wa kidunia.' Hapo mimi nikamsimulia yale yote yaliyotendeka baina yangu na mke wangu na binti yangu. Kusikia hivyo, Mtume[saw] akacheka na akasema: 'Sio kweli kwamba mimi nimewataliki wake zangu. Mimi nimeonelea tu ya kuwa ni afadhali nipitishe muda kidogo mbali nao" (Bukhari, Kitabun-Nikaah).

Yeye alikuwa mwangalifu sana kuhusu maono ya wanawake kiasi hiki kwamba safari moja alipokuwa akisalisha alisikia mtoto akilia na akamaliza sala upesi upesi, akielezea baadaye kwamba aliposikilia kilio cha mtoto yeye alihisi kwamba kitamhangaisha mama wa yule mtoto na hivyo basi yeye alikuwa amehitimisha sala upesiupesi kusudi aweze yule mama kwenda na kumwangalia mtoto wake.

Wakati wa safari yake yoyote walipotokea wanawake kuwemo safarini daima yeye aliagizia msafara kwenda taratibu na kwa vituo visivyokuwa vya mbali. Kwenye mojawapo ya safari kama hizi wanaume walipotia shime ya kusonga mbele, yeye alitamka akisema: "Tunzeni vioo! Tunzeni vioo!" akimaanisha kwamba wanawake walikuwemo kundini na kwamba kama ngamia na farasi wataharakishwa basi wao watasumbuliwa na msukusuko wa wanyama wale (Bukhari, Kitabul-Adab). Wakati wa vita fulani sokomoko ilizuka miongoni mwa askari wapanda-wanyama na wanyama wenyewe kutoongozeka. Mtume Mtukufu[saw] akaanguka farasini na baadhi ya wanawake nao pia wakaanguka kutoka wanyama wao. Mmoja wa Masahaba wake, aliyekuwa amepanda ngamia nyuma ya Mtume[saw] akaruka chini na kumkimbilia Mtume[saw] huku akisema: "Na niwe kafara kwako, Ewe Mtume wa Allah." Mguu mmoja wa Mtume[saw] ulikuwa bado uko kwenye kikuku cha farasi. Akauondoa haraka na kumwambia Sahaba wake: "Usinijali, enenda ukawasaidie wanawake." Punde tu kabla ya kifo chake agizo moja alilowakumbusha Waislamu na kulisisitizia lilikuwa kwamba inawabidi kuwatendea wanawake kwa huruma na upole. Ilikuwa ni kauli ya mara kwa mara ya Mtume[saw] ya kwamba kama mtu anao mabinti naye akawaelimisha na kujibidiisha na ulezi wao, Mwenyezi Mungu atamwepushia moto wa Jahanamu (Tirmidhi).

Yalikuwa ni mazoea ya Waarabu kuwaadhibu wanawake kwa kila kijikosa. Mtume Mtukufu[saw] akafundisha kwamba wanawake ni viumbe wa Mwenyezi Mungu sawa na wanaume wala si watumwa wa wanaume, na si stahili yao kupigwa. Walipofahamu hivyo wanawake wakaruka mpaka na kuanza kupinga wanaume katika kila kitu, ikaishilizia kwamba katika nyumba nyingi amani ikavurugika. Hadhrat Umar[ra] akalalamikia jambo hili kwa Mtume Mtukufu[saw] na akasema kwamba isipokuwa wanawake wawe wakati mwingine wanachapwa basi wataruka ugo na haitawezekana tena kuwasimamia. Kwa vile mafundisho kamili ya Kiislamu kuhusu jinsi ya kuwatendea wanawake yalikuwa bado hayajafunuliwa, basi Mtume[saw] akasema kwamba kama mwanamke akipatikana na kosa baya anaweza akatiwa

adabu. Hili nalo kwa upande wake likawaelekeza wengi wa wanaume katika visa vingi kurejelea desturi za kizamani za Waarabu. Ukawa sasa ni wakati wa wanawake kulalamika nao wakayafikisha malalamiko yao kwa wakeze Mtume[saw]. Kutokana na hayo, Mtume[saw] akawakaripia wanaume na akawaambia kwamba wale wanaowatendea wanawake kwa ukatili wasingeliweza kupata radhi ya Mwenyezi Mungu. Nyumaye haki za wanawake zikatambulikana, na kwa mara ya kwanza wanawake wakaanza kutendewa kama watu huru kama inavyostahili (Abu Dawud, Kitabun-Nikaah).

Hadhrat Mu'awiya al-Qushairi[ra], yuwasimulia kwamba: "Mimi nilimwuliza Mtume Mtukufu[saw] ni nini anachoniwia mke wangu," akanijibu akisema: "Mlishe kile Mwenyezi Mungu anachokujaalia wewe kama riziki, na mvishe kile Mwenyezi Mungu anachokuvalisha wewe kama kivazi na usimpige wala kumtusi wala kumtupa nje ya nyumba yako." Yeye alikuwa mwangalifu sana kuhusu maono ya wanawake kiasi hiki kwamba wakati wote aliwanasihi iliyowabidi kusafiri warejee nyumbani upesi inavyowezekana kusudi wake na watoto wao wasiachwe pweke kwa muda mrefu kupita kiasi. Kila alipotoka safarini wakati wote yeye aliwasili nyumbani wakati wa mchana. Kama aliona usiku unaingia karibu na mwisho wa safari, basi ilikuwa yeye kwa usiku ule kupiga kambi nje ya Madina na kuingia mjini asubuhi kunapokucha. Halikadhalika yeye aliwashauri Masahaba wake ya kuwa warudipo kutoka safarini basi na wasifike nyumbani kwa ghafla pasi na ishara ya kurudi kwao (Bukhari na Muslim). Katika kutoa agizo hili yeye alikuwa akitilia maanani ukweli kwamba uhusiano wa kijinsia kwa kiwango kikubwa hutawaliwa na maono. Wakati mumewe anapokuwa hayupo mara nyingi anaweza mwanamke kutojiweka nadhifu na kama ingetokea mumewe kurejea nyumba bila kutazamiwa basi huenda yakatiliwa walakini maono ya mume au ya mke. Kwa kutoa agizo kwamba anaporejea mtu kutoka safarini basi yambidi kuwasili wakati wa mchana na baada ya kuwajulisha kimbele watu wa nyumbani kwake, yeye alihakikisha kwamba watu wa nyumbani kwa mtu yule wangelitokea kuwa tayari kumpokea huyo mtoka-safarini kwa njia inayofaa.

MSIMAMO WAKE KUWAHUSU MAREHEMU

Alifundisha kwamba kila mtu ni sharti afanye wasia kuhusu vile mambo yake yatakavyoendeshwa baada ya kifo chake kusudi wale wanaofungamana naye wawe hawatasumbuka sana baada ya yeye kuaga dunia.

Aliagiza kwamba haimpasi mtu kumsema vibaya mtu aliyekufa lakini wema wowote aliokuwa nao basi huo yafaa usisitiziwe, kwani hapana manufaa yoyote mtu atakayoyapata kama matokeo ya kutaja upungufu au ubaya wa marehemu lakini kwa kusisitizia wema wake watu watavutika kumwombea (Bukhari). Yeye alisisitizia madeni ya marehemu kulipwa kabla hajazikwa. Mara nyingi yeye mwenyewe alitimiza jukumu la kumlipia marehemu madeni yake, lakini alipotokea kutoweza kufanya hivyo, basi aliwahimiza warithi na jamaa za marehemu au watu wengine kumtimizia wajibu wake huu na hangelisalisha sala ya jeneza ya mtu aliyekufa hadi madeni yake yawe yamelipwa.

ALIVYOWACHUKULIA MAJIRANI

Wakati wote yeye aliwatendea majirani zake kwa ukarimu mkubwa na upole. Alikuwa akisema kwamba malaika Jibrili alikuwa amesisitizia sana mtu kuwatendea wema jirani zake hivi kwamba wakati mwingine alianza kufikiria huenda jirani atahesabiwa miongoni mwa warithi waliofaradhishwa. Hadhrat Abu Dharr[ra] yuwasimulia kwamba Mtume[saw] alimwambia hivi: "Abu Dharr, familia yako inapopikiwa mchuzi, basi ongeza maji kidogo kusudi jirani yako naye pia aweze kuutabaruku." Hii haimaanishi kwamba jirani na asikaribishwe katika mambo mengine lakini, kwa vile Waarabu sana sana walikuwa ni watu wa kuhamahama na mchuzi waliupenda sana, Mtume Mtukufu[saw] alikitaja chakula hiki walichokizoelea na akafundisha ya kuwa mtu na asitilie maanani zaidi utamu wa chakula kuliko wajibu wake wa kumpatia jirani yake.

Hadhrat Abu Huraira[ra] yuwasimulia kwamba: "Safari moja Mtume Mtukufu[saw] alitamka akisema: 'Wallahi si muumini! Wallahi si

muumini! Wallahi si muumini!' Masahaba wakauliza wakisema: 'Ni nani asiyekuwa muumni, Ewe Mtume wa Allah?' naye akajibu akisema: 'Yule mtu ambaye kwa shari za mikono yake jirani yake hapati salama.' Safari moja alipokuwa akihutubia wanawake, alisema: 'Kama mtu yeyote atokee kuwa na rondo la mbuzi tu la kufanya kitoweo, basi yafaa mtu huyo amgawie jirani yake.' Aliwanasihi watu kutowakataza majirani zao kupigilia kwenye kuta za nyumba zao vijiti au kutumia kuta za nyumba zao kwa njia yoyote ile isiyokuwa na madhara." Hadhrat Abu Huraira[ra] yuwasimulia akisema: "Mtume[saw] alisema: 'Yule anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Hukumu basi na asimsumbue jirani yake kabisa: Yule anayemwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Hukumu basi na asimsumbue mgeni wake kabisa, na yule mwenye kumwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Hukumu basi na atoe kauli njema tu la sivyo anyamaze" (Muslim).

ALIVYOWATENDEA NDUGUZE

Watu walio wenge zaidi wana hii kasoro moja ya kwamba wanapooa na kujiwekea jiko lao, basi huanza kutowajali wazazi wao. Hivyo basi, Mtume Mtukufu[saw] alitilia mkazo sana ustahilifu wa mtu kuwahudumia wazazi wake kwa huruma na upole. Hadhrat Abu Huraira[ra] yuwasimulia hivi: "Mtu mmoja alimjia Mtume Mtukufu[saw] na kutaka aambiwe ni nani mwenye kuzistahili zaidi huduma zake. Mtume[saw] akajibu akimwambia: "Mamako." Yule mtu akauliza 'Na nani tena?' Mtume[saw] akarudia kesma, 'Na tena mamako'. Kwa mara ya tatu yule mtu akauliza, 'Na baada ya mamangu?' na Mtume[saw] akajibu, 'Tena mamako', na yule mtu alipomwuliza kwa mara ya nne, akasma: 'Baada yake ni babako na baada yake ni jamaa wa karibu na baada ya hao ni jamaa wa kando zaidi." Wazazi wa Mtume[saw] mwenyewe na mababuze walikuwa wamefariki yeye alipokuwa bado yu mtoto. Lakini wazazi wa baadhi ya wakeze walikuwa bado wakali hai, na daima yeye aliwatendea kwa ukarimu na heshima kubwa. Ulipotekwa mji wa Makka na Mtume[saw] kuingia humo kama jemadari mshindi, Hadhrat Abu Bakr[ra] alimleta babake kukutana na Mtume[saw]. Akamwambia Hadhrat Abu Bakr[ra]: "Imekuwaje kumsumbua babako

afike kwangu? Ningefurahia sana mimi mwenyewe kwenda kwake" (Halabiyya, J. 3, uk.99). Moja ya kauli zake ilikuwa hii: Mkosa bahati ni yule mtu ambaye wazazi wanaishi mpaka kuchakaa na hata hivyo yeye kuikosa Pepo," akimaanisha kwamba kuwahudumia wazazi hususan wanapochakaa huvutia rehema na baraka za Mwenyezi Mungu na, hivyo basi, mwenye kujaaliwa fursa ya kuwahudumia wazazi wake waliochakaa na mwenye kuichukulia fursa hii vilivyo hana budi kuthibitika katika njia za utawa na kuwa mpokeaji wa rehema za Mwenyezi Mungu.

Safari moja mtu alilalamika mbele ya Mtume[saw] akisema kwamba nduguze kadiri alivyozidi kuwafanyia ukarimu ndivyo walivyozidi kumhasimu na kwamba kadiri alivyozidi kuwaonea huruma ndivyo walivyozidi kumtaabisha, na kadiri alivyozadi kuwaonesha upendo ndivyo walivyozidi kumchukia. Mtume[saw] akasema: "Kama wasema kweli basi wewe una bahati sana, kwani daima wewe utakuwa mpokeaji wa msaada wa Mungu (Muslim, Kitabul-Birr was-Sila). Safari moja alipokuwa Mtume[saw] akiwahimizia watu utoaji wa sadaka na kuwafadhili wengine, mmoja wa Mashaba wake, Hadhrat Abu Talha Ansari[ra] alimjia na kukitoa kiunga chake cha mitende kuwa ni sadaka. Mtume[saw] akafurahi na akatamka akisema, "Ni sadaka bora ilioje! "Ni sadaka bora ilioje! Ni sadaka bora ilioje!" na akazidi kusema "Baada ya wewe kukitoa kiunga hiki kuwahudumia maskini, sasa mimi nataka wewe ukigawie nduguzo walio maskini" (Bukhari, Kitabut-Tafsiir). Safari moja mtu fulani alimjia na akasema: "Ewe Mtume wa Allah! Mimi niko tayari kuahidi kwenda kuhiji na niko tayari kuahidi kupigana jihadini, kwani mimi natamani kupata radhi ya Mwenyezi Mungu." Mtume Mtukufu[saw] akamwuliza kama mmoja wa wazazi wake alikuwa hai, na yule mtu akamwambia wote walikuwa hai. Kisha akamwuliza: "Kweli wewe watamani kupata radhi ya Mwenyezi Mungu?" na kufuatia jawabu la kuthibitisha la yule mtu Mtume[saw] akasema: "Basi rudi kwa wazazi wako ukawahudumie na ukawahudumie kwa dhati." Yeye alisema kwamba hata ndugu za mtu wasiokuwa Waislamu nao pia wanastahili

kutendewa kwa huruma na upole pamwe na ndugu zake wengine walio ni Waislamu. Mmoja wa wakeze Hadhrat Abu Bakr[ra] ambaye hakuwa Mwislamu, alimtembelea bintiye, Asmaa, naye akamwuliza Mtume Mtukufu[saw] kama huyu mama (asiyekuwa Mwislamu) angeweza kumhudumia bintiye na kumpatia zawadi, ambapo Mtume Mtukufu[saw] alijibu akisema: "Naam, kwani yeye ni mamako" (Bukhari, Kitabul-Adab).

Hakuwatendea tu nduguze wa karibu bali hata wale wa kando na kila afunganaye nao yeye aliwatendea kwa upole mkubwa. Wakati wowote alipotoa dhabihu ilikuwa yeye kuwapelekea sehemu ya nyama ile marafiki wa Hadhrat Khadija[ra] (marehemu mkewe) na aliwaambia wakeze wasiwasahau wakati kama huo. Miaka mingi baada ya kifo cha Hadhrat Khadija[ra] alipokuwa akiketi na baadhi ya Masahaba wake, dadake Hadhrat Khadija[ra], Hala, alifika kumwona na akataka aruhusiwe kuingia. Sauti yake ilisikika masikioni mwa Mtume[saw] kama ile ya Hadhrat Khadija[ra] na alipoisikia akasema: "Mola wangu! Huyu ni Hala, dadake Khadija." Na kweli kabisa, upendo wa dhati daima hujidhihirisha kwa njia hii ya kwamba mtu huwapenda na kuwawia mpole wale wote ambao huenda wana fungamano na yule anayempenda au kumheshimu.

Hadhrat Anas bin Malik[ra] yuwasimulia kwamba wakati wa safari yeye alijikuta akiwa na Jarir[ra] bin Abdullah na akaona kwamba huyu mwenzake alijishughulisha na kumhudumia chambileche mtumishi amhudumiavyo bwana wake. Kwa vile Hadhrat Jarir[ra] bin Abdullah alikuwa ni mzee kuliko Hadhrat Anas[ra], basi huyu mwenzake hayakumpendeza na akadadisi akimtaka Hadhrat Jarir[ra] bin Abdulla[ra] asijidharau vile. Hadhrat Jarir[ra] akajibu akimwambia: "Mimi nilikuwa nikiona ni kwa unyenyekevu jinsi gani vile ma-Ansari walivyo-mtumikia Mtume Mtukufu[saw], nami nikiwa nimevutiwa na ule unyenyekevu na upendo wao juu ya Mtume Mtukuu[saw], nilikuwa nimeamua kwamba kama wakati wowote nikitokea kuwa pamoja na Ansari, basi nitamtumikia kama mtumishi wake. Mimi, hivyo basi, natimiza tu nia yangu wala wewe usiwe na haja ya kunikataza"

(Muslim). Kisa hiki chathibitisha kwamba atokeapo mtu kumpenda mwingine kwa dhati, basi mapenzi haya huwafikia pia wale wanaoendeleza shabaha za fungamano lake. Vivyo hivyo wale wawaheshimuo wazazi wao kwa dhati ni wastahifu daima kwa wale wawezao kuwa na fungamano na wazazi wao kwa njia ya uhusiano wa upendo au udugu. Safari moja Mtume Mtukufu[saw] aliutilia mkazo kuwa ndio wema wa daraja ya juu zaidi kwa mtu kuwastahi marafiki wa babake. Miongoni mwa watu walioambiwa hivyo alikuwemo Hadhrat Abdullah bin Umar[ra]. Miaka mingi baadaye alipokuwa safarini kwenda kuhiji, alikutana na Bedui mmoja na akampatia mnyama wake aliyekuwa amempanda na pia akamzawadia kilemba chake. Mmoja wa wenzake akamwambia kwamba alikuwa amemzidishia ukarimu kwani Bedui huwa yuwatosheka na kitu kidogo tu. Hadhrat Abdullah bin Umar[ra] akasema: "Baba wa mtu huyu alikuwa ni rafiki wa babangu na nimemsikia Mtume Mtukufu[saw] akisema kwamba ulikuwa ni miongoni mwa wema wa daraja ya juu kabisa kwa mtu kuwastahi marafiki wa babake."

KUKAA NA WATU WEMA

Daima yeye alipendelea kuwa pamoja na watu wema na kama alitokea kuona upungufu wowote katika yeyote miongoni mwa Masahaba wake basi yeye alimkosoa kwa upole tena faraghani. Hadhrat Abu Musa Ash'ari[ra] yuwasimulia kwamba: "Mtume Mtukufu[saw] alionesha manufaa ya kupatikana kutokana na wenzi walio wema na madhara ya kufahamika kutokana na wenzi walio waovu kwa kutamka akisema: 'Mtu mwenye kukaa na watu wema yuwafanana na mtu mwenye kubeba miski. Akiula anafaidika; akiuuza anapata faida na akiuweka anafurahia harufu yake. Mtu mwenye kukaa na watu waovu yuwafanana na mtu mwenye kuchochea tanuri; kile anachoweza kutarajia ni kwamba itokee cheche kuziangukia nguo zake na kuziunguza au kwamba ule moshi utokanao na makaa umtie kichaa" Alikuwa akisema kwamba tabia ya mtu huwa na rangi ya wale wenzi anaokaa nao na kwamba hivyo basi inambidi mtu kuwa mwangalifu kupitisha wakati wake pamoja na watu wema (Bukhari na Muslim).

ALISITIRI IMANI YA WATU

Mtume Mtukufu[saw] alikuwa mwangalifu sana kuweka sitara dhidi ya uwezekano wa kutokea hali ya kutoelewana. Safari moja mkewe Hadhrat Safiyya[ra] alifika msikitini kumwona. Ulipofika wakati wake wa kurejea nyumbani giza lilikuwa limeingia na hivyo basi ikawa Mtume Mtukufu[saw] kuamua kumsindikiza nyumbani kwake. Njiani akapishana na watu wawili na akikusudia kuwaondolea mbali shaka ya kuwa huyu mwenzake alikuwa ni nani, akawasimamisha na huku akimfunua mkewe mtandio akasema: "Hebu angalieni, huyu ni mke wangu Safiyya." Wale watu wakalalamika wakisema: "Ewe Mtume wa Allah! imekuwaje kutudhania sisi tutakushuku wewe?" Mtume[saw] akajibu akisema: "Shetani (dhana mbaya) mara nyingi humwingia mtu damuni. Mimi nilichelea isije imani yenu ikaathirika" (Bukhari, Kitabul-I'tikaaf).

ALIZIBA AIBU ZA WENGINE

Yeye hakutangaza abadani makosa na kasoro za watu wengine na akawaonya watu kutotangaza makosa yao wenyewe. Alikuwa akisema kwamba: "Akitokea mtu kuziba aibu za mwingine, basi Mwenyezi Mungu atamziba aibu zake Siku ya Hukumu." Na kasema, "Kila mmoja wa wafuasi wangu anaweza akayakwepa matokeo ya makosa yake (yaani, kwa toba ya dhati na kujirekebisha) isipokuwa wale wenye kuendelea kutangaza ukosefu wao" na akafafanua kwa kusema: "Mtu katenda dhambi usiku na Mwenyezi Mungu kalifunikiza; asubuhi kakutana na marafiki zake na kajigamba mbele zao (akisema): "Usiku mimi kafanya hivi, usiku mimi kafanya vile, na hivyo basi yeye mwenyewe kuumbua kile alichokuwa kakifunikiza Mwenyezi Mungu" (Bukhari na Muslim).

Baadhi ya watu hufikiria kipumbavu kwamba kuungama dhambi huhamasisha kutobu; laikini ukweli wenyewe ni kwamba kuungama dhambi huzidi kutokomeza madhambini. Dhambi ni uovu na mwenye kutumbukia humo na kujionea haya na kujuta anayo nafasi ya kujirejeshea hali ya utawa na uchamungu kwa njia ya toba. Yeye yuwafanana na yule mtu aliyeghuriwa na maovu lakini kumbe

yuwaandamwa na utawa na mara itokeapo fursa, uovu hufutiliwa mbali na mtenda madhambi kurejelewa na uchamungu. Hata hivyo, wale ambao hutangaza madhambi yao na wanayajivunia huwa mema na mabaya hawayajali tena na kutubu huwa hawakuwezi tena.

Safari moja mtu alimjia Mtume Mtukufu[saw] na kutamka akisema: "Mimi nimezini" (linapothibitishwa kwa ushahidi wa kuaminika linakuwa kosa la kuadhibika chini ya Sheria za Kiislamu). Kusikia hivyo, Mtume Mtukufu[saw] akampa yule mtu kisogo na kujishughulisha na mambo mengine. Alitaka kuonesha kwamba tiba hasa katika jambo sampuli hii ilikuwa ni toba wala sio kuungama. Lakini hili yule mtu hakulitambua na huku akifikiria kwamba huenda Mtume Mtukufu[saw] hakuwa amemsikia, akaenda kujikita mbele yake na kumkariria kosa lake. Mtume[saw] akageuka tena upande mwingine lakini yule mtu akamgeukia tena na kumwungamia kosa lake. Alipokuwa amefanya hivyo mara nne, Mtume[saw] akatamka akisema: "Mimi nia yangu ilikuwa kwamba mtu huyu kosa lake asingelitangaza hadi iwe itatokea Mwenyezi Mungu kuonesha uamuzi Wake kamhusu yeye, lakini kwa kuwa amekariri kosa lake mara nne, sina budi kumchukulia hatua" (Tirmidhi). Kisha akazidi kutamka akisema "Mtu huyu ameungama mwenyewe wala hakushtakiwa na yule mwanamke ambaye kutokana naye, yeye yuwaungama. Yule mwanamke na ahojiwe na, kama akitokea kulikanushilia mbali kosa lake, basi na asisumbuliwe na aadhibiwe mtu huyu peke yake sawa na alivyoungama, lakini kama naye akitokea kuungama basi na adhibiwe vile vile." Ilikuwa ni desturi ya Mtume Mtukufu[saw] kufuata Sheria ya Torati katika yale mambo ambayo Kurani ilikuwa bado haijayazungumzia, na kwa vile Torati yahukumu kwamba mzinifu auawe kwa kupigwa mawe basi akampatia mtu huyu hukumu ile ile. Hukumu ilipokuwa akitekelezwa yule mtu alijaribu kukimbia lakini watu wakamkimbiza na kumkamata kuhitimisha ile hukumu. Alipopata habari hii Mtume[saw] hakukiridhia kitendo chenyewe. Akasema kwamba yule mtu alikuwa amehukumiwa sawa na kuungama kwake yeye mwenyewe. Lile jaribio lake kuponyoka

lilikuwa kwa hakika ni kubatilisha kuungama kwake na baadaye asingelitwishwa ile hukumu aliyokuwa amepewa kwa sababu tu ya kuungama kwake.

Mtume[saw] alifundisha kwamba Sheria ilitilia maanani yale makosa yaliyokuwa ya kidhahiri peke yake. Wakati wa vita, kikosi cha Waislamu kilimtia mbaroni mtu mmoja aliyekuwa na mazoea ya kuvizia faraghani na kila alipompata Mwislamu aliye peke yake basi ilikuwa yeye kumshambulia na kumuulia mbali. Safari hii Hadhrat Usama bin Zaid[ra] alimfukuza na baada ya kumkamata akamchomolea upanga amuulie mbali. Yule mtu alitambua kwamba hapakuwa na pa kukimbilia, akapiga Shahada yaani, "Hapana apasaye kuabudiwa ila Allahu", akiashiria kwamba sasa yeye alikuwa amesilimu. Hadhrat Usama[ra] hili hakulijali na akamuua. Kiliposimuliwa kisa hiki miongoni mwa visa vya vitani Mtume Mtukufu[saw] akamwita Hadhrat Usama[ra] na kumuuliza. Alipothibitisha kisa hiki Mtume[saw] akasema: "Utakuwa hali gani siku ya Hukumu wakati shahada yake itakapomwunga mkono?" Hadhrat Usama[ra] akajibu akisema, "Ewe Mtume wa Allah! Yule alikuwa ni muuaji wa Waislamu na kujifanya kwake Mwislamu zilikuwa ni janja zake za kutaka kukwepa kulipwa stahili yake." Lakini Mtume[saw] akazidi kukariri akisema "Usama, utakuwa hali gani wakati Shahada yake itakapokusuta Siku ya Hukumu?" — akimaanisha kwamba Mwenyezi Mungu atamwuliza Hadhrat Usama[ra] juu ya kifo cha yule mtu, kwani ingawaje yeye alikuwa na hatia ya kuua Waislamu, kule kupiga kwake Shahada ilikuwa ni dalili kuwa yeye sasa alikuwa ametubia makosa yake. Hadhrat Usama[ra] akalalamika akisema kwamba Shahada ya mtu yule ilitokana na kuhofia kwake mauti wala haikuwa dalili ya kutubu kwake. Hapo Mtume Mtukufu[saw] alisema:

> "Je, ulimchungulia moyoni kujua kama alikuwa akisema kweli au la," na akaendelea kukariri akisema: "Utasemaje wakati Shahada yake itakapotolewa kama ushahidi dhidi yako?" Hadhrat Usama[ra] yuwasema: "Nilipomsikia Mtume[saw] akikariri hayo mara kwa mara nilitamani laiti ingelikuwa ndio saa hii mimi kusilimu wala kutokuwa na lile kosa ninalolishitakiwa" (Muslim, Kitabul-Iman).

Daima Mtume Mtukufu[saw] alikuwa tayari kuwasamehe watu makosa yao na hatia zao. Mmoja wa wahusika katika yale masingizio dhidi ya mkewe, Hadhrat Aisha[ra] maisha yake yalitegemea msaada wa Hadhrat Abu Bakr[ra] (babake Hadhrat Aisha[ra]). Uwongo wa yale masingizio dhidi ya Hadhrat Aisha[ra] ulipothibitika vilivyo, Hadhrat Abu Bakr[ra] alimkomeshea mtu huyu ufadhili wake. Hata hii ni dalili ya utu bora wa Hadhrat Abu Bakr[ra] na subira yake. Mtu wa kawaida angelijitenga mbali mno na mtu mfadhiliwa anayempaka matope bintiye. Ilipomfikia habari ya vile Hadhrat Abu Bakr[ra] alivyokuwa amefanya, Mtume[saw] akazungumza naye na kumwambia kwamba ingawaje yule mtu alikuwa makosani, haikumpasa mtu kama vile Abu Bakr[ra] kumsitishia riziki yake kwa sababu ya yale makosa yake. Papo hapo Hadhrat Abu Bakr[ra] akaanza tena kumfadhili yule mtu. (Bukhari, Kitabut-Tafsiir).

UVUMILIVU KATIKA DHIKI

Mtume Mtukufu[saw] alikuwa akisema: "Kwa Mwislamu, maisha ni chungu nzima ya fadhili na hapana mwingine ajikutaye katika hali hiyo ila muumini halisi; kwani, anapofanikiwa yeye humshukuru Mwenyezi Mungu na anakuwa mpokeaji wa fadhili kubwa kutoka Kwake. Kwa upande mwingine, aonjapo machungu au huzuni yeye huvumilia kwa subira na hivyo basi yeye kujistahilishia tena fadhili za Mwenyezi Mungu." Kifo chake kilipokaribia naye kupiga kite kwenye kilele cha udhaifu wa hali yake, bintiye, Hadhrat Fatima[ra], ilimtoka kauli kusema hakuweza kuvumilia kumwona katika hali ile. Hapo yeye alisema: "Kuwa mvumilivu! Babako hatakuwa tena na maumivu baada ya hivi leo." akimaanisha kwamba taabu zake zote zilikuwa ziishilizie humu duniani na mara tu yeye atakapotolewa nje ya duara la maisha haya na kuipata ile hali ya kuwa mbele ya Muumba wake basi hatakuwa tena na taabu. Wakati kulipoenea maradhi haikuwa yeye kuruhusu watu kuutoka mji ulioathiriwa kuhamia mji mwingine, kwani jambo kama hili lingelipanua eneo lililoathiriwa na maradhi yale. Alikuwa akisema kwamba wakati wa magonjwa ya mlipuko ikiwa mtu atabakia mwake mjini na kujizuia kusambaza maradhi hadi mji mwingine na kisha kufa kwa maradhi yale, basi yeye atahesabiwa kuwa ni shahidi (Bukhari, Kitabut-Tibb).

USHIRIKIANO

Yeye alikuwa akifundisha kwamba sifa bora za Islam zilikuwa ni kwamba mtu asiingilie mambo ambayo hayamhusu na kwamba wasiwe watu wakipitapita kuwalaumu watu wengine na kuingilia mambo yasiyowahusu. Hii ni desturi ambayo kama ikifuatwa kotekote na kusisitiziwa itasaidia sana kuleta amani na utangamano humu duniani. Mengi ya matatizo yetu yanatokana na mazoea ya watu walio wengi ya kuingilia mambo ya watu wengine isivyotakikana na kubana ushirikiano wao unapoweza kutakikana katika kutoa msaada kwa wale walio na dhiki.

Mtume Mtukufu[saw] alitilia mkazo hali ya kushirikiana. Yeye alikuwa ameifanya kuwa ni desturi ya kwamba kama akitokea mtu yeyote kutakiwa alipe kiasi fulani cha pesa kama faini na akawa hawezi kupata pesa hizo zote, basi majirani zake au wananchi wenzake au watu wa kabila lake na watoe kiasi kilichosalia kwa njia ya mchango. Watu wakati mwingine walikuja kuishi karibu na Mtume[saw] wakijitolea kuhudumia Islam kwa njia mbalimbali. Daima yeye aliwashauri jamaa zao kuchukua jukumu la kugharamia mahitaji yao ya wastani. Yasimuliwa na Hadhrat Anas[ra] ya kuwa wakati wa Mtume Mtukufu[saw] mtu na kakake walisilimu na mmoja wao akaendelea kukaa na Mtume Mtukufu[saw] wakati yule mwingine aliendelea na shughuli zake za kawaida. Huyu siku moja alimnung'unikia Mtume[saw] ya kwamba kakake yuwapitisha wakati wake akijikalia bure. Mtume Mtukufu[saw] akajibu akisema: "Mwenyezi Mungu Hukuruzuku wewe pia kwa sababu ya kakako na inakubidi kwa hivyo umfadhili na kumwacha aitumikie Dini (Tirmidhi).

Wakati wa safari, msafara wa Mtume[saw] ulipofikia mahali pao pa kupiga kambi, mara moja Masahaba wake walijishughulisha na kazi yao ya kukita kambi ya usiku mmoja. Mtume Mtukufu[saw] akasema: "Mimi hamkunipa kazi. Basi nitakwenda kutafuta kuni za kupikia." Masahaba wakalalamika wakisema: "Ewe Mtume wa Allah, itakuwaje wewe kujihangaisha vile wakati sisi sote tukiwepo hapa

kufanya chochote kilicho cha lazima?" Yeye akasema: "La, La. Ni wajibu wangu nami kufanya sehemu yangu ya chochote kile kitakikanacho kufanywa," na akafuata kuni mwituni za kupikia chakula (Zurqani, J. 4, uk. 366).

MSEMA KWELI

Kama vile tulivyosema Mtume Mtukufu[saw] mwenyewe alikuwa thabiti sana katika tabia yake ya ukweli hivi kwamba miongoni mwa watu wake yeye alijulikana kama 'Mwaminifu' na 'Mkweli'. Alitaka sana kwamba Waislamu wazingatie viwango vile vile vya ukweli alivyovizingatia yeye mwenyewe. Yeye uliuhesabu ukweli kuwa ndilo chimbuko la njema zote, utawa na tabia njema. Alifundisha kwamba mkweli ni yule anayethibitika kwa kweli kwamba yuwahesabiwa mkweli na Mwenyezi Mungu.

Safari moja alifikishwa kwa Mtume Mtukufu[saw] mahabusi aliyekuwa na hatia ya kuua Waislamu wengi. Hadhrat 'Umar[ra] ambaye pia alikuwepo pale, aliamini kwamba mtu yule alistahili sana kupewa adhabu ya kifo na tena na tena akamtupia jicho Mtume Mtukufu[saw] wakati wowote akimtarajia kuashiria kwamba yule mtu auawe. Baada ya Mtume Mtukufu[saw] kumsamehe yule mtu, Hadhrat Umar[ra] ikamtoka kauli kwamba alistahili kuuawa kwani hiyo peke yake ndiyo iliyokuwa adhabu inayostahili. Mtume[saw] akajibu akisema: "Kama ni hivyo, basi mbona hukumuulia mbali?" Hadhrat Umar[ra] akajibu akisema: "Ewe Mtume wa Allah! Kama ungelinipa ishara hata kwa kunikonyezea jicho lako, mimi ningelimuulia mbali." Akimjibu Mtume[saw] akasema: "Nabii hasemi kisebusebu. Ningewezaje kutumia jicho langu kuashiria adhabu ya kifo kwa mtu yule huku ulimi wangu ukitumiwa kuongea naye kwa upole?" (Hisham, J. 2, uk 217).

Safari moja mtu alimjia Mtume Mtukufu[saw] na akasema: "Ewe Mtume wa Allah! Mimi nina maovu matatu: Uwongo, ulevi na uasherati. Nimejitahidi sana kuepukana nao lakini sijafaulu. Utaniambia cha kufanya?" Mtume[saw] akamjibu akimwambia: "Ukiniahidi kwa dhati kwamba utaachilia mbali ubaya mmojawapo

mimi ninakuhakikishia utaondokewa na mengine mawili." Yule mtu akatoa ahadi na akamwuliza Mtume[saw] amwambie ni ubaya upi atakaouachilia mbali. Mtume[saw] akasema: "Achana na uwongo." Wakati fulani baadaye yule mtu alirejea na akamwambia Mtume Mtukufu[saw] ya kuwa baada ya kuzingatia ushauri wake sasa maovu yote matatu yamemtoka. Mtume[saw] akataka kujua ilikuwa-kuwaje na yule mtu akasema; "Siku moja nilitaka kulewa na nilikuwa nusura nifanye hivyo ambapo nilijiuliza mimi mwenyewe ahadi yangu niliyokupa na nikatambua kwamba kama akitokea yeyote miongoni mwa marafiki zangu kuniuliza kama nilikuwa nimekunywa pombe, basi nisingelikuwa na budu kukiri kwani nisingeliweza tena kusema uwongo. Hii ingemaanisha kwamba mimi ningelijichumia sifa mbaya miongoni mwa marafiki zangu na baadaye wao wangejitenga nami. Yaliponijia mawazo haya, mimi nilijikalifisha nafsini kuahirisha ulevi hadi wakati mwingine na nikaweza kuzuia hamu ya kulewa wakati ule. Vivyo hivyo, nilipojikuta nikitamani uasherati nilijidadisi nafsini ya kwamba kutenda ubaya huu kutanikosesha staha za marafiki zangu na ingenibidi nidanganye kama wakitokea kuniuliza, na hivyo basi kuvunjila mbali ile ahadi niliyokupa, au niwe nitakiri kosa langu. Kwa njia hii mimi nikaendelea kujitahidi baina ya azima yangu ya kutimiza ahadi niliyokupa na hamu yangu ya kuingilia ulevi na uasherati. Ulipokuwa umepita muda fulani nikaanza kuondekewa na tamaa ya kuingilia ubaya huu na ile azima ya kuachana na uwongo sasa imeniepushia huo ubaya mwingine.

UDADISI

Mtume Mtukufu[saw] daima aliwanasihi watu dhidi ya udadisi na kuwa na moyo mweupe baina yao. Hadhrat Abu Huraira[ra] yuwasimulia kwamba: "Mtume[saw] alisema: 'Jihadharini dhidi ya kufanyiana kinyongo kwani huu ndio upotovu mkubwa, na msiwe wadadisi au kuvishana vilemba vya ukoka wala msioniane kijicho na msifanyiane husuda; kila mmoja wenu na ajifikirie kuwa yu mtumishi wa Mungu na kuwatendea wengine kama ndugu kama Mwenyezi Mungu alivyofaradhisha,' na pia akasema, 'Kumbukeni kwamba kila

Mwislamu ni ndugu ya kila Mwislamu mwingine. Mwislamu na asimdhulumu mwingine wala kutomjali mwingine nyakati za dhiki au kumdharau mwingine kwa sababu ya utovu wake wa mali au elimu au kitu chochote kingine. Utawa huanzia moyoni na ni kitibua-moyo tosha ya kwamba mtu awe atamdharau nduguye. Kila Mwislamu ni sharti ayachukulie maisha ya Mwislamu mwingine, hesihima na mali zake kuwa ni vitu vitakatifu visivyochafulika. Mwenyezi Mungu hatilii maanani miili yenu wala sura zenu wala matendo yenu ya kidhahiri bali huzitazama nyoyo zenu" (Muslim, Kitabul-Birr was-Sila).

UNYOFU NA UAMINIFU BIASHARANI

Yeye alitaka sana kuwanusuru Waislamu dhidi ya kufanya kinyume cha aina yoyote katika shughuli zao. Safari moja alipokuwa akipitapita sokoni, aliona lundo la nafaka lililotaka kunadiwa. Akaliingiza mkono wake na kugundua kwamba ingawaje upande wa nje lilikuwa kavu upande wa ndani nafaka yenyewe ilikuwa yazizima. Akamtaka mwenyewe kusema kilichosababisha hali hii. Yule mtu akasema kwamba mvua ya ghafla ilikuwa imeilowesha maji sehemu ya ile nafaka. Mtume[saw] akasema kwamba kama ni hivyo basi yeye ilimpasa kuiacha peupe sehemu iliyokuwa majimaji ya bidhaa ile yake kusudi wale waliotarajia kuwa wanunuzi waweze kuijulia hali yake halisi. Akaendelea kutamka akisema: "Yule anayewafanyia wengine kinyume hawezi kamwe kuwa raia mwenye manufaa kwa umma" (Muslim). Alisisitizia shughuli za kibiashara na kiuchumi kuepukana kabisa na hali ya tashwishi na ulaghai. Aliwanasihi wanunuzi daima kukagua bidhaa na vitu wanavyotaka kununua, akakataza mtu yeyote kutoanza kupiga bei kutaka kununua bidhaa ambazo mtu mwingine yeyote tayari yuwazipigia bei. Yeye pia alikataza ulundikaji wa bidhaa (ghalani) kwa kuchelea sokoni kusije kukawa na bidhaa nyingi kupita kiasi, na akasema kwamba sokoni kuwe kukipelekwa bidhaa wakati wote.

KUKATA TAMAA

Yeye alichukia sana hali ya mtu kukata tamaa. Alikuwa akisema kwamba yeyote yule aliye na kosa la kueneza miongoni mwa watu mazoea ya kukata tamaa ndiye mwenye kuzorotesha taifa, kwani

fikara za kukata tamaa huelekea kuwavunja watu moyo na kusitisha maandeleo (Muslim, Sehemu ya II, J. 2). Aliwaonya watu wake kwa upande mmoja dhidi ya tabia ya majivuno na kujigamba na kwa upande mwingine dhidi ya tabia ya kukata tamaa. Akawanasihi kushika njia ya katikati baina ya haya mawili. Waislamu ni sharti wafanye kazi kwa bidii wakiwa na matumaini kwamba Mwenyezi Mungu atalijazi jasho lao matunda bora kabisa. Ni sharti kila mmoja wao kujaribu kusonga mbele na kuwa na nia ya kuendeleza masilahi na ustawi wa jamii, lakini kila mmoja hana budi kutoingiwa na mawazo ya majivuno au kuwa na tabia ya majisifu.

UKATILI KWA WANYAMA

Aliwaonya watu dhidi ya kuwafanyia wanyama ukatili na akaagiza watendewe kwa huruma. Yeye alikuwa akisimulia kisa cha mwanamke wa Kiyahudi aliyeadhibiwa na Mwenyezi Mungu baada ya yeye kumfisha njaa paka wake. Aidha Mtume[saw] alikuwa akisimulia kisa cha mwanamke aliyemkuta mbwa mwenye kiu karibu na kisima chenye kina. Akateka maji kwa kiatu chake. Na akamnywesha yule mbwa. Tendo hili jema likayapatia msamaha wa Mwenyezi Mungu madhambi yake yote ya hapo kabla.

Hadhrat Abdullah bin Mas'uud[ra] yuwasimulia kwamba: "Tulipokuwa safarini pamoja na Mtume Mtukufu[saw] tuliona makinda mawili ya hua kiotani na tukayakamata. Yalikuwa bado ni madogo sana. Mama yao aliporudi kiotani na kutoyakuta mle, alianza kuruka na kuzungukazunguka ovyo. Mtume Mtukufu[saw] alipofika pale akaiona hali ya yule hua na akatamka akisema, endapo yeyote miongoni mwenu kamkamatia makinda yake basi ni lazima ayaachilie mara moja ili amtulize" (Abu Dawud). Hadhrat Abdullah bin Mas'uud[ra] pia yuwasimulia kwamba safari moja waliona kichuguu cha mchwa na, baada ya kukiwekelea nyasi kavu, wakakichoma moto; hapo walikaripiwa sana na Mtume Mtukufu[saw]. Safari moja Mtume Mtukufu[saw] alimwona punda akitiwa alama usoni kwa chuma cha moto. Akataka kujua kisa na maana yake na akaambiwa kwamba

Warumi walikuwa wakiitumia njia hii kwa kutaka kutambulisha wanyama bora. Mtume akasema kwamba kwa kuwa uso ulikuwa ni sehemu chungu mno ya mwili, mnyama na asichomewe alama usoni na inapotokea kuwa lazima kuwekwa alama basi na atiwe alama matakoni, (Abu Dawud na Tirmidhi). Tokea hapo Waislainu daima wanawachomesha chapa wanyama wao matakoni na kutokana na desturi hii ya Waislamu, Wazungu nao pia wanafanya vivyo hivyo.

KUSTAHIMILIANA KATIKA MAMBO YA DINI

Sio tu kwamba Mtume[saw] alisisitizia haja ya kustahimialana katika mambo ya dini bali yeye katika uwanja huu aliweka mfano bora kabisa. Ujumbe kutoka kabila moja la Kikristo la huko Najran ulimtembelea mjini Madina kuja kubadilishiana mawazo juu ya mambo ya kidini. Walikuwemo viongozi kadha wa Kanisa. Mazungumzo yakafanyika msikitini na kuchukua masaa kadha. Ukafika wakati fulani ambapo kiongozi wa ujumbe ule alitaka ruhusa waende kufanyia ibada yao mahali pengine. Mtume Mtukufu[saw] akasema hapakuwa na haja ya wao kutoka nje ya msikiti ambao wenyewe umewekwa wakfu kwa ajili ya ibada ya Mwenyezi Mungu, nao wangeweza kufanyia ibada yao humo (Zurqani).

USHUJAA

Visa kadha vya ujasiri na ushujaa wake vimetajwa katika sehemu ya maelezo ya maisha yake. Hapa yatosha kutaja kisa kimoja. Wakati mmoja Madina kulijaa uvumi kwamba Warumi walikuwa wakiutayarishia uvamizi wake jeshi kubwa. Wakati ule Waislamu usiku walikuwa wanachukua hatua za tahadhari. Usiku mmoja sauti za ghasia zilisikika kutoka jangwani. Waislamu wakatoka upesi majumbani mwao na baadhi yao wakakusanyika msikitini na kumsubiri Mtume Mtutufu[saw] aje awaamrishe dhidi ya tishio hili. Mara wakamwona Mtume Mtukufu juu ya farasi akija kutoka upande zilikotoka zile sauti za msukosuko. Ndipo wao wakagundua kwamba mara tu ilipotokea ishara ya hatari Mtume[saw] alikuwa amepanda farasi na kuelekea zilikotoka zile sauti kuona kama kulikuwepo na haja

yoyote ya kupiga kamsa na wala hakuwa amengojea watu kukusanyika pamoja ili yeye kuweza kwenda pamoja nao. Aliporejea aliwahakikishia Masahaba wake kwamba hapakuwa na sababu yoyote ya kutaharuki na kwamba wangeliweza kurudi majumbani mwao kuuchapa usingizi (Bukhari, mlango kuhusu Shaja'at fil Harb).

KUVUMILIA WASHENZI

Yeye alikuwa mvumilivu hususan kwa wale watu ambao kwa sababu ya ukosevu wa malezi ya utamaduni wa Kiislamu hawakuwa na adabu. Safari moja mkazi wa jangwani aliyekuwa amesilimu hivi punde tu na aliyekuwa ameketi msikitini pamoja na Mtume Mtukufu[saw] alinyanyuka na kwenda hatua chache kwenye kona moja ya msikiti na kuketi chini kutabawali. Baadhi ya Masahaba wa Mtume[saw] wakasimama kutaka kumkatiza. Mtume[saw] akawakataza, akiwaambia kwamba jaribio lolote la kumkatiza lisingelikosa kumletea msukosuko na pengine huenda likamletea madhara. Akawataka kutomjali na baadaye wao wapasafishe mahali pale.

KUZINGATIA MIKATABA

Mtume Mtukufu[saw] alikuwa mwangalifu sana kuhusu suala la kuzingatia mikataba. Safari moja balozi mmoja wa ujumbe maalumu alimjia na alipokwisha kaa naye kwa siku kadha ukampambanukia ukweli wa Islam na akapendekeza kwamba yeye awe ataikubali. Mtume[saw] akamwambia kwamba hatua hiyo isingelikuwa sawa kwa vile yeye alikuwa pale akiwa kama mwakilishi na ilimlazimu yeye kurejea kwenye makao makuu ya Serikali yake pasi na kujichumia utiifu uliokuwa ni mpya. Ikiwa baada ya yeye kuwa amerejea makwao, bado atajiona yuwaridhika na ukweli wa Islam basi hapo angeliweza kurejea kama mtu huru na kutangaza imani yake (Abu Dawud, mlango kuhusu Wafaa bil 'Ahd).

KUWASTAHI WATUMISHI WA UMMA

Yeye aliwafanyia staha za kivyake wale waliochangia wakati wao na mali katika huduma za wanadamu. Kabila la Kiarabu la Banu Ta'ii lilianzisha uadui wake dhidi ya Mtume[saw] na katika vita vilivyofuatia

majeshi yao yalishindwa na wengine kutekwa. Mmoja wa hawa alikuwa ni bintiye Hatim Ta'ii ambaye ukarimu wake ulikuwa ni mashuhuri mno miongoni mwa Waarabu. Huyu bintiye Hatim alipomjulisha Mtume Mtukufu[saw] wazazi wake akamtendea kwa ukarimu mkubwa na kutokana na uombezi wa bibi huyu yeye akafutilia mbali adhabu zote walizopewa watu wake kwa sababu za uchokozi wao (Halabiyya, J. 3, uk. 227).

Hulka za Mtume Mtukufu[saw] zina pande nyingi kiasi hiki kwamba haiwezekani kuzizungumzia kikamilifu katika hizi kurasa chache, bali kwa kuwa hiki ambacho kimsingi hakina madhumuni ya kuzungumzia hulka zake sisi ni sharti, kwa kutilia maanani kima cha Kifungua Mlango cha kawaida kama hiki, tutosheke na yale ambayo tayari yameishazungumziwa.

MKUSANYO WA KURANI

Imeoneshwa kwenye sehemu tangulizi ya hiki 'Kifungua Mlango' kwamba hapana hata matini moja ya vile vitabu, vinavyosemekana vilifunuliwa kabla ya Kurani, ambayo imehifadhiwa yote nzima. Matini hizo zote zimechafuliwa vibaya kiasi hiki kwamba mtafuta-kweli mwenye shauku analikuta kuwa jambo lisilowezekana kuiteua yoyote ile kuwa ndio mwongozo wa mwenendo ulio sawa. Kinyume chake, matini ya Kurani imehifadhiwa yote nzima na kila neno lake limetufikia likiwa bila ya mapenyezo na uchafuzi kama vile vile lilivyokuwa wakati lilipofunuliwa kwa Mtume Mtukufu[saw] miaka elfu moja mia tatu na hamsini iliyopita.

Kurani ilianza kufunuliwa ulipoanza wadhifa wa Mtume Mtukufu[saw]. Wahyi wa kwanza kabisa, zikiwemo aya chache tu, ulipokelewa naye katika Pango la Hiraa. Baada ya hapo wahyi uliendelea kushuka hadi kifo chake. Kwa hiyo kipindi kizima ambamo humo ilifunuliwa Kurani nzima kiliendelea kwa muda wa miaka ishirini na mitatu. Sisi twajua, kutokana na ushuhuda wa watu waliokiishi wakati wake, ya kuwa hapo mwanzoni wahyi ulimshukia Mtume[saw] kwa vipindi na katika vijisehemusehemu, lakini kadri ulivyopita wakati, ukazidi

kuongezeka kuwa wingi na kufululiza hadi kufikia miaka ya mwisho mwisho ya maisha yake ukawa wabubujika ukikaribia kuwa kama mkondo wa mfululizo. Mojawapo ya sababu ya mambo kuwa hivyo miongoni mwa sababu zingine ilikuwa ni hii ya kwamba mafundisho yaliyokuwemo ndani ya wahyi huu yalikuwa ni mageni kabisa na haikuwa rahisi kwa watu kuelewa maana hasa za mafundisho haya. Hivyo basi, Kurani ikafunuliwa vijipande-vipande hapo awali. Lakini baada ya kanuni za Islam za kimsingi kuwa zimeeleweka sawasawa na kwa namna fulani kuwa sasa ni rahisi kwa watu kufahamu mafundisho na mambo yanayoangaziwa Kuranini wahyi ukaanza kushuka upesi-upesi tena kwa kiasi kikubwa zaidi. Shabaha yenyewe ilikuwa kwamba Waislamu wote wawe watawezeshwa kuyaelewa kabisa mafundisho ya Kurani. Sababu nyingine ilikuwa hii ya kwamba idadi ya Waislamu mwanzoni ilikuwa ni ndogo sana na kwa vile Mwenyezi Mungu alikusudia kwamba maneno ya Kurani ni sharti yahifadhiwe kwa uangalifu mkubwa na kwamba yasitokee kuwa ni kitu cha kutiliwa shaka, vijipande vidogovidogo tu vilifunuliwa kwa wakati mmoja hapo awali na daima palikuwepo na kipindi cha kukatizwa wakati mwingine kilichochukua miezi kadha, baina ya kufunuliwa kwa fungu moja la aya na kufunuliwa kwa fungu jingine. Kwa njia hii wale Waislamu wachache wakawezeshwa kuhifadhi wahyi huo wote kwa moyo, ili kwamba kuhifadhiwa kwa maneno ya Kurani kusitilike shaka kabisa. Idadi ya Waislamu ilipoanza kuongezeka na kulindwa na kuhifadhiwa kwa Kurani kurahisika, nao wahyi ukaanza kufika upesi-upesi. Karibu na mwisho wa maisha ya Mtume Mtukufu[saw] idadi ya Waislamu ilizidi laki moja na kuhifadhiwa kwa mayo kwa Kurani kukawa rahisi. Wakati huo wahyi ulizidi kuja kwa kasi zaidi. Kwa hii plani ya Mungu usafi wa maneno ya Kurani ukahakikika.

Wakati wa Ukhalifa wa Hadhrat Uthman[ra] nakala saba za Kurani zilipelekwa sehemu mbalimbali za himaya ya Waislamu na hizo nazo zikawa ndizo matini ya asili ambazo kutokana nazo nakala zingine zilinakiliwa na baada ya hapo katika kila zama mamia ya maelfu ya

watu wamekuwa na desturi ya kuhifadhi Kurani nzima kwa moyo. Hata wale maadui sugu wa Islam hawadai kwamba pametokea uchafuzi wowote wa maneno ya Kurani tangu wakati wa Hadhrat Uthman[ra]. Wale wanaotafuta kuzusha shuku dhidi ya usafi wa maneno ya Kurani huelekeza lawama zao kwenye kile kipindi cha baina ya kifo cha Mtume Mtukufu[saw] na Ukhalifa wa Hadhrat Uthman[ra].

Kila alipofunuliwa sehemu yoyote ya Kurani, yeye alikuwa akiihifadhi moyoni na, kwa kuwa aliisoma Kurani mfululizo toka mwanzo hadi mwisho, basi yeye wakati wote alikuwa nayo moyoni mwake ile sehemu nzima ya Kurani iliyofunuliwa. Pamoja na desturi hii njia hizi zifuatazo zilitumiwa kulindia na kuhifadhia kikamilifu maneno ya Kurani:

NJIA ZILIZOTUMIWA KULINDIA NA KUHIFADHIA MANENO YA KURANI

(1) Mara tu wahyi ulipopokelewa na Mtume Mtukufu[saw] huo ulirekodiwa kimaandishi moja kwa moja kutoka kinywa chake. Wanafahamika watu kadha kuwa ndio waliotumiwa na Mtume Mtukufu[saw] kwa madhumuni haya. Miongoni mwao majina ya hawa kumi na watano wafuatao yametajwa hadithini (Fat-hul Bari, J. 9, uk. 19):

1. Hadhrat Zaid bin Thabit[ra]
2. Hadhrat Ubayy ibn Ka'b[ra]
3. Hadhrat Abdullah bin Sa'd bin Abi Sarh[ra]
4. Hadhrat Zubair bin al-'Awwam[ra]
5. Hadhrat Khalid bin Sa'id bin al-'Aas[ra]
6. Hadhrat Aban bin Sa'id bin al-'Aas[ra]
7. Hadhrat Handhala bin ar-Rabii' al-Asadii[ra]
8. Hadhrat Mu'aiqib bin Abi Fatima[ra]
9. Hadhrat Abdullah bin Arqam az-Zuhr[ra]
10. Hadhrat Shurahbil bin Hasana[ra]
11. Hadhrat Abdullah bin Rawaha[ra]
12. Hadhrat Abu Bakr[ra]

13. Hadhrat Umar[ra]

14. Uthman[ra]

15. Hadhrat Ali[ra]

Mtume Mtukufu[saw] kila alipopata wahyi, basi alikuwa yeye kumwita mmoja wa hawa waja na kuandikisha maneno ya ule wahyi aliokuwa ameupokea.

(2) Kama inavyofahamika sana, zile sala tano za kila siku ni faradhi kwa kila Mwislamu na sharti kipande cha Kurani kisomwe katika kila moja ya sala hizo kusudi kila Mwislamu ajue sehemu ya Kurani kwa moyo. Basi kama kila mia ya Masahaba wa Mtume[saw] waliokuwa zaidi ya laki moja walikuwa kati yao wameihifadhi Kurani nzima kwa moyo basi ni sharti iwe Kurani nzima ilikuwa imehifadhiwa mara elfu nyoyoni mwa Masahaba wake.

(3) Sheria nzima, itikadi, falsafa, miongozo ya maadili na mafundisho mengine ya Islam vimo ndani ya Kurani. Ujenzi na ukuzaji wa taifa wavihitaji hivi vyote. Mtume Mtukufu[saw] alikuwa akiwafundisha Waislamu yale majukumu na zile nyadhifa mbalimbali zilizo katika ujengaji na uongozaji wa jamii ya kistaarabu na ya malezi mema. Mathalan, palihitajikana mahakimu, wanasheria, wafafanuaji wa itikadi na wale waliofafanua amri za Islam za kisheria na maadili na watu hawa wasingeliweza kutekeleza wajibu wao barabara isipokuwa wawe walikuwa wameijua Kurani kwa moyo. Hivyo basi, watu wote sampuli hii walikuwa na dharura ya kuijua Kurani nzima kwa moyo.

(4) Mtume Mtukufu[saw] alikuwa daima akisisitizia sana ustahilifu wa kuijua Kurani kwa moyo, kiasi hiki kwamba yuwaripotiwa kupata kusema kwamba kama mtu akiijua Kurani kwa moyo, basi ataepushiwa adhabu ya Jahanamu. Mwenyezi Mungu alikuwa amemjazi Mtume Mtukufu[saw] masahaba ambao daima walitamani kujichumia njema kwa kila njia hivi kwamba alipotoa tangazo hili idadi kubwa miongoni mwao walianza kuihifadhi Kurani kwa moyo, wakiwemo wale ambao ndimi zao hazikuwa fasaha sana na hawakuwa wenye elimu yoyote. Imam Ahmad Hambal amesimulia

kufuatia Hadhrat Abdullah bin Umar[ra] ya kuwa mtu alimjia Mtume Mtukufu[saw] na akmwambia: "Ewe Mtume wa Allah! Mimi naijua Kurani kwa moyo lakini akili yangu haifahamu vizuri maana zake." Hii yaonesha kwamba haikuwa tu watu wenye elimu bali hata watu wa kawaida walikuwa na mazoea ya kuihifadhi Kurani kwa moyo. Hadithi nyingine, iliyosimuliwa na Imam Ahmad Hambal kufuatia huyo huyo Hadhrat Abdullah bin Umar[ra], yasema kwamba mtu alimletea Mtume Mtukufu[saw] mwanawe na akasema: "Ewe Mtume wa Allah! Huyu mwanangu hushinda akisoma Kurani mchana kutwa na kulala usiku mzima". Mtume Mtukufu akatamka akisema: "Sasa, pana lipi la kukutia mshawasha? Mwanao hushinda akimkumbuka Mwenyezi Mungu na usiku badala ya kuleta udhia wowote yeye hujilalia." Kisa hiki chaonesha kwamba hata wale watu wa kawaida waliokiisha mbali na Mtume Mtukufu[saw] walikuwa wameanza desturi ya kuhifadi Kurani kwa moyo.

WAKUFUNZI WA KURANI

(5) Kadri shauku ya watu ya kuhifadhi Kurani kwa moyo ilivyoongezeka, Mtume Mtukufu[saw] aliteua wakufunzi wakuu wanne wa Kurani ambao walikuwa wakiikariri chini ya usimamizi wa Mtume Mtukufu[saw] na kisha kuwafunza watu wengine kuihifadhi kwa moyo. Hawa wanne nao wakawafundisha watu kadha wengine ambao nao wakawa stadi kuifundisha Kurani. Hawa wanne walikuwa ni:

1. Hadhrat Abdullah bin Mas'uud[ra]
2. Hadhrat Saalim Maula Abi Hudhaifa[ra]
3. Hadhrat Mu'adh bin Jabal[ra]
4. Hadhrat Ubayyi bin Kab[ra]

Hao wawili wa kwanza walikuwa ni watu wa Makka waliokuwa wamehamia Madina na hao wawili wa mwisho walikuwa ni Ma-Ansari. Hadhrat Abdullah bin Mas'uud[ra] alikuwa akishughulika kama mpagazi, Hadhrat Saalim[ra] alikuwa ni mtumwa mwachiliwa huru, na Hadhrat Mu'adh[ra] na Hadhrat Ubayy[ra] walikuwa ni wawili wa

viongozi wa Madina. Kwa hiyo, Mtume[saw] alichagua wakufunzi wa Kurani toka miongoni mwa wenyeji mbalimbali asije mtu yeyote akapata shida kuwaendea na kujifunza kutoka kwao. Mtume Mtukufu[saw] alikuwa akisema: "Wale miongoni mwenu wanaotaka kujifunza Kurani basi na wakajifunze kwa Abdullah bin Mas'uud, Saalim Maula Abi Hudhaifa, Mu'adh bin Jabal au Ubayyi bin Ka'b (Muslim). Hawa masahaba wanne walikuwa wameisoma Kurani nzima chini ya uangalizi wa Mtume Mtukufu[saw]. Bali masahaba wengine wengi nao pia walikuwa wamesoma vipande vipande vya Kurani moja kwa moja kutoka kwa Mtume Mtukufu[saw]. Yasimuliwa kwamba safari moja alipokuwa Hadhrat Abdullah bin Mas'uud[ra] akisoma Kurani Hadhrat Umar[ra] alishauri kwamba neno fulani lilikuwa litamkwe kimaalumu. Hadhrat Abdullah bin Mas'uud[ra] akalalamika akisema kwamba yeye alikuwa amefundishwa na Mtume Mtukufu[saw] kulitamka neno lile vile alivyokuwa amelitamka. Hadhrat Umar[ra] akampeleka kwa Mtume Mtukufu[saw] na kunung'unika ya kuwa yule mwenziwe hakuisoma Kurani vilivyo. Mtume Mtukufu[saw] akamtaka Hadhrat Abdullah bin Mas'uud[ra] aisome ile sehemu iliyozusha maoni yanayotofautiana, na alipoisoma Mtume[saw] akasema, barabara kabisa. Hapo Hadhrat Umar[ra] akasema kwamba nilikuwa nimefundishwa nawe kulitamka neno lile kivingine. Mtume Mtukufu[saw] akamtaka aisome aya yenyewe, na alipofanya hivyo akamwambia na hivyo navyo ni barabara kabisa.

Kisa hiki chaonesha kwamba pamoja na wale Masahaba wanne ambao Mtume Mtukufu[saw] alikuwa akiwasomesha Kurani nzima walikuwepo wengine ambao walikuwa wakijifunza kwake sehemu sehemu za Kurani. Kauli ya Hadhrat Umar[ra] ya kwamba alikuwa amefundishwa kutamka neno fulani kwa njia maalumu yaonesha kwamba yeye naye alikuwa akijifunza sehemu za Kurani kutoka kwa Mtume Mtukufu mwenyewe[saw].

Ile tofauti iliyotokea baina ya Hadhrat Umar[ra] na Hadhrat Abdullah bin Mas'uud[ra] haikuhusikana na mageuzi yoyote ya maneno ya Kurani. Hii ilihusikana tu na irabu moja. Hali ya kuafikiana kwa

baadhi ya irabu ni sifa ya kipekee ya lugha ya Kiarabu na kuhusu vitenzi fulani kubadilishana irabu kwa irabu nyingine kwaruhusiwa wala hakuathiri maana. Mathalan, wakati mwingine herufi yenye irabu ya 'a' kuitamka kwa irabu ya 'i' kunakubalika kilugha ama kama kipindua-ulimi cha kawaida au kama mazoea ya kikabila au kifamilia. Lakini katika hali hizo zote mbili maana ya kitenzi chenyewe inabakia pale pale. Kwa kufahamu mbinu hizi za kilugha, Mtume Mtukufu[saw] kwa maelekezo ya kiungu akatoa ruhusa yatumike matamshi haya na haya, kwa kuwa kutumika kihivyo hakukuwa na athari mbaya ya kubadili maana au tafsiri za maneno. Kwa kuwa watu wasioongea lugha ya Kiarabu sifa hii ya kipekee ya lugha ya Kiarabu hawakuizoelea, basi wao huelekea kujiwa na hii dahana ya kimakosa kwamba matamshi hayo ya hivi na vile yanamaanisha mabadiliko katika matini ya Kurani na kwamba Mtume Mtukufu[saw] alikuwa na mazoea ya kumsomesha mtu mmoja aya fulani za Kurani kwa njia moja na mwingine kumsomesha kwa njia nyingine. Kusema kweli hapakufanyika kitu chochote cha aina hiyo. Hizi tofauti ambazo zimekuja kuwa jambo la kuzungumziwa hazikuwa ni tofauti za mageuzo ya maneno ya Kurani wala hata hayakuwa mageuzi ya neno. Zote zilihusikana na matamshi ya irabu ambayo hayakubadilisha kivyovyote vile maana au uzito wa neno. Tofauti ya pekee ilikuwa kwamba baadhi ya makabila au familia, kwa kuzoelea kwao kutamka vitenzi fulani kwa vina mahususi na kwa njia fulani, waliruhusiwa kufanya hivyo.

MAKARII WA KURANI

Pamoja na wale wakufunzi wanne wakuu wa Kurani waliokuwa wamefunzwa na Mtume Mtukufu[saw] mwenyewe palikuwepo na makarii fulani wengine waliokuwa wameihifadhi Kurani nzima kwa moyo. Miongoni mwao walikuwemo hawa:

(1) Hadhrat Zaid bin Thabit[ra], aliyekuwa pia mmoja wa waandishi wa wahyi.

(2) Hadhrat Abu Zaid Qais bin As-Sakan[ra] aliyekuwa Ansari wa

kabila la Banu Najjaar, ambalo ndilo lililokuwa kabila la mamake Mtume[saw] (Fat'hul-Baari, J. 9, uk. 49).

(3) Hadhrat Abu Dardaa Ansari (Bukhari).

(4) Hadhrat Abu Bakr[ra], ambaye kumhusu yeye pia inasimuliwa kwamba alikuwa na mazoea ya kuhifadhi Kurani kwa moyo.

(5) Hadhrat Ali[ra] si tu kwamba aliijua Kurani kwa moyo bali punde tu baada ya kifo cha Mtume Mtukufu[saw] yeye aliipanga Kurani sawa na vile ilivyokuwa imefunuliwa.

(6) Nasai yuwasimulia kwamba Hadhrat Abdullah bin Umar[ra] naye pia aliijua Kurani nzima kwa moyo na alikuwa akiisoma yote usiku mmoja. Mtume Mtukufu[saw] alipojua hivyo akamwambia awe akiisoma kwa muda wa mwezi mmoja na kutojaribu kusoma Kurani nzima usiku mmoja kwani kufanya hivyo huenda kukamwia mzigo mzito.

(7) Hadhrat Abu 'Ubaid[ra] yuwasimulia kwamba miongoni mwa Muhajirina, hawa wafuatao walikuwa wameihifadhi Kurani nzima kwa moyo: Hadhrat Abu Bakr[ra], Hadhrat Umar[ra], Hadhrat Uthman[ra], Hadhrat Ali[ra], Hadhrat Talha[ra], Hadhrat Sa'd[ra], Hadhrat Ibn Mas'uud[ra], Hadhrat Hudhaifa[ra], Hadhrat Saalim[ra], Hadhrat Abu Huraira[ra], Hadhrat Abdullah bin Sa'ib[ra], Hadhrat Abdullah bin Umar[ra] na Hadhrat Abdullah bin Abbas[ra].

Na miongoni mwa wanawake, hawa wafuatao waliijua Kurani nzima kwa moyo: Hadhrat Aisha[ra], Hadhrat Hafsa[ra] na Hadhrat Ummi Salama[ra].

Wengi wa hawa walikuwa wameihifadhi Kurani nzima maishani mwa Mtume Mtukufu[saw] na wengine wao baada ya kifo chake. Ibn Abi Dawud yuwasimulia katika kitabu chake, kiitwacho Ash-Shari'ah, ya kuwa miongoni mwa Muhajirina Hadhrat Tamim bin Aus ad-Dari[ra] na Hadhrat 'Uqba bin 'Aamir[ra] nao pia walikuwa wakiijua Kurani nzima kwa moyo. Wanahistoria wengine wanaongezea katika orodha hii majina ya Hadhrat 'Amr bin al-Aas[ra] na Hadhrat Abu Musa Ash'ari[ra].

Wale waliofahamika sana kuwa waliihifadhi Kurani nzima kwa moyo

miongoni mwa ma-Ansari walikuwa ni hawa wafuatao:

Hadhrat 'Ubada bin Samit[ra], Hadhrat Mu'adh[ra], Hadhrat Majma' bin Haritha[ra], Hadhrat Fudhala bin 'Ubaid[ra], Hadhrat Maslama bin Mukhallad[ra], Hadhrat Abu Dardaa[ra], Hadhrat Abu Zaid[ra], Hadhrat Zaid bin Thabit[ra], Hadhrat Ubayy bin Kab[ra], Hadhrat Sad bin 'Ubada[ra], na Hadhrat Ummi Waraqa[ra].

KURANI YAHIFADHIWA KWA MOYO

Kusema kweli yafahamika sana kwamba idadi kubwa ya Masahaba wa Mtume Mtukufu[saw] walikuwa wakiijua Kurani nzima kwa moyo. Kama ilivyotangulia kusimuliwa katika kurasa za mwanzo-mwanzo kuhusikana na kile kisa cha mahali paitwapo Bi'ri Ma'una, kwenye mwaka wa nne wa Hijra Mtume Mtukufu[saw] aliyatumia makabila fulani Mashaba zake sabini wakawe wakufunzi na kila mmoja wao aliijua Kurani kwa moyo.

Wale waliokuwa wakiijua Kurani nzima kwa moyo walipitisha sehemu kubwa ya wakati wao wakiisomea wengine saa zote za mchana na usiku. Hafidh Abu Ya'la yuwasimulia kwamba safari moja Mtume Mtukufu[saw] aliambiwa kwamba Hadhrat Abu Musa[ra] alikuwa akiwafundisha watu usomaji wa Kurani katika nyumba yake. Mtume Mtukufu[saw] akataka apelekwe mahali ndani ya nyumba ile angelipoweza kumsikiliza Hadhrat Abu Musa[ra] bila kujulikana na wale waliokuwepo. Basi akapelekwa mahali kama hapo kule nyumbani na baada kumsikiza Hadhrat Abu Musa[ra] akisoma Kurani akaridhia usomaji wake na ukamfurahisha mno na akatamka akisema: "Yuwasoma Kurani kwa ule mtindo wa kuvutia wa Nabii Daudi[as]" (Muslim, Kitabus-Salat). Kisa hiki chaonesha kwamba Mtume Mtukufu[saw] alifanya juhudi kusimamia usomaji wa Kurani wa watu minghairi ya wale wanne aliokuwa ameteua kama wakufunzi wakuu wa Kurani na alitaka sana kuona kwamba haliingii kosa lolote katika usomaji wao.

Hadhrat Imam Ahmad Hambal yuwasimulia kufuatana na kauli ya Hadhrat Jabir bin Abdullah[ra] ya kuwa safari moja Mtume Mtukufu[saw] alipofika msikitini aliwakuta watu wakisoma Kurani na akatamka

akisema: "Someni Kurani na isomeni vizuri na jitahidini kujipatia radhi ya Mwenyezi Mungu kwa njia hiyo, kabla haujaja wakati ambapo watu wataisoma sawasawa, lakini kwa lengo la kuifanya kuwa ni kiwezesho cha kujichumia riziki zao badala ya kuwa ni kiwezesho cha kujitakasia nyoyo zao" (Musnad Ahmad bin Hanbal, J. 3).

Hadhrat Jabir bin Abdullah[ra] yuwasimulia kwamba wale waliokuwa wakiisoma Kurani katika kisa hiki hawakuwemo Muhajirin na ma-Ansari tu bali pia wakazi wa jangwani na wasiokuwa Waarabu.

Wale waliokuwa wamepata ustadi wa usomaji wa Kurani maishani mwa Mtume Mtukufu[saw] waliweza kuhesabiwa kwa maelfu. Punde tu baada ya kifo cha Mtume Mtukufu[saw], wakati Musailima (Kadhabu) alipotangaza vita na kwenda kuishambulia Madina akiongoza laki nzima ya wapiganaji, Hadhrat Abu Bakr[ra] alimtuma Hadhrat Khalid bin Walid[ra] akiongoza askari elfu kumi na tatu kwenda kukabiliana naye. Kwa kuwa kundi hili lilikuwa na wengi ambao walikuwa wamesilimu hivi punde tu na walikuwa bado hawajajipatia moyo wa Islam au desturi zake, jeshi la Waislamu lilitiwa mapengo hapa na pale. Hapo baadhi ya Masahaba wa Mtume Mtukufu[saw] wakatoa rai ya kwamba wale wote waliokuwemo jeshini walioijua Kurani nzima kwa moyo wafanywe kikosi kimoja na wapelekwe mbele kabisa kukabiliana na watu wa Musailima. Ilionelewa kwamba kwa vile watu hawa walitambua thamani halisi ya Islam na haja ya wao kuilinda kwa maisha yao, basi jazba na uaminifu wao vitasimama imara dhidi ya idadi kubwa mno ya maadui. Hadhrat Khalid bin Walid[ra] akairidhia rai hii na akateua kikosi maalumu cha wale walioijua Kurani nzima kwa moyo. Hawa walifikia elfu tatu. Kikosi kikalishambulia jeshi la Musailima kwa ukali kiasi hiki kwamba lililazimika kurudi nyuma na hatimaye kuzingirwa na kuangamizwa. Wakati wa kisa hiki hawa elfu tatu ukelele wao wa kivita ulikuwa ni huu: "Enyi mjuao Sura al-Baqara kwa moyo" (sura al-Baqara ilitajwa kwani ndiyo Sura ndefu zaidi ya Kuran). Watu mia tano wa kikosi hiki spesheli cha watu elfu tatu waliuawa katika vita hivi. Kasema Sir William Muir: "Damu miongoni mwa Makarii ilimwagika kwa wingi kiasi cha kumpatia

Umar wazo la kwanza kabisa la kuyakusanya pamoja haya Maandiko Matakatu isije sehemu yake yoyote ikapotea" (The Caliphet).

Hivyo basi twakuta ya kwamba katika maisha ya Mtume Mtukufu mwenyewe[saw] Kurani ilikuwa ikirekodiwa kimaandishi, ilihifadhiwa kwa moyo na ilikuwa ikisomwa mfululizo na maelfu ya watu waliijua yote kwa mayo, ingawaje haikuwa imekusanywa katika jalada moja.

KURANI YAKUSANYWA KATIKA JALADA MOJA

Ilipoonekana kwamba makarii mia tano wa Kurani walikuwa wameuawa kwenye mapigano na jeshi la Musailima, Hadhrat Umar[ra] akamshauri Hadhrat Abu Bakr[ra] (Aliyekuwa Khalifa wakati huo) akimwambia kwamba kama wale waijuo Kurani kwa moyo watatokea kuuawa vitani kwa wingi jinsi hiyo basi kuhifadhi usafi wa matini yake litakuwa ni jambo gumu na kwamba hivyo basi wakati umewadia ambapo Kurani nzima haina budi kukusanywa katika jalada moja. Hadhrat Abu Bakr[ra] kwanza alisitasita lakini hatimaye akaridhia wazo hilo na akamteua Hadhrat Zaid bin Thabit[ra], akiwa ni mmoja wa wale waliokuwa wakiandika Kurani moja kwa moja toka kauli ya Mtume Mtukufu[saw], kuikusanya matini ya Kurani kwenye jalada moja na akachagua Masahaba mashuhuri wa Mtume Mtukufu[saw] kumsaidia katika kazi hii. Hadhrat Abu Bakr[ra] akaagiza akisema kwamba matini ya Kurani yakusanywe kutoka vile vipande vipande vya maandiko yake na kwamba usahihi wa matini yenyewe ni sharti uthibitishwe na watu wawili walioijua Kurani nzima kwa moyo. Punde si punde kazi hii ikamalizika na matini yaliyoandikwa ya Kurani nzima kuwekwa katika jalada moja, iliyothibitishwa na wale walioijua Kurani nzima kwa moyo kuwa ni sahihi kabisa. Kutokana na ukweli huu, je panaweza pakawa na sababu hata chembe ya kudai eti mageuzo katika maneno ya Kurani yalikuwa yamepenya ndani kunako na kipindi cha baina ya kifo cha Mtume Mtukufu[saw] na ukusanyaji wa Kurani katika jalada moja chini ya uongozi wa Hadhrat Abu Bakr[ra] na usimamizi wa Hadhrat Zaid bin Thabit[ra]? Je, linaweza likaingia akilini wazo kuwa eti ugumu wowote ungeweza ukapatikana

katika kukusanywa kwenye jalada moja kwa Kitabu kilichokuwa kikisomwa kwa mfululizo kila siku na kundi kubwa la watu, ambacho maneno yake yote yalikuwa yakisomwa toka mwanzo hadi mwisho kwenye mwezi wa Ramadhani na watu waliokuwa wameyahifadhi yote kwa moyo wakiwasomea Waislamu waliokusanyika kwenye sala ya jamaa, humo salani mkiwa na kundi kubwa la watu waliokijua Kitabu chote kizima kwa moyo, na kilichoandikishwa na Mtume Mtukufu mwenyewe[saw] kadiri wahyi wenyewe ulivyokuwa ukipokelewa wakati baada ya wakati; na tena hususan wakati ambapo kazi ya ukusanyaji ilikuwa imewekwa chini ya uangalizi wa mtu aliyekuwa yeye mwenyewe mmoja wa waandikaji wa Kurani na ambaye alikuwa ameihifadhi yote kwa moyo? Lingekuwa jalada hili lililokusanywa lina kosa hata moja kinyume na maneno aliyoyaandikisha Mtume Mtukufu[saw] na kinyume na vile yalivyohifadhiwa kwa moyo chini ya uongozi wake na kundi kubwa la watu, basi kosa hilo lingegunduliwa mara moja na kusahihishwa. Hivyo, hali ya uhalisi na usahihi wa maandiko ya Kurani inathibitishwa na dalili zisizopingika kabisa. Hapana usahihi wa maandiko mengineyo humu duniani usiokuwa na uwezekano wa kutiliwa shaka kama vile Kurani.

NAKALA ZILIZOSAWAZIKA ZA KURANI

Wakati wa Ukhalifa wa Hadhrat Uthman[ra] yalianza kupokelewa manung'uniko kwamba makabila mbalimbali yalikuwa yakitamka kivyao maneno fulani ya Kurani na kwamba kutokana na hali hii watu wasiokuwa Waislamu waliosikia maneno haya yakitamkwa hivi na vile walipatwa na fikara ya kimakosa kwamba yalikuwemo mageuzo katika maneno ya Kurani. Tayari imekwisha elezwa kwamba hizi zilikuwa ni tofauti zilizotokana na mazoea ya kikabila au kifamilia na hazikuhusikana kwa vyovyote vile na mageuzo yoyote ya matini wala hazikuathiri maana ya neno lolote. Hata hivyo Hadhrat Uthman[ra] alilionelea kuwa ni jambo la busara kupiga marufuku tofauti zozote hata zile za kimatamshi ya irabu. Yeye akaandikisha nakala za yale matini yaliyokuwa yamekusanywa wakati wa Hadhrat

Abu Bakr[ra] na hizi akazipeleka sehemu mbalimbali za himaya ya Waislamu na akatoa maagizo ya kwamba kusiruhusiwe tofauti zozote katika usomaji wa Kurani katika yale matini yaliyosawazika, hata kama iwe ni katika utamkaji wa irabu peke yake. Wakati wa Mtume Mtukufu[saw] hali ya kijamii maishani ilifuatia misingi ya kikabila; kila kabila likiishi kivyake na bila kutegemea wengine. Katika usemaji wao walizoea kutamka maneno fulani kivyao. Waliposilimu wakafungamanishwa katika jamii moja ya kistaarabu na mara Kiarabu kikawa ndicho mbebaji wa ustaarabu ule. Hali ya kujua kusoma na kuandika ikaenea haraka miongoni mwa Waarabu na ikamrahisikia kila mmoja wao kutumia matamshi ya kisawasawa ya kila neno la Kiarabu. Lahaja ya Makka ikatokea kuwa ni kipimio kwa ajili hii. Hivyo basi, kufikia wakati wa Hadhrat Uthman[ra] haikuwepo tena sababu nzuri ya kuwepo na tofauti katika utamkaji wa irabu kulingana na mazoea ya kikabila kwenye usomaji wa Kurani, hususan wakati ambapo tofauti hizo zilielekea kueleweka visivyo akilini mwa wasiokuwa Waarabu. Hatua thabiti tena iliyofaa ya Hadhrat Uthman[ra] imefanywa kuwa ndio msingi wa shutuma za waandishi wasiokuwa Waislamu ya kuwa yeye alifanya mabadiliko Kuranini au kuwa zile nakala za Kurani alizozitoa yeye zilikuwa kwa namna fulani tofauti na matini iliyosawazishwa au tofauti na maneno jinsi yalivyofunuliwa kwake Mtume Mtukufu[saw]. Waandishi hawa wanadhani kwamba wao wamegundua silaha kali ya mashambulio dhidi ya usahihi wa maneno ya Kurani, lakini wale wanaoifahamu lugha ya Kiarabu pamwe na historia ya kukusanywa pamoja kwa Kurani wanajichekea tu kwa huu utovu wa busara uliooneshwa na wasingiziaji hao.

Hapana shaka kabisa kwamba matini ya Kurani iliyoidhinishwa na Hadhrat Uthman[ra] ilikuwa ni ile ile iliyofunuliwa kwa Mtume Mtukufu[saw]. Bali nafasi ya tashwishi yazidi kupungua zaidi ya kwamba maneno ya Kurani yameendelea kuwa safi kabisa na bila kuchafuliwa tangu alipokuwa Hadhrat Uthman[ra] amepeleka nakala za ile matini iliyosawazishwa hadi sehemu mbalimbali za himaya ya Waislamu. Nakala hizo nazo zikanakiliwa kwa wingi tena kwa haraka haraka

kiasi hiki kwamba punde si punde takriban kila Mwislamu msomi alijimilikia nakala yake mwenyewe ya Kurani. Yarekodiwa kwamba miaka michache ulipokuwepo mzozo baina ya Hadhrat Ali[ra] na Mu'awiya askari wa jeshi la Mu'awiya walifungilia nakala za Kurani kwenye ncha za mafumo yao na kutangaza kwamba Kurani na ihukumu baina ya hayo makundi mawili yanayopingana (The Caliphate). Kisa hiki chaonesha kwamba kufikia wakati huo lilikuwa ni jambo la kawaida kwa kila Mwislamu kuwa na nakala yake mwenyewe ya Kurani.

DESTURI YA KUIHIFADHI KURANI KWA MOYO ILIENDELEA

Kusoma, kunakili na kueneza Kurani daima yamehesabiwa kuwa ni amali njema sana katika Islam. Historia yatuambia kwamba mawalii wa Kiislamu na hata wafalme Waislamu walikuwa wakijishughulisha na kunakili maneno ya Kurani. Hata katika nchi zisizokuwa za Kiislamu, kama vile India, karne nyingi baada ya wakati wa Mtume Mtukufu[saw], ambapo kwa njia nyingi Waislamu walikuwa wameiga desturi na mila za Kibaniani, Mfalme Mkuu Aurangzeb, wa jamii ya Kimughali, alikuwa akipitisha wakati wake wa burudani akinakili maneno ya Kurani. Imerekodiwa kwamba yeye alikuwa ameandika kwa mkono wake mwenyewe nakala saba za Kurani nzima.

Desturi ya kuhifadhi Kurani kwa moyo haikuishilizia kwenye wakati wa Mtume Mtukufu[saw] au wakati wa Makhalifa. Hata baada ya nakala za kuandikwa za Kurani kuanza kuongezeka na kuweza kupatikana kwa urahisi, katika kila zama Kurani ilihifadhiwa kwa moyo na idadi kubwa ya Waislamu. Makisio ya wastani ni kwamba baina ya Waislamu laki moja na laki mbili wamehifadhi Kurani kwa moyo katika vipindi vyote vya historia ya Waislamu na wakati mwingine idadi ya watu kama hao ilikuwa ni kubwa sana kuliko makisio haya. Waandishi wa Ulaya wakiwa hawayaelewi maono ya Waislamu na wingi wa mapenzi yaliyoletwa na Kurani nyoyoni mwao, wanasitasita kuamini kwamba usafi na usahihi wa maneno ya Kurani iwe ulihifadhiwa na Waislamu kwa njia hii. Wanakuta kwamba historia

hairekodi hata kisa kimoja cha mtu mmoja aliyeijua Biblia nzima kwa moyo na hivyo basi linaonekana jambo lisiloaminika ya kwamba matini nzima ya Kurani iwe ilihifadhiwa kwa moyo na idadi kubwa ya watu katika kila zama. Haina budi kukumbukwa ya kuwa ni mojawapo ya sifa kubwa ya Kurani ya kwamba maneno yake yanaimbika kabisa na kwamba yanajirahisisha sana kuhifadhika. Mwana mkubwa wa mwandishi wa kitabu hiki Mirza Nasir Ahmad mwenye shahada ya B.A. ya Chuo Kikuu cha Punjab na ya M.A. ya Chuo Kikuu cha Oxford, alikuwa chini ya uongozi wake amehifadhi Kurani nzima kwa moyo kabla hajaanza masomo yake ya shuleni. Kwenye kijiji kidogo kama vile Qadian madaktari wawili na wasomi kadha wanaijua Kurani nzima kwa moyo. Mmoja wa hawa madaktari wawili aliihifadhi Kurani nzima katika muda wa miezi minne au mitano. Babake Sir Zafrulla Khan, (aliyekuwa) Hakimu wa Mahakamu Kuu nchini India, aliihifadhi Kurani nzima katika muda wa miezi michache baada yeye kufikisha umri wa miaka hamsini. Hafidh Ghulam Muhammad, aliyekuwa wakati mmoja Mbashiri wa Jumuiya yetu wa Kisiwa cha Mrisi, aliihifadhi Kurani nzima katika muda wa miezi mitatu. Mwandishi wa kitabu hiki alipokuwa amekwenda kuhiji Makka, alikutana na mjukuu wa Munshi Muhammd Jamalud-Din Khan (aliyekuwa amepata kwa miaka kadha kuwa Waziri katika Jimbo la Bhopal, India) na akamwambia huyu mwandishi ya kwamba alikuwa ameweza kuihifadhi Kurani nzima katika muda wa mwezi mmoja. Visa hivi vyaonesha kwamba maneno ya Kurani yamo katika lugha inayojirahisisha kuhifadhika kwa moyo. Imesimuliwa kwa mwandishi wa kitabu hiki na wazee waliochakaa sana ya kwamba Mzee Mirza Gul Muhammad, babu wa kale wa Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahamadiyya, aliyeishi wakati wa Mfalme wa Kimughali, Alamgir wa Pili, alikuwa akiweka barazani mwake watu mia tano walioijua Kurani nzima kwa moyo. Mzee Mirza Gul Muhammad alikuwa ni chifu aliyekuwa akitawala eneo la maili mraba mia mbili na hamsini tu. Kwenye baadhi ya sehemu za nchi ya India, ambayo ni nchi ambako lugha ya

Kiarabu haijulikani sana, imekuwa ni desturi ya Waislamu walio wengi katika karne nyingi kuhifadhi Kurani kwa moyo.

Mojawapo ya mbinu itumiwayo na Waislamu ya kuhifadhi usafi wa maneno ya Kurani na ambayo imeshikiliwa kwa karne nyingi ni hii ya kwamba watoto wazaliwao vipofu au wapofukao macho utotoni wanahimizwa kujifunza Kurani nzima kwa moyo. Jambo hili hufanyika kwa kuonekana kwamba kwa vile kipofu hawezi kushughulikia kazi ya kawaida upungufu wake anaweza akaupatia thamani kwa njia ya yeye mwenyewe kuwa ni mlinzi wa maneno ya Kurani. Hii ni desturi iliyo ya kawaida hivi kwamba nchini India Mwislamu kipofu hupewa jina la utani la Hafidh (yaani, mlinzi) likimaanisha mtu ambaye amekuwa mlinzi wa Kurani kwa njia ya kuihifadhi kwa moyo.

Katika mwezi wa Ramadhani, Kurani nzima husomwa kwa sauti kubwa katika sala za jamaa katika misikiti yote mikubwa duniani kote. Imamu husoma Kurani na Hafidh mwingine husimama nyuma yake na kufuatilia usahihi wa usomaji, huku akimkumbusha Imam inapohitajika. Kwa njia hii Kurani nzima husomwa kwa ghaibu katika mwezi wa Ramadhani ndani ya mamia ya maelfu ya misikiti kote duniani.

Hizi ndizo mbinu mbalimbali na tahadhari zilizofuatwa na Waislamu kuhifadhi usafi na usahihi wa maneno ya Kurani, matokeo yake yakawa kwamba hata maadui wakali wa Islam hawakuwa na budi kukiri kwamba maneno ya Kurani yamehifadhiwa kikamilifu tangu wakati wa Mtume Mtukufu[saw]. Hivyo basi, inaweza ikasemwa kwa uthabiti mkubwa kwamba leo hii Kurani iko vile vile Mtume Mtukufu[saw] alivyoipatia dunia hii. Hapa chini tunanukuu ushahidi wa baadhi ya waandishi wa Ulaya kuhusu jambo hili:

Sir William Muir, katika kitabu chake kiitwacho "The Life of Muhammad" (Uk. xxviii), yuwamalizia maoni yake juu ya jambo hili hivi:

> "Ile tuliyonayo, ingawaje huenda kaisahihisha yeye mwenyewe, bado ni ile ile yake yeye mwenyewe…". "Tunaweza juu ya

misingi ya uwezekano mkubwa kusadikisha kwamba kila aya ndani ya Kurani ni uandikishaji halisi bila mapenyezo, wa Muhammad mwenyewe" (uk. xxviii).

"Ama kwa upande mwingine, pana kila uhakikisho wa nje na ndani, kwamba tunayo maneno yale yale ambayo Muhammad mwenyewe aliyaandikisha na kuyatumia (uk. xxvii). Na tena, "...na yuwamalizia angalau kwa kukaribiana na uamuzi wa Bwana Von Hammer ya kuwa tunaichukulia Kurani kuwa kweli maneno ya Muhammad chambileche Waislamu wanavyoichukilia kuwa ni neno la Mungu" (uk. xxviii).

Bwana Noldeke yuwasema hivi:

"Huenda yalikuweko makosa madogo madogo ya uandishi, lakini Kurani ya Uthman haina ila mambo halisi, ijapo penginepo kwa mpangilio wa kiajabu. Juhudi za Wanazuoni wa Ulaya kuthibitisha kuwemo mapachiko ya baadaye katika Kurani haikufua dafu" (Enc. Brit. Toleo la 9, chini ya neno "Quran").

MPANGILIO WA SURA ZA KURANI

Wakati mwingine inadaiwa kwamba mpangilio wa Sura za Kurani ni kazi ya Hadhrat Uthman[ra]. Si sawa kusema hivyo. Yajulikana vizuri sana kwamba Mtume Mtukufu[saw] alikuwa akiisoma Kurani nzima katika mwezi wa Ramadhani na baadhi ya masahaba wake nao pia walifanya vivyo hivyo. Aidha inaripotiwa katika Hadithi ya kwamba Mtume Mtukufu[saw] alikuwa akimsomea Hadhrat Jibrail Kurani nzima katika mwezi wa Ramadhani (Bukhari). Mtu asiyekuwa Mwislamu huenda asiwe tayari kuikubali kauli hii ya sasa hivi, lakini hapana shaka ya kwamba Mtume Mtukufu[saw] alikuwa akiisoma Kurani na sharti yeye awe alifanya hivyo kulingana na mpango fulani.

Baada ya kifo cha Mtume Mtukufu[saw], Hadhrat Ali[ra] kwa muda fulani hakufika kwa Hadhrat Abu Bakr[ra] (aliyekuwa amechaguliwa kuwa Khalifa). Hadhrat Abu Bakr[ra] akamwita na akamwuliza kama yeye hakupendezwa na kuchaguliwa kwake kuwa Khalifa. Hadhrat Ali[ra]

akajibu akisema haikuwa hivyo, lakini yeye alikuwa akishughulika kuinakili Kurani katika ule mpangilio ambao ilikuwa imefunuliwa, kwani alikuwa amekata shauri alipofariki Mtume[saw] kwamba yeye angelifanya kazi hii. Hii pia yaonesha kwamba wakati wa Mtume Mtukufu[saw] Kurani ilikuwa ikisomwa kwa mpangilio fulani na kwamba mpangilio wenyewe ulikuwa tofauti na ule mpangilo ambao ilikuwa imefunuliwa. Ndiposa Hadhrat Ali[ra] akaamua kuinakili katika ule mpangilio ambao ilikuwa imefunuliwa kusudi kihistoria mpangilio huo nao pia upate kuhifadhiwa. Zipo Hadithi zinazosimulia kwamba wakati wowote ilipofunuliwa aya au kundi la aya kwa Mtume Mtukufu[saw], yeye alikuwa akimwita mmoja wa waandikaiji na kumwelekeza aiandike au aziandike wakati huo huo akimwambia ni aya ya au aya za Sura ipi. Hii yaonesha kwamba wakati wa kupokea wahyi Mtume Mtukufu[saw] pia alijulishwa aya hiyo au hizo zilikuwa ni za Sura gani.

Ushahidi mkubwa zaidi, wa kuungia mkono mpangilio uliofuatwa katika ukusanyaji pamoja wa Kurani ni ushahidi wa mada yenyewe. Kuitalii Kurani huonesha kwamba mada ya kila Sura yaambatanishwa na mada ya Sura inayotangulia na ile inayofuatia. Kama mpangilio wa Kurani uliopo ulifuatwa na Hadhrat Uthman[ra] kutokana tu na urefu wa kila Sura, basi imekuwaje ya kwamba mpangilio huu wadhihirisha hali ya mfululizo wa mada hii kuhusiana na hii? Kama kwa mfano, Sura al-Fatiha ilifunuliwa Makka ndiyo Sura ya awali ya Kurani. Sura Al-Baqara ilifunuliwa Madina na kimpangilio yafuata mara tu baada ya Sura Al-Fatiha, ikiacha Sura kadha zilizokuwa zimefunuliwa hapo katikati. Waandishi wa Ulaya wanadai kwamba Sura al-Baqara ilikuwa imetangulizwa kwa kuwa eti ndiyo Sura ndefu zaidi ya Kurani. Kwanza kabisa, wao wanasahau ya kuwa Sura ya awali ya Kurani sio al-Baqara bali al-Fatiha, ambayo ni Sura fupi mno ikiwa nazo aya saba tu. Isitoshe, tuisomapo Sura al-Fatiha twakuta kwamba yamalizikia na dua ikisema: "Tuongoze katika njia iliyonyooka", na Sura al-Baqara, ambayo ndiyo Sura inayofuata, yaanzia na aya ikisema: "Hiki ni Kitabu halisi; hakina shaka ndani yake, ni

mwongozo kwa wamchao (Mwenyezi Mungu)". Kama Sura al-Baqara ilichaguliwa kuwepo baada ya "Sura al-Fatiha eti kwa sababu tu ya kuwa ndiyo Sura ndefu zaidi ya Kurani, basi inakuwaje kwamba aya yake ya mwanzo tu yaijibu aya ya mwisho ya ile Sura inayoitangulia, Sura al-Fatiha? Naam, Sura al-Fatiha imalizie na dua ya kuomba mwongozo na Sura al-Baqara nayo ianzie na aya inayoudokezea ule mwongozo uliokuwa umeombwa mwishoni mwa Sura iliyotangulia. Hili si jambo la kibahati; kwani hii hali ya mfululizo wa miktadha na mada inatukia kupatikana ndani ya Kurani nzima licha ya ukweli kwamba wakati mwingine Sura iliyofunuliwa Makka yafuatia Sura iliyofunuliwa Madina na kadhalika. Hii yathibitisha kwamba mpangilio wa Sura na aya za Kurani ulifuatwa chini ya maelekezo ya Mungu.

Na hapo basi swali linazuka ni kwa nini mpangilio uliofuatwa katika ukusanyaji pamoja wa Kurani ulitofautiana na utaratibu wa vile aya zake zilivyofunuliwa? Jibu ni kwamba Kurani ilipokuwa ikifunuliwa, yale mafundisho na itikadi zilizokuwemo humo yalikuwa ni mambo mapya kabisa tena mageni kwa Waarabu. Ilibidi mawazo yao kuzoeshwa na kupatiwa msingi wa visababisho vya itikadi na mafundisho ya Kiislamu kusudi waandaliwe kwa ajili ya mapokezi ya tafsili ya mafundisho na itikadi hizo. Wahyi wa mwanzoni hivyo basi, ulikuwa wa namna ya Sura fupi fupi zilizokuwa na mafundisho ya kimsingi kama vile Umoja wa Mungu, uraufu na kuwahurumia maskini, umuhimu wa kumwabudu Mwenyezi Mungu na manufaa ya kupatikana katika kumwabudu na kumkumbuka, na pia bishara zinazoonesha ni aina gani ya upinzani atakaotokea Mtume Mtukutu[saw] kukabiliana nao, vile Waislamu watakavyotendewa, vile Islam itakavyostawi, na vile utakavyokuwa mwisho wa maadui na wapinzani wake. Kadiri idadi ya Waislamu ilivyoongezeka na Islam kuanza kusambaa, tafsili za Sheria za Kiislamu na mafundisho yake nayo pia yakaanza kufunuliwa. Hivyo basi, mpangilio wa vile Kurani ilivyofunuliwa uliafikiana vilivyo na mahitaji ya ule wakati ilipofunuliwa, lakini ulipokuwa wahyi umeishafunuliwa na mamia ya

maelfu ya watu kuukubali na hata wasiokuwa Waislamu kuwa na habari nao, ikawa ni lazima mafundisho yake kuyawasilishia Waislamu na wasiokuwsa Waiaslmau kwa mtazamo mpya. Ili kukidhia haja hii Mtume Mtukufu[saw] akiongozwa na Mungu aliendelea kutoa maagizo kuhusu mpangilio wa kudumu wa Kurani kwa matumizi ya siku zijazo. Ama kusema kweli ni muujiza mkubwa wa Kurani ya kwamba katika mpangilo ulioziafiki vilivyo haja za ule wakati ambapo ilifunuliwa na ikakusanywa kwa ajili ya matumizi ya daima dawamu katika mpangilio ambao uliafikiana kabisa na haja za Waislamu katika nyakati za baadaye. Bali kwa kitabu kufunuliwa vipande vipande kwa muda wa miaka ishirini na mitatu katika mpangilio ulioyaafiki vilivyo mahitaji ya wakati ule na hapo hapo kuwekwa katika umbo mwafaka kwa mahitaji ya siku zijazo ilikuwa ni kazi iliyoweza tu kufanyika chini ya uongozi wa Mungu.

Uhusiano baina ya mada ya Sura moja na ile ya Sura inayofuatia umefafanuliwa kwenye maelezo tangulizi yaliyopo mwanzoni mwa kila Sura (katika tafsiri).

BAADHI YA BISHARA ZA KURANI

Imeelezwa kwenye sehemu tangulizi ya 'Kifungua Mlango' hiki kwamba Vitabu vilivyofunuliwa kabla ya Kurani vilikuwa na bishara kuihusu Kurani. Waandishi wa Ulaya wamedai kwamba Kurani yenyewe haina bishara asilani. Hii si sawa. Wahyi wa awali kabisa kupokewa na Mtume Mtukufu[saw] kwenye Pango la Hiraa unayo bishara ya kuwa kwa njia ya Kurani itatolewa elimu kwa mwanadamu ambayo yeye hakuwa amewahi kuitabaruki hapo kabla. Kama matokeo yake twakuta mifano kadha ambapo Kurani yaonesha makosa ambayo yalikuwa yamepenya ndani ya Vitabu vilivyotangulia na katika mambo haya Kurani imekuja kusadikishwa na matukio ya baadaye. Kwa mfano, ilifunuliwa ndani ya Kurani kwamba Firauni alipokufa maji mwili wake uliokolewa na kuhifadhiwa kusudi upate kuwa Ishara kwa ajili ya vizazi vijavyo. Mwenyezi Mungu Yuwasema hivi ndani ya Kurani:

> Na tukawafikisha wana wa Israeli katika bahari; lakini Firauni na majeshi yake wakawafuata kwa uasi na jeuri hadi ilimpomfikia gharika, akasema: 'Naamini kwamba hakuna mwenye kuabudiwa ila Yule wanayemwamini wana wa Israeli, na mimi ni miongoni mwa wanaomtii.' 'Je! Sasa! huku wewe uliasi zamani na ukawa miongoni mwa waharibifu. Basi leo tutakuokoa kwa (kuuweka) mwili wako kusudi uwe Ishara kwa ajili ya wa nyuma yako.' Na kwa kweli, wengi wa wanadamu wamezighafilikia Ishara Zetu (Sura Yuunus, 10:91-93).

Yaani, Mwenyezi Mungu aliwavusha bahari wana wa Israeli salama salimini na wakafuatwa na Firauni na jeshi lake kwa uadui tu na udhalimu nao wakaendelea kuwafukuza hadi walipokumbana na gharika. Na pale pale Firauni akatamka akisema: 'Sasa naamini kwamba hapana mungu ila Yule wanayemwamini Waisraeli nami najitupa Kwake.' Hapo Mwenyezi Mungu akatoa amri akisema, "Sasa watangaza imani yako ilihali mbeleni wewe uliasi na kufanya uharibifu. Basi kukulipia hili tangazo lako la imani ya dakika ya mwisho Sisi tutauepushia maangamizo mwili wako tu kusudi uwe ni Ishara kwa vizazi vinavyokuja, ingawaje kwa hakika wengi wa wanadamu wamezighafilikia Ishara Zetu." Kisa hiki hakielezewi katika Biblia wala katika historia yoyote ya Mayahudi au kwenye rekodi sashihi za wakati ule. Kurani ilikitaja kisa hiki karne kumi na tano na nusu zilizopita. Karne kumi na tatu baadaye mwili wa Firauni huyu uligunduliwa na kutambuliwa jambo lililothibitisha dhahiri shahiri bila wasiwasi wowote ule ukweli kwamba baada ya yeye kufa maji maiti yake ilivuliwa baharini ikatiwa dawa isioze na ikahifadhiwa. Licha ya kutiwa dawa isioze ingeweza kuharibiwa kwenye misukosuko mingi ilimopitia nchi ya Misri baada ya zama za Nabii Musa[as], lakini ikaukwepa uharibifu na ikahifadhiwa kuwa ni Ishara na funzo kwa wanadamu na kusadikisha ukweli wa Kurani.

Tena, wahyi wa mwanzomwanzo unayo aya hii isemawo: "Naapa kwa usiku, ufunikizao" (Al-Lail, 92:2), inayomaanisha kwamba Mwenyezi Mungu yuwaapa kwa usiku kudokezea ukweli kwamba

Islam ingekumbwa na mfululizo wa mitihani mikali na mateso. Bishara hii ilifanywa wakati hata Mtume Mtukufu[saw] hakutarajia ya kwamba watu wake wangezusha upinzani mkali dhidi ya Ujumbe wake. Punde tu baada ya kuwa yeye amepokea wahyi wa kwanza, Hadhrat Khadija[ra] alimpeleka Mtume Mtukufu[saw] kwa binamuye, Waraqa bin Naufal. Baada ya Mtume Mtukufu[saw] kumaliza kumsimulia kisa chake cha hivi punde, Waraqa alitamka akisema: "Yule malaika aliyeleta wahyi kwa Musa nawe pia amekushukia. Hata hivyo, wasiwasi wangu ni kwamba watu wako watakutesa na kukufukuza kutoka Makka." Mtume Mtukufu[saw] alistaajabishwa sana na maneno haya na kwa mshangao mkubwa akauliza akisema: "Kweli watu wangu watanifukuza?" (Bukhari). Alijua kwamba yeye alipendwa sana na watu wake wala hakutarajia kwamba angelipingwa nao. Hata hivyo, wakati ule ule Mwenyezi Mungu akamjulisha kwamba Islam na Waislamu itabidi wapitie kwenye usiku wa giza wa upinzani na mateso. Mara usiku ule ukaanza na ukaendelea kwa miaka kumi ya dhiki.

Ukweli kwamba kipindi hiki cha mateso kingeendelea kwa zaidi ya miaka kumi nao pia ulibashiriwa mahali pengine Kuranini. Katika aya za kwanza za Sura al-Fajr Mwenyezi Mungu yuwaapa kwa mausiku kumi yatakayoyatangulia mapambazuko. Sir William Muir na waandishi wengine wa Ulaya wanakubali kwamba Sura hii ilifunuliwa kwenye mwishomwisho wa mwaka wa tatu wa Ujumbe wa Mtume[saw]. Hadi kufikia wakati ule upinzani wa watu wa Makka ulikuwa bado haujajipatia sura ya ukali. Wakati huo Kurani iliwaonya Waislamu kwamba itabidi wapitie kwenye mausiku kumi ya giza la mateso. Wale wanaoielewa lugha ya Vitabu vitakatifu wanajua kwamba mara nyingi siku au usiku huwa na maana ya mwaka. Biblia inayo mifano mingi ya jambo hili ingawaje inatumia tamko la "siku" kudokezea mwaka ambapo Kurani inapodokezea kipindi cha dhiki hutumia tamko la "usiku", kwani kipindi cha dhiki ni kipindi cha giza na hudokezewa kinagaubaga zaidi na tamko la "usiku". Aya hii ilitoa onyo la mitihani mikali na mateso yangeliyoendelea kwa muda wa

miaka kumi. Kipindi hicho takriban kilianza mara tu baada ya aya hii kufunuliwa na kikaendelea kwa miaka kumi. Mdadisi mwenye husuda labda atasema kwamba zama aya hii ilipofunuliwa Mtume Mtukufu[saw], lilikuwa kwake jambo la kutarajiwa kwamba karibuni watu wa Makka wangegeuza upinzani wao kuwa mateso; lakini je, zilikuwepo njia zipi zingine, minghairi ya wahyi, ambazo kwazo yeye angeliweza kuyakinishia kwamba kipindi cha mateso kingeendelea kwa miaka kumi wala sio kwa miaka mitano au minane au kumi na miwili au kumi na mitatu? Wahyi uliweka miaka kumi na Mtume Mtukufu[saw] akaruhusiwa kukaa Makka kwa miaka kumi tu baada ya wahyi huu kuwa umepokelewa na akapatishwa taabu muda huo wote. Baada ya miaka kumi akalazimika kuitoka Makka ambayo haikuwa na kingine cha kumpatia yeye na wafuasi wake minghairi ya mateso na akafika Madina ambako Mwenyezi Mungu alijaalia fursa ya ustawi wa haraka wa Islam na Waislamu na hivyo basi kuuhama kwake mji wa Makka kukawa ndiko kifungua mlango wa kuenea na kustawika kwa Islam.

Inaweza ikaonelewa kwamba ule muda wa miaka kumi lilikuwa ni kisio tu la kuona mbele la Mtume Mtukufu[saw], lakini je, lilikuwa pia ni kisio lake la kuona mbele ya kwamba miaka kumi baada ya kupokelewa kwa wahyi huo idadi kubwa ya watu wa Madina wangesilimu na kwamba yeye angelihijiria mji ule? Je, ilikuwa ni hiari yake kuchagua kuwasilimisha watu wa Madina na je, ilikuwa ni hiari yake kuchagua kutimiza safari ya Makka hadi Madina kwa usalama salimini?

Bali wahyi haukuishia pale. Uliendelea kusema: "Na usiku utakapokuwa umepita" (Sura Al-Fajr, 89:5). Katika aya hii Mwenyezi Mungu yuwaapa kwa usiku mwingine ambao kwao giza litaondolewa, ikimaanisha kwamba baada ya mapambazuko yatakayotokea mwishoni mwa miaka kumi ya mateso giza halitatoweka kabisa kabisa bali kwamba mapambazuko yenyewe yangefuatiliwa na usiku mwingine na kwamba baadaye hapatakuwepo tena na kipindi kingine cha giza. Na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Kuhajiri kutoka Makka

kulifuatiwa na mwaka mwingine wa vitisho na mahangaiko pale ambapo Waislamu mjini Madina waliendelea kuwa katika hali ya kuhofia shambulizi la watu wa Makka. Vita vya Badr vilipiganwa yapata mwaka mmoja tu baada ya Hijra ya Mtume[saw] kutoka Makka na vita hivi, kama vile ilivyokuwa imetabiriwa katika Biblia kama vile ambavyo sisi tumekwishasema kwenye sehemu ya awali ya 'Kifungua Mlango' hiki, vilivulia mbali kilemba cha Kedari na kukomeshelea mbali msururu mzima wa mateso ya watu wa Makka dhidi ya Waislamu. Iliwabidi Waislamu waje wapigane vita vingine tena vikubwa hapo baadaye, lakini vita vya Badr viliwafanya kuwa ni taifa na himaya yake na kuwatokomezelea mbali viongozi wakubwa wakubwa wa Makureishi kwenye shimo la maangamio na mahilikisho, waliokuwa ni watesaji wabaya wa Waislamu.

Na tena, alipokuwa bado yu mjini Makka, Mtume[saw] akapokea wahyi usemao:

> Hakika Yule aliyekufaridhishia mafundisho ya Kurani atakurejesha mahali palipokadiriwa pa marejeo (Sura Al-Qasas, 28:86).

Aya hii yamaanisha kwamba Mwenyezi Mungu Ambaye amemfunulia Kurani Mtume Mtukufu[saw] na amemfaradhia wajibu wa kuitii yuwamdhaminia kwamba atamrudisha tena mjini Makka. Aya hii sio tu kwamba ilifichua ya kuwa Mtume Mtukufu[saw] hatakuwa na budi kuhajiri kutoka Makka bali pia ilikuwa nayo hii bishara ya kuwa baada ya Hijra yeye angerejea Makka akiwa mshindi. Hapana yeyote mwenye kupitia katika ile hali iliyomzunguka Mtume Mtukufu[saw] zama ilipofunuliwa aya hii angeliyeweza kudhani kwamba baada ya kuwa amelazimika kuitoka Makka yeye angelirudi kuko huko hali ya kuwa mshindi. Imo bishara nyingine ndani ya Kurani inayotabiri tukio hilo hilo na aya hiyo nayo pia ilifunuliwa zama Mtume Mtukufu[saw] alipokuwa bado yu mjini Makka:

> Na sema: "Ee Mola wangu uniingize mwingizo mwema, na unitoe kutoka kwema. Na unijaalie nguvu kutoka Kwako isaidiayo (Sura Banii Israaiil, 17:81).

Katika aya hii Mwenyezi Mungu alimwamuru Mtume[saw] kuomba ya kwamba Yeye afanye kuingia kwake (katika ule mji aliokuwa akimpeleka) kuingia kwa ufaulu na hapo baadaye amwezeshe kujitokeza kwa ufaulu kwenda kuwashambulia na awe Msaidizi wake kwenye shambulio hilo. Aya ilitabiri kwamba Mtume[saw] angehajiri kutoka Makka hadi Madina na kwamba angeishambulia Makka kutota mjini Madina na kwamba hatimaye Makka ingesalimu amri yake.

Tena, Mtume Mtukufu[saw] alipokuwa bado yuko mjini Makka alipokea wahyi usemao kwamba saa ya ushindi wa Islam inawadia na kwamba mwezi ungepasuliwa (Sura Al-Qamar, 54:2). Mwezi ndio uliokuwa ni alama ya himaya ya Waarabu na mwezi kupasuliwa ilikuwa na maana kwamba himaya ya Waarabu ilikuwa karibu ivunjiliwe mbali. Aya hii ilifunuliwa wakati ambapo Waislamu walikuwa wamelazimika kuhamia pande mbalimbali na Mtume Mtukufu[saw] kuteswa mjini Makka na hakuruhusiwa kusali sala zake ndani ya Kaaba. Safari moja alipotaka kwenda kusali ndani ya Kaaba, alibururwa nje yake na madharau. Wakati ule ulipokuwa mji mzima wa Makka ulijaa moto wa upinzani dhidi yake Mtume Mtukufu[saw] aliwaambia watu wa Makka kwamba Mwenyezi Mungu ameamua kwamba nguvu zao zitavunjiliwa mbali na kwamba ushindi wa Islam unasogea karibu. Baada ya miaka michache, bishara hii ikatimia kwa uwazi kabisa. Katika vita vya Badr sifa ya nguvu za Kedari ilitiwa komesha na beramu ya Islam kusimikwa milele na milele. Ama kwa hakika mwezi ulipasuliwa mbali kabisa. Hiyo ilikuwa ni Siku ya Hukumu kwa Waarabu. Siku hiyo mbingu mpya na ardhi mpya viliumbwa.

Islam na Waislamu vilipokuwa bado ndivyo shabaha ya dhuluma za Waarabu mjini Makka, ilifika habari kwamba Waajemi walikuwa wamewakomolea mbali Warumi kwenye vita. Habari hii ilizusha nderemo na vifijo miongoni mwa watu wa Makka, kwani Waajemi walikuwa ni waabuduo masanamu na Warumi walikuwa ni Wakristo. Watu wa Makka waliuchukulia ushindi wa Waajemi kuwa ni ndege nzuri ya kuonesha ushindi wao wenyewe wa hapo mwishoni dhidi ya Waislamu. Wakati huo Mtume Mtukufu[saw] akapokea wahyi ya kuwa

Warumi wameshindwa kwenye maeneo ya jirani lakini kunako na miaka tisa baada ya ushinde wao watakuwa tena washindi (Sura Ar-Ruum, 30:3-5); neno lililomo ndani ya aya hii, yaani بِضْع huelezea idadi ya kuanzia tatu hadi tisa. Ulipotangazwa wahyi huu miongoni mwa watu wa Makka, wao waliwacheka na kuwadhihaki Waislamu. Wakatokea baadhi yao kuwekeana bima ya ngamia mia moja na Hadhrat Abu Bakr[ra] kusisitizia kuwa bishara hiyo isingelitimia asilani. Matukio yalionesha kwamba ulikuwepo uwezekano haba sana wa Warumi kuwashinda Waajemi kwani ule ushinde wao huko Siria ulifuatiwa na ushindi mwingine zaidi wa Waajemi na jeshi la Warumi kusukumwa nyuma hatua kwa hatua hadi kwenye fuo za bahari ya Marmora. Konstantina ikatenganishwa na himaya zake za Mashariki na Dola la Kirumi kuambulia kuwa himaya ndogo. Lakini hata hivyo neno la Mungu halikuwa na budi kutimia na lilitimia. Wartumi, ingawaje wachache kwa idadi na bila ya silaha nzuri kama Waajemi, wakapata ushindi mkubwa na Waajemi kulazimika kutoroka. Walikimbilia Uajemi na Warumi wakaziteka himaya zao za Kiafrika na za Kiasia.

Kurani ina bishara kadha zihusuzo siku za usoni, ambazo baadhi yao tayari zimeishatimia. Mathalan, mahali pamoja yasema hivi:

> Bila shaka Ameziendesha bahari mbili zikutane, Baina yao pana ukingo haziuvuki... Katika hizo mbili hutoka lulu na marijani... Na majahazi ni Yake yaliyoinuka baharini, kana kwamba ni milima (Sura Al-Rahmaan, 55:20, 21, 23, 25).

Aya hizi zina maana ya kusema kwamba bahari mbili zinamopatikana lulu na marijani na ambazo zimetenganishwa, zitakutana na merikebu zenye nguvu nyingi kupita humo. Bishara hii ilitimia kwa ujenzi wa mfereji wa Suez na ule wa Panama. Bahari zilizounganishwa pamoja kwa mifereji hii ni maarufu mno kwa uvuvi wa lulu na marijani.

Sura Al-Kahf inazo bishara zihusuzo ustwi na maendeleo makubwa ya mataifa ya Kikristo, nguvu zao za kibaharia na uongozi wao wa eneo kubwa la ardhi, na vita vya wao kwa wao. Ushindi wa hatimaye

wa Islam na ufaulu wake pia ni mambo ambayo yametabiriwa. Sehemu iliyo kubwa ya ile bishara kuhusu kustawi na kuangamia kwa mataifa ya Kikristo tayari imeishatimia. Hatua inayofuatia ni kutimia kwa ile bishara inayohusikana na ushindi na ufaulu wa lslam. Mkristo Mzungu au mkosa-dini, kwa kutazama tu hali ya sasa ya Waislamu, haya yanaweza yakamchekesha; lakini Yule Mungu aliyefunua bishara hizi na aliyezitimiza zile miongoni mwazo zilizohusikana na mataifa ya Kikristo bila shaka atasababisha zile bishara zihusuzo ufaulu wa Islam nazo pia zitimie. Siku za ushindi wa Islam zimewadia. Miali ya jua la Islam inalipenya pazia zito la giza totoro. Malaika wa Mwenyezi Mungu wanashuka kutoka mbinguni. Ardhi bila shaka imepagawa na nguvu za kishetani lakini siku za ushindi komesha wa nguvu za kimbinguni dhidi ya nguvu za Shetani zinakaribia upesi upesi. Hapo Umoja wa Mungu utasimikwa kabisa kabisa humu ardhini na wanadamu watatambua na kukiri kwamba Kurani pekee yaweza kujenga amani, baina ya Mungu na mwanadamu na kuleta maadili na kutendeana haki baina ya mwanadamu na mwanadmu mwingine na kusimika Ufalme wa Mungu humu ardhini.

SIFA ZA PEKEE ZA MAFUNDISHO YA KURANI

Sifa moja maalumu inayoitofautisha Kurani na Vitabu vingine vyote vya dini ni kwamba inayaangazia kikamilifu matatizo yote yanayozuka kwenye uwanja wa dini, na kwa kusisitiza wajibu wa dini inaonesha eneo stahili la dini na manufaa yanayoweza kutokana nayo. Asomaye Agano la Kale na Agano Jipya au ma-Veda au Zend Avesta hubakia na dhana ya kwamba mtu fulani mwenye kudhihiri katikatini mwa msururu wa muda mrefu wa matukio ya kimaumbile alikuwa akielezea zile hatua za msururu huo ambazo yeye mwenyewe alikuwa amezishuhudia. Hivyo sivyo ilivyo hali ya Kurani. Yafafanua falsafa ya kuumbwa kwa viumbe na mambo yote yahusikanayo nayo. Yaeleza ni kwa nini Mwenyezi Mungu aliuumba ulimwengu na shabaha ya kuumbwa kwa mwanadamu na njia za kutumiwa kutekelezea shabaha hiyo. Yaainisha silika ya Uungu na sifa Zake na jinsi sifa hizo zidhihirikavyo. Kuhusu shabaha ya kuumbwa kwa

mwanadamu yafafanua zile kanuni ambazo kuendeshwa kwa utaratibu wa malimwengu kunatokana nazo. Kurani yasema kwamba kwa ajili ya ustawi wa kimwili wa mwanadamu na mabadiliko yake yenye kuendelea, Mwenyezi Mungu amejaalia kanuni za kimaumbile zinazosimamia hali za mwanadamu za kimwili na kiakili na kwamba kundi mojawapo la malaika limekabidhiwa jukumu la uendeshaji wa kanuni hizi. Kwa ajili ya kuistawisha na kuijazi roho maarifa, Mwenyezi Mungu amewafunulia Manabii Wake kanuni ya Sheria (yaani, Sheria Takatifu). Wakati mwingine wahyi ulio na Sheria Takatifu umekuwa ni wa kiasi tu, lakini pamekuwepo pia na wahyi ulio na kanuni kamili tena timilifu za Sheria Takatifu. Wakati mwingine madhumuni ya wahyi yamekuwa ni kuirejesha tena Sheria Takatifu kwenye usafi wake wa hapo awali baada ya kuwa imetiliwa dosari ya maelezo yasivyo ya kibinadamu. Kwa neno zima, Mwenyezi Mungu huinua Manabii miongoni mwa wanadamu kwa madhumuni mbalimbali. Baadhi ya Manabii ni waleta-sheria, na kwa njia ya Manabii hawa silsila mpya hufunuliwa. Kazi ya wengine ni kiasi tu cha urekebishaji wa Sheria iliyofunuliwa tayari ambapo pia wengine wanafaradhishwa jukumu la kufagilia mbali tafsiri ghafi za Sheria. Aidha, Kurani yaelezea haja ya kanuni ya Sheria na manufaa yawezayo kutokana nayo na matumizi yake kuhusikana na mabadiliko yenye maendeleo ya mwanadamu.

KUAMINI MUNGU ALIYE HAI

Kurani yaonesha tofauti baina ya Mwenyezi Mungu na sifa Zake, jambo ambalo kulifahamu kunatuwezesha kuwatia makosani wale ambao wamesema. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu (Yoh. 1:1). Kurani yafundisha kwamba sifa haiwezi ikawa ni badala ya yule mwenye sifa hiyo na kwamba hivyo vinatofautiana kabisa.

Kurani yaeleza ni kwa kiasi gani mwanadamu yuko huru kujiamulia mambo yake kufanya apendavyo na ni kwa kiasi gani yuwashurutishwa. Yafundisha kwamba mwanadamu amejaliwa hiari

ya kutosha kumfanya awajibike matendo yake mbele ya Mwenyezi Mungu na kumwezesha kuanza mpango wa daima dawamu wa kujistawisha. Kwa upande mwingine, eneo la matendo yake limo ndani ya mipaka na haiwezekani kwake yeye kuiruka. Licha ya juhudi zote, haiwezekani kwa mwanadamu kuondolea mbali vikomo yalivyoviwekewa maisha ya mwanadamu. Hawezi akagandamana mahali pamoja wala kujikweza kwenye hali ya maisha ya vile visivyoonekana. Hata hivyo, katika eneo la matendo yake yeye anavyo vipawa vikubwa na uwezo mkubwa na yuwaweza kujipatia ustawi wa siku zote na maendeleo.

Kurani yaelezea haja ya kuamini Mwenyezi Mungu na kuonesha mathibitisho ya kuwepo Kwake. Yasisitiza ya kuwa daima dawamu Mwenyezi Mungu alileta neno Lake kwa njia ya wahyi katika nyakati za giza na kwamba Yeye hudhihirisha uwezo Wake kwa njia ya Ishara zisizokuwa za kawaida na hivyo kutoa uthibitisho usiopingika wa kuwepo Kwake. Manabii pamwe na wafuasi wao halisi ni kitu cha lazima cha kutilia nafsini mwa watu imani halisi juu ya Mwenyezi Mungu. Ingetokea Mwenyezi Mungu kuacha kudhihirisha sifa Zake kwa njia ya Manabii na wafuasi wao, basi wanadamu wangekabiliwa na shuku na tashwishi, na Imani thabiti juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu kutoweka. Hivyo basi, ni jambo la lazima ya kwamba kadiri wanadamu wanavyoendelea kuwepo, wahyi wa Mungu hauna budi kuendelea kuwashukia baadhi yao. Imani juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu inaweza tu ikadumishwa kwa njia hii. Tangu mwanzo wa malimwengu, Mwenyezi Mungu ameongea na mwanadamu kwa njia ya Manabii Wake hadi Yesu na hadi Mtume Mtukufu[saw] wa Islam, sambamba na ambavyo ameendelea kudhihirisha sifa Zake za kuumba, kusikia na kuona. Vivyo hivyo Yeye ataendelea kuzungumza na vipenzi Vyake hadi mwisho wa wakati na ataendelea kudhihirisha kuwepo Kwake kwa njia hizi. Ni wazo lisiloingia akilini ya kwamba Mwenyezi Mungu alitumia sifa Yake ya kuongea hadi wakati wa Yesu lakini akajinyamazia baadaye au kwamba Yeye alitumia sifa Yake hii hadi kufikia zama za Mtume Mtukufu[saw] na baadaye kuwa

kimya milele. Kama vile tunavyolikatalia mbali na kulihesabu kuwa ni kufuru wazo lolote lile ya kuwa eti Mwenyezi Mungu alikuwa na sifa ya kuona hadi kufikia wakati wa Yesu au hadi zama za Mtume Mtukufu[saw] lakini eti baadaye alikoma kuona au kwamba Yeye aliweza kuumba hadi kufikia wakati wa Yesu au hadi kufikia zama za Mtume Mtukufu[saw] lakini eti baadaye Yeye aliipoteza sifa ya uumbaji au kwamba Yeye alikuwa Mwenye Uwezo wote hadi kufikia wakati wa Yesu au hadi kufikia zama za Mtume Mtukufu[saw] lakini baadaye akakoma kuwa na uwezo wowote, vivyo hivyo ni sharti tulikatalie mbali wazo ya kwamba Mwenyezi Mungu aliongea hadi kufikia wakati fulani wowote na baadaye akakoma kuongea. Sifa Zake zote ni timilifu na ni za milele. Huu ni ukweli ulio wazi, lakini kumbe Wakristo, Mayahudi, Wazoroasta na idadi iliyo kubwa zaidi ya wale wanaojiita eti Waislamu wametokea kuamini kwamba wahyi uliishilizia na Zorastar au na Manabii wa Israeli au na Yesu au ulishilizia na Mtume Mtukufu[saw]. Kurani yalikatalia mbali wazo sampuli hii. Kurani yafundisha kumwamini Mungu aliye hai na inawasilisha kuwa ni uthibitisho huu ukweli kwamba Yeye daima dawamu ataendelea kuongea na vipenzi Vyake na watumishi Wake watawa jinsi alivyodumu kuongea nao. Ukweli wa imani hii inayofundishwa na Kurani umethibitika katika zama hizi na kudhihiri kwa Masihi Aliyeahidiwa[as], Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Kwa mara nyingine tena wahyi alioupokea yeye na kupokelewa na wafuasi wake halisi wajitokeza kuwatolea mwito wale wote wanaodai, kama si kwa ndimi zao, ni kwa zile itikadi wanazozihubiri, ya kuwa eti Mwenyezi Mungu kapotewa na sifa ya kuongea.

Kurani yafundisha kwamba wahyi wa Mungu haukuishilizwa kwenye taifa lolote fulani, bali ya kwamba Mwenyezi Mungu ameinua Manabii baina ya watu wote. Yaelezea ni kwa nini ilikuwa ni lazima kuwaleta Manabii mmoja baada ya mwingine; kwa nini Sheria timilifu haikufunuliwa katika vipindi vya mwanzomwanzo vya historia ya mwanadamu. Yalizungumzia kwa marefu na mapana yake jambo la Umoja wa Mungu na kutoa hoja zenye kuridhisha za kuliungia mkono.

Yaonesha kwamba wingi wa miungu ungezivuruga akili na hata ukweli wa mambo yalivyo. Yaeleza ni kwa njia gani imani ya Umoja wa Mungu inavyomsaidia mtu katika maendeleo yake ya kiroho.

Kurani yaifafanua vilivyo habari ya unabii. Neno hili "nabii" au yaliyo sawa nalo yanatumiwa sana katika Maandiko ya kidini, lakini hapana maandiko yoyote yanayoeleza unabii wadokezea kitu gani. Ni nani awezaye kuitwa Nabii na ni nani asiyeweza kuitwa hivyo na ni zipi aina mbalimbali za unabii? Kurani peke yake yaelezea Nabii ni nani na kuelezea tofauti kati ya aina mbalimbali za unabii. Yaelezea tofauti baina ya Nabii na yule asiyekuwa nabii na kuelezea wajibu wa Nabii na uhusiano wa Nabii na Mwenyezi Mungu. Aidha, yaeleza ni kwa nini Manabii huinuliwa na uweje uhusiano baina yao na wafuasi wao na baina yao na wale watu wasiowaamini. Yaainisha haki za Nabii na kueleza kama Nabii ni kizingiti baina ya Mwenyezi Mungu na mwanadamu au ni msaidizi na kiongozi.

Kurani yaelezea kwa kirefu suala la malaika, kazi zao na shabaha ya kuumbwa kwao.

Pia yaeleza Shetani ni nini na ni kwa njia gani kuwepo kwa kiumbe kama huyo kunamsaidia mwanadamu. Upo uhusiano gani baina ya mwanadamu na Shetani? Mtu yuwaweza kujilinda namna gani dhidi ya vishawishi vya kishetani? Je, Shetani ana uwezo wa kumlazimisha mtu kufanya hivi au vile? Yasema kwamba daima malaika humtakia mwanadamu heri na Shetani daima humtakia mwanadamu shari na kwamba mwanadamu anayo hiari ya kukubali au kutokubali heri ya malaika na pia anayo hiari ya kukubali au kutokubali shari ya Shetani. Viumbe wa aina hizi mbili wameumbwa kumsaidia mwanadamu afikie utimilifu wake na kuyatilia maisha yake hali ya uhalisi. Bila ya hii mivuto ya heri ya malaika na ile ya shari ya Shetani mwanadamu asingelistahilia thawabu wala adhabu. Juhudi za mtu dhidi ya mawazo ya kishetani humstahilishia thawabu na kumfungulia njia ya maendeleo; kukatalia kwake mbali mawazo na mivuto ya malaika humfaradhishia adhabu.

Kurani yaelezea falsafa ya maombi na yaonesha vile impasavyo mtu kuomba, ni katika hali gani maombi yanaweza yakakubaliwa na ni maombi sampuli gani yasiyoweza kukubaliwa na ni eneo gani maombi yanamofanya kazi.

Yazungumzia wema na ubaya na kuyafafanua yote mawili na kuelezea inapokutania mipaka yao. Yaufafanua wema halisi na ubaya halisi na wema nusunusu na ubaya nusunusu. Yaonesha njia ya kujichumia tabia njema na wema na vile ubaya unavyoweza kuepukwa. Yayafafanua machimbuko ya wema na ubaya na kumfunza mwanadamu alifulilie mbali chimbuko la ubaya.

Yalizungumzia suala la toba na kueleza ni nini toba halisi. Inataja manufaa ya kutokana na toba, na kufafanua hali halisi ya toba na pale anapotakikana mtu kuigeukia toba. Aidha yazielezea zile kanuni ambazo ndizo misingi ya thawabu na adhabu na yale mambo yanayotiliwa maanani katika kuamulia thawabu au adhabu. Yaelezea uhusiano baina ya uhalifu na adhabu na jinsi mizani ya vitu hivi viwili inavyowza kusawazishwa.

WOKOVU SAWA NA KURANI

Kurani yauelezea wokovu ni kitu gani na jinsi unavyopatikana. Yafundisha kwamba wokovu ni wa aina tatu: (1) Wokovu halisi; (2) Wokovu usiokuwa halisi; na (3) Wokovu ulioahirishwa. Wokovu halisi huchumwa katika maisha haya haya. Mwenye kujichumia wokovu usiokuwa halisi katika maisha haya basi yeye pole pole huitimilizia njia ya kujipatia wokovu baada ya mauti. Wokovu ulioahirishwa huchumwa tu baada ya kuonja kwa muda adhabu ya Jahanamu. Mafundisho ya Kikristo na Islam kuhusu hii aina ya mwisho ya wokovu yana kitu kinachofanana lakini yanatofautiana katika jiha za kimsingi. Ukristo wafundisha kwamba hata aina hii ya wokovu inaweza ikachumwa tu na wale wanaoziamini kwa dhati itikadi za Ukristo lakini ambao hawakufaulu kujichumia wokovu halisi katika maisha haya. Hawa ndio watu ambao, baada ya kupitisha kipindi kwenye adhabu ya Jahanamu, wangejichumia wokovu halisi.

Islam, kwa upande mwingine, yafundisha kwamba kila mwanadamu ameumbwa kwa madhumuni ya kwamba yeye hatimaye atajichumia wokovu halisi. Kafiri sugu kupindukia na mhalifu baada ya yeye kufanyiwa huduma fulani za marekebisho, mojawapo ikiwa ni adhabu ya Jahanamu, hatimaye angetokea kujichumia wokovu halisi na kuingia Peponi. Kuhusu ukweli huu Kurani yasisitizia fundisho la matendo kupimwa kwa mizani. Yafundisha kwamba wingi wa matendo mema maishani mwa mtu kwa upande wake ni dalili ya juhudi za kikwelikweli za kujichumia wokovu halisi na kwamba anayekufa na huku yuwafanya bidii ya kikwelikweli kujipatia shabaha yake yuwafanana na askari anayeuawa kabla ya kupatikana ushindi. Mauti yanasimamiwa na Mwenyezi Mungu kabisa. Askari katika uwanja wa vita hana uwezo wa kuahirisha mauti mpaka baada ya kupatikana ushindi. Vivyo hivyo mtu ambaye yuwajitahidi kikwelikweli kujichumia wokovu hana uwezo wa kuahirisha mauti mpaka jitihada zake zitakapoishilizia na ushindi. Mtu sampuli hiyo kama akifilia katikati ya juhudi hii, anakuwa yu mwenye kustahili Huruma na Ukarimu wa Mwenyezi Mungu wala sio ghadhabu yake na adhabu. Halijapata taifa lolote kuwalaumu mashujaa wake kwa kuuawa kwao kabla ya kupatikana ushindi. Kila askari mwenye kuutilia ushindi shime ya kikwelikweli huheshimiwa. Na hivyo ndivyo ilivyo kwa mtu ajibidiishaye kumshinda Shetani, na licha ya milima na mabonde, kuzidi kushikilia uzi ule ule kwa uthabiti na ujasiri hadi mwisho ndiposa Ufalme wa Mungu upate kusimikwa. Sawa na Kurani mtu kama huyo kwa kweli yuwastahili wokovu. Udhaifu wake sio dosari bali ni pambo, kwani haukumzulia ajiunge na kundi la wale wanaopigana upande wa Mwenyezi Mungu wala hakusita kujitoa dhabihu humo mapiganoni.

Kurani yazielezea hatua za mabadiliko ya kiroho na kuieleza idadi yake na tafsili. Kwa mfano, yazielezea aina na vima vya usafi, wema, usemaji kweli, uraufu, uhurumiaji, n.k. Ndiposa, inamwezesha mtu kupanga sawa na kukua kwake kwa kimaono na kiroho. Kwa kule kuifanya shabaha tangulizi ifikilike na mwanadamu yampatia

changamoto ashike njia ya maendeleo, na kwa kumwekea mbele yake msururu wa shabaha zinazodumu kuwa za juu zaidi yamhimizia juhudi kubwa zaidi katika kila hatua. Kwa njia hiyo humpeleka mtu mbele katika njia ya maendeleo hatua kwa hatua na manzili baada ya manzili.

Aidha, Kurani yatoa ufafanuzi wa mabadiliko ya kuendelea mbali ya mwanadamu ya kiakili na huelelezea vile yanavyotekelezwa na kufundisha kwamba hekima ya kimbinguni katika upimaji wa matendo ya mwanadamu hutilia maanani hali ya maendeleo yake ya kiakili. Yule aliyekuwa na bahati ya kulelewa katika mazingara yanayofaa na aliyerahisishiwa njia kutenda heri huenda matendo yake yatatokea kupimwa na mizani tofauti kabisa na ya yule mtu ambaye maendeleo yake ya kiakili yalikuwa ni duni na ambaye hali ya mazingara alimokulia haikuwa nzuri vile. Ingebidi huyu mtu wa pili kupunguziwa uzito wa makosa yake kutokana na vile vizingiti ilivyombidi kupambana navyo.

Kurani yafafanua Imani ni kitu gani, yapatikanaje, na iwezavyo kutambulika. Yaelezea haja kanuni ya Sheria (ya Mungu) na falsafa yake. Yafundisha kwamba Sheria ya Mwenyezi Mungu yatokana na hekima na imekusudiwa kamsukuma mtu mbele katika njia ya maendeleo. Amri za Mwenyezi Mungu hazikukadiriwa kuwa mzigo au adhabu kwa watumishi Wake, bali kila moja yao imefanywa kuwa ni msaada na tegemeo kwa mwanadamu kuendelea mbele na imlainishie mazingara yake ya kijamii. Kurani haiungi mkono itikadi ya kushurutizia amri na adhabu. Yafundisha kwamba Mwenyezi Mungu hamhukumu mtu yeyote bila kutilia maanani kikamilifu kila hali ambayo inaweza ikaruhusu au kuitia tabia yake makosani. Pia yafundisha kwamba na asitokee mtu yeyote kuadhibiwa isipokuwa awe alipata kuonywa kimbele.

MIUJIZA

Waandishi wa Kikristo wamedai kwamba, mbali na madai kwamba ni ya kipekee katika mtindo wa maneno yake na falsafa yake, Kurani haitoi madai yoyote ya miujiza. Hapana budi kuelezea kwa kifupi

msimamo wa Kurani kuhusu miujiza.

Kurani yatoa mafundisho mawili ya kimsingi. Kwanza, ya kuwa kunazo baadhi ya kanuni za kiungu zisizobadilika. Kama kwa mfano, Kurani yafundisha kwamba maiti katu hafufuki humu ardhini, na kwamba hapana yeyote minghairi ya Mwenyezi Mungu aliye na uwezo wa kuumba. Dunia inaweza ikatoa mafundi, wahandisi na wavumbuzi, lakini sifa ya uumbaji hujidhihirisha tu kwa njia ya kazi ya Mwenyezi Mungu. Kuhusu hilo la kwanza la haya mambo mawili ndani ya Kurani Mwenyezi Mungu yuwasema hivi:

> Hata yatakapomfikia mmoja wao mauti, husihi akisema: Mola wangu, nirudishe, ili nikafanye mema katika yale niliyoyaacha. Hapana! Hakika hili ni neno tu analolisema; na nyuma yao pana kinga mpaka siku watakapofufuliwa. (Sura Al-Mu'minuun, 23:100-101).

Na tena:

> Na ni kanuni isiyotanguka kwa mji tuliouangamiza, ya kwamba wao hawatarejea. Itakuwa hivyo hata (zama) Atakapofunguliwa Yajuja na Majuja, nao watakuja mbio mbio kutoka kila mahali pa juu (Sura Al-Ambiyaa, 21:96-97).

Aya hizi zamaanisha kwamba Mwenyezi Mungu amekadiria ya kwamba wale watu ambao wameaga dunia hawatarejea tena humu ardhini hata pale watakapofunguliwa Yajuja na Majuja na kutapakaa ardhini kutoka juu ya kila kilima na juu ya kila wimbi. Hii yaonesha waziwazi kwamba wafu hawawezi wakarejea humu ardhini. Kutajwa kwa Yajuja na Majuja katika hiyo aya ya mwisho hakumaanishi kwamba wafu wataruhusiwa kurudi ardhini wakati ule. Kwa kuwa huko kufunguliwa kwa Yajuja na Majuja ni mojawapo ya ishara za kukaribia kwa mwisho wa dunia, aya hii yamaanisha kwamba kanuni hii itaendelea kufanya kazi hadi mwisho wa dunia. Baadhi ya watalaamu wa lugha wameifasiri hii sehemu ya aya hii kumaanisha kwamba baada ya kuzuka kwa Yajuja na Majuja zitafanyika jitihada za kuwafufua watu lakini kwamba jitihada zenyewe zisingefua dafu,

ikimaanishwa kwamba taaluma ya sayansi ingetokea kufanya jitihada za bure za kulitatua hili tatizo la mauti. Kwa neno zima, Kurani yafundisha kwamba mfu hawezi akaruhusiwa kurejea tena ardhini.

Aidha, yafundisha kwamba hapana mwenye uwezo wa kuumba ila Mwenyezi Mungu. Yasema hivi:

> Na wale wanaowaomba msaada badala ya Mwenyezi Mungu hawaumbi chochote bali wao wameumbwa. Ni wafu, si wazima, na hawajui watafufuliwa lini (Sura An-Nahl, 16:21-22).

Kurani pia yafundisha kwamba kwa kuwa hekima ni mojawapo ya sifa za Mwenyezi Mungu, hakiwezi kunasibishwa naye chochote kinachokwenda kinyume na hekima. Mwenyezi Mungu yuwaitwa Mwenye Hekima mahali kadha wa kadha katika Kurani. Mahali pamoja Kurani yasema hivi:

> Mmekuwaje ya kwamba hamtarajii hekima na uthabiti kutoka kwa Allah (Sura Nuuh, 71:14).

Katika aya hii Mwenyezi Mungu yuwawakaripia makafiri akisema kwamba wakati wao wanadai kwamba matendo yao yote yanatokana na hekima, hawafikiri vivyo hivyo kumhusu Mwenyezi Mungu na humnasibishia vitu vinavyokwenda kinyuma na hekima.

Basi kwa sababu hiyo kama kitu chochote chenye kuvunja hizi kanuni tatu, ambazo zimetajwa kama mifano, chadaiwa kimepata kutokea wakati wowote, Kurani yakikatalia mbali haidhuru matukio kama hayo yawe yaelezewa kuwa ni miujiza au maajabu au usihiri. Kurani haikubalii uwezekano wa matukio yoyote sampuli hiyo wala miujiza kama hii haiinasibishii Nabii yeyote, wala kudai miujiza yoyote kama hiyo kumhusu Mtume Mtukufu[saw] mwenyewe. Haiwi mtu yeyote mwenye akili zake timamu kufikiriwa ya kwamba atokee kutunga sheria au kuweka kanuni na kisha yeye mwenyewe kuanza kuihalifu. Basi yawezekanaje kufikiri kwamba Mwenyezi Mungu, Aliye Hekima halisi, angeweza kufanya hivyo? Yule mwenye kunasibisha vitu sampuli hii kwa Manabii wa Mungu haongezii kwa

vyovyote vile heshima na taadhima yao bali yeye kwa hakika yu mwenye kosa la kutuhumu busara na unyofu wao. Hivyo basi, ni wajibu wa kila mwenye akili zake kusuta madai ya aina hii kwani hayo sio sifa bali ni masingizio kwa wale watu ambao yanafanywa juu yao.

Kurani kwa upande mwingine, sio tu haikatai bali yadai kikweli-kweli kwamba Mwenyezi Mungu huwafanya Manabii Wake njia ya madhihirishio ya aina fulani ambayo hayapingi kwa vyovyote vile kanuni Zake za kimsingi. Huu ni ukweli usioweza kupingika na hii ndiyo aina ya muujiza Kurani inayomdaia Mtume Mtukufu[saw]. Je, huu sio muujiza ya kwamba Mwenyezi Mungu amjazi mwanadamu ukweli halisi wa mambo yaliyofichama sirini mwa siku zinazokuja? Je, sio muujiza kwa Mwenyezi Mungu kujaalia ufaulu na ushindi kwa mtu dhaifu na mnyonge asiyeonekana na viwezesho vyovyote dhidi ya wapinzani wengi wenye uwezo na nguvu? Kurani haidai tu kwamba ni ya kipekee bali pia kwamba Mwenyezi Mungu alimjaalia Mtume Mtukufu[saw] elimu ya mambo yaliyofichika na kwamba alifululiza kudhihirisha uwezo na utukufu Wake kumwungia mkono Mtume Mtukufu[saw]. Basi yawezaje kasemwa kwamba Kurani haimnasibishii Mtume Mtukufu[saw] miujiza yoyote? Ukweli wenyewe ni kwamba yakariri madai hayo mara kwa mara. Je, huu haukuwa ni muujiza ya kwamba Mtume Mtukufu[saw] alionywa kimbele ya kuwa yeye atakuja kuwa shabaha ya upinzani mkali na mateso kutokana na watu wa Makka alipokuwa yeye mwenyewe hakuwa na sababu ya kushuku kwamba angelikuja kuwa shabaha ya upinzani na mateso kama hayo? Je, huu haukuwa ni muujiza ya kwamba yeye alijulishwa ya kuwa itakujambidi kuhama kutoka Makka na kwamba hata wakati wa kuhajiri huko ulidokezewa kimbele? Je, haukuwa ni muujiza ya kwamba miaka kadha kabla ya vita vya Badr yeye alijulishwa ya kuwa mapigano yatakuja kutokea ambamo Waislamu wangekuwa washindi na maadui wao kushindwa na kwamba hata wakati wa mapigano hayo uliainishwa? Je, huu haukuwa ni muujiza ya kwamba Mtume Mtukufu[saw] miaka mingi kabla ya tukio lenyewe alijulishwa ya kwamba sio tu ya kuwa yeye ingelimbidi kuhajiri kutoka Makka bali

pia ya kuwa angeliingia tena Makka kama mshindi? Je, huu haukuwa ni muujiza ya kwamba baada ya Warumi kushindwa na Waajemi nchini Siria, Mtume Mtukufu[saw] akajulishwa kwamba kwenye muda wa miaka tisa Warumi wangeliwashinda Waajemi? Je, huu haukuwa ni muujiza ya kwamba Mtume Mtukufu[saw] aliambiwa kwamba Islam ingelikuja kuenea Arabuni nzima na hapo kuzishinda dini zingine zote? Wakati ambapo kila moja la matukio haya lilikuja kutukia sawa na wakati wake, basi ni tashwishi gani ingeliyoweza kubakia ya kuwa kila moja la matukio haya lilikuwa ni muujiza? Mambo haya yote na mengi mengine ya aina hii yanazugumziwa katika Kurani. Sasa inawezekanaje kusemwa kwamba Kurani haiimdaii Mtume Mtukufu miujiza yoyote? Wale wanaohusikana na madai haya wamedaganyika kuyafanya kwa sababu ya kutokuwa kwao na ujuzi wa lugha ya Kiarabu na nahau na mtindo wa Kurani. Pale, kwa mfano, Kurani inaposema: Na hakuna kingelichotuzuia kupeleka ishara ila ya kwamba watu wa zamani walizikadhibisha (Sura Banii Israaiil, 17:60), haimanishi kama vile waandishi wa Kikristo wanavyoonekana waliifahamu, ya kwamba eti Mwenyezi Mungu yuwakataa kuonesha Ishara zaidi. Aya yamaanisha kwamba watu ambao kwa manufaa yao ziloneshwa Ishara katika vizazi vilivyopita hawakuzikubali na huenda hii ndiyo ilikuwa sababu ya kutooneshwa Ishara zaidi, lakini Mwenyezi Mungu hangeliacha kuonesha Ishara Zake kwa sababu hiyo. Watu walizikataa Ishara zilizooneshwa na Manabii wa mwanzo lakini hata hivyo Ishara zikaoneshwa kuwaungia mkono Manabii wa baadaye; ndiposa haikuwepo sababu ni kwa nini Ishara zisiwe zilioneshwa kumuungia mkono Mtume Mtukufu[saw] wa Islam.

Tena, katika kuwajibu makafiri pale alipotukia Mtume Mtukufu[saw] kuelekezwa katika Kurani aseme kwamba yeye ni mwanadamu tu kama wanadamu wengine, haikumaanisha kwamha Mwenyezi Mungu hakuonesha Ishara za kumwungia mkono. Kilichomaanishwa kilikuwa kwamba Ishara zilioneshwa na Mwenyezi Mungu na kwamba Mtume Mtukufu[saw] asingeliweza kuzionesha apendavyo. Huu ni ukweli asilia na kule kugusiwa kwake katika Kurani

kwatuzidishia kuutambua. Ni yupi wa hawa wawili aifuataye kweli na ni yupi aliye makosani: Yule mwenye kusisitiza kwamba Mwenyezi Mungu sifa Zake na mamlaka Yake kavikabidhi baadhi ya viumbe Wake au ni yule mwenye kutangaza kwamba yeye si chochote ila ni kiumbe wa Mwenyezi Mungu na kwamba Mwenyezi Mungu huzidhihirisha Ishara Zake kwa njia ya watumishi Wake wapenzi?

Pamoja na bishara Kurani yataja pia miujiza mingine. Mathalan, yautaja huu muujiza ufuatao: Katika tukio la Hijra Mtume Mtukufu[saw], akiandamana na Hadhrat Abu Bakr[ra], aliitoka Makka na akakimbilia kwenye Pango la Thaur, yapata maili tatu nje ya mji wa Makka. Walipogundua watu wa Makka kwamba Mtume Mtukufu[saw] kawaponyoka, walimwajiri msakaji wao stadi na wakamfuatilia hadi penye mlango wa lile pango. Kurani yadokezea ukweli kwamba, mara alipohisi kwamba wasakaji walikuwa wamefika penye mlango wa pango lile, Hadhrat Abu Bakr[ra] alipatwa na hofu isije baada ya kumgundua wakamdhuru Mtume Mtukufu[saw] kwa vyovyote vile. Lakini mwenyewe Mtume Mtukufu[saw] ikamtoka kauli ya kumtulizia sahibuye akamwambia, "Usihuzunike kwani Allah yu pamoja nasi (Sura At-Tauba, 9:40), akimaanisha kwamba maadui zao hawatafaulu kuwatia mbaroni. Sasa je, yale yaliyotukia katika kisa hiki haukuwa muujiza usio na kifani? Waja wawili wasiokuwa na msaada wa kidunia watokee kukimbia wimbi la hasira za maadui zao na kujibanza pangoni. Igunduliwapo kwamba wameutoka mji katika giza la usiku, maadui zao wanapandwa na ghadhabu na fadhaa. Wanaona kwamba huku kuponyoka kwa wakimbizi hawa wawili sio tu kwamba kungewapokonya windo lao bali kungewapatia aibu na fedheha za kudumu. Hapo wanatangaza zawadi ya ngamia mia moja kwa mtu yeyote yule atakayemkamata na kumleta kwao yule mkimbizi mkubwa, iwe yu mzima au maiti. Kisha wanamwajiri msakaji wao hodari kabisa anayewaongoza hadi kwenye mlango wa lile pango walimojibanza wale waja wawili, na kutamka kwa uthabiti akisema kwamba nyayo za wakimbizi zaishia hapa. Genge la wasakaji linapandwa na hamaki za kisasi na wanadhamiria kutowapatia

wakimbizi wale nafasi yoyote ya kutorokea. Baada ya usakaji wa masafa zaidi ya maili tatu wanafika karibu sana na windo lao na yabakia tu wao kuchungulia ndani ya lile pango lililo wazi pao miguuni kugundua mahali walipo wale wanaowasaka, lakini Mwenyezi Mungu anatawala fikara zao na macho yao kiasi hiki kwamba haoni yeyote haja ya kuchungulia pangoni na wanarejea makwao wakiwa wamekatwa chenga na kuudhika. Je, mmepata dunia kushuhudia muujiza mkubwa sampuli hii?

Na kisha, kuhusu vita vya Badr Kurani yasema kwamba Mtume Mtukufu[saw] alitupa fumba la changarawe upande wa maadui na kwamba hili lilizusha vurugu miongoni mwao (Sura Al-Anfaal, 8:18). Katika Hadithi tukio hili laelezewa kwa kirefu sana. Yaonekana kwamba vilipokuwa vita vikiwaka moto kamili na maadui kuwalemea vikali Waislamu, Mtume Mtukufu[saw] alitwaa fumba la changarawe na kuzitupa upande wa maadui huku akisema: "Nyuso zao na zikunjanekunjane" (Tabari na Zurqani). Papo hapo, Mwenyezi Mungu akavumisha upepo mkali kutoka upande wa Waislamu kuelekea watu wa Makka uliopeperusha mchanga na kuutupa nyusoni na machoni mwa maadui. Matokeo yakawa kwamba wale watu wa Makka hawakuweza tena kuona vizuri na ikawawia vigumu kulenga shabaha za mishale yao. Bali mishale yao ikakomeshwa njia na upepo mkali uliovuma kuwaelekea. Kwa upande mwingine, Wailsmu waliwaona watu wa Makka waziwazi na ule upepo ukazidi kuisukumiza mishale yao dhidi ya maadui zao. Hali hii ikakipatia ushindi mkubwa kile kikundi cha Waislamu dhaifu wasiokuwa na silaha nzuri juu ya jeshi kubwa la watu wa Makka lililokuwa na silaha bora na wanyama wa vita pia. Je, huu haukuwa ni muujiza na je, Kurani haimaanishi kuuelezea kuwa ni muujiza?

Naam, Kurani yamnasibishia Mtume Mtukufu[saw] miujiza kwa uwazi kabisa na yaitaja baadhi ya miujiza hiyo. Ila tu, yajizuia kumnasibishia upuzi kama ule wa kufufua maiti au kusimamisha jua na mwezi au kukwamisha mito au kuhamisha milima. Masimulizi ya matukio sampuli hii ni ngano tupu ambazo hutumika tu kuviongoa vijitoto

katika mabembea yao. Kurani haimnasibishia Mtume Mtukufu[saw] wala Nabii mwinginewe visa sampuli hii. Kwa upande mwingine Kurani yatoa ufafanuzi wa maneno yanayopatikana katika baadhi ya Vitabu vya zamani ambayo maana zake za kidhahiri zimewafanya watu waamini kwamba matukio kama yale yaliyokaririwa hapo juu kweli kabisa yalitukia. Kurani yabainisha ikisema kwamba lugha kama hiyo ilitumiwa tu kimithali wala haiafiki maana za kidhahiri.

IBADA YA MWENYEZI MUNGU

Kurani yalielezea kwa kirefu suala la ibada ya Mwenyezi Mungu. Inaigawanya ibada nzima kuifanya ya aina nne:

(1) Ibada ambayo shabaha yake ni kuimarisha uhusiano wa mwanadamu na Mwenyezi Mungu na kujiongezea mapenzi juu Yake.

(2) Ibada inayopangiwa kuboresha hali ya mtu ya kimwili na kumhamasisha ajitolee kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

(3) Ibada inayopangiwa shabaha ya kuleta utangamano na umoja miongoni mwa wanadamu na kuwezesha kupapenda mahali pa kuendewa na watu wote.

(4) Ibada ambayo shabaha yake ni kusababisha hali mwafaka ya kiuchumi katika jamii.

Kurani yafaradhisha ibada za namna mbalimbali katika kila moja ya hizi aina nne. Yafundisha kwamba ibada haimaanishi kwamba mwanadamu azingatie tu kumsabihi Mwenyezi Mungu na kumsujudia bali pia ni pamoja na kuwashughulikia wanadamu wenzake. Aidha, yasisitiza kwamba sio eti ya mtu mmoja mmoja tu bali pia ni ya kujumuika pamoja. Wajibu wa mwanadamu kuhusu ibada hauishilizii kwa yeye kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu; bali ni sharti pia awaandae nduguze kwenda kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu. Ndiposa amri zote za Kurani kuhusikana na ibada zina vielekezo vya (watu) kujumuika pamoja na vya mtu mmoja mmoja pia.

Katika hiyo aina ya kwanza Kurani imefaradhisha zile sala tano za kila siku. Sala ya Kiislamu yatofautiana kabisa na sala zinazoamrishwa

katika dini zingine. Sala hii ina sehemu ya mtu mmoja mmoja na sehemu ya kujumuika pia na imeepukana kabisa na mikogo yote na hali za kitamasha-tamasha. Kurani haioni ulazima wa majumba yaliyowekwa wakfu kama vile makanisa na mahekalu na hali zote za kirasimirasimi katika ibada ya Mwenyezi Mungu. Yafundisha kwamba kila sehemu ya uso wa ardhi ni halali kutumiwa kwa ajili ya ibada ya Mwenyezi Mungu. Mtume Mtukufu[saw] alikuwa akigusia jambo hili hili pale alipotamka akisema: "Dunia nzima imefanywa kuwa ni msikiti kwa ajili yangu" (Bukhari). Kauli hii yake ina maana nyingi, moja ikiwa hii ya kwamba Mwislamu anaweza akasali sala zake kokote aliko wakati wa sala unapowadia. Sio faradhi kwake yeye eti kukimbilia kanisani au hekaluni wala yeye katika kutekeleza ibada yake hategemei uongozi wa kasisi au mwanachama wa ushirika mtakatifu. Islam haiungi mkono desturi ya ukasisi. Yamchukulia kila mtu mwema kuwa yu mwakilishi wa Mwenyezi Mungu na yatambua uhalai wa mtu yeyote kama huyo kuongoza sala.

MSIKITI WA ISLAM

Waislamu huutumia msikiti kwa madhumuni ya sala za jamaa lakini hii haitokani na fikara yoyote ya kuwa eti viwanja na majengo ya misikiti hii yanao utakatifu wowote wa kipekee kwa minajili ya ibada ya Mwenyezi Mungu. Msikiti hujengwa kuwawezesha Waislamu wa janibu zile kukusanyika pamoja kwa ajili ya sala ya jamaa. Misikiti huwezesha ibada ya pamoja na pia hutumiwa kwa shughuli zinginezo za kidini na kijamii. Hapahitajiki utaratibu rasmi wowote maalumu wa kuiweka wakfu misikiti na kuifaradhishia ibada ya Mwenyezi Mungu, jinsi yanavyofanyiwa mahekalu na makanisa. Nyumba yoyote ile itumiwayo na Waislamu kwa ajili ya sala za jamaa ni msikiti. Msikiti haukufaradhishiwa umbo au sura yoyote maalumu wala haukugawanywa sehemu za mashekhe na za wasalihina wa kawaida, wala hauna chochote kifananacho na madhabahu. Msikitini hamna picha au sanamu wala hamna mabaki ya watakatifu. Waislamu huikusanyikia ibada ya Mwenyezi Mungu kwa njia isiyokuwa na makuu kabisa na sala za dini ya Kiislamu zimeepukana na vibetua

mawazo vyote viwe ni vya kisanaa au kimaono. Humo hamna ngoma wala kuimba nyimbo, hamna dansi za mahekaluni, hamna majoho ya kikasisi, hamna uradi wa kuwasha mishumaa wala hamna jaribio la kuchochea msisimko wa kimaono kwa kutumia vinanda na ubani. Mwangaza wa ndani ya msikiti haufifishwi kitaalamu ili kuleta humu hali ya kuogofyaogofya na hamna sanamu za watakatifu zibetuazo maono ya wenye kusali mbali na Mwenyezi Mungu. Ufikapo wakati wa sala, wenye kusali hukusanyika msikitini na kujipanga safu safu kuonesha kwamba, baada ya wao kuwa wametekeleza ibada ya kila mtu mwao majumbani au msikitini, sasa walikuwa tayari kumfanyia Mwenyezi Mungu ibada ya pamoja. Humtukuza Mwenyezi Mungu na kumshukuru na kujiombea dua kwa ajili ya maendeleo yao wao wenyewe ya kiroho, ya kimaadili na ya kimwili na pia yale ya marafiki zao jamaa zao na ya wanadamu wote kwa jumla. Haya wao huyafanya katika hali ya utulivu kabisa pasi na kuvurugwa na chochote hata na midundo ya muziki. Wanapokiabudu hivyo hapana mmoja wao aruhusiwaye kutazama huku na huku au kuongea na mwenzake. Matajiri na maskini, wote husimama bega kwa bega; mfalme anaweza akatokea kusimama bega kwa bega na mpiga viatu vyake rangi; anaweza hakimu akatokea kukuta kumbe jirani yake ni yule yule mtu aliye mashtakani mbele yake na jemadari akatokea kusimama bega kwa bega na askari chipukizi. Hawezi msalihina yeyote akamkataza msalihina mwenzake asisimame karibu naye wala haitokei msalihina kugurishwa toka mahali pake hadi mahali penginepo. Bali wote husimama kinyenyekevu na kitiifu mbele ya Mwenyezi Mungu wakirukuu na kusujudu na kusimama tena wakimfuata Imamu. Katika baadhi ya sala Imamu husoma kwa sauti aya kadha za Kurani ili kuwasilisha maana za aya zenyewe mawazoni mwa maamuma. Katika sehemu fulani fulani za sala kila maamuma husoma dua zilizowekwa au dua alizojibunia yeye mwenyewe binafsi.

Pamoja na sala za faradhi, Waislamu husali na kuzama katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu kimoyomyo na kuzitafakaria sifa Zake popote pale usiku na mchana wanapopata fursa ya kufanya

hivyo. Misikiti haitumiwi tu kwa minajili ya ibada za jamaa na za mtu mmoja mmoja bali kwa minajili ya kila aina ya shughuli za kidini na zile za kiutu. Hutumika kama shule na kwa shughuli za kutangaza ndoa, kama mahakama na makutanio ambamo huandaliwa plani kwa ajili ya maendeleo ya umma ya kijamii na ya kiuchumi.

MFUNGO WA KIISLAMU

Aina ya pili ya ibada ambayo shabaha yake kubwa iliyonayo ni kuboresha hali ya kimwili ya mwenye kuabudu ni Mfungo. Mfungo wa Kiislamu watofautiana na mifungo iliyowekwa katika dini zingine. Akiwa yuwafunga Baniani yuwaruhusiwa kula aina fulani fulani za vyakula; kwaresima ya Kikristo hali kadhalika hutekelezwa kwa kutokula aina mahususi ya vyakula, mathalan, nyama au mkate ulioumuliwa. Lakini Mwislamu akiwa mfungoni hali wala hanywi toka alfajiri hadi baada ya kuchwa jua. Sehemu ya faradhi inayofungamana na Mfungo wa Kiislamu ni kwamba pamoja na kuacha kula na kunywa wakati wa kufunga Mwislamu ni sharti ajitahidi mwezi mzima wa kufunga kujichumia madaraja makubwa makubwa ya utawa na unyofu. Somo moja lifundishwalo na huu Mfungo ni kwamba mtu aachaye matumizi ya vitu halali wakati wa Mfungo asitokee kwa sababu yoyote ile na wakati wowote ule kutumia kile kilichoharamishwa. Wakati wa kufunga, yaani, tangu alfajiri hadi ibada ya kuchwa jua, umefaradhishwa nchi zote kuliko na mfuatano wa mchana na usiku ndani ya muda wa masaa ishirini na manne. Katika yale maeneo ya utosini zaidi ya ardhi usikopatikana vizuri huu utaratibu wa usiku na mchana katika muda wa masaa ishirini na manne muda wa kufunga na upimwe kwa kuzingatia urefu wa siku ya kawaida. Aina hii ya ibada nayo ni ya mtu mmoja mmoja na ya watu wengi kwa pamoja. Waislamu wanatarajiwa kufunga mmoja mmoja katika siku mbalimbali za mwaka lakini katika mwezi Ramadhani Waislamu wote, popote wawapo, ni sharti wafunge.

HAJI

Aina ya tatu ya ibada iliyofaradhishwa na Islam ni kwenda kuhiji Makka. Madhumuni ya ibada hii ni kuwafanya Waislamu wajihisi kwamba wanalo fungamano na Mahali pa Kitovuni. Ili kutekeleza Haji, Waislamu wanaoiweza safari hii hukusanyika pamoja mjini Makka katika majira yaliyowekwa. Hivyo wanapatiwa fursa ya kukusanyika pamoja kutoka sehemu mbalimbali za dunia, kuimarisha uhusiano wao na kubadilishana maoni juu ya matatizo ya kitaifa na yale ya kimataifa. Aina hii ya ibada nayo pia ni ya kujumuika na ya mtu mmoja mmoja. Haji inaweza ikatekelezwa tu katika kipindi cha siku zilizowekwa, lakini 'Umra (Haji ndogo) inaweza ikatekelezwa wakati wowote ule. Majira yoyote ya mwaka Mwislamu anapoweza kuiandaa hii safari anaweza akaenda zake Makka kutekeleza 'Umra. Aina hii ya ibada yawafundisha Waislamu kwamba kwa minajli ya kupadumisha na kupaimarisha Mahali pa Kitovuni hawana budi kuwa tayari kujitoa dhabihu wote kwa pamoja na kwa mtu mmoja mmoja pia.

Aina ya nne ya Ibada ni sadaka na hisani. Hii nayo pia ni ya kujumuika na ya mtu mmoja mmoja na ya faradhi na ya hiari. Mathalan, wakati wa sikukuu ya Idul-Fitr (sikukuu ya kufungua Mfungo) ni faradhi kwa kila Mwislamu, mke kwa mume, mtu mzima na mtoto, ya kwamba kabla ya kusali sala iliyowekwa kwa ajili ya siku hiyo, kutoa ratili tatu za ngano au mahindi au kutoa pesa taslimu za thamani ya ratili hizo kama mchango wa kuwasaidia maskini. Hata yule maskini wa mwisho hakusamehewa faradhi hii. Mwenye kuweza ni sharti atoe mchango huu kutoka mali yake, lakini yule asiyeweza kuchanga hata hivyo ni sharti atoe mchango wake kutoka kile atakachokizawadiwa kama sadaka siku ile.

ZAKA

Wajibu mwingine wa kifedha uliofaradhishiwa Waislamu ni Zaka, inayotozwa kila mtu anayemiliki kiasi fulani cha pesa au vitu au wanyama. Ukadiriaji wa kiwango cha Zaka watofautiana. Kama kwa mfano, kiwango ni aslimia kumi kwa mazao ya shambani na mbili

unusu kwa pesa za kibiashara na faida. Utaratibu unapotazmwa kwa mara ya kwanza unakuwa na sura ya kubagua na wa kiumoja, lakini kile kiwango cha pesa za mtaji na faida si hafifu kama kinavyoonekana. Pale ambapo makadirio ya kiwango cha Zaka juu ya mazao ya shambani kinatozwa mazao tu, kiwango cha shughuli za kibiashara chatozwa mtaji uliopo pamwe na faida zake. Shabaha yenyewe sio tu kuweka njia ya kuwasaidia wenye shida na ustawi wa wale wenye hali dhaifu ya kiuchumi katika jamii bali pia kuzuia ulundikaji wa pesa na bidhaa na hivyo basi kuhamasisha uzungukaji maridhawa wa hivyo vyote viwili, vikiwa na matokeo ya ukuaji mzuri wa kiuchumi.

Kurani yaelezea kwa kirefu zile sera ambazo inabidi ziwe ndizo msingi wa shughuli za kibinadamu. Yasisitizia haja ya kushirikiana na yafafanua mipaka ya haki za mtu mmoja mmoja na zile za watu wote kwa pamoja pamwe na majukumu. Yaelezea misingi ya utawala na majukumu yake na uhusiano unaotakiwa kuwepo baina ya Serikali na raia zake. Yarekebisha uhusiano wa bwana na mtumishi na kuweka kanuni zinazotakiwa kusimamia uhusiano wa kimataifa.

Kurani yaagiza kwa uwazi kwamba mali zisiruhusiwe kulundikana mikononi mwa watu wachache na kwamba hazina budi kufanywa ziendelee kuzunguka. Ili kufikia lengo hili, yapiga marufuku desturi ya riba katika ukopeshaji wa pesa ambayo kufuatana nayo watu wachache werevu wanaweza kumiliki sehemu iliyo kubwa ya utajiri wa umma na yafaradhisha ugawanyaji wa urithi. Haimruhusu mtu yeyote kumrithisha mtu mmoja mali zake zote miongoni mwa warithi wengi bali hata kuzidisha fungu la mrithi mmoja kuliko la mwingine. Kurani yataka kufanya marekebisho mwafaka katika ugawaji wa utajiri ikitumia njia ya Zaka, sadaka na kufanyiana hisani. Inalifanya jukumu tangulizi la mapato yote ya serikali na rasilimali kugharamia masilahi na maendeleo ya wale walio masikini zaidi katika jamii. Kwa njia hizi Kurani inakidhia ustawi wa kiuchumi wa tabaka zote za umma.

Kurani yatilia mkazo haja ya elimu na ustawi wa kimawazo. Yapendekeza kutafakari na kudhukuru kuwa ni faradhi za kidini.

Yawashawishi watu kutojiingiza mizozoni na kupigana vita na yakatalia mbali uchokozi. Yasimika kwa kirefu kanuni kwa ajili ya kusimamia uhusiano baina ya wafuasi wa dini mbalimbali. Inawakataza Waislamu wasiseme lolote la matusi juu ya Waanzilishi au Viongozi wa dini zingine. Ama kuhusu mabishano ya kidini Kurani yagusia kutostahili kwa lawama zitolewazo dhidi ya dini pinzani ambazo mwenye kulaumu imani na itikadi zake mwenyewe zinakabiliwa na lawama hizo hizo. Yafundisha kwamba dini zote kubwa msingi wao ni wahyi na kwamba uchakazi wa dini hizo watokana na uchafuzi wa baadaye unaofanywa na mikono ya wanadamu. Hivyo basi, Kurani yakataza mashutumu ya kupita kiasi dhidi ya dini zingine.

Kurani yazilinda kikamilifu haki za wanawake. Ndicho Kitabu cha kwanza kwanza ambacho kimefundisha kinagaubaga ya kuwa wanaume wamewajibishiwa wanawake kama vile wanawake walivyowajibishiwa wanaume. Yafafanua haki na wajibu wa wazazi, ndugu na dada, bwana na bibi, wana na mabinti, majirani, maskini, mayatima, wajane, marafiki na wapita njia wa nchini mwa mtu na watoka-nje ambao wamekuwa wakazi wa nchini mwa mtu au ambao ni watembezi tu.

SERIKALI YA KIISLAMU

Kurani yawasilisha mawazo mapya kabisa kwenye uwanja wa siasa. Ndicho Kitabu cha kwanza kilichoweka kanuni hii ya kwamba hapana mtu awezaye kujipatia haki ya kuwatawala wengine kwa uwezo wa kurithi kijadi. Yafundisha kwamba kutawala ni amana ambayo ni sharti ikabidhiwe wale ambao watu wanawachagua. Kanuni ya demokrasia inayojivuniwa sana na bara la Ulaya na kutumiwa vibaya sana leo hii iliwekwa kwa mara ya kwanza na Kurani. Kurani yaamrisha usimamizi, nidhamu na utiifu kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine yawataka wahudumu wa umma kutekeleza wajibu wao kwa uaminifu na unyofu. Ni Kitabu cha kwanza ambacho kimeubana uwezo wa wale walio na mamlaka na

kuwanidhamisha. Kurani hairuhusu haki ya mtu yeyote kuwa yeye peke yake na amri zote juu ya umma wala hairuhusu wazo kwamba ukarimu utawalani na usimamizini ni hisani mtawala awafanyiayo raia. Kurani yasisitizia hii kanuni ya kwamba utawala ni mali ya umma na kwamba wale waliomo mamlakani wameyakabidhiwa kwa niaba ya Mwenyezi Mungu (Sura An-Nisaa, 4:59). Kuyatumia mamlaka inapofaa na kwa njia nzuri sio hisani iliyofanyiwa umma bali ni kutekeleza tu jukumu walilokabidhiwa wale ambao mamlaka yamewekelewa juu yao. Kurani yasisitiza, hivyo basi, ya kuwa katika utumizi wa haki yao (ya kuchagua) wenye kuchagua wasikumbwe na fikara za vyama au za kibinafsi bali ya kuwa mizani ya pekee iwe ni hali stahilivu ya mgombea kuyamudu yale majukumu atakayokabidhiwa. Ni hapo tu ambapo mchaguliwa angelipokuwa katika hali ya kuweza kutekeleza majukumu yale kwa njia yenye manufaa zaidi. Yule ambaye kwa fikara za vyama au za kibinafsi anasaidia kusimika mamlakani mtu asiyefaa basi hana budi kushirikishiwa lawama za utawala wake mbovu. Hawezi akadai kwamba ubovu huo haukuwa wake, kwani alichangia kumweka yule mhusika mahali angelipoweza kuzifanyia masihara shughuli za umma.

Kurani yaisisitizia Serikali kuwa na ile ile mienendo mizuri ambayo ni faradhi juu ya raia. Haiungi mkono hii rai ya kwamba tabia ya kudumisha mienendo mizuri haina haja ya kusisitiziwa kwa upande wa Serikali na utawala. Yafundisha kwamba tabia ya kusema kweli ni kitu cha lazima na kisichoachika kwa upande wa viongozi wa nchi kama vile kilivyo cha lazima kwa upande wa raia wa kawaida na kwamba chokochoko ni kitu kibaya na kinacholaumika kwa upande wa utawala kama vile kilivyo kwa upande wa raia. Yaiwekea Serikali utendaji wa haki na uadilifu sio tu kwa watu wake yenyewe bali pia, kama ilivyo kwa upande wa mtu binafsi, kwa Serikali jirani.

Kurani yamtaka muumini kujitahadhari wakati wote. Yawahimiza Waislamu kufanya bidii na yalaumu woga, uchokozi na upayukaji. Yahimizia utumiaji wa akili na busara. Yakataza mtu kujiua na matendo yote au mazoea yanayoweza kuishilizia na kujiangamiza.

Inaziwekea Serikali wajibu wa kulinda mipaka ya nchi zao. Yakataza uchokozi lakini yafaradhisha upingaji kabambe wa uchokozi. Vitani Kurani yakataza mashambulio ya ghafla ya usiku. Yasisitizia kuijali vilivyo mikataba na yafundisha kwamba fursa yoyote ya kufanya mapatano ya amani na isitupiliwe mbali.

ISEMAVYO KURANI JUU YA UTUMWA

Kurani hairuhusu kumtia utumwani raia wa nchi wala mgeni. Hata hivyo, yaruhusu utekaji wa wafungwa wa kivita lakini yatoa maagizo kwamba kila mfungwa yuwastahili uhuru alipapo fidia (Sura Muhammad, 47:5). Hapana awezaye kumdumisha mwingine kifungoni baada ya huyo mwingine kujilipia fidia. Endapo mtu aliyeshikwa mateka vitani hawezi kujilipia fidia mara moja, basi yeye yuwastahili kujichumia uhuru wake kwa njia ya kuchapa kazi. Asipoweza hata kufanya hivyo, Kurani yawahimiza Waislamu kumsaidia na kutafuta njia za kupatia uhuru wake (Sura An-Nuur, 24:34). Hata hivyo, inaweza ikatokea kwamba mfungwa apendelee kubakia na yule bwana wake Mwislamu badala ya kurejea kwa nduguze wasiokuwa Waislamu kwenda kuishi chini ya Serikali isiyokuwa ya Kiislamu. Katika hali kama hii Kurani yafundisha kwamba mtu kama huyo atendewe kwa haki na uadilifu. Mtume Mtukufu[saw] amesema kwamba katika hali kama hiyo yule bwana hana budi kumlisha mfungwa wake chakula kile kile alacho yeye mwenyewe na kumvisha aina ile ile ya nguo anazovaa yeye mwenyewe na ampatie rikabu kama rikabu yake yeye mwenyewe au wapokezane mnyama wake yule yule mmoja (Bukhari).

Kurani yasisitizia usawa wa wanadamu wote. Ndicho Kitabu cha kwanza kifundishacho kwamba wanadamu ni jamii moja. Yatambua hali ya wanadamu ya kugawanyika katika sura ya nchi, mataifa na makabila lakini yaelezea kwamba hii ni kwa shabaha ya utambulikanaji tu na kwamba kuhusu haki wanadamu wote ni sawa. Yazikanusha tofauti zote zenye misingi ya kudai ubora wa kitaifa, kiuchumi au ubora wowote ule unaootwa. Yawaonya watu kwamba

wanaojipambia aina yoyote ya ubora watadunishwa na watadharaulishwa na kwamba wale wanaodharauliwa na jamaa hao siku moja watakujanyanyuliwa juu zaidi yao. Kama fundisho hili murua linalofundishwa na Kurani litokee kukubaliwa na dunia nzima, vile vizingiti vikubwa dhidi ya kusimika amani humu duniani vitaondolewa mbali.

Kurani yakataza kila kitu chenye kuelekea kuwavutia watu kwenye upotovu na upuuzi. Mathalan, yaharamisha kamari na unywaji wa pombe. Yakataza tabia zote za kipuuzi na uzembe. Yapiga marufuku desturi ya wanaume kuvaa mapambo na nguo za hariri, lakini yawaruhusu wanawake kuvitumia vitu hivi kwa kiasi.

ROHO YA MWANADAMU

Kurani ni Kitabu cha pekee chenye kulizungumzia kwa kirefu suala la roho ya mwanadamu na kuumbwa kwake. Vitabu vingine havilijali suala hili kabisa au hulikisia-kisia tu. Kurani yasema hivi: "Na wanakuuliza juu ya roho. Sema: Roho imetokana na amri ya Mola wangu; nanyi hamkupewa katika elimu ya roho ila kidogo (Sura Banii Israaiil, 17:86). Aya hii yaisuta ile rai ya kwamba roho zinajifanya zenyewe kuwepo na ni za azali na kwamba zinajikalia kama akiba kwenye ulimwengu mwingine na hushuka ardhini mara kwa mara na kupenya miilini mwa wanadamu. Yasema kwamba roho ya mwanadamu, kama viumbe vinginevyo, huumbwa na Mwenyezi Mungu na hukua chini ya uongozi wa kiungu. Pia yaonesha kwamba kuzalika kwa roho sio mbali na kuzalika kwa mwili. Ule msururu wa maendeleo usababishao kuzalika kwa mwili, huo pia husababisha kuzalika kwa roho na kuiandalia ukuaji wake na ustawi wake. Jamho hili laelezewa kwa fasili zaidi mahali pengine ndani ya Kurani inaposemwa hivi:

> "Na kwa yakini tulimwumba mwanadamu toka mateuzi ya udongo. Kisha tukamfanya mbegu katika kao lililohifadhika. Kisha tukaiumba mbegu kuwa pande la damu, na tukaumba pande la damu kuwa pande la nyama. Kisha tukaumba pande la

> nyama kuwa mifupa, na mifupa tukaivisha nyama, kisha tukaifanya kiumbe kingine. Basi Mwenye mibaraka ni Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbao'' (Sura Al-Mu'minuun, 23:13-15).

Aya hii yaeleza kwamba mwanadamu huzalika kama matokeo ya lishe alayo mume na mke kuendeleza uhai na kujidumishia nguvu zao. Lishe hii huzalisha mwilini mwa mtu maada ambayo kwayo uzaanaji hufanyika. Maada hii inapoingia ndani ya tumbo la uzazi, sehemu yake yenye kipawa cha uzaanaji hushikamana na tumbo la uzazi na kuanza kujipatia lishe. Katika siku chache huanza kuganda na kuwa chipuo laini-laini ambalo ndani yake mifupa kuumbika na baadaye, mifupa inapofunikwa nyama, hatua zote za uzaanaji wa kimwili hukamilika. Sawia na uumbikaji huu huanza kuzalika maada fulani ambazo matokeo yake chipuo hili hujipatia hulka za kinyama na mwishowe huishilizia na kuzaliwa kwa mwanadamu mwenye fahamu zake. Aya yaonesha kwa uwazi kwamba roho haijipenyezi mwilini kutoka nje bali ni chujo kutoka lile chipuo linalokuwa linaumbika ndani ya tumbo la mama la uzazi. Bila shaka hii ni tofauti na lile chipuo ambalo huchujwa kutokana nalo na inayo athari ya kulipatia hili chipuo hulka za kinyama na ya kuligeuza kuwa mwanadamu mwenye kujaaliwa akili na fahamu na kipawa cha ukuaji (maendeleo). Kimfano mtu kwa kiasi fulani anaweza akalinganisha na tabia fulani ya kubadilika kwa kemikali ambapo vitu fulani vilivyomo hujumuika vikawa kitu kipya kabisa chenye sifa tofauti. Mathalan, kemikali ya alikoholi huchujwa kutoka maboga, ngano, mahindi au asali ya miwa. Ina sifa tofauti na za vile vitu vya awali inavyovitengenezewa. Ingawa mali hizo ghafi inazozitengenezewa huweza kuoza, alikoholi yenyewe ni kago ya uozefu. Tena, wakati utumiaji wa hizo mali zake ghafi haudhuru moja kwa moja uwezo wa akili ya mwanadamu, hii kemikali ya alikoholi ndio ulevi wenyewe.

Kwa neno zima, Kurani yawasilisha rai mpya kabisa kuhusu kuzalika kwa roho ya mwanadamu isiyopatikana katika Kitabu chochote cha hapo kabla. Kama ilivyokwisha semwa, baadhi ya Vitabu hivi viko kimya kabisa juu ya jambo hili. Vimekomea kumzungumzia

mwanadamu jinsi vilivyomkuta wala havioni haja ya kuliangazia suala la kuumbwa kwa mwanadamu na kwa roho ya mwanadamu. Vile vinavyodai vinalizungumzia suala hili vyatoa mojawapo ya nadharia mbili. Moja ya nadharia hizi ni kwamba roho za wanadamu haziumbwi na Mwenyezi Mungu bali ni za azali na zinajidumisha zenyewe kama vile Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu huzifanya roho hizi za azali kupenya miilini mwa wanadamu wakati unapowadia. Nadharia ya pili ni kwamba roho zimeumbwa na hazijidumishi zenyewe lakini Mwenyezi Mungu aliumba idadi inayotakikana wakati ule ule alipoyaumba malimwengu na kwamba roho zimewekwa akiba na kutoka akiba hii Mwenyezi Mungu huzifanya zingine kupenya miilini mwa wanadamu wakati huu na ule. Kurani ni Kitabu cha kwanza kinachowasilisha rai sahihi juu ya jambo hili. Yafundisha kwamba kuzalika kwa roho ndiyo hatua ya kileleni ya mabadiliko ya mwili wa mwanadamu katika hali ya kuumbika kwake. Haipenyi mwilini kutoka nje bali huzalika kama matokeo ya mabadiliko mwilini unayoyapata katika ukuaji wake. Lakini hata hivyo ni kitu tofauti kabisa na mwili wenyewe. Sio chemchemi ya dhamira za mwili tu bali ni kitu tofauti kabisa chenye kudumu kilichochujwa kutoka kiumbio cha mwili, kama ilivyo hali ya alikoholi na siki, ingawa huchujwa kutoka nafaka au matunda, lakini hata hivyo vyatofautiana kabisa na vile viumbio inavyokitengenezewa. Kwa kuangazia ukweli huu Kurani imeyapindulia mbali maoni ya mwanadamu kuhusu uhusiano baina ya mwili na roho. Wale wanaoamini kwamba roho za wanadamu zajidumisha zenyewe na ni za azali au kwamba ziliumbwa zote kundi zima zama yalipoumbwa malimwengu na hushushwa ardhini inapohitaji hapa na pale, wanakanusha wazo lolote kwamba hali ya kimwili na ukuaji wa kimwili vina athari yoyote juu ya ukuaji wa roho. Kwa upande mwingine, Kurani kwa kubainisha ukweli na hali ya mambo yalivyo, imetilia uzito ya kwamba hali na ukuaji wa mtu inao uhusiano wa karibu zaidi na hali yake ya kiroho na ukuaji wake wa kimwili. Ni kweli kwamba hata chini ya haya mafundisho ya

Kurani kila mwili wa mwanadamu hauna budi kwenye hatua fulani ujichipuzie roho, lakini mafundisho ya Kurani yakumbusha hii kanuni ya kwamba kama ukuaji wa mwili wa mwanadamu ukifanyiwa makini katika hali ya kiafya na utu bora, basi nafsi (ya mtu) itakayotokana na hali hiyo itakuwa na usimeme na werevu zaidi ya vile ingelivyokuwa kama ukuaji huo usingelitiliwa maanani. Kwa kukumbusha ukweli huu Kurani imemfungulia mwanadamu njia mpya mpya kwa ajili ya maendeleo yake ya kiakili la kiroho.

Watu wengine wanadai kwamba roho haina vipawa vyake yenyewe na hivyo basi haiwezi ikaathiriwa na mabadiliko yoyote mwilini. Rai hii sio sawa. Kudai kwamba roho haina vipawa hakuna maana yoyote. Kama roho haina vipawa vyake basi haiwezi ikaishi peke yake (mbali na mwili). Kwa kweli inavyo vipawa vyake lakini inaweza tu ikavidhihirisha kwa njia ya kiwilwili (cha mtu). Kunazo hali fulani fulani hata katika haya malimwengu ya kimwili tunamokuta ya kwamba vitu fulani vinaweza tu kujidhihirisha kwa njia ya vitu vingine. Mathalan, sisi wakati wote tuna kumbana na hii hali ya kwamba umeme unaweza tu kudhihirisha athari yake kwa njia ya vitu vingine (waya). Vivyo hivyo, vipawa vya roho hujionesha kwa njia mbalimbali kupitia mwili.

Kurani yayazungumzia haya yote pamwe na masuala mengine kama haya, lakini kwa sababu zilizo wazi hayo yote hayawezi yakazungumziwa ndani ya 'Kifungua Mlango' hiki. Kurani yadai kwamba yayazungumzia mambo yote yaliyo ya lazima kwa ukuaji wa mwanadamu wa kimwili, kitabia na kiroho na maendeleo na katika kila zama madai haya yamekutwa yakiwa yanastahili. Pia katika hii karne ya ishirini inapofikiriwa kwamba sayansi na elimu vimefikia hatua ya kimaendeleo ya juu sana, twakuta kwamba Kurani yatosheleza haja zote halisi na kwamba hapana suala linalofungamana na maendeleo ya mwanadamu ya kimwili, kitabia, kiakili au usafi wa kiroho ambalo hailizungumziwi kikamilifu ndani ya Kurani. Masuala haya yanaweza yakagusiwa hapa kwa ufupi tu. Maelezo ya kirefu yanaweza yakapatikana kutoka Tafsiri na vile vifafanuzi vya aya

mhusika. Vifafanuzi katika Maelezo haya imelazimika vipunguzwe lakini tafsili ya habari kuhusu masuala haya itapatikana kutoka yale Maelezo ya Kiurdu ya Kurani.

PLANI YA KURANI YA MALIMWENGU YA KIROHO

Baada ya kutoa muhtasari wa sifa za mafundisho ya Kurani sasa tungekumbusha malimwengu ya kiroho yanayoelezewa na Kurani. Utalii wetu wa malimwengu ya kimwili waonesha kwamba yafanya kazi kwa utaratibu ambamo sayari kadha hulizunguka jua, nalo jua pamwe na sayari zake zote kusafiri kuelekea kikomoni pake ambapo kupahusu hapo wanahesabu mamboleo wanadai kwamba ni kitovu ambacho majua kadha na sayari zao yanahusikana napo. Rai hii isimame juu ya ukweli wa mambo yalivyo au la, ni jambo lisilokatalika ya kuwa haya malimwengu mazima ya kimwili yafanya kazi kiutaratibu; waila yangekuwa yamemalizika na vurugu zamani za kale. Utaratibu huu watawaliwa na kanuni zinazosimamia jiha mbalimbali za maada na kama matokeo yake malimwengu yamejawa na aina nyingi mno za maada za kimwili na vitu. Maendeleo na ukuaji wa malimwengu ya kimwili vyategemea utumiaji na hali ya kujinufaisha na maada hizi za kimwili na vitu. Kurani yafundisha kwamba malimwengu ya kiroho hali kadhalika hufanya kazi kwa utaratibu unaozunguka Kitovu chenye uwezo wote kinachotawala malimwengu yote. Hamna chochote malimwenguni kilicho nje au kilichoepukana na utawala wa Kitovu hiki. Kituvu hiki ni Dhati Mwenye kujidumisha na Ambaye Hakuumbwa. Hategemei chochote kile kwa mintarafu ya kutekeleza malengo yake. Hakuzaliwa wala hazai wala hana mshirika anayeshirikiana naye katika uwezo Wake na kazi Zake. Haya yamebainishwa wazi katika Sura Ikhlaas (sura ya 112). Katika Sura hiyo Mwenyezi Mungu Yuwamwamuru Mtume Mtukufu[saw] kutangaza kwamba ukweli wenyewe ni kuwa Mungu ni wa kipekee katika uwezo Wake wote na sifa Zake. Wakati mwingine mtu anaweza akagundua mfanano baina ya sifa za kitu au mtu na baadhi ya sifa za Mwenyezi Mungu lakini mfanano wenyewe sio halisi na ni wa kijuujuu tu. Kwa mfano, twasema ya kuwa Mungu

yupo na inaweza ikasemwa kwamba watu na wanyama na vitu vingine pia vipo. Neno lililotumiwa kuleta wazo la kuwepo ni lile lile pande zote mbili, lakini halimaanishi uhakika ule ule kila upande. Tusemapo Mungu yupo tuna maana ya kwamba Yeye yuwajifanya kuwepo na yu mkamilifu katika Dhati Yake wala kuwepo Kwake hakutegemei dhati mwinginewe au kitu chochote. Lakini tusemapo kwamba mtu yupo au mnyama yupo au kitu kinginecho kipo, tunachomaanisa ni kwamba mradi vinaendelea kuwepo vile visababisho na hali ambavyo uhusiano wao ulikuwa na matokeo ya kuumbika kwa mtu yule au mnyama yule au kitu kile, basi vitaendelea kuwepo; lakini ya kwamba kama visababisho hivyo na hali hizo zikiondolewa au kufikwa na athari basi mtu yule na mnyama yule na kitu kile navyo pia vitakoma kuwepo au vitaathirika. Kwa mfano, mwanadamu husemewa yu hai mradi uhusiano baina ya roho na mwili wake unaendelea kuwepo. Lakini uhusiano huu ni wa muda tu wakatizika, na unapokatizwa mwili wa mwanadamu huendelea kuwepo lakini hauko hai. Tena, mwili wenyewe ni chungu nzima ya atomu ambazo katika hali fulani fulani hupata sura maalum na kuwa mchanganyiko fulani. Michanganyiko hii inapoyeyushwa basi mwili hukoma kuwa kama mwili. Maiti inapozikwa ardhini mabadiliko fulani ya kemikali hutokea na huozalea mbali. Zile atomu zilizokuwa zimefanya mwili bado huendelea kuwepo lakini zile hali zilizokuwa zimeleta mchanganyano wao katika sura ya mwili zikiwa zimebadilika, mwili hukoma kuwepo. Hali hii hii hutokea wakati mwili unapoozeshwa na athari ya maji au moto au umeme. Zile atomu za maada zilizokuwa zimefanya mwili huendelea kuwepo lakini hupata sura mpya na mwili hauwezi tena kubakia na umbo lake au mchanganyano wake. Hali hizi zote hazihusikii Mwenyezi Mungu. Hapana visababisho vya nje au hali vilivyomuumbisha au kusaidia kudumisha kuwepo Kwake. Yeye huwepo kwa sababu Yu mtimilifu na Ameepukana kabisa na kizingio cha dahari. Yadaiwa kwamba bongo la mwanadamu haliwezi kutaamuli awezavyo kuwepo Mwenyezi Mungu nje ya kizingio cha dahari ambapo maada yote

inakabiliwa na kizingio hicho. Lakini ukweli wenyewe ni kwamba Mungu yupo katika maana tofauti na ile anayokuwepo mtu au dhati za kimwili au vitu na ule mfanano baina ya hivyo viwili katika hili jambo la kuwepo ni mfanano wa mbele za macho tu na ni wa kijuujuu. Mwenyezi Mungu ni wa Kipekee na hagawanyani sifa Yake yoyote na dhati yeyote mwingine au kitu kingine. Mahali pengine Kurani yasema kwamba Mwenyezt Mungu ndiye Muumba wa mbingu na ardhi. Ameumba mwanadamu na wanyama, vitu vyote jozi jozi na amefanya maandalizi kwa ajili ya maendeleo ya malimwengu ya kimwili kupitia njia hizi (Sura Ash-Shuura, 42:12). Hii yamaanisha kwamba wanadamu na wanyama na mimea na hata vitu vilivyo mango vimeumbwa jozi jozi hali inayoweza kuelezewa kuwa ya kiume na kike, au hali ya chanya na hasi au kuelezewa kwa jina jingine lolote na kwamba malimwengu mazima yanasonga mbele katika huu msingi ya kwamba kila kitu kimeumbwa jozi jozi. Tena, Kurani yasema: "Na katika kila kitu tumeumba jozi ili mpate kufahamu (Sura Adh-Dhaariyaat, 51:50). Hii yamaanisha kwamba mwanadamu, kwa kukitafakaria kila kitu malimwenguni na kuona kwamba kila kitu kimeumbwa jozi jozi, apate kuamua kwamba hapana kimojawapo cha viumbe hivi kiwezacho kuwa Mungu, kwani kila kimoja chao binafsi sicho kikamilifu na chaweza tu kuendelea na hali ya kuwepo kwake na kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa msaada wa mwenzi.

Kwa neno zima, Kurani yafundisha kwamba Kitovu cha malimwengu ni Dhat aliye Binafsi wa Kipekee na kwamba hapana dhati mwingine au kitu kilicho mfano Wake halisi. Malimwengu mazima yanategemea kitu kingine kwa ajili ya kuendelea kwake na kwa ajili ya kutekeleza kazi zake lakini Yule Dhati Ambaye ndiye Kitovu cha malimwengu yote si mwenye kumtegemea dhati mwingine au kitu kingine kwa ajili ya kuwepo Kwake au kudhihirisha sifa Zake. Kurani yafundisha kwamba Dhati Huyo hakuzaliwa wala hazai.

Hii yayatofautisha mafundisho ya Kurani na yale ya Kikristo juu ya jambo hili. Ukristo na baadhi ya madhehebu mengine ya Kiaria

vyamnasibishia Mwenyezi Mungu uzaaji wa watoto. Kurani, kwa upande mwingine, yafundisha kwamba ni wale dhati wasiojitegemea au wakabiliwao na utowekaji tu ndio wenye kuhitaji watoto. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu si mhitaji wala hatakoma kuwepo, Hahitaji watoto. Kwa kuwa Yeye yuwajidumisha, hana baba. Ndiposa Yeye ni wa kipekee kwani hakuzaliwa wala hazai na kwamba Yu wa kipekee kwa kuwa hapana dhati mwingine mwenye uwezo na sifa kama Zake.Yaani, Mwenyezi Mungu hakuumbwa wala hazai wala hana kifani chake. Fundisho hili la mwisho la Kurani lasuta itikadi ya wingi wa miungu linalofundishwa na dini kama vile Uzorasta (dini ya Kifarsi).

Sura *Ikhlaas* katika aya zake chache fasaha yatangaza kwamba Kitovu cha malimwengu yote ni Mwenyezi Mungu, Aliye Dhati wa Kipekee. Yeye ndiye chimbuko la malimwengu na hamtegemei mwingine au kitu kingine kwa ajili ya udhihirishaji wa sifa Zake. Hakuzaliwa wala hazai. Hapana nguvu iliyo sambamba inayoshirikiana naye sifa Zake wala hapana dhati mwingine mwenye manzili ya kipinzani ya kupingana naye. Sura hii fupi kwa maneno machache rahisi yasuta makosa ya itikadi za dini nyingine zote kuhusu Yule Dhati Mtakatifu na yatangaza Umoja halisi wa Mwenyezi Mungu.

MUNGU WA MATAIFA YOTE

Wafuasi wa baadhi ya dini waamini kwamha Mwenyezi Mungu ana hali maalumu ya uhusiano nao walioinyimwa wanadamu wengine wote. Wanaamini kwamba ingawaje Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa malimwengu yote, Yeye kwa maana maalumu ni Mungu wa watu fulani maalumu, kama vile Waisraeli, Mabaniani na Wazoroasta. Kurani yalikatalia mbali fundisho hili na kufundisha kwamba Mwenyezi Mungu sio tu kwamba ni wa kipekee katika dhati Yake bali kwamba Yeye ndiye chimbuko la malimwengu yote. Neno Allah lionekanalo kwenye aya ya kwanza ya Sura Ikhlaas lamaanisha ‘wa kipekee’ na pia ‘Mmoja’, yaani chimbuko ambalo kibinafsi limeepukana na idadi lakini ambalo zinaanzia idadi zote. Aya hii yaonesha kwamba Mwenyezi Mungu ni mwongozi wa wanadamu

wote kwa usawa wala hana upendo wowote maalumu kwa taifa lolote mahususi. Wale wanaojitahidi kupata ukaribu naye Yeye huwaongoza kwenye njia zifikishazo Kwake. Waarabu, Mayahudi, Waajemi, Wahindi, Wachina, Wagiriki na Waafrika machoni pake wote wako sawa, kwani Ndiye chimbuko la kuumbwa kwa hao wote. Yeye peke yake ndiye umoja ulio ni chanzo cha wingi malimwenguni. Kwa kutangaza kwamba Yeye hakuzaliwa, Kurani yakanusha itikadi kubwa ya Ukristo pamwe na imani kadha za Kibaniani, kwani yule ambaye mwenyewe kazaliwa asingeliweza kuwa Mungu kwa kuwa angelitokea kumtegemea mwinginewe kwa ajili ya kuumbwa kwake. Kwa kubainisha kwamba hana kifani chake, Kurani yakanusha ile itikadi inayofundishwa na dini zingine ya kwamba nuru na giza ni nguvu tofauti zinazopingana na hivyo dini hizo kuzusha miungu wawili.

MWENYEZI MUNGU – CHANZO CHA VIUMBE VYOTE

Kurani yafundisha pia ya kwamba Mwenyezi Mungu ndiye chanzo cha viumbe vyote; ndio kusema kwamba viumbe vyote vimetokana naye na hurejea Kwake. Kurani yasema: "Yeye ndiye wa Mwanzo na wa Mwisho" (Sura Al-Hadiid, 57:4). Hii yamaanisha kwamba kila kitu malimwenguni kuwepo kwake kumetokana na Mwenyezi Mungu na kwamba kukoma kwa kila kitu nako pia hutokea kwa kanuni za Mungu. Asingeliridhia Mwenyezi Mungu kuyajazi malimwengu hali ya kuwepo, kamwe yasingelipata kuwepo; na asingelikuwa Mwenyezi Mungu amejaalia kanuni kwa ajili ya kuangamia kwa malimwengu, yasingeliweza kuangamia. Hivyo basi, uumbaji wote na uangamizaji unatawaliwa na kanuni za Mungu na hili ni thibitisho la ukweli kwamba utaratibu wa malimwengu umejaaliwa na Dhati mwenye hekima. Kurani yasema:

> Mwanzishaji wa mbingu na ardhi! Iweje Yeye kuwa na mwana hali hana mke, hali Yeye aliumba kila kitu na ni Mwenye ujuzi wa vitu vyote? Huyo ndiye Allah, Mola wenu. Hapana aabudiwaye ila Yeye, Muumba wa vitu vyote, basi mwabuduni Yeye. Na Yeye ni Mlinzi wa kila kitu (Sura Al-An'aam, 6:102-103).

Aya hizi zatangaza kwamba kwa kuwa Mwenyezi Mungu ni chanzo cha viumbe vyote, Yeye Hahitaji mwana. Mwana huzaliwa kiajali tu au kukidhia haja fulani. Kujamiiana kwa mke na mume hata bila ya lengo la uzaaji kunaweza kukawa na matokeo ya kuzaliwa kwa mtoto. Uwezekano wa kitu hiki kwa upande wa Mwenyezi Mungu wakanushwa katika aya iliyokaririwa hapo juu kwa kukumbushwa huu ukweli kwamba Hana mke. Inadaiwa, hata hivyo, na baadhi ya watu kwamba anaweza Mwenyezi Mungu Akamuumba dhati fulani na kumjazi cheo cha mwana. Lakini mwana yuwahitajika tu kwa minajili ya kumsaidia baba kuendesha kazi zake au kuendeleza nasaba yake. Kurani yasema kwamba Mwanyezi Mungu akiwa ndiye Muumbaji na Msimamizi wa vitu vyote, Hahitaji usaidizi, na akiwa ni wa azali jina Lake litadumu milele na milele. Hivyo, hautakuwa na maana yoyote uumbaji au upangaji Wake wa mwana. Mwanadamu wakati mwingine hujiwekea akiba kukidhia hali isiyoyamkinika ya siku za usoni, lakini Kurani yasema kwamba kwa kuwa Mwenyezi Mungu ana ujuzi kamili wa vitu vyote, haimlazimu kuwekea akiba hali yoyote isiyoyamkinika. Yeye yuwajua wakati uliopita na ujao wala hana haja ya kuutahadharia wakati ujao. Kisha Kurani yaendelea kukumbusha ukweli kwamba Mwenyezi Mungu sio tu kwamba alimuumba mwanadamu bali Yeye pia Humlea na kumkuza tokea unyongeni na udhaifuni hadi kufikia hali ya nguvu na uwezo. Hapana mungu pamoja Naye. Yeye ameumba malimwengu yote. Wanadamu wote, wawe ni Waajemi au Waarabu, Mayahudi au Mabaniani, machoni pake wote ni sawa. Yeye amewaumba wote hao na kuwajaalia wote njia za maendeleo. Hivyo, ni wajibu ya kuwa wanadamu wote wamwabudu Yeye peke yake, kwani Yeye peke yake yuwayasimamia malimwengu na mwanadamu anaweza tu akaepukana na maangamio na mahilikisho kwa kuimarisha uhusiano wake naye wala hawezi akajipatia utulivu akiwa mbali naye.

Kurani yafundisha kwamba Mwenyezi Mungu yuwajua mambo yote ya kila kitu malimwenguni. Wala hapana kilicho nje ya ujuzi Wake. Yasema hivi: "Ujuzi Wake umezienea mbingu na ardhi" (Sura Al-

Baqara, 2:256) Kisha yasema:

> Nawe hukishughulikii chochote, wala husomi kutoka Kwake sehemu yoyote ya Kurani, na hamfanyi kazi yoyote, isipokuwa Sisi tu Mashahidi juu yenu mnapoishughulikia. Wala haikufichikana kwa Mola wako hata chembe ndogo ilioje ardhini au mbinguni. Wala hapana kidogo kuliko hicho au kikubwa, isipokuwa kimo ndani ya Kitabu kielezacho (Sura Yuunus, 10:62).

Aya hizi zaonesha kwamba hali ya moyo wa mwanadamu na kile akitamkacho kwa mdomo na kile akitendacho kwa kutumia viungo vyake hivyo vyote viko dhahiri shahiri kwa Mwenyezi Mungu. Vitu hata vile vidogo chambileche atomi au hata vidogo zaidi havikufichikana machoni Pake. Yeye yuwaviona vile vidogo kupita vyote kama vile anavyoviona vile vikubwa kupita vyote na sio tu kwamba kila kitu ki ujuzini Mwake bali yote yale yafanywayo na yanayofanyika yanahifadhiwa kwa namna ambayo kwamba huzalisha matokeo yake kwenye msimu wake. Aya yasema kwamba vitu hivi vyote vinarekodiwa ndani ya Kitabu kielezacho. Hii yamaanisha kwamba wakati rekodi za kawaida zinafichwa na baada ya kuwa zimerekodiwa hutoweka hata kutoka mbele za macho ya mwenye kuzirekodi, rekodi za kiungu ni za hali ambayo kwamba zinajielezea, yaani, kila tendo huelekeza kwenye matokeo yake sawa na kanuni za Mungu na kadari ya Mungu. Kisha, Kurani yasema kwamba kwa kuwa Mwenyezi Mungu haonekani, "Macho hayawezi yakamfikia" (Sura Al-An'aam, 6:104), ndio kusema kwamba Mwenyezi Mungu kihali Yake alivyo yuwatofautiana kabisa na vitu vyote vya kimwili na haiwezekani hivyo basi kumwona kwa njia ya vipawa vyovyote vya kimwili.

Kurani yafundisha kwamba Mwenyezi Mungu ana uwezo kamili wa kutekelezea kazi Zake zote. Yasema hivi: "Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kufanya akitakacho" (Sura Al-Baqara, 2:110). Tambueni ya kwamba aya haisemi eti Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kufanya mambo yote, kwani usemi sampuli hii utawapatia wapumbavu fursa

ya kuzusha maswali ya kipuuzi. Imepata kuulizwa, kwa mfano, Je Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kujiangamiza au kama ana uwezo wa kuumba mungu mfano Wake. Ni wazi kwamba kutokea Mwenyezi Mungu kufanya kitu chochote sampuli hiyo ingelikuwa upuzi mtupu na usiokuwa na haja tena, ni kinyume na Shani Yake na Ukamilifu Wake kushughulikia chochote cha kipuuzi au kisichokuwa na haja. Hivyo basi, Kurani ilijizuia kusema kwamba Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kufanya kila kitu, imesema tu ya kwamba Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kutimiliza yale yote anayoyakadiria kufanya. Mwenyezi Mungu akiwa halisi, hukadiria kile tu kilicho halisi na ungelikuwa ni upumbavu mkubwa kumnasibishia hamu ya kujiangamiza au kuumba mungu mwingine mfano Wake Yeye Mwenyewe.

SIFA KUU ZA MWENYEZI MUNGU

Sura ya kwanza ya Kurani (Sura al-Faatiha) yaeleza zinavyofanya kazi sifa za Mwenyezi Mungu. Yaelezea kwamba sifa za kiungu, ambazo ufanyaji kazi wake unamwathiri mwanadamu katika jiha yoyote, zinachipua kutoka sifa nne kuu.

Miongoni mwa sifa hizi, ya kwanza ni Rabbul-Aalamiin (رَبُّ الْعَالَمِيْنَ); yaani, Mwenyezi Mungu Huumba kila kitu na kisha kukikuza kila kitu hatua kwa hatua kuelekea utimilifu.

Pili, Yeye ni Rahman (اَلرَّحْمٰن). Hii yamaanisha kwamba bila ya jitihada yoyote kwa upande wa viumbe Vyake, Yeye huandaa kila kitu kilicho cha lazima kwa ajili ya ukuaji wao na maendeleo.

Tatu, Yeye ni Rahiim (رَحِيْم). Hii yamaanisha kwamba pale wale viumbe Wake waliojaaliwa hiari na akili waamuapo kwa hiari yao kutenda wema na kushindana na ubaya, Mwenyezi Mungu huwajazi malipo ya juu zaidi na malipo hayo kuendelea bila mwisho.

Nne, Yeye ni Maaliki Yaumid-Din (مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِ). Hii yamaanisha kwamba hukumu ya mwisho kabisa kuhusikana na kila kitu i mikononi Mwake. Kila kitu kuwepo kwake kumetokana naye na mwisho wa kila kitu pia u mikononi Mwake. Wanadamu na viumbe

wengine wanaweza wakaleta mabadiliko ya muda na ya kupita upesi, lakini hawana uwezo wa kuleta mabadiliko yoyote ya kudumu humu malimwenguni. Mathalan, mwanadamu hana uwezo wa kuumbia maada wala roho. Na vivyo hivyo ndivyo asivyokuwa na uwezo wa kuviangamizia, ingawaje anaweza akasababisha mabadiliko katika maada na kuipatia sura mbalimbali. Kama vile sifa ya uumbaji ilivyo ya Mwenyezi Mungu peke yake na sifa ya uangamizaji nayo pia ni Yake Yeye tu. Hapana kinachoweza kuangamizika kabisakabisa mpaka Mwenyezi Mungu akadirie maangamizo yake. Huu ni ukweli ulio wazi na Kurani yauelezea kwa kusema kwamba Mwenyezi Mungu ni Mmiliki wa wakati wa hukumu. Yaani, hukumu ya mwisho kuhusikana na kila kitu i mikononi Mwake na hukumu zenyewe zinatolewa naye katika enzi Yake ya kuwa Mmiliki wa malimwengu wala sio eti kama hakimu ambaye huzifanyia maamuzi haki za wanaolumbana mbele yake. Hakimu hana budi kufanya maamuzi bila ya mapendeleo juu ya jambo linalolumbaniwa baina ya makundi akitilia maanani haki na wajibu wa kila upande. Mwenyezi Mungu haiimlazimu, kwani ingawaje Yeye atoapo hukumu yake hapana adhulumiwaye au mwenye kunyimwa haki yake, Yeye ana hiari ya kusamehe apendavyo kutoka zile zinazoweza kuhesabika kuwa ni haki Zake Yeye Mwenyewe. Kwake hakuna kusisitiza kulipiza kisasi. Kwa vile bwana anaweza akawatendea watumishi wake kwa huruma na kuwa mkarimu kwao na kuwajazi fadhila, hivyo basi Mwenyezi Mungu anaweza akasamehe madhambi ya viumbe Wake na kusahaulia mbali makosa yao na kuwajazi fadhili Zake. Kutoielewa sifa hii ya Mwenyezi Mungu kumesababisha kukubaliwa na Wakristo kwa itikadi zisizothibitika kama ile ya Kafara. Imani ya Kikristo ni kwamba Mwenyezi Mungu chambileche hakimu wa kibinadamu, hana uwezo wa kumsamehe yeyote makosa yake. Katika kufanya dhana hii yao ya kimakosa Wakristo hawaujali huu ukweli ya kuwa hakimu hutakiwa kutoa maamuzi baina ya pande mbili na kwamba yeye mwenyewe hana haki kuhusu lile jambo linalogombaniwa. Lakini uhusiano baina ya Mwenyezi Mungu na viumbe Vyake uko

tofauti kabisa na ule uhusiano baina ya hakimu na wale wanaolumbana. Mwenyezi Mungu ni mdai na pia ndiye mwenye mamlaka yanayostahili kutoa hukumu. Lakini hakimu (wa kibinadamu) hawi mdai asilani. Yeye hutakiwa tu kuyakinisha haki za wanaolumbana mbele yake. Kwa neno zima, hakimu yambidi kufikia maamuzi baina ya watu wawili; mmoja akifanya madai dhidi ya mwingine. Watu hawa wote wanaweza wakawa ni watu binafsi au mmoja akawa ni mwakilishi wa Utawala na yule mwingine akawa ni mtu binafsi. Lakini Mwenyezi Mungu huamua baina ya Yeye Mwenyewe na viumbe Wake. Hivyo basi, Yeye huwa na wajibu wa pande mbili. Yeye yu mdai na hakimu pia. Akiwa kama mdai Yeye ana haki ya kuachilia mbali kiasi apendacho cha madai Yake. Kuachilia mbali huko kunakuwa ni rehema wala sio dhuluma, kwani kuachilia huko kwahusikana na madai ya Mungu Mwenyewe wala hakufanyiki kumnyima mtu haki zake. Jambo hili laafikiana sana na akili.

Kwa upande mwingine itikadi ya Kafara inakwenda kinyume kabisa na akili. Kama imani juu ya kusulubiwa kwa Yesu ni faradhi katika msamaha wa madhambi, basi wale Manabii waliodhihiri kabla ya Yesu na wafuasi wao walijipatiaje wokovu? Je, haikuwa lazima kwa kusulubiwa huku kuwe kulitokea pale malimwengu yalipoumbika ili wanadamu wote wawe waliweza kujipatia wokovu? Tena, iweje madhambi kusamehewa kwa njia ya kuamini kusulubiwa lakini sio kwa njia ya toba, iliyo njia ya kiasili ya utakaso wa mayo. Kuamini vitu vya nje sio njia ya kiasili ya kuutakasia moyo, ilihali toba na majuto, hali zinazoulia mbali matamanio na matakwa ya mtu na kumjazi nia mpya ya kuishi maisha ya kitawa, ni njia za kiasili na halisi za kuutakasia moyo. Ni kitu cha kushangaza ya kuwa Wakristo watokee kuamini kwamba moyo wa mwenye madhambi hutakaswa na imani juu ya kusulubiwa kwa Yesu na kwamba kama matokeo ya imani hii Mwenyezi Mungu humsamehe madhambi yake, lakini watokee kuukatalia mbali ukweli kwamba zama mtenda madhambi apatapo majuto na kukiri makosa yake mbele ya Mwenyezi Mungu na kumwomba msamaha, Mwenyezi Mungu humsamehe madhambi yake na makosa yake.

Ukweli wenyewe ni kwamba katika kutekeleza shughuli zao za kila siku Wakristo wenyewe hufuata kanuni hii. Mtu afanyapo kosa na kisha yakampata majuto halisi na, huku akikiri makosa yake, aahidi kujirekebisha, wao humsamehe. Kwa mfano, kanuni hii hufuatwa shuleni mwao. Mwalimu anapogundua ya kuwa mwanafunzi alikuwa amefanya makosa au masomo kayafanyia uzembe au kutegea wajibu wake mwingine na kuwa na hakika kwamba yule mwanafunzi ametubu na yuko tayari kujirekebisha siku za usoni, basi humsamehe tu. Ilihali kama itikadi ya Kafara ingelifuatika, yote yanayotakikana kufanywa katika hali sampuli hii ingelikuwa ni huyu mwanafunzi kutamka akisema kwamba ingawaje alikuwa amehalifu sheria yeye alikuwa yu mumini wa kusulubiwa kwa Yesu na kwamba yafaa makosa yake kutotiliwa maanani. Lakini hii haifanyiki. Mwalimu husisitiza akisema kwamba ili asamehewe mwanafunzi yule ni sharti aoneshe kwamba wayajutia makosa yake na yuko tayari kujirekebisha siku za usoni. Naam, mwalimu hayuko tayari kusamehe kwa hakikisho kwamba eti mwanafunzi yuwaamini kusulubiwa (kwa Yesu).

Hata hivyo, inaweza ikadaiwa kwamba kuamini kusulubiwa ni jambo sawa na utakaso wa moyo. Lakini madai haya yanasutwa na tabia ya Wakristo duniani kote. Ufisadi na uchafu ulioenea katika nchi za Kikristo hakipatikani hata nusu ya kifani chake katika sehemu yoyote nyingine ya dunia hii.

Basi ni kitu gani kile Wakristo walichojichumia kupitia huku kuamini Kafara? Kama wakidai kwamba watajipatia wokovu kwa njia ya itakadi hii, hili litakuwa haliwezekani, kama vile tulivyokwisha onesha ya kwamba wokovu unaweza tu ukapatikana kwa njia ya toba halisi na kwamba wale Manabii waliodhihiri kabla ya Yesu pamwe na wafuasi wao walijichumia wokovu kwa njia hii peke yake. Kama Wakristo wanadai kwamba imani ya Kafara huleta usafi wa moyo, basi hali hii haijafikiwa na Wakristo licha ya kuamini kwao Kafara. Hatuna nia ya kumaanisha kwamba hapana Mkristo mwenye usafi wa moyo, lakini twasisitiza ya kwamba usafi wa moyo wa Mkristo yeyote haukutokana na kuamini Kafara.

Kama moyo wa Mkristo usafike basi umesafika, kama vile nyoyo za watu wengine, kwa njia ya majuto na toba au kwa njia ya kumwabudu Mwenyezi Mungu, yaani, sala na saumu kama alivyosema Yesu mwenyewe: "Namna hii haiwezi kutoka kwa neno lolote, isipokuwa kwa kuomba na kufunga saumu." (Marko 9:29).

SIFA NYINGINE ZA MWENYEZI MUNGU

Haiwezekani kuelezea kirefu sifa mbalimbali za Mwenyezi Mungu zinazodokezewa katika Kurani, iwe waziwazi au kimaana zilizomaanishwa na baadhi ya aya za Kurani zinavyochipuka kutoka zile sifa kuu nne zilizoelezewa hivi punde. Hata hivyo, kuzitaja kimuhtasari kunaweza kukafanywa kama ifuatavyo:

(1) Al-Maalik, yaani Mmiliki.

(2) Al Quddus, yaani Mtakatifu.

(3) As-Salaam, yaani Chemchemi ya Amani.

(4) Al-Mu'min, yaani Mhifadhi.

(5) Al-Muhaimin, yaani Mtoaji wa Hifadhi.

(6) Al-'Aziiz, Yaani Mwenye Nguvu.

(7) Al-Jabbaar, yaani Mtiishaji, Mshindi.

(8) Al-Mutakabbir, yaani Mtukufu.

(9) Al-Khaaliq, yaani Muumbaji.

(10) Al-Baari, yaani Mtengenezaji.

(11) Al-Musawwir, yaani Mfanyaji sura, umbo.

(12) Al-Ghaffaar, yaani Msamehevu Mkuu.

(13) Al-Qahhaar, yaani Mkuu Zaidi, Mbora.

(14) Al-Wahhaab, yaani Mpaji Mkuu.

(15) Al-Razzaaq, yaani Mwenye Kuruzuku,

(16) Al-Fattaah, yaani Mfunguliaji (wanadamu milango ya ufaulu, Hakimu

(17) Al-'Aliim, yaani Ajuaye sana.

(18) Al-Qaabidh, yaani Msimamizi; Mzingiaji wa kila kitu; Mkamataji

(19) Al-Baasit, yaani Mpanuliaji njia za riziki

(20) Al-Khaafidh, yaani Mdhalilishaji; Mkunjishaji mikia

(21) Ar-Raafi‘, yaani Mnyanyuaji vyeo, Daraja

(22) Al-Mu‘izz, yaani Mjaliaji heshima, Taadhima.

(23) Al-Mudhil, yaani Mdhalilishaji; Mfedheheshaji.

(24) As-Samii‘, yaani Asikiaye sana.

(25) Al-Basiir, yaani Aonaye sana.

(26) Al-Hakam, yaani Hakimu Mwenye Hekima.

(27) Al-‘Adl, yaani Mwadilifu.

(28) Al-Latiif, yaani Asiyekadirika; Mjuzi wa siri zote; Mwema

(29) Al-Khabiir, yaani Mwenye Habari zote.

(30) Al-Haliim, yaani Mvumilivu; Mwenye Subira.

(31) Al-‘Adhiim, yaani Mkuu.

(32) Al-Ghafuur, yaani Mwenye Kusamehe Sana, Msamehevu.

(33) Ash-Shakuur, yaani Mwingi wa Shukrani

(34) Al-‘Alii, yaani Aliye Juu.

(35) Al-Kabiir, yaani Mkuu asiye na kifani.

(36)Al-Hafiidh, yaani Mhifadhi; Mlinzi.

(37) Al-Muqiit, yaani Mwenye Kuhifadhi vipawa vya viumbe vyote, Mwenye Nguvu.

(38) Al-Hasiib, yaani Mwenye Kuhesabu

(39) Al-Jaliil, yaani Jalili.

(40) Al-Kariim, yaani Mbora, Mwema.

(41) Ar-Raqiib, yaani Mwangalizi Mwenye makini.

(42) Al-Mujiib, yaani Mwenye Kuitikia Maombi.

(43) Al-Waasi‘, yaani Mwenye Wasaa; Asiye na Mipaka.

(44) Al-Hakiim, yaani Mwenye Hekima.

(45) Al-Waduud, yaani Mwingi wa Mapenzi.

(46) Al-Majiid, yaani Mola Mwenye Heshima.

(47) Baa'ith yaani, Mfufuaji wa wafu.

(48) Ash-Shahid, yaani Shahidi; Mwangalizi.

(49) Al-Haqq, yaani Mkweli, Aliye Halisi.

(50) Al-Wakiil, yaani Mlinzi Mwema.

(51) Al-Qawii, yaani Mwenye Uwezo.

(52) Al-Matiin, yaani Thabiti.

(53) Al-Walii, yaani Rafiki.

(54) Al-Hamiid, yaani Msifika.

(55) Al-Muhsii, yaani Mwenye Kurekodi

(56) Al-Mubdi', yaani Mwanzilishi wa Uhai.

(57) Al-Mu'iid, yaani Mwenye kurudia tena uumbaji.

(58) Al-Muhyii, yaani Mwenye Kujazi Uhai.

(59) Al-Mumiit, yaani Msimamizi wa Visababisho vya Mauti; Mwangamizaji.

(60) Al-Hai, Yaani Mzima.

(61) Al-Qayyuum, yaani Ajidumishaye; Ajitoshelezaye

(62) Al-Waajid, yaani Mgunduzi; Mvumbuzi.

(63) Al-Majiid, yaani Mwenye utukufu.

(64) Al-Qaadir, yaani Mmiliki wa uwezo na Mamlaka.

(65) Al-Muqtadir, yaani Mwenyezi.

(66) Al-Muqaddim, yaani Mpaji (wa njia za Ukuaji na Maendeleo)

(67) Al Mu'akhkhir, yaani Mdunishaji; Muahirishaji.

(68) Al-Awwal, yaani Wa Mwanzo.

(69) Al-Aakhir, yaani Wa Mwisho.

(70) Adh-Dhaahir, yaani Dhahiri; Ambaye kila kilichoumbwa chaashiria waziwazi kuwepo Kwake.

(71) Al-Baatin, yaani Wa Siri; Ambaye Kwaye unadhihirika uhakika uliofichika wa vilivyo ghaibu.

(72) Al-Waali, yaani Mtawala.

(73) Al-Muta‘aali, yaani Aliyetukuka zaidi; Mwenye Sifa Njema.

(74) Al-Barr, yaani Mpaji.

(75) At-Tawwaab, yaani Mpole, Apokeaye Toba.

(76) Al-Mun‘im, yaani Mfadhili.

(77) Al-Muntaqim, yaani Mtoa Adhabu Stahilifu; Mlipizaji Kisasi.

(78) Al-‘Afuww, yaani Mfuta Madhambi.

(79) Al-Ra’uuf, yaani Raufu.

(80) Maalikul-Mulk, yaani Mola Mwenye Ufalme.

(81) Dhul Jalaali wal Ikraam, yaani Jalali Mwenye heshima.

(82) Al-Muqsit yaani, Mwadilifu.

(83) Al-Jaami‘, yaani Mhudhurishaji; Mkusanyaji.

(84) Al-Ghanii, yaani Mwenye Kujitosheleza.

(85) Al-Mughni, yaani Mwenye Kujazi njia za ujitoshelezaji; Mtajirishaji.

(86) Al-Maani‘, yaani Mkwamishaji, Mzuiliaji.

(87) Adh-Dhaarr, yaani Mwadhibuji.

(88) Al-Naafi‘ yaani Mfadhili.

(89) An-Nuur, yaani Nuru.

(90) Al-Haadi, yaani Mwongozi.

(91) Al-Badii‘, yaani Mwanzishaji.

(92) Al-Baaqi, yaani Abakiaye.

(93) Al-Waarith, yaani Mrithi.

(94) Ar-Rashiid, yaani Mwongozaji njia sawa.

(95) Al-Sabuur, yaani Mwenye subira.

(96) Dhul ‘Arsh, yaani Mola wa Arshi.

(97) Dhul Waqaar, yaani, Mwenye Makini; Mtulivu; Mwenye kufanya kila jambo kwa sababu zake na kwa shabaha ya kutimiza lengo fulani.

(98) Al-Mutakallim, yaani Msemaji; Mwenye kuongea na watumishi Wake.

(99) Al-Shaafii, yaani Mponyeshaji.

(100) Al-Kaafii, yaani Mwenye Kutosheleza.

(101) Al-Ahad, yaani Wa Kipekee; Mola wa Umoja.

(102) Al-Waahid, yaani Mmoja.

(103) Al-Samad, yaani Mwenye Kuhitajiwa na vyote; Mwenye Kujitegemea; Mwenye Kudumu Milele.

AINA TATU ZA SIFA ZA MWENYEZI MUNGU

Sifa hizi ama zimetajwa waziwazi katika Kurani au zinaweza zikamaanishwa na aya za Kurani. Kuzitilia maanani sifa hizi husaidia kuleta taswira ya utaratibu wa malimwengu ya kiroho Kurani inayoyawasilisha. Sifa hizi zinaweza zikagawanywa katika makundi ya aina tatu:

Kwanza, zile sifa zimhusuzo Mwenyezi Mungu peke yake na hazihusikani kivyovyote na viumbe Vyake, kwa mafano, Al-Hai — Mzima; Al-Qadir — Mmiliki wa Uwezo na Mamlaka; Al-Majiid, — Mwenye Adhama.

Pili, zile sifa zinazohusikana na kuumbwa kwa malimwengu na zaonesha uhusiano baina ya Mwenyezi Mungu na viumbe Vyake na msimamo wake juu ya viumbe hivyo, kama kwa mfano, Al-Khaaliq — Muumbaji; Al-Malik — Mwenyezi, n.k.

Tatu, zile sifa zinazoanza kufanya kazi kama matokeo ya matendo mema au mabaya ya wale viumbe wa Mwenyezi Mungu ambao wamejaaliwa hiari, kama kwa mfano, Ar-Rahiim — Mwenye kuyalipa sana tena na tena matendo mazuri ya kihiari ya mwanadamu; Maaliki Yaumd-Din — Mmiliki wa Siku ya Hukumu; Al-'Afuww — Mfuta Madhambi; Ar-Ra'uuf, — Raufu, n.k.

Baadhi ya sifa hizi ni kana kwamba ni marudio ya zingine, lakini mtu anapozitafakaria hukuta tofauti miongoni mwao. Kwa mfano, baadhi ya sifa hizi zahusikana na uumbaji kama vile ***Khaaliqu Kulli Shai'in***, Al-badii', Al-Faatir, Al-Khaaliq, Al-Baari, Al-Mu'iid, Al-Musawwir, Ar-Rabb. Mwanzoni huonekana kana kwamba zinafanana lakini ukweli

wenyewe ni kwamba zinaashiria jiha mbalimbali.

Sifa ya ***Khaaliqu Kulli Shai'in*** yamaanisha kwamba Mwenyezi Mungu ameviumba vitu vyote na yaonesha kwamba Yeye ndiye pia Muumbaj wa maada na roho. Baadhi ya watu wanaamini kwamba Mwenyezi Mungu huunda lakini haumbi. Kwa mfano, wao hawamchukulii kuwa ndiye Muumbaji wa maada na roho; wanaamini kwamba maada na roho vyajidumisha chambileche Mwenyezi Mungu mwenyewe. Angelikuwa Mwenyezi Mungu ameelezewa Kuranini kuwa yu Muumbaji tu, watu hawa wangelidai ya kuwa nao pia wanamwamini Mwenyezi Mungu kuwa yu Muumbaji kwa hii maana ya kwamba Yeye husababisha muungano wa mwili na roho na hivyo kuunda na kwa namna fulani kuumba mwanadamu. Tafsiri hii ingeliipatia walakini maana halisi ya Kurani katika jambo hili. Kwa kumwelezea Mwenyezi Mungu kuwa Yu Muumba wa vitu vyote, Kurani imelipanua eneo la sifa ya uumbaji, kusudi ijumuishe kuumbwa kwa maada na roho.

Badii‘ yaashiria kwamba Mwenyezi Mungu kauplani na kuubuni utaratibu wa malimwengu na utaratibu huu, hivyo basi, si kitu cha kibahati tu au kilichoigwa kutoka mahali penginepo.

Faatir yamaanisha Yule Ambaye hutoa kitu kwa kuvunjilia mbali ganda lake. Hivyo basi, hii sifa ya Faatir yaonesha kwamba Mwenyezi Mungu kaiumba maada ikiwa na vipawa vya ukuaji na kwamba wakati unapowadia Yeye huvunjila mbali ganda lake au kifuniko chake kizuiacho vipawa hivyo kufanya kazi, na kuvihamasisha kufanya kazi. Kwa mfano, mbegu inacho kipawa cha kukua hadi kuwa mmea au mti, lakini kipawa hiki chafanya kazi majira fulani na katika hali fulani. Zinapotokea hali hizo na msimu huo fulani uwadiapo, basi mbegu huanza kuhamasisha kipawa chake cha ukuaji. Basi, sifa hii yaonesha kwamba Mwenyezi Mungu kayaumba malimwengu kulingana na kanuni zilizowekwa na kwamba maeneo yote ya malimwengu yanazidi kukua sawa na kanuni hizo. Wakati wote maeneo fulani ya malimwengu huendelea kupitia hatua za

mwanzo mwanzo na majira fulani vipawa vyao vya kiasili kuhamasika kufanya kazi na hapo namna mpya za uhai kuweza kuonekana.

Sifa ya Khalq (uumbaji) pia yaonesha upangaji. Hivyo, neno Khaaliq (Muumbaji) lamaanisha pia ya kwamba Mwenyezi Mungu Amevipanga vitu vyote katika utaratibu wao mstahilifu na kwamba malimwengu yanasimamiwa na utaratibu.

Baadi yaashiria kwamba Mwenyezi Mungu huanzisha madhihirisho mbalimbali na kisha huweka kanuni ambazo kwa kuzitii hizo kile kitu kilichoumbwa huendelea kurudiarudia na kuongezea aina yake. Hali hii huthibitiwa na sifa ya Mu'iid, inayoashiria urudiajirudiaji.

Musawwir yaashiria kwamba Mwenyezi Mungu amekijazi kila kilichoumbwa umbo linaloafikiana na wajibu wake. Hii yaonesha kwamba kukikamilisha kiumbe ndani yake hamna tu ile hali ya kukijazi kitu kilichoumbwa vipawa vinavyostahili bali hutimilizwa pia kwa kukijazi umbo linalofaa.

Rabb yaashiria kwamba Mwenyezi Mungu baada ya kuumba huendelea kuvikuza vipawa vya vitu vilivyoumbwa hatua kwa hatua na hivyo kuvifikisha kwenye utimilifu.

Hivyo basi, sifa hizi zote zinaonesha jiha mbalimhali za uumbaji. Vivyo hivyo sifa nyingine kadha ambazo kwanza huwa kana kwamba zinafanana au ni marudio ya sifa zingine kusema kweli zinanuiwa kuonesha tofauti. Mara tu inapoeleweka maana ya kila mojawapo ya sifa hizi, mtu huweza kuona uzuri na taadhima ya maumbile ya kiroho Kurani inayoyaelezea.

Agano Jipya yataja kidogo sifa za Mwenyezi Mungu. Sio Torati wala Kitabu kimoja chochote kinachozielezea sifa hizi zote. Kwa vyovyote, kama Vitabu vya dini vya Kiyahudi vyote vichukuliwe kwa pamoja, mtu hukuta nyingi ya sifa tulizozitaja hapo juu zimetajwa mahali mbalimbali, lakini pamoja na hayo hazikutajwa zote. Kwa kawaida inafikiriwa na Waislamu kwamba Mwenyezi Mungu ana sifa tisini na tisa. Wazo hili lahusikana na imani fulani za Kiyahudi

zinazotokana na zile sifa za Mwenyezi Mungu zinazotajwa katika Vitabu vya Mayahudi. Kurani yataja sifa nyingi zaidi ya zile mia na tatu ambazo tumezitaja hapo juu lakini zingine sisi hatukuzitaja. Kusema kweli sifa nyingi za Mwenyezi Mungu, ambazo ufanyaji kazi wake hauhusikani na mwanadamu, hazikutajwa Kuranini na isingelikuwa sawa, hivyo basi, kuziwekea idadi fulani sifa za Mwenyezi Mungu. Popote pale katika vitabu vya Kiislamu inapotajwa idadi kuhusiana na suala hili huko ni kulinganisha tu na yale madai ya Kiyahudi wala sio kwa shabaha ya kutaja uhalisi wa mambo yalivyo.

Vitabu vya Veda vyataja sifa chache mno za Mwenyezi Mungu na hiyo hiyo ndiyo hali ya Vitabu vya Zend-Avista. Ukweli wenyewe ni kwamba kwa kuwa Kurani ndicho Kitabu kikamilifu na kinao mwongozo kamili kwa kila hatua ya maendeleo ya kiroho, yazitaja sifa zote za Mwenyezi Mungu ambazo kuzijua hizo ni jambo la muhimu kwa mwanadamu, zikiwemo zile sifa zilizotajwa katika Vitabu vya zamani na zile ambazo bado hazijatajwa.

SIFA ZA MWENYEZI MUNGU HAZIPINGANI

Wakati mwingine hudaiwa kwamba baadhi ya sifa hizi hazipatani na nyingine. Kwa mfano, Mwenyezi Mungu ni Mrehemevu na kumbe pia Huadhibu. Yeye si Mhitaji wa chochote ilihali huumba na kufanya maandalizi kwa minajili ya kuongoza mwanadamu jambo linaoonesha matamanio kwa upande wake kutaka kumuumba mwanadamu na viumbe wengine. Shutuma sampuli hii mara nyingi huanzia katika nafsi zenye utovu wa kutafakaria ukweli wa mambo yalivyo. Hawatambui ya kwamba sehemu kubwa ya uzuri wa haya malimwengu ni kutokana na tofauti zake na kwamba kile wanachokiita eti kutopatana na kutoafikiana ni dalili tu ya wingi wa mifumo malimwenguni. Kila kitu malimwenguni chaenda katika duara lake na kinaweza kikahesabiwa kuwa ni kiungo katika mfumo mkubwa sana.

Ni kweli kwamba Mwenyezi Mungu Huadhibu, lakini jambo hili hufanyika kulingana na kanuni Zake zinazosimamia adhabu na faini.

Utendaji kazi wa kanuni hizi unapotaka patolewe adhabu, basi Mwenyezi Mungu hutoa adhabu. Kama ilivyo kinyume na haya, Mwenyezi Mungu ameweka kanuni ambazo kufuatana nazo sifa Zake za huruma na usamehevu hupata kudhihirika. Utendaji kazi wa kanuni hizi unapolazimisha patumiwe sifa ya huruma au usamehevu, basi sifa hiyo hutokea kufanya kazi. Ndiposa pale pale sifa Yake ya kuadhibu ijidhihirishapo kulingana na kanuni Zake kumhusu mtu mmoja nayo sifa Yake ya usamehevu au huruma au upole hujidhihirisha kumhusu mtu mwingine. Mtu mmoja azaliwa katika udhihirishaji wa sifa ya Mwenyezi Mungu ya uumbaji na wakati ule ule Mtu mwingine yuwafa katika udhihirishaji wa sifa ya Mwenyezi Mungu ya uangamizaji. Kwa jumla swali huulizwa ya kwamba mbona Mungu huwafisha watu ilihali Kurani yamwelezea kuwa yu ***Rabbul-'Aalamiin***, inayomaanisha kwamba Mungu huumba na kukuza na kufikisha ukamilifuni. Swali hili laonesha utovu wa fahamu kwa upande wa mwenye kuliuliza. Kurani haimwelezei Mwenyezi Mungu kuwa ni ***Rabb*** wa dunia hii peke yake bali kama ***Rabb*** wa dunia zote. Kifo chamaanisha mabadilisho kutoka malimwengu haya hadi malimwengu mengine. Mtu abadilishwapo hivyo, sifa ya ***Rubuubiyyat*** (uumbaji na ukuzaji) hujidhihirisha kumhusu mtu yule katika yale malimwengu alikobadilishiwa. Chochote kilichomo katika malimwengu yoyote chaendelezwa chini ya sifa ya ***Rubuubiyyat***. Lakini hata hivyo, kama tutokee kudhania kwamba kitu fulani kimekoma kuwepo, basi hicho kimekoma kuwa ni sehemu ya malimwengu yoyote yale na hili suala la kudhihirika kwa sifa ya ***Rabbul-'Aalamiin*** (Muumba, Mlezi na Mwendelezaji wa viumbe vyote) kuhusikana na kitu kile linakuwa haliko tena.

Kurani yafundisha kwamba kwa minajili ya kusimamia na kuratibisha zile sifa zimwathirizo mwanadamu Mwenyezi Mungu ameweka kanuni mbili: Ya kwanza ni "Rehema yangu inakienea kila kitu (Sura Al-A'raaf, 7:157); na ya pili imo ndani ya aya isemayo: "Mmekuwaje hamtumainii hekima Kwake Allah" (Sura Nuuh, 71:14). Hii aya ya pili yamaanisha kwamba chochote kile Afanyacho Mwenyezi Mungu

chatokana na hekima. Mojawapo ya sifa za Mwenyezi Mungu zilizotajwa ndani ya Kurani ni Mwenye Hekima ambayo pia inaashiria jambo hilo hilo.

Hizi kanuni mbili zaonesha kwamba kila dhihirisho la sifa ya Mwenyezi Mungu ni kwa ajili ya kutimiliza lengo au shabaha maalumu. Pia zaonesha kwamba wakati wowote kutokeapo hali ya kung'ang'ania baina ya kanuni zitakazo adhabu na zile zitakazo ifanyike huruma, hizo za pili zitashinda na adhabu kutiishwa. Kutafakaria utendaji kazi wa kanuni hizi mbili huujaza moyo wa Mwislamu mapenzi ya Mwenyezi Mungu yanayolifunikiza dhati yake nzima. Kwa ajili ya kujijengea mapenzi moyoni mwake juu ya Mwenyezi Mungu, Mwislamu hana lazima ya kujikera akilini au lazima ya kukubali itikadi ya Kafara na kusulubiwa kwa mwanadamu eti aliyejichukulia mzigo wa madhambi yote. Yatosha kwake yeye ya kwamba Kurani yafundisha kwamba kila dhihirisho la Mwenyezi Mungu linatokana na hekima na lina shabaha na lengo maalumu na kwamba, akiwa mwanadamu, atokeapo wakati fulani kuwa na hatia ya udhaifu au kufanya kosa na kisha kupatwa na majuto na toba na kuamua kuepukana na kila aina ya makosa katika siku za usoni, basi upendo na msamaha wa Mwenyezi Mungu vitamfunikiza kabisa. Kufahamu ukweli huu humlainisha moyo nao huyeyuka katika ashiki ya mapenzi juu ya Mwenyezi Mungu. Mwislamu hutambua kwamba ingawaje Mwenyezi Mungu ndiye Muumba na Mfalme, lakini hata hivyo Yeye husamehe makosa ya watumishi Wake, kuachilia kuteleza kwao, na kuyafanyia maendeleo yao kila aina ya maandalizi. Atoapo adhabu, lengo lake sio kuumiza au kudhalilisha bali ni kuwawezesha watumishi Wake wakosaji kujirekebisha na kupiga hatua kwenye njia ya maendeleo. Hutambua kwamba Mwenyezi Mungu yuko tayari daima kuridhia toba ya kikwelikweli na hufunikiza makosa ya watumishi Wake na kwa njia ya majuto na toba huyafutilia mbali. Yeye hukuta kwamba Mwenyezi Mungu, Ambaye ni Mola wa utukufu na taadhima hutakabali dua za watumishi Wake na kwamba shauku Yake kuwasogelea watumishi

Wake imepita mara nyingi shauku ya watumushi Wake ya kumkurubia Yeye. Akiyatambua haya, moyo wake hujawa na mapenzi juu ya Mwenyezi Mungu naye huvutwa Kwake katika kishindo cha mapenzi na imani kinachozidi hata kile kimsukumacho mtoto kwenye mikono ya mamaye; Mwenyezi Mungu naye pia humuinukia bawa Lake mtumishi Wake sampuli hiyo kwa upendo na huruma inayozidi mara nyingi upendo na ile huruma ya mama achomokaye kumwendea mtoto wake anayelia na kudhikika.

MWANADAMU – KITOVU CHA MALIMWENGU

Kurani yafundisa kwamba Mwenyezi Mungu alitaka kuyaleta malimwengu yawe yatakuwa kama dhihirisho la Utukufu Wake na Nuru Yake na kwamba hiki ndicho kilichokuwa kisababisho cha kuumbwa kwa malimwengu. Yasemwa kwamba Mwenyezi Mungu aliziumba mbingu na ardhi katika nyakati sita. Kabla ya hapo Mwenyezi Mungu enzi Yake ilisambaa juu ya maji. Shabaha ya Mwenyezi Mungu katika kuziumba mbingu na ardhi kutokana na maji ilikuwa ni kumleta dhati aliyejaaliwa hiari ya kuchagua baina ya wema na ubaya. Viumbe hawa wangepitia kwenye mitihani mbalimbali na wangejaribu kushindana katika kutenda wema na hivyo kuonesha ni yupi miongoni mwao aliyefikia utimilifu, (Sura Huud, 11:8). Aya yaonesha kwamba kabla hiki maada haijajipatia hali yake ya hivi sasa ilikuwa katika hali ya majimaji, au, tuseme, kuumbwa kwa malimwengu ya kimwili kulianzia na atomi tuputupu ya haidrojeni na kwamba malimwengu yenyewe yalihulukiwa hatua kwa hatua kutokana na atomi hizo. Kuhusu zile hatua za kabla ya kufikia hali ya kimwili Kurani yasema hivi:

> Je, hawaoni ya kwamba mbingu na ardhi zilikuwa ni kitu kilichofumbatana kisha tukavifumbatua? Na tukafanya kutokana na maji kila kitu kilicho hai. Basi je, hawataamini? (Sura Al-Ambiyaa, 21:31).

Aya hizi zina maana ya kusema kwamba mbingu na ardhi mwanzoni vilikuwa ni bonge lisilokuwa na umbo na sura maalum na kisha

Mwenyezi Mungu akalitengenisha na akalifanya hilo kuwa ni mfumo wa jua na sayari zake na tokea mwanzo Yeye daima ameumba uhai kutokana na maji. Aya yaonesha kwamba malimwengu ya kiroho nayo pia yalikuwa yafanyike kama vile yalivyokuwa yamefanyika malimwengu ya kimwili. Mwenyezi Mungu sawa na kanuni alizokuwa ameziweka, lile bonge la maada lisilokuwa na umbo wala sura maalum akalipasuapasua, na zile sehemu zake zilizotawanyika zikawa ni mfumo huu wa jua. Kwa njia hiyo hiyo Mwenyezi Mungu huleta mabadiliko kwenye malimwengu ya kiroho. Wakati hali za kiroho za wanadamu zinapopotoka na mazingara ya kiroho kusongamana na kuwa magandamivu, basi Mwenyezi Mungu hufanya nuru idhihirike ambayo husababisha mtukuto mle gizani na kulitikisa na kutoka ndani ya hili 'bonge' lisilo na uhai kidhahiri, huumbika mfumo wa jua wa kiroho unaokwenda wakati wote, ambao huanza kuenea kuanzia kitovuni pake na hatimaye huzifunukiza nchi zote au ardhi yote, kulingana na msukumo wake. Kuumbwa kwa malimwengu ya kimwili huanzia na maji; vivyo hivyo malimwengu ya kiroho nayo pia hujipatia uhai kutokana na maji ya kimbinguni ambao ndio wahyi.

Kulingana na Kurani malimwengu yalipitia hatua moja baada ya nyingine hadi pale ardhi ilipojipatia umbo na kujitengenezea hali zilizoweza kuendeleza maisha ya mwanadamu. Kurani yafundisha kwamba kuumbwa kwa mwanadamu ndiko kulikokuwa ni shabaha ya kileleni ya kuumbwa kwa akali kwa mfumo wetu wa jua. Hatua ile ilipowadia, Mwenyezi Mungu akamuumba mwanadamu katika malimwengu ya kimwili kusudi yeye awe ni dhihirisho la sifa za kiungu na awe kana kwamba ni kioo cha kuoneshea picha nzuri ya Mwenyezi Mungu na ili awe ndiye msingi wa malimwengu ya kiroho. Viumbe wa Mwenyezi Mungu kunazo aina mamilioni. Kurani yasema hivi: "Wala hapana yeyote ajuaye majeshi ya Mola wako ila Yeye tu (Sura Al-Muddath-thir, 74:32). Kwa vyovyote mwanadamu yuwashikilia nafasi ya heshima miongoni mwa vilivyoumbwa kutokana na hii sababu ya kuwa yeye yuwatumika kuwa ni kioo cha kuoneshea sifa za Mwenyezi Mungu. Ndiposa masufii wa Kiislamu

wamemwita mwanadamu kijimalimwengu kumaanisha kwamba mwanadamu anazo sifa za vyote vilivyoumbwa na anaweza akahesabiwa kuwa ndiye mhtasari wa malimwengu mazima. Kama vile ramani, inavyoonesha, ijapo kwa kiwango kidogo, kila kijisehemu cha nchi mhusika, ndivyo kinavyowakilishwa mwilini mwa mwanadamu kila kipawa cha malimwengu. Hivyo, basi, mwanadamu ndiye mhimili au kitovu cha malimwengu yaliyoumbwa. Kurani yasema kwamba malimwengu mazima huumbwa na Mwenyezi Mungu kumhudumia mwanadamu na uzoefu wetu wathibitisha kwamba yuwavitawala vyote vilivyoumbwa na kwamba hapana sehemu ya malimwengu inayomtawala yeye. Bila shaka yeye huathiriwa na mabadiliko ya hali ya anga, na nuru za sayari na nyota, na ngurumo na radi, na tufani na dhuruba kali ya theluji, magonjwa ya mlipuko na tauni, lakini yeye kwa vyovyote vile hatawaliwi na vitu hivi. Wale wanaotawala mara nyingi huathiriwa na wale wanaowatawala lakini hata hivyo hamna shida yoyote ya kutambua ni nani atawalaye na ni nani atawaliwaye. Kwa hiyo, ingwwaje mwanadamu yuwaathiriwa na zile sehemu zingine za vilivyoumbwa, lakini hata hivyo yeye yuwavitawala. Yeye yuwaisimamia mito, bahari, milima, pepo, ngurumo, mvua, mitishamba na dawa na yeye kwa uwazi ndiye kitovu cha vilivyoumbwa au kwa akali ni kitovu cha ile sehemu ya vile vilivyoumbwa vinavyohusikana na haya malimwengu yetu. Malimwengu aliyoyaumba Mwenyezi Mungu ni mapana sana na zinaweza zikawepo dunia ambazo sisi hatuna habari nazo. Hivyo basi, sisi hatuwezi tukazibahatishia.

KILELE CHA MFULULIZO WA MABADILIKO YAENDELEAYO

Kinyume na habari zilizo ndani ya Agano la Kale na Agano Jipya, Kurani yafundisha kwamba mwanadamu aliumbwa kupitia mfululizo wa hatua baada ya hatua. Sisi tayari tumelitaja jambo hili hapo juu na tumekariri msimamo wa Kurani kuhusikana na ile rai ambayo tumeiwasilisha. Kunayo aya nyingine ndani ya Kurani inayoonesha kwamba kuumbwa kwa mwanadamu kilikuwa ni kilele cha mfululizo wa hatua kwa hatua na kwamba si sawa kudai kwamba Mweneyzi

Mungu alimtengeneza mtu kutokana na udongo na kumpulizia roho Yake. Kurani yasema kwamba: "Naye amewaumbeni kwa hatua mbalimbali na hali mbalimbali" (Sura Nuuh, 71:15). Hivi ndio kusema kwamba Mwenyezi Mungu kamuumba mwanadamu kwa kumfanya apitie hatua baada ya hatua na hali baada ya hali. Hivyo basi, sawa na Kurani, mwanadamu hakuumbwa mara moja bali kama matokeo ya mfululizo wa hatua kwa hatua. Vivyo hivyo, ukuaji wa mwanadamu wa kiakili nao pia ulipitia hatua baada ya hatua. Kurani yaonesha kwamba wanadamu walikuwepo kabla ya Adamu lakini kwamba wao bado walikuwa hawajawa tayari kuhimili majukumu ya Sheria. Waliishi mapangoni na maficho ya milimani. Ni kwa sababu hii ya kwamba Kurani imewaita kwa lakabu ya jini, ambayo kiasili inamaanisha wale waishio mafichoni. Baadhi ya watu wamelitumia neno hili kwa maana ya wale majini wa hekayani na nganoni, lakini Kurani haiungi mkono tafsiri hii. Yasema kwa uwazi kwamba Adamu[as] na watu wake walipoitoka bustani (ambayo pia, sawa na Kurani, lilikuwa ni eneo la ardhini na yafaa lisichanganywe na Pepo) Mwenyezi Mungu aliwaonya dhidi ya Iblisi "aliyekuwa mmoja wa Majini" na akawatahadharisha wajihadhari naye na watu wake kwani walikuwa wote wakiishi pamoja humu ardhini watakamopitishia maisha yao mazima na watakamofia (Sura Al-A'raaf, 7:26, 28). Tena, Mwenyezi Mungu Awasihi Hadhrat Adamu[as] na watu wake na Iblisi na watu wake wawakubali Manabii Wake watakapodhihiri miongoni mwao mara kwa mara (Sura Al-Baqara, 2:39). Haya yote yanaonesha kwamba wale Majini wa zama za Hadhrat Adamu[as] na kiongozi wao Iblisi walikuwa ni wanadamu tu. Wale majini wa nganoni na hekayani hawaishi pamoja na watu wala wao hawafungamani kivyovyote na wanadamu. Kurani hailiungi mkono kivyovyote vile hili wazo la majini wa nganoni na hekayani. Wale Kurani inaowaelezea kuwa Majini kuhusikana na Hadhrat Adamu[as] walikuwa ni wanadamu walioishi humuhumu ardhini lakini ambao akili zao zilikuwa bado kupevuka. Ilipofikia hatua ya upevu kamili wa akili ya mwanadamu, Mwenyezi Mungu akamletea wahyi Wake mja mkamilifu zaidi wa

zama zile, yaani Hadhrat Adamu[as]. Wahyi wenyewe uliishilizia tu na amri chache za kijamii zihusikanazo na uundaji wa jamii na utoaji wa chakula na njia zingine za ulezi wa jamii. Wale ambao fikara zao za kijamii zilikuwa bado hazijapevuka sawa sawa wakakataa kumtii Hadhrat Adamu[as]. Mwenyezi Mungu akawaadhibu na kumpatia Hadhrat Adamu[as] ushindi dhidi yao. Kwa ajili ya siku za usoni Mwenyezi Mungu akakadiria kwamba Manabii wataendelea kudhihiri na wale waliotokea kuwaamini watajinasibisha na Hadhrat Adamu[as] na wale watakaotokea kuwakataa watajinasibisha na Majini waliompinga Hadhrat Adamu[as]. Kila Nabii huinuliwa ili asaidie kuendeleza mabadliko ya mwanadamu ya kimwili na ya kiroho. Wale waipingao hatua ifuatiayo ya mabadiliko na hawako tayari kutii mipaka na maamrisho Mwenyezi Mungu anayotaka kuyafaradhisha kwa njia ya Manabii Wake ili kusukuma mbele mfululizo wa mabadiliko, huwakatalia mbali Manabii.

Kwa neno zima, Kurani yafundisha kwamba kuumbwa kwa mwanadamu na ukuaji ni matokeo ya mfululizo wa mabadiliko na vivyo hivyo ukuaji wake wa kiakili nao pia ni matokeo ya mfululizo wa mabadiliko. Hadhrat Adamu[as] hakuwa mwanadamu wa kwanza bali yeye alikuwa ni mwanadamu wa kwanza ambaye akili yake iliweza kukubali na kuhimili majukumu ya wahyi. Kurani haisemi popote pale kwamba Mwenyezi Mungu alitaka kuumba mwanadamu na hivyo akamuumba Hadhrat Adamu[as]. Kurani yasema kwa uwazi kwamba Mwenyezi Mungu aliamua kujaalia "Khalifa ardhini" na akamchagua Hadhrat Adamu[as]. Hii yaonesha kwamba wakati wa kuchaguliwa kwa Hadhrat Adamu[as] kuwa Khalifa wa Mwenyezi Mungu humu ardhini palikuwepo na watu waliokiishi ardhini lakini hapana mmoja wao aliyekuwa mpokeaji wa wahyi wa kiungu kwa kuwa uwezo wao wa kiakili ulikuwa bado haujapevuka sawasawa. Ukuaji wa akili ya mwanadamu ulipofikia hatua alipoweza mwanadamu kujenga jamii na kuishi sawa na utaratibu uliopangwa, Mwenyezi Mungu alimpelekea Hadhrat Adamu[as] wahyi Wake, aliyekuwa na akili iliyopevuka zaidi katika zama zake, na hivyo basi

yeye akawa Nabii wa kwanza. Yeye hakuwa mwanadamu wa kwanza bali Nabii wa kwanza, na wahyi uliopokewa naye zilikuwemo sheria chache za kijamii na maelezo rahisi ya sifa za Mwenyezi Mungu.

Mahali pengine Kurani yasema: "Na kwa hakika tuliwaumbeni, kisha tukawapatieni sura, kisha tukawaambia malaika: Mtiini Adamu" (Sura Al-A'raaf, 7:12). Aya hii yamaanisha kwamba Mwenyezi Mungu alimuumba mwanadamu na kisha akavipatia umbo vipawa vyake na kisha akawaamuru malaika wamtii Adamu. Aya pia yaonesha kwa uwazi kwamba mwanadamu alikuwa amekuwepo kabla ya wakati wa Adamu. Ukuzaji wa vipawa vya kiakili vya mwanadamu waonesha kwamba kabla ya kudhihiri Adamu, mwanadamu tayari alikuwa ameishapitia hatua kadha za mabadiliko ya kimaumbile. Aya yaonesha kwamba mwanadamu baada ya kuwa ameumbwa vipawa vyake vilikua hatua kwa hatua na kujipatia maumbo mbalimbali na akaanza kutofautiana na wanyama wengine pembezoni mwake na ilipopata akili yake kukua hadi hatua fulani akaumbwa Adamu na Mwenyezi Mungu akampelekea wahyi Wake.

SHABAHA YA KUUMBWA KWA MWANADAMU

Kurani yafundisha kwamba mwanadamu ameumbwa awe ni dhihirisho la sifa za Mwenyezi Mungu na kuzieleleza katika maisha yake. Yasema hivi: "Na nimewaumba majini na watu kusudi waniabudu na kujipatia rangi ya sifa Zangu" (Sura Adh-Dhaariyaat, 51:57).

(Kama ilivyokwisha elezewa neno Jinn halimaanaishi aina fulani ya viumbe wasioonekana bali lainuiwa kuonesha jamii fulani ya watu). Mahali pengine Kurani yasema, "Yeye ndiye aliyewafanyeni makhalifa ardhini; na anayekufuru, basi kufuru yake ni juu yake" (Sura Al-Faatir, 35:40). Hii yamaanisha kwamba kama mwanadamu kwa hiari yuwajing'atua kutoka kile cheo Mwenyezi Mungu alichomjazi, basi yeye kwa kufanya hivyo hamdhuru Mwenyezi Mungu kwa vyovyote vile bali mwenyewe tu yuwajiondoa kutoka mahali pa heshima na zitamfika yeye mwenyewe athari zake. Aya hizi zaonesha kwamba mwanadamu ameumbwa azieleleze sifa za

Mwenyezi Mungu katika maisha yake yeye mwenyewe na kwamba yeye ni khalifa wa Mwenyezi Mungu humu ardhini. Hivyo basi, yeye ndiye kitovu cha malimwengu ya kimwili. Kwa kuwa Manabii huinuliwa kwa minajili ya marekebisho ya wanadamu na kuwakumbusha shabaha ya maisha yao na kuwaelekeza sawasawa kwenye utimilizaji wake, wao katika nyanja zao wanakuwa ni vituo kwa ajili ya wanadamu. Kwa maneno mengine, mwanadamu ndilo jua yanalolizunguka malimwengu ya kimwili na kila mmoja wa Manabii ndiye jua wanalolizunguka wale watu ambao kwa ajili ya uongozi wao Nabii yule anatumwa.

KANUNI YA MAUMBILE NA KANUNI YA SHERIA YA KIROHO

Kurani yaonesha kwamba Mwenyezi Mungu ameweka kanuni za aina mbili kwa minajili ya kumkumbushia mwanadamu wajibu wake na kumsaidia kwenye njia ya maendeleo. Moja ya hizi ni kanuni ya maumbile inayohusikana na maendeleo ya kimwili ya mwanadamu. Kwa kuwa kanuni hii haihusikani moja kwa moja na maendeleo ya mwanadamu ya kiroho, uvunjaji wa kanuni hii humsababishia mwanadamu hasara ya kimwili lakini hauhusishi chuki ya Mwenyezi Mungu au hasira. Malimwengu mazima ya kimwili yamejaaliwa mvuto unaofaa wa kanuni hii nayo yanahimizwa na kanuni hii. Hapana wahyi wa moja kwa moja unaofanywa na Mwenyezi Mungu juu ya tafsili ya kanuni hii.

Ya pili ni ile Kanuni ya Sheria ya kiroho inayosimamia maendeleo ya kiroho ya mwanadamu. Uvunjaji wa kanuni hii huhusisha chuki ya Mwenyezi Mungu, kwani ni kwa kuitii tu kanuni hii ambapo mwanadamu anaweza akafaulu katika kutimiza yale madhumuni aliyoyaumbiwa na uvunjaji wa kanuni hii hukwamisha upigaji wake wa hatua kuelekea lengo lile. Lakini kila uvunjaji wa kanuni hii hauna athari ya kumnyima kabisa mwanadamu nafasi yake ya kufikia lengo la kuumbwa kwake. Kurani yafundisha kwamba hii Kanuni ya Sheria ya kiroho kijumla humsaidia mwanadamu kujichumia usafi wa kiroho na utukufu. Kama vile kila uvunjaji wa kanuni ya kimaumbile

usivyomhusishia mwanadamu maangamizo na shari ya kabisa kabisa wala kila uzembe katika jambo la maakuli hausababishi maradhi, ndivyo kila uvunjaji wa hii Kanuni ya Sheria ya kiroho usivyomletea mwanadamu ghadhabu ya Mwenyezi Mungu au kumnyima uwezekano wote wa kufikia lengo lake. Shabaha yenyewe ya hii Kanuni ya Sheria ni kumsaidia mwanadamu kuhitimisha kujipatia utimilifu wa kiroho. Unaponuiwa utaratibu kuleta matokeo fulani, basi kutofaulu kwake kwa upande fulani kunaweza kukasahihishwa au kufidiwa na kufaulu kwake kwa upande mwingine na matokeo yaliyokusudiwa kupatikana vile vile. Mwili wa mwanadamu, kwa mfano, ni mpangilio wa sehemu nyingi na uhai wa mwanadamu unategemea kwa ajili ya maendelezi yake mazuri vitu mbalimbali kama vile chakula, maji, hewa, n.k. Wakati mwingine kimoja au baadhi ya vitu hivi hupata walakini, lakini haitokei kuwa lazima kwa chembechembe za uhai kupata maradhi. Dosari inayoletwa na upungufu katika kitu kimoja inaweza ikashindwa nguvu na hali ya kufanya kazi sawasawa ya vile vitu vingine. Hivyo hivyo ndivyo ilivyo hii Kanuni ya Sheria ya kiroho. Inayo maagizo na sera ambavyo kwa pamoja vimenuiliwa maendeleo ya kiroho ya mwanadamu. Isipokuwa ukataaji wa Ufalme wa Mungu au maamrisho ya Manabii Wake, dosari yoyote inayoweza kuzushwa katika mienendo ya mwanadamu na makosa au udhaifu yarekebishika. Ikiwa ni dosari kubwa, basi inaweza tu ikarekebishwa kwa njia ya toba halisi na maombi ya kiaminifu.

Kurani yaonesha kwamba pamoja na hizi kanuni mbili ziko kanuni zingine mbili zinazofanya kazi wakati wote, yaani, kanuni ya kijamii na kanuni ya maadili. Lakini hizi kwa hakika ni upanuzi tu wa mipaka ya ile Kanuni ya kimaumbile na ile Kanuni ya Sheria ya kiroho. Kanuni ya maadili ni upanuzi wa Kanuni ya Sheria ya Kiroho na kanuni ya kijamii ni upanuzi wa ile kanuni ya kimaumbile nazo hufanya kazi na kushughulikiana kwa kiasi kikubwa. Maagizo mengi ya kanuni ya kijamii yametokana na maadili na maagizo mengi ya kanuni ya maadili yametokana na taaluma ya maendeleo ya kijamii. Kwa vile mwanadamu amekusudiwa kuishi kama sehemu ya jamii,

yeye yuwazihitaji aina hizi zote mbili za kanuni. Kanuni ya kijamii ikiwa, kama ilivyo, upanuzi wa kanuni ya kimaumbile, mwanadamu amepewa hiari maridhawa katika utungaji wake. Kanuni ya maadili ikiwa yahusiana na Kanuni ya Sheria ya Kiroho, misingi yake yasimamiwa na kanuni ile, ingawaje baadhi ya tafsili zake zimeachiwa hiari ya mwanadamu. Utaratibu mzima wa malimwengu wafanya kazi katika misingi ya kanuni hizi. Kanuni ya maumbile na Kanuni ya Sheria ya Kiroho zote mbili zimejaaliwa na Mwenyezi Mungu na mwanadamu hana mchango katika utungaji wazo. Hata hivyo, kanuni ya kijamii na ya maadili ni mseto wa maamrisho ya kiungu na ya mwanadamu, na kwa njia hii kwa kujumuisha pamoja ushirikiano wa mwanadamu na makusudio ya kiungu mwongozo bora kabisa hupatikana wa kuyaendeshea malimwengu. Maadamu mikondo hii miwili inaendelea kwenye mitiririko iendayo sambamba, basi dunia huendelea kupiga hatua kwa amani na mwanadamu huweza kusimika humu ardhini utaratibu unaofaa ambao unaafikiana na Ufalme wa Mungu, lakini inapotokea mikondo hii kutiririka pande tofauti, au kwa neno zima, inapotokea akili ya mwanadamu kubetuliwa mbali na ule mkondo unaokwenda sambamba na mwongozo wa kiungu na kuwa sasa imenyimwa baraka za Mungu, basi dunia huingiwa na hali ya mizozo na ugomvi. Hapo haiwi inatawalaiwa na Mwenyezi Mungu wala mwanadamu bali inakuwa ni yenye kuvamwa na nguvu za kishetani; kwani mwanadamu anaweza yu akajiita mwanadamu kadri anavyofuata mwongozo wa kimbinguni. Akomapo kufanya hivyo, basi hushuka kwenye daraja ya wanyama.

Ili kumwezesha mwanadamu kujipatia ukaribu na Mwenyezi Mungu ilikuwa ni sharti kumpatia hiari ya kuchagua jambo la kufanya. Kurani yafundisha kwamba mwanadamu katika eneo fulani yuko huru na katika eneo jingine yuwashurutishwa. Yeye yuko huru katika upande wa Kanuni ya Sheria ya Kiroho na hana hiari yoyote katika upande wa ufanyaji kazi wa kanuni ya kimaumbile. Yeye yuwashurutishwa katika hili eneo la pili kwa hii sababu ya kwamba maendeleo yake ya kiroho hayahusikani moja kwa moja na ufanyaji

kazi wa kanuni ya kimaumbile. Yeye amejaaliwa hiari upande wa Kanuni ya Sheria ya Kiroho kwa kuwa yeye amekuwa mstahilishiwa fadhili za kimbinguni kwa kufuata Kanuni ya Sheria ya Kiroho tu na thawabu haziwezi zikapatikana isipokuwa pawe pana hiari katika uwanja wa matendo ya mtu. Kile anachokishurutishiwa mwanadamu kukifanya hakiwezi kikampatia thawabu.

Kurani yatambua kwamba masilahi ya kiroho ya mwanadamu na maendeleo yake yanaathiriwa na mazingara yake ya kimwili na kwa ile ile kadiri yanavyoathiriwa jinsi hiyo vitendo vyake vimewekewa mipaka, lakini pia yafundisha kwamba matendo ya mwanadamu huthaminiwa na Mwenyezi Mungu kwa kutilia maanani uelewa wake na mazingara yake. Kwa mfano, kama atokee tajiri mkubwa kutumia kajisehemu kadogo ka utajiri wake kuwahudumia wanadamu, na maskini ambaye rasilimali yake nzima ni sawa na kajisehemu kale aitumie yote kwenye huduma za wanadamu wenzake, basi machoni pa Mwenyezi Mungu, wote wawili hawastahili thawabu kadiri moja. Yule tajiri mkubwa alitoa kajisehemu kadogo tu ka utajiri wake kujipatia radhi ya Mwenyezi Mungu ambapo yule maskini alitoa mali yake yote kwa shabaha ile ile. Thawabu alizojichumia kila mmoja wao zitalingana na kiasi cha kujinyima alichofanya kila mmmja wao. Mwenyezi Mungu haangalii ukubwa wa matendo ya mtu lakini huyathamini sawa na kiini halisi cha matendo yenyewe. Hasahaulii mbali upungufu unaomkabili mtu unaompunguzia kiwango cha matendo yake wala wasaa ulionao mtu unaomwezeshea matendo yake.

MABADILIKO YA UUMBIKAJI WA MALIMWENGU YA KIROHO YALIHITIMIKA KATIKA MTUME MTUKUFU[SAW]

Twajifunza katika Kurani ya kuwa malimwengu ya kimwili yameumbika hatua kwa hatua, mfululizo wa uumbikaji kama huo huo ulikadiriwa kwa ajili ya malimwengu ya kiroho. Ndiposa sheria halisi na timilifu haikufunuliwa mwanzoni mwa malimwengu. Wahyi ulishushwa kwa mwanadamu kufuatana na hatua ya ukuaji aliyoifikia. Hatimaye mwanadamu akaifikia hatua ambapo angeliweza kuyahimili

majukumu ya Kanuni Timilifu ya Sheria ya Kiroho. Mwenyezi Mungu akasababisha kudhihiri kwa mwanadamu mtimilifu kabisa katika dhati ya Mtume Mtukufu[saw] wa Islam na akamfunulia Kanuni Timilifu ya Sheria ya Kiroho na Kitabu Kitimilifu. Ile Kanuni Timilifu ndiyo Islam na kile Kitabu Kitimilifu ndio Kurani. Mabadiliko ya uumbikaji wa malimwengu ya kiroho yalihitimika katika Mtume Mtukufu[saw]. Kama vile ambavyo mwanadamu ni kitovu cha malimwengu ya kimwili na Manabii walikuwa ni vitovu vya mataifa na vya zama ambazo kwa ajili ya hizo walikuwa wametumwa, Mtume Mtukufu[saw] wa Islam ndiye kitovu kwa ajili ya wanadamu wote. Hivyo basi, plani ya malimwengu inayowasilishwa na Kurani ni kwamba kitovu cha awali cha malimwengu ni mwanadamu. Katika maeneo yao mbalimbali wanadamu huzungukia Manabii wao wahusika, Manabii humzungukia Mtume Mtukufu[saw] naye, kwa upande wake, huzunguka na kuyaongoza malimwengu mazima kwake Mwenyezi Mungu na kwa njia hiyo malimwengu ya kiroho yanafikishwa kwenye utimilifu wake.

KURANI NDICHO KITABU KITIMILIFU

Imekwishasemwa ya kwamba Mwenyezi Mungu kwa njia ya Manabii Wake amefanya maandalizi kwa ajili ya maendeleo na utimilifu wa mwanadamu kwa njia ya Kanuni ya Sheria ya Kiroho, kanuni ya maadili na kanuni ya kijamii. Kwa kuwa Kurani ndicho Kitabu kitimilifu, chazizungumzia kanuni hizi zote tatu. Inaiweka kikamilifu Kanuni ya Sheria ya Kiroho na Kanuni ya maadili na kutoa maagizo ya kimsingi ya ile kanuni ya kijamii ikiyaacha maeneo mengine ya kanuni ya kijamii kubuniwa na kujalizwa na mwanadamu mwenyewe. Kwenye eneo la kanuni ya maadili Kurani yatoa hili agizo la kimsingi ya kuwa ni utumiaji mzuri wa vipawa vya kimaumbile ambao ndio tabia tukufu. Kuvizima au kuviulia mbali vipawa vya kimaumbile au matamanio ni kosa la kimaadili kama vile lilivyo kosa kutawaliwa navyo. Yule mwenye kutaka kuviulia mbali vipawa vyake vya kimaumbile au kuvizima kabisa huwa yuwaipinga kanuni ya kimaumbile. Yule ambaye mawazo yake yamejawa, na ambaye

jitihada zake zote zinaelekezewa utoshelezaji wa matamanio yake ya kimaumbile huwa yuwapinga Kanuni ya Sheria ya Kiroho na yuwaelekea kwenye maangamio ya kiroho. Haya yote mawili ni sumu kwa ukuaji wa mwanadamu. Haiwezi kanuni ya maumbile wala Kanuni ya Sheria ya Kiroho ikavunjwa kwa makusudi. Ndiposa Kurani yafundisha kwamba kwa kuwa vitu vyote vimeumbwa kwa ajili ya huduma na manufaa ya mwanadamu, kuvitumia amekuruhusiwa ila kwamba yeye anakatazwa kuvifanyia matumizi ambayo kwa yakini yana madhara. Kulingana na agizo hili, ukapera wahesabiwa na Islam sio kama wema bali kama ubaya. Vivyo hivyo kuacha utumiaji wa vyakula vizuri, vinywaji na mavazi sio wema bali ni ubaya, kwa kuwa ukatazaji sampuli hii huwa ni upingaji wa kanuni ya maumbile na utovu wa shukrani juu ya rehema za Mwenyezi Mungu. Pia ni ubaya kwa mtu kupitisha maisha yake mazima akiviinamia vitu hivi na kujitosa kabisa kwenye anasa zao, kwani kwa njia hii mwanadamu husahaulia mbali ukuaji wa roho yake, ambayo ndiyo shabaha halisi ya uwepo wake. Kama vile ilivyo makosa kwa mtu kuendelea kuchapa kazi mfululizo na kujizuilia lishe — kwani hapo atajisababishia kifo chake yeye mwenyewe na ataiacha kazi yake ikiwa nusu — vivyo hivyo ni makosa kwa mtu kujishughulisha kabisa kabisa na utoshelezaji wa matamanio yake ya kimwili na kuachilia mbali mambo ya manufaa, kwani mtu kama huyo yuwapitisha maisha yake katika kujipatia viwezesho huku shabaha yenyewe akiisahaulia mbali. Shabaha haiwezi ikafikiwa bila ya kuwepo viwezesho na viwezesho vinavyofaa haviwezi vikabunika bila kuzingatia shabaha halisi.

MISINGI YA UJENZI WA UTARATIBU WA KIJAMII

Ili kusimika utaratibu katika uwanja wa kijamii na kuuelekeza kwenye upande mwema, Kurani imeweka misingi inayofuata:

(1) Umilikaji kamili Anao Mwenyezi Mungu peke yake na vitu vyote ni Vyake Yeye.

(2) Kila kitu Amekitiishia usimamizi wa mwanadamu kwa ajili ya manufaa ya wanadamu wote.

(3) Kwa kuwa shabaha ya kuwepo kwa mwanadamu ni utimilifu wa kiroho, basi hana budi kupatiwa kiasi fulani cha uhuru wa kuchagua katika matendo yake na hana budi kupatiwa uwanja wa kufanyia shughuli zake.

(4) Kwa kuwa vile vitu vilivyo msingi wa maendeleo ya mwanadamu ni urithi wa wanadamu wote, mazao ya utendaji kazi wa mwanadamu hayana budi kugawanywa kwa njia ambayo itamhakikishia fungu lake stahilifu mtu binafsi na hata jamii nzima.

(5) Kwa ajili ya usimamizi unaofaa wa utaratibu wa mwanadamu wa kijamii hapana budi mtu fulani kupewa madaraka, ambaye ni sharti achaguliwe kama matokeo ya mashauriano miongoni mwa umma ambao yeye atakuwa na madaraka juu yao. Kazi yake sio kutunga sheria bali kutekeleza sheria za Mwenyezi Mungu.

(6) Ikitilia maanani tofauti katika utaratibu wa kisiasa katika jamii mbalimbali Kurani yafundisha kwamba:

(a) Panapokuwa na ubishi utokanao na madola yoyote mawili au zaidi ya kisiasa, yale madola mengine na yajumuike pamoja kuleta suluhisho la ubishi ule.

(b) Ikitokea kutopatikana suluhisho mwafaka baina ya yale madola yanayobishana, basi madola mengine na yatangaze uamuzi wa haki kwa kutilia maanani lile jambo ambalo ndilo sababu ya ubishi wenyewe.

(c) Likitokea dola lolote baina ya madola yanayobishana kutokubali uamuzi ule au, baada ya kuukubali kudinda kuutekeleza, yale madola mengine na yajumuike pamoja kulishawishi dola kinzani kukubali ule uamuzi kwa faida ya amani ya kimataifa. Utokeapo ushawishi kutofanya kazi, basi madola mengine yote yaishurutishe kwa nguvu ile Serikali mhusika kuliridhia lile suluhisho.

(d) Ile Serikali kinzani inapolikubali lile suluhisho, zile Serikali zingine zijizuie kutoingilia ndani zaidi ya kushurutishia lile suluhisho lihusikanalo na ubishi wa tangu mwanzo wala zisitafute kujipatia

manufaa kutokana na hali ilivyo, kwani hili lingesimika msingi wa ubishi mpya.

Haya yote yaliagizwa na Kurani zaidi ya karne kumi na tatu na nusu zilizopita. Umoja wa Mataifa umekubali baadhi ya maagizo haya lakini yaelekea kutofaulu katika shabaha zake kwa sababu ya kuyaachilia mbali mengine. Shirikisho la Mataifa halikufaulu kwa sababu hii ya kwamba halikulitimiliza agizo la Kurani ya kuwa Serikali kinzani na ishurutishwe kwa nguvu kukubali uamuzi wa kimataifa au suluhisho. Umoja wa Mataifa hauonekani kulinda ya kwamba mataifa yanayosimamia usuluhishi na yasijitafutie kujinufaisha yenyewe kwa kutojali mataifa yaliyoshindwa na hayana budi kukomeshea juhudi zao kwenye kusimamia usuluhishi wa ule ubishi uliozusha mazozano. Hivyo basi, inahofiwa ya kwamba Umoja wa Mataifa utakumbwa na janga lile lile lililolikumba Shirikisho la Mataifa; kwani amani inaweza tu ikapatikana na kudumishwa juu ya ile misingi iliyowekwa ndani ya Kurani.

MAISHA BAADA YA KIFO

Kurani yafundisha kwamba mtu afapo roho yake huingia malimwengu mapya na kujipatia mwili mpya. Mwili huu watofautiana na mwili wa udongo uliotengenezewa mahitaji ya maisha haya ya sasa. Ni aina mpya ya mwili wa kiroho wenye vipawa vya kivyake vya kufahamia sifa nzuri za Mwenyezi Mungu. Roho timilifu zitaingizwa mara moja katika ile hali inayoelezewa kuwa ni Pepo. Roho zinazotimilika nusu nusu katika maisha haya ya sasa zitakumbana na ile hali inayoelezewa kuwa ni Jahanamu ambayo ni hali ya uponyevu wa maradhi ya kiroho. Kadiri harakati za uponyaji zinavyomalizika kuihusu kila roho, basi itaifikia Pepo; hadi pale ambapo mwishowe roho zote zitakapokuwa zimeipata Pepo na ile hali ya Jahanamu itakomeshelewa mbali. Zote zilitoka kwa Mwenyezi Mungu, hatimaye zitarejea Kwake. Furaha zao, raha na faraja zao, vyote vitakuwa ni vya kiroho. Kumkumbuka Mwenyezi Mungu na mapenzi juu ya Mwenyezi Mungu vitakuwa lishe yao na kumwona Mwenyezi Mungu

kutakuwa ndiyo malipo yao makubwa zaidi. Kurani yakumbusha ukweli huu kwa kudai ikisema kwamba 'Mwisho wake ni kwa Mola wako' (Sura An-Naazi'aat, 79:45). Hii yamaanisha kwamba malimwengu yalianza na Mwenyezi Mungu na yatamalizikia naye. Kile kilichotokana na Mwenyezi Mungu kitarudi kwa Mweneyzi Mungu, alivyosema Yesu: "Wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni, ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni"(Yohana 3:13).

HADHRAT AHMAD, MASIHI ALIYEAHIDIWA[AS]

Kurani yaelezea hii kanuni ya kwamba kwa kuwa Kanuni ya Sheria ya Kiroho imefunuliwa kwa njia ya Mtume Mtukufu[saw] wa Islam, hapana Nabii Mleta Sheria atakayedhihiri baada yake. Kurani ni Kitabu cha mwisho kilichofunuliwa wala haiwezi sehemu yake au kitabu kizima kutanguliwa na wahyi wa baadaye. Malimwengu ya kiroho yataendelea kutawaliwa na Kurani na Mtume Mtukufu[saw] hadi mwisho. Lakini mwanadamu huelekea kusahau, ni mwepesi kuingia makosani na ni mzoefu wa maasi. Ili kuendeleza mamlaka ya Kurani ilikuwa lazima kuandaa tiba ya ubovu huu wote. Kupatikana kwa tiba lilikuwa ni jambo la lazima ili kwamba wanaosahau wakumbushwe, wanaokosa wasahihishwe na wanaoasi washikishwe adabu. Twajua kutoka Kurani ya kuwa kama vile mwezi huiangazia ardhi inapokuwa nuru ya jua haipatikani moja kwa moja, vivyo hivyo waja wataendelea kudhihiri watakaojipatia nuru kutoka kwa Mtume Mtukufu[saw] nao wataendelea kuyaangazia malimwengu ya kiroho. Waja hawa, sawa na kiwango cha haja wanayokadiriwa kuitosheleza, watadhihiri katika sura ya Wajadidi, lakini unapozagaa upotovu na uharibifu katika mambo ya kiroho basi wao wangechaguliwa kama Manabii wasaidizi katika utiifu halisi wa Mtume Mtukufu[saw]. Kurani yaonesha mahali mbalimbali kudhihiri kwa Nabii mmoja kama huyo angeliyekuwa mfano wa kiroho wa Mtume Mtukufu[saw] na ambaye ujaji wake ungelihesabiwa kuwa ujaji wa Mtume Mtukufu[saw] mwenyewe. Katika Hadithi, huyu afananaye na Mtume Mtukufu[saw] amepewa jina la Masihi, na Kurani pia mahali pamoja yaonesha kupasika kwa jina hili juu yake (Sura Az-Zukhruf, 43:58).

Jina jingine linalotajwa ndani ya Hadithi kwa ajili ya Nabii huyu ni Mahdi[as]. Majina haya yote mawili yanamhusu mja yule yule mmoja, ijapo yanaelezea vipawa mbalimbali. Na Injili pia zaudokezea huu ujaji wa mara ya pili wa Mtume Mtukufu[saw] kwa kushikilia ahadi ya ujaji wa mara ya pili wa Yesu. Zile ishara zilizotajwa ndani ya Vitabu vya kale zaidi na katika Kurani ambazo ziwe zinaonesha wakati wa ujaji wa Nabii huyu zimetimia katika zama hizi, nayo ni dalili kubwa ya ukweli wa Kurani ya kuwa, sawa na bishara zilizotolewa ndani yake, mja aliinuliwa na Mwenyezi Mungu katika zama hizi aliyedai kuwa ni mfano wa kiroho wa Mtume Mtukufu[saw] na ambaye katika ujaji wake zile bishara zilizomo ndani ya Kurani na Vitabu vingine zilitimia. Yeye alieleza kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa amemwinua kwa ajili ya kuuleta kwa mara ya pili ushindi wa Islam na kufafanua mafundisho halisi ya Kurani. Mja aliyetoa madai haya alikuwa ni marehemu Hadhrat Mirza Ghulam Ahamad[as], Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahamadiyya. Takriban miaka sitini (tangu kuandikwa maandishi haya) iliyopita yeye aliambiwa na Mungu kwa njia ya wahyi ya kwamba amechaguliwa kuhudumia Islam na Mtume Mtukufu[saw] na kushughulikia utukuzwaji wa jina la Mwenyezi Mungu malimwenguni. Aliambiwa kwamba Mwenyezi Mungu amemjazi heshima ya utume kwa hili sharti ya kwamba yeye aendelee kuwa mfuasi halisi wa Mtume Mtukufu[saw] na wa Kurani na kwamba ule wahyi aliouteremshiwa ungelikuwa chini ya Kurani wala hazitakuwemo Sheria mpya. Miongoni mwa wahyi aliopokea ulikuwemo huu, "Kila baraka yatokana na Muhammad na mbarikiwa ni yule aliyefundisha," yaani, Mtume Mtukufu[saw], "na mbarikiwa ni yule aliyejifunza," yaani, Hadhrat Ahmad[as] aliyekuwa mpokeaji wa wahyi huu (Haqiiqatul-Wahyi). Tena, akapokea wahyi uliosema: "Mwonyaj amedhihri duniani lakini dunia haikumkubali. Lakini Mwenyezi Mungu Atamkubalia na Atathibitisha ukweli wake kwa njia ya misukosuko mikubwa" (Baraahine Ahmadiyya). Katika istilahi ya Kurani, mwonyaji maana yake ni Nabii na katika kauli nyingine ya huu wahyi uliopokewa na Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu

Waahamadiyya neno lililotumiwa mahali pa "Mwonyaji" lilikuwa ni Nabii (Ek Ghalati Ka Izala). Wadhifa wake ulikuwa ni kumleta mwandamu ana kwa ana na Muumba wake katika zama hizi za giza na kupanda mbegu ya maendeleo ya kiroho katika dunia hii ya kimwili kwa njia ya Ishara mpya mpya na wahyi. Wakati alipotangaza mara ya kwanza madai yake yeye alikuwa peke yake na hakuwa na wafuasi. Alidhihiri kwenye kijiji cha wakazi elfu moja na mia nne au mia tano ambacho hakikuwa na vifaa vya kisasa kama vile ofisi ya posta, simu au njia ya reli. Akatangaza wakati huo kwamba Mwenyezi Mungu Atathibitisha ukweli wake kwa njia ya Ishara zenye nguvu na kwamba jina lake litafikishwa hadi pembe za dunia. Pamoja na lile tangazo kwamba Jumuiya iliyoanzishwa naye itastawi na kuenea na kwamba wafuasi wake watajipatia ukaribu na Mwenyezi Mungu, yeye alizidi kutangaza akisema kwamba ndani ya miaka tisa kufuatia tarehe ya tangazo lenyewe atazaliwa mwana ambaye kwa njia yake nyingi za bishara zake zitatimia na ambaye jina lake litafikishwa pembe za dunia. Mwana huyo atapiga hatua upesi upesi kutoka ufaulu hadi ufaulu naye atajaaliwa Roho Takatifu. Wakati Hadhrat Ahmad[as] alipotangaza madai yake na wahyi uliopokelewa naye, alikabiliwa na tufani kali ya upinzani kutoka kila upande na kila jamii. Mabaniani, Waislamu, Masingasinga na Wakristo wote waliungana katika upinzani na kupanga kummalizia mbali. Upinzani huu wenyewe ulikuwa ni ishara ya kwamba Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahamadiyya alikuwa akiongozwa na Mungu, kwani upinzani wa kote kote kama huo kwa kawaida huwa tu dhidi ya Manabii wa kweli. Licha ya ukweli kwamba yeye alikuwa peke yake na alipingwa na jamii zote, Mwenyezi Mungu alianza kuimarisha sauti yake na watu mmoja mmoj na wawili wawili walianza kumwamini. Pole pole wafuasi wake wakaenea huko Panjab na kisha wakaenea mikoa mingine ya India na hata nje yake.

MWANA MWAHIDIWA WA MASIHI ALIYEAHIDIWA[AS]

Wakati Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahamadiyya alipofariki katika mwaka 1908, wapinzani wake walitangaza kwamba

Jumuiya itajifilia mbali. Hata hivyo, wanajumuiya walishikamana, sawa na kanuni za Kiislamu, kumchagua marehemu Hadhrat Maulawii Nur-ud-Din[ra] kama Khalifa wa kwanza. Wakati wa Ukhalifa wa Kwanza baadhi ya wanajumuiya waliokuwa wameathiriwa na mawazo ya Kimagharibi walianza kuidadisi desturi ya Ukhalifa. Rai zao zikapata kuungwa mkono miongoni mwa watu fulani katika Jumuiya hata ikatokea kwamba wakati Hadhrat Maulawii Nur-ud-Din[ra] alipofariki mwaka 1914, harakati kabambe na za pamoja zikafanywa na watu hawa kuifutilia mbali desturi ya Ukhalifa. Mimi, niliye mwana wa Hadhrat Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa[as] aliye Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, wakati ule nilikuwa na umri wa miaka ishirini na mitano tu na sikuwa na rasilimali zozote. Kamati Kuu ya Jumuiya wenye sauti wengi walikuwa ni wale walioiasi dhidi ya Ukhalifa. Idadi iliyo kubwa zaidi ya Wanajumuiya ambao wakati ule walikuweko Qadian na ambao walielezewa na wale waliokuwa uasini dhidi ya Ukhalifa kuwa eti ni majahili, walikuwa wamekazania kwamba watadumisha desturi ya Ukhalifa kulingana na maagizo yaliyomo ndani ya Kurani na walisisitiza kwamba mimi nichukue mzigo wa kushikilia majukumu ya kazi ya Khalifa. Katika hali kama hii mimi nikakubali ahadi za Baiati za Jumuiya kama Khalifa wa Pili na katika cheo kile nilianza kuitumikia Jumuiya, Islam na wanadamu. Kwa kuwa idadi kubwa zaidi ya wale waliohesabiwa kuwa wenye kushikilia nyadhifa za juu humo Jumuiyani walikuwa ni wapinzani wa Ukhalifa, Jumuiya ikatokea kuwa mzozoni. Watu wa nje walianza kutarajia kwamba kumalizika na kuvunjika kwa Jumuiya hakukuwa mbali sana. Wakati ule Mwenyezi Mungu akanifunulia kwamba Atanisaidia na kunipatia ushindi na kuleta vurugu miongoni mwa wapinzani wangu wenye nguvu na atawatia komesha. Kisha muujiza mkubwa ukatokea. Idadi iliyo kubwa zaidi ya wale waliohesabiwa kuwa ndio waliokuwa sehemu ya Jumuiya ya wasomi na wenye uzoefu mkubwa wakaihama Jumuiya katika wakati huu mgumu. Wale waliohesabiwa kuwa ni watu wenye mali na sauti wakajiondoa. Wale waliohesabiwa kuwa watu wajuzi wa Jumuiya, wakaitenganishiwa. Wale waliokuwa

wameasi dhidi ya Ukhalifa wakaanza kutangaza wakisema kwamba kwa vile uongozi wa shughuli za Jumuiya ulikuwa umewekwa mikononi mwa kijana asiyekuwa na uzoefu, basi hivi karibuni Jumuiya itaangamia. Lakini yale yaliyokadiriwa na Yule aliyekuwa ameifunua Kurani na Ambaye ndiye Mwanzilishi wa malimwengu ya kiroho ambayo kulingana na kanuni zake dunia inasonga mbele na Aliyekuwa Amemfunulia Hadhrat Ahmad, Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa[as] ya kuwa ndani ya miaka tisa kuanzia mwaka wa 1884 atajaaliwa mwana ambaye kwa fadhili na huruma za Mwenyezi Mungu atajulikana hadi pembe za dunia na ambaye kwa njia ya kuhubiri Islam atakuja kuwa chombo cha kuwakombolea wale walio utumwani na kuwafufulia wale waliokuwa wafu wa kiroho, yakatimizwa na neno Lake likatukuzwa. Kila kulipokucha yalipatikana mambo yaliyochangia ufaulu wangu na kila siku iliyopita iliacha nyuma mambo yaliyoharakisha kutofaulu kwa wapinzani wangu. Hivyo basi Mwenyezi Mungu alinifanya chombo cha kusambazia Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani kote. Kwenye kila hatua Yeye amenibariki kwa mwongozo Wake na mara nyingi kanitunukia baraka za wahyi Wake. Kisha ikafika ile siku aliyonifunulia kwamba mimi ndimi niliyekuwa yule Mwana Mwahidiwa, ambaye habari za ujaji wake zilikuwa zimetangazwa na Masihi Aliyeahidiwa[as] katika mwaka 1884, miaka mitano kabla sijazaliwa. Kutoka siku ile kiwango cha msaada wa Mwenyezi Mungu na shime kikaanza kuongezeka upesi upesi na leo hii Wabashiri wa Kiahmadiyya wanapigana jihadi ya Islam katika kila bara. Kurani ambayo ilikuwa imebaki kama kitabu kilichofunikwa mikononi mwa Waislamu, sasa kimefanywa kitabu kilichofunuliwa tena na Mwenyezi Mungu kwa ajili yetu kwa njia ya baraka za Mtume Mtukufu[saw] na utumishi wa Masihi Aliyeahidiwa[as]. Chemchem mpya za elimu zinafunuliwa kwetu kwa njia ya Kurani. Wakati wowote linapotokea fundisho lolote au imani iliyomo ndani ya Kurani kufanywa lengo la lawama kutokana na maendeleo mapya ya kisayansi, Mwenyezi Mungu hunifunulia jawabu halisi lililomo ndani ya Kurani. Sisi tumechaguliwa kuwa ni chombo cha kunyanyulia beramu ya ushindi

wa Kurani. Tukijipatia imani na uhakika kutokana na maneno na wahyi wa Mwenyezi Mungu tunaionesha dunia ubora wa Kurani. Uwezo wetu ni haba sana ukilinganishwa na uwezo wa dunia nzima. Hata hivyo tunahikikishiwa ya kwamba licha ya upinzani wa kupindukia, ushindi wa Kurani utasimama imara. Naam, jua linaweza likaipotea njia yake, na nyota zinaweza zikaviondoka vitua vyao, ardhi inaweza ikakoma kuzunguka kwake, lakini sasa hapana kitu wala mtu anayeweza kuzuia ushindi wa Islam na Mtume Mtukufu[saw]. Ushindi wa Kurani utasimikwa kwa mara ya tena. Watu wataachilia mbali kuabudu watu wengine na miungu wengine waliojitengenezea kwa mikono yao na watasujudu wakimwabudu Yule Mungu Mmoja. Licha ya ukweli kwamba hali ya mambo katika jamii ya wanadamu yaonekana inaelekea upande unaokwenda kinyume na mafundisho ya Kurani, Ufalme wa Islam utasimikwa kwa mara nyingine tena kwa uthabiti kiasi hiki kwamba watu wataukuta kuwa ni kitu kisichowezekana kuitikisa misingi yake. Mwenyezi Mungu amepanda mbegu yenye manufaa kwenye jangwa la dunia ambalo Shetani alikuwa amelifanya kuwa mahali kame, nami natangaza kwamba mbegu hii itaota na kumea katika sura ya mti utakaozagaa na kuzaa matunda mengi. Zile roho zinazotamani kupaa juu sana na zinahamasishwa na shauku ya kutaka kuungana na Mwenyezi Mungu siku moja zitaamshwa na kuachishwa matamanio yao ya mali za kidunia na zitapewa hamu ya kwenda kutua kwenye matawi ya mti huu. Hapo machafuko yote yatatoweka na taabu zote zitakomeshwa. Ufalme wa Mungu utasimikwa tena humu ardhini na kumpenda Mwenyezi Mungu ndicho kitakachokuwa kitu cha thamani zaidi kwa mwanadamu. Mapinduzi haya yataanzisha kipindi cha amani na utangamano. Jitihada zote za kuleta amani duniani na kuondolea mbali machafuko zinazokwenda kinyume na kanuni hizi hazitafua dafu.

TAFSIRI KATIKA LUGHA ZINGINE

Kurani ilimwelekeza Mtume Mtukufu[saw] afanye jitihada zake zilizokuwa kubwa zaidi kwa msaada wa Kurani iliyokuwa silaha ifaayo zaidi kwa ajili hii (Sura Al-Furqaan, 25:53). Ni katika kutimiza maelekezo haya ya Kurani ya kwamba linatolewa hili jalada la Tafsiri

ya Kiingereza. Yatumainiwa kwamba kutolewa kwa ile sehemu iliyosalia ya Tafsiri ya Kiingereza hakutacheleweshwa sana. Pamoja na Tafsiri ya Kiingereza, zimetayarishwa Tafsiri katika hizi lugha saba za Kizungu nazo zitatolewa mara tu vikwazo vya hali ya vita vitakaporuhusu: Kirusi, Kijerumani, Kidachi, Kifaransa, Kiitalia, Kireno na Kihispania. Hapo baadaye yatumainiwa kwamba msururu huu wa Tafsiri utaendelea hadi ujumuishe Tafsiri katika lugha zote kubwa. Tafsiri ya Kiswahili tayari inafanyiwa maandalizi.[6]

Vituo vya Jumuiya ya Waislamu Waahamadiyya vimefunguliwa katika sehemu mbalimbali za dunia kwa lengo la kuhubiri Islam na kuelezea mafundisho ya Kurani. Kiko Kituo kikubwa huko Uingereza na Wabashiri wanafanya kazi pia huko Ufaransa, Uhispania, Italia na Uswizi. Katika bara la Marikani tunao Wabashiri huko Marikani kwenyewe na nchi ya Ajentina, na mipango imo mbioni yenye shabaha ya kufungua Vituo nchini Kanada na Brazil. Vituo vimefunguliwa katika nchi zote za Afrika ya Magharibi za Uingereza,[7] na Wabashiri kumi wanafanya kazi katika nchi mbalimbali za Afrika ya Mashariki za Uingereza.[8] Shughuli za kubashiri pia zinafanyika nchini Misri, Sudan na Uhabeshi. Wako Wabashiri Palestina, Siria na Iran katika eneo la Mashariki ya Kati, na huko Malaya, Java, Sumatra na Borneo katika eneo la kusini mwa Asia ya Mashariki. Twaamini kwamba tafsiri hizi na Vituo vya kubashiri vitauanzishia ushindi wa Islam kampeni yenye kufaulu, kwani sio tu kwamba juhudi zetu zinaelekezewa kwenye kulitimiza lile ambalo tayari limeshakadiriwa na Mwenyezi Mungu, bali juhudi zenyewe zimefanywa katika kuitii amri ya Mwenyezi Mungu.

Pamoja na kupeana hii zawadi ya taaluma sisi tunawakumbusha watu wote wapendao ukweli, haidhuru wakiwa na dini gani, wasia huu maarufu ya kuwa mti hujulikana kwa matunda yake. Kurani hutoa

[6] Kwa fadhili za Allah Tafsiri hii ilitolewa katika mwaka 1953 na leo hii msururu huu wazijumuisha Tafsiri za zaidi ya lugha 50, Alhamdu Lillahi — Mfasiri.

[7, 8] Sasa nchi zote zimeishajipatia uhuru.

matunda yake katika kila zama na wale wenye kuishika kuwa wapokeaji wa wahyi wa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu kuonesha uwezo Wake kwa njia ya waja hao. Basi ni kwa nini, katika kutafuta kwetu ukweli, tusijipatie msaada sio kutokana na akili zetu tu bali pia kutokana na yale matunda ya Vitabu vingine tunayoyaona? Ama kusema kweli dunia ingenufaika sana katika harakati zake za kutafuta kweli kama wangetokea Wakristo kuweza kumhimiza Papa au wakuu wengine wa Kanisa kuwasilisha ule wahyi walioupokea kulinganisha na ule niliopokea kwa madhumuni ya kudhihirisha ni upi katika wahyi huo ambao ni madhihirisho halisi ya uwezo na ujuzi wa Mwenyezi Mungu. Papa na makasisi wengine walio watangulizi wao, kwa kuasi mafundisho ya Yesu ya amani, daima walikuwa na shauku ya kuzichochea nchi za Kikristo kuzipiga vita nchi za Kiislamu, ingekuwa yeye kuwa tayari mno kuchukua fursa ya mashindano haya ya kiroho. Kama watokee kuridhia, au kuweza kuhimizwa na wafuasi wao kukubali mwaliko huu, basi hii ingelitokea kuwa njia ya kuponyesha maradhi ya kiroho ambayo wanadamu wameyaugua kwa muda mrefu. Utakatifu na Uwezo wa Mwenyezi Mungu hapo ungejidhihirisha kwa njia isiyokuwa ya kawaida na ingesaidia kuthibitisha imani ya mwanadamu na kuongoza ukuaje wake wa kiroho.

SHUKRANI

Katika kumalizia ningependa kutaja msaada usiokuwa na kifani uliotolewa na Maulawii Sher Ali B.A., ambaye, licha ya kudhoofika kwa afya yake, alitumia sehemu kubwa mno ya wakati wake kufanya kazi ya kutafsiri matini nzima ya Kiingereza. Pia ningependa kumshukuru yeye pamoja na Hadhrat Mirza Bashir Ahmad, M.A., Malik Ghulam Farid, M.A, na Marehemu Ch. Abul Hashim Khan, M.A., kwa kazi waliyofanya ya kudondoa kutoka hotuba na maandiko yangu yale madondoo yaliyokuja kuwa msingi wa Maelezo ya Tafsiri na pia kwa kazi yao ya kutayarisha maelezo haya. Mimi sijawahi kupata fursa ya kuyatupia jicho maelezo haya, lakini ukitiliwa maanani uzoefu na ikhlasi ya waungwana hawa, nina hakika ni lazima wawe

wameyatafsiri sawasawa yale ambayo kwa fadhili za Mungu mimi nimeweza kujichumia kwa mintarafu ya mradi huu moja kwa moja kutoka Kurani au mafundisho ya Masihi Aliyeahidiwa[as]. Aidha, nigependa kuchukua fursa hii kumshukuru Qadhi Muhammad Aslam, M.A., Profesa wa Chuo cha Serikali, Lahore, na Sir Muhammad Zafrullah Khan, ambao wamekitafsiri 'Kifungua Mlango' hiki kwa Lugha ya Kiingereza kutoka Kiurdu. Namwomba Mwenyezi Mungu awapake wao na wazao wao uturi wa baraka Zake na kuwa pamoja nao na kuwasaidia katika maisha haya na ya Akhera. Amina.

Halikadhalika, ningependa kusema kwa kuwa mimi nilikuwa mwanafunzi wa Marehemu Maulawii Nur-ud-Din, Khalifatul Masih wa Kwanza[ra], mengi ya yale niliyojifunza kwake yanabainishwa kwenye 'Maelezo ya Tasiri.' Maelezo haya kusema kweli, yanatokana na ufasiri wa Kurani wa Masihi Aliyeahidiwa[as], Khalifa wa Kwanza[ra], na ufasiri wangu mimi mwenyewe. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu alimbariki Masihi Aliyeahidiwa[as] kwa Roho Yake na akamtukuza kwa kumtunukia elimu ambayo ilihitajika kwa ajili ya maendeleo ya kizazi hiki na vizazi vinavyofuatia, ni matumaini yangu kwamba Maelezo haya yatatokea kuwa ni tiba ya maradhi yao. Kwa njia ya Maelezo haya vipofu wataona, viziwi watasikia, mabubu watanena, viwete na wanaochechemea watatembea na malaika wa Mwenyezi Mungu watayabariki kiasi hiki kwamba yatafaulu katika kutimiza hili lengo yaliloandikiwa. Ee Mola, tutakabalie!

MIRZA BASHIR-UD-DIN MAHMUD AHMAD
(Khalifatul Masih II)
QADIAN.
28 Februari 1947.
6 Rabi uth-Thani 1366 Hijri.
28 Tabligh 1326 H.Sh.